TRIODI YA KWAREZIMA MKUBWA
YA KANISA ORTHODOKSE

CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE
KOLWEZI KONGO
2001

T R I O D I

SIKU YA MUNGU YA MFARISAYO NA MTOZA KODI.
SIKU YA POSHO KWA SALA YA MAGARIBI (ESPERINOS)

Elezo*: Waimbaji wataimba wimbo saba ya Paraklitiki na kisha hii wimbo tatu.*

Sauti ya kwanza.

Wa ndugu, tusiombe kama Mfarisayo, kwa maana huyu atajipandisha atashushwa; tujinyenyekeze kwa Mungu, kama Mtoza Kodi, tuseme kama yeye*:* Ee Bwana, unihurumie mimi mwenye zambi. *(mara mbili).*

Mfarisayo aliposhindwa kwa majivuno yake, na Mtoza-Kodi alipojinyenyekeza kwa toba, wakaonekana wote wawili mbele yako, peke yako Bwana; wa kwanza alipojivuna yeye mwenyewe hakupata mema yako; mwingine asiye na maneno mengi, akajazwa na neema zako nyingi. Tazama machozi yangu, unipe nguvu, ee Kristu Mungu wetu, kwani wewe ni mpenda-wanadamu. *(mara moja).*

Utukufu kwa Baba . . *Sauti ya mnane.*

Ee Bwana Mwenyezi, hii machozi inalia naijua*:* Yaliokoa Ezekia toka milango ya mauti, kwa kahaba alisamehewa zambi zake, tena kwa hii Mtoza-Kodi alihakikishwa, hapana Mfarisayo. Unihesabie pamoja nao, ee Bwana, unihurumie.

Sasa na siku zote. . .

Elezo*: Tunaimba Theotokion ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma.*

Prokimenon ya hii siku ya Mungu*: Bwana anatawala, amevikwa utukufu (mara tatu).*

APOSTIKHA.

Elezo: *Tunaimba ku mwanzo wimbo ya Paraklitiki na kisha:*

Utukufu. . . . *Sauti ya tano.*

Kwa ajili ya zambi zangu macho yangu ni mzito na hayawezi kuinuka kwa kutazama nuru ya mbinguni; lakini kwa mfano wa Mtoza-Kodi unipe toba; ee Mwokozi, unihurumie.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Bikira Muheshimiwa kamili, uko hekalu na mulango, nyumba na kiti cha Mufalme; kwa wewe Kristu, Bwana na Mukombozi wangu, alifunuliwa kwa wale waliokaa katika giza; eko jua la haki, akitaka kwangaza wale walioumbwa kwa mufano wake kwa mikono yake; kwa hii mwimbiwa kamili, kwa sababu uko na uhodari ya umama mbele yake, upatanishe bila kuacha, kwa kuokoa nafsi yetu.

Elezo: *Sasa padri anasema ombi hii:*

Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

Msomaji: Trisagion: Mungu Mtakatifu...

Kisha Mwimbaji ataimba: Apolitikion ya Ufufuo ya Kristu na sauti ya hii Juma. Apolitikion ya Mtakatifu wa leo na Theotokion na sauti yake. Kisha Padri atafanya Kuaga.

SIKU YA MUNGU ASUBUI KWA ORTHROS.

Elezo: *Kisha Eksapsalmos, tunaimba Bwana ndiwe Mungu...Kathismata na Anavathmi ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma, kisha Prokimenon na Evangelion ya asubui. Kisha: tunasoma:* Tukiona Ufufuo wa Kristu*. . . Kisha zaburi 50 (51) na kisha tunaimba:*

Utukufu*. . . Sauti ya mnane.*

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana chemchem ya uzima; roho yangu ikeshe hekalu lako takatifu, ikichukua hekalu chafu la mwili wangu, lakini katika wema wako unitakase kwa mapendezi yako kubwa na mapendo yako ya huruma.

Sasa na siku zote*. . . Sauti ya mnane.*

Uniongoze njiani ya wokovu, ee Mzazi-Mungu, kwani nilichafua roho yangu kwa zambi, na kwa uvivu wangu nilitumia vibaya uzima wangu, lakini kwa maombezi yako takatifu uniopeo ku uovu wote.

Sauti ya sita

Unirehemu, ee Mungu sawasawa ni wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uufute makosa yangu.

Nikikumbuka wingi wa matendo yangu mabaya, mimi mwenye zambi, naogopa ile siku ya ajabu ya hukumu, lakini ninapotumainia rehema na ruhuma yako, napaza sauti kama Daudi*:* Unihurumie, ee Mungu, kadiri ya wema wako kubwa.

KANUNI

Wimbo ya kwanza. **Sauti ya sita. Os en ipiro pezefsas.**

Kwa mifano, Kristu anatualika tubadilishe maisha yetu*:* anamupandisha Mtoza-Kodi mwenyi kupenda unyenyekevu, na anatuonyesha namna gani Mfarisayo alishushwa sababu ya majivuno yake mwenyewe.

Tukiona ukubwa huko anapandishwa mwenye kujishusha, na shimo huko anangukia mwenye kujitukuza, fanana na fazila ya Mtoza-Kodi, kataa ukosefu wa Mfarisayo.

Tukitafuta ukubwa tutapoteza mema yote, lakini unyenyekevu inatutakasa kwa ubaya wote*:* enyi waaminifu tuipokee, tuzarau waziwazi sifa ya bure.

Alipotaka kupata unyenyekevu rohoni mwa Wafuasi wake, Mfalme wa ulimwengu akawaamuru wafanane na Mtoza-Kodi kwa unyenyekevu wake.

Ee Bwana, nalia na siache kulalamika kama Mtoza-Kodi, hivi nikipata njia ya roho yake*:* unihurumie mimi pia ambaye sasa najikaza kuishi na unyenyekevu.

THEOTOKION

Ee Bikira, mawazo yangu, matumaini yangu, roho yangu, mwili wangu na akili yangu nataka kuinua kwako; uniopoe kwa vishahishi vya Adui, kuja uniokoe siku ya hukumu.

IRMOS: Wakati Waisraeli waliposafiri kilindini kama pa inchi kavu, na walipoomuona Farao muzalimu ameangamizwa katika mawimbi, hapo wakapaza sauti*:* Tuimbeni wimbo wa ushindi kwa utukufu wa Mungu wetu.

Wimbo ya tatu. *Uk estin agios os si.*

Munyenyekevu anainuka toka kuzarauliwa kwa mateso, lakini roho yote yenyi kujivuna inabomolewa kwa ncha ya fazila, kwa hii kosa tuache tamaa mbaya.

Sifa ya bure inapunguza haki na hazina zake, unyenyekevu inasambaza mateso mengi*:* Ee Mwokozi, utupe tufanane na Mtoza-Kodi.

Kama Mtoza-Kodi, sisi pia tunajipigapiga kifua, na kwa toba tunakupazia sauti*:* Utuhurumie sisi wenyi zambi, ee Bwana, utuondolee zambi zetu.

Enyi waaminifu, tuache kiburi na majivuno, hasira ya upumbafu, majivuno yenyi kuchukiza na neno mbaya la Mfarisayo kwa Mungu.

THEOTOKION

Makimbilio yangu ni kwako peke yako, nakutumainia wewe, usizarau matumaini yangu, lakini nipate msaada wako; Ee Bikira, uniokoe kwa uovu wa Adui.

IRMOS*:* Hakuna hata mmoja aliye Mtakatifu kama wewe Bwana Mungu wangu; ulitukuza nguvu ya Waaminifu katika wema wako, na ulitutia msingi pa mwamba imara wa maungamo ya jina lako**.**

KATHISMA

Sauti ya ine. Takhi prokataleve.

Alipandishwa kwa kujishusha kwake, huyu Mtoza-Kodi aliyelia, akisikia haya ya zambi zake, na kuomba huruma kwa Muumba; majivuno ilipoteza haki yote ya Mfarisayo aliyejivuna; tutafuteni basi fazila, tuache zambi.

Utukufu... *Sauti umoja.*

Alipandishwa kwa kujishusha kwake huyu Mtoza-Kodi alilia zamani; alihakikishwa sababu alisema*:* Ee Bwana, unisamehe, nilitenda zambi, ni yeye tunafananisha toka zimuni huko tulianguka. Moyoni mwetu tutasema*:* Utusamehe kwa ajili ya zambi zetu, ee Mwokozi, peke yako Mpenda-wanadamu.

Sasa na siku zote. . .

Ee Bikira, ujiharikishe kupokea maombi tunayokutolea; Ee Bibi Mtakatifu kamili uyatoe kwa Mwana na Mungu wako; tuliza sikitiko ya wale wenye kukukimbilia; tengua uerevu wa shetani, haribu moto ya adui mwenye kushindana na watumishi wako.

KONTAKION

Sauti ya ine. Epefanis simeron.

Tukimbie majivuno ya Mfarisayo, tufunze unyenyekevu wa Mtoza-Kodi, tulilie zambi zetu tukimwambia Mwokozi*:* Utuhurumie, ee Bwana, peke yako uliye mwema.

KONTAKION INGINE.

Sauti ya tatu. I Parthenos simeron.

Kwa Bwana tutalia kama Mtoza-Kodi, na mbele yake tutasujudu kama waovu, kwani anataka wokovu wa watu wote na anasamehe roho zote zenye kutubu*:* na kwa ajili yetu alikuja mwilini, yeye Neno la Mungu wa milele pamoja na Baba.

IKOS

Ndugu, kila mumoja wetu ajinyenyekeze, kwa machozi na vilio tuhuzunikie zamiri yetu ili kwa siku ya hukumu ya milele tuwe safi na tupate usamehe; kwa sababu ni huko kuna mapumziko ya kweli, ile tunatumainia kuona siku moja na tunaombea, huko hakuna mateso,

huzuni na vilio, hii shamba la ajabu tena Edeni mpya Kristu anatupa, Yeye Neno la Mungu wa milele pamoja na Baba.

SINAKSARI.

Elezo: *Sasa ku mwanzo tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha Sinaksasi ya hii siku.*

Leo tunakumbuka mfano wa Evangeli wa Mfarisayo na Mtoza-Kodi.

Ukiishi kama Mfarisayo, unajitenga ku Hekalu. Kristu yumo ndani na munyenyekevu anamutazama.

Ee Muumba wa mbingu na dunia, pokea kwa Malaika wako wimbo wa Trisagion na Utatu pia kinywani mwa wanadamu.

Kwa maombi ya Watakatifu wote wenye kuimbia utukufu wako, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

KATAVASIES

Wimbo wa kwanza.

Wakati Waisraeli waliposafiri kilindini kama pa inchi kavu, na walipoomuona Farao muzalimu ameangamizwa katika mawimbi, hapo wakapaza sauti*:* Tuimbeni wimbo wa ushindi kwa utukufu wa Mungu wetu.

Wimbo wa tatu.

Hakuna hata mmoja aliye Mtakatifu kama wewe Bwana Mungu wangu; ulitukuza nguvu ya Waaminifu katika wema wako, na ulitutia msingi pa mwamba imara wa maungamo ya jina lako.

Wimbo wa ine.

Kristu ni nguvu yangu, Bwana wangu na Mungu wangu*:* Huu ni wimbo kimungu Eklezya Takatifu inatangaza, na moyo kutakasa inamuheshimu Bwana.

Wimbo wa tano.

Ewe Mungu mwema mno, nakuomba, angaza na nuru yako ya umungu roho za wapenda wako wenye kukesha mbele yako ili wakujue, ewe Neno la Mungu, Wewe Mungu wa kweli mwenye kutuondoa giza ya zambi.

Wimbo wa sita.

Wakati ninapoona bahari ya hii uzima inanyanyuliwa kwa tufani ya vishahishi, nakimbilia ku bahari yako ya amani na napaza sauti, ee Mungu wa wema*:* Komboa uzima wangu ku shimo.

Wimbo wa saba.

Katika tanuru ya moto Malaika akawamwangia Vijana washarifu umande, lakini moto ukawateketeza wakaldea kwa amri ya Mungu, na mzalimu akalazimishwa kuimba*:* Umetukuzwa, Bwana Mungu wa Baba zetu.

Wimbo wa mnane.

Tunamsifu, tunamuhimidi, na tunamusujudu Bwana.

Toka moto ukachirikiza umande kwa ajili ya Watakatifu wako na kwa maji ukawakisha sadaka ya mwenyi haki, kwani ulitimiza vitu vyote paka kwa mapenzi yako*:* Ee Kristu, tunakutukuza milele.

Wimbo wa tisa.

Kwa wanadamu haiwezekane kumuona Mungu ambaye hata Malaika hawasubutu kutazama, lakini Neno aliyejifanya mtu kwako alionekana kwa wenye kufa, ewe Safi kamili, na wakati tunamutukuza pamoja na majeshi ya mbinguni tunakutangaza mwenye heri.

EKSAPOSTILARIO

Elezo: *Sasa tunaimba Eksapostilarion ya Paraklitiki na sauti ya hii siku na kisha hii:*
Sauti ya mbili. Tis mathites sinelthomen.

Tutupilie mbali majivuno ya Mfarisayo, tufunze unyenyekevu kamili wa Mtoza-Kodi ili tuinuliwe tukisema pamoja naye*:* Ee Bwana, samehe watumishi wako; wewe uliyezaliwa kwa

Bikira, ee Kristu Mwokozi wetu, uliteswa msalabani kwa kutaka kwako, na kwa uwezo wako wa umungu ulifufua dunia pamoja nawe.

THEOTOKION. *Sauti umoja*

Muumba wa viumbe tena Mungu wa ulimwengu alichukua mwili wa mauti tumboni mwako, ee Mzazi-Mungu; alifanya kuwa mupya hali yangu yote yenyi kuharibika; sisi waaminifu tunakuimbia*:* Salamu, ewe utukufu wa ulimwengu.

MASIFU.

Elezo*: Tunaimba mbele wimbo 4 ya Ufufuo ya Kitabu Paraklitiki na kisha wimbo 4 ya hii kitabu.*

Ndugu tusiombe kama Mfarisayo, kwa sababu huyu mwenye kujipandisha anapaswa kujinyenyekeza; tujinyenyekeze kwa Mungu kwa mfano wa Mtoza-Kodi, na tuseme kama Yeye*:* ee Bwana unihurumie mimi mwenye zambi.

Mfarisayo aliposhindwa kwa majivuno yake, na Mtoza-Kodi alipojinyenyekeza kwa toba, wakaonekana wote wawili mbele yako, peke yako Bwana; wa kwanza alipojiivuna yeye mwenyewe, hakupata mema yako; mwingine asiye na maneno mengi, akajazwa na neema zako nyingi. Tazama machozi yangu, unipe nguvu, ee Kristu Mungu wetu, kwani wewe ni Mpenda-wanadamu.

Shairi: Usimame, ee Bwana, nyanyua mukono wako, usisahau masikinim kwa nini mwovu anazarau Mungu.

Sauti ya tatu.

Umetambua tafauti kati ya Mfarisayo na Mtoza-Kodi, ee roho yangu; kataa maneno ya majivuno ya wa kwanza, fanana na wa mbili kwa ombi la unyenyekevu na sema*:* Unisamehe, ee Bwana, mimi mwenye zambi, ee Mungu unihurumie.

Shairi: Nitashukuru Bwana kwa moyo wangu wote, katika baraza ya wenye haki, na katika makutano.

Sauti ya tatu.

Enyi waaminifu, tukatae sauti ya kiburi ya Mfarisayo; tufananishe ombi la Mtoza-Kodi lenye kujaa na sikitiko; tusitafute njia ya ukubwa, lakini tujishushe sisi wenyewe, kwa unyenyekevu tuseme mara ingine*:* utuhurumie, ee Bwana, kwa ajili ya zambi zetu.

Utukufu kwa Baba. *Sauti ya mnane.*

Ee Bwana, ulimuhukumu Mfarisayo aliyehakikisha mwenyewe akijivuna kwa matendo yake mema, na ulihakikisha Mtoza-Kodi aliyejishusha akiomba huruma yako; kwa sababu hausikilize maneno ya majivuno, lakini hauzarau moyo yenyi kuvunjika; wewe uliyeteswa kwa ajili yetu, utupe usamehe na neema ya wokovu.

Sasa na siku zote. . **THEOTOKION**

Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa u Kristu Mungu wetu, uliyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA.

SIKU YA MUNGU YA MWANA MUPOTEVU

SIKU YA POSHO KWA MANGARIBI

Elezo*: Waimbaji wataimba wimbo sita ya Paraklitiki na kisha hii wimbo mbili.*

Sauti ya kwanza. Idiomelon

Nimepanda zambi katika udongo safi na ya uzima; nimevuna masuke ya uzembe, nimefunga miganda ya matendo yangu; sikuyaweka katika kiwanja cha toba; lakini nakuomba, ee Mungu wangu, wewe mwenye kulima daima udongo wetu, lisha roho yangu kwa neema na rehema, uniweke katika rala zako za mbinguni na uniokoe. *(mara mbili).*

Wa ndugu, tutambueni uwezo wa fumbo kimungu, maana Mwana Mpotevu ametambua kosa lake kwa kurudi nyumbani mwa baba yako; kwa wema wake kubwa Baba anakuja kukutana naye kwa kumukumbatia; anamurudisha mara ingine katika utukufu wa nyumba yake, mbinguni anamutayarishia karamu ya siri; anamuchinjia mwana ngombe mwenye kunona ili tusharikie furaha yake, ya Baba anayetoa kwa mapendo, na hii ya Mwana-kondoo mwenye kujitoa kwa ajili yetu. *(mara mbili).*

Utukufu. . . *Sauti ya mbili.*

Mema gani nimejikatalia mimi mwenye mateso, nilikimbilia ufalme gani! Nimetumia vibaya mali nilipokea kwako, nilitembea mbali ya amri yako. Ole wako, ee roho yangu maskini, utatolewa kwa moto ya milele, lakini mbele ya mwisho umwambie Kristu Mungu wetu*:* Ee Bwana, unipokee kama Mwana-Mpotevu na unihurumie.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Elezo*: Tunaimba Theotokion ya Paraklitiki ya sauti ya hii Juma.*

Prokimenon ya hii siku*:*

Bwana anatawala, amevikwa utukufu *(mara tatu).*

APOSTIKHA.

Elezo*: Tunaimba ku mwanzo wimbo ya Paraklitiki na kisha:*

Utukufu. . . . *Sauti ya sita.*

Nimetumia vibaya mali Baba yangu alinipa, niliishi kati ya wanyama bila sababu, nilitamainia chakula cha nguruwe, nilikuwa na njaa, na sawa hakuna mutu alinipa chakula, nilirudi kwa Baba yangu mwema kamili, na kwa machozi nilimulilia*:* Uniweke kuwa sawa mumoja wa Watumishi wako, sistahili mapendo yako, lakini kwa wema wako uniokoe.

Sasa na siku zote. . .

Muumba na Mukombozi wangu, Bwana Kristu, ewe safi kamili, alitoka ku tumbo lako, na akinivaa, aliopoa Adamu toka apizo la kale; kwa hii tunakuita bila kuacha, ewe safi kamili, kwani wewe wiko Muzazi-Mungu na Bikira kweli, na tunasema Salamu ya Malaika*:* Salamu, ee Bibi Malkia, mulinzi na kivuli na wokovu wa nafsi yetu.

SIKU YA MUNGU ASUBUI KWA ORTHROS.

Elezo: *Kisha Eksapsalmos, tunaimba Bwana ndiwe Mungu...Kathismata na Anavathmi ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma, kisha Prokimenon na Evangelion ya asubui. Kisha: tunasoma:* Tukiona Ufufuo wa Kristu. . . *Kisha zaburi 50 (51) na kisha tunaimba:*

Utukufu. . . *Sauti ya mnane.*

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana. . . . . (*Angalia ukurasa 2).*

KANUNI

Wimbo ya kwanza

Sauti ya mbili. Tin Moseos odin.

Ee Yesu, pokea sasa toba yangu, nimekosa kama Mwana Mpotevu, kama yeye nilihangaika katika maisha yangu, nikichokoza hasira ya Mungu.

Kwa upumbafu nimetumia vibaya mali ya kimungu ulinipa zamani; kwa maisha yangu ya upumbafu nimejitenga mbali nawe; unipokee, ee Baba Mwema kamili, maana narudi Kwako.

Ee Bwana, unipokee kama Mwana Mpotevu zamani, unifungulie mikono yako ya ubaba, kwa shukrani nitaimbia utukufu wako na wema wako.

THEOTOKION

Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, ee Bwana, unionyeshe mema yako na zidisha alama za wema wako ukizima wingi wa zambi zangu.

IRMOS: Imba, ee roho yangu, wimbo wa Musa*:* Bwana ni msaada wangu na mlinzi wangu, ni yeye aliyeniokoa, ndiye Mungu wangu, na nataka kumutukuza.

Wimbo ya tatu.

Stirothenta mu ton nun.

Nilipopoteza haki ya kweli, nilifwata mwendo wa tamaa zangu, lakini kama Mwana-Mpotevu, kubali kunipokea, ee Bwana.

Kama Mwana mpotevu, nakulalamikia*:* ee Baba, nimekosa; unikumbatie kama ulivyomutenda yeye, usinitupe mbali nawe.

Ee Kristu, fungua mikono yako, na kwa huruma yako unipokee, maana narudi toka inchi ya mbali, ile ya tamaa na zambi.

THEOTOKION

Ewe Mzuri katika wanawake wote, Bikira Safi kamili, tajirisha roho yangu ilio katika umaskini, uipe kuona ile iliyo nzuri ili niweze kukutukuza.

IRMOS. Ee Bwana, jangwa kavu ya roho yangu uifanye iwe yenyi kutoa na yenyi neema, wewe mwenye kukesha ku ustawi wa mema yote katika wema wako wa umungu.

KATHISMA

Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.

Ewe Bwana, ujiharikishe kunifungulia mikono yako ya ubaba, kwani nilitumia vibaya uzima wangu; tazama hazina ya huruma yako isiyokuisha, ee Mwokozi, usizarau umaskini wa moyo

wangu; kwako, ee Bwana, napaza sauti nikijaa na sikitiko*:* ee Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.

Utukufu kwa Baba. . . *(mara ingine hii).*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.

Ee Bikira usiyeolewa, Mtakatifu Mzazi-Mungu peke yako mwenye kutulinda na kutuchunga, okoa taifa la waaminifu wenye kukutumainia wewe kwa kila makamio na hatari yote inaamwelemea; ee Bikira, umuombe Mungu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

KONTAKION.

Sauti ya tatu. I Parthenos simeron.

Nilipojikatalia utukufu wako wa ubaba, nilitumia vibaya mali ulinipa, ndio maana nakutolea toba ya Mwana Mpotevu*:* Nimekopsa mbingu na wewe pia; ee Baba wa huruma, unipokee mimi mwenye kutubu na uniweke kuwa sawa mumoja wa watumishi wako.

IKOS

Kila siku Mwokozi alisema sana na sisi, kwa kutufundisha kwa sauti lake mwenyewe*:* Tusikilize hii Maandiko inatufundisha juu ya Mwana Mpotevu anayetubu, tufananishe kuongoka kwake kwa ajabu. Kwa Mungu wetu mwenye kuona siri zetu zote tuseme na unyenyekevu wa roho zetu*:* Ee Baba wa huruma, tumekukosea, sababu hii hatustahili tena kuitwa wana wako; lakini kwa sababu ya mapendo unatupenda nayo, unipokee mimi mwenye kutubu, na uniweke kuwa sawa mumoja wa watumishi wako.

SINAKSARI.

Elezo: *Sasa ku mwanzo tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha Sinaksasi hii.*

Leo tunakumbuka mfano wa Evangelio wa Mwana Mpotevu ambao wapadri wetu watakatifu waliweka pa fasi ya pili katika Triode.

Mpotevu, kama mimi, jongea bila woga maana Mungu anawafungulia mlango wa moyo wake.

Kwa mapendo isiyokadirika unayopenda nayo wanadamu, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

KATAVASIES.

Sauti ya mbili.

Wimbo wa kwanza.

Imba, ee roho yangu, wimbo wa Musa*:* Bwana ni msaada wangu na mlinzi wangu, ni yeye aliyeniokoa, ndiye Mungu wangu, na nataka kumutukuza.

Wimbo wa tatu

Ee Bwana, jangwa kavu ya roho yangu uifanye iwe yenyi kutoa na yenyi neema, wewe mwenye kukesha ku ustawi wa mema yote katika wema wako wa umungu.

Wimbo wa ine.

Nabii alipoona Bikira amekuzaa akatangaza. akasema*:* Bwana, nilisikia sauti yako na nimejaa na woga, maana umetoka ku Themani, ee Kristu, ku mulima takatifu wa kivuli.

Wimbo wa tano.

Usiku umepita, na sasa hivi jua limeonekana litakaloangaza ulimwengu kwa nuru yake, ndiyo maana kundi la Malaika wote wanaimba wimbo wao kwa kutukuza, ee Kristu Mungu wetu.

Wimbo wa sita.

Mungu Mwokozi, nazama katika shimo ya zambi, nazama katika bahari ya hii uzima, lakini kama Yona alivyotoka tumboni mwa samaki, uniiondoshe ku shimo ya tamaa na uniokoe, ee Bwana.

Wimbo wa saba.

Katika tanuru ya moto Vijana wakawaza wakeruvi wakati walipoimba*:* Utukuzwe, ee Mungu wetu, ulileta hukumu ya haki, ni kwa makosa yetu unatutendea hivi, utukufu na sifa ya milele ni kwako.

Wimbo wa mnane.

Tunamsifu, tunamuhimidi, na tunamusujudu Bwana.

Kwa huyu ambaye katika kichaka mulimani wa Sinai mbele ya Musa akatangulia kuonyesha fumbo ya ajabu ya Bikira, imbeni wimbo wa utukufu*:* Utukufu kwake milele.

Wimbo wa tisa.

Nani mwenyi mauti alisikia hii? Na nani amekuisha kuona Bikira kupata mimba na kuzaa mutoto bila uchungu? Lakini hii ni fumbo yako ya ajabu, Mtakatifu Mzazi-Mungu, tyunakutukuza.

EKSAPOSTILARION

Elezo: *Sasa tunaimba Eksapostilarion ya Paraklitiki na sauti ya hii siku na kisha hii: Sauti ya mbili. Ginekes akutisthite.*

Ee Mungu Mwokozi, hazina ya mema ulinipa nimetumia vibaya; kwa bahati mbaya nimeiharibu; nimeipoteza kwa kuishi mbali nawe pamoja na wenzangu wabaya; lakini sasa ninaporudi kwako, ee Baba wa mapendo, kama ulivyomupokea zamani Mpotevu, unipokee mimi pia na uniokoe.

Ingine. Sauti Umoja.

Ee Bwana mali yako ulinia nimeipoteza, nilisaidia mashetani wabaya, mimi maskini, lakini wewe Mwokozi kwa mapendo ya roho yako; unihurumie mimi mpotevu na safisha zambi yangu, na unipe, ee Bwana, nguo yangu nzuri katika Ufalme wako.

THEOTOKION. Sauti Umoja.

Ee Bikira Mtakatifu tena Mzazi-Mungu, utukufu wa Mitume, wa Mashahidi, wa ma Nabii na wa watakatifu wote, inamisha roho ya Mwana na Bwana wako kwa ajili ya watumishi wako, wakati atakapoketi katika kiti chake cha ufalme kwa kuhukumu kila mumoja wetu kadiri ya matendo yake.

MASIFU

Sauti ya mbili.

Elezo: *Tunaimba mbele wimbo 5 ya Ufufuo toka Paraklitiki na kisha wimbo 3 ya hii kitabu.*

Sauti ya mbili

Ee Bwana, nakutolea toba ya mwana mupotevu*:* Nimekosa mbele yako, niliharibu hazina ya neema yako; pokea kutubu kwangu, ee Mwokozi, na uniokoe.

Shairi*:* Nitashukuru Bwana kwa moyo wangu wote, katika baraza ya wenye haki, na katika makutano.

Sauti ya ine.

Ee Mungu wa wema, kama Mwana Mpotevu, mimi pia narudi kwako kisha kuishi mbali nawe; ee Baba, nimetumia vibaya mali ulinipa; pokea kutubu kwangu, ee Bwana, na unihurumie.

Shairi*:* Usimame, ee Bwana, nyanyua mukono wako, usisahau masikinim kwa nini mwovu anazarau Mungu.

Sauti ya mnane.

Kwa upumbafu nilipoteza mali yote ya baba, nimekuwa peke yangu maskini, lakini sawa sikuweza kuwavumilia, narudi kwako, ee Baba Mwema kamili, na nakulalamikia*:* Nimekosea mbingu na wewe pia, sistahili tena kuitwa mwana wako, uniweke kuwa sawa mumoja wa watumishi wako na unihurumie.

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya sita.*

Ee Baba wa mapendo nilijitenga mbali nawe; usiniache usinikatalie ufalme wa mbinguni, kwa sababu Adui mbaya ameniondolea, ameninyanganya mali yangu yote; kwa upumbafu nilitumia vibaya mali yangu ya roho, lakini nasimama na narudi kwako nikisema*:* uniweke kuwa sawa mumoja wa watumishi mbaya na kunivika nguo yangu ya kwanza kwa wema wako.

Sasa na siku zote. . **THEOTOKION**

Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa u Kristu Mungu wetu, uliyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA .

MU POSHO (SABATO) YA WAFU.

SIKU YA TANO KWA MANGARIBI (ESPERINOS).

Elezo*: KIsha:* «Bwana nimekuita...» *Tunaimba wimbo ya paraklitiki 3 na kisha hii wimbo 3 ya Triodi.*

Sauti wa mnane. O en Edem paradisos.

Enyi waaminifu, leo tuwakumbuke marehemu waaminifu wote waliolala na heri tangu milele; tumuimbie Bwana na Mwokozi wetu na kumuomba sana kusudi kwa wakati wa hukumu awahukumu na haki kwa baraza ya Mungu wetu atakayeketi kuhukumu dunia yote na wapate kusimama na furaha kuume kwake pamoja na wenye haki na Watakatifu kwa kuriti nuru na amani, na wawe wenye kustahili ufalme wake mbinguni.

Ee Mungu Mwokozi, kwa damu yako unakomboa wanadamu, kwa lufu yako unatuokoa toka uchungu wa mauti, kwa Ufufuo wako unatupatia uzima wa milele; ee Bwana, leta mapumziko kwa waaminifu wote waliolala na imani katika miji ao jangwa, inchini, baharini wala popote, wafalme ao mapadri, maaskofu, watawa wa waaminifu, wa umri yote na wa daraja yote, uwastahilishe katika ufalme wako wa mbinguni.

Ee Kristu, kwa Ufufuo wako katika wafu, mauti haina na uwezo juu ya marehemu waaminifu; ndio maana tunakuomba sana uwape watumishi wako mapumziko katika uwanja wa Mungu na katika kifua cha Abraamu, kwa watumishi wako wote, tangu Adamu mpaka leo, waliokutumikia kwa kukuabudu na moyo safi, baba zetu na ndugu zetu, wazazi wetu, marafiki zetu, mutu wowote aliyetimiza na imani mapashwa yako; wote wale unaita kwako kwa namna mbalimbali*:* ee Bwana, uwastahilishe katika ufalme wako wa mbinguni.

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya mnane.*

Nalia na nalalamika wakati ninawaza mauti, wakati ninaona imelala kaburini bila hali, bila utukufu na bila uzuri, neema tuliyopewa kwa mfano wa Mungu*:* Ni fumbo ya ajabu kuliko bahari

yetu! Namna gani unashuka kaburini? Namna gani tunafungwa kwa mauti? Kama ilivyo Maandiko, ni kwa amri ya Mungu anayewapa wafu mapumziko.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Elezo*: Tunaimba Theotokion ya Paraklitiki ya sauti ya hii Juma.*

KUINGIA

Mwangaza upole. . .

Elezo*: Pahali pa fasi ya Prokimenon tunaimba na Sauti ya tatu:*

Alliluia *(mara tatu).*

Shairi*:* Heri mutu wewe unayemuchagua na kumukaribisha ajaw viwanjani mwako.

Alliluia *(mara tatu).*

Shairi*:* Ukumbusho wako vizazi hata vizazi, ee Bwana.
Alliluia *(mara tatu).*

Kisha: Ee Bwana, utujalia mangaribi hii kutulinda na zambi. . .

APOSTIKHA.

Elezo*: Tunaimba ku Kitabu ya Paraklitiki ya hii siku. Kisha:*

Utukufu. . . *Sauti ya sita.*

Kwa neno lako la uumbaji uliniruhusu nizaliwe na niishi; kwa kunifanya mimi kuwa mutu mzima uliunganisha ndani yangu yenyi kuonekana na isiyoonekana; kwa udongo uliumba mwili wangu, ulinipa roho kwa pumzi yako ya umungu na yenyi kuleta uzima; ee Mungu Mwokozi, uwape pia watumishi wako mapumziko katika makao ya wenye haki inchini mwa wazima.

Sasa na siku. . . **THEOTOKION**. *Sauti umoja.*

Ee Kristu, kwa maombezi ya huyu aliyekuzaa, ya Manabii, ya Mitume, ya Mashahidi, ya Maaskofu, ya wenye haki, ya wenye heri, na ya watakatifu wote, uwape marehemu watumishi wako mapumziko ya milele.

Apolitikion. *Sauti ya mnane*.

Ee zimu ya hekima yenyi kupenda wanadamu na kuongoza vitu vyote kwa ajili ya wokovu, peke yako Muumba ambaye kila mumoja anapokea ile yenye kumufaa, ee Bwana, leta mapumziko kwa roho za watumishi wako, kwa sababu matumaini yao ni kwako, ewe Fundi wetu, Muumba wetu tena Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Kwa sababu matumaini yao ni kwako, ewe Fundi wetu, Muumba wetu tena Mungu wetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Wewe ni boma na bandari yetu ya wokovu, muombezi wa kweli kwa Mungu uliyezaa, ee Bikira Mzazi-Mungu, ndiwe wokovu wa waminifu.

Elezo: *Kisha Sala ya Mangaribi tunafanya Sala ya Panihida kwa mapumuziko ya wafu. Tafuta hii sala mu Kitabu ya Saa Mukubwa.*

SABATO KWA SALA ASUBUI.

Elezo*: Kisha somo ya Eksapsalmos tunaimba na Sauti ya mnane.*
Alliluia *(mara tatu).*

Shairi*:* Heri mutu wewe unayemuchagua na kumukaribisha ajaw viwanjani mwako.

Alliluia (mara tatu).

Shairi*:* Ukumbusho wako vizazi hata vizazi, ee Bwana.

Apolitikion*:* Ee zimu ya hekima yenyi kupenda . . . Utukufu. . . Sasa. . . *(Ona yulu, mu sala ya mangaribiu).*

MAHIMIDI YA WAFU.

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.

Kundi la Watakatifu, lilipata chemchem ya uzima na mulango wa Paradizo, na mimi nitapata njia kwa kutubu, mimi ni kondoo mupotevu, uniite tena, ee Mwokozi, na uniokoe.

Ee Bwana, umehimidiwa U. . .

We wa zamani, uliniumba toka si kitu, na ulinisifu kwa sura yako takatifu, lakini juu ya kuvunja amri, ulinirudisha tena ku udongo kule ulinitosha, kwa mufano wako sasa unirudishe, na ufanye mara ingine uzuri wangu wa kwanza.

Ee Bwana, umehimidiwa U. . .

Mimi ni sura, ya utukufu wako usiyonewa, hata niko na alama ya zambi, ee Rabi unirehemu kiumbe chako, na unisafishe kwa wema wako, tena unipatie inchi ninayotamania, unifanye mara ingine mwana inchi wa Paradizo.

Ee Bwana umehimidiwa U. . .

Ee Mungu, pumzisha mtumishi (wa) wako, na u(uwa)mupangishe katika Paradizo, fasi ya kundi la watakatifu, ee Bwana, na wenyi haki watangaa sawa nyota za mwangaza, u(uwa)mupumzishe mu(wa)tumishi wako huyu (hawa) anayelala(wanao), umusamehe (uwa) zambi zake (zao) zote.

Utukufu kwa Baba na kwa Bwana na kwa Roho Mtakatifu

Tuimbe na kupaza sauti, kwa uaminifu mianga tatu ya umungu moja, ewe Mtakatifu, Baba wasiyo mwanzo, Mwana aliye na Baba bila mwanzo na Roho Mtakatifu, ; angaza sisi tuliokuabudu kwa imani, na utuopoe ku moto ya milele.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Salamu Muheshimiwa, uliyemzaa Mungu mwilini, juu ya wokovu wa wote, kwa ajili yako kabila la wanadamu ilipara wokovu, katika yako tutapata Paradizo, Mzazi-Mungu, safi mbarikiwa.

Alliluia, Alliluia, Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu. *(mara tatu).*

Maombi ya wafu.

Shemasi*:* Utuhurumie, ee Mungu, mu huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Tena tunakuomba kwa ajili mapumziko ya roho za marehemu watumishi wa Mungu ili makosa yao ya kujua na yasiyokujua yasamehewe.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Ili Bwana Mungu aweke roho zao kule wamepumzika wenye haki.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Tumuombe Kristu Mungu wetu na Mfalme wetu wa milele awape rehema yake, maondoleo ya makosa ya ufalme wa mbinguni.

Waimbaji*:* Uwape, ee Bwana.

Shemasi*:* Tumuombe Bwana.

Waimbaji*:* Bwana hurumia.

Padri*:* Ee Mungu wa roho na wa mwili, uliyeshinda lufu na kumuharibu shetani, wewe uliyeleta uzima duniani, leta, ee Bwana, mapumuziko kwa roho ya m(wa)tumishi wako (jina lake), pahali pa mwangaza, pa majani mazuri, pa mapumziko, kule kunakimbia maumivu, sikitiko na masumbuko. Umusamehe zambi zake(zao) zote a(wa)litenda kwa sauti, kwa matendo na kwa mawazo, kwa sababu wewe ni Mungu mwema na mpenda-wanadamu, kwani hakuna mutu hata moja, anakaa mu uzima huu pasipo kufanya zambi, kwa sababu wewe peke yako msiye zambi, haki yako, ni haki ya milele, na amri yako ni ya kweli.

Kwa kuwa wewe ni ufufuo, uzima na mapumziko ya mu(wa)tumishi wako (jina lake) huyu (hawa) a(wa)melala, Kristu Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu pamoja na Baba wako wasipo mwanzo na Roho Mtakatifu wako kamili. Mwema, Mpaaji wa uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Waimbaji*:* Amina.

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya tano.

Ee Mungu Mwokozi, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu, pamoja na wenye haki pumzisha watumishi wako na uwaruhusu wakae katika uwanja wako, usihesabie makosa yao ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Utukufu. . . Sasa. . . **THEOTOKION**.

Ee Kristu Mungu wetu uliyezaliwa kwa Bikira sababu ya kuangazia ulimwengu, kwa maombezi yake utufanye sisi kuwa wana wa nuru, ee Bwana, utuhurumie.

KANUNI

Wimbo ya kwanza.

Sauti ya mnane.

IRMOS. Enyi mataifa, tumuimbieni Mungu wetu aliyefanya maajabu kwa kuwaondoa waisraeli katika utumwa, tuimbeni wimbo wa ushindi tukisema: Tutakuimbia wewe peke yako Bwana wetu.

WIMBO

Wote tumuombe Kristu tukiwakumbuka leo wafu wote ili aokoe kwa moto ya milele waaminifu waliolala kwa matumaini ya kupata uzima wa milele.

Ee Kristu uliye shimo ya hukumu, kwa hekima ulipimia kila mumoja mwisho ya uzima yake, saa na kazi; kwa wale wenye kulala kaburini, uwaokoe, ee Mwamzi wa huruma.

Wewe mwenyi kumaliza maisha yetu, kwa wema wako, ee Bwana, uwape wale wenye kuamka toka usingizi wao kisha giza ya hii uzima, wafalme, mapadri na wakristu wote, wakuwe wana wa nuru ya milele.

Ee Bwana wale waliongamizwa kwa wawimbi, wale waliouawa kwa vita, wale waliouawa kwa mtetemeko wa inchi, wale waliouawa kwa wauaji, wale walioteketezwa kwa moto, uwape sehemu ya uriti wa Watakatifu.

Ee Mungu Mwokozi na Muumba, unapofunga macho kwa uovu wa wanadamu wa kizazi hata kizazi na wa daraja yote, uwalinde ili uwachilie wakati watakapohukumiwa mbele yako.

Utukufu kwa Baba. . .

Naimbia hali moja ya watu wa tatu katika Mungu mmoja, imungu moja wa Baba na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu ufalme kubwa wa milele.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira usiyeolewa, uko kweli mbingu duniani, uliye juu kabisa kupita nyota zote za mbinguni, kwani Bwana alitoka kwako, Yeye Juu ya haki kwa kuangazia ulimwengu.

WIMBO WA MBILI.

IRMOS. Tazameni na oneni, ni mimi niliye Mungu wenu, niliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati, na karibu ya mwisho wa nyoka nilizaliwa kwa Bikira Mtakatifu kamili, sababu ya kumukomboa Adamu baba yenu wa kwanza na kumuopoa toka zambi.

WIMBO

Tazameni na oneni, ni mimi niliye Mungu wenu, niliyeamua kuweka mwisho wa uzima wote na kuwaondoa kaburini mpaka uzima wa milele wale waliolala kwa matumaini ya ufufuo wa milele.

Ee Bwana, toka pande ine za ulimwengu kusanya waaminifu wote waliokufa duniani, baharini wala katika mito, poromoko la mto, birika kubwa na viziwa na wamekuwa mateka ya nyama kali ya pori, ya watambaa-inchi na ya ndege*:* Ee Bwana, kwa wafu hawa wote uwape mapumziko.

Ee Bwana, zamani mkono wako ulitenga hewa, moto, udongo na maji; lakini siku ya kurudi kwako duniani mara ya mbili utakusanya watu wote wenyi kutawanyika katika pano zote ine za dunia sababu ya kuwafufua ukiwasamehe zambi zao.

Ee Bwana, siku ya kuja kwako mara ya mbili duniani itakuwa ya ajabu wakati utakapokuja kama umeme kufufua viumbe vyote juu ya hukumu, lakini wale waliishi katika imani yako wakufikie ili waishi pamoja nawe.

Utukufu kwa Baba. . .

Umungu kamili na moja katika watu tatu, Baba asiyezaliwa Mwana wa pekee na Roho Mtakatifu anayetoka kwa Baba na kufunuliwa na Mwana, ubwana na ufalme wa asili moja, okoa watu wote.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Kuzaa kwako kwa ajabu ni isiyokadirika, ee Bikira tena Mzazi-Mungu; namna gani unaweza kupata mimba na kuwa bikira? Na kuzaa mtoto bila kujua mume? Ni siri ya Neno la Mungu aliyezaliwa kwako kwa namna ya ajabu anafanya ulimwengu mupya na sheria zake.

WIMBO WA TATU.

IRMOS. Ee Neno la Mungu uliyesabitisha mbingu kwa mkono wako, kwa nuru ya maarifa yako ya kweli utusabitishe na sisi pia: kwa maana tunakutumainia wewe.

WIMBO

Ee Bwana, wale waliomaliza safari ya uzima wao katika utukufu na ibada, uwape taji ya haki na fanya ili wapate mema ya milele.

Ee Bwana, wale walioondolewa kwa rafla katika hii uzima, kwa radi, kwa baridi wala kwa kila namna ya mateso, uwape mapumziko wakati utakapojaribu watu wote kwa moto.

Ee Kristu, wale wenye kuvuka daima bahari ya hii uzima ya mahangaiko uwaongoze mpaka kwa bandari ya uzima yako ya milele, imani ya Orthodokse iwasaidie kuwa njia.

Ee Bwana Mungu wetu, wale waliraruliwa kwa nyama ya bahari, wale walikuwa chakula cha ndege za anga, kwa haki yako uwafufue siku ya mwisho wakati utakapokuja katika utukufu wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Naona katika roho umoja wa watu tatu usiyotengana, nawakusanya wote pamoja kwa kuwatambua*:* kama katika mkusanyo mmoja wa nuru munakazana alama tatu za nuru yao ya ushindi.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ajabu ya fumbo yako inapita ufahamu*:* Ulizaa mtoto bila mume, kisha kuzaa ulichunga ubikira wako, ndio maana malaika wengi na wanadamu wote wanakuimbia milele.

KATHISMA.

Sauti ya tano. Ton sinanarhon Logon.

Ee Mwokozi, ulikufa msalabani kwa ajili yetu, ulishinda hadeze na ulifufua wafu*:* Ee Bwana, kwa wema wako wa umungu pumzisha marehemu wetu; ee Chemchem ya uzima, kwa rehema yako kubwa uwastahilishe katika ufalme wa mbinguni.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ujiharikishe kutusaidia na kutulinda, onyesha huruma yako kwa watumishi wako, ee Bikira Mtakatifu, tuliza mawimbi ya mawazo yetu ya upumbafu, ee Mzazi-Mungu kufanya yote ile unapenda.

KONTAKION.

Pamoja na Watakatifu pumuzisha, ee Kristu, roho ya watumishi wako, mu fasi pasipo umivu, bila sikitiko, bila muchoko, lakini uzima wa milele.

IKOS.

Ee Bwana, peke yako ni msiyekufa, Fundi na Muumba wa wanadamu; sisi wenye kufa tulioumbwa kwa udongo, tutarudi kwa udongo kama alivyoamuru Muumba wakati aliniambia*:* Wewe ni udongo na utarudi kwa udongo; ni huko tunaenda sisi wote wenyi kufa, na kama maombolezi tunaimba*:* Alliluia.

SINAKSARI.

Elezo: *Sasa ku mwanzo tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha Sinaksasi hii.*

Leo, kama walivyotuamuru wa Padri wetu Watakatifu, tunakumbuka waaminifu wote ambayo tangu wamelala na ibada katika matumaini ya ufufuo kwa ajili ya uzima wa milele.

Ee Neno, sahau makosa ya wafu, na roho yako tajiri kabisa ya rehema isiwe kali.

Leta, ee Bwana , ku roho za marehemu, fasi katika hema za wenye haki na utuhurumie sisi wote, wewe peke yako uliye wa milele. Amina.

KATAVASIES

Sauti ya mnane

Wimbo wa kwanza.

Enyi mataifa, tumuimbieni Mungu wetu aliyefanya maajabu kwa kuwaondoa waisraeli katika utumwa, tuimbeni wimbo wa ushindi tukisema*:* Tutakuimbia wewe peke yako Bwana wetu.

Wimbo wa mbili

Tazameni na oneni, ni mimi niliye Mungu wenu, niliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati, na karibu ya mwisho wa nyoka nilizaliwa kwa Bikira Mtakatifu kamili, sababu ya kumukomboa Adamu baba yenu wa kwanza na kumuopoa toka zambi.

Wimbo wa tatu.

Ee Neno la Mungu uliyesabitisha mbingu kwa mkono wako, kwa nuru ya maarifa yako ya kweli utusabitishe na sisi pia*:* kwa maana tunakutumainia wewe.

Wimbo wa inne

Ee Neno, Nabii mwenyi kuongozwa na Mungu alitambua umwilisho wako ku mlima wa kivuli aliye peke yake Mzazi-Mungu, na kwa woga alitukuza uwezo wako.

Wimbo ya tano.

Ee Mungu, roho yangu kwa sala inaongojea alfajiri yako, maana nuru ni amri yako; kwa hii, basi, angaa akili yangu, ee Rabi na uniongoze mu njia ya uzima.

Wimbo wa sita

Bwana mpenda-wanadamu, unipokee: zambi zangu zimenizunguka, ee Mungu wa rehema, nasujudu mbele yako; kama Nabii, ee Bwana, uniokoe.

Wimbo wa mnane

Huyu aliyetukuzwa juu ya mlima takatifu na kumufunulia Musa katika kichaka cha moto siri ya Mama bikira daima ni Bwana, mumuimbieni, atukuzeni milele.

Wimbo wa tisa

Huyu alifunulia Mtunga sheria kuzaa kwa fumbo kwa Bikira daima kule mlima katika kichaka cha moto kwa ajili ya wokovu wetu, tunamutukuza kwa daima nyimbo zetu.

EKSAPOSTILARION.

Sauti ya tatu. O Uranon tis astris.

Ee Mungu, uko Rabi wa wazima na wafu*:* Pumzisha watumishi wako katika hema ya wateule; na hata walitenda zambi, Mungu Mwokozi, hawatengwe mbali nawe.

Ingine. **.**

Sauti ya mbili. Ginekes akutishtite.

Ee Bwana, pumzisha watumishi wako katika inchi ya wazima, pahali hakuna mateso sikitiko na malalamiko; kwa mapendo yako, samehe zambi zote walizotenda katika hii uzima, kwani wewe peke yako ni msiye na zambi, peke yako tena mwenye rehema, ee Rabi wa wazima na wafu.

Ingine Umoja**. THEOTOKION**.

Ee Maria Bikira wa Mungu, umuombe daima Kristu kwa ajili ya sisi watumishi wako, pamoja na Manabii wenye kuongozwa, na kundi la Mashahidi, la Mapadri wenye heri na la watakatifu wote ili tuwe na sehemu ya ufalme wa mbinguni.

MASIFU.

Elezo*: Tunaimba wimbo 4:*

Sauti ya ine. O en Edem Paradisos.

Njooni enyi ndugu wote, tuone mbele ya mwisho uzaifu wa hali yetu ya udongo, tutambue uzaifu wa mwili wetu, maana mwanadamu ni uvumbi, uharibifu na chakula cha nondo, mifupa ya kukauka, bila pumuzi ya uzima; tuone kaburi*:* Wapi utukufu, wapi uzuri? Wapi ulimi wa msemaji, wapi uso, wapi macho? Yote ni uvumbi na giza, lakini Wewe, Mungu Mwokozi, okoa watumishi wako.

Mara ngapi mwanadamu anadanganyika wakati anajivuna na wakati anawaza mawazo ya bure, yeye ambaye sasa hivi atakuwa takataka! Kwa nini mwanadamu haujui matope inafanya mwili wake? Kwa nini hii ambatano kwa udongo, kwa sababu ni huko tunatoka? Kama sisi tuko pamoja na Kristu, na kwa nini hatuelekeze moyo wetu kwake tukiacha vitu visivyodumu juu ya uzima wa milele? Kwani uzima wetu ni Kristu aliye nuru ya roho zetu.

Ee Mwokozi, kwa mkono wako uliumba Adamu, ukamuweka kwa mpaka wa uzima wa milele na mauti, ulimuumba mwenyi kujaliwa neema na uzima; kisha ulipomuokoa toka mauti ukamurudishia uzima wake wa kwanza; ndio maana, ee Rabi, tunakuomba*:* Pumzisha watumishi wako ulichukua pamoja na wenye haki katika kundi la wateule, andika majina yao katika kitabu

cha uzima, wakati Malaika mkuu atawaamusha kwa sauti ya baragumu, uwastahilishe ufalme wa mbinguni.

Kristu alifufuka, alivunja minyororo ya Adamu na ya wanadamu wote, aliharibu nguvu ya Hadeze, Muwe na moyo, enyi wafu*:* mauti imeuawa, Hadeze imetualiwa, Kristu ameshinda msalabani, amefufuka na ameipatia mwili wetu uzima wa miele, ametufufua pamoja naye; tumesharikishwa kwa ufufuo wake; kwa hii utukufu amewastahilisha wote wale waliomutumainia kwa haki na furaha.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu. Sauti ya mbili.*

Kila mutu anafifia na kutoonekana kama ndoto wala ua, lakini wakati baragumu italia itakikisa wafu wote na wataamka sababu ya kwenda kukutana na wewe, ee Kristu Mungu wetu; hapo, ee Rabi, weka marehemu wetu katika makao ya wenye haki, weka roho za watumishi wako katika uzima wa milele.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Salamu, ee Bikira Mzazi-Mungu, Hekalu ya Mwokozi isiyoweza kuharibika, Patakatifu ambapo Nabii alisema*:* takatifu ni hekalu yako, ya ajabu kwa wenye haki.

APOSTIKHA

Elezo*: Tunaimba wimbo ya Paraklitiki na sauti ya ile juma na kisha:*

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita*

Zamani Adamu alipata uchungu wakati alionja tunda lililokatiziwa katika shamba la Edeni, maana nyoka alimuingiza sumu yake, na katika yeye mauti yenyi kuangamiza wanadamu imeingia duniani; lakini Bwana alikujam, aliua yule nyoka na akatupatia mapumziko; tumulalamikia*:* Ee Mungu Mwokozi okoa wale ulichukua pamoja nawe, na uwapumzishe kati ya wateule wako.

Sasa na siku zote. . . Sauti umoja.

Wewe ni Mungu wetu, kwa hekima uliumba ulimwengu na kuijaza; ee Kristu, ulituma Manabii kutangaza kuja kwako kwa mara ya mbili na Mitume kutangaza matendo yako makubwa*:* Wamoja waliagua kuja kwako, wengine kwa ubatizo waliongazia mataifa; kwa mateso yao Mashahidi walipata chombo cha matumaini yao na wanaomba mbele yako pamoja na huyu aliyekuzaa. Ee Mungu, pumzisha roho za wale ulichukua na uwafanye kuwa wenye kustahili ufalme wa mbinguni, wewe ambaye kwa kuzima hukumu yangu, uliteswa msalabani, ee Mwokozi na Mungu wangu.

Kisha Padri**:** Ni neno jema kushukuru Bwana na kuimba sifa kwa jina lako, ee wewe uliye juu; kuonyesha wema wako asubui na uaminifu wako kila usiku. (Zab. 92, 1).

Elezo: *Sasa tunasoma Trisagion na kisha tunaimba apolitikia ya asubui, kisha Eksapsalmos. Nikusema:*

Apolitikion. *Sauti ya mnane.*

Ee zimu ya hekima yenyi kupenda wanadamu na kuongoza vitu vyote kwa ajili ya wokovu, peke yako Muumba ambaye kila mumoja anapokea ile yenye kumufaa, ee Bwana, leta mapumziko kwa roho za watumishi wako, kwa sababu matumaini yao ni kwako, ewe Fundi wetu, Muumba wetu tena Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Kwa sababu matumaini yao ni kwako, ewe Fundi wetu, Muumba wetu tena Mungu wetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Wewe ni boma na bandari yetu ya wokovu, muombezi wa kweli kwa Mungu uliyezaa, ee Bikira Mzazi-Mungu, ndiwe wokovu wa waminifu.

Elezo: *Sasa, kama tunataka,tunasoma na Saa wa kwanza.*

Elezo: *Ndani ya Liturgia Takatifu tunaimba Ushirika hii:*

Heri wale uliowachagua na kuwapokea, ee Bwana; tena ukumbusho wago mpaka kizazi kwa kizazi. Alliluya.

SIKU YA MUNGU YA APOKREO

MU POSHO KWA SALA YA MANGARIBI (ESPERINOS).

Elezo*: Kisha:* «Bwana nimekutita...» *tunaimba wimbo ya Paraklitiki 6 na kisha hii wimbo 4 ya Triodi.*

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Wakati utakapokuja kuhukumu na haki, wewe Mwamuzi wa haki, utaketi juu ya kiti chako cha utukufu; Mto ya moto itatiririka mbele ya baraza yako ya hukumu, ezi za mbinguni zitakuzunguka, watu wenye kujaa na woga watahukumiwa kila mumoja kadiri ya matendo yake; kwa hii wakati, ee Kristu, utuhurumie, weka waaminifu wenye kukuomba katika makao ya wateule kwa ajili ya mapendo yako.

Vitabu vitafunguliwa na siri zitafunuliwa mbele ya baraza ya hukumu, bonde yote ya machozi italia wakati itaona waovu wamehukumiwa kwa ajabu ya milele wakililia hali yao; ndio maana tunakuomba, ee Mungu wa mapendo, utusamehe sisi tunakuimbia, peke yako Mwema.

Baragumu italia na makaburi yatafunguliwa*:* watu watatoka wenye kutetemeka*:* Wale waliotenda mema watakuwa na furaha kwa kuongojea tuzo watakalopokea; wale waliotenda uovu watalia kwa woga, wataazibiwa na kutengwa na wateule. Ee Bwana wa utukufu, kwa wema wako utuhurumie, utupe tupate bahati ya marafiki zako.

Ninalia na kuomboleza wakati nasikia giza za inje, moto ya milele, Hadeze, nondo yenyi kutafuta, kusaga memo na mateso watakayopata wale waliotenda zambi nyingi zenyi kukasirikisha sana, wewe Mungu mwema; Ole hawa waovu mimi ni wa kwanza, lakini kwa rehema yako kubwa, ee Mwamuzi, uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane.*

Wakati kiti cha ufalme itakapowekwa na kitabu cha uzima itakapofunguliwa na Mungu atakapokaa kwa kuhukumu, woga gani nitapata hii wakati! Wakati Malaika watatetemeka pempeni yake na mtoni ya moto itakapoonekana, hapo tutafanya nini sisi watu wakosefu? wakati tutakapomsikia akiita wenye kubarikiwa na Baba yake kwa ufalme wa mbinguni na waovu kwa azabu ya milele, nani basi atavumilia hukumu yake ya ajabu? Lakini wewe peke yako Mwokozi wangu ujiharikishe kunigeuza mbele ya mwisho, ee Mfalme wa milele, unihurumie.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Elezo*: Tunaimba Theotokion ya Paraklitiki na sauti ya hii juma.*

Mwangaza upole. . .

Prokimenon ya Sabato.

Bwana anatawala, amevikwa utukufu *(mara tatu).*

APOSTIKHA.

Elezo*: Tunaimba Apostikha ya Paraklitiki na kisha:*

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya mnane.*

Ole, ee roho yangu muovu, mpaka wakati gani utadumu katika zambi? Mpaka wakati gani utakaa mwivi? Nini unaweza kwa wakati ya ajabu ya kufa? Hauogopi hukumu kali ya Mwokozi? Namna gani utajitetea, namna gani utajihakikisha? Matendo yako yameonekana kama masubutu hakika, matendo yako yanakushuhudia; lakini, ee roho yangu, wakati inaendelea*:* Uitangulie, kama utaweza, na kwa imani paza sauti*:* Nimekosa, ee Bwana, nimekosa; lakini najua mapendo na huruma yako; ee Mchungaji mwema, usinikatalie kusimama kuume kwako, kwa wema wako.

Sasa na siku zote*. . .* **THEOTOKION**.

Bikira usiyeolewa, mwenye kuchukua Mungu katika mwili usiyosemwa, Mama wa Mungu aliye juu na bila doa, pokea usihi wa watumishi wako; wewe uliyeleta kwa wote safisho ya makosa, sasa pokea ombi letu, na patanisha kwa ajili ya wokovu wa sisi wote.

Elezo: *Sasa padri anasema ombi hii:*

Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

Msomaji: Trisagion: Mungu Mtakatifu...

Kisha Mwimbaji ataimba: Apolitikion ya Ufufuo ya Kristu na sauti ya hii Juma. Apolitikion ya Mtakatifu wa leo na Theotokion na sauti yake. Kisha Padri atafanya Kuaga.

SIKU YA MUNGU MU SALA YA ASUBUI (ORTHROS).

Elezo: *Kisha Eksapsalmos, tunaimba Bwana ndiwe Mungu...Kathismata na Anavathmi ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma, kisha Prokimenon na Evangelion ya asubui. Kisha: tunasoma:* Tukiona Ufufuo wa Kristu*. . . Kisha zaburi 50 (51) na kisha tunaimba:*

Utukufu*. . . Sauti ya mnane.*

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana*. . . .* (*Angalia ukurasa 2).*

KANUNI

WIMBO WA KWANZA. *Sauti ya sita. Voithos ke skepastis.*

Natetemeka nikiwaza kuja kwako kwa mara ya pili*:* hii siku ya ajabu, naiona kwa woga, wakati utakapoketi, ee Mungu mwenyezi, kuhukumu wazima na wafu.

Ee Mungu wetu, wakati utakapokuja mwenye kuzunguka na ezi za mbinguni pamoja na malaika wengi, ee Kristu, unipe mimi pia nienda kukutana pamoja nawe mbinguni.

Tuende, ee roho yangu, waza hii saa na hii siku ambayo Mungu atakapoonekanana machozi mwa wote; ondoa vilio vyako na malalamiko yako kusudi akupate safi hii wakati wa hukumu!

Naogopa gehema ya ajabu na moto isiyozimika, nondo na kusaga meno*:* Ee Kristu, zima na samehe zambi zangu, uniweke kati ya wateule wako.

Nitaweza kusikia sauti yako yenye kuwaita kwa furaha watakatifu wote, na kupata mapumziko ya ufalme wako mbinguni!

Usinitaje katika hukumu, ukinikumbusha deni, ukitazama matendo yangu na kusimamisha uzulumu wangu, lakini kwa rehema yako, usitazame maovu yangu na uniokoe, ee Mungu Mwenyezi.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Mungu mumoja katika watu tatu, ubwana wa ulimwengu wote, mwanzo na mwisho wa vitu vyote, wewe mwenyewe, utuokoe, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Mtoto gani aliyezaliwa bila mbegu ya baba? Huyu Baba alizaa inje ya tumbo la mama*:* Ni jambo la ajabu? Bikira anazaa Mungu-Mtu.

WIMBO WA TATU. *Stereoson Kirie.*

Bwana atakuja, nani basi atavumilia woga wakati atakapomuona? Na uso wake nani ataweza kuingalia? Ujitayarishe, ee roho yangu, kwa kukutana naye.

Tumutangulieni Mungu kwa kulia kwetu, tupatane naye mbele ya mwisho, maana matendo yetu yatafunuliwa mbele ya baraza yake ya hukumu.

Nakuomba, unihurumie, ee Bwana, unihurumie wakati utakapokuja pamoja na Malaika wako Watakatifu kumulipa kila mumoja kadiri ya matendo yake.

Ee Bwana, namna gani nitaepuka hasira yako? Kwani sikutii amri zako, lakini kwa wakati wa hukumu unisamehe.

Ee roho maskini, umurudishie Mungu kwa machozi na maondolezo mbele ya mwisho wa hii uzima, mbele ya Bwana hajakufungia mlango ya karamu.

Ee Bwana, nimekosa kuliko mutu hata mumoja, lakini mbele ya kunihukumu unisamehe kwa mapendo yako.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Utatu wenye kustahili nyimbo zetu, Mungu mumoja katika watu tatu, utuokoe sisi wenye kusujudia na ibada mbele ya ufalme wako.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira safi kamili, bila mbegu ulizaa Neno la Uzima aliyetwa mwili tumboni mwako na kujifanya mutu bila kugeuka*:* ee Mzazi-Mungu, utukufu kwa kuzaa kwako.

IRMOS. Ee Bwana, sabitisha roho yangu juu ya mwamba ya amri zako kusudi isipepee, maana pake yako ndiwe Mtakatifu na Bwana.

KATHISMA WA KWANZA.

Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.

Baraza ya hukumu ni ya kuogopa, hukumu yako ni ya kweli, matendo yangu na mbaya; lakini wewe, Mungu wa mapendo, kuja uniokoe na kunikomboa toka azabu; ee Rabi, unikinge toka wenye kulaaniwa na unistahilishe nisimame kuume kwako, ee Mwamuzi wa kweli.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira safi kamili, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu ulichunga na kuzaa bila uchafu tumboni mwako Mungu wako, Muumba wako na wa wote; na sisi wenye kumutukuza, ee Bikira, tunakuimbia, wewe ukombozi wa dunia tena makao ya Mfalme wa utukufu.

KATHISMA INGINE.

Sauti ya sita.

Nawaza siku ya ajabu ya hukumu na nalilia matendo yangu mbaya; namna gani nitajipatia haki mbele ya Mfalme msiyekufa? Namna gani nitasubutu kumutazama mwamuzi wangu, mimi maskini? Ee Baba mwema kamili, Mwana wa pekee na Roho Mtakatifu unisamehe, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti umoja.*

Ee Mungu wa mapendo, katika bonde la machozi, pahali ulipochagua kukaa na kutoa hukumu ya kweli, usifunue siri za roho yangu sababu nisipate haya mbele ya malaika, lakini unisamehe, ee Mungu, unihurumie, ee Bwana.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Sauti umoja.*

Ee Bikira Mzazi-Mungu uliye matumaini ya ulimwengu, naomba ulinzi wako wenye kustahili heshima, hurumia watu wenye kukimbilia kwako, umuombe Mungu atuonyeshe mapendo yako ukiopoa roho zetu toka azabu, ee Bikira mbarikiwa katika wanawake wote.

KONTAKION.

Sauti ya kwanza.

Wakati utakapokuja na utukufu duniani, ee Mungu wetu, viumbe vyote vitatetemeka, mto ya moto itapita mbele ya baraza yako ya hukumu, vitabu vitafunguliwa na siri zitafunuliwa; kwa hii siku uniokoe toka moto ya milele, na unistahilishe nisimame kuume kwako, ee Mwamuzi mwenyi haki.

IKOS.

Wakati nawaza hukumu yako ya ajabu, ee Bwana wa wema wote, na siku ya haki yako, natetemeka kwa woga, maana zamiri yangu inanihukumu; wakati utakapokuja mwenyi kuketi katika kiti chako cha ufalme kuhukumu dunia yote, mutu hata mumoja hatakataa makosa yake, kwa sababu ukweli itashinda na hakuna hata mumoja atakuwa na nguvu ya kukataa; hapo itasikilika moto ya gehena na waovu watasaga meno. Lakini wewe, Bwana, unihurumie, Mwamuzi mwenyi haki.

SINAKSARI.

Elezo: *Sasa ku mwanzo tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha Sinaksasi hii.*

Leo tunafanya makumbusho ya kuja kwa mbili (majilio) katika utukufu wake Bwana wetu Yesu Krtistu.

Wakati utakaposhuka, ee Mwamuzi wa ulimwengu na utaohukumu dunia yote unifanya mimi pia kuwa mstahili wa kusikiliza mwito huu*:* «Kujeni, enyi wabarikiwa wa Baba yangu».

Kwa mapendo unapenda nayo wanadamu, ee Kristu Mungu wetu, utustahilishe kusikia mwito wako, utuhesabie katika wale watakaokuwa kuume kwako, na utuhurumie. Amina.

KATAVASIES

Wimbo wa kwanza. *Sauti ya sita.*

Bwana na msaada wangu, ulinzi wangu, ni yeye aliyeniokoa, ndiye Mungu wangu, na nataka kumutukuza, Mungu wa Baba wangu, na nitamutukuza, kwani amevaa utukufu.

Wimbo wa tatu.

Ee Bwana, sabitisha moyo yangu pa mwamba wa amri zako ili isiyumbeyumbe, kwani peke yako ndiwe Mtakatifu na Bwana.

Wimbo wa ine.

Bwana, Nabii aliposikia kuja kwako akashangaa, kwani ulitaka kuzaliwa kwa Bikira na kuonekana kati ya wanadamu na akasema*:* Nimesikia sauti yako na nimejaa na woga; Bwana, utukufu ku uwezo wako.

Wimbo wa tano.

Usiku ninakesha mbele yako, ee Bwana Mpenda-wanadamu, nakuomba uniangaze uniongeze njiani mwa amri zako na unifundishe, Mungu-Mwokozi, kufanya mapenzi.

Wimbo wa sita.

Nimelalamika na moyo wangu wote kwa Mungu wa mapendo, anasikiliza mwito wangu toka chini ya Hedeze na ku shimo anakomboa uzima wangu.

Wimbo wa saba.

Tulitenda zambi, uovu na uzulumu mbele yako, hatukuchunga wala kushika amri zako, usitutupe mpaka mwisho, ee Bwana, Mungu wa Baba zetu.

Wimbo wa mnane.

Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Huyu Malaika wote wanatukuza, mbele yake wakeruvi na Waserafi wanatetemeka, kila kiumbe na kila mwenye pumuzi amuimbe, amutukuze na kumusifu milele.

Wimbo wa tisa.

Ulipata mimba, bila mbengu, uzazi wako ni usiyokadirika, ee Mama, usiyeolewa*:* Mungu anajifanya mtu kwa Bikira na anabadirisha amri za ubinadamu; na kadiri ya imani ya kweli, ee Bikira Mzazi-Mungu, tunakutukuza kizazi hata kizazi.

EKSAPOSTILARION.

Sauti ya mbili. Tis mathites sinelthomen.

Ee Bwana, ninapowaza siku ya ajabu ya hukumu na ya utukufu wako isiyokadirika, natetemeka kwa woga na napaza sauti*:* Ee Kristu, wakati utakapokuja duniani katika utukufu wako kuhukumu dunia yote, ee Rabi, unisameha na uniokoe kwa azabu, unistahilishe nisimame kuume kwako.

INGINE. *Sauti umoja. Ginekes akutisthite.*

Tazama imekuja siku ya Bwana mwenyezi*:* nani hataogopa kuja kwake? Ni siku ya hasira, ni chungu chenyi kuwaka moto wakati Mwamuzi atakapoketi kumulipa kila mumoja kadiri ya matendo yake.

THEOTOKION. *Sauti umoja.*

Nawaza wakati wa hukumu, ee Bwana Mpenda-wanadamu, nawaza kuja kwako kwa hatari; ninapotetemeka nikifazaika, nakulalamikia*:* Ee Mwamuzi wa haki peke yako uliye na huruma, unirudishe kwako na unipokee mimi maombezi ya Mzazi-Mungu.

MASIFU

Elezo*: Tunaimba mbele wimbo 5 ya Ufufuo ku Paraklitiki na kisha wimbo 3 ya hii kitabu.*

Sauti ya sita.

Nawaza juu ya hii siku ya hatari ambako sisi wote tutafunuliwa kama washitakiwa sababu ya kuhuzuria mbele ya Mwamuzi wa haki; hapo baragumu italia, misingi ya inchi yatatikisika, wafu watafufuka kaburini watu wote watakuwa kama watoto wachanga, siri zao zote zitafunuliwa mbele yako, watalia na kuomboleza, wasiotubu watatupwa katika katika moto ya inje, lakini wenye haki watafurahiwa, na wataingia katika uwanja wa mbinguni.

Shairi*:* Nitashukuru Bwana kwa moyo wangu wote, katika baraza ya wenye haki, na katika makutano.

Woga gani itakuwako hii siku wakati Mwamuzi atakapoketi katika kiti chake cha hukumu! Vitabu vitafunguliwa, matendo yatafunuliwa, malaika watakusanya mataifa yote*:* Kujeni, enyi wasultani na wafalme, sikieni ya kwamba Mwamuzi atakuja kuhukumu dunia yote! Mutu gani atasimama wakati malaika watamuzunguka kwa kufunua alama, mawazo na tamaa, ya mchana na ya uziku? Ole! Woga gani hii siku! Ee roho yangu, tangulia mbele, ujiharikishe kulalamika*:* Ee Bwana, narudi kwako, uniokoe kwa wema wako.

Wimbo ingine. Sauti ya mnane.

Shairi*:* Usimame, ee Bwana, nyanyua mukono wako, usisahau masikinim kwa nini mwovu anazarau Mungu.

Danieli Nabii, mutu wa mapendo, alipoona uwezo wa Mungu, akaagua*:* Mungu ameketi kwa kuhukumu, vitabu vinafunguliwa. Ee roho yangu, unapofunga usisahau jirani yako; usihukumu ndugu yako, wakati unapofunga kusudi usiungue kama nta motoni huko utakapoenda; lakini Kristu akupeleke katika ufalme wake mbinguni.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya kwanza.*

Wa Ndugu, tujitakaseni kwa toba iliyo Malkia wa fazila, tazama imetupatia mema ya kila namna, inatunza vidoma vya tamaa, inapatanisha Rabi na waovu; tukiipokea na furaha, tumulalamikia Kristu Mungu wetu*:* Ee Mfufuliwa katika wafu, usituhukumu sisi wenye kukutukuza wewe peke yako usiye na zambi.

Sasa na siku zote. . .

Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa u Kristu Mungu wetu, uliyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA .

Kuaga.

MU JUMA YA APOKREO KWA MANGARIBI

Elezo*: Kwa Ibada ya Mangaribi tunaimba wimbo 6 ya Paraklitiki na Mineon, Utukufu. . . Sasa. . . Theotokion.*

Pa fasi ya Apostikha hatuimbe ya Paraklitiki, lakini paka ya Triodion hii wimbo.

Sauti ya mnane.

Tamaa ilitustahilisha utupu wetu wa kwanza, uchungu ya tunda ilitupoteza, tulijitenga mbali na Mungu; Turudi sasa kwa toba, tutakaseni tamaa ya mahasa yetu, kufunga iwe chakula; kwa matumaini ya neema tusabitishe roho zetu, apana kwa chakula cha mwili, maana chakula chetu atakuwa Mwana-Kondoo wa Mungu, katika usiku takatifu wa ufufuo wake wa nuru, Mwana-Kondoo aliyejitoa kwa ajili yetu, kwa karamu ya fumbo huko Mitume walishariki, Mwana-Kondoo aliyeondoa giza ya usiku kwa nuru ya Ufufuo wake takatifu.

Shairi*:* Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama macho ya watumishi yanaangalia kwa mkono wa Bwana kama macho ya kijakazi kwa mkono wa bibi yake, hivyo macho yetu yanavyoangalia kwa Bwana Munbgu wetu hata akatuhurumia.

(Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu).

Shairi*:* Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa. Nafsi yetu inayala na kuzarauliwa kwa wenye kuikala na salama tena na kuzarau kwa wenye kiburi.

Enyi Mashahidi wa Bwana wenye kutakasa ulimwengu na kuponyesha ugonjwa wote, ombeni sasa kwa ajili yetu ili roho zetu ziokolewe toka mtego wa Adui.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . *Sauti umoja.*

Ee Mama, usiyeolewa, mbingu zinaimbia neema yako, na sisi tunakuja kuzaa kwako isiyokadirika, ee Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA JIVINI (TIROFAGU)

Elezo: *Kisha Eksapsalmos tunaimba ma shairi wa ine, «Bwana ndiwe. . . ». Apolitikia ya Watakatifu ya leo na kisha tunaimba moja kathisma ya Paraklitiki na ingine ya hii kitabu.*

Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.

Milango ya toba takatifu inafunguliwa kwetu sisi, tuingieni na furaha na tutakaseni yetu; tufunge na tuache tamaa zetu, tukiongozwa kama watumishi wa Kristu mwenye kuwaita watu wote kwa ufalme wa mbinguni, tumutolee Mfalme wa ulimwengu zaka ya mwaka kusudi tuone na mapendo ufufuo wake takatifu.

Utukufu kwa Baba. . .*(mara ingine)*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulibeba mikononi mwako Muumba aliyejifanya mtu sababu ya kutuokoa; hii mikono takatifu uiinue umuombe ondoe mabli yetu vishawishi na hatari; na sisi wenye kukulamikia tunakuimbia na mapendo*:* Utukufu kwa huyu aliyekaa ndani yako utukufu kwa huyu aliyetoka kwako, utukufu kwa huyu aliyezaliwa kwako sababu ya kutuokoa.

KANUNI

Wimbo wa kwanza.

Sauti ya kwanza. Odin epinikion.

Leo ni matangulizi ya siku kuu ya nuru, ni mwanzo wa Kwarezima*:* ndugu, tuendeni wenye kujaa na matumaini, furaha na uchanganyiko.

Nilipofafanisha uasi wake, nilifukuza Paradizoni kama Adamu; ndio maana nasujudu mbele yako, na kwa toba yangu nakulalamikia*:* Ee Bwana, uniokoe.

Ni mwanzo wa toba na wa sikitiko, ni kuepuka ubaya na tamaa; tunapojaa na juhudi, tuache tangu leo matendo yetu ya zambi.

THEOTOKION

Nilipopofushwa kwa giza ya zambi, narudi kwako, ee Mzazi-Mungu*:* Wewe uliyezaa Kristu aliye Jua la haki, nakuomba, ee Bibi yetu, uniokoe.

Wimbo ingine. Sauti na Irmos umoja

Enyi marafiki za Mungu, tazamnei imefunguka mulango ya toba*:* Kujeni, tujiharakisheni kuingia mbele Kristu hayaifunga juu ya uovu wetu.

Yenyi kueleza wakati, tazama imeendelea Juma ya utakaso yenyi kututayarisha kwa Kwarezima takatifu tukitakasa miili na roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Utatu Mtakatifu na wa asili moja, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Umoja kamili na usiyouumbwa, okoa waaminifu wenye kusujudu mbele yako.

Sasa na siku zote. . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu kamili, kwako sheria za mwili zimeshindwa, ulizaa Mungu bila mbegu, umekaa bikira kama kwa mwanzo.

IRMOS. Tuimbe wote wimbo wa ushindi kwa maajabu ya Mungu wetu ambaya kwa mkono wake wa uwezo aliokoa Israeli akivaa utukufu.

APOSTIKHA YA ASUBUI.

Sauti ya tatu. Idiomelon .

Siku zote Kwarezima inatuwezesha kushindana na werevu na nguvu ya mashetani, Malaika walio walinzi wa uzima wetu wanatuangalia kama kwa kufunga tunajitakasa.

Shairi*:* Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu zote. Utufurahishe kadiri ya siku ulizotutesa, kadiri ya miaka tulipoona mabaya. Matendo yako yaonekana kwa watumishi wako, na utukufu wako kwa wana wao. (Zaburi 89(90), 14-16).

Elezo: *Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.*

Shairi*:* Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya mikono yetu uistawishi, ndiyo kazi ya mikono yetu uiimarishe. (zaburi 89(90), 17.

Kujeni, enyi mataifa yote, tutukuzeni makumbusho ya Mashahidi Washindaji wa Bwana, Kwani mbele ya Malaika na ya wanadamu walipokea kwa Kristu taji ya Washindi na wanamuomba kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti umoja.*

Bila mbegu, ulipata mimba kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, tunakutukuza tukiimba*:* Salamu, ee Bikira Mtakatifu kamili.

Elezo*: Kisha mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma hii sala:*

Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

Elezo: *Kisha Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Na Apolitikia ya Watakatifu ya hii siku na theotokion.*

Kisha padri atafanya Kuaga, katika desturi ya kila siku.

MU KAZI MOJA YA JUMA YA JIVINI KWA MANGARIBI.

Tunaimba wimbo ya Paraklitiki na sauti ya hii siku, Utukufu. . . Sasa. . . Theotokion ya Paraklitiki, Mwangaza upole. . . Prokimenon ya hii siku.

APOSTIKHA

Sauti ya mnane.

Kwa kufunga tunajikaza kutakasa uchafu wa zambi zetu; kwa rehema na mapendo ya jirani, kwa bidii yetu ya kusaidia maskini, tutaweza kuingia katika nyumba ya arusi ya Kristu mwenye kutupa sisi neema ya wokovu.

Shairi*:* Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala*. . . (ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi*:* Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na*. . .*

Enyi Mashahidi wa Bwana, mumuombe Mungu na kwa ajili ya roho zetu ombeni ili kwa wema wake kubwa atuondolee zambi zetu nyingi.

Utukufu*. . .* Sasa*. . .* **THEOTOKION.** Sauti umoja*.*

Tumuimbie Bikira Mtakatifu kamili kama Mzazi-Mungu kweli na kwa ibada tumuamkie kama Malaika*:* Salamu, Mama Mtakatifu kwako Mwana wa Mungu alijifanya mtu, ewe makao ya Roho Mtakatifu mwenye kutuombea daima kwa ajili ya wokovu wa roho zetu*.*

Elezo*: Kisha Mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma:*

Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli*.*

Msomaji*:* Trisagion*:* Mungu Mtakatifu*. .* Utatu Mtakatifu*. . .* Baba yetu*. . .* Kwa kuwa*. . .*

Elezo: *Kisha tunaimba Apolitikia ya Watakatifu ya leo.*

Kisha padri atafanya Kuaga, katika desturi ya kila Sala ya mangaribi.

MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA JIVINI.

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos. . . Ma shairi. . . Bwana ndiwe. . . Apolitikia ya Watakarifu ya leo. Na kisha tunaimba kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na kisha hii hapa:*

Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.

Ee Neno la wema, pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, kwa hekima yako isiyokadirika uliumba vitu vyote vyenyi kuonekana na visivyoonekana. Utastahilishe tuishi na amani katika hii wakati wa Kwarezima ya nuru, na kwa wema wako ukituokoa toka uchungu wa zambi, na kutupatia machozi ya sikitiko juu ya wokovu na maondoleo ya makosa yetu kusudi, roho ikipata nguvu na tukianza kwarezima yetu na furaha ya roho, tuimbie utukufu wako kubwa pamoja na Malaika*.*

Utukufu kwa Baba*. . .(Mara ingine hii wimbo ya juu).*
Sasa na siku zote*. .* **THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu, ulipata mimba ya hekima na Neno la Mungu kwa namna ya ajabu na isiyokadirika, ulizaa huyu aliyeumba ulimwengu, ulibeba mikononi mwako huyu mwenye kushika inchi mikononi mwake nilishi wa ulimwengu, Muumba na Bwana. Ndio maana, ee Bikira Mtakatifu kamili, nakutukuza, na kwa ibada naomba maondoleo ya zambi zangu; kwa wakati nitakutana usoko kwa uso na Muumba wangu, ee Bikira Mtakatifu na Bibi yetu, unisaidie sababu ya fazili unayo kwa Mungu*.*

Elezo: *Sasa tunasoma Zaburi 50 (51).*

KANUNI.

Wimbo wa mbili. *Sauti ya tatu*.

Kama alfajiri inapoangaa, Kwarezima inangaza kwa nuru yake toka ya roho zetu*.*

Ee Kristu, kwa wema wako inisamehe na kuniopoa toka giza za inje na ya mauti*.*

Ee Mwokozi, uniokoe ku moto ya milele, uniopoe ku uondo yenyi kutafuna daima na kwa toba takasa roho yangu.

THEOTOKION.

Ee Bikira mwenye kustahili nyimbo zetu, uwe kwa sisi njia ya toba, ongoza hatua zetu mpaka kwa mlango ya wokovu.

Wimbo ingine. *Sauti ya mbili.*

Wakati ya toba imefika*:* Enyi marafiki za Kristu, tuondoeni zambi yote sababu ya kuwa na furaha ya kumutazama Bwana.

Tangu sasa tufunge na bidii tukitakasa mawazo yetu na matendo yetu sababu ya kupata maondoleo ya zambi zetu.

Ee Kristu, Bwana wa neema na wa rehema mwenye kutupokea wote wakati wa toba, tunaimbia utukufu wako daima.

Utukufu kwa Baba. . .

Tunataka kukutukuza katika watu tatu, ewe Utatu mumoja, usiyogawanyika, usiyochanganyika na Mtakatifu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ee Bikira Mtakatifu tena Mzazi-Mungu, umuombe Neno aliyejifanya mtu tumboni mwako aokoe watumishi kwa kila hatari.

IRMOS. Ee taifa langu, sikiliza sheria yangu, tega sikio ku maneno ya kinywa changu ukiomba jina la Bwana.

APOSTIKHA.

Sauti ya tatu. Idiomelon

Enyi mataifa, tuimbieni na kushangilia Kwarezima kwa hii mwanzo wa mashindano ya roho; tuacheni tamaa zetu za mwili sababu ya kuongeza vipaji vya roho; kama tulivyo watumishi wa Kristu tuteswe kama yeye kusudi tutukuzwe kama wana wa Mungu; na Roho Mtakatifu anayekaa moyoni mwetu angaze roho zetu kwa nuru yake.

Shairi*:* Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Elezo*: Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.*

Shairi*:* Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Maaskari wa Kristu walifukuza woga yote mbele ya Wafalme na ya wazulumu; walimuungama Bwana wa ulimwengu, Mungu na Mfalme wetu, sasa wanaombea roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, mlinzi wa wote wale wenye kukuomba, unatupa sisi nguvu na usabiti, tunakutumainia wewe*:* Umuombe Mwana wako kwa ajili ya watumishi wako wasiostahili.

Elezo*: Kisha mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma hii sala:*

Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

Kisha Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Elezo*: Waimbaji wanaimba Apolitikia ya Watakatifu ya hii siku na Theotokion.*

Kuaga

MU KAZI MBILI YA JUMA YA JIVINI KWA MANGARIBI.

Elezo*: Tunaimba wimbo ya Paraklitiki na Mineon. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Theotokion ya Paraklitiki. Mwangaza upole. . . Prokimenon ya hii siku*

APOSTIKHA.

Sauti ya kwanza. Idiomelon.

Enyi waaminifu, tupokeeni na furaha hatari ya Kwarezima kama walivyofanya Waninawe zamani, na kama makahaba na watoza Kodi walivyopokea kwa Yoane habari ya kugeuza nia, kwa kufunga tujitayarishe kwa karamu takatifu ya Bwana katika Sayuni; tujitakaseni sasa kwa machozi yetu mbele hajatuosha kama Wafuasi Watukufu; na tuombeni neema ya kuweza kuona utimizo wa fumbo huko inafunguliwa Paska ya ukweli; tujitayarisheni kwa kusujudu Msalaba sababu ya kutukuza Ufufuo wa Kristu Mungu wetu, na tumuambieni*:* Ee Bwana Mpenda-wanadamu, wewe ni matumaini yetu, usitukatae.

Shairi*:* Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Elezo*; Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.*

Shairi*:* Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Enyi Mashahidi, neema gani kwa ushujaa yenu! Mulitoa damu yenu, pokeeni uriti ya mbinguni; kwa majaribu ya muda kidogo furaha yenu inakaa ya milele; kweli ni ubadili ya ajabu; Maana muliacha uharibifu sababu ya kupokea mema isiyokufa; sasa munafurahiwa pamoja na malaika na munaimbia daima Utatu wa asili moja.

Utukufu. . . Sasa. . . **THEOTOKION**. *Sauti umoja.*

Bikira alipoona msalabani huyu aliyezaa kwa safi, hakuweza kuvumilia kidonda cha moyo wake, na kwa huzuni yake akapaza sauti*:* Ee Bwana, wewe mwenye kuweka imara viumbe vyote, namna gani unakaa msalabani kama mwenye kuhukumiwa? Lakini unataka kuokoa wanadamu.

Elezo: *Padri ao Mukubwa ya Kanisa:*

Sasa Bwana umuache mutumishi wako. . . .

Msomaji*:* Amina. Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. *S*asa na siku. Utatu Mtakatifu....Utukufu.... Sasa na siku.. Baba yetu

Padri*:* Kwa kuwa Ufalme, na uwezo, na utukufu ni kwako, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hasa milele na milele.

Elezo: *Na wimbo inafuata ya Kwarezima:*

Ewe Bikira Mzazi-Mungu, salamu, umejaliwa neema Maria, Bwana ni nawe, mbarikiwa wewe katika wanawake na mbarikiwa tunda la tumbo lako, kwani umemzaa Mwokozi wa roho zetu.

Ewe Mbatizaji wa Kristu, utukumbuke sisi wote juu ya kuokolewa ku makosa yetu; kwani Kwako kulipatikana neema ya kutuombea.

Utukufu kwa Baba. . .

Enyi Mitume Watakatifu na Watakatifu Wote, mutuombee juu ya kuokolewa ku hatari na sikitiko, kwani ninyi ni Walinzi wetu wa nguvu kwa Mwokozi.

Sasa na siku zote. .

Ewe Mzazi-Mungu, tunakimbilia ku wema wako, usizarau maombi yetu katika vishawishi, lakini utuokoe ku hatari, kwani peke yako ndiwe Safi na Mbarikiwa.

Bwana hurumia, *(mara makumi ine).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee Padri.

Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, daima sasa na siku zote, hata milele na milele.

Padri ao Mukubwa ya Kanisa:

Ewe Mfalme wa mbinguni, chunga waaminifu wafalme wetu; sabitisha imani; leta amani kwa inchi zote; ukimya duniani; linda vema Kanisa yetu Takatifu (*Monasteri, Parokia, ao Mission);* wale walioondoka toka hii dunia*:* Mapadri na ndugu zetu uwaweke pahali pa wenye haki; na sisi utupokee katika toba na ungamo kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Elezo*: Kisha tunafanya Metania tatu makubwa (kupika magoti), kisha metania kidogo kumi na mbili na kisha ku mwisho moja metania kubwa. Ya kila Metania tunasema kwa siri hii sala ya Mtakatifu Efremi:*

Bwana na Rabi wa uzima wangu, usinipe nia ya uvivu, tamaa ya kujua mambo vya wengine, ya ukubwa, na ya kusema bure.

(tunafanya sasa moja metania kubwa).

Umupe mtumishi wako zawadi ya roho ya kadiri, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo.

(Metania kubwa ya mbili).

Ndiyo, ee Bwana, unipe nione makosa yangu na nisiamue ndugu yangu; kwani unabarikiwa milele na milele. Amina.

(Metania kubwa ya tatu).

Elezo*: Kisha tunafanya metania kidogo kumi na mbili na kisha tunasema ile sala ya yulu:*

Ndivyo, ee Bwana, unipe nione makosa yangu na nisiamua ndugu yangu; kwani unabarikiwa milele na milele. Amina.

Padri*:* Hekima.
Waimbaji*:* Himidi
Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Waimbaji*:* Amina. Bwana Mungu aimarishe imani takatifu, isiyo na lawama ya wakristu, watawa waorthodoksi katika mji na inchi hii, milele na milele. Amina.

Padri*:* Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Msomaji*:* Uliye wathamani kuwashinda wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli, tunakutukuza wewe.

Padri*:* Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Msomaji*:* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu),* Rabi mtakatifu barikia.

Padri*:* Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa Msalaba uheshimiwa na uhuitaji, kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili, kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtakatifu, Mbatizaji,

Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume Watakatifu wetu na waekumeniki Wakubwa, Walimu na Waaskofu, ya Washahidi, Watakatifu, Watukufu, Washindaji, wazuri ya Wapadri Wabebaji-Mungu, ya mpadri Mtakatifu Yoane Krisostomo, muarkiepiskopo wa Konstantinopoli, ya wa Babu Mungu wetu na nwenye haki Yoakimu na Anna, ya Mtakatifu *(ya hii siku),* makumbusho yake ni leo, hata ya Watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe yu Mungu mwema, murahimu na mpenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

Waimbaji*:* Amina.

Elezo*: Hii mufano ku mwisho ya Esperinos inapaswa kuifanya na mu kazi ine Mangaribi ya hii Juma na mpaka ku mwisho ya Juma wa tano ya hii Kwarezima.*

MU KAZI TATU YA JUMA YA JIVINI KWA ASUBUI

Elezo*: Hii Juma, mu Kazi Tatu asubui na mu Kazi Tano asubui pahali fasi ya Bwana ndiwe, kisha Eksapsalmos, tunaimba Alliluia na ma shairi ingine ya kuachana.*

1)Ee Bwana, tangu usiku roho yangu kwa sala inaongojea alfajiri yako, maana amri zako ni nuru duniani.

Waimbaji*:* Alliluia *(mara tatu).*

2) Jifunzezi haki, ninyi wote wakaaji wa dunia.

Waimbaji*:* Alliluia *(mara tatu).*

3)Wivu utangukia watu wapotevu, sasa moto itawateketesa maadui zako.

Waimbaji: Alliluia (mara tatu).

4)Mwaajibu, ee Bwana, uwazibu vikali kwa mateso Wenye sifa wote wa dunia.

Waimbaji: Alliluia (mara tatu).

Tunaimba mbele Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na kisha hii

KATHISMA.

Sauti ya mbili. Efsplaxnias Iparhusa.

Kwa amani utuache tuonje katika Kwarezima utakaso, na kwa mapendo isiyokadirika unapenda nayo wanadamu ondosha mbali yetu werevu wa adui na utuokoe kwa Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu pekee yako unajua siri roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *(Mara ingine hii).*

Sasa na siku zote. Sauti umoja. **STAYROTHEOTOKION**.

Bikira aliyekuzaa alisimama chini ya msalaba, na alipoweza kuvumilia kukuona kuteswa bila haki, akalia na kuomboleza akasema*:* Ee Mwanangu mvumilivu, namna gani unateswa? Naimbia nakutukuza wema wako kubwa.

Tunasoma Zaburi 50 (51)

KANUNI

Wimbo wa kwanza. *Sauti ya ine.*

IRMOS. *Ninakuimbia mwilini, Bwana anatupa sisi mfano na anashinda kishawishi; anatuonyesha namna gani na sisi tunaweza kufanya, na anatukumbusha mipaka Mungu aliweka.*

Kwa kufunga Musa katika mulima wa Sinai akapata uwezo wa kuzungumuza uso kwa uso na Mungu*:* Tumufananisheni.

Ee Bwana, uwasamehe watu wako, , kwa neema yako takatifu uwatazame; na kwa wema kubwa hurumia wanadamu wote.

Ee Mzazi-Mungu, tunakimbilia kwako wewe uliye boma letu, tunatumainia maombezi yako sababu ya kuokoa waaminifu wako toka hatari yote.

THEOTOKION

Ee Mzazi-Mungu, wewe uliyezaa Mungu wetu umuombe kwa ajili yetu, kwani wewe ni kimbilio la ukosefu maskini.

Elezo*: Pahali pa fasi ya Eksapostilarion tunaimba Fotagogikon ya sauti ya hii juma. (Tafuta ku mwisho ya hii Kitabu ya Triodion). Na kisha:*

APOSTIKHA

Sauti ya kwanza. Idiomelon.

Ee roho yangu, ukikataa chakula bila kutakasa tamaa zako, ni kwa bure unafunga na kujitukuza kwani kama hautake tugeuka utakuwa muongo kwa Mungu, utafanana na mashetani, kwa sababu hawana na chakula; usiharibu Kwarezima yako kwa zambi, lakini usisikilike kwa tamaa zako; fanya kama uko karibu ya Mwokozi mfufuliwa, ao sulubiwa pamoja naye Yeye aliyesulubiwa msalabani kwa ajili yako, na umugeukie ukimwambia*:* Unikumbuke, ee Bwana, wakati utakapoingia katika ufalme wako.

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . . *(mara ingine).*

Shairi*:* Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Enyi Mashahidi Watakatifu wenye kustahili sifa yote, haiko wala majaribu, wala huzuni, wala njaa, wala uzulumu, wala hatari, wala ugonjwa, wala upanga, wala moto ambayo kwa makamio yao ikiwatenga ninyi mbali ya Mungu; lakini ni kwa mapendo yenu kwa ajili yake mulisahau dunia mukawa wageni kwa mwili wenu na mukashindana kwa kuzarau mauti; tena mulipokea tuzo ya kazi yenu mukawa wariti wa ufalme wa mbinguni*:* Ombeni kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.

Wakati Bikira Mtakatifu kamili aliona Mwana-Kondoo ametundikwa msalabani akapaza sauti akilia*:* Ee Mwanangu mpole, hii ni jambo gani la ajabu na mpya? Namna gani huyu mwenyi kushika ulimwengu mkononi mwake anasulubiwa mwilini juu ya muti?

Kisha mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma hii sala:

Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

Kisha Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha Trisagion hatuimbe Apolitikia, lakini padri ao Mukubwa padri ya Kanisa anasema hii sala:

Ee Mzazi-Mungu, mlango wa mbingu, tunaposimama hekaluni kwa utukufu wako, tunazani ya kama tunasimama mbele ya mbingu, basi, utufungulie mlango ya huruma yako.

Msomaji*:* Bwana hurumia *(mara makumi ine).* Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana bariki, ee Rabi.

Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Padri ao Mukubwa ya Kanisa anasoma hii sala:

Ewe Mfalme wa mbingu, chunga waaminifu, wafalme, wetu; sabitisha imani; leta amani kwa inchi zote; ukimya duniani; linda vema Kanisa yetu Takatifu (Mission ao Monasteri); wale walioondoka toka hii dunia*:* Mapadri na ndugu zetu uwaweke pahali pa wenye haki; na sisi utupokee katika toba na ungamo kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Elezo*: Kisha tunafata ma desturi ya kupika magoti pamoja na ma sala ya Mtakatifu Mutawa Efremi (ona yulu).*

Kisha tunasoma Saa wa Kwanza ya kusema:

Njooni tumwanamie. . . .

Na padri anafanya Kuaga, katika desturi.

MU KAZI TATU YA JUMA YA JIVINI KWA MANGARIBI.

Elezo*: Tunasoma Proimiakos, tunaimba wimbo ya Paraklitiki na Mineon. Kisha Utukufu. . . Sasa. . . Theotokion ya Paraklitiki.*

Mwangaza upole. . .

Prokimenon. *Sauti ya tano.*

Uniokoe, ee Bwana, kwa jina lako, na unihukumu kwa uwezo wako.

Shairi*:* Ee, Mungu, sikia maombi yangu.

Somo ya Nabi Yoeli tutasoma. (4, 12-21).

Mataifa yaondoke, wapande kwa bonde la Yosafati; kwa maana nitakaa pale kuhukumu mataifa yote yanayonizunguka. Ingisheni mundu kwani mavuno yameiva; kujeni mukanyage kwa sababu shinikizo la mvinyo limejaa, mashinikizo yamejaa na kufurika; kwa maana uovu wao ni mukubwa. Wingi, wingi katika bonde la kukata maneno! Kwa maana siku ya Bwana ni karibu katika bonde la kukata maneno. Jua na mwezi na giza na nyota zinaacha kuangaza. Bwana atanguruma toka Sayuni, atatoa sauti yake toka Yerusalema; na mbingu na dunia zitatetemeka; lakini Bwana atakuwa kimbilio kwa watu wake, na boma la nguvu kwa wana wa Israeli. Hivi mutajua ya kama mimi ni Bwana, Mungu wenu, nikikaa katika Sayuni, mulima wangu mutakatifu; halafu Yerusalema utakuwa mutakatifu, wala wageni hawatapita tena katikati yake. Na itakuwa katika siku ile milima itadondoza mvinyo mpya, na vilima vitamwanga maziwa, na mito yote ya Yuda itatoa maji mengi; na chemchemi itatokea katika nyumba ya Bwana na kunyesha bonde la Sitimu. Misri itakuwa ukiwa, na Edomu itakuwa jangwa la ukiwa, kwa sababu ya ukali waliofanyiwa wana wa Yuda kwa sababu wamemwanga damu safi katika inchi yao. Lakini Yuda atakaa milele, na Yerusalema kwa kizazi na kizazi. Na nitasafisha damu yao nisioisafisha, kwa maana Bwana anakaa katika Sayuni.

Prokimenon. *Sauti ya sita.*

Ee Israeli utarajie Bwana, tangu sasa na hata milele.

Shairi*:* Ee Bwana, moyo wangu hauna kiburi, wala macho yangu hayanyanyuliwi;

Kisha tunasoma: Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi. . .

APOSTIKHA

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Wakati wa Kwarezima imefika pamoja na ua la roba; enyi ndugu, tujitakaseni kwa zambi yote na tumuimbieni chemchem, yetu ya nuru; tumuambieni; Ee Mpwenda-wanadamu, utukufu kwako.

Shairi*:* Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*
Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi*:* Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Ee Bwana, Mashahidi wako waliposaidiwa kwa imani, waliposabitishwa kwa matumaini, na walipoungana katika roho kwa mapendo ya Msalaba wako, wakaharibu uzulumu wa adui; walipopokea taji ya milele, wanaomba pamoja na malaika kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Malkia wa utakatifu, wewe utukufu wa majeshi ya mbinguni, wimbo wa Mitume, utimilifu wa maandiko ya unabii, ee Bibi wetu, pokea maombi na nyimbo zetu.

Kisha Mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma:

Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

Msomaji*:* Trisagion*:* Mungu Mtakatifu. . Utatu Mtakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Kisha tunaimba Apolitikia ya Watakatifu ya hii siku.
Kisha padri atafanya Kuaga, katika desturi ya kila Sala ya Mangaribi.

MU KAZI INE YA JUMA YA JIVINI KWA ASUBUI.

Kisha Eksapsalmos. Bwana ndiwe. . . Apolitikia ya Watakatifu ya hii siku. Kathisma ya kwanza ya Paraklitiki na kisha hii Kathisma ya Triodio.

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya tano. Ton Sinanarhon Logon.

Leo, Mitume wote wanafaa taji kwa hii siku Kuu yenyi kutangulia Kwarezima ya utakaso, na kwa kufunga wanatakasa wakati kwa amri ya Kristu Mwokozi wetu; wanawatangazia watu wote Ufufuo wake na wanamuomba Bwana kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu. . . *(mara ingine hii).*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. Sauti umoja.

Ee Bikira Mtakatifu, wewe boma la wenye kukutumainia, utuokoe kwa kishawishi yote, kwa masumbuko yote na kwa hatari yote; pamoja na Mitume wa Kristu umuombe Mwana wako kwa ajili ya wokovu wa wote wale wenye kukutolea nyimbo.

Pa fasi ya Eksapostilarion tunaimba Fotagogikon ya hii siku.

DOKSOLOGIA KIDOGO

na kisha:

APOSTIKHA.

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Uzuri wa kufunga inangaa, inafukuza giza ya mashetani; utakatifu wa Kwarezima imeonekana, inaleta dawa ya tamaa; zamani Nabii Danieli na Vijana wa Babyloni waliisikia*:* Wa Kwanza alifunga kinywa cha simba, wengine walishinda tanuru ya moto; ukitupatia fazila ileile, ee Kristu Mungu wetu Mpenda-wanadamu, utuokoe.

Shairi*:* Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .
Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi*:* Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .
Kama nyote, mwangaza ulimwengu hata kisha kufa kwenu, ee Mashahidi takatifu; muliposhindana vema, muna uwezo wa kumuomba Kristu kusudi alete neema ya wokovu kwa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Katika wanawake wote, peke yako ni Mama asiyeolewa, ee Mtakatifu Mzazi-Mungu umuombe Mfalme Mtakatifu aliye Mwana wako, atuokoe kwa mapendo yake kwa wanadamu

Elezo*: Kisha mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma hii sala:*
Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

Kisha Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .
Elezo*: Waimbaji wanaimba Apolitikia ya Watakatifu ya hii siku.*
Katika desturi padri anafanya Kuaga.

MU KAZI INE YA JUMA YA JIVINI KWA MANGARIBI.

Elezso: Tunaimba Wimbo ya Paraklitiki na Mineon. Utukufu. . . Sasa. . . Theotokion katika desturi, kisha Mwangaza upole. . . , Prokimenon ya hii siku.

APOSTIKHA.

Sauti ya mbili. Idiomelon.

Kwa wabudu wake Msalaba wa Bwana ni kuzuio ya furaha yote na inawaalika kufunga, kwani wakimutazama msulubiwa wanasulubisha mwili na tamaa zake; na sisi pia kwa kufunga tujitakaseni kusudi tuungane na huyu aliyetupenda na kutupokea katika mateso yake, akatufanya zawadi ya hali yake ya uvumilivu na kutupatia neema ya wokovu.

Shairi*:* Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*
Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.
Shairi*:* Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Walipokataa furaha ya hapa chini, Mashahidi Watakatifu walipokea hazina ya mbinguni; wakawa wenzao ya Malaika*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie na kutuokoa.

Utukufu. . . Sasa. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira, wakati uliona ametundikwa msalabani zabibu uliyezaa bila kulima ukapaza sauti ukilia*:* Ee Mwanangu, acha kutelemuka kinywaji kitamu kitaachisha ulevi ya tamaa wakati nikapokuomba kama mama, ewe Mungu wa mapendo tena Mwema.

Elezo*: Padri ao Mukubwa ya kanisa anasoma:*

Sasa Bwana umuache. . .

Elezo*: Trisagion na Apolitikia ya Kwarezima na Metania na sala ya Mtakatifu Efremi, sawa ni desturi mu kazi mbili mangaribi ya hii Juma.*

MU KAZI TANO YA JUMA YA JIVINI KWA ASUBUI .

Elezo*: Kisha Eksapsalmos tunaimba pamoja na ma shairi Alliluia, katika desturi na siku ya hii Juma Mukazi Tatu asubui. Pahali fasi ya Apolitikia tunaimba Wimbo ya Utatu Mtakatifu (Triadika Megalinaria) na sauti ya hii Juma. Tafuta hii Wimbo ku mwisho ya hii Kitabu Triodi. Kisha tunaimba Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na wa mbili tunaimba hii:*

KATHISMA .

Sauti ya saba. Os ehusa to simpathes.

Ee Msalaba heshimiwa, pandisha uso ya waaminifu na kwa uwezo wako shusha majivuno ya wahalifu; uwape wakristu wa Orthodoksi wafurahi katika wewe na uturuhusu twende kukutana na wewe kwa maandamano kusudi ya kusujudu mbele ya kiti cha Kristu, kwa kuwa wewe ni utukufu wetu, ee Msalaba takatifu na Mwokozi.

Utukufu. . . *(mara ingine hii).*

Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**. *Sauti umoja.*

Unahurumia mateso yetu na unaona watu wa dunia*:* Hurumia watu wenye kutwaliwa, ee Mzazi-Mungu tena Bikira Mtukufu; ujiharikishe kuombea sababu ya kutuondolea mwisho mbaya; ee Bikira Mtakatifu na safi kamili, umuombe Mungu wa wema aokoe roho zetu.

Tunasoma Zaburi 50 (51) na kisha Kanuni.

KANUNI.

Sauti ya mnane. Igran diodefsas.

Wimbo wa kwanza.

Kwa kufunga, wakati takatifu inawangazia wote nuru ya toba yenye kufukuza giza ya zambi*:* tuipokee na furaha rohoni mwetu.

Tazama neema ya toba, Kwarezima inageuza roho zetu, tuiendee kwa kadiri sababu ya kupokea maondoleo ya zambi zetu.

Wafalme Watawala, Wakheruvi na Majeshi yote ya mbinguni, ombeni ili tutimize wakati wa kufunga na akili ya toba na ya utakaso.

THEOTOKION

Ee Bikira Mtakatifu, peke yako boma ya waaminifu, saidia watu wote kwa wakati wa Kwarezima ombea wote wale wenye kukutambua kama Mzazi-Mungu.

Sauti umoja. Uranias apsidos.

Wimbo wa tatu.

Kwa uvumilivu tufukuzeni tamaa, kwa kufunga tusabitisheni roho yetu; tuonyesheni matunda ya kweli ya toba, maana kwa makosa yetu tulimusirikisha Mungu wa rehema.

Wote tushike mikononi taa yenye kuwaka na mafuta ya matendo mema ili pamoja na mabikira wenye akili tuingie na furaha katika nyumba yenye kujaa na nuru.

Enyi Manabii wenye kuongozwa, enyi Mashahidi wa Mungu na Mitume Watakatifu wa Mwokozi, ombeni kwa Mungu kusudi wote tuanze na tumalize vizuri muda wote wa Kwarezima.

THEOTOKION.

Ee Bibi wetu, shima la mema yote, sisi waaminifu tunakuomba*:* Kuja utusaidie katika mashindano, kwa mwisho ya Kwarezima utuokoe.

IRMOS*:* Ee Bwana uliyefunika paa la mbingu na uliyejenga Eklezya katika siku tatu, kwa mapendo yako unifanye kuwa imara wewe peke yako Mpenda-wanadamu, pahali pa juu pa matakwa yetu tena ngome ya waaminifu.

Elezo*: Pa fasi ya Eksapostilaria tunaimba Foragogikon ya sauti ya hii Juma. Tafuta ku mukongo ya hii Kitabu.*

APOSTIKHA.

Sauti ya sita. Idiomelon.

Mbele ya Msalaba wa Mwokozi wakati zambi na uovu zilitawala, watu walitukuza furaha na nguvu za mwili; lakini ilipotimizika fumbo ya Msalaba uzulumu wa Hadeze ikaondolewa kwa maarifa ya Mungu, fazila ya mbinguni inaenezwa duniani; na tena Kwarezima ikaheshimiwa, kufunga ikawa na nuru, maombi ikasabitishwa*:* Mshuhuda ni wakati wa sasa tunaopewa na Kristu Mungu wetu mfufuliwa kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Shairi*:* Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .
Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi*:* Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .
Ee Bwana, kwa kuwakumbuka Mashahidi wako ni siku Kuu ya viumbe vyote*:* Dunia ya watu inafurahi pamoja na Malaika mbinguni; kwa maombezi yao utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili alipokuona umetundikwa msalabani, kwa machozi akakulalamikia*:* Ee Mwanangu na Mungu wangu, ee Mwanangu mupendwa, namna gani unaweza kuteswa na hii Mateso isiyo na haki?

Elezo*: Kisha mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma hii sala:*
Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

Kisha Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .
Elezo*: Kisha Trisagion, hatuimbe Apolitikia, lakini padri ao Mukubwa padri ya Kanisa anasema hii sala:*

Ee Mzazi-Mungu, mlango wa mbingu, tunaposimama hekaluni kwa utukufu wako, tunazani ya kama tunasimama mbele ya mbingu, basi, utufungulie mlango ya huruma yako.

Msomaji*:* Bwana hurumia *(mara makumi ine).* Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana bariki, ee Rabi.
Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
Padri ao Mukubwa ya Kanisa anasoma hii sala:

Ewe Mfalme wa mbingu, chunga waaminifu, wafalme, wetu; sabitisha imani; leta amani kwa inchi zote; ukimya duniani; linda vema Kanisa yetu Takatifu (Mission ao Monasteri); wale walioondoka toka hii dunia*:* Mapadri na ndugu zetu uwaweke pahali pa wenye haki; na sisi utupokee katika toba na ungamo kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Kisha tunafata ma desturi ya kupika magoti pamoja na ma sala ya Mtakatifu Mutawa Efremi (ona yulu).

Kisha tunasoma Saa wa Kwanza ya kusema:

Njooni tumwinamie. . . .

Na padri anafanya Kuaga, katika desturi.

MU KAZI TANO YA JUMA YA JIVINI KWA MANGARIBI.
(Makumbusho ya Watawa Watakatifu)

Elezo*: Tunasoma Zaburi ya Proimiakos, kisha:* «Bwana nimekuita. . . » *na tunaimba wimbo hii, kila wimbo mara mbili.*

Sauti ya mnane. Defte apantes pisti.

Kujeni, enyi waaminifu wote, tushangilie makumbusho ya Wapadri wetu Watakatifu. Ya Antonio mkubwa, ya Eftimi wa nuru, ya wote na ya kila mumoja; na kama Paradizo mpya ya furaha munamotembea uzima yao, tutaimbia na furaha hii miti Mungu wetu alipanda iliyozaa matunda ya milele ya uzima na akawaleta kwa Kristu kuwa Chakula cha roho zetu. Enyi Wapadri wenyi heri na Wabebaji-nuru, ombeni kwa ajili ya wokovu wetu. *(mara mbili).*

Salamu, ewe Misri ya imani, salamu ewe Libya takatifu, salamu ewe Thabaidi mchaguliwa! Ifurahiwe pahali pote, inchi yote, mji yote iliyolisha wazaliwa wa ufalme wa mbinguni, kwa kuwastawisha kwa kufunga na kazi na wakawa, kwa mapendo ya Mungu, watu kamilifu, na kwa ajili ya roho zetu wakawa nyota za nuru zenye kuangazia mipaka ya ulimwengu kwa nuru ya matendo yao na ya miujiza yao. Enyi wa Padri wenye heri na Wabebaji-nuru, ombeni kwa ajili ya wokovu wetu. *(mara mbili).*

Mutu gani wa mauti anaweza kueleza uzima yenu ya ajabu, enyi wa padri Watakatifu kamili? Luga gani itatangaza mashindano yenu ya kiroho, kazi yenu ya kupata fazila, mateso ya mwili wenu, mashindano yenu juu ya mateso, machozi, kukesha ao maombi? Katika hii dunia mumeonekana kweli kuwa kama Malaika, muliharibu nguvu ya mashetani, mulifanya miujiza na alama za ajabu. Enyi wa padri wenye heri, mutuombee ili tupate furaha ya milele. *(mara mbili).*

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita.*

Mulipolinda salama sura na mfano, mashindano ya roho juu ya mateso, mulikaza ulimwengu kwa kushinda uovu kwa mema, mwili kwa roho; mulifikia ncha ya uzima, ya utawa, enyi watu wa jangwa, walimu wa uvumilivu tena mifano ya fazila; na sasa mbinguni, ee wa Padri Watakatifu, munaona waziwazi apana kwa kioo, lakini katika Utatu Mtakatifu ambako munaombea wale wenye kuwatukuza ninyi kwa imani na mapendo

Sasa na siku zote. . .

Theotokion ya sauti ya hii Juma.

Mwangaza upole. .

Prokimenon ya hii siku.

Somo ya Unabii ya Nabii Zakharia. (8, 19-23)

Bwana wa majeshi anasema hivi*:* Kufunga chakula kwa mwezi wa ine, na kufunga chakula kwa mwezi wa tano, na kufunga chakula kwa mwezi wa saba, na kufunga chakula kwa mwezi wa kumi, kutakuwa furaha na shangwe, na karamu za furaha kwa nyumba ya Yuda; kwa sababu hii pendeni kweli na salama. Bwana wa majeshi anasema hivi*:* Itakuwa tena mataifa na wenyeji wa miji mingi watakuja; na wenyeji wa muji mumoja watakwenda kwa mwingine, wakisema, twende kwa haraka kuomba ukubali kwa Bwana, na kutafuta Bwana wa majeshi*:* Mimi nitakwenda vilevile. Ndiyo, watu wengi na mataifa ya nguvu watakuja kutafuta Bwana wa majeshi katika Yerusalema, na kuomba rehema ya Bwana. Bwana wa majeshi anasema hivi*:* Itakuwa kwa siku zile watu kumi wa lugha zote za mataifa watakamata upindo wa nguo yake aliye Muyuda; ndiyo, wataushika wakisema*:* Tutakwenda pamoja nanyi, kwa maana tumesikia ya kuwa Mungu ni pamoja nanyi.

Prokimenon. *Sauti ya sita.*

Ee Israeli utarajie Bwana, tangu sasa na hata milele.

Shairi*:* Ee Bwana, moyo wangu hauna kiburi, wala macho yangu hayanyanyuliwi;

Padri*:* Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi. . .

APOSTIKHA

Sauti ya mbili. Idiomelon.

Ee Ndugu, tujitakaseni kwa zambi yote ya mwili na ya roho, na kwa ajili ya roho zetu tushike taa yenye kuwaka na mapendo kubwa bila kujirarua vibaya sisi wenyewe wamoja kwa wengine, kwani tazama saa imekuja Bwana Arusi atakuja kulipa kila mumoja kadiri ya matendo yake; pamoja na mabikira wenye akili tuendeni kukutana na Kristu tukimulalamikia kama munyanganyi*:* Utukumbuke, ee Bwana, wakati utakapoingia katika Ufalme wako.

Shairi*:* Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi*:* Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Mashahidi Watakatifu wanatuombea, nyimbo zao zinamutukuza Kristu*:* Tangu hapo upotevu imeondolewa, wanadamu wanaokolewa kwa imani.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane.*

Tunawatukuza ninyi watawa wote, ee wa padri Watakatifu, kama waongozi wetu wa roho; kwa ninyi tulifunza kutembea katika njia sawa; ninyi ni wenye heri maana mulimutumikia Kristu wakati mulipoharibu nguvu ya adui, enyi rafiki za malaika, za wenyi haki na za watakatifu; pamoja nao ombeni Bwana ahurumie roho zetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.** *O, tu paradoksu thavmatos*

Salamu, ewe hazina ya usafi, salamu, ewe makao ya nuru, salamu, ewe mwanzo wa wokovu wetu; salamu, ewe utukufu wa Mitume na wa mashahidi, salamu ewe utimilifu wa Manabii, salamu, ewe mapambo ya watawa, salamu, ewe wokovu wa waaminifu.

APOLITIKION

Sauti ya ine.

Ee Mungu wa Baba zetu, wewe mwenye kutuhurumia daima, usiondoe mbali nasi rehema yako, lakini kwa maombezi yao ongoza uzima yetu katika amani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Sauti umoja.

Siri ya kificho tangu milele iliyokuwa isijulikane na Malaika, imeonekana duniani katika wewe, ee Mzazi-Mungu; maana Mungu alitwaa mwili kwa muungani bila muchanganyo, na alikubali msalaba kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; juu ya hii akifufua Muumbwa wa kwanza, akaokoa toka lufu nafsi yetu.

Elezo: Kesho asubui, kisha Eksapsalmos tutaimba: «Bwana ndiwe. . . » na hii wimbo ni yulu.

SIKU YA POSHO YA JUMA YA JIVINI KWA ASUBUI.

KATHISMA WA KWANZA.

Sauti ya mnane. To prostahthen mistikos.

Tunapoangazwa kwa nuru ya wa Padri Watakatifu, tuingieni sasa katika Paradizo ya siri na tufurahie maji yake; tunapoona ushujaa wao, tushindane kwa fazila na tumulalamikie Mwokozi*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana, utupe tuingie katika Ufalme wa mbinguni.

Utukufu kwa Baba. . . Umoja.

Wote pamoja na kwa sauti moja tuimbie watawa wa kwanza Paulo wa Thebes, Antonio mwenye hekima, Efthimi Mkubwa na wa Padri wengine wote waliwafwata; tuwaombe wamuombe daima Bwana kwa ajili yetu sisi kushangilia makumbusho yao kimungu na yenye kujaa na nuru, tukimutukuza katika nyimbo zetu Kristu Mwokozi wetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Umoja.*

Tunakushukuru, ee Mzazi-Mungu, tunakutukuza na tunasujudu mbele yako, tunaposhangilia uzazi wako tunakulalamikia daima*:* Utuokoe, ee Bikira Mjalizwa neema, kwa neema yako, utuokoe kwa maneno mabaya ya shetnai kusudi wakati wa hukumu watumishi wako wasipate haya.

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya mnane. Anestis ek nekron.

Kujeni wote tuwaimbie wa padri wetu Watakatifu, Antonio mkubwa, Efthimi na Wabebagi-Mungu wengine, na kwa nyimbo zetu tushangilie makumbusho yao, kwani mbele ya Bwana wanaombea dunia yote kusudi tuokolewe toka laana ya zamani na kwa azabu ya milele.

Utukufu kwa Baba. . .*(Mara ingine)*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Sauti umoja. *To prostahthen mistikos.*

Ee Kristu, kwa maombezi ya wa Malaika wako na ya Mtangulizi, ya wa fuasi wako, ya Manabii na ya Mashahidi, ya wenye haki wote na ya Watakatifu wote, na hasa ya Mama yako Bikira Mtakatifu kamili, utupe tutembee katika nuru yako na kwa wema wako utupe Ufalme wa mbinguni.

Tunasoma Zaburi 50 (51).

KANUNI

Sauti ya mnane. Asma anapemsomen.

Wimbo wa kwanza.

Tuimbe kwa sauti moja nyimbo za kiroho tukitukuza wale walioangaa kwa utawa wao, wa padri wetu watakatifu wa Misri, wa Thebaidi na wa Libya, wa pahali pote na wa mji yote.

Salamu, ewe mwalimu wa Watawa, Antonio mtukufu, pamoja na Ammoni mbebabji-Mungu, tukufu wa Nitria, Arseni huyu Malaika katika mwili na Ammonasi mwenye kujaa na Roho Mtakatifu.

Furahi, ewe Agathoni mbebaji-Mungu, Akila, Amoe, mana ya jangwa, Anubi, Alonios, Amonathas pamoja na Anthimi, lulu ya samani ya fazila.

Tuimbieni mianga ya akili, Aresi na Apollo mkubwa, hii taa ya utii, Athre na Akakios; pamoja nao anangaa Abakiri kama nyota ya asubui.

Afksentios ameonekana kuwa mlima wa uzima kubwa, Abramios mkubwa ni bingwa wa usafi, Afrodisios na Athenodoros walikuwa pamoja nao nguzo za utaratibu.

Watawa Ammonios na Aninas wanangaa kama nyota mbinguni; pamoja nao anangaa Antiohos na kupita wote ni Mtakatifu Agapitos.

Kwa nyimbo zetu takatifu tunatukuza Athanasi ambaye utawa wake iliangaza mulima takatifu, yeye nyota mwenyi kuangazia ulimwengu yote*:* Kwa maombezi yake sisi wote tumeokolewa.

Kwa uzima wenu wenyi kujaa na Mungu mumekuwa kwa Eklezya paradizo ya kweli; enyi wa Padri Watakatifu, kila mumoja kadiri ya jina lake, mutuombee sisi kwa Bwana.

Kujeni, enyi waaminifu rafiki za Mashahidi, tushangilieni kila mwaka makumbusho ya Washuhuda wa Kristu, tukimutolea Kristu Mungu wetu utukufu; tutakuimbia wewe peke yako Bwana wetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Naimbia, hali moja ya watu tatu katika Mungu mumoja, umungu mumoja wa Baba, wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu ufalme wa milele.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Salamu, ewe Hekalu Takatifu, manyonya yenyi kujaa na umande, kisima cha uzima wa milele, ee Bibi yetu, linda taifa lako kwa mashambulio ya ma adui.

Sauti umoja. Uk estin agios os si. . .

Wimbo wa tatu.

Tuingieni katika hii Paradizo mpya, hii ya fazila za wa Padri wetu watakatifu, ambayo tunashangilia na ibada tukionja furaha za kiroho zenye kuleta uzima wa milele.

Kwa nyimbo zetu tutukuzeni Zosima wa ajabu, mtukufu Zakharia, Zenoni na Zoila, Isaya mkubwa; na mtukufu Elia, pamoja na pokea alama zetu za heshima.

Naimbia Theodoro mwema wa Thermis na Ennatoni mwenyi kustahili kamili nyimbo zetu; pamoja nao natukuza Theonasi na Theoduli; natukuza pia Theodosi mkubwa na wa ajabu.

Tutukuzeni Theoktistos, huyu mwalimu wa ajabu, Thalassios mkubwa, Theodoro mkubwa anayeitwa Musikeoti mabaye alionekana kuwa wa mbinguni duniani kwa miujiza na ishara yake.

Nyota zingine zinainuka zenye kuangaa*:* Yoane mdogo pamoja na wabebaji-nuru ya Mungazi, na wengine wengi ambao waliangazwa kwa utukufu.

Kujeni tutukuzeni kwa nyimbo zetu za kiroho makumbusho ya kila mwaka ya Mashahidi Watakatifu, kwani wanamuomba daima Kristu kwa ajili ya wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Utatu wa asili moja, Umungu moja, wenye kuchunga umoja bila kutengana, utukusanye sisi kwa hamu ya amri zake.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira, alipoeleza hekalu takatifu na wa Serafi waliofunika Patakatifu Musa alitangulia kuonyesha kuzaa kwako kwa ubikira na Kristru aliyekaa tumboni mwako.

IRMOS. *Hakuna aliye mtakatifu kama Bwana, hakuna aliye mwenye haki kama Mungu wetu viumbe vyote vinaimbia, na hakuna aliye mtakatifu kama wewe Bwana mpenda-wanadamu.*

KATHISMA.

Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.

Enyi waaminifu, kwa nyimbo zetu tutukuzeni upole na utakatifu wa Antonio, miujiza na ukubwa wa Efthimi, utulivu na fazila ya Paulo na ya Arsenios utukufu wa Theoktistos na fazila za Watakatifu wengine wote; pamoja nao tumuimbie bikira Efpraksian pamoja na wanawake wote waliopokea hekima kwa Mungu na tulalamike kwa sauti moja*:* Mutuombee kwa Kristu Mungu wetu awasamehe makosa yao wale wenye kushangilia na mapendo makumbusho yenu takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Umoja.

Mulipovunja minyororo ya mateso, mukaambatana na mapendo ya fazila, katika Kristu mukavaa utukufu wa milele, na kwa mateso yenu mulipata mapumziko, kwa kiasi yenu mulipokea uzima wa milele; mulistahili kufurahi pamoja na Majeshi ya mbinguni, kwa nyimbo za furaha munasimama mbele ya Mungu, enyi wa Padri wabebaji-Mungu, muwaombee wale wenye kushangilia na mapendo makumbusho yenu takatifu maondoleo ya zambi.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. Umoja.

Nimezama katika matope ya zambi, nguvu imenikosa; mawimbi ya makosa yangu yamenizamisha, lakini wewe uliyezaa Neno, peke yake rafiki yetu, nakuomba tazama mtumishi wako; uniokoe kwa zambi, kwa mateso ya mauti na kwa uharibifu wote wa adui ili niimbe na furaha, ee Bibi wetu*:* Umuombe Kristu Mungu anisamehe makosa yangu, kwani mimi ni mtumishi wako, na wewe ni matumaini yangu.

KONTAKION

Sauti ya mnane

Kama watangazaji wa ibada walivyonyamazisha makafiri, uliangazia Wapateri wetu Watakatifu wabebaji-Mungu sababu ya kuangazia dunia yote; kwa maombezi yao linda katika amani wale wenye kukutukuza na kukuimbia*:* Alleluia.

IKOS.

Nilipokuwa mwekevu kwa uzuri wa hii dunia, niliweza kuona kwa akili hii inatoa, nilipima mateso yake na nilihurumia uzima wa wanadamu; peke yenu kati ya wote, na wazania nini kuwa wenye heri, ninyi muliochagua sehemu nzuri kwa kuteswa pamoja na Kristu na kuishi pamoja naye, na mukiimba daima pamoja na Nabii Daudi*:* Allyluia.

SINAKSARI.

Elezo: *Sasa ku mwanzo tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha Sinaksasi hii.*

Leo tunakumbuka Watakatifu wote, wanaume na wanawake, waliangaa kwa utawa wao.

Kwa kukumbuka milele roho za watawa na sifa yangu ya milele.

IRMOS YA SABA.

Zamani wewe uliyefunika katika tanuru ya moto Vijana kwa umande na kulinda ubikira wa Mama yako kisha kuzaa, ee Bwana Mungu wa Baba zetu, umetukuzwa.

IRMOS YA MNANE.

Tunamusifu, tunamwimbia na tunamusujudu Bwana.

Huyu aliyetukuzwa juu ya mlima takatifu na kumufunulia Musa katika kichaka cha moto siri ya Mama bikira daima ni Bwana, mumuimbieni, atukuzeni milele.

IRMOS YA TISA.

Huyu aliyemufunulia mpana-sheria mlimani katika kichaka cha kuzaa kwa ajabu kwa Bikira daima kwa ajili ya wokovu wetu, tunamutukuza kwa nyimbo zetu.

EKSAPOSTILARION

Sauti ya mbili. Ginekes akutisthite.

Enyi wa padri watakatifu wengi muliokataa dunia kwa kuchukua msalaba na kundi la Mashahidi, Waierarka na pia Wanawake Watakatifu, angazeni roho zetu ili tustahili kuimbia makumbusho yenu tukufu.

INGINE.

Tis Mathites sinelthomen.

Kwa nyimbo zetu za furaha tutukuzeni wote wale waliangaa katika utawa, wa Padri wetu wabebaji-Mungu pamoja wa ma askofu, ma kundi wa Wabawake watakatifu na ya mashahidi ili tutakaswe na kwa furaha tufanye Kwarezima nzuri kwa maombezi yao na yale ya Mzaz-Mungu.

MASIFU.

Sauti ya mnane. O en Edem Paradisos.

Enyi waaminifu, kwa nyimbo zetu tutukuzeni wa padri wote waliyoishi safi katika utawa, enyi ndugu kwa moyo mumoja tusifuni wa Ierarka wa Kristu wale ambao waliishi kwa kufunga na kiasi na walituangazia kwa Habari njema ya Kristu; pamoja nao tutukuzeni pia wanawake waliobeba nuru takatifu; tufananishe rohoni mwetu utakatifu wa uzima yao sababu ya kupata maondoleo ya zambi.

Ndugu, wale wote waliangaa kwa utawa wao na kuishi kwa utakatifu tutukuzeni utukufu wao, maana wanakaa katika furaha ya uzima wa milele, wanafurahi milele na heri kisha kutembea njiani sawa kwa utakatifu; tuwatukuzeni kusudi watupokelee kwa Mungu, pamoja na rehema yake, furaha na utukufu wa milele na ukombozi wa azabu isiyo na huruma.

Ninyi wote, Wenye haki, Watawa, Waierarka na pia Wanawake watakatifu, ninyi muliyoishi na uzima takatifu, kwa mapendo yenu inameni kwa ajili yetu na mumuombe Bwana ambaye peke yake aliye na mapendo na wema, atuhurumie, asituhukumu, lakini atupe, kwa maombezi yenu, furaha ya mapumziko ya milele, kusudi na sisi pia tuweze kumuimbia milele Bwana aliye chemchem ya uzima.

Enyi waaminifu, leo tupigeni mikono na furaha kwa kuwakumbuka wa Ierarka Watakatifu, Watawa, Mashahidi, Wanawake Watakatifu wa Watakatifu wote; kwani, kweli walizarau uharibifu waliikadirisha kama majivu na moshi sababu ya kupata ufalme wa Kristu na mema yaliyotayarishwa na Mungu ambaye jicho halikuona na sikio halikusikia. Kwa maombezi, ee Bwana , okoa roho zetu kwa mauti.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita.*

Enyi wa padri watakatifu, makelele ya mambo yenu makubwa ilisikilika duniani kote, tuzo ya mateso yenu muliipata mbinguni; muliharibifu majeshi ya mashetani, mulipata Malaika mbinguni kisha kufananisha uzima yao; ninyi muliyo na uwezo wa kusema na Bwana, mumuombe amani kwa ajili ya roho zetu.

Sasa na siku zote. . . *Sauti umoja.*

Ee Mzazi-Mungu, uko kweli Mzabibu uliyostawisha tunda la uzima, ee Bibi wetu, tunakuomba*:* katikati ya Mitume na ya Watakatifu wote, ombea roho zetu wokovu.

DOKSOLOGIA KUBWA.
Kuaga.

SIKU YA MUNGU YA JIVINI (TIROFAGU).

SIKU YA POSHO KWA MANGARIBI.

Elezo*: Kisha* «Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo ya Paraklitiki sita na ine ya hii Kitabu.*

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Bwana Mungu wangu aliniumba kwa utope, akanipa roho kwa pumuzi yake ya hai, akaniweka kuwa mkubwa wa vitu vyote vyenyi kuonekana duniani, na akanifanya kuwa mwenzao wa Malaika, lakini shetani kwa msaada ya nyoka akanikamata vibaya kwa ndoano, na Mungu akanitenga ku utukufu, akanitoa duniani kwa mauti; lakini wewe Bwana wa mapendo, uniite kwako.

Ole wangu, ee Bwana! Niliondoa vazi la Mungu wakati nilivunja amri yako kwa shauri la adui; nilivaa majani ya mtini na kanzu ya ngozi; nilikula chakula changu kwa jasho, na kwa kosa langu inchi imehukumiwa kuota miiba na mimea yenyi majani ya miiba, lakini wewe Bwana uliyezaliwa kwa Bikira nyakati za mwisho, unirudishe sababu ya kuingiza katika paradizo mupya.

Ee Paradizo pendelevu, uzuri ya kwanza, makao Mungu alifanya, furaha ya milele, utukufu wa wenye haki, uzuri wa manabii na makao ya watakatifu, kwa kivuno ya majani umuombe Muumba wa ulimwengu anifungulie milango nilifunga kwa kosa langu na aniache kuchuma ku muti wa uzima furaha nilipata kwako zamani.

Kwa uasi wake Adamu alifukuzwa Paradizoni na kuondolewa furaha yake wakati alidanganywa kwa maneno ya mwanamuke; alipokuwa uchi, akakaa mbele ya shamba na kulia. Ndiyo sababu, wote tupokee na bidii hii wakati, tufunge na kutii mafundisho ya Malaika ili tukubaliwe kwa Kristu na tukae mara ingine katika Paradizo.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita.* .

Adamu alikaa mbele ya paradizo akiomboleza, akalilia utupu wake*:* Ole wangu! Nimedanganywa na kuondolewa kwa werevu, nikajitenga mbali ya utukufu; Ole! Mimi niliyekuwa mujinga mutupu sijui nitafanya nini sasa. Ee Paradizo, hata mara moja sitaona furaha yako, hata mara moja sitamuona Bwana Mungu wangu, yeye Muumba wangu; kwa sababu ninapaswa kurudi kwa udongo huko nilitoka. Ee Mungu wa mapendo, nakulalamikia*:* Kisha kosa langu, unihurumie.

Sasa na siku zote. . **THEOTOKION**.

Elezo*: Tunaimba Theotokion ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma.*

Mwangaza upole. . .
Prokimenon*:*
Bwana anatawala, amevikwa utukufu. *(mara tatu).*

APOSTIKHA.

Elezo*: Tunaimba Apostikha ya Paraklitiki na sauti ya hii juma na Utukufu. . . tunaimba hii:*

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya sita.*

Adamu alifukuzwa Paradizoni sababu ya tunda lililokataziwa; alipokaa mbele ya mlango akalia kwa sauti kubwa akisema*:* Ole wangu! Ni nini imenifikia, mimi maskini? Nimevunja amri moja ya Mungu, na tazama nimenyanganya namna yote ya mema. Ee Paradizo uliyewekwa kwa ajili yangu ambamo Eva aliwekwa, umuombe Muumba wako aliye pia Muumba wangu anitulize na maua yako. Mwokozi akamujibu*:* Sitake kuharibu kiumbe changu, lakini nataka aokolewe na atembee mpaka kwa kujua ukweli, kwa sababu sikatae huyu anayekuja kwangu.

Sasa na siku zote*. . .* **THEOTOKION**. *Sauti umoja.*

Muumba na Mukombozi wangu, Bwana Kristu, ewe safi kamili, akitoka ku tumbo lako, na akinivaa, aliopoa Adamu toka apizo la kale; kwa hii tunakuita bila kuacha, ewe safi kamili, kwani wewe wiko Mzazi-Mungu na Bikira kweli, na tunasema «Salamu» ya malaika*:* Salamu, Bibi-Malkia mulinzi na kivuli na wokovu wa nafsi yetu.

Elezo*: Padri ao Mukubwa ya kanisa anasoma:*
Sasa Bwana umuache*. . .*
Msomaji: *Trisagion. . . Apolitikia na Kuaga katika desturi.*

SIKU YA MUNGU YA JIVINI KWA ASUBUI

Elezo*: Eksapsalmos, Bwana ndiwe. . . Apolitikion ya ufufuo ya Kristu, Theotokion. . . Kathisma ya Ufufuo. Kisha Zaburi 50(51) tunaimba hii wimbo ya wakati ya Kwarezima:*

Utukufu*. . . Sauti ya mnane.*

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana chemchem ya uzima; roho yangu ikeshe hekalu lako takatifu, ikichukua hekalu chafu la mwili wangu, lakini katika wema wako unitakase kwa mapendezi yako kubwa na mapendo yako ya huruma.

Sasa na siku zote*. . . Sauti ya mnane.*

Uniongoze njiani ya wokovu, ee Mzazi-Mungu, kwani nilichafua roho yangu kwa zambi, na kwa uvivu wangu nilitumia vibaya uzima wangu, lakini kwa maombezi yako takatifu uniopeo ku uovu wote.

Sauti ya site

Shairi: Unirehemu, ee Mungu sawasawa ni wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uufute makosa yangu.

Nikikumbuka wingi wa matendo yangu mabaya, mimi mwenye zambi, naogopa ile siku ya ajabu ya hukumu, lakini ninapotumainia rehema na ruhuma yako, napaza sauti kama Daudi*:* Unihurumie, ee Mungu, kadiri ya wema wako kubwa.

Tunasoma Zaburi 50 (51).

KANUNI

Sauti ya sita. Os en ipiro pezefsas o Izrail.

Wimbo wa kwanza.

Twende, ee roho yangu maskini, inakufai kulia sasa ukikumbuka mambo ya zamani, ya utupu wa zamani katika Edeni ambako ulipoteza furaha ya milele.

Ee Muumba wa viumbe vyote tena Fundi wa ulimwengu, zamani kwa mapendo yako kubwa uliponiumba kwa matope, ukanipa uzima na ukaniweka pamoja na Malaika wako kwa kukuimbia.

Ee Muumba na Bwana, kwa wingi wa wema wako ulipanda furaha mu Paradizo, ukaniamuru nitumie katika Edeni matunda mazuri na yenye kupendeza ya kutoharibika.

Ole wako, ee roho yangu maskini, katika Edeni ulipata uwezo wa kula tunda lote ile ile iliyokataziwa*:* Sababu gani ulivunja amri ya Mungu wako?

THEOTOKION

Ee Bikira Mzazi-Mungu, Binti wa Adamu katika mwili, wewe ambaye kwa neema ya Kristu ulizaa Mungu wetu, unirudishe sasa mimi kule Paradizo nilipoteza.

Sauti umoja. Uk estin Agios os si.

Wimbo wa tatu.

Zamani, nyoka aliponisikilia wivu sababu ya ukubwa wangu, akanongoneza kwa sikio la Eva kwa werevu na kwa kumudanganya; na kwa kosa lake nilifukuzwa kwa uzima.

Niliponyosha mkono kwa muti wa kujua mema na mabaya, nilikula tunda Bwana alilonikataza, kwa mshahara wa ujasiri wangu nilifukuzwa kwa utukufu wa Mungu.

Ole wako, ee roho yangu maskini, namna gani haukutambua ubaya, namna gani haukusikia udanganyifu na wivu wa adui? Akili yako ilipofuka na ulivunja amri ya Muumba!

THEOTOKION

Ee Bikira, matumaini yangu na ulinzi wangu, wewe ambaye peke yako ulifunika utupu ya zamani wa Adamu, unipe mara ingine kanzu ya milele.

IRMOS. Hakuna hata mmoja aliye Mtakatifu kama wewe Bwana Mungu wangu; ulitukuza nguvu ya waaminifu wema wako, na ulitutia msingi pa mwamba imara wa maungamo ya jina lako.

KATHISMA

Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.

Adamu aliondolewa furaha ya Pradizo kwa uchungu wa tunda; kwa ulafi wake alivunja amri ya Bwana, akatumwa kulima udongo huko alitoka; akapata chakula chake kwa jasho ya uso wake;. Ndiyo maana, tulindeni kiasi kusudi tusilie kama yeye mbele ya mlango wa Paradizo, lakini tujikaze kuingia.

KATHISMA INGINE.

Utukufu kwa Baba. . .

Sauti ya ine. O Ipsothis en to Stavro.

Tazama imeonekana wakati wa fazila, Mwamuzi eko mlangoni*:* Tusichafuke; lakini kwa kufunga tumutolee machozi yetu, sadaka yetu na sikitiko ya roho yetu tukipaza sauti*:* Tulikosa mingi sana kupita mchanga ya bahari, samehe wote, ee Mkombozi wa ulimwengu kusudi na sisi pia tupate ufalme wa milele.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Sauti umoja.*

Ee Mzazi-Mungu, japo uovu wetu, hata mara moja hatutaacha kutukuza utukufu wako; kwa sababu kama hautuombee, nani atatuokoa kwa hatari nyingi? Ni wewe mwenye kutuchunga katika uhuru; ee Bibi yetu, usitutenge mbali nawe, kwani unaokoa watumishi wako kwa kila hatari.

KONTAKION

Aftomelon

Sauti ya sita.

Ee Mwongozi wa hekima tena Rabi wa uwezo, mwalimu mwenye kutufundisha mlinzi wa maskini, sabitisha na kufundisha roho yangu, unipe neno, ee Neno la Mungu, maana siwezi kuzuia midomo yangu kukuimbia*:* Ee Mungu wa mapendo unihurumie mimi maskini mkosefu.

IKOS

Zamani Adamu alikaa akilia mbele ya mlango ya Paradizo; kichwa mikononi mwake, akasema*:* Ee Mungu wa Paradizo, unihurumie mimi maskini mkosefu.

Aliposukumwa kwa Malaika aliyemufukuza mu Paradizo na kumufungia mlango wa shamba la mbinguni, Adamu aliomboleza akisema*:* Ee Mungu wa mapendo, unihurumie mimi maskini mkosefu.

Ewe Paradizo ya furaha, hurumia uchungu wa bwana wako aliyeanguka, na kwa kivumo cha majani yako umuombe Muumba asikufunge milele*:* Ee Mungu wa mapendo, unihurumie mimi maskini mkosefu.

Ewe Paradizo yenye kujaa na nzuri na utamu uliyepandwa kwa ajili ya Adamu na kufungwa kwa ajili ya Eva, umuombe Bwana kwa ajili ya bwana wako aliyeanguka*:* Ee Mungu wa mapendo, unihurumie mimi maskini mkosefu

SINAKSARI.

Elezo: *Sasa ku mwanzo tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha Sinaksasi hii.*

Leo tunafanya makumbusho ya Adamu, Baba yetu wa kwanza, aliyefukuzwa Paradizoni.

Pamoja na Adamu na Eva walioanguka ubinadamu unalia na uchungu Paradizo yake iliopotea.

Kwa rehema yako isiyokadirika, ee Kristu Mungu wetu, utustahilishe ku furaha za Paradizo na katika mapendo yako kwa wanadamu, utuhurumie. Amina.

KATAVASIES

Sauti ya sita.

Wimbo wa kwanza.

Wakati wa Israeli walisafiri kilindini kama pa inchi kavu, na walipomuona Farao mzulumu ameangamizwa katika mawimbi, hapo wakapaza sauti*:* Tuimbieni wimbo wa ushindi kwa utukufu wa Mungu wetu.

Wimbo wa tatu.

Hakuna aliye mtakatifu kama wewe Bwana Mungu wangu; kwa wema wako ulitukuza nguvu ya waaminifu, na ukatuweka juu ya mwamba imara kwa kukiri jina lako.

Wimbo wa ine.

Kristu ni nguvu yangu, Bwana wangu na Mungu wangu*:* Huu ni wimbo kimungu Eklezya Takatifu inatangaza, na moyo kutakasa inamuheshimu Bwana.

Wimbo wa tano.

Ewe Mungu mwema mno, nakuomba, angaza na nuru yako ya umungu roho za wapenda wako wenye kukesha mbele yako ili wakujue, ewe Neno la Mungu, Wewe Mungu wa kweli mwenye kutuondoa giza ya zambi.

Wimbo wa sita.

Wakati ninapoona bahari ya hii uzima inanyanyuliwa kwa tufani ya vishahishi, nakimbilia ku bahari yako ya amani na napaza sauti, ee Mungu wa wema*:* Komboa uzima wangu ku shimo.

Wimbo wa saba.

Katika tanuru ya moto Malaika akawamwangia Vijana washarifu umande, lakini moto ukawateketeza wakaldea kwa amri ya Mungu, na mzalimu akalazimishwa kuimba*:* Umetukuzwa, Bwana Mungu wa Baba zetu.

Wimbo wa mnane.

Tunamsifu, tunamuhimidi, na tunamusujudu Bwana.

Toka moto ukachirikiza umande kwa ajili ya Watakatifu wako na kwa maji ukawakisha sadaka ya mwenyi haki, kwani ulitimiza vitu vyote paka kwa mapenzi yako*:* Ee Kristu, tunakutukuza milele.

Wimbo wa tisa.

Kwa wanadamu haiwezekane kumuona Mungu ambaye hata Malaika hawasubutu kutazama, lakini Neno aliyejifanya mtu kwako alionekana kwa wenye kufa, ewe Safi kamili, na wakati tunamutukuza pamoja na majeshi ya mbinguni tunakutangaza mwenye heri.

EKSAPOSTILARION.

Sauti ya mbili. Tis Mathites sinelthomen.

Ee Bwana, wale ulifukuza mu Paradizo sababu ya kula tunda lililokataziwa unawarudishimo kwa Msalaba wako na Mateso yako, ee Mwokozi wangu na Mungu wangu; ndiyo maana utupe sisi nguvu tufike safi ku mwisho ya hii Kwarezima sababu ya kuabudu Ufufuo wako Takatifu kwa kutimiza Paska ya wokovu kwa maombezi ya Mzazi-Mungu aliyekuzaa.

MASIFU.

Elezo*; Tunaimba Wimbo 5 ya Paraklitiki na 3 ya Triodion.*

Sauti wa tano.

Adamu kwa machozi alilalamika*:* Ole wangu! Mwanamuke na nyoka wameniondolea uraki wangu na Mungu, na kwa tunda la muti iliyokataziwa nimenyanganywa furaha za Paradizo. Ole wangu! Sasa sitasikia haya namna gani? Mimi zamani niliyekuwa mfalme duniani wa viumbe vyote vya Mungu sasa nakuwa mtumwa wao sababu ya shauri mbaya; zamani nilivaa nuru ya milele, lakini sasa, mimi maiti, nafunikwa sanda ya mauti. Ole wangu! Nani atalia pamoja na mimi? Lakini wewe, Bwana Mpenda-wanadamu uliyeniumba kwa udongo, uniondoe kwa utumwa wa adui, na kwa rehema yako uniokoe.

Shairi: Nitashukuru Bwana kwa moyo wangu wote, katika baraza ya wenye haki, na katika makutano.

Imefunguliwa, uwanja ya fazila*:* Wanaoingiamo na wale wanataka kujizoea! Jiwekeni tayari kwa mashindano ya Kwarezima! Washujaa watapokea taji ya ushindi, tuchukueni silaha ya msalaha sababu ya kushindana na adui tukichukua imani kama boma imara, maombi kama kanzu ya chuma, mapendo kama kofya, na kufunga kama upanga wenye kukata uovu wote wa roho zetu. Huyu atafanya hivi atapokea kweli taji mikononi mwa Kristu mwenyezi siku ya hukumu.

Sauti ya sita.

Shairi: Usimame, ee Bwana, nyanyua mukono wako, usisahau masikinim kwa nini mwovu anazarau Mungu.

Adamu alifukuzwa Paradizoni sababu ya kula chakula kilichokataziwa, lakini Musa alistahili maono ya Mungu kisha kutakasa macho ya roho yake kwa kufunga. Na sisi wenye kutamani siku moja kukaa katika Paradizo tujikatalie chakula cha upotevu; kama tunataka kumuona Mungu, sawa Musa tufungeni siku makumi ine tukidumu katika sala na maombi, na tutulizeni tamaa za roho zetu, tushideni mwili, tutembeeni kwa mwanendo wepesi katika njia yenye kwenda mbinguni, huko makundi ya malaika kwa sauti moja wanaimbia Utatu

usiyogawanyika sababu ya kuona uzuri wa ajabu wa Bwana. Ee Mwana wa Mungu, chemchem ya uzima, tunakutumainia wewe*:* Utuunganishe katika kundi la majeshi ya mbinguni, kwa maombezi ya Mama yako aliyekuzaa na ya Mitume, Mashahidi na ya Watakatifu wote.

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya sita.*

Tazama imekuja wakati wa mashindano ya roho, ushindi juu ya mashetani, kiasi kama silaha, sifa kuu ya malaika, tena matumaini kwa Mungu; katika hii Musa akawa msiri wa Muumba na aliweza kusikia sauti yake katika mafunuo isiyoonekana; katika hii, ee Bwana, utupe pia, kwa wema wako, tuabudu Mateso yako na Ufufuo wako Takatifu.

Sasa na siku zote. . **THEOTOKION**

Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa u Kristu Mungu wetu, uliyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA.

Kuaga.

MU JUMA MANGARIBI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA

Elezo: *Tunasoma Zaburi Proimiakos, «Bwana nimekuita. . . » na tunaimba wimbo ya Paraklitiki (Tafuta ku mukongo ya hii kitabu) na sauti ya hii juma na kisha tunaimba hii wimbo ya Triodi:*

Sauti ya mbili. Agelos men to Khere.

Tunapoingia katika kipindi cha Kwarezima, tujikaze kwa kiasi kuzarau mwili wetu, kwa maombi na machozi tumutafuteni Bwana Mwokozi wetu na tumwambie sababu ya kusahau matendo yetu mbaya*:* Tulikukosea, utuokoe kama Waninawe zamani, ee Kristu Mfalme wetu, kwa wema wako utupe ufalme wa mbinguni.

Ee Bwana, nasikitika wakati naona matendo yangu yenye kustahili azabu ya hii namna, kwa sababu nilivunja amri zako takatifu na niliishi kama mpumbafu; ndiyo maana nakuomba*:* Unitakase kwa maji ya toba takatifu, kwa kufunga na maombi, ee Mwokozi mwenye kujaa na wema, usinitupilie mbali, ee Mfazili wa ulimwengu.

Sauti ya mbili. Ton iper nun doreon.

Tuanzeni wakati wa hii Kwarezima ya nuru kwa kujitoa ku mashindano ya roho, tutakaseni roho yetu na tusafisheni mwili wetu tusifunge paka chakula tukatae pia tamaa yote tukistawisha fazila roho; kwa hii tukidumu na ibada, tutastahili kuona Mateso ya Kristu Mungu wetu na furaha ya Ufufuo wake takatifu.

Elezo*: Tunaimba kisha wimbo tatu ya Mineon na kisha Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Theotokion ya Mineon.*

Kisha padri atafanya Kuingia (Isodos) pamoja na chetezo. Vile atafanya kila mu Juma kwa Sala ya Mangaribi, kwani waimbaji inapaswa kuimba ma Prokimenon makubwa.

Mwangaza upole. . .
Prokimenon kubwa.
Sauti ya mnane.

Wala usifiche uso wako kwa mutumihsi wako kwa sababu mimi ni katika taabu; mbio inijibu ukaribie nafsi yangu na kuikomboa.

Shairi: Wokovu wako, ee Mungu, uninyanyue.

(mara ingine Prokimenon).
Shairi: Wapole waliona na wanafurahi. *(mara ingine).*

APOSTIKHA

Sauti ya ine. Idiomelon.

Ee Bwana, nuru ya neema yako iliangaa rohoni mwetu; tazama hii ni wakati wa kufaa, ile ya kubadilika; tuacheni matendo ya giza, tuvaeni silaha za nuru kusudi tukivuka bahari ya Kwarezima, tuifikie bandari ya Ufufuo siku ya tatu pamoja na Bwana wetu Yesu Kristu, Mwokozi wa roho zetu.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Ee Kristu Mungu wetu mwenye kutukuzwa katika makumbusho ya Watakatifu wako, kwa maombezi yao ututumie sisi neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Sauti umoja. Os geneon en martisin.

Ee Bikira Mtakatifu kamili, Malaika wanakutukuza kwa sababu ulizaa duniani Mungu wetu wa milele pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, huyu ambaye kwa kutaka kwake aliumba majeshi ya mbinguni; umuombe atume nuru ya wokovu rohoni mwa wale wenye kukiri imani ya kweli kwa kukuimbia kama Mzazi-Mungu.

Kisha Mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma:

Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

Msomaji*:* Trisagion*:* Mungu Mtakatifu. . Utatu Mtakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Elezo*: Kisha waimbaji wataimba Wimbo ya Mangaribi ya Kwarezima:*

Ewe Bikira Mzazi-Mungu, salamu, umejaliwa neema Maria, Bwana ni nawe, mbarikiwa wewe katika wanawake na mbarikiwa tunda la tumbo lako, kwani umemzaa Mwokozi wa roho zetu.

Ewe Mbatizaji wa Kristu, utukumbuke sisi wote juu ya kuokolewa ku makosa yetu; kwani Kwako kulipatikana neema ya kutuombea.

Utukufu kwa Baba. . .

Enyi Mitume Watakatifu na Watakatifu Wote, mutuombee juu ya kuokolewa ku hatari na sikitiko, kwani ninyi ni Walinzi wetu wa nguvu kwa Mwokozi.

Sasa na siku zote. .

Ewe Mzazi-Mungu, tunakimbilia ku wema wako, usizarau maombi yetu katika vishawishi, lakini utuokoe ku hatari, kwani peke yako ndiwe Safi na Mbarikiwa.

Bwana hurumia, *(mara makumi ine).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana bariki, ee Padri.

Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, daima sasa na siku zote, hata milele na milele.

Padri ao Mukubwa ya Kanisa:

Ewe Mfalme wa mbinguni, chunga waaminifu wafalme wetu; sabitisha imani; leta amani kwa inchi zote; ukimya duniani; linda vema Kanisa yetu Takatifu (*Monasteri, Parokia, ao Mission);* wale walioondoka toka hii dunia*:* Mapadri na ndugu zetu uwaweke pahali pa wenye haki; na sisi utupokee katika toba na ungamo kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Kisha tunafanya metania tatu makubwa (kupika magoti), kisha metania kidogo kumi na mbili na kisha ku mwisho moja metania kubwa. Ya kila metania tunasema kwa siri hii sala ya Mtakatifu Efremi:

Bwana na Rabi wa uzima wangu, usinipe nia ya uvivu, tamaa ya kujua mambo vya wengine, ya ukubwa, na ya kusema bure. *(Tunafanya sasa moja metania kubwa).*

Umupe mtumishi wako zawadi ya roho ya kadiri, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo. *(metania kubwa ya mbili).*

Ndiyo, ee Bwana, unipe nione makosa yangu na nisiamue ndugu yangu; kwani unabarikiwa milele na milele. Amina. *(metania kubwa ya tatu).*

Kisha tunafanya metania kidogo kumi na mbili na kisha tunasema hii sala ya yulu:

Ndivyo, ee Bwana, unipe nione makosa yangu na nisiamua ndugu yangu; kwani unabarikiwa milele na mielel. Amina.

Padri*:* Hekima.
Waimbaji*:* Himidi
Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Waimbaji*:* Amina. Bwana Mungu aimarishe imani takatifu, isiyo na lawama ya wakristu, watawa waorthodoksi katika mji na inchi hii, milele na milele. Amina.

Padri*:* Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Msomaji*:* Uliye wathamani kuwashinda wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli, tunakutukuza wewe.

Padri*:* Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Msomaji*:* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu),* Rabi mtakatifu barikia.

Padri*:* Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa Msalaba uheshimiwa na uhuitaji, kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili, kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtakatifu, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume Watakatifu wetu na waekumeniki Wakubwa, Walimu na Waaskofu, ya Washahidi, Watakatifu, Watukufu, Washindaji, wazuri ya Wapadri Wabebaji-Mungu, ya mpadri Mtakatifu Yoane Krisostomo, muarkiepiskopo wa Konstantinopoli, ya wa Babu Mungu wetu na nwenye haki Yoakimu na Anna, ya Mtakatifu *(ya hii siku),* makumbusho yake ni leo, hata ya Watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe yu Mungu mwema, murahimu na mpenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya Wapadri Watakatifu wetu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

Waimbaji*:* Amina.

Elezo*: Hii desturi ya mwisho ya sala ya mangaribi tunafanya kila Mangaribi ya kila mu Juma mpaka mu Juma wa tano ya hii wakati ya Kwarezima.*

MWANZO YA KWAREZIMA MKUBWA NA TAKATIFU

JUMA YA KWANZA

SIKU YA KWANZA ASUBUI KWA ORTHROS.

Elezo*: Kisha Eksapsalmos tunaimba Alliluia pamoja na ma shairi, sawa ni desturi ya Kwarezima. Nikusema hivi:*

1)Ee Bwana, tangu usiku roho yangu kwa sala inaongojea alfajiri yako, maana amri zako ni nuru duniani.

Waimbaji*:* Alliluia *(mara tatu).*
2) Jifunzezi haki, ninyi wote wakaaji wa dunia.
Waimbaji*:* Alliluia *(mara tatu).*
3)Wivu utangukia watu wapotevu, sasa moto itawateketesa maadui zako.

Waimbaji: Alliluia *(mara tatu).*

4)Mwaajibu, ee Bwana, uwazibu vikali kwa mateso Wenye sifa wote wa dunia.

Waimbaji: Alliluia (mara tatu).

Tunaimba mbele Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na kisha hii

KATHISMA YA MBILI

Sauti ya mbili. Efsplaknias iparkusa pigi.

Tushangilieni mwanzo wa Kwarezima kwa toba ya roho zetu tukimulalamikia Bwana*:* Pokea maombi yetu kama uvumba, utuopoe toka uharibifu wote na azabu ya ajabu. Wewe peke yako mwenye kuweza kutuhurumia.

Utukufu kwa Baba. . . *(Mara ingine hii ya yulu).*

Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**. *Umoja.*

Ee Mzazi-Mungu uliye chemchem ya rehema, utustahilishe rehema yako; tazama watu wako wakosefu, onyesha uwezo wako wa siku zote; tunakutumainia wewe na tunakupazia sauti*:* salamu! Kama alivyofanya zamani Malika Mkuu.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya mbili. Tin Akhranton Ikona su.

Tuanzezi hii Kwarezima na furaha, tuangae na mafundisho ya Kristu Mungu wetu katika nuru ya mapendo na ya sala katika usafi wa roho na nguvu ya wenye kuweza, ili tujiharikishe kwa Ufufuo Takatifu siku ya tatu, yenye kweneza duniani nuru yake ya milele.

Utukufu kwa Baba. . . *(Mara ingine hii ya yulu).*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Umoja.*

Umetukuzwa kuwapita wote, tunakuimbia, ee Mzazi-Mungu; mauti imeuawa, na Hadeze imevunjwa kwa Msalaba wa Mwana wako; ametufufua ku lufu, ametupatia uzima wa milele; paradizo imepewa mara iongine kwa sisi sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena kwa shukrani tunatukuza mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

Tunasoma Zaburi 50 (51).

KANUNI.

Sauti ya mbili. Defte lai.

Wimbo wa kwanza.

Namna gani nitalilia kufukuzwa kwangu? kwa tendo gani nitanzia wokovu wangu mimi niliyeishi kwa upumbafu? Ndiyo maana, uniokoe, ee Bwana, katika wema wako kwa haki unazojua.

Tazama, hii ni wakati wa wokovu, tazama hii ni siku ya wokovu, tazama hii ni mwanzo wa Kwarezima, uwe macho, ee roho yangu, funga mlango ya mateso, umuendee Bwana.

Ninapotikiswa kwa mawimbi ya zambi, nazama katika zimu ya sikitiko, ndiyo maana nakimbilia kwa mapendo yako kubwa*:* Uniokoe, ee Bwana.

Peke yangu nilikuwa mtumwa wa zambi, peke yangu nilifungua mlango ya mateso; ee Neno, kwa rehema yako, uniokoe mimi mwenye kukurudiria.

Ee Bikira uliyezaa umungu vumilivu, ponya roho yangu yenye kuumizwa kwa tamaa, uniondoe ku moto ya milele, wewe mjaliwa neema ya Mungu.

Kujeni, ninyi mataifa yote, tupokeeni neema ya Kwarezima hii inaanz, na kama zawadi ya Mungu hii wakati wa toba sababu ya kutupatanisha na Mwokozi.

Tazama, sasa imefika wakati wa mashindano*:* Kwa roho ya motomoto twanze wakati wa Kwarezima tukichukua fazila zetu kama zawadi kwa Bwana.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee nuru tatu ya ubwana mumoja, Baba Mwenyezi, Bwana na Mungu wa uzima, Mwana wa Baba na Roho Mtakatifu, okoa wale ambao unajua ibada yao.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Tuimbieni mulima takatifu wa umungu, Maria Mtakatifu kamili kwake alitoka kwa ajili ya wale waliokuwa katika giza, kristu aliye Jua la haki na Mungu wetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Gari ya moto ilichukua Nabii Elia kwa kufunga; kufunga ilimupa Musa maono; na sisi wenyewe, kwa kufunga, tutamuona Kristu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Adamu alipokula tunda iliyokataziwa, kwa ulafi wake, akafukuzwa Paradizoni; ee Bwana Mpenda-wanadamu, Kwarezima ituletee matunda mazuri ya toba.

IRMOS. Kujeni, enyi mataifa, tuimbie Kristu Mungu wetu aliyegawanya bahari kwa ajili ya taifa aliloopoa toka utumwa wa Wamisri, maana anavaa utukufu.

Elezo*: Kisha Maombi kidogo ya Shemasi ao Padri tunaimba Fotagogikon ya sauti ya hii Juma, mara tatu (Uitafute ku mukongo ya hii Kitabu).*

FOTAGOGIKON.

DOKSOLOGIA KIDOGO.

APOSTIKHA.

Sauti ya tano. Idiomelon.

Kwarezima imefika iliyo mchongezi wa uovu na mlinzi wa toba; inaleta kiasi, inaleta wokovu kwa watu na tunaishi kama malaika; enyi waaminifu, tupazeni sauti*:* Ee Bwana, utusamehe.

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu zote. Utufurahishe kadiri ya siku ulizotutesa, kadiri ya miaka tulipoona mabaya. Matendo yako yaonekana kwa watumishi wako, na utukufu wako kwa wana wao. (Zaburi 89(90), 14-16).

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya mikono yetu uistawishi, ndiyo kazi ya mikono yetu uiimarishe. (zaburi 89(90), 17.

Litukuzwe jeshi la Wafalme wa mbinguni! Kwani, walipozaliwa duniani, Mashahidi washindaji hawakutamainia cheo cha Malaika*:* Walipozarau mwili na kuteswa na mateso yao, walistahili utukufu wa malaika; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Tunakutukuza kwa nyimbo zetu kama Mzazi-Mungu na Bikira safi na Mtakatifu kamili kuwapita bila kiasi Waserafi; kwa kinywa na kwa roho yetu tunaungamama uzazi wako takatifu, kwani ulizaa kweli Mungu aliyejifanya mutu. Ee Bikira Mtakatifu kamili, ombea roho zetu.

Kisha mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma hii sala:

Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

Kisha Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Elezo*: Kisha Trisagion, hatuimbe Apolitikia, lakini padri ao Mukubwa padri ya Kanisa anasema hii sala:*

Ee Mzazi-Mungu, mlango wa mbingu, tunaposimama hekaluni kwa utukufu wako, tunazani ya kama tunasimama mbele ya mbingu, basi, utufungulie mlango ya huruma yako.

Msomaji*:* Bwana hurumia *(Mara makumi ine).* Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana bariki, ee Rabi.

Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Padri ao Mukubwa ya Kanisa anasoma hii sala:

Ewe Mfalme wa mbingu, chunga waaminifu, wafalme, wetu; sabitisha imani; leta amani kwa inchi zote; ukimya duniani; linda vema Kanisa yetu Takatifu (Mission ao Monasteri); wale walioondoka toka hii dunia*:* Mapadri na ndugu zetu uwaweke pahali pa wenye haki; na sisi utupokee katika toba na ungamo kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Elezo*: Kisha tunafata ma desturi ya kupika magoti pamoja na ma sala ya Mtakatifu Mutawa Efremi (ona yulu).*

Kisha tunasoma Saa wa Kwanza ya kusema: Njooni tumwanamie. . . .

Na padri anafanya Kuaga, katika desturi.

SIKU YA KWANZA YA KWAREZIMA KWA MANGARIBI.

Elezo*: Tunasoma Zaburi ya Proimiakos,* «Bwana nimekuita. . . » *na wimbo tatu ya Hii Kitabu na tatu ya Mineon.*

Sauti ya mbili. Pantas iperevin.

Nilitenda zambi za kila namna, kwa zote nilikosa; Wapi nitapata machozi kama ninataka kutubu? Nikiendelea na uzaifu nitastahili azabu; lakini kwa wema wako unisamehe, ee Bwana, unihurumie.

Ee Kristu, kwa hii Kwarezima inaanza unipe machozi ya toba sababu ya kuzima uchafu wa tamaa zangu kusudi nionekane mwenye kutakawa wakati utakapokuja toka mbinguni kuhukumu wanadamu kadiri ya hukumu zako za haki.

Sauti wa tano. *Osie pater.*

Kujeni, enyi waaminifu, tupokee kwa Kwarezima ngao sababu ya kuacha werevu ya Adui; tuacheni kupenda tamaa, tusiogope moto ya vishawishi, maana Kristu atatukuza uvumilivu wetu kwa kushindana. Ndiyo maana, tunapojua na matumaini, tumuombe, tusujudu mbele yake, tuombe amani ya dunia na neema ya wokovu kwa ajili ya roho zetu.

Elezo*: Tunaimba kisha wimbo tatu ya Mineon na kisha Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Theotokion ya Mineon.*

Mwangaza upole. . .

Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi wa tatu.

Wokovu ni wa Bwana; baraka yako iwe juu ya watu wako.

Shairi*:* Bwana, watesi wangu wamezidi kwangu?

Somo ya Mwanzo tutasoma. (1, 1-13)

Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia. Na dunia ilikuwa ukiwa na utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa kilindi; Roho ya Mungu akatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema*:* Nuru iwe*:* na nuru ilikuwa. Mungu akaona nuru ya kama ilikuwa vizuri; Mungu akatenga nuru na giza. Mungu akaita nuru Muchana na giza aliita Usiku. Na ilikuwa mangaribi na ilikuwa asubui, siku moja. Mungu akasema*:* Iwe nafasi katikati ya maji, itenge maji na maji. Mungu akafanya nafasi, akatenga maji yaliyo chini ya nafasi na maji yaliyo juu ya nafasi; na ilikuwa hivi. Mungu akaita nafasi Mbingu. Na ilikuwa mangaribi na ilikuwa asubui, siku ya pili. Mungu akasema*:* Maji chini ya mbingu yakusanyike kwa pahali pamoja, na inchi kavu ionekane; na ilikuwa hivi. Mungu akaita inchi kavu Inchi kusanyiko la maji akaita Bahari. Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Mungu akasema*:* Inchi itoe majani, mboga ikitoa mbegu, na muti wa matunda ukizaa matunda ya namna yake, mbegu yake iliyo ndani yake, juu ya inchi; na ilikuwa hivi. Inchi ikatoa majani, mboga ikitoa mbegu ya namna yake, na muti ukizaa matunda, mbegu yake iliyo ndani yake, ya namna yake. Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Na ilikuwa mangaribi, na ilikuwa asubui, siku ya tatu.

Prokimenon. *Sauti ya tano.* Zaburi ya ine.

Bwana atasikia wakati ninapomaita.

Shairi*:* Unijibu wakati ninapoita, ee Mungu wa haki yangu.

Somo ya Mezali za Solomono tutasoma. (1, 1-20).

Mezali za Solomono, mwana wa Daudi, mufalme wa Israeli*:* Kujua hekima na mafundisho; kutambua maneno ya ufahamu; kufundishwa matendo ya hekima, katika haki na hukumu na adili; kuwapa wajinga akili, kumupa kijana maarifa na akili*:* Ili mutu mwenye hekima asikie, na kuongezewa elimu; na mutu wa ufahamu afikiie mashauri ya akili njema. Kufahamu mezali na maana yake; Maneno ya wenye hekima na mafumbo yao. Kuogopa Bwana ni mwanzo wa maarifa*:* Lakini wapumbafu wanazarau hekima na mafundisho. Mwana wangu, sikia mafundisho ya baba yako, na usiache sheria ya mama yako*:* Kwa maana yatakuwa kilemba cha neema kwa kichwa chako, na mikufu shingoni mwako. Mwana wangu, kama wenye zambi wakikushawishi, usikubali. Kama wakisema*:* Kuja pamoja nasi, tuvizie ili kumwanga damu, tujifiche kwa siri kwa yeye asiye na kosa, pasipo sababu; tuwameze hai kama Hadeze, na wazima, kama wale wanaoshuka shimoni; Tutapata mali yote ya damani, tutajaza nyumba zetu nyara; Wewe utashirikiana nasi; sisi sote tutakuwa na vitu vyote shirika.

Mwana wangu, usitembee njiani pamoja nao. Zuiza muguu wako usiende katika mapito yao*:* Maana miguu yao inakwenda mbio kwa uovu, na wanafanya haraka ili kumwanga damu. Lakini wavu unatandikwa bule, mbele ya macho ya ndege ya yote. Na hawa wanavizia damu yao wenyewe, wanajidicha kwa siri kwa uzima wao wenyewe. Ndivyo zilivyo njia za kila mutu anayetamani mali; Inaondosha uzima wao walio nayo. Hekima inapaza sauti katika njia kubwa; Inatoa sauti yake katika viwanja.

Kisha tunasoma: Ee Bwana utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi. . .

APOSTIKHA

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Tumutoleeni Bwana Kwarezima yenyi kumpendeza, kwa sababu kufunga kwa kweli kunatenga zambi mbali; hakuna kusemasema na kupumzika kwa ukali, hakuna tamaa, matusi, uwongo, kiapo ya bure; tukikataa hii yote, tutafanya kwarezima yenyi kumupendeza Bwana.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Nguvu ta Mashahidi ni kubwa*:* Wanapolala kaburini wanafukuza pepo muchafu; waliharibu nguvu ya adui wakati walishindana juu ya imani katika Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, mlinzi wa wote wale wenye kukuomba, unatupa sisi nguvu na usabti, tunakutumainia wewe*:* Umuombe Mwana wako kwa ajili ya Watumishi wako wasiostahili.

Kisha Mukubwa ya Kanisa ao padri atasoma:

Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

Msomaji*:* Trisagion*:* Mungu Mtakatifu. . Utatu Mtakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

Elezo*: Kisha waimbaji wataimba Wimbo ya Mangaribi ya Kwarezima:*

Ewe Bikira Mzazi-Mungu. . .
Ewe Mbatizaji wa Kristu. . .
Utukufu. . . Enyi Mitume Watakatifu. . .
Sasa. . . Ewe Mzazi-Mungu, tunakimbilia. . .

Bwana hurumia, *(mara makumi ine).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee Padri.

Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, daima sasa na siku zote, hata milele na milele.

Padri ao Mukubwa ya Kanisa:

Ewe Mfalme wa mbinguni, chunga waaminifu wafalme wetu; sabitisha imani; leta amani kwa inchi zote; ukimya duniani; linda vema Kanisa yetu Takatifu (*Monasteri, Parokia, ao Mission);* wale walioondoka toka hii dunia*:* Mapadri na ndugu zetu uwaweke pahali pa wenye haki; na sisi utupokee katika toba na ungamo kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Kisha tunafanya metania tatu makubwa (kupika magoti), kisha metania kidogo kumi na mbili na kisha ku mwisho moja metania kubwa. Ku kila metania tunasema kwa siri hii sala ya Mtakatifu Efremi:

Bwana na Rabi ...*(Tunafanya sasa moja metania kubwa).*

Umupe mtumishi wako ...*(metania kubwa ya mbili).*

Ndiyo, ee Bwana, unipe...*(metania kubwa ya tatu).*

Elezo*: Kisha tunafanya metania kidogo kumi na mbili na kisha tunasema hii sala ya yulu:*

Ndivyo, ee Bwana, unipe...

Kisha Trisagion*:* Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mtakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia mara kumi na mbili na padri atasoma hii sala*:*

Padri*:* Utatu Mtakatifu kamili, ...

Msomaji*:* Jina la Bwana hilidiwe tangu sasa, na mpaka milele *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Kisha tunasoma ma zaburi 33(34) na 144(145).

SIKU YA MBILI KWA ASUBUI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA

Elezo*: Kisha Eksapsalmos, Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu (Triadika) na sauti ya hii juma tunaimba Kathisma ya kwanza ya Paraklitiki na ingine ya hii Kitabu Triodion.*

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya mbili.

Kwarezima inaleta neema tukufu, katika hii Musa alitukuzwa na akapokaa mbao ya Amri; kwa ajili yake Vijana walikuwa na nguvu kupita moto, katika yeye tutazima kivukutu ya tamaa zetu za mwili tukimwambia Kristu Mwokozi wetu*:* Utupe sisi toba na utuokoe toka Hadeze.

Utukufu kwa Baba. . . Sauti umoja.

Wakati wa toba imefika, ee roho yangu, onyesha matunda ya kufunga; tazama wale waliyotubu zamani, umwambie Kristu*:* Ee Bwana, nimekosa, uniokoe kama ulivyomuokoa Mtoza-Kodi, ee Mungu wa mapendo, peke yako mwenye rehema.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, wewe uliye mlinzi wa wakristu, umuombe Mwana wako atuokoe toka werevu wa adui na atuondolee maovu yetu, kwa rehema yake na kwa maombezi yako kama mama.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya tano.

Ee Bwana, kwa hii siku ya mbili ya Kwarezima, tunakulalamikia*:* Weka toba rohoni mwetu na pokea maombi tunakutolea na woga; utupe tufike vizuri mpaka mwisho wa kufunga, utupe rehema yako na neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . *(mara ingine hii wimbo).*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Sauti umoja. Ton Sinanarkhon Logon.

Ee Bikira uliyestawisha ua takatifu, safina ya agano, kinara na makao yenye kupambwa na zahabu, meza takatifu ambako kunakaa mkate wa uzima, umuombe Mwana wako aliye Mungu wetu, pamoja na Mtakatifu Mtangulizi, awape neema ya wokovu wale wenye kukutambia wewe kama Mzazi-Mungu.

Fotagogikon ya sauti ya hii juma na kisha tunaimba:

APOSTIKHA

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Enyi mataifa, twanzezi Kwarezima takatifu yenyi kuleta wokovu kwa roho zetu; tumutumikie Bwana kwa woga, tupakaeni kichwa mafuta ya fazila; tunaweni uso na maji ya utakaso, tusiseme maneno mengi wakati tunapoomba, lakini kama tulivyofundishwa na Bwana, tuseme*:* «Baba yetu uliye mbinguni, utusamehe makosa yetu, kwa mapendo yako kwa wanadamu».

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Maaskari wa Kristu walifukuza woga wote mbele ya Wafalme na ya wazulumu; kwa usabiti kubwa walimukiri Bwana wa ulimwengu, Mungu na Mfalme wetu, na sasa wanaomba roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, mlinzi wa wote wenye kukuomba, unatupa sisi nguvu na usabiti; tunakutumainia wewe*:* Umuombe Mwana wako kwa ajili ya Watumishi wako.

SIKU YA MBILI KWA MANGARIBI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Elezo*: Kisha Zaburi ya Proimiakos, tunaimba «Bwana nimekuita. . . » na kisha wimbo 3 ya hii Kitabu na tatu ya Mineon.*

Sauti ya mbili. Os orathis Kriste.

Zamani tulipofukuzwa Paradizoni sababu ya kuonja uchungu wa tunda, tujikaze kurudiamo kwa kuacha tamaa tukimulalamikia Mungu wetu*:* Wewe uliyepanua mikono msalabani, ukanywa divai na kuonja siki, ulipovumilia mateso ya misumari sababu ya kuondoa misumari ya tamaa rohoni mwetu, okoa watumishi wako kwa wema wako kubwa.

Zamani tulipofukuzwa Paradizoni kwa kula tunda lililokatazwa, turudiemo kwa muti wa Msalaba; ni hii muti tunakutolea kuwa mwombezi; na sisi waaminifu wako tunakuomba*:* Kwa hii wakati wa kufunga, ee Mungu wa wema, fungua chemchem ya machozi yetu sababu ya kutakasa haya yote ya tamaa zote na kuzima maovu yetu ili tuweze kukuimbia*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Kwa kujikatalia unipe furaha, ee Neno, kama zamani ulipowapa wazazi wetu wa kwanza Paradizo; uniache nionje matunda ya Amri yako kwa kukataa daima ile ya zambi kusudi niifikie kwa furaha Mateso ya Msalaba wako wenyi kuleta uzima.

Wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Mangaribi Prokimenon. *Sauti ya tano.* Zaburi ya saba.
Ee Bwana Mungu wangu, ninakukimbilia wewe.
Uniponyeshe na wote wanaonifuata, uniokoe.

Somo ya Mwanzo tutasoma (Sehemu 1, mustari 14-23).

Mungu akasema*:* Iwe miangaza kwa nafasi ya mbingu ipate kutenga kati ya muchana na usiku; nayo iwe kwa alama na kwa nyakati na kwa siku na kwa miaka. Nayo iwe kwa nuru kwa nafasi ya mbingu, iangaze juu ya dunia; na ilikuwa hivi. Mungu akafanya miangaza miwili mikubwa; mwangaza mukubwa kutawala muchana na mwangaza mudogo kutawala usiku; na nyota vilevile. Mungu akaiweka kwa nafasi ya mbingu kuangaza juu ya dunia, na kutawala juu ya muchana ya juu ya usiku, na kutenga nuru na giza; na Mungu aliona ya kama ilikuwa vema. Na ilikuwa mangaribi na ilikuwa asubui, siku ya ine. Mungu akasema*:* Maji yajae kwa wingi na viumbe vilivyo hai, na ndege waruke juu ya inchi kwa nafasi ya mbingu. Mungu akaumba nyama wakubwa za bahari, na kila kiumbe kilicho hai na kinachotembea, maji yaliyotoa wingi kwa namna zao, na kila ndege kwa namna yake. Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Mungu akawabariki, akisema*:* Muzidi na kuongezeka, mujaze maji baharini, na ndege wazidi inchini. Na ilikuwa mangaribi, na ilikuwa asubui, siku ya tano.

Prokimenon. *Sauti ya tano.* Zaburi wa mnane.
Ee Bwana, Bwana wetu, jina lako ni lenye utukufu duniani mwote!
Shairi*:* Wewe uliyeweka utukufu wako juu ya mbingu.

Somo ya Mezali tutasoma (Sehemu 1, mstari 20-33).

Hekima inapaza sauti katika njia kubwa; Inatoa sauti yake katika viwanja; Inalia katika pahali pakubwa pa makutano; kwa kungia malangoni, katika muji, inatoa maneno yake*:* Hata wakati gani, ninyi wajinga, mutapenda ujinga? Na mwenye kuzarau kupenda kuzarau, na wapumbafu kuchukia maarifa? Geukeni kwa ajili ya maonyo yangu. Kwa kuwa nimeita, nanyi mukakataa; Nimenyosha mukono wangu, wala hakuna mutu aliyeangalia, lakini mukaona bule shauri langu lote, wala hamukutaka maonyo yangu. Mimi vilevile nitacheka kwa siku ya taabu yenu; Nitazihaki wakati woga wenu unapowafikia ninyi; wakati woga wenu unapofika kama zoruba, na hasara yenu inapofika kama upepo wa kuzunguka; wakati taabu na uchungu zinapowafikia ninyi. Halafu wataniita, lakini sitajibu; watanitafuta kwa bidii, lakini hawatanipata*:* Kwa kuwa walichukia maarifa, wala hawakuchagua woga wa Bwana*:* hawakutaka shauri langu; wakazarau maonyo yangu yote*:* Kwa hivi watakula ya matunda ya njia yao wenyewe, na watashibishwa kwa mashauri yao wenyewe. Maana kurudi nyuma kwa wajinga kutawaua, na usitawi wa wapumbafu utawaharibu. Lakini mutu ye yote anayenisikiliza mimi atakaa salama, naye atatulia pasipo kuogopa mabaya.

APOSTIKHA.

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Kufunga kwetu kusiwe paka kwa chakula, lakini kuondoa tamaa yote ya mwili kusudi tukishinda mwili kututawala, tustahili kuungama na Mwana-Kondoo, ndiye Mwana wa Mungu, aliyejitoa kwa kutaka kwake kwa ajili ya ulimwengu, na tushangilie katika roho Ufufuo wake katika wafu, tukielekea juu mbinguni kwa nuru ya fazila na tukifurahia Mwokozi mpenda-wanadamu kwa ukuu wa matendo yetu.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Ee Bwana, waliposahau hii uzima na kuzarau pia mateso kwa ajili ya uzima wa milele, Mashahidi wako wakapokea uriti wa mbinguni na wanafurahi pamoja na malaika*:* Kwa maombezi yao uwape watu wako neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Kweli ni ajabu! Ni fumbo ya ajabu na mpya, ndivyo alivyosema Bikira alipomuona Msalabani ametundikwa katikati ya wanyanganyi huyu alizaa bila uchungu; na akiomboleza, akalia akisema*:* Ole wangu, ee Mwanangu mpendwa, namna gani hawa watu wabaya, kwa kukosa kwao shukrani wamekusulubisha msalabani?

Kisha tunaendelea Ibada katika desturi ya ma siku ya mukongo.

SIKU YA TATU KWA ASUBUI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Elezo*: Ku mwanzo tunaimba Kathisma ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma na kisha hii:*

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya mbili. O Efskhimon Iosif.

Ee Bwana Mpenda-wanadamu, wewe ambaye kwa mateso yako unawapa wote uzima wa milele, msalabani uliharibu tamaa za mwili wangu; unipe nione Mateso yako kisha kupendeza utukufu wako kwa kufunga sababu ya kupokea neema nyingi za wokovu.

Utukufu kwa Baba. . *(mara ingine wimbo ya yulu).*

Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, alipoona lufu yako msalabani, Bikira Mama yako akalia kwa uchunga akasema*:* Ee Mwanagu, hii ni fumbo gani? Wewe mwenye kuwapa wote uzima wa milele namna gani unazaraulizwa na kuuawa kwa kutaka kwako msalabani?

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya mbili. Ton zoopion Stavron.

Wakati wa hii Kwarezima ya nuru uliyotakasa sababu ya kutupayo sisi zawadi, utustahilishe tuipitishe kwa usafi, wenye kujaa na toba na amani kwa uwezo wa Msalaba wako, wewe peke yako Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . *(mara ingine hii wimbo ya yulu).*

Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Malkia Mzazi-Mungu, tukilindwa kwa Msalaba heshimiwe wa Mwana wako, tunaweza wepesi kutenga mishale ya adui; ndiyo maana tunakutaja Mwenye heri, ee Mama wa Nuru, tena peke yako matumaini ya roho zetu.

Tunasoma Zaburi 50 (51).

KANUNI

Sauti ya mbili Eksinthisen i erimos.

Wimbo wa tatu.

Kwa kufunga tunasulubisha viungo vyetu na mwili wetu, tusiseme maneno mengi katika maombi, kama inavyoandikwa, tufwateni alama ya Msalaba takatifu tukiua tamaa zetu.

Tunapokataa uchungu wa zambi, tujikaze kumupendeza Mungu wetu aliyetaka kuonja siki wakati aliharibu adui msalabani.

Nilipozoea kukosa, nasukumwa kwa upotevu wangu, lakini wewe, Bwana, uniokoe kwa Msalaba, ee Mungu Mwema.

Ee Malkia wa Viumbe vyote, wewe uliyezaa Bwana wa ulimwengu uniokoe toka utumwa huko inanifunga werevu wa adui yetu moja.

Irmos ingine*: Stereoson imas en si Kirie.*

Kufunga ilichanuka juu ya muti wa Msalaba, ulimwengu ikiikumbatia itapata mauua mengi ile mafundisho ya Kristu inachamusha.

Tunapovumilia sasa kujikatalia tamaa, tusulubishe mwili wetu na roho yetu kwa ajili ya Kristu, tukiregeza tamaa zetu na mawazo yetu sababu ya kuishi katika akili ya Mungu.

Utukufu kwa Baba. . .

natukuza watu tatu wa Mungu mumoja, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, uwezo moja wa umungu, na ufalme wake tukufu.

Sasa na siku zote. . .

Ya kushangaa ni namna ya kuzaa kwako, ee Bikira Mtakatifu, kwani ni Mungu aliyejifanya, akazaliwa kwa Baba bila mwanzo, na ulimuzaa bila mbegu wakati wa mwisho.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Naimbia kusulubiwa kwako na ubavu wako uliyochomwa mkuki*:* katika hii nachota uzima wa milele, na kila siku natakaswa, ee Kristu.

IRMOS. Ee Bwana, sabitisha roho zetu kwa mapendo yako, wewe uliyeondoa zambi msalabani, panda woga ya jina lako katika roho za wale wenyi kukutukuza.

Tunaimba wimbo ya Fotagogika na kisha:

APOSTIKHA.

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Kwa kufunga tutiishe tamaa za mahasa yetu, tujizungushe mabawa ya roho kusudi tukishinda tufani yaadui tustahili kuabudu Msalaba wa Mwana wa Mungu aliyejitoa kwa ajili ya ulimwengu na tushangilie rohoni Ufufuo wake katika wafu; na tutapanda mlima pamoja na Mitume sababu ya kutukuza Mwana wa Baba na Mpenda-wanadamu huyu alipewa mamlaka yote.

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Enyi Mashahidi wa Kristu muliyoshinda udanganyifu kwa uwezo wa Msalaba, mulipokea neema ya uzima wa milele; muliteswa bila woga mbele ya vitisho vya wazulumu; sasa munafurahi, roho zetu zimeponyeshwa kwa damu yenu*:* Ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Bwana, ni maono gani naona machoni mwangu? Wewe mwenye kushika mikononi viumbe vyote, umesulubiwa na kuuawa msalabani, wewe Muumba wa uzima wote! Ni hivi

alisema Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili wakati aliona msalabani Mungu-Mtu aliyezaa kwa namna ya ajabu.

MU KAZI TATU KWA MANGARIBI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Elezo*: Kisha Zaburi ya Proimiakos, tunaimba «Bwana nimekuita. . . » na kisha wimbo 3 ya hii Kitabu na tatu ya Mineon.*

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Ee wa Ndugu, tufungeni mwilini, tufungeni pia katika roho, tufungueni kifungo chote cha uovu, tuvunjeni vifungo vya tamaa zetu, tupasueni mapatano yote ya uzulumu, tuwape maskini chakula na tupokeeni wasio na makao kusudi tupokee kwa Kristu Mungu wetu neema ya wokovu. *(mara mbili).*

Utukufu wote na sifa yote ni kwa Mashahidi*:* Waliinamisha shingo kwa upanga kwa ajili yako wewe uliyeshuka kwa kuinamisha mbingu; walimwanga damu yao juu yako wewe uliyejishusha kwa kuchukua hali ya mtumishi; na walijinyenyekeza mpaka kufa, walifwata umaskini wako*:* Ee Bwana, kwa maombezi yao na kwa rehema yako, utuhurumie.

Sauti ya mbili. Os orathis Kriste.

Mulipoangaa kama umeme, Bwana Yesu, yeye kweli Jua la roho, akawatuma duniani kote kuondoa giza ya udanganyifu kwa nuru ya mafundisho yenu; Enyi Mitume Watakatifu muliyeona Kristu, muombeni atutumie sisi nuru yake na neema ya wokovu.

Alipoaangazwa kwa kufunga, Elia akachukuliwa juu ya gari ya fazila mbinguni. Tufanane naye, ee roho yangu maskini, tukifunga juu ya uovu wote, kasirani, wivu na furaha isiyodumu sababu ya kuepuka mateso ya milele ya Hadeze, na umwambie Kristu*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Sauti ya tano. Osie Pater.

Enyi Mitume wa Mungu, waombezi waheshimiwa wa ulimwengu tena wasimamizi wa kwanza wa wakristu, ninyi mulio na uwezo wa kusema na Kristu Mungu wetu, tunawaomba ninyi mutuombee utimizo nzuri wa hii Kwarezima tukufu na neema ya Utatu wa asili moja; Enyi Watangazaji wa Neno, ombeni kwa ajili ya roho zetu.

Wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Mangaribi Prokimenon. *Sauti ya tano.* Zaburi 11.
Wewe, ee Bwana, utawalinda, utawaponyesha na kizazi hiki milele.
Shairi*:* Saidia, ee Bwana, kwa sababu mutu mutawa anakoma.

Somo ya Mwanzo tutasoma. (Sehemu 1, 24 mpaka 2, 3).

Mungu akasema*:* Inchi itoe kila kiumbe kilicho hai kwa namna yake, ngombe na mutambazi, na nyama ya inchi kwa namna yake; na ilikuwa hivi. Mungu akafanya nyama ya inchi kwa namna yake, na ngombe kwa namna yake na kila mutambazi juu ya udongo kwa namna yake; Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Mungu akasema*:* Tufanye mutu kwa mufano wetu, mwenye sura yetu, na watawale juu ya samaki za bahari na juu ya ndege za hewa na juu ya ngombe, na juu ya inchi nzima, na juu ya kila mutambazi anayetambaa juu ya inchi. Mungu akaumba mutu kwa mfano wake mwenyewe, kwa mufano wa Mungu akamwumba; mume na muke akawaumba. Mungu akawabariki, Mungu akawaambia*:* Muzidi na kuongezeka, na mujaze tena inchi na kuitiisha; na mutawale juu ya samaki za bahari, na

ndege za anga na kila kiumbe kinachotambaa inchini. Mungu akasema*:* Tazameni, nimewapa ninyi kila mboga ikizaa mbegu iliyo juu ya uso wa inchi, na kila muti ndani yake ni tunda la muti likizaa mbegu; kwenu utakuwa kwa chakula, na kwa kila nyama ya dunia, na kwa kila ndege ya anga na kwa kila mutambazi juu ya inchi, uliyo hai; nimewapa majani yote ya mboga kwa chakula; na ilikuwa hivi. Na Mungu aliona kila kitu alichofanya, na tazama, kilikuwa kizuri sana. Na ilikuwa mangaribi, na ilikuwa asubui, siku ya sita. Mbingu na dunia zikamalizwa, na jeshi lao lote. Siku ya saba Mungu akamaliza kazi yake aliyofanya, akastarehe siku ya saba katika kazi yake yote aliyofanya. Mungu akabariki siku ya saba, akaitakasa; kwa sababu ndani yake alistarehe katika kazi yake yote Mungu aliyoumba na kuifanya.

Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 12.

Ee Bwana Mungu wangu, uangalie na kunijibu.

Shairi*:* Hata wakati gani, ee Bwana, utanisahau hata milele?

Somo ya Mezali tutasoma. (Sehemu 2, mstari 1-22).

Mwana wangu, kama ukikubali maneno yangu, na kuweka akiba maagizo yangu ndani yako. Halafu utategа sikio lako kusikia hekima, na kuta moyo wako kwa ufahamu; Ndiyo, kama ukiita akili, na kupaza sauti yako kwa ufahamu; kama ukiutafuta kama feza, na kuutafutafuta kama hazina zilizofichwa; halafu utafahamu woga wa Bwana, na kupata maarifa kwa Mungu. Maana Bwana anawapa watu hekima; Kinywani mwake zinatoka maarifa na ufahamu*:* Anawekea wenye haki akiba ya hekima njema, yeye ni ngabo kwao wanaotembea kwa ukamilifu; ili apate kulinda njia za hukumu na kulinda njia ya watakatifu wake. Halefu utafahamu haki na hukumu na adili na kila njia njema. Maana hekima itaingia moyoni mwako, na maarifa yatapendeza nafsi yako; akili njema itakulinda, ufahamu utakuchunga*:* Ili kukuponyesha kwa njia ya uovu, na watu wanaosema maneno ya kuasi; Wanaoacha niia za haki, ili kutembea katika njia za giza; wanaofurahi kutenda mabaya, na kupendezwa na ubaya wa uovu; wasio haki katika njia zao, na wakaidi katika mapito yao*:* Ili kukuponyesha na mwanamuke mugeni hata na mugeni anayebembeleza kwa maneno yake, anayeacha rafiki ya ujana wake na kusahau agano la Mungu wake*:* Maana nyumba yake inaelekea mauti, na mapito yake yanakwenda wafu*:* Kati yao wanaokwenda kwake hakuna anayerudi tena, wala hawafikili mapito ya uzima*:* Ili upate kwenda kwa njia ya watu wema na kushika mapito ya wenye haki. Maana wenye haki watakaa katika inchi, na wakamilifu watabaki ndani yake. Lakini waovu watakatiliwa mbali na inchi nao, wanaotenda kwa hila watangolewa.

Kisha tunaanza kuimba: « Maombi yangu ya elekezwe. . . ».

MU KAZI INE KWA ASUBUI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Elezo*: Tunaimba Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na kisha ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya mbili. O sofisas iper ritoras.

Ee Neno la Mungu, wewe uliyeangaza kwa mahubiri yao Wafwasi wako mpaka ku mwisho wa ulimwengu, angaza roho zetu na nuru ya fazila; Kwa hii Kwarezima uwape watumishi wako wakurudirie na watubu kusudi waimbie utukufu wako na neema yako.

Utukufu kwa Baba. . *(mara ingine wimbo ya yulu).*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, usizararu mtumishi wako mwenye kuhitaji msaada wako, kwani roho yangu inakutumainia wewe*:* Unihurumie.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya tano. Agiotera ton Kheruvim.

Enyi Mitume Watakatifu, ombeni ili tutimize kwa amani kwarezima ya nuru, kuliko fazila, kwa sababu inatufanya sisi kuishi kama mbinguni, inatupatia matunda ya wokovu; ninyi kweli ni nguvu ya wanadamu tena kimbilio la roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . *(mara ingine wimbo ya yulu).*

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira mwenye kustahili nyimbo zetu, wewe uliye Mtakatifu kupita Wakheruvi, uliye juu kabisa mbingu, wakati tunakutambua kweli kama Mzazi-Mungu, japo makosa yetu, tunapata wokovu, na katika majaribu unatulinda; ndiyo maana usichoke kutuombea, wewe nguvu ya wanadamu tena kimbilio la roho zetu.

Elezo*: Tunaimba wimbo ya Fotagogika na kisha:*

APOSTIKHA

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Ee Bwana, unipe toba mimi muovu, kwani unataka kuokoa mtumishi wako muovu; najusudu mbele yako nikiomba wema wako kubwa*:* katika Kwarezima inamisha roho yangu, maana kwako peke yako napata kimbilio na rehema.

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Enyi Mashahidi Watakatifu, munangaza ulimwengu kama nyota; muliposhindana mashindano nzuri, muna uwezo wakumuomba Kristu alete neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, mlinzi wa wote wale wenye kukuomba, unatupa sisi nguvu na usabiti; tunakutumainia wewe*:* Umuombe Mwana wako kwa ajili ya Watumishi wako wasiostahili.

MU KAZI INE KWA MANGARIBI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Kisha Zaburi ya Proimiakos, tunaimba «Bwana nimekuita. . . » na kisha wimbo 3 ya hii Kitabu na tatu ya Mineon.

Sauti ya mbili. Ton fotismon imon.

Ee Kristu, angaza roho yangu yenye kuwa katika giza kwa uwezo wa adui, wewe ambaye zamani Msalabani uligeuza Jua kuwa giza; angaza waaminifu wako kwa nuru ya kweli ya rehema kusudi nikitembea katika nuru ya Amri yako, niifikie kwa usafi wote nuru ya wokovu siku ya Ufufuo wako takatifu.

Ee Kristu, kama mzabibu wenye kutundikwa juu ya mtii, ulitirikiza vinyo ya milele mpaka mwisho wa ulimwengu; ndiyo maana, ee Bwana, nakulalamikia*:* mwangia roho yangu yenye

kuchafuka na ulevi wa zambi kinywaji tamu cha toba ya kweli; na kwa nini kuweza kufunga juu ya tamaa zangu, unipe nguvu yako, ee Bwana, kwa wema na mapendo yako kwa wanadamu.

Nguvu ya Msalaba kwa Eklezya ilichanua kukataa yenyi kuondoa maneno ya Adamu mu Paradizo iliyoingiza mauti duniani, kwa wanadamu inatirikiza uzima wa milele kama chemchem ingine ya Edeni, ikionyesha maji ya uzima na damu yako ambayo unalisha nayo ulimwengu; utupe sisi kuonja kwa hii Kwarezima furaha na huruma, ee Mungu wa Israeli, chemchem ya neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Mangaribi Prokimenon. *Sauti ya ine.* Zaburi 15(16).
Nitabariki Bwana, aliyenipa shauri.
Shairi*:* Unichunge, ee Mungu, kwa maana nilikuwekea wewe tumaini langu.

Somo ya Mwanzo tutasoma (2, 4-19)

Hivi ni vizazi vya mbingu na vya dunia wakati zilipoumbwa, kwa siku Bwana Mungu alipofanya dunia na inchi. Wala haijakuwa bado mbegu ya shamba duniani, wala mboga ya shamba haijaota bado; kwani Bwana Mungu hajanyesha bado mvua duniani wala mutu wa kulima udongo hakuwa; lakini umande ukapanda toka inchi, ukanyesha maji juu ya uso wote wa inchi. Bwana Mungu akafanya mutu wa mavumbi ya inchi, akapuliza pumuzi ya uzima ndani ya pua yake; na mutu alikuwa nafsi ya uhai. Bwana Mungu akapanda shamba kwa upande wa mashariki kwa Edeni, akatia pale mutu aliyemufanya. Toka udongo Bwana akaotesha kila muti wa kupendeza macho, na muzuri kwa chakula; muti wa uzima vile vile ulikuwa katikati ya shamba, na muti kujua uzuri na ubaya. Muto ukatoka katika Edeni kunyesha maji shambani; na toka kule ukatengwa na ulikuwa vichwa vine. Jina lake la kwanza ni Pisoni; ndio unaozunguka inchi nzima ya Havila, pale zahabu ilipokuwa. Na zahabu ya inchi ile ni nzuri, kule kuna bedola na kitchafrangi. Jina la muto wa pili ni Gihoni; ndio unaozunguka inchi nzima ya Etiopia. Jina la muto wa tatu ni Hidekeli, ndio unaotembea mbele ya Asuria. Muto wa ine ni Furati. Bwana Mungu akatwaa mutu, akamutia shambani mwa Edeni kulilima na kulichunga. Bwana Mungu akaagiza mutu akisema*:* Wa kila muti wa shamba unaweza kula; lakini wa muti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula, hakika utakufa. Bwana Mungu akasema*:* Si vema mutu awe peke yake; nitamufanyia musaidia anayefaa kwake. Na kwa udongo Bwana Mungu akafanya kila nyama ya mwitu na kila ndege ya hewa, akawaleta karibu na mutu kuona atakavyowaita; na sawasawa mutu alivyoita kila kiumbe cha uzima, hili jina lake.

Prokimenon Mangaribi. *Sauti ya ine.* Zaburi 16(17).
Unilinde kama mboni ya jicho.
Shairi*:* Usikie haki usikilize kilio changu.

Somo ya Mezali tutasoma. (3, 1-19)

Mwana wangu, usisahau sheria yangu; lakini moyo wako ushike amri zangu*:* Maana zitakuongezea wingi wa siku, na miaka ya uzima na salama. Rehema na kweli zisikuache*:* Uzifunge shingoni mwako; usiandike juu ya ubao wa moyo wako*:* Hivi utapata ukubali na ufahamu muzuri kwa macho ya Mungu na ya mutu. Tumainia Bwana kwa moyo wako wote wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe*:* Katika njia zako zote umukiri yeye naye ataongoza mapito yako. Usiwe mwenywe hekima kwa macho yako mwenyewe; Ogopa Bwana na kuacha uovu; itakuwa afya kwa mwili wako, na mafuta kwa mifupa yako. Heshimu Bwana kwa mali yako na kwa malimbuko ya mazidio yako yote*:* Hivi gala zako zitajazwa kwa wingi na mashinikizo yako yatafurika mvinyo mpya. Mwana wangu, usizarau kuazibiwa na Bwana; wala usichoke na maonyo yake, maana mutu Bwana anayemupenda anamwonya; hata kama baba mwana anayependezwa naye. Heri mutu anayepata ufahamu. Maana biashara yake ni njema kuliko biashara ya feza na faida yake ni nyingi kuliko zahabu safi. Ana damani kuliko

marijani*:* Wala vyote unavyotamani haviwezi kusawanishwa naye. Siku nyingi ni katika mukono wake wa kuume; Katika mukono wake wa kushoto ni mali na heshima. Njia zake ni njia za kupendeza. Na mapito yake yote ni salama. Yeye ni muti wa uzima kwao wanaomushika sana*:* Na heri ni kila mutu anayeshikamana naye. Kwa hekima Bwana aliweka misingi ya inchi; kwa ufahamu alisimamisha mbingu.

APOSTIKHA

Sauti ya ine. Idiomelon.

Tunapotamainia kusharikia Paska ya Mungu, apana ile ya Msiri, lakini ya Sayuni, tupunguze kwa toba chachu ya zambi tujifungeni kiuno tukiregeza tamaa zetu, tuvaeni viatu sababu ya kuepuka njia yote ya uovu, tuegemee juu ya baokra ya imani, tusifanane na maadui wa msalaba, wao amabo wanafanya tumbo lao kuwa Mungu, tufwate mfano wa huyu aliyeshinda shetani, Mwokozi wa roho zetu.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Ee Kristu Mungu wetu, unapotukuza katika makumbusho ya Watakatifu wako, kwa maombezi yao ututumie sisi neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Sauti umoja. *Os geneon en Martisin.*

Ee Bwana, alipokuona umesulubiwa msalabani, Bikira Mama yako akashangaa na kusema*:* Hii ni ndoto gani, ee Mwanangu mpendwa! Hii ndiyo wanakutolea hawa watu wasio na shukrani ambao ulijaza na mema mengi na wanavunja Amri yako pahali pa kukuimba*:* Ee Rabi, utukufu kwa mapendo yako.

MU KAZI TANO KWA ASUBUI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Elezo*: Kisha Kathisma ya Paraklitiki tunaimba Hii Kathisma:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya mbili. O Efskhimon Iosif.

Ee Bwana mpenda- wanadamu, wewe ambaye kwa mateso yako unawapa wote uzima wa milele, msalabani uliharibu tamaa za mwili wangu; utupe sisi tuone Mateso yako kisha kupendeza utukufu wako kwa kufunga sababu ya kupokea neema nyingi za wokovu.

Utukufu kwa Baba. . *(mara ingine hii wimbo ya yulu).*

Sasa na siku zote. . **STAYROTHEOTOKION**.

Sauti umoja.

Ee Malkia Mzazi-Mungu, tukilindwa kwa Msalaba heshimiwa wa Mwana wako, tunaweza wepesi kutenga mishale ya adui; ndiyo maana, tunakutaja mwenye heri, ee Mama wa Nuru, tena peke yako matumaini ya roho zetu.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya mbili. Efsplaknias iparkhusa.

Ee Chemchem ya usafi yote, kwa kufunga utulinde, ee Bwana wa wema; ututazame sisi wenye kusujudu mbele yako na sikiliza kuinua kwa mikono yetu, wewe uliyepanua mikono msalabani kwa ajili ya wokovu wa watu wote, ee Bwana mwenyezi.

Utukufu kwa Baba. . *(mara ingine hii wimbo ya yulu).*

Sasa na siku zote. . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, alipoona lufu yako msalabani Bikira Mama yako akalia kwa uchungu akasema*:* Ee Mwanangu, hii fumbo gani? Wewe mwenye kuwapa wote uzima wa milele namna gani unazarauliwa na kuuawa kwa kutaka kwako msalabani.

Elezo*: Tunaimba Fotagogikon ya sauti ya hii Juma na kisha:*

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Tupokeeni na furaha maagizo ya Kwarezima! Kama Baba yetu wa kwanza aliichunga, hatungaliondolewa shamba la Edeni; tunda lilikuwa nzuri kwa kulitazama na nzuri kwa kulikula, hii tunda na sababu ya kufa kwangu! Tusidanganywe kwa macho yetu ao kwa utamu wa vyakula visipo na utamu kama tunashiba; tukimbieni ulevi na tamaa ya kushiba, tuingie katika damu ya huyu aliyekufa kwa ajili yetu. Tusiwe mateka ya Muovu, lakini tuleni Paska Takatifu kamili ya Kristu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Namna gani tutawaita, enyi Mashahidi Watakatifu? Wakheruvi? Kwani ninyi ni kiti cha ufalme cha Kristu; Waserafi? Maana munamutukuza daima; Malaika; Kwa sababu mumejikatalia mwilini; Wenye uwezo? Sababu ya miujiza yalifanyika*:* MUna majina mengi na zawadi nyingi zaidi! Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Mwokozi, Viumbe vyote vilipokuona umesulubiwa msalabani kule Kalvario, vikafifia, na bila kuweza kuona hii ndoto, vikatetemeka; na Bikira Mtakatifu Mama yako akapaza sauti na kulia*:* Ole wangu, ee Mwanangu na Mwokozi wangu mpendwa, ni ajabu gani hii naona machoni mwangu!

Kisha tunaendela Ibada sawa ma siku ingine ya zamani.

MU KAZI TANO KWA MANGARIBI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Elezo*: Kisha* «Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo 10; ya kwanza tunaimba hii wimbo ni chini mara mbili. Kisha wimbo wa ine ya Sauti ya hii Juma na kisha wimbo wa ine ya Mtakatifu Theodoros.*

Sauti ya tano. Idiomelon.

Enyi waaminifu, kwa nuru tutimizeni matendo ya Mungu, tutembeeni na heshima kama mchana; tuvunjeni mapatano isiyo na haki na tuondoe ndani yetu machukizo yote juu ya jirani; tukatae tamaa ya mwili sababu ya kuongeza zawadi zetu za roho; tuwapeni maskini chakula, tumuendee Kristu, na kwa toba tumwambie*:* Ee Mungu wetu, utuhurumie. *(mara mbili).*

Elezo*: Sasa tunaimba wimbo 4 ya Sauti ya hii Juma. (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu).*

Kisha wimbo hii wa chini ya Mt. Theodoros.

Sauti ya mbili.

Kujeni, enyi marafiki wote wa Mashahidi, tushangilieni hii siku kuu katika furaha ya Roho Mtakatifu, kwani leo Mtakatifu Theodoro Shahidi anatutayarishia karamu ya kiroho sababu ya kufurahisha roho zetu zilizo marafiki wa siku Kuu wenye kumulalamikia*:* Salamu, wewe Mshindani uliyeangusha wazulumu wenyi majivuno na ambaye kwa ajili ya Kristu Mungu wetu, ukatoa mwili wako kwa mateso; salamu, kwani katika hatari ulionekana kuwa askari shujaa wa majeshi ya mbinguni, ndio maana tunakuomba*:* Ee Utukufu wa mashahidi, ombea kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Ee Shahidi Mtakatifu Theodore, kwa wakristu wote wenye kukukimbilia uwape, kwa miujiza yako, neema ya Mungu; kwa hii tunakutukuza tukiimba*:* Ewe Mkombozi wa wafungwa na mganga wa wagonjwa, bahati ya maskini tena wokovu wa wasafiri, mlinzi wa wale kupenda makumbusho yako takatifu, utupokelee na sisi pia kwa Kristu neema ya wokovu.

Theodore, Shahidi Mtakatifu, uko kweli «zawadi ya Mungu» kwa sababu, unapoishi kisha kufa, unasikiliza maombi ya wale wenye kukukimbilia*:* Zamani mtoto mumoja aliponyanganywa kwa mama yake na kufungwa katika jeshi la Wapagani, mama mjane akaosha altare yako na machozi yake; na wewe ulipomuonea huruma, ulipopanda juu ya frasi mweupe, ukamurudishia kwa ajabu mwana wake, na kisha haukwache kufanya miujiza. Umuombe Kristu Mungu wetu wokovu wa roho zetu.

Ee Theodore mara tatu mwenye heri, kwa jina lako naimbia zawadi ya Mungu, wewe taa yenye kuangaa na nuru ya Mungu; kwa ushuja wako uliangaza ulimwengu, ukionekana kuwa mwenye nguvu kabisa kuliko moto ulivunja kichwa cha nyoka mbaya; ndiyo maana Kristu aliweka taji ya ushindi kichwani mwako; na kwa sababu uko na neema ya Mungu, ee Shahidi mkubwa na Mtakaktifu, umuombe Mungu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya sita.*

Adui alipotumia mfalme kafiri juu ya waminifu kwa Kwarezima yenye kutakaswa, akajaribu kuwachafua na vuakula vyenye kuchafuka na damu ya wasiyo na kosa, lakini kwa hekima ukatengwa werevu wake wakati ulipomutokea kwa ndoto askofu wa hii wakati sababu ya kumupasha habari ya hatari; ndiyo maana tunakutolea sadaka zetu za shukrani na tunakupa cheo cha Mwokozi wakati tunaposhangilia makumbusho yako ya hii mambo, na tunakuomba utulinde tena kwa nia mbaya ya Adui ukituombea kwa Mungu, ee Shahidi Mtakatifu Theodore.

Sasa na siku zote*. . .* **THEOTOKION** (*mu Sauti ya sita ya Paraklitiki).*

KUINGIA KUBWA.

Mwangaza upole. . .

Mangaribi Prokimenon. *Sauti ya tano.* Zaburi 19 (20).

Bwana akujibu siku ya taabu;.

Shairi*:* Akutumie Mungu wa Yakobo likunyanyue;

Somo ya Mwanzo tutasoma (2, 20- 3, 20).

Mutu akawapa majina ngombe zote na ndege za hewa na kila nyama ya mwitu, lakini musaidia kwa mutu hakuonekana. Na Bwana Mungu alileta usingizi muzito kuangukia mutu, akalala; akatwaa mumoja wa mifupa ya mbavu zake, akafunga nyama kwa pahali penyewe; na mufupa wa mbavu Bwana Mungu alioondosha kwa mutu, akafanya mwanamuke, akamupeleka karibu na mutu. Adamu akasema*:* Huyu sasa mufupa wa mifupa yangu, na nyama ya nyama yangu; ataitwa Mwanamuke kwa maana ameondoshwa katika mume. Kwa sababu hii mume ataacha baba yake na mama yake na ata-fungana na muke wake; nao watakuwa mwili mumoja. Nao wawili walikuwa watupu, mume na muke wake, wala hawakuona haya. Basi nyoka alikuwa na hila kuliko nyama zote za mwitu Bwana Mungu aliofanya. Akamwambia mwanamuke*:* Ndiyo, Mungu amesema*:* Musile ya miti yote ya shamba? Mwanamuke akamwambia nyoka*:* Matunda ya miti ya shamba tunaweza kula ; lakini matunda ya muti ulio katikati ya shamba Mungu amesema*:* Musile yake wala rnusiyaguse, musife. Nyoka akamwambia mwanamuke*:* Hakika hamutakufa, kwani Mungu anajua ya kama siku mutakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama Mungu mukijua uzuri na ubaya. Na wakati mwanamuke alipoona ya kama muti ulikuwa muzuri kwa chakula, na ya kama ulipendeza macho, na ya kama ulikuwa muti wa kutamaaniwa, akatwaa ya matunda yake, akakula; akamupa mume wake vilevile pamoja naye, naye alikula. Nao wawili, macho yao yali-funguliwa; wakajua ya kama walikuwa watupu; wakashona majani ya mutini, wakajifanyia nguo. Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu akitembea shambani mangaribi; mume na muke wake wakajificha wenyewe mbele ya macho ya Bwana Mungu katikati ya miti ya shamba. Bwana Mungu akaita Adamu, akamwambia*:* Wewe ni wapi? Akasema*:* Nimesikia sauti yako shambani, nikaogopa, kwa sababu nilikuwa mutupu; nikajificha. Akasema*:* Nani alikuambia ya kama ulikuwa mutupu? Umekula wa muti juu yake nili-kuagiza*:* Usile? Mwanamume akasema*:* Mwanamuke uliyenipa awe pamoja nami, yeye alinipa ya muti, na nilikula. Bwana Mungu akamwambia mwanamuke*:* Nini hii uliyofanya? Mwanamuke akasema*:* Nyoka alinidanganya, na nilikula. Bwana Mungu akamwambia nyoka*:* Kwa sababu umefanya maneno haya, umelaaniwa kuliko nyama zote, na kuliko kila nyama ya mwitu; juu ya tumbo lako utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako; na nitatia uadui katikati yako na mwanamuke, na katikati ya uzao wako na uzao wake ; ataponda kichwa chako, na wewe utaponda kisigino chake. Akamwambia mwanamuke*:* Nitazidisha sana uchungu wako na kuzaa kwako; kwa uchungu utazaa watoto; kutaka kwako kutakuwa kwa, mume wako, naye atakutawala. Akamwambia Adamu*:* Kwa sababu umesikia sauti ya mwana-muke wako, na umekula ya muti, juu yake nilikuagiza nikisema*:* Usile matunda yake; udongo umelaaniwa kwa sababu yako; kwa uchungu utakula ya matunda yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba utakuotesha; na utakula majani ya shamba; kwa jasho ya uso wako utakula mukate, hata utakaporudi kwa udongo; kwa maana umetwa1iwa katikati yake; kwa sababu mavumbi wewe na utarudi kwa mavumbi. Mwanamume akaita Jina la muke wake Hawa, kwa sababu alikuwa mama ya wote walio hai.

Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 20.

Utukuzwa, ee Bwana, kwa nguvu zako;.

Shairi*:* Mufalme atafurahi kwa nguvu yako, ee Bwana.

Somo ya Mezali tutasoma. (3, 19-24).

Kwa hekima Bwana aliweka misingi ya inchi; kwa ufahamu alisimamisha mbingu. Kwa maarifa yake vilindi viligawanyika; na mawingu yanaangusha umande. Mwana wangu, yasiondoke mbele ya macho yako; shika hekima njema na akili; hivi zitakuwa uzima kwa nafsi yako na neema shingoni mwako. Halafu utakwenda katika njia yako salama, wala muguu wako hautakwaa. Wakati unapolala, hutaogopa; ndiyo, utalala, na usingizi wako utakuwa mutamu.

Kisha inafwata Ibada ya Liturgia ya wenyi kutakaswa (Proigiasmeni).

MU POSHO KWA ASUBUI YA JUMA YA KWANZA YA KWAREZIMA.

Elezo*: Kisha Eksapsalmos tunaimba: «Bwana ndiwe Mungu...»na sauti ya mbili na kisha Apolitikion ya Mt. Theodoros. (mara mbili) na kisha Theotokion na sauti yake.*

Apolitikion ya Mt. Theodoros. *Sauti ya mbili*

Matendo ya imani ni makubwa! Mtakatifu mushindi Theodoro aliyekuwa ndani ya chemchem ya moto, alishangilia, kama mapumziko ndani ya maji; kwani alilungua na moto, alijitoa kwa Utatu Mtakatifu kama mkate utamu. Kwa maombezi yake, ee Kristu Mungu, okoa nafsi zetu.

Utukufu kwa Baba... *(mara ingine apolitikion yake).*

Sasa na siku zote..**.THEOTOKION.** *Sauti ya mbili.*

Siri zako zote, zinapita wazo lolote na zote ni utukufu sana, ee Mzazi-Mungu, wewe uliyewekwa alama ya safi, uliyelindwa kwa ubikira, ulijulikana kuwa Mama msema kweli, ulizaa Mungu kweli; umwombe aokoe roho zetu.

Tunaimba kathisma wa kwanza ya kitabu Paraklitiki na kisha tunaimba hii kathisma ya Triodi.

KATHISMA ya Mtakatifu Theodoros.

Sauti ya tatu. Thias pisteos.

Unipojaa na juhudi juu ya imani, ulimaliza upotevu wa Wapagani, ukaondoa makufuru ya sanamu; na ulipokuwa wewe mwenyewe sadaka takatifu, unamwanga umande wa miujiza yako mpaka mwisho ya dunia*:* Ee Shahidi mtukufu, umuombe Kristu Mungu wetu atupe kama zawadi ya neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . *Umoja.*

Bwana, shujaa kwa mashindano, alipotaka kuponyesha magonjwa ya roho na kushinda tamaa za mwili, akakufanya wewe kuwa zawadi takatifu kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu; Ee Shahidi Mtakatifu Theodore, umuombe Kristu Mungu wetu alete mwetu neema ya wokovu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. Umoja.

Ee Bikira Mtakatifu, tumboni mwako ulipata mimba ya Mungu ambaye dunia haiwezi kuchukua, huyu ambaye bila mbegu alizaliwa kwa Baba mbele ya nyakati, Neno mwenye kukaa ndani yake, Mwana wa asili moja na Baba na Roho Mtakatifu*:* Umuombe pamoja na Manabii, Mashahidi, Wenye haki, Watawa na Watakatifu atuondolee makosa yetu.

Tunasoma Zaburi 50 (51).

KANUNI.

Sauti ya ine. Anikso to stoma mu.

Wimbo wa kwanza.

Wewe uliyemzaa kwa namna ya ajabu, Mungu mkuu akakuweka ku mustari wa kwanza wa mateule wako; ndiyo maana tunanzia pako wewe Bikira mwenye kustahili nyimbo zetu, wakati leo tunamwimbia huyu aliyekutukuza.

Naimbia Shahidi Mkubwa, Mshindani mwenye kuangaa, mwenye kujulikana popote duniani, mtukufu Theodore.

Siku moja ya furaha imeonekana katika hizi siku za sikitiko, inaangaza uso ya giza*:* Ni mwanzo wa matangulizi ya siku Kuu yenye kuangaa mbali kwa neema ya Shahidi Mtakatifu.

Inatakasa Eklezya kwa damu yake, sadaka ya Shahidi Mtakatifu*:* Mungu aliipokea ambaye Yeye mwenyewe alijitoa sadaka na anapokea kama sadaka ya malipo, huyu aliyeshindania utukufu wake kimungu.

THEOTOKION.

Hata kama siku Kuu inaonekana inje ya wakati, ni vema kutukuza hii siku ya leo, kwani Bikira mwenye kupamba ulimwengu wote anasharikia hii makumbusho ya huyu ambaye kwa ajili yake alitoa damu na uzima yake.

Sauti ya sita. Os en ipiro pezefsas o Israil.

Bwana Mungu, wa ajabu katika Watakatifu, ee Kristu, onyesha ndani yangu Maajabu ya mapendo yako ukinipa uwezo wa kuimbia ushujaa wa Shahidi wako kama inavyostahili.

Katika mateso na mashindano ulionyesha usabiti na nguvu; ee Mshindani wa Kristu, onyesha wepesi mara ya pili kwa ajili yetu msaada wako.

Mzalimu kwa uovu wake alipokataa rohoni mwake imani ya Padri na ibada yao, akakusudia kushindana daima na Mungu.

THEOTOKION

Katika wewe yametimizika waziwazi uaguzi wa Manabii ya zamani, ee Bikira na mama uliyezaa kweli Mungu kwa namna ya ajabu.

Sauti ya ine. Tus sus imnologus Theotoke.

Wimbo wa tatu.

Ee Bikira, watu wenye kuitwa wakristu wanapotamainia kuona siku ya Mwana wako, wanatangulia kushangilia, kwa kumufananisha hii siku Kuu kwa heshima yako na ile ya Shahidi wako mtukufu.

Mema inashinda, kwani aliye mkubwa kabisa katika mashindano aligeuza na furaha tabia ya uchungu ya hii wakati, akishangilia ngumu wa Kwarezima kubwa.

Ee Theodore, kwako inafaa zawadi, kwani ni moja ya tabia zako; na sisi uliyoweka katika sehemu ya uriti wako, tunakutolea zawadi ya furaha ya sifa zetu.

Kwa uhodari na ushujaa wako unangusha moja nzuri kabisa ya majengo na kushinda nyoka mwenyi kurarua huyu alipuliza mauti na moto kama inavyoongezeka ushujaa yako.

Kafiri mpya aliye mkali kabisa tena kuliko wa kwanza, alichangaa sadaka na vyakula kama sumu, lakini Shahidi akamucheza mlaanifu.

THEOTOKION

Ee BIkira, dunia yote imejaa na maarifa ya Bwana aliyezaliwa kwako; lakini neema nyingi yakapewa kwa Mashahidi watakatifu waliosabitisha imani ya kweli.

KATHISMA.

Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.

Ulipovaa silaha ya Mungu wako na kukataa udanganyifu ya sanamu, Malaika wakaimbia mashindano yako; na roho ilipowaka na mapendo ya kimungu, ukazarau kwa ushujaa mauti kwa moto; unapojibu kwa jina ulipolewa, kwa wale wenye kukuomba uwape zawadi za Mungu na vipaji vya kuponyesha. Ee Mtakatifu Shahidi Theodore, umuombe Kristu Mungu wetu, kwa wema wake, awaondolee zambi zao wale wanatukuza kwa moyo wote makumbusho yako ya utakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . *Umoja.*

Bila kukamatiwa katika masifu ya Maksimino, lakini uliposabitishwa kwa maneno ya Kristu, ukabomoa mahekalu ya miungu ya uwongo mashindani mshujaa mwenye kushinda adui; na uliposhika unabii, ukavuka moto kama maji; basi inastahili kweli kwa tuzo ya mashindano yako uwe Chemchem ya maponyesho ya wale wenye kukuomba na imani. Ee Shahidi Mtakatifu Theodore, umuombe Kristu Mungu wetu awaondolee zambi zao wale wenye kutukuza na mapendo makumbusho yako ya utakatifu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Umoja.*

Ee Bikira Bibi arusi wa Muumba, ee Mama wa Mwokozi usiye na doa, makao ya aliye-Juu mwenye kustahili nyimbo zetu, ujiharikishe kija kuniokoa mimi niliye makao ya haya na ya zambi, na kwa mawazo yangu nimekuwa mchezo wa Shetani; angaza makao yangu na nuru ya fazila; ee Kinara chenye kuangaa na nuru, ondoa giza ya tamaa zangu na unistahilishe nuru na mbinguni ukiniangaza na nuru yako ya milele.

KONTAKION.

Sauti ya mnane.

Ulipovaa imani ya Kristu moyoni mwako kama kanzu ya chuma, ulishinda nguvu za adui kwa mashindani yako na ulipokea taji ya milele mbinguni, ee Shahidi mushindi.

IKOS.

Wewe mwenye kukaa katika kiti cha nuru, kwa shukrani tunakuimbia na imani, kwani ulitupatia kama zawadi takatifu Mtakatifu Theodore mshindani, katika hii uzima mara tatu mwenye heri kama mlinzi wa ukweli, anapomjua Kridstu katika roho yake ya Ibada, akashindana na Shetani, Shahidi mshindi.

SINAKSARI

Elezo: *Sasa ku mwanzo tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha Sinaksasi hii.* Hii Siku ya posho ya Juma wa Kwanza ya Kwarezima tunashangilia muujiza ya Koliva iliyefanya Mtakatifu Theodoros.

EKSAPOSTILARON.

Sauti ya mbili. Tis Mathites sinelthomen.

Ee Mchukuzi wa taji takatifu, unasimama sasa pamoja na Malaika karibu ya kiti cha ufalme cha Kristu, ewe Mshindi, unangaa na nuru ya juu mbinguni; ombea daima dunia yote amani na wokovu wa wale wenye kutukuza makumbusho yako ya nuru, ee mwenye heri Theodore mwenye kuangaa na utakatifu.

THEOTOKION.

Ee Mzazi-Mungu, alipotaka kufufua watu wenye kupokea, Bwana akakaa tumboni mwako; na sisi wote tuliopata wokovu, tunakulalamikia*:* Salamu, ewe utukufu wa malaika, mbarikiwa katika wanawake wote, kwa maana ulizaa furaha ya ulimwengu.

MASIFU.

Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.

Enyi waaminifu, kwa nyimbo za siri tunatukuza shujaa wa majeshi ya mbinguni kama mlinzi wa imani yetu na tumuambie kwa sauti moja*:* Ee Shuhuda wa ajabu wa Yesu, utuombee.

Kwa jina unakuitwa na haki, Theodore mwenye heri mara tatu, ukawa kweli, kwa ajili ya roho zenye kuhuzunika, «zawadi ya Mungu», mutu yoyote mwenye kuingia katika patakatifu pako anapokea kweli zawadi ya ushujaa wako na anatukuza Kristu kwa furaha.

Kwa mateso yako na kwa mashindano yako ulikusanya hazina ya ibada, na kwa nguvu yako ukaitoa kwa Mungu kama zawadi yenye kupendeza, ukatimiza kwa bidii yako kwa mashindano hii zawadi ya Mungu ambayo jina lako lina maana.

Enyi marafiki za siku Kuu, munapofurahi kwa ibada ya nuru ya Shahidi Mtakatifu, kujeni wote tushangilie tukitukuza ukubwa wa utukufu wake, na kwa nyimbo zetu tutukuzeni Kristu aliyetukuza makumbusho yake.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita.*

Ee Shahidi Mtakatifu Theodore, ulionekana kwa watu kuwa hazina ya uzima ya kimungu na zawadi ya utakatifu, kwani Kristu alitukuza makumbusho yako; na sisi waaminifu, kwa sauti moja tunaimbia na furaha makumbusho ya mateso na mashindano yako.

Sasa na siku zote. . .

Ee Mzazi-Mungu, wewe kweli ni Mzabibu uliyestawisha tunda la uzima; ee Bibi yetu, tunakuomba*:* Katikati ya Mitume na ya Watakatifu wote omba kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

APOSTIKHA.

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Leo, kundi la Mashahidi wanacheza na furaha katika patakatifu pako, na Malaika wanashangilia ushujaa wa mashindo yako; Kristu mwenyewe eko pale yeye aliyekuvika taji ya shahidi; anajaza na zawadi zake nyingi wale wenyi kukutukuza kwa nyimbo zao; kwa hamu yako ulimutafuta ulipomupata, unakaa katika mapendo yake. Umuombe alete nuru na wokovu rohoni mwetu.

Shairi: Mwenye haki anafurahi katika Bwana na anamutumainia.

Kwarezima takatifu ni zawadi kwa sisi, inatupatia kushangilia pamoja naye maajabu ya Shahidi Mtakatifu; kwa kufunga tunatakaswa kwa madoa yenye kuchafua roho zetu; kwa mfano wa fazila ya mashahidi tunapata nguvu ya kushindana na tamaa; tukiangazwa kwa neema ya kwarezima takatifu na kwa ushujaa wa Shahidi Theodore, tunasabitishwa katika imani yetu kwa Kristu, na tunamuomba wokovu kwa ajili ya roho zetu.

Shairi: Mwenye haki atastawika kama mtende, atakua kama mti mkubwa wa Liban.

Kwa uwezo ushuhuda wako inakupa kwa Mungu, ulitengwa werevu wa kafiri juu ya imani ya Kristu; ulipolinda taifa takatifu, ukaliepusha kwa vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; ndiyo maana tunakutukuza kama mshindani wa miungu ya uongo, kama Mwokozi na mlinzi wa kondoo za Kristu; na tunapokuimbia kama mlinzi, tunakuomba upokee kwa ajili yetu nuru na usamehe.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane.*

Ulipovaa ushujaa ya Mashahidi, ukalinda, kwa uwezo wako, ibada ya roho juu ya ukafiri wa sanamu, ee shuhuda mshindi wa Kristu; uliharibu nguvu ya wazulumu, ulizarau mateso na moto ya dunia; ee Theodore, «Zawadi ya Mungu» kwa jina na kwa tendo, kwa maombezi yako okoa wale wenye kushangilia makumbusho yako.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bibi yetu, pokea ya watumishi wako*:* Utuokoe toka hatari na mateso yote.

MU JUMA SIKU KUU YA ORTHODOKSIA

Elezo*:* Kisha wimbo ya «Bwana nimekuita. . . » tunaimba Wimbo ya Paraklitiki 6 na ya hii Kitabu 4*:*

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Ee Bwana ambaye ulimwengu haiwezi kuchukua, ulizaliwa kwa Baba wa milele na asiye na mwili mbele ya wakati, na kwa tendo la Roho Mtakatifu Manabii, walitangaza kuja kwako kama Mwana atakaye pata mwili kwa Bikira Mtakatifu sababu ya kuzungumuza na kuonekana na wanadamu. Ee Bwana wa huruma, utustahilishe kwa nuru yako, sisi wenye kutukuza Ufufuo wako takatifu usiyokadirika.

Manabii wenye kuongozwa walipokutanga kwa neno na kukutumikia kwa matendo walistahili uzima wa milele; na walipotaka kutumikia viumbe bila kukuchukia wewe Mungu Muumba, wakazarau dunia sababu ya kukutangaza na wanashika Mateso yako ambako walipokea unabii. Kwa maombezi yao utupe sisi tutimize kwa usafi wote hii Kwarezima, ee Bwana wa huruma.

Ee Bwana, wewe ambaye kwa hali yako ya umungu ni wa milele kwa nyakati za mwisho ulitaka kujua mipaka ya mwili, na kwa umwilisho wako ulichukua hali yote ya ubinadamu; na mufano wa sura yako tunayandika sababu ya kuiheshimu na kutuinua mpaka kwa mapendo yako huko tunashota neema ya wokovu kufwatana na matoleo takatifu ya Mitume wako watakatifu.

Ni pambo ya bei kubwa Eklezya ya Kristu ilipokea katika ma Ikone takatifu ya Mwokozi, ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu wote; tunapoyaweka juu, inangaa nuru ikifukuza uhalifu, na furaha inatukuza Mungu ambaye kwa mapendo yake kwa ajili yetu aliteswa kwa kutaka kwake.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mbili.*

Neema ya ukweli iliangaa*:* Hii zamani ilikuwa katika giza sasa inatimizika mchana; tazama Eklazya inavaa kama pambo ya mbinguni Sura ya mwili ya Kristu ile hema ya ushuhuda ilitangulia kuonyesha; inahakikisha iomani ya kweli ili tuwe na sura yasipo kosa ya huyu tunatukuza. Naye ni ya wale wanawaza namna ingine, kwani tunajitukuza katika sura ya Neno aliyejifanya mtu ambaye tunaabudu. Enyi waaminifu, tuitukuzeni na tuimbe*:* Ee Kristu, okoa watu wako na bariki uriti wako.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION** *(na Sauti ya Paraklitiki).*

Apostikha tunaimba ya Kitabu ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma. Na hapa tunaimba paka Utukufu. . .

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mbili.*

Sisi tuliokataa giza ya ukafiri na kuangaziwa na nuru ya maarifa, tuimbeni nyimbo za furaha; sifa yetu na shukrani yetu ya pande kwa Mungu! Tusujudu na heshima mbele ya ma Ikone Takatifu ya Kristu, ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu wote tukikataa ukafiri wa wale wasio na imani ya kweli; Kwani Mtakatifu Basile anasema*:* Kuheshimu Ikone ni kuheshimu huyu aliyepo. Kwa maombezi ya Mama yako Mtakartifu kamili na ya Watakatifu wote, tunakuomba, ee Kristu Mungu wetu, utupe neema ya wokovu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Sauti umoja.*

Hii ni jambo la ajabu lenye kupita maajabu yote ya zamani*:* Hakuna hata mumoja amekwisha kuona bikira amezaa na kuchukua mikononi mwake huyu mwenye kukumbatia viumbe vyote. Hii kuzaa ni Mungu aliitaka; na kama ulivyomubeba mikononi mwako kama

mtoto na mbele yake unatumainia kama mama, ee Bikira safi kamili utuombee wokovu wa roho zetu.

Apolitikion. *Sauti ya mbili.*

Tunaabudu Ikone wako safi kabisa, ee Mwema, na tunaomba rehema ya makosa yetu, ee Kristu Mungu. Ulipanda Msalabani kwa kutaka kwako mwilini mwako sababu ya kuokoa ku utumwa wa adui hawa ulioumba. Ndiyo maana tunakushukuru tukipaza sauti*:* Ulijaza vitu vyote na furaha, ee Mwokozi wetu, ulipokuja kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Siri zako zote, zinapita wazo lolote na zote ni utukufu sana, ee Mzazi-Mungu, wewe uliyechahapiwa alama ya safi, uliyelindiwa kwa ubikira, ulijulikana Mama msema kweli, ulizaa Mungu kweli; umwombe aokoe roho zetu.

MU JUMA ASUBUI YA ORTHODOKSIA

SALA YA ASUBUI (ORTHROS).

Elezo*: Kisha Eksapsalmos tunaimba «Bwana ndiwe. . . » na hii Apolitikia: Nikusema Apolitikion ya Ufufuo na sauti ya hii Juma. Kisha:*

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mbili.*

Tunaabudu Ikone wako safi kabisa,....

Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.

Siri zako zote, zinapita wazo lolote....

Kisha tunaimba Kathisma ya Paraklitiki. Mahimidi. Anavathmi na padri atasoma Evangelion ya Asubui.

Kisha Zaburi 50(51) tunaimba hii wimbo ya Kwarezima:

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane.*

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana chemchem ya uzima; roho yangu ikeshe hekalu lako takatifu, ikichukua hekalu chafu la mwili wangu, lakini katika wema wako unitakase kwa mapendezi yako kubwa na mapendo yako ya huruma.

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya mnane.*

Uniongoze njiani ya wokovu, ee Mzazi-Mungu, kwani nilichafua roho yangu kwa zambi, na kwa uvivu wangu nilitumia vibaya uzima wangu, lakini kwa maombezi yako takatifu uniopeo ku uovu wote.

Sauti ya sita

Unirehemu, ee Mungu sawasawa ni wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uufute makosa yangu.

Nikikumbuka wingi wa matendo yangu mabaya, mimi mwenye zambi, naogopa ile siku ya ajabu ya hukumu, lakini ninapotumainia rehema na ruhuma yako, napaza sauti kama Daudi*:* Unihurumie, ee Mungu, kadiri ya wema wako kubwa.

KANUNI

Sauti ya ine. Thalasis to erithreon pelagos.

Wimbo wa kwanza.

Enyi waaminifu tunapofurahi na furaha na sherehe, tuimbe leo*:* Ee Kristu, matendo yako ni ya ajabu, uwezo wako ni kubwa, ee Bwana, wewe uliyeweka umoja kati yetu.

Kujeni tushangilie hii siku kwa furaha na maastajabu ya Mungu*:* Mbingu na inchi zinafurahi, makundi ya malaika na ya wanadamu wanajibu kwa sauti ya furaha.

Kwa kuona hii mema kubwa, kujeni enyi waaminifu, tupigeni mikono*:* Viungo vya Kristu vilivyotengana vinaungana; tutukuzeni Bwana mwenye kutupa sisi amani.

Leo Eklezya inapewa tuzo ya ushindi wake kwa amri na kusudi yenye kuongoza na Mungu ya Wafalme wema Mikaeli na Theodora.

THEOTOKION

Ee Bikira Mtakatifu kamili, upanga wa uhalifu imeondolewa, tunapata furaha takatifu wakati tunaona Hekalu yako, yenye kupambwa na Sura Takatifu.

Sauti umoja. Efrenete epi si.

Wimbo wa tatu.

Wahalifu makafiri hawanyanyuo juu uso wao, kwa sababu Uorthodoksi inashinda kwa uwezo wa Mungu.

Leo kama zamani, mawingu yanatumwangia umande wenyi kuleta uzima sababu ya kuzaliwa mara ya mbili katika imani.

Isikilike na furaha baragumu ya siri ya Mitume wa Kristu kwa kurudisha Sura takatifu.

Tumwimbie Kristu aliyetupa sisi Malkia mwenyi ibada, rafiki yake, pamoja na mwana wake aliyevikwa taji kwa Mungu.

THEOTOKION

Katika patakatifu pako, ee Bikira Mtakatifu kamili, sisi waaminifu tunakuomba*:* Utuangazie na nuru yako.

IRMOS. Eklezya yako, ee Kristu, inafurahiwa katika wewe na inakulalamikia*:* Bwana, ndiwe nguvu yangu, kimbilio langu na msaada wangu.

KATHISMA

Sauti ya kwanza. Khoros angelikos.

Ee Kristu, ulipoonyesha hali ya umungu wako juu ya Ikone, tunaimbia waziwazi kuzaliwa kwako, miujiza yako na kusulubiwa kwako kwa kutaka, mashetani wanafukuzwa na wanaogopa, makafiri wanalia.

Utukufu kwa Baba. . *Umoja.*

Ikone ya ma Nabii, ya Mitume na ya ma Shahidi, sura takatifu ya Watakatifu wote yanapamba Yerusalema ya mbinguni yenyi kuangaa na Uzuri wa kiroho wa Bwana Arusi na wa Bikira asiyeolewa.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira, uwe boma na ulinzi wa wale wenye kutukuza na mapendo Ikone yako takatifu, wakikutangaza kuwa Mzazi-Mungu kweli na kusujudu mbele yako.

KONTAKION.

Sauti ya mnane. Aftomelon.

Neno la Mungu ambaye ulimwengu haiwezi kuenezwa anatahiriwa akijifanya mtu kwako, ee Mzazi-Mungu, na anatengeneza sura iliyochafuka zamani kwa zambi akiongezako uzuri wake wa kimungu, turudishe na sisi pia mfano wetu na Mungu.

IKOS.

Fumbo ya wokovu wetu ilitangaziwa zamani na ma Nabii wenye kuongozwa na Mungu*:* Kwa ajili yetu sisi tunafika kwa mwisho wa nyakati, walieleza hii nuru. Katika hii tunapokea maarifa ya Mungu, Mungu mumoja na Bwana katika watu tatu watukufu, ni yeye peke tunatumikia; tunapokuwa na imani moja, ubatizo moja, tulivaa Kristu. Tunapoungama wokovu kwa maneno na kwa matendo, turudishe na sisi pia mfano na Mungu.

SINAKSARI.

Leo, siku ya Mungu ya kwanza ya kufunga, tunafanya makumbusho ya kurudisha ma Ikone Takatifu Hekaluni iliofanyika wakati wa utawalo wa Mikaeli, mfalme wa Konstantinopoli na mama yake Theodora wa Makumbusho milele, na wakati wa uwongozi wa patriache mtakatifu na muungamizi Methodios.

Zamani ma Ikone yalikataziwa*:* Nafurahi wakati ninaona ibada yao yamerudishwa tena.

Ee Kristu, Ikone ya Baba isiyoweza kuharibika, kwa maombi ya Waungamizi wako Watakatifu, utuhurumie. Amina.

KATAVASIES

Sauti ya ine.

Wimbo wa kwanza.

Wakati walipovuka katikati ya bahari nyekundu kwa inchi kavu, wa Israeli wa zamani wakakimbiza jangwani jeshi la Amaleki kwa nguvu ya mikono Musa aliyopanua mu alama ya msalaba.

Wimbo wa tatu.

Eklezya yako, ee Kristu, inafurahiwa katika wewe na inakulalamikia*:* Bwana, ndiwe nguvu yangu, kimbilio langu na msaada wangu.

Wimbo wa ine.

Ilipokuona umetundikwa msalabani, wewe Jua la Haki, Eklezya tangu pa fasi yake ikalalamika kweli*:* Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo wa tano.

Bwana, ulikuja kama nuru duniani, nuru takatifu kuondoa ku ujinga wa giza hawa wenye kukuimbia na imani.

Wimbo wa sita.

Eklezya yako inakulalamikia na sauti kubwa*:* nitakutolea Sadaka ya sifa, Bwana, katika rehema yako ulitakasa ku damu ya mashetani kwa damu yenye kutoka ku ubavu wako.

Wimbo wa saba.

Katika tanuru ya Persi waana wa Abrahamu japo mwako wa moto uliyowaka kwa ibada yao, wakalalamika*:* Umetukuzwa, ee Bwana, katika hekalu la utukufu.

Wimbo wa mnane.

Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamsujudu Bwana.

Danieli alipopanua mikono katika shimo akafunga kinywa cha Simba; Vijana, wenye kujaa na bidi ya imani yao, wenye kuvaa fazila, wakazima nguvu ya moto wakati walipolalamika*:* Tukuzeni Bwana, enyi wote bviumbe vya Bwana.

Wimbo wa tisa.

Kristu, jiwe la pembe ambalo mkono hata mmoja haukuchonga lakini likachongwa nawe, ee Bikira, mulima haramu; ni yeye aliyeunganisha hali zenye kutengana*:* Tena tunapojazwa na furaha, ee Mzazi-Mungu, tunakutukuza.

EKSAPOSTILARION.

Tufurahiwe, tupigeni mikono, na kwa furaha tuimbeni*:* Matendo yako na ya ajabu, ee Kristu! Nani atasema uwezo wako, ee Bwana? Kwa maana ulikusanya Eklezya yako katika umoja.

THEOTOKION.

Upanga wa uhalifu imetoweka, makumbusho yake imeondolewa; na wakati tunaona hekalu yako yote yenye kupambwa na neema ya ikona yako tukufu, tumejazwa wote na furaha.

MASIFU.

Sauti ya ine. Edokas simioson.

Katika wewe Eklezya inafurahi sasa, ee Bwana Mpenza-wanadamu, wewe uliye Bwana Arusi wake na Muumba wake uliyemuokoa toka uzongo wa sanamu kwa mapenzi yako sababu ya kuiunganisha kwako kwa Da, u yako heshimiwa; na Eklezya yako inapopokea na furaha kurudisha kwa Ikona takatifu, inaimbia sifa yako na kutukuza jina lako.

Shairi: Nitashukuru Bwana kwa moyo wangu wote, katika baraza ya wenye haki, na katika makutano.

Ee Bwana, unapoonyesha sura yako ya ubinadamu sababu ya kuitukuza, tunatangaza fumbo kubwa ya tendo lako la wokovu; Ee Kristu Mpenza-wanadamu, ulionekana machoni mwetu apana kwa kuonekana bure tu kama wanavyozania Wamanikea, lakini kwa ukweli wa mwili ambayo hali inatuongoza kwa mapendo yako.

Shairi: Usimame, ee Bwana, nyanyua mukono wako, usisahau masikinim kwa nini mwovu anazarau Mungu.

Leo inaonekana siku ya furaha na shangilio ya kujaa, kwa sababu mafundisho ya kweli inangaa; Eklezya ya Kristu inangaa na nuru ya Sura ya Watakatifu wote; kwa hivi mapatano inatawala na inafanyika kati ya waaminifu kwa ushindi ya Mungu.

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya sita.*

Wakati wa kufunga, Musa alipokea Amri; alipofunga Elia akafunga mbingu; na watoto tatu wa Abrahamu wakashinda mzulumu muovu kwa kadiri yao. katika hii utupe na sisi pia, ee Mungu Mwokozi, tusharikie Ufufuo wako tukiimba*:* Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Msiyekufa Mtakatifu, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa u Kristu Mungu wetu, uliyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA .

LITURGIA TAKATIFU.

Antifonon ya kwanza

Shairi: Bwana ni Mfalme, amevaa utukufu. Bwana amevaa utukufu, amejifunga ezi kiunoni.
Kwa maombi ya Mzazi-Mungu...
Shairi:Amekaza ulimwengu usitikisike.
Kwa maombi ya Mzazi-Mungu...
Shairi:Nani anayeweza kutaja matendo ya uwezo wa Bwana ao kuonyesha sifa yake yote?
Kwa maombi ya Mzazi-Mungu...
Utukufu... Sasa... Kwa maombi ya Mzazi-Mungu...

Antifonon ya Mbili

Shairi: Watu washukuru Bwana kwa ajili ya wema wake, na kwa ajili ya kazi zake za ajabu kwa wana wa watu!
Utuokoe... aliyefufuka katika wafu...
Shairi:Wamutukuze vilevile katika kusanyiko la watu na kumusifu katika baraza ya wazee.
Utuokoe... aliyefufuka katika wafu...
Shairi:Macho yangu yatakuwa juu ya waaminifu wa inchi, ili wakae pamoja nami.
Utuokoe... aliyefufuka katika wafu...
Utukufu. Sasa. Uliye Mwana wa pekee...

Antifonon ya tatu

Shairi:Mbingu na inchi zimusifu.
Apolitikion ya Orthodoksia.
Shairi:Hii ni siku Bwana aliyofanya; tunafurahi na kushangilia ndani yake.
Apolitikion ya Orthodoksia.
Shairi:Ee Bwana Mungu wangu, kwa milele ninakushukuru.
Apolitikion ya Orthodoksia.
Kuingia (Isodikon). Njooni tumwabudu... aliyefufuka katika wafu... Apolitikion ya Ufufuo, ya Orthodoksia, ya Mtakatifu ya leo, ya Kanisa. Kontakion: Apostolos na Evangelion ya hii siku ya Orthodoksia. Liturgia tunaendelea ya Mt. Basile. Pahali kwa fasi ya Niwajibu kweli tunaimba wimbo ingine ya Muzazi Mungu ile iko kwa Liturgia ya Mt. Basile. Kinonikoni: Msifuni...

Elezo: *Kisha Liturgia tunafanya Kujuguluka pembeni ya Kanisa pamoja na Waaminifu wale wanakamata ma Ikona mikononi wao na tunakumbuka ma jina ya Wale Watakatifu wetu walikombana kupingana ya wale wafunfisho ya uongo. Inje ya Solea Shemasi anasema:*
«Ee Rabi, bariki kuingia Kitakatifu».
Padri: Kubarikiwa kuingia kwa patakatifu pako, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele».
Vile inaanza Kujuguluka (Litania).
Tunaimba, wakati tunaanza kutembea inje, Apolitikion ya Orthodoksia, mara ine. Padri ku mwisho anafanya makumbusho ya Watakatifu wetu wale walikombana na walichunga imani Orthodokse.
Elezo: *Waimbaji wanaimba mara ya kwanza Apolitikion ya Orthopdoksia.*
Usimamisho wa kwanza inje ya Kanisa:
PADRI ao SHEMASI: Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.
MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu, watawa na waorthodoksi wote.
MWIMBAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*
PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu (jina lake).
MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

PADRI: Kwa kuwa Wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu, na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Mwimbaji: Amina.*Wanaimba mara ya mbili Apolitikion ya Orthodoksia.*

Usimamisho wa mbili pa fasi ya kuume ya kanisa.

PADRI ao SHEMASI: Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya padri mkubwa wetu Arhimandriti Meletios na waorthodoksi wote katika Kristu.

PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Watumishi wa Mungu, Wakristu wote wenyi Ibada na wa Ortodoksi, wanaokaa katika mji huu na ya jamii ya parokia, ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, msaada, usamehe na maondoleo ya zambi.

PADRI: Kwa kuwa Wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu, na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Mwimbaji: Amina. *Wanaimba mara ya tatu Apolitikion ya Orthodoksia.*

Usimamisho ya tatu, pa fasi, inje ya Altari Takatifu.

PADRI ao SHEMASI: Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba mapumziko ya moyo wa watumishi wa Mungu tangu mwanzo ya dunia mupaka sasa na uwasamehe makosa yao yote ya kupenda na yasiyo kupenda.

MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

PADRI: Kwa kuwa Wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu, na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Mwimbaji: Amina. *Wanaimba mara ya inne Apolitikion ya Orthodoksia*

Usimamisho wa ine pa fasi ya kushoto ya kanisa

PADRI ao SHEMASI: Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya kulinda hii Hekalu Takatifu hii mji, kila mji na kila inchi, na ya wanaoishiimo toka hasira, huzuni, njaa, mtetemeko wa inchi, garika, moto, upanga, mashambulio ya adui, vita kati ya raia, na lufu kwa rafla, ili Mungu wetu mwema kamili na mpenda-wanadamu atufazilie na kuturehemu, aondoe mbali hasira yote na magonjwa yenye kuelekeza kwa sisi, atuopoe toka makamio na atuhurumie.

PADRI: Kwa kuwa Wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu, na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Mwimbaji: Amina.

Kisha hii usimamisho ya inee padri atasoma Kanuni ya Sinodi Ikumeniki ya saba.

KANUNI YA SINODI IKUMENIKI YA SABA JUU YA UORTHODOKSI

Ushukuru kwa Mungu wetu siku ya Makumbusho ya kurudisha upya katika Eklezya ya Mungu pamoja na taarifa ya kanuni za imani na uharibifu wa makosa mbaya ya ukafiri.

Kufwata na neno la Nabii, tunapotii mashauri ya Mtume na kufundishwa kwa habari ya habari Njema tunatukuza siku ya upya. Isaya anasema ya kama Visanga vinapaswa kuwa mpya

kwa Mungu, akitajaa hivi Maeklezya ya mataifa. Hh Maeklezya haiko paka majengo mazuri ya hekalu lakini ni makutano ya Waaminifu wenyi kujaamo na kutukuziamo ibada takatifu kwa nyimbo na mashairi. katika maana ileile Mtume anashauria kuishi na uzima mpya na anaamuru kwa kila kiumbe mupya katika Kristu ijifanye kuwa mupya. Maneno ya Bwana yanasema kwa namna ya unabii*:* «Walishangilia huko Yerusalema Siku Kuu ya Upya; ilikuwa ni wakati wa baridi». ao wakati baridi ya kiroho ambayo wayuda walitayarisha mvurugo na fujo sababu ya kumuua ya hewa. Ndiyo, tulipata wakati wetu wa baridi, wakati wa baridi apana yeyota yenye kutumwangia ngumu wa neema takatifu, na kwa ajili ya mema tunavuka tunakuja kumushukuru Mungu;sababu ya kumwambia kama inavyosema Zaburi*:* «Hari na wakati wa baridi ni wewe uliifanya; kumbuka, ee Bwana. . . ». Halafu, maadui walikufuru, walitukana kutukuza Maikone takatifu na walijitukuza kwa ukafiri wao, ni Mungu Yeye mwenye aliwaharibu, Yeye aliye Muumba wa maajabu; aliangusha majivuno ya makafiri na hakuzarau sauti ya wale walimulalamikia*:* «Ukumbuke, ee Bwana, haya waliazibiwa watumishi wako*:* Nina mwilini mwangu matusi ya wapagani wote, matukano ya maadui zako, ee Bwana, matusi yao kwa alama za Kristu wako». Alama za Kristu ni wale waliokolewa kwa lufu yake na kumusadiki Yeye katika muhubiri ya neno lake na Ikone ya sura yake; katika hii tendo kubwa la wokovu limejulikana kwa wenye kuokolewa katika mateso yake na miujiza yake mbele na kisha kusulubiwa kwake; na kwa mateso yake mfano ikawapata Mitume, Mashahidi mpaka watawa na wenye kukiri imani

Hii makutano, hii mateso ya maadui za Bwana kwa alama ya Kristu wake Mungu wetu aliyekumbuka katika rehema yake, na kwa jibu ya maombezi ya mama yake, ya Mitume na ya Watakatifu wote ambao walizarauliwa na kutukanwa pamoja naye katika Maikone (kama walivyoteseka pamoja naye mwilini, vivyo hivyo walipaswa kutukanwa pamoja naye katika Maikone Takatifu), sababu ya kutimiza ile aliamuru leo, akifanya mara ingine ile alitimiza mara ya kwanza. Ya kwanza, kisha miaka mingi ambako Maikone Takatifu yalizarauliwa akairudishia ibada; sasa basi ni mara ya pili, kidogo kisha miaka makumi tatu ya sikitiko alitupatia, japo kutostahili kwetu, mwisho wa mateso yetu, ukombozi toka wazulumu wetu, mahubiri ya imani, neema ya kutukuza ikone kwa utaratibu na hii Siku Kuu yenyi kuleta wokovu. Katika Maikone tunaona Mateso aliteswa Rabi kwa ajili yetu, Msalaba, Maziko, Hadeze imeeeeuawa na kunyaganya, mashindano na utukufu wa Mashahidi, basi wokovu ambao Mgawanyi wetu wa kwanza wa zawabu na wa utukufu alitimiza Yeye mwenyewe duniani.

Basi, tunashangilia leo hii Siku Kuu*:* katika maombi na sala tunaunganisha mioyo yetu kwa furaha na kutukuza sababu ya kusema pamoja na zaburi na nyimbo*:* «Mungu gani aliye mkubwa kuliko Mungu wetu? Wewe ni Mungu mwenye kufanya maajabu». Ulimaliza ubishi ya watu wenyi kuzarau utukufu wako; wale walijaa na ujasiri juu ya maikone uliwakimbiza wakisitasita. Hii basi ni shukrani yetu kwa Mungu na tazama ushindi wa bwana juu ya maadui zake. Kwa ile inaelekea vita ma mashindano juu ya wenyi kuzarau Ikone tutaonyesha habari yote katika maneno mengine. Tazama, sasa sisi ni kama katika mapumziko kisha kuvuka jangwa, tuapata Yerusalema ya kiroho; kwa mfano wa Musa ao kwa shauri la Mungu kama juu ya mnara wenyi kujengwa na mawe kubwa na tayari kwa kupokea maandiko, ilitustahili na haki kwandika moyoni mwa ndugu zetu baraka wanastahili wenyi kushika imani na laana wanajiwekea wahalifu Ndio maana tunasema*:*

Kwa wale wenye kuungama kwa kinywa, kwa roho na kwa akili kwa neno, kwa rangi na kwa Ikone kuja katika mwili wa Neno la Mungu*:* Makumbusho milele!

Kwa wale wenye kutambua katika Kristu tafauti ya hali ya kama kuna yenye kuumbwa na isiyoumbwa, ya kuonekana na isiyoonekana, ya mateso na isiyotesema, ya kutahiriwa na isiyotahiriwa; na wenye kuipatia hali ya umungu alama ya isiyoumbwa, kwa hali ya ubinadamu alama zingine mpaka ile ya kutahiriwa, na wanaifanya kwa neno na kwa Ikone*:* makumbusho milele!

Kwa wale wenye kuamini, kusema ao kutangaza maneno kwa maandiko na vitu kwa mufano; na wanawaza ya kama inafaa kuhubiri kwa maneno kuliko kuhakikisha ukweli kwa Ikone*:* makumbusho milele!

Kwa wale wenye kutakasa midomo yao kwa neno, kisha wasikilizi kwa neno ileile; na wanajua na kusoma ya kama macho ya wenye kuona na macho yao yanatakaswa vilevile kwa maikone Takatifu na ya kama katika hii akili yao inawapeleka kwa kumutambua Mungu, kama kwa hekalu takatifu, vyombo takatifu na kwa vitu vingine takatifu*:* makumbusho milele!

Kwa wale wanajua ya kama bakora ya Haruni na mbao ya Amri, Sanduku ya Agano na Kinara, meza na chetazo vilitangulia kueleza na kuonyesha Maria Mzazi-Mungu na Bikira Mtakatifu kam;ili; ya kama hivi vitu vilitangulia kumuonyesha mbele hajakua hivi, ya kama alikuwa binti na kukaa bikira kisha kuzaa Mungu; kwa wale ambao sababu ya hii wanataka kumuonyesha kama bikira kwa Ikone kuliko kwanza kumuonyesha kwa mifano> Makumbusho milele!

Kwa wale wenyi kujua na kuitikia maono ya manabii kama umungu wenyewe ilitangulia kuyaonyesha; na wanasadiki ile manabii walieleza kisha kuiona; na wanahakikisha mapokeo yenye kuandikiwa wala ya neno Mitume waliwapatia Wapateri takatifu; kwa wale wenye kuonyesha kwa mfano vitu vitakatifu na kuviheshimu*:* makumbusho milele!

Kwa wale wanamusikiliza Musa wakati anasema*:* «Jilindeni ninyi wenyewe! Siku Bwana Mungu alisema juu ya mlima Horebu, mulisikia sauti ya maneno yake, lakini hamukuona umbo hata moja» na wanajua kujibu safi*:* «Kama yungelijua kitu chochote, kama tungeliona kweli alivyotufundisha Mwana wa mungurumo, ile ilikuwa kwa mwanzo ile tulisikia, ile tulitazama, ile tuliona na macho yetu, ile mikono yetu ilipokea kwa Neno la uzima, na tunashuhia n;a vilevile kama Wafuasi wengine wa Neno*:* »Tulikula na kunywa pamoja naye, apana paka mbele ya mateso yake, lakini tena kisha Mateso na Ufufuo»; kwa wale, ninasema, wenye kupokea kwa Mungu ufahamu wa kutambua mafundisho yenyi kuwa katika sheria na mafundisho neema inatupatia, kutoonekana kwa Mungu mbele, tabia yake yenyi kuonekana wazi kisha; kwa wale ambao kwa hii sababu wanaonyesha ile tuliweza kuona na kugusa waakti tunatukuza Ikone*:* Makumbusho milele!

Kwa Manabii walivyomuona, kama Mitume walivyomutangaza, kama Eklezya ilivyomupokea kama Waalimu walivyomufundisha, kama ulimwengu ilivyomufaa, kama neema ilivyoangaa, kama ukweli ilivyoonyeshwa na uwongo kukataliwa, kama hekima ilivyojaribu kumueleza, kama Kristu alivyoitangaza hivi tunaweza, hivi tunasema, hivi tunahubiri, tunamutukuza Kristu Mungu wetu kweli na Watakatifu wake kwa maneno yetu, kwa maandiko yetu, kwa mawazo yetu, kwa sadaka zetu, kwa mahekalu yetu na kwa maikone yetu, tunasujudu na mapendo mbele ya mumoja kama Mungu na Bwana, tunatukuza wengine sababu ya Rabi moja ambao wao ni watumishi, na kuwapa alama ya ibada yenye kuwastahili.

Hii ni imani ya Mitume, hii ni imani ya wapateri, hii ni imani ya Wakristu, sababu ya utukufu na heshima ya imani walishindania, na tunasema*:*

Kwa Germanos, Tarasios, Nikiforos na Methodios, Waongozi wa kweli wa Mungu, Washindaji na waalimu wa Uorthodoksi*:* Makumbusho milele!

Kwa Ignatios, Fotios, Stefanos, Antonios na Nikolaos, Mapatriarkhi Watakatifu Orthodoksi*:* Makumbusho milele!

Kwa maandiko yote na maneno yote mbaya juu ya Mapatriarkhi Watakatifu Germanos, Tarasios, Nikiforos na Methodios, Ignatios, Fotios, Stefanos, Antonios na Nikolaos*:* Yalaamiwe.

Kwa mambo yote mapya, ya zamani ao yatakayokuja, yenye kushindana na mapokeo ya Eklezya, na mafundisho, na kanuni za Wapateri Watukufu*:* Yalaaniwe.

Kwa Shahidi Mkubwa na Muungamizi Stefanos kijana*:* makumbusho milele!

Kwa waungamizi Watukufu na Markiaskofu Efthimios, Theofilos na Emilianos*:* makumbusho milele!

Kwa Wamitropoliti wenye heri Petros, Mikaeli na Yosefu*:* makumbusho milele!

Kwa Waungamizi mara tatu wenye heri na Markieaskofu Yoane, Nikola na Georgie, na kwa maaskofu wote waliokubali wazo lao*:* makumbusho milele!

Kwa Theodoros, Igumeni mtukufu wa Studioni*:* Makumbusho milele!.

Kwa Isaaki mwenyi kufanya miujiza na kwa Yoakimu mwenyi kujaa na roho ya unabii*:* Makumbusho milele!

Kwa Ilarioni arkimandriti mtukufu tena Igumeni wa Dalmato*:* makumbusho milele!

Kwa Simeoni Mtawa mtukufu*:* Makumbusho milele!

Kwa Theofani, Igumeni mtukufu wa Shamba-kubwa*:* Makumbusho milelel!

Kwa Watangamizi wote wa ikweli*:* makumbusho milele!

Kama vile hii baraka zote za Wapateri zinatushukia sisi wana wao wenye kutaka ibada yao, vivyo ;aana iwafikie wauaji wa wazazi wao na wale wenye kuzarau mafundisho ya Bwana; ndio maana wote pamoja kwa ukamilifu wa imani tunawatupia laana ambayo wao wenyewe walitamainia kupata*:*

Kwa wale wanaitikia kwa maneno kuja mwilini kwa neno-Mungu lakaini wanakataa kumutazama katika maikone, halafu wanamupokea paka kwa elimu tupu, lakini wanakana imani yetu*:* Walaaniwe!

Kwa wale wenye kuambatana na wazo la muovu na kwa hii sababu hawataki sura ya Kristu Mungu wetu kweli ionyeshwe, yeye aliyetwaa mwili wetu na damu yetu, na kwa hii wanaonekana kuwa vidudu-watu. Walaaniwe!

Kwa wale wenyi kukubali kwa kuitaka ao bila kutaka, maono ya manabii lakini hawaitikie sura waliona, ni ajabu, mbele ya umwilisho wenyewe wa neno, lakini wanahadisia ya kama ni hali moja isiyoweza kutambulikana na isiyoonekana machoni mwa watu, ao ya kama ni sura za ukweli zilionekana kwa watu, lakini hawavumilie Neno aliyejifanya mtu aonyeshwe na mateso aliteswa kwa ajili yetu*:* Walaaniwe!

Kwa wale wanasikiliza neno la Bwana akisema*:* «Kama mulimuamini Musa, muniamini na mimi pia. . . » na wanasikia lile la Musa akisema*:* «Bwana Mungu atawaletea ninyi toka ndugu zanu Nabii mumoja kama mimi», kisha wanasema wanaitikia Nabii lakini hawaingize katika Maikone neema ya Nabii na wokovu wa dunia yote, kama alivyoonekana na kuzungumuza na wanadamu alivyoponyesha mateso na magonjwa, alivyosulubiwa, alivyopikwa na kufufuka yote ile alifanya na kuvumilia kwa ajili yetu; kwa wale basi hawaitikie kuona katika maikone matendo yake juu ya wokovu wa dunia na hawataki ao kuiheshimu ao kusujudu mbele yao*:* Walaaniwe!

Kwa wale wenye kudumu katika uhalifu wa Ikone, ao kwa kumukufuru Kristu na hawataki ao kuufikia wokovu katika imani ya Ikone, ao kurudia katika imani kwa njia ya mafundisho ya Mitume, ao kuacha makosa yao kwa njia ya mashauri ya Wapateri, ao hawahangaishwe kwa umoja wa Maeklezya ya Mungu yenye kutawanyika ulimwenguni, lakini wanatii kabisa mambo ya Wayuda na ya Wapagani*:* Kwa sababu hawasikii haya ya kusubutu kukufuru, katika Ikone yake, huyu ekwapo na sura yake, makufuru ambayo hawa wanakufuru nayo mfano wa kwanza! Kwa wale basi wanadamu katika hii kosa bila kutubu na wanafunga masikio yao kwa mashindani kimungu na kwa mafundisho ya kiroho; na ambao, kama watu wamekwisha kuoza, wanajitenga wao wenyewe toka mwili wa Eklezya*:* Walaaniwe!

Kwa ile yenyi kujitaja kuwa Sinodi iliyokufuru Ma Ikone Takatifu*:* Ilaaniwe!

Kwa wale wenyi kutaja Maikone takatifu ya Kristu Mungu wetu na ya watakatifu wake kuwa sanamu, kama inavyosema Maandiko Takatifu*:* Walaaniwe!

Kwa wenyi kuungana na wale wenye kutukana na kuzarau Maikone takatifu*:* Walaaniwe!

Kwa wale wenyi kusema ya kama inje ya Kristu Mungu wetu kuna Mungu mwingine alituokoa toka udanganyifu wa sanamu*:* Walaaniwe!

Kwa wale ambao wanaposubutu kusema ya kama Eklezya katholika imekwisha kukubali sanamu, wanaharibu yote ile iliyo takatifu na wanazarau imani ya Wakristu*:* Walaaniwe!

Kama mumoja hakiri ya kama Kristu Mungu wetu alitahiriwa mwilini mwake na hawamwabudu katik;a Sura yake*:* Alaaniwe!

Kwa Konstantino na Eleni mama yake na kwa Wafalme wetu wote waaminifu Orthodoksi waliyogeuza ufalme wa dunia kufanya kuwa ufalme wa mbinguni*:* Makumbusho milele!

Kwa Mikaeli mfalme wetu Orthodoksi na mama yake Theodora malkia wetu mwenye kulindwa na Mungu tena mwenye heri aliyerudisha Uorthodoksi na kuheshimu Maikone takatifu*:* makumbusho milele!

Utatu Mtakatifu iliwatukuza.

Tunamuomba Mungu ili tufundishwe kwa mafundisho yao na kusabitishwa kwa mashindano walishindana mpaka kufa kwao kwa ajili ya imani, na tunamusihi atufanye mpaka mwisho kuwa Wafuasi wa uzima yao takatifu, tustahili ile tunaomba kwa rehema na neema ya Mwongozi wetu mkubwa wa kwanza, Kristu Mungu wetu kweli, kwa maombezi ya Maria Bibi yetu Mtukufu Mzazi-Mungu na Bikira daima, ya malaika Watakatifu na ya Watakatifu wote. Amina.

Kama itaisha kuzuguluka mara moja pembeni ya Kanisa tunarudia mu Kanisa na katikati yake tunaimba mara tatu: Nani aliye Mungu mukubwa kama Mungu? Wewe ni Mungu anayefanya maajabu;
Kisha Padri atasema: Kwa maombezi ya Watakatifu Wapadri wetu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

SIKU YA ORTHODOKSIA KWA MANGARIBI.

Elezo*; Tunaimba wimbo 10, nikusema 4 ya Paraklitiki (Tafuta ku mwisho ya hii Kitabu, mu sauti ya hii Juma), 3 ya hii Kitabu na 3 ya Mineon.*

Sauti ya ine. Edokas simiosin.

Ee Mfalme Mtakatifu wa ulimwengu, kwa roho yangu yenye kuzama katika zimu ya tamaa na kutengana na wewe bila matumaini, uipatie sikitiko na uitenge mbali ya uovu kusudi nipate haki na ukamilifu, uniokoe mimi muovu kwa rehema yako kubwa, ee Bwana Mwenyezi na Mwokozi wa roho zetu.

Musa Nabii Mtakatifu, kwa kufunga aliona huyu alitamainia; na wewe roho yangu maskini ujiharikishe kufanana naye, kwa hii wakati wa kufunga ujitakase toka uovu wote kusudi uone pia Bwana mwenye kukusamehe*:* Yeye ni Mwema na Mpenda-wanadamu, Bwana Mwenyezi.

Sauti ya sita. Arkhagelikos animnisomen.

Tuangazeni na furaha hii juma ya mbili ya Kwarezima, tuzoee, ee ndugu zangu, siku kwa siku, kama Nabii Elia wa Thesvitis*:* Fazila ine za asili ziwe gari yetu ya moto! Tuinueni akili yetu kwa kukataa tamaa, kwa utakaso tushindane juu ya mwili kusudi tufukuze na kushinda adui.

Wimbo tatu ya Kitabu Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION** ya Mineon.

KUINGIA.

Mwangaza upole. . .

Mangaribi Prokimenon*:*

Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

Shairi*:* 1)Toka mwisho wa dunia nitakuita.
Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

Shairi: 2)Nitakimbilia maficho ya mabawa yako.

Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

APOSTIKHA.

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Kujeni, tujitakaseni kwa kugawanya na maskini, bila kutangaza sadaka zetu na mema yetu; mkono wa kushoto isijue ile inafanya mkono wetu wa kuume kusudi sifa ya bure isitunyanganye tunda! Lakini kwa siri tumwambie huyu mwenye kujua siri zetu*:* Ee Baba, utusamehe makosa yetu, kwa wema wako kwa ajili ya wanadamu.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Enyi ma Shahidi wa Bwana wenye kutakasa ulimwengu na kuponyesha magonjwa yote, mutuombee sasa kwa ajili ya kuokoa roho zetu toka mtego ya adui.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mama usiyeolewa, mbingu inaimba neema yako, na sisi tunatukuza kuzaa kwako isiyokadirika, ee Mzazi-Mungu, ombea aokoe ma roho zetu.

MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA MBILI.

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.

Ee Kristu, kwa kufunga na toba leta uzima kwa roho yangu yenyi kuuawa kwa tunda lililokatazwa na unipe nitembee daima katika njia sawa ya amri zako takatifu kusudi nikifurahi na utukufu wa Mungu pamoja na wale wenye kukupenda nitukuze, ee Yesu, wema wako kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira, ninapotikiswa kwa mawimbi ya tamaa, nakuomba daima. Usiniache bila kunisaidia, wewe uliyezaa Bwana wa rehema kubwa; sina matumaini ingine ila wewe, usiache shetani kuchekelea matumaini yangu; wewe uko na uwezo wote kama Mzazi-Mungu.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya sita. Kirie eleison imas.

Ee Bwana, utuongoze katika hii juma ya mbili ya Kwarezima, utuangazie sisi na nuru ya amri zako na utustahilishe wakati tunapiga magoti kukutolea ombi lenye kukubaliwa; Maana wewe ni Baba yetu na sisi ni waana wako, tunakutukuza wa woga, Jina lako linakaa juu yetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Mwanzo wa wokovu wetu ni habari njema ya malaika Gabrieli kwa Maria; Wakati Malaika alimutokea, hakukataa kupokea salamu; hakusita kama Sara katika hema, lakini alisema*:* Tazama mimi ni mutumishi wa Bwana, ifanyike kwangu kama ulivyosema.

Tunasoma Zaburi 50 (51).

KANUNI.

Sauti ya ine. Tristatas krateus.

Wema moja, Chemchem ya rehema , Mwana-kondoo wa Mungu anayeondoa zambi za dunia, uniokoe toka maangamizi ya zambi na uniongoze mpaka kwa bandari ya toba.

Kwarezima ya kweli ni ile yenyi kututenga mbali na zambi, yenyi kutuachiza tamaa*:* Ni mapendo ya Mungu ni nguvu katika maombi, ni machozi ya sikitiko, ni tunzo ya maskini, kama Kristu anavyoifundisha katika Maandiko Matakatifu.

Ee Nganga wa roho zetu tena Mpenda-wanadamu, weka dawa ya wema wa amri zako za hekima juu ya roho yangu yenyi kujeruhiwa kwa upanga wa zambi na kuchafuliwa na maovu mengi.

THEOTOKION

Ee Bikira Mtakatifu, makao takatifu kamili, ondoa roho yangu toka tamaa zenye kuishambulia, ee Bibi yetu, uitakase kwa chemchem ya rehema yako, na mvua ya sikitiko ijaze zimu ya zambi zangu.

Sauti ya sita. Voithos ke skepastis.

Kisha siku Kuu iliyotufurahisha tupokee pia na mapendo hii juma ya mbili ya Kwarezima ya nuru na tutukuzeni Kristu katika furaha na sherehe ya Mungu.

Tazama Kwarezima, na wakati wa toba; tulie na kuomboleza, tuinue mikono yetu kwa Mkombozi peke yake kusudi aokoe roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Mungu mumoja katika watu tatu, ubwana wa wote, mwanzo na mwisho wa vitu vyote, wewe mwenyewe utuokoe, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Mtoto gani alizaliwa bila mbegu ya baba? Ni huyu Baba alizaa bila mama. Ni mambo ya ajabu*:* Bikira anazaa Mungu-mutu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Namna gani nitavumilia hasira yako, ee Kristu, wakati utakapokuja kunihukumu? Jibu gani nitakupa mimi sikufanya mapenzi yako? Ee Kristu, mbele ya mwisho, uhihurumie.

IRMOS. Bwana ni msaada na ulinzi wangu, ni yeye aliniokoa; yeye ni Mungu wangu na nataka kumutukuza, yeye ni Mungu wa Baba yangu, nitamutukuza, maana amevaa utukufu.

APOSTIKHA.

Sauti ya tano. Idiomelon.

Ni ya ajabu kweli, silaha ya maombi na ya kufunga! Kwa Musa iliandikisha Sheria na kwa sadaka ikawakisha bidii ya Elia. Tukiitenda na sabiti tutamulalamikia Mwokozi, tulikukosea wewe peke yako, utuhurumie.

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Litukuzwe jeshi la Mfalme wa mbinguni! Kwani walipozaliwa duniani, ma Shahidi Washindaji hawakutumainia cheo cha Malaika*:* Walipozarau mwili, na kuteswa kwa mateso yao, wanastahili utukufu wa Malaika; kwa maombezi yao, okoa roho zetu, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira mtukufu, tunakuomba kama Mzazi-Mungu, ombea roho zetu wokovu.

MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA MBILI.

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo 3 ya hii Kitabu na 3 ya Mineon.

Sauti ya mnane. Ti imas kalesomen.

Nitakufananisha na nani, ee roho yangu zaifu, wewe ambaye bila kutenda mema unavumilia kuishi katika zambi? Tubu, hukumu ni kwa mwanzo; kwa maombi na kufunga ujitakase na umwambie Bwana; Nimekosa juu yako, kwa wema wako uniondolee na kunisamehe makosa yangu.

Ee bahari ya wema isiyoweza kufumbuliwa, kausha bahari ya giza ya zambi zangu, ee Kristu, Mungu safi, tena uipe roho yangu toba sababu ya kupoteza njia ya mito ya uovu kusudi niimbe na kutukuza mapendo yako isiyokadirika, ee Bwana mvumilivu na mfazila wa roho zetu.

Sauti umoja. *O en Edem Paradisos.*

Ee Mungu ambaye sasa unatuleta tena kwa hii kipindi cha Kwarezima na kutupa sisi kuingia katika juma ya mbili, ongoza, ee Bwana, mwendo wetu mpaka mwisho nzuri, jaza roho zetu na miili yetu na neema na nguvu kusudi ku mwisho wa hii mwendo tuitangulie siku kubwa ya Ufufuo wako takatifu na wote tupate taji sababu ya kukutukuza daima kwa furaha.

Wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Mangaribi Prokimenon. Sauti ya kwanza. Zaburi 23(24).
Bwana mwenye nguvu na uwezo, Bwana mwenye uwezo vitani.

Shairi*:* Inchi na kujaa kwake ni mali ya Bwana.

Somo ya Mwanzo tutasoma (3, 21- 4, 7).

Bwana Mungu akafanyia Adamu na muke wake mavazi ya ngozi, akawavalisha. 22 Bwana Mungu akasema*:* Tazama, mutu amekuwa kama mumoja wetu, kwa kujua uzuri na ubaya; na sasa, isiwe anyoshe mukono wake na kutwaa vile wa muti wa uzima na kula na kuishi milele; kwa hivi Bwana Mungu akamutoa toka shamba la Edeni, alime udongo pale alipotwaliwa. Hivi akafukuza mutu akaweka Makerubi kwa mashariki ya shamba la Edeni na upanga wa ulimi wa moto uliogeuka pande zote kuchunga njia ya muti wa uzima. Mwanamume alijua Hawa muke wake; akachukua mimba, akazaa Kaina, akasema*:* Nimepata mume kwa bwana. Akazaa tena ndugu yake Abeli. Na Abeli alikuwa muchungaji kondoo, lakini Kaina alikuwa mulimaji udongo. Siku zilipopita, Kaina akapeleka ya matunda ya udongo kwa bwana. Na Abeli, yeye vilevile alipeleka wa wazao wa kwanza wa kundi lake na ya mafuta yake. Bwana akaheshimu Abeli na zabihu yake, lakini hakuheshimu Kaina na zabibu yake. Kaina akakasirika sana, uso wake akakunjamana. Bwana akamwambia Kaina*:* Kwa nini unakasirika? Na kwa nini uzo wako unakunjamama? Kama ukitenda vema, hutakubaliwa? Na kama hutendi vema, zambi inakaa kwa mulango wako na inakutamani wewe, lakini sharti uishinde.

Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 24 (25).
Geuka kwangu, na kunihurumia.
Shairi*:* Kwako, ee Bwana, ninanyanyua nafsi yangu.

Somo ya Mezali tutasoma. (3, 34- 4, 22).

Hakika anazarau wenye kuzarau, lakini anawapa wanyenyekevu neema. Wenye hekima watariti utukufu; Lakini haya itakuwa kukuzwa kwa wapumbafu. Sikia, wana wangu, mafundisho ya baba, na tegeni masikio kujua ufahamu*:* Maana ninawapa ninyi mafundisho mazuri; Musiache sheria yangu. Maana nimekuwa mwana kwa baba yangu, mupole, mupenzi pekee wa mama yangu. Naye alinifundisha, akaniambia*:* Moyo wako ukumbuke maneno yangu; Shika maagizo yangu na inshi*:* Pata hekima, pata ufahamu; Usisahau, wala usikatae maneno ya kinywa changu*:* Usimwache, naye atakulinda; Umupende, naye atakuchunga. Hekima na kitu cha kwanza; basi ujipatie hekima*:* Ndiyo, pamoja na yote uliyopata pata ufahamu. Umutukuze, naye atakukuza*:* Atakupatia heshima, wakati unapomukumbatia. Atakupa neema kuwa kilemba kichwani*:* Taji ya utukufu atakupa. Sikia, ee mwana wangu, na pokea maneno yangu; na miaka ya maisha yako itakuwa mingi. Nimekufundisha katika njia ya hekima; Nimekuongoza katika mapito ya haki. Wakati unapokwenda, hatua zako hazitazikishwa; na kama ukikimbia hutakwaa. Ukamatane na elimu; uzimwache kwenda zake; Umushike, maana yeye ni uzima wako, usiingie katika mapito ya waovu, wala usitembee katika njia ya watu wabaya. Ujiepushe nayo wala usipite karibu nayo; Geuka mbali nayo, na kwenda zako. Maana hawalali, ila wamekwisha kutenda mabaya*:* Na usingizi wao unaondolewa isipokuwa wameangusha mutu. Maana wanakula chakula cha uovu, na kunywa mvinyo ya jeuri. Lakini mapito ya wenye haki ni kama nuru inayongaa inayozidi kungaa hata muchana mukamilifu. Njia ya waovu ni kama giza; Hawajui ni kitu gani kinachowakwaza. Mwana wangu, sikia maneno yangu; tega sikio lako kwa misemo yangu. Yasiondoke kwa macho yako; Uyashike ndani ya moyo wako. Maana ni uzima kwao wanaoyalinda na afya kwa mwili wao wote.

APOSTIKHA.

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Tufunge na Kwarezima ya kiroho, tuache unafiki wote, tukimbie pia mitego ya zambi, tuwasamehe ndugu zetu makosa yao ili na sisi pia tusamehewe makosa yetu, ni hivi tutaweza kuimba*:* Maombi yetu yaelekezwe kama uvumba mbele yako, ee Bwana Mungu wetu.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala. . . *(ona yulu).*

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na. . .

Sauti umoja.

Ma Nabii, Mitume wa Kristu na ma Shahidi walitufundisha kuimbia Utatu wa asili moja, walileta nuru ya Ubatizo kwa mayaifa yenye kupotea*:* Malaika na wanadamu wanakuwa sawasawa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bibi yetu, usisahau maskini mpaka mwisho, ndiyo maana kwa maombezi yako utuokoe toka hatari yenye kutushambulia na toka hukumu itakuja sasa; ee Mzazi-Mungu, ondoa watumishi wako toka hasira ya Bwana.

MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA MBILI.

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya mnane. Anestis ek nekron.

Tunapozuia tamaa zetu kwa kizuio cha Kwarezima takatifu tujikaze kufikia mawazo ya kimungu kwa ukamilifu wa imani yetu ili tukizarau furaha ya hii uzima tupate uzima wa mbinguni na nuru ya Mungu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Nimeanguka katika zimu la ajabu la kutotumaini, na kwa ajili ya matendo yangu mbaya nimehangaika, sasa nimeshikwa kwa shaka na sikitiko. Ee Mzazi-Mungu na Bibi yetu, kuja unisaidie na kuniokoa, maana wewe ni msaada na wokovu wa waovu.

KATHISMA WA TATU.

Sauti umoja. *Anestis ek nekron.*

Kwarezima inatutolea karamu ya siri na inatualika kuishota kama chakula tukamate zawadi za milele za Roho Mtakatifu, na kama kinywaji tulie machozi ya sikitiko tukimutolea Mungu na furaha sifa yetu ya milele.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu kamili, utuokoe toka uovu wote na hatari yote, kwani wewe ni boma na ulinzi wa wale wenye kukukimbilia wewe pamoja na Mungu aliyezaliwa tumboni mwako; umuombe aokoe roho zetu toka hatari na mateso yote.

APOSTIKHA.

Sauti ya tano. Idiomelon.

Ee Roho maskini na zaifu, sababu gani uko mtumwa wa zambi, sababu gani, kwa uzaifu wako, hawende kwa mganga? Tazama wakati nzuri, tazama siku ya wokovu; amka, nawisha uso wako kwa machozi ya sikitiko, shika taa yako yenye kuwaka na mafuta ya fazila sababu ya kupata kwa Kristu Mungu wetu maondoleo ya zambi na neema ya wokovu. .

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Ee Bwana waliposhinda mashindano yao, washindani wa malaika wa wabila mwili, waliteswa; kwa ajili ya matumaini moja walipata mema ya ahadi*:* Kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira, Mzazi-Mungu, mji imara, boma isiyoweza kuharibiwa, mulinzi hadari tena makimbilio ya roho zetu, sisi waaminifu wako tunakutukuza, katika wanawake wote tunakutaja mwenye heri.

MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA WA MBILI

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo 3 ya hii Kitabu na 3 ya Mineon.

Sauti ya kwanza Panefimi Martires.

Ee Kristu Msalabani ulipanua mikono yako takatifu, sababu ya kuunganisha mipaka ya ulimwengu; ndiyo maana nakulalamika*:* Leta umoja kwa akili yangu yenye kutawanyika, samehe roho yangu yenye kuvutwa kwa tamaa, unipe nisharikie mateso yako, kwa kufunga uniatakase mimi wote.

Imeandikwa hivi*:* Zamani vijana waliposabitishwa kwa kufunga wakashinda moto ya tanuru; na wewe roho yangu maskini funga pia, ongeza mapendo yako kwa Bwana sababu ya kuepuka gehena, ukichoma tamaa zako mbaya.

Sauti ya tatu. Genei Martires

Tuonjeni furaha ya hii wakati wa Kwarezima iangae kwa usafi na kwa mapendo ya kweli, katika nuru ya maombi na wingi wa fazila zote! Kwa furaha tutaimba*:* Ee Msalaba takatifu kamili wa Kristu uliyestawisha tunda tamu la uzima, utupe roho safi ili tukuabudu kama inavyostahili, ukitupatia toba na neema ya wokovu.

Na wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Mangaribi (Esperas)Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 27.
Ee Bwana, okoa watu wako na ubariki uriti wako.
Shairi*:* Nitakuita wewe, ee Mungu wangu.

Somo ya Mwanzo tutasoma. (4, 8-15)

Kaina akasemezana na Abeli, ndugu yake. Na ilikuwa wakati walipokuwa shambani, Kaina akasimama juu ya ndugu yake Abeli, akamwua. Bwana akamwambia Kaina*:* Abali, ndugu yako ni wapi? Akasema*:* Sijui; mimi ni muchungaji wa ndugu yangu? Akasema*:* Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inalia kwangu kutoka katika inchi. Na sasa umelaaniwa katika inchi, iliyofungua kinywa chake kupokea damu ya ndugu yako kwa mukono wako; wakati utakapolima shamba, halitakupa tena nguvu yake; utakuwa mukimbizi na mwenye kutangatanga duniani. Kaina akamwambia Bwana*:* Azabu yangu inanipita kuichukua. Tazama, umenifukuza leo katika uso wa inchi na mbele ya uso wako nitafichwa, nitakuwa mukimbizi na mwenye kutangatanga inchini, na itakuwa kila mutu atakayeniona ataniua. Bwana akamwambia Kaina*:* Mutu gani atakayeua Kaina, atalipizwa kisasi mara saba. Bwana akaweka alama kwa kaina hata mutu akimwona, asimupige.

Prokimenon. Sauti ya saba. Zaburi 28.
Bwana atawapa watu wake nguvu.
Shairi*:* Mumupe Bwana ninyi wana wa wenyi amri.

Somo ya Mezali tutasoma (5, 1-15)

Mwana wangu, sikia hekima yangu; Tega sikio lako usikie ufahamu wangu*:* Ili upate kulinda akili njema, na midomo yako ishike maarifa. Maana midomo ya mwanamuke mugeni inaangusha asali, na kinywa chake ni laini kuliko mafuta*:* Lakini mwisho wake ni muchungu kama pakanga, mukali kama upanga wa makali mawili. Miguu yake inashuka kwa mauti; Hatua zake zinashikamana na Hadeze; hata asiweze kuona njia sawa ya uzima*:* Njia zake zinatangatanga, naye hajui. Basi kwa hivi, wana wangu, munisikilize, na musiache maneno ya kinywa changu. Ondosha njia yako mbali naye. Wala usikaribia mulango wa nyumba yake*:* Usiwape wengine heshima yako, na wenye jeuri miaka yako*:* Wageni wasishibishwe na nguvu yako; na kazi zako zisiwe nyumbani mwa mugeni; nawe ukaziomboleza kwa siku zako za mwisho, wakati nyama yako na mwili wako itakapoharibiwa, na kusema*:* Kweli nimechukia mafundisho, na moyo wangu umezarau maonyo; wala sikutii sauti ya walimu wangu, wala kutegea wale walionifundisha sikio langu! Nilikuwa karibu na kuingia katika maovu yote, katikati ya makutano na kusanyiko. Kunywa maji ya birika lako mwenyewe, na maji ya kupita upesi toka kisima chako mwenyewe.

APOSTIKHA

Sauti ya tatu

Ee Bwana, wakati uliposulubiwa mwilini, ulisulubisha mutu wetu wa zamani pamoja nawe, na wakati mkuki ilichoma ubavu wako, ikafikia mara moja adui wetu nyoka; toboa mwili wangu na misumari ya woga wako tena umiza roho yangu na mapendo yako kusudi nikitazama Mateso yako, nifunge vema, nishinde apana paka tamaa yangu, lakini tena kisa zingine za uovu; nakutolea toba ya moyo wangu na unyenyekevu wa roho yangu; hivi nitatengeneza makosa yangu ya zamni*:* uniokoe kwa mapendo yako kwa wanadamu. *(mara mbili)*

Wimbo ya Mashahidi (Martirikon)

Manabii, Mitume ya Kristu na Mashahidi walitufundisha kuimbia Utatu wa asili moja; walitangaza nuru ya Ubatizo kwa mataifa yenye kupotea: Malaika na Wanadamu wanakuwa pamoja.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu, ulipoona Mwana wako ametundikwa Msalabani, ukalia na kupaza sauti*:* Ole wangu, ee mwanangu mpendwa, imeenda wapi uzuri uliyopamba nayo ulimwengu wa wanadamu.

MU KAZI TATU ASUBUI KWA ORTHROS

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir

Ee Kristu ulipokufa msalabani, uliua nyoka adui, uliwapa uzima wale waliyouawa kwa vidonda vya Muovu; ndiyo maana makuomba, ee Mwokozi, leta uzima kwa roho yangu yenye kuuawa yenyi kukutazama wewe kwa maombi na sala.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **STAYROTHEOTOKION**

Ee Kristu, wakati kondoo jike alipoona Mwanza-kondoo wake ametundikwa msalabani katikati ya wanyanganyi, akalia kwa uchungu na kupaza sauti*:* Hii ni ndoto gani, ee Mwanangu

mpendwa! Wewe ukamilifu*:* Ee Mama Mtakatifu kamili, hii ndoto itafunua uzima wa ulimwengu.

KATHISMA WA TATU

Sauti ya tatu. Tin oreotita.

Kwa sauti kubwa ya nyimbo zetu tutukuzeni hii siku ya leo yenye kubarikiwa, tupitishe wakati wa Kwarezima tukisema*:* Hii siku inastawisha Uzima wa ulimwengu, inafifisha maneno mengi na mauti; kwa uwezo wa Msalaba wako takaitfu, ee Kristu tena Neno, chunga watumishi wako katika amani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**

Ee Mungu wa mapendo, kwa kusulubiwa kwako uliitika matusi ya mauti; alipoona hivi, ee Kristu, moyo wa Mama yako ikajeruhiwa, kama mama akalia; kwa rehema yako na kwa maombezi yake, wewe unayeondoa zambi za dunia, umuhurumie na utuokoe.

IRMOS (*Kisha wimbo wa tatu).*

Ee Bwana, sabitisha roho zetu kwa mapendo yako na utupe nuru yako sababu ya kukuimbia na kukutukuza, ee Mwokozi milele na milele.

IRMOS *Kisha wimbo wa tisa.*

Musa alikutambua juu ya mlima Sinai katika kichaka cha moto wewe ambaye bila kuteketezwa ulizaa tumboni mwako moto ya umungu; Danieli alikuona kama mlima takatifu Isaya tawi la fumbo lililochamka juu ya shina la Daudi.

Elezo*: Fotagogikon tafuta ku mwisho ya hii Kitabu na sauti ya hii Juma.*

APOSTIKHA

Sauti ya saba

Ee Bwana, kwa Msalaba wako, uliharibu mauti iliyoingia duniani kwa tunda lililiwa katika Paradizo la muti iliyokataziwa; kwa hii Kwarezima utuopoe toka furaha yote ya hatari, utupe sisi tutumike juu ya chakula cha uzima wa milele kusudi tupate taji ya heri ya milele uliyowatayarishia wale wanafunga kweli. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi (martirikon)

Mashahidi Watakatifu waliyotukuzwa kwa ushindi wao katika mashindano wamekuwa taa za kuangazia ulimwengu wote; wanamwambia Kristu*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAYROTHEOTOKION**.

Wakati Bikira Mtakatifu kamili alipokuona Msalabani umesulubiwa kwa kutaka kwake, akaimba akilalamika*:* Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana!

MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA WA MBILI

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo kumi; wa sita ya hii inafwata na wa inne ya Mineon.

Sauti ya kwanza. Idiomelon.

Enyi ndugu, tukifunga katika roho ulimi wetu isidanganye! Tusiwe kikwazokwa ndugu yetu, lakini kwa toba tuangaze taa ya roho yetu, na kwa machozi tumuombe Kristu*:* Utusamehe makosa yetu kwa wema wako kwa ajili ya wanadamu*(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi (Martirikon)

Enyi Mashahidi wenye kustahili utukufu yote, haiko udongo iliwaficha ninyi, ni mbingu iliwapokea ninyi; milango ya Paradiso yalifunguliwa kwa ajili yenu na huko munakuwa na muti wa uzima; ombeni kwa Kristu alete amani yake na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Sauti ya tatu. Megali ton Martiron su.

Ee Bwana, kwa maombezi ya Mitume Watakatifu, utupe tutimeze hii Kwarezima kama inavyostahili, weka toba moyoni mwetu kusudi, wote tukiokolewa, tuimbie rehema yako, utukufu wako na wema wako.

Ee Bwana, kuja kwako ni kubwa tena ni kwa ajabu wakati utakapoketi kutoa hukumu ya kweli! Usinihukumu, nimekwisha kuhukumiwa, unifazili, pokea maombezi ya Mitume wako.

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Enyi Mitume wa Kristu, ninyi taa za wanadamu, hazima ya hekima takatifu ya Mungu wetu, kwa maombezi yenu okoeni toka majaribu wote wale wenyi kuwatukuza ninyi; ongozeni vema hii Kwarezima, tunapoinua macho kwa Mateso ya Kristu, tunamutolea utukufu yenyi kumustahili Mungu wetu.

Sasa tunaimba wimbo inne ya Mineon

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION** ya Mineon.

Mangaribi (Esperas). Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 31, .
Mufurahi ndani ya Bwana, na mushangilie, ninyi wenye haki.
Shairi*:* Heri yeye aliyesamehewa nmakosa yake.

Somo ya Mwanzo tutasoma (4, 16-26)

Kaina akatoka usoni mwa Bwana, akakaa inchini mwa Nodi, kwa upande wa mashariki wa deni. Kaina akajua mwanamuke wake; akapata mimba, akazaa Enoka; akajenga muji, akaita jinala muji nyuma ya jina la mwana wake, Enoka. Kwa Enoka Iradi akazaliwa; Iradi akazaa Mehuyaeli; Mehuyaeli akazaa Metusaeli ; Metusaeli akazaa Lameki. Lameki akajitwalia wakewawili; jina la mumoja lilikuwa Ada, na jina la pili Sila. Ada akazaa Yabali ; allkuwa baba ya wenye kukaa hemani, wenye ngombe. Jina la ndugu yake lilikuwa Yubali; alikuwa baba ya wote wanaopiga kinubi na filimbi. Na Sila, yeye vilevile akazaa Tubali-Kaina mufua wa chuma wa kila kitu cha kukata, cha shaba na cha chuma. Na ndugu muke wa Tubali-Kaina alikuwa Nama. Lameki akawaambia wanawake wake wawili*:* Ada na Sila, sikieni sauti yangu, ninyi wanawake wa Lameki, sikilizeni usemi wadgu; kwani nimeua mutu kwa sababu ya kuniumiza, na kijana kwa sababu ya kuni- ponda; kama Kaina atalipiwa kisasi mara saba, hakikd Lameki mara makumi saba na saba. Adamu akajua mwanamuke wake tena, akazaa mwana, akaita jina lake Seti; kwani akasema*:* Mungu ameniwekea uzao mwingine pahali pa Abeli; kwa sababu Kaina alimwua. Na Seti, kwake vilevile mwana akazaliwa*:* akaita jina lake Enosi ; halafu watu walianza kuitia jina la Bwana.

Prokimenon. *Sauti ya kwanza.* Zaburi 32.
Rehema yako, ee Bwana, iwe juu yetu.
Shairi*:* Mufurahi ndani ya Bwana, ee ninyi wenye haki.

Somo ya Mezali tutasoma (5, 15-6, 3)

Kunywa maji ya birika lako mwenyewe, na maji ya ya kupita upesi toka kisima chako mwenyewe. Chemchemi zako zitawanyike mbali, na mito ya maji katika njia kubwa. Yawe yako mwenyewe peke yako, wala si kwa wageni pamoja nawe. Chemchemi yako ibarikiwe; na furahia muke wa ujana wako. Kama ayala anayependa na paa anayependeza; Maziwa yake yakutoshe siku zote; na ushangiulie siku zote kwa mapendo yake. Maana kwa nini wewe, mwana wangu, utashangilia mwanamuke mugeni, na kukumbata kifua cha mugeni? Maana njia za mutu ni mbele ya macho ya Bwana, naye anapima sana mapito yake yote. Maovu yake mwenyewe

yatapata mwovu, naye atashikwa kwa kamba za zambi yake. Atakufa kwa kukosa mafundisho, na katika ukubwa wa upumbafu wake atapotea. Mwana wangu, kama umekuwa zamana kwa jirani yako, kama umepiga mikono yako kwa mugeni, basi umetegwa kwa maneno ya kinywa chako, umekamatwa kwa maneno ya kinywa chako. Sasa fanya hivi, mwana wangu na ujiponyeshe, kwa kuwa umejitia mukononi mwa jirani yako; Kwenda, ujinyenyekeze, na sihi jirani yako.

MU KAZI INNE ASUBUI KWA ORTHROS

Elezo*:Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya tatu. Tin Oreotita.

Enyi Mitume Watakatifu, Kristu aliwachukua ninyi kama mashada tamu ya Mzabibu wa kweli sababu ya kuleta duniani maji ya wokovu; muniopoe toka ulevi wa tamaa, mwangieni roho yangu toba nyingi wakati wa hii Kwarezima takatifu kusudi mipate wokovu na uzima wa milele.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . **THEOTOKION**. *Umoja*

Ninapofikiri juu ya hazina ya milele ya rehema yako na juu ya nguvu isiyoweza kushindwa ya uwezo wako, nakimbilia kwa ulinzi wako, na kwa sikitiko yenyi kutusonga, kwa fazaa ya mawazo yangu ya sikitiko, kwa moyo wangu wote nakulalamikia*:* Kuja unisaidie, ee Mzazi-Mungu, wewe peke yako mwenye kulinda ulimwengu.

KATHISMA YA TATU

Sauti ya sita. Kirie paristato.

Kwa hii wakati wa huruma, utufazilie, ee Bwana, chemsha machozi ya mioyo yetu juu utakaso wa roho zetu zenye kuchafuka na juu ya ustawi wa amri zako takatifu ili kwa kufunga tuweze kukupendeza kweli, na kwa wote tupewe kutazama Mateso yako takatifu kwa maombezi ya Mitume wako Wataaktifu; utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . **THEOTOKION**. *Tis Efsplaknias.*

Ee Bikira Mtakatifu tena Mzazi-Mungu, mwangia katika mioyo yetu, ewe Safi kamili, huruma yako kubwa; utusamehe makosa yetu*:* Wewe ni boma yetu, ulinzi wetu.

IRMOS WA TISA.

Ulipata mimba bila mbegu, kuzaa kwako ni kusiyokadirika, ee Mama usiyeolewa: Mungu anajifanya mtu kwa Bikira na anatengeneza sheria za ulimwengu; kwa imani ya kweli, ee Bikira Mzazi-Mungu, tunakutukuza kizazi na kizazi.

Kisha tunaimba Wimbo ya Mwangaza (Fotagikon) na sauti ya hii Juma.

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Tukinyosha mikono kwa wema wako, wakati wa toba na mashindano ya Kwarezima yanatupa sisi uzima wa milele; juu ya wokovu wa roho hakuna kitu kingine ila kugawanya na maskini; sadaka na kufunga yanatuokoa toka mauti; katika hii tupende hazina kubwa yenye kuweza kulipa wokovu wa roho zetu. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi. Martirikon.

Mulivaa na uhodari kanzu ya imani, kama silaha mulishika alama ya Msalaba, mulionekana kuwa askari washujaa, mulishindanna vema na wazulumu, muliondoa uwongo ya shetani, mulistahili taji ya washindaji*:* Mumuombe Kristu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira Mtakatifu Mzazi-Mungu, nakimbilia kwa ulinzi wako kwa matumaini ya kupata wokovu*:* Ee Bikira safi, uko na uwezo wa kuja kunisaidia.

MU KAZI INNE MANGARIBI YA JUMA YA MBILI

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo sita; tatu ya hii inafwata na tatu ya Mineon.

Sauti ya ine. Edokas simiosin.

Nilipotiishwa mpaka mauti kwa uovu wa nyoka aliyenipa tunda la muti iliyokataziwa, nilionja chemchem ya uzima wa milele wakati askari alichoma ubavu wako kwa mukuki juu ya msalaba huko tulitundikwa; ndiyo maana, ee Kristu, natukuza na naomba huruma yako; unipe nimalize na sikitiko kipindi cha Kwarezima sababu ya kuabudu Mateso yako na Ufufuo wako takatifu.

Ee Mwokozi, ulifukuza mutu wa kwanza toka Paradizo wakati alichuma tunda la muti wa mateso; unamurudisha tena katika Paradizo wakati ulisulubiwa msalabani katika mwili; ndiyo maana nakulalamikia, ee Mkombozi*:* Unitakase kwa kufunga kwa kulia na kwa toba, sababu ya kuniokoa toka mateso yote ee Yesu, hazina ya mema tena Mwokozi wa roho zetu.

Sauti ya tano. Kirie epi Moiseos.

Ee Bwana, tunatukuza, kadiri ya amri ya Muumba, wazazi wetu wa kwanza kwa uasi wao chini ya muti wa mema na mabaya, pahali pa tunda walichuma mauti; ni hivi walipoteza muti wa uzima na furaha ya paradizo; lakini sisi waaminifu tukatae chakula cha mauti na tamaa zetu mbaya kusudi tuchume uzima kwa muti taaktifu wa Msalaba na tuingie pamoja na Munyanganyi katika inchi yetu ya zamani kwa rehema ya Kristu Mungu wetu.

Sasa tunaimba na wimbo ya Mineon tatu.

Utukufu...Sasa na siku zote...**STAYROTHEOTOKION** ya Mineon

Mangaribi (Esperas). Prokimenon. *Sauti ya ine.* Zaburi 35.
Haki yako ni kama milima ya Mungu.
Shairi*:* Wema wako ni wa damani sana, ee Mungu!

Somo ya Mwanzo tutasoma (5, 1-24)

Hiki ni kitabu cha vizazi vya Adamu. Kwa siku Mungu alipoumba mutu; kwa sura ya Mungu alimufanya; aliwaumba mume na muke, akawabariki, akaita jina lao Adamu, kwa siku walipoumbwa. Adamu akaishi miaka mia moja makumi tatu, akazaa mwana kwa sura yake, kwa mufano wake mwenyewe; akaita jina lake Seti; siku za Adamu nyuma ya kuzaa Seti zilikuwa miaka mia nane; akazaa wana na. binti. Na siku zote Adamu alizoishi zilikuwa miaka mia tisa makumi tatu ; akakufa. Seti akaishi miaka mia moja na mitano, akazaa Enosi; Seti akaishi nyuma ya kuzaa Enosi miaka mia nane na saba, akazaa wana na binti; na siku zote za Seti zilikuwa miaka mia tisa kumi na miwili; akakufa. Enosi akaishi miaka makumi tisa, akazaa Kenani; Enosi akaishi nyuma ya kuzaa Kenani miaka mia nane kumi na mitano, akazaa wana na binti; na siku zote za Enosi zilikuwa miaka mia tisa na mitano ; akakufa. Kenani akaishi miaka makumi saba, akazaa Mahalali; Kenani akaishi nyuma ya kuzaa Mahalali miaka mia nane makumi ine; akazaa wana na binti; na siku zote za Kenani zilikuwa mia tisa na kumi; akakufa. Mahalali

akaishi miaka makumi sita na mitano, akazaa Yaredi; Maha-lali akaishi nyuma ya kuzaa Y aredi miaka mia nane makumi tatu ; akazaa wana na binti; na siku zote za Mahalali zilikuwa miaka mia nane makumi tisa na mitano; akakufa. Yaredi akaishi miaka mia moja makumi sita na miwili ; akazaa Enoka. Yaredi akaishi nyuma ya kuzaa Enoka miaka mia nane, akazaa wana na binti; na siku zote za Yaredi zilikuwa miaka mia tisa makumi sita na miwili; akakufa. Enoka akaishi miaka makumi sita na mitano, akazaa Metusela; Enoka akatembea pamoja na Mungu nyuma ya kuzaa Metusela miaka mia tatu; akazaa wana na binti; na siku zote za Enoka zilikuwa miaka mia tatu makumi sita na mitano; Enoka akatembea pamoja na Mungu; kisha hakuonekana kwa sababu Mungu alimutwaa.

Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 36.
Ngojea Bwana, na shika njia yake.
Shairi*:* Usijisumbushe mwenyewe kwa sababu ya watenda mabaya.

Somo ya Mezali tutasoma. (6, 3-20).

Sasa fanya hivi, mwana wangu, na ujiponyeshe, kwa kuwa umejitia mukononi mwa jirani yako; Kwenda, ujinyenyekeze, na sihi jirani yako. Usiache macho yako kupata usingizi, wala kope zako kusinzia. Ujiponyeshe kama paa toka mukono wa muwindaji, na kama ndege toka mukono wa muwindaji ndege. Kwenda kwa siafu, wewe muvivu, fikili njia zake na pata hekima*:* Kwa maana hana akida wala musimamizi wala mutawala, lakini anajiwekea akiba ya chakula kwa wakati wa jua kali, na anakusanya chakula chake kwa wakati wa mavuno. Utalala hata wakati gani, wewe muvivu? Utaamka wakati gani katika usingizi wako? Kulala kidogo, kusinzia kidogo, kukunja mikono kidogo kupata usingizi*:* Hivi umasikini wako utakuja kama munyanganyi, na uhitaji wako kama mutu mwenye silaha. Mutu asiye na faida, mutu mwovu, anatembea njiani mwenye kinywa cha ukaidi, anakonyeza kwa macho yake, na kusema kwa miguu yake, anafanya alama na vidole vyake; Ukaidi ni moyoni mwake, anatunga mabaya daima, anapanda mbegu ya ugomvi. Kwa hivi matata itamupata kwa gafula, atavunjwa kwa gafula, napasipo njia ya kupona. Kuna maneno sita Bwana anayoyachukia; ndiyo saba yaliyo machukizo kwake*:* Macho ya kiburi, ulimi wa kusema uwongo, na mikono inayomwanga damu isiyo na kosa, na moyo unaowaza mawazo mabaya, muguu iliyo mepesi kukimbilia uovu, mushuhuda wa uwongo anayesema uwongo, naye anayepanda mbegu ya fitina kati ya ndugu*:* Mwana wangu, shika maagizo ya baba yako, wala usioache sheria ya mama yako.

APOSTIKHA

Sauti ya tano. Idiomelon.

Walipokosa kufunga kadiri ya amri ya Muumba, wazazi wetu wa kwanza kwa uasi wao chini ya muti wa wema na mabaya, pahali pa tunda walichuma mauti; ni hivi walipoteza muti wa uzima na furaha ya paradizo; lakini sisi waaminifu tukatae chakula cha mauti na tamaa zetu mbaya kusudi tuchume uzima kwa muti takatifu wa Msalaba na tungie pamoja na Munyanganyi katika inchi yetu ya zamani kwa rehema ya Kristu Mungu wetu. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi. (Martirikon).

Enyi Mashahidi Watukufu muliyozarau mema ya hii uzima sababu ya kupambana na mateso, hamukudanganyike kwa matumaini ya heri, lakini kwa uriti mulipokea ufalme wa mbinguni; na sababu muko na uwezo wa kumdai Mungu mwema, mumuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAYROTHEOTOKION**.

Sauti ya tano. Kheris askitikon.

Wakati Bikira asiye na doa alipomuona Mwana-Kondoo amejiharikisha kwenda kuuawa, akamufuata haraka na akamwambia*:* Unaenda wapi, ee Mwanangu mpendwa? Ee Kristu, unamufuata nani kwa hii mwendo bila kukawa? Ee Yesu Bwana mpendwa mwenyi kujaa na

rehema na asiye na zambi, umujibu mtumishi wako, ee Mwanangu mpendwa; kwa kunyamaza kwako usizarau huyu aliyekuzaa, ee Mungu wa mapendo na rehema, wewe mwenye kuleta duniani neema ya wokovu.

MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA YA MBILI

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya inne. Takhi prokataleve.

Tulipoinuliwa kwa kufunga juu ya tamaa za dunia, tumutukuzeni Bwana aliyetukuzwa Msalabani sababu ya kuinua ulimwengu pamoja naye; kwa udahamu wote tunyweni maji ya sikitiko, tufikiri siku na wakati ambako tutakapohukumiwa mbele ya mwamzi wa milele.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**. *Umoja.*

Wakati Mama Bikira alipokuona Msalabani, akalia machozi na akasema akiomboleza*:* Hii ni ajabu gani, ee Mwanangu? namna gani watu hawa wasiyo na shukrani wamekusulubisha Msalabani Wewe uliye uzima wa milele tena nuru ya macho yangu?

KATHISMA YA TATU

Sauti ya tano. Lampi simeron.

Ee Bwana, neema ya Msalaba wako inangaza ulimwengu, inaondoa nguvu ya shetani, na kwa kufunga inapunguza mwendo wetu; Ee Bwana wa Majeshi utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ton Sinanarkhon Logon.

Alipotazama utukufu wako Msalabani, Mama yako alilia na kuomboleza akasema*:* Ole wangu, ee Mwanangu mpendwa! Roho yangu inajeruhiwa wakati nakuona umesulubiwa Msalabani kama mwovu katikati ya wanyanganyi wawili.

IRMOS YA TISA. *Sauti ya tano. Isaia Khoreve.*

Isaya, cheza na furaha kwani Bikira alizaa mwana, tumboni mwake amezaliwa Emmanueli: Kati yetu Mungu amejifanya mtu, jina lake ni «Jua la haki»; na sisi wenye kumutukuza, ee Bikira, tunakuita mwenyi heri.

Kiha tunaimba Wimbo ya Mwangaza (Fotagogikon) na sauti ya hii Juma.

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Kwarezima, yenyi kuharibu tamaa, inatunza roho zenyi kuuawa kwa zambi; tuiendeleshe kama msaada wenyi kutoka kwa Mungu, tupokeeni kwa Musa mbao za amri bila kutamani kupitisha kipimo yao yenyi kuweza kuzivunja, tusifanane na wale walikufa jangwani, tusisikitike, lakini uso wetu yangae na furaha! Tusiwe wanafiki kama Wafarisayo, lakini tutumainie Habari Njema tukitukuza Msalaba wa Kristu aliye Mkombozi wa roho zetu. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi. *(Martirikon).*

Namna gani tutawaita ninyi Mashahidi Watakatifu? Wakheruvi? Maana ninyi ni kiti cha Kristu; Waserafi? Kwa sababu munamutukuza daima; Malaika? Kwani mulikataa mwili wenu;

Majeshi? Juu ya miujiza yalifanyika*:* Muna majina mengi, na zaidi tena vipaji! Ombeni kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**

Ni ajabu kupita maajabu yote ya zamani! Ndivyo alivyosema Mama Bikira kwa Mwana wake aliye Bwana wetu; Uchungu sikusikia waakti nilikuzaa naisikia sasa moyoni mwangu. Namna gani nitateswa nikikuona umesulubiwa Msalabani wewe uliye nuru ya macho yangu? Ujiharikishe kufufuka ili pamoja na ulimwengu nitukuze fumbo ya ajabu ya tendo lako la wokovu.

MU KAZI TANO MANGARIBI MU JUMA YA MBILI

Elezo*: Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo kumi; Hii inafwata mara mbili wa inne ya Paraklitiki ku mwisho na sauti ya hii Juma na wimbo inne ku Mineon. .*

Sauti ya ine.

Tazama, sasa wakati wenyi kufaa, tazama sasa siku ya wokovu; tazama roho yangu kwa mapendo yako kubwa, na kwa wema wako punguza uzito wa mzigo wa zambi zangu.*(mara mbili)*

Mangaribi. (Esperas). Prokimenon. *Sauti ya ine.* Zaburi 39.

Wapate haya na kufazaishwa pamoja.

Shairi*:* Nilingojea Bwana na saburi.

Somo ya Mwanzo tutasoma (5, 32-6, 8)

Noa alikuwa na miaka mia tano; Noa akazaa Semu, Hamu na Yafeti. Na ilikuwa wakati watu walipoanza kuzidi juu ya uso wa dunia, na binti walizaliwa kwao, wana wa Mungu wakaona binti za watu ya kama walikuwa wazuri; wakajitwalia wake wa wote waliowachagua. Bwana aka-sema*:* Roho yangu haitashindana na mutu milele, kwa sababu yeye vilevile ni mwili; hata hivi siku zake zitakuwa miaka mia moja na makumi mbili. Wanefili walikuwa duniani kwa siku zile, na vile nyuma yake, wakati wana wa Mungu walipoingia kwa binti za watu, wakawazalia wana; wao walikuwa watu hodari wa zamani, watu wenye sifa. Bwana akaona ya kama uovu wa watu ulikuwa mukubwa duniani, na ya kama mawazo yote ya mafikili ya mioyo yao yalikuwa mabaya tu siku zote. Na Bwana aljuta ya kwamba amefanya watu duniani, ikamuhuzunisha moyoni mwake. Bwana akasema*:* Nitaharibu mutu niliyemwumba toka uso wa inchi; mutu na nyama vilevile, na kitu kinachotambaa na ndege ya anga; kwani ninajuta ya kwamba nimewafanya. Lakini Noa akapata neema machoni mwa Bwana.

Prokimenon. Sauti uya sita. Zaburi 40.

Nimesema, ee Bwana, unihurumie.

Shairi*:* Heri ni yeye anayekumbuka masikini.

Somo ya Mezali tutasoma (6, 20-7, 1)

Mwana wangu, shika maagizo ya baba yako, wala usiache sheria ya mama yako*:* Uyafunge daima katika moyo wako, uyavae shingoni mwako. Wakati unapotembea yatakuongoza; wakati unapolala, yatakulinda, na wakati unapoamka, yatasemezana nawe. Maana maagizo ni taa, na sheria ni nuru, na maonyo ya mafundisho ni njia ya uzima*:* Ili kukulinda na mwanamuke mwovu, na ubembelezi wa ulimi wa mugeni. Usitamani nzuri wake moyoni mwako; wala usikubali akunase kwa kope za macho yake. Maana kwa sababu ya mwanamuke wa ukahaba mutu anatiwa katika hali ya kuhitaji kipande cha mukate*:* Na mwanamuke muzini anawinda uzima ulio wa damani. Mutu anaweza kutia moto kifuani mwake, na mavazi yake hayateketezwi? Ao mutu anaweza kutembea juu ya makaa ya moto, na miguu yake haiungui? Ndivyo alivyo mutu anayeingia kwa muke wa jirani yake; mutu ya yote anayemugusa hatakuwa pasipo azabu. Watu hawazarau mwizi, kama akiiba kushibisha nafsi yake wakati anaposikia njaa*:* lakini kama

akikamatwa, atarudisha mara saba; atatoa mali yote ya nyumba yake. Mwenye kuzini na mwanamuke anakosa ufahamu*:* Yeye anayetaka kuharibu nafsi yake mwenyewe anafanya hivi. Atapata vidonda na haya; wala laumu lake halitafutwa. Maana wivuni gazabu ya mutu. Naye hataachilia kwa siku ya kujilipiza kisasi. Hataangalia ukombozi wo wote; wala hatakuwa na salama hata ukiwa unamupa zawadi nyingi. Mwana wangu, shika maneno yangu, na weka amri zangu akiba kwako.

MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA MBILI

Elezo: *Kisha Eksapsalmos tunaimba Alliluia, katika desturi na kisha Apolitikion hii:*

Sauti ya mbili.

Mitume, Manabii na mashahidi, Maaskofu Watakatifu na wenye haki wote, ninyi muliyolindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Bwana, kwa wema wako uwakumbuke, watumishi wako na wenye haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mama wa Nuru isiyokadirika, kama Malaika mbinguni tunakuimbia kwa kukutukuza.

Elezo*: Kisha Ektenia Kidogo ya padri ao shemasi waimbaji wanaimba wimbo ya wafu na sauti ya hii Juma ndani ya hii Kitabu ku mukongo. Kisha waimbaji wanaimba Mahimidi ya Wafu (Evlogitaria).*

Kisha Evlogitaria padri atasema:

Maombi ya wafu.

Shemasi*:* Utuhurumie, ee Mungu, mu huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Tena tunakuomba kwa ajili mapumziko ya roho za marehemu watumishi wa Mungu ili makosa yao ya kujua na yasiyokujua yasamehewe.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Ili Bwana Mungu aweke roho zao kule wamepumzika wenye haki.

Mwimbaji*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Shemasi*:* Tumuombe Kristu Mungu wetu na Mfalme wetu wa milele awape rehema yake, maondoleo ya makosa ya ufalme wa mbinguni.

Waimbaji*:* Uwape, ee Bwana.

Shemasi*:* Tumuombe Bwana.

Waimbaji*:* Bwana hurumia.

Padri*:* Ee Mungu wa roho na wa mwili, uliyeshinda lufu na kumuharibu shetani, wewe uliyeleta uzima duniani, leta, ee Bwana, mapumuziko kwa roho ya m(wa)tumishi wako (jina lake), pahali pa mwangaza, pa majani mazuri, pa mapumziko, kule kunakimbia maumivu, sikitiko na masumbuko. Umusamehe zambi zake(zao) zote a(wa)litenda kwa sauti, kwa matendo na kwa mawazo, kwa sababu wewe ni Mungu mwema na mpenda-wanadamu, kwani hakuna mutu hata moja, anakaa mu uzima huu pasipo kufanya zambi, kwa sababu wewe peke yako msiye zambi, haki yako, ni haki ya milele, na amri yako ni ya kweli.

Kwa kuwa wewe ni ufufuo, uzima na mapumziko ya mu(wa)tumishi wako (jina lake) huyu (hawa) a(wa)melala, Kristu Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu pamoja na Baba

wako wasipo mwanzo na Roho Mtakatifu wako kamili. Mwema, Mpaaji wa uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Waimbaji*:* Amina.

Elezo: *Sasa tunaimba Kathisma ya Wafu.*

Sauti ya tano

Ee Mungu Mwokozi, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu, pamoja na wenye haki pumzisha watumishi wako na uwaruhusu wakae katika uwanja wako, usihesabie makosa yao ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Utukufu kwa Baba. . .

Ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Kristu Mungu wetu uliyezaliwa kwa Bikira sababu ya kuangazia ulimwengu, kwa maombezi yake utufanye sisi kuwa wana wa nuru, ee Bwana, utuhurumie.

Elezo: *Sasa tunasoma Zaburi 50 (51).Kisha tunasoma Kanuni.*

IRMOS YA TATU

Zimu ya mateso imefunguka mbele yangu katika vumbi ya adui: ujiharikishe kuniokoa, ee Mwokozi, kama ulivyookoa Nabii toka tumbo la samaki.

IRMOS YA TISA.

Ee Chemchem msiyekufa wa huruma wa maponyesho, wewe mwenyi kuwapa wanadamu wokovu, Bikira Mtakatifu, tunakutukuza wewe.

Kisha tunaimba wimbo ya Mwangaza (Fotagogikon) na kisha Apostikha toka wimbo ya wafu ya hii kitabu ku mukongo.



MU JUMA YA PILI KWA KWAREZIMA

UKUMBUSHO YA MT. GRIGORIO PALAMAS, ASKOFU YA THESALONIKI YA GREKIA

MU POSHO KWA MANGARIBI (ESPERINOS)

Elezo*: Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo ya Ufufuo wa Kristu wa sita na kisha Wimbo wa inne ya Mtakaitfu Grigorio.*

Sauti ya mbili. Piis efimion.

Sifa gani tutaimba kwa kutukuza Askofu Mtakatifu? Yeye ni neno la maarifa ya Mungu ni mwimbaji wa neema, ni chombo cha bei cha Roho Mtakatifu, ni nguzo imara ya Eklezya, ni furaha kubwa ya ulimwengu, ni mtoni ya hekima, kinara ya mwangaza, ni nyota ya nuru yenye kuangaza viumbe. *(mara mbili).*

Na maua ya nyimbo gani nitamutukuza nayo Askofu Mtakatifu? Yeye ni msaada wa ibada, ni adui wa ukafiri, mlinzi wa imani, ni mwalimu wa watawa Wataaktifu, ni kinubi cha ulinganyifu cha Roho Mtakatifu, ni kinywa cha kuangaa kama zahabu, ni chemchem huko waaminifu wanashota maponyesho mengi Mtakatifu Grigori anastahili utukufu wote.

Na midomo gani wanadamu wataweza kuimbia Askofu Mtakatifu? Yeye ni mwalimu wa Eklezya, ni mnadi wa nuru takatifu, ni mwalimu wa Utatu ya mbinguni, ni pambo nzuri la watawa watakatifu kwa mawazo yake takatifu na kwa fazila zake, utukufu wa Thessaloniki na usharifu wake, na Mtakatifu Dimitri wa manukato ya harufu nzuri anagawanya naye uriti wa ufalme wa mbinguni.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita.*

Ee Baba Mtakatifu kamili na mara tatu mwenye heri, mfuasi wa Kristu aliye kuhani mkuu tena wewe mwenyewe mchungaji mwema, ulitoa uzima wako kwa ajili ya kondoo zako; na sasa, ee Mtakatifu Grigori mbebaji-Mungu, umuombe tena atupe neema ya wokovu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Sasa tunaimba Theotokion ya Kitabu Paraklitiki na sauti ya hii Juma.

APOSTIKHA

Tunaimba Apostikha ya Ufufuo na sauti ya hii Juma na kisha tunaimba Doksastikon ya Mtakatifu Grigorio.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane.*

Sauti yako siku zote ni wepezi kwa kufundisha ilisikilika kwa masikio ya mioyo yetu, inaamsha roho za wavivu; na kwa maneno yako yenye kuongoza unatuonyesha mungazi na madaraja yake yenyi kupeleka watu wa dunia kwa Mungu. Ee Mtakatifu Grigori ajabu ya Thesalia, umuombe Kristu awangazie na nuru yake ya umungu wale wenyi kutukuza makumbusho yako.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. Sauti umoja.

Ee Bikira usiyeolewa ambaye kwako Mungu alipata mwili kwa namna isiyokadirika Mama wa Mungu aliye-juu, ee Mtakatifu asiye na doa, pokea maombi yetu; wewe mwenye kuwapokelea wanadamu maondoleo ya zambi zao, utusikilize sasa na omba kwa ajili ya wokovu wetu.

Kisha tunaimba Apolitikion ya Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu na hii chini ya Mt. Grigorio.

Utukufu kwa Baba. . .

Mwogozi wa Orthodoksi, msaada wa Eklezya na mwalimu, utukufu ya Watawa, mkubwa padri kati ya walimu ya Kanisa yetu, ee Griogie mwenye muujiza, Utukufu ya muji Thessaloniki na muhubiri wa Neema. Umwombe Kristu Mungu wetu ili aokoe roho zetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

SIKU YA MUNGU KWA ASUBUI (ORTHROS)

Kisha Eksapsalmos, «Bwana ndiwe Mungu. . . tunaimba Apolitikia sawa jana. Kisha Zaburi 50 (51) tunaimba:

Utukufu. . . *Sauti ya mnane.*

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana chemchem ya uzima; roho yangu ikeshe hekalu lako takatifu, ikichukua hekalu chafu la mwili wangu, lakini katika wema wako unitakase kwa mapendezi yako kubwa na mapendo yako ya huruma.

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya mnane.*

Uniongoze njiani ya wokovu, ee Mzazi-Mungu, kwani nilichafua roho yangu kwa zambi, na kwa uvivu wangu nilitumia vibaya uzima wangu, lakini kwa maombezi yako takatifu uniopeo ku uovu wote.

Sauti ya sita

Unirehemu, ee Mungu sawasawa ni wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uufute makosa yangu.

Nikikumbuka wingi wa matendo yangu mabaya, mimi mwenye zambi, naogopa ile siku ya ajabu ya hukumu, lakini ninapotumainia rehema na ruhuma yako, napaza sauti kama Daudi*:* Unihurumie, ee Mungu, kadiri ya wema wako kubwa.

KANUNI

Elezo*: Sasa tunaimba wimbo ya Ufufuo ya Kitabu Paraklitiki na kisha wimbo ya Mt. Grigorio.*

Wimbo wa kwanza

*Sauti ya ine*e. *Anikso to stoma mu.*

Enyi Wahubiri wenye kuongozwa, walimu wakubwa, kujeni kusanyikeni sababu ya kumuimbia kwa sauti moja Mtakatifu Grigorie huyu mwalimu wa roho.

Ee Mtakatifu Grigorie, wewe nguzo la imani tena mshindi wa Eklezya, nataka kukuimbia, ewe mchungaji wa Thessaloniki tena uzuri kweli wa Maaskofu.

Tangu utoto ulitamani kuishi na uzima safi, wa fazila, tangu ujana ulipenda mawazo mazuri na ulionyesha nia illeile kama majina yako Mtakatifu Grigorie.

THEOTOKION.

Ee Bikira Mtakatifu, uwe njia yenyi kuniongoza kwa makao takatifu, maana nimepoteza njia

yangu na nazama katika zimu ya uovu*:* Kwa usimamizi wako uniokoe.

Wimbo wa tatu.

Tus sus imnologus Theotoke.

Tunapolinda imara njia za mafundisho yako takatifu, tunakimbia walimu wa uwongo, na kwa usafi wa maandiko yako, ee Mtakatifu Grigorie, tunakimbiza, mbali majeshi yao.

Ee mwenye heri, ulitangua elimu ya mpumbafu ya wenye kuwaza mbaya, ulikuwa moyoni na hekima ya kipekee ambayo ulivunja nayo majivuno yao.

Uliporegeza furaha ya mwili ambayo uharibifu inaongojea, kwa utawa ulileta na hekima uzima ku mwendo wa roho yako sababu ya kuifanya kuwa chombo cha maarifa ya Mungu.

THEOTOKION.

Kwa ufahamu na kwa nia mbaya nimeishi na uzima ya haya na ya upumbafu, lakini wewe Bikira Mama wa Mungu uniambatishe sasa kwa mapendo ya Mungu katika maombezi yako.

KATHISMA

*Sauti ya ine*e. *Takhi prokataleve*

Uliharibu mafundisho ya uwongo, uliangaza imani ya kweli, kwa hekima yako uliangaza ulimwengu, na ulipata taji ya mshindi, ewe Nguzo ya Eklezya tena Askofu wa ukweli, umuombe Kristu atuokoe sisi wote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira, ujiharikishe kupokea maombi tunayokutolea; ee Bibi Mtakatifu kamili, uyatoe kwa Mwana wako tena Mungu wetu*:* Tuliza sikitiko ya wale wenye kukukimbilia; tenga werevu wa Muovu na haribu nguvu ya Adui mwenyi kukombanisha watumishi wako.

KONTAKION

Sauti ya mnane. Ti Ipermakho.

Tunakuimbia kama chombo takatifu cha hekima, kama mutume mwenyi kuangaa wa maarifa ya Mungu, ee Mwongozi Grigorie. Ulipotiisha akili yetu kwa ile ya Mungu, ongoza roho zetu kwa yeye tuimbe*:* Salamu, ee Muhubiri wa Neema.

IKOS

Duniani ulionekana Malaika wa mbinguni, ukiwatangazia wanadamu mafumbo ya mbinguni; uliunganisha akili yako kwa Wabila-mwili, unaongoza roho zetu tukuimbie hivi*:* Salamu, wewe mjumbe wa Mungu asiyeumbwa salamu, wewe mwenye kuharibu mifano yenyi kuumbwa.

Salamu, mahali pa juu penye kufunua hali ya Mungu,
Salamu, wewe maarifa makuu ya nguvu ya Mungu,
salamu wewe mfasiri mukuu wa utukufu wa Mungu,
salamu, wewe mchongezi wa mafundisho ya ukafiri.
Salamu, wewe kianga cha Jua ya milele,
Salamu, katika wewe ukweli inaangaa,
Salamu, katika wewe uwongo imefifia,
Salamu, wewe muhubiri wa Neema.

SINAKSARI

Elezo**:** *Sasa tunasoma Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha hii:*

Leo, siku ya Mungu ya mbili kwa Kwarezima tunashangilia ukumbusho ya Mtakatifu Grigorio, askofu mkubwa ya mji Thessaloniki ya Grekia, Muhubiri ya Neema Takatifu.

Kwa maombezi yake, ee Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

KATAVASIES YA MZAZI-MUNGU

Nitafungua kinywa changu. . . *(tafuta mu Kitabu Saa Ukubwa)*

EKSAPOSTILARION

Elezo: *Tunaimba Eksapostilarion ya Ufufuo ya Kristu na kisha hii:*

Sauti ya mbili. Tis mathites sinelthomen.

Salamu, wewe matumaini ya wapadri wetu watakatifu, salamu, wewe kiungo cha Walimu wa dini wenye kuongozwa, hema na makao ya maarifa, bahari ya kiroho huko kunachanyika matendo na mawazo, mganga wa magonjwa ya wanadamu; wewe ni hekalu ya Roho Mtakatifu, Baba mwenyi kuishi mpaka mauti hata milele.

THEOTOKION Sauti umoja.

Ee Bikira, wewe Malkia wa ulimwengu, utukinge toka hatari na sikitiko utusaidia katika tabu ya siku ya mwisho, ukituondoa kwa shetani, kwa Hadeze na kwa upotevu; kwa maombezi yako takatifu utustahilishe tusimame mbele ya baraza ya hukumu ya Mwana wako, ee Mzazi-Mungu.

MASIFU.

Elezo: *Tunaimba wimbo tano ya Ufufuo ya Kristu na tatu ya Mt. Grigorie.*

Sauti ya kwanza. Ton uranion tagmaton.

Heri ilikuwa ni ile uzima ulishi duniani, na unafurahi sasa katika makusanyo ya wenye heri, pamoja na wapole ulipokea inchi yao, ewe Askofu Grigorie, wewe ni tajiri kwa Mungu wa hazina ya mema kwa ajili ya wale wenye kutukuza jina lako.

Shairi: Kinywa cha mwenye haki kinanena hekima na ulimi wake inatangaza haki.

Ulistawisha mafundisho ya Uorthodoksi, ukakata miiba ya walimu wa uwongo, ulizidisha katika udongo nzuri mbegu ya Imani, ukaimwangia mvua ya mafundisho yako ni mara mia zaidi ulitoa kwa Mungu kama mtunza shamba muhodari.

Shairi: makuhani wako, ee Bwana, wanavaa haki, waaminifu wako wanashangilia.

Nuru ya uzima yako timilifu inasangaza Malaika na wanadamu, kwa sababu ulionekana kwa mtawa na mshindani, rafiki wa kweli, mkubwa na mtumishi mwenye kustahili mafumbo takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita.*

Juu ya wale walitembea katika giza ya zambi, kwa hii wakati wa kufunga uliinuka kama nuru, ee Kristu*:* Utuonyesha siku ya utukufu ya Mateso yako kusudi tukuimbie*:* Simama, ee Mungu, na utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA

MU JUMA MANGARIBI YA MT. GRIGORIO PALAMAS.

Elezo*: Kisha Zaburi 103 (104) nikusema Proimiakos, tunaimba: «Bwana nimekuita. . » na wimbo kumi, nikusema: Wimbo wa inne na sauti ya hii Juma ku mwisho ya hii Kitabu, wimbo tatu ya Triodi na wa tatu ya Mineon.*

Wimbo ya Triodi:

Sauti ya mnane. Ametritos iparkhis.

Nilikosa bila kipimo juu yako, azabu yangu itakuwa kubwa sana*:* Kusaga memo, kulia bila kutulizana, gehena yamoto, giza ya Hadeze; lakini wewe Mwamzi mwenye haki kamili unipe machozi ya toba sababu ya kupata, kwa kufunga, maondoleo ya zambi zangu, na napaza sauti kwako, ee Kristu tena*:* Unihurumie kwa wema wako kubwa.

Ee neno, juu ya mlima huko makosa yangu yalinipoteza, kuja unitafute, uniite kwako, ukifukuza mbali yangu mawazo mbaya; unipe niishi mara ingine, natolewa kwa mauti; kwa machozi nakulalamikia na nakuambia, ee Kristu tena Bwana*:* Unihurumie kwa wema wako kubwa.

Sauti umoja. Tin Endokson.

Enyi waaminifu, tunapoanza Juma ya tatu ya Kwarezima, tutukuzeni Utatu Mtakatifu, na tufurahi kwa hii wakati yote itafwata; twache yafifie tamaa za mwili wetu na tuchume, kwa ajili ya roho yetu, maua takatifu sababu ya kutukuza Siku ya Yenga mfalme wa masiku, na tukibeba taji tutaimbia ushindi wa Kristu. .

Wimbo tatu ya Mineon. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION** ya Mineon.

Kisha padri atafanya Kuingia (Isodos) pamoja na chetezo. Vile atafanya kila mu Juma kwa Sala ya Mangaribi, kwani waimbaji inapaswa kuimba ma Prokimenon makubwa.

Mwangaza upole. . .

PROKIMENON KUBWA.

Sauti ya mnane.

Wala usifiche uso wako kwa mutumihsi wako kwa sababu mimi ni katika taabu; mbio inijibu ukaribie nafsi yangu na kuikomboa.

Shairi: Wokovu wako, ee Mungu, uninyanyue.
Wala usifiche uso wako kwa....
Shairi: Wapole waliona na wanafurahi.
Wala usifiche uso wako kwa....

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Mimi ni mupumbafu, nilikataa kizuio ya baba, nimelisha kondoo na mawazo mbaya, nimetumia vibaya uzima wangu wote; mimi maskini! Nilipokosa chakula chenui kuleta nguvu kwa roho, nilionja furaha yenyi kushidisha kwa muda kidogo tu. Ee Baba, kwa wema wako usinifungie mlango ya roho yako*:* Unifungulie sababu ya kunipokea kama Mwana mpotevu na uniokoe. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi. Martirikon.

Enyi Mashahidi wa Bwana, ninyi wenye kutakasa ulimwengu na kuponyesha magonjwa yote, mutuombee sasa sababu ya kuokoa roho toka mtego wa Adui.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Mama usiyeolewa, mbingu zinaimbia huruma yako, na tunatukuza kuzaa kwako kusiyokadirika*:* Ee Mzazi-Mungu, omba kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA WA TATU YA KWAREZIMA

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mukongo ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya mnane. To prostakhthen.

Na moto ya kujikatalia tuchome sasa nyasi mbaya ya tamaa zetu, na kwa kutuliza moto isiyozimika tuache machozi yetu yatelemuko mingi, tumulalamikia huyu atakayekuya kuhukumu dunia yote*:* Ee Bwana na Mwokozi mwenyi kujaa na wema, utuokoe toka hukumu yote, utupe maondoleo ya zambi zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira mtukufu na mjaliwa neema ya Mungu, pamoja na Malaika Wakuu na Majeshi yote ya mbiguni, umuombe daima kwa ajili yetu huyu ambaye kwa kutaka kwake amekuwa mwana wako*:* Fanya ili atupe, mbele ya mwisho, usamehe na maondoleo ya zambi zetu na hali ingine ya uzima wetu kusudi tustahili rehema yake.

KATHISMA YA TATU.

Sauti ya mnane. To prostakhthen.

Ee Bwana mara tatu Mtakatifu, kwa hii juma ya tatu, linda wenye kufunga na uwastahilishe wakae imara kwa kushika amri zako kusudi tuweze, kwa usafi wote kuona na kutukuza Ufufuo wako tukufu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu mlinzi wa waaminifu, furaha ya roho zenye kuteswa tena mfariji wa wenye kusikitika, pamoja na malaika Wakuu na wenye mamlaka umuombe daima kwa ajili yetu huyu aliyezaliwa tumboni mwako kwa namna ya ajabu ili wakati wa hukumu tusihukumiwe kwa hukumu yoyote.

KANUNI

Elezo*: Ya Mineon na kisha ya Triodio. Ni hii:*

Sauti ya mnane. Asma anapempsomen.

Wimbo wa kwanza.

Ee Mungu mwenye kuhurumia waovu, pokea machozi ya toba yangu*:* Kwa ujinga nimetumia vibaya uzima wangu wote; sikiliza kulia kwangu*:* Nimekosa, hakuna lazima ya mwenyi kushitaki kwa sababu niko na haya ya matendo yangu.

Nilipoacha karamu ya Malaika, nimefanana na nguruwe kwa kuonja uovu wa zambi; lakini sasa narudi kwako*:* Ee Baba wa mbinguni, unipokee kama mumoja wa warafiki wako.

Enyi waaminifu, tufukuzeni kabisa giza ya furaha za dunia, tukimbilieni kwa nuru ya ukweli sababu ya kusharikia kwa karamu ya mbinguni.

THEOTOKION

Salamu, ee Hekalu Takatifu, nywele zenye kufunikwa na umande takatifu, Kisima cha uzima wa milele chenye kusabitishwa, ee Bibi yetu, linda watu juu ya mashambulio ya adui.

Wimbo ingine.

Sauti ya mnane. Asomen odin to Theo.

Katika juma tatu tujitakaseni kama walivyojitakasa wana wa Israeli katika siku tatu, hivi tutaufikia mlima wa matakio yetu sababu ya kusikiliza sauti takatifu na kumuimbia Kristu.

Kwa kufunga, kama Samsoni, tupate nguvu yetu sababu ya kushinda shetani, huyu simba mwenye kunguruma, na tusiache tamaa kutuchekelea sisi kama Dalida.

Utukufu kwa Baba. . .

Katika watu tatu maimbia umungu, umoja wa Utatu wa nuru na wa uzima*:* Mungu ni Baba, Mungu na Mwana aliyezaliwa, na Mungu ni Roho wa uzima anayetoka kwa Baba.

Sasa na siku zote. . .

Salamu Bikira Safi kamili*:* Ulikuwa furaha ya Eva, kwa kuzaa kwako kulia kwake kulimalizika; salamu, ee wingu lenye kuangazwa la nuru ya milele huko alitoka Jua la haki ndiye Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Na ibada, kama Daudi, tuvae sisi pia silaha ya unyenyekevu*:* Tutashinda majivuno, huyu Goliati mwingine, hivi tutaondoa tamaa nyingi.

IRMOS*:* Tumwimbie Mungu wetu*:* Aliokoa Israeli toka utumwa mbaya wa farao, alimuongoza katika wingu la nuru na nguzo ya moto*:* Tumuimbie, kwani amevaa utukufu.

Elezo*: Pa fasi ya Kontakion tunasoma Martirikon (Wimbo ya mashahidi). Tafuta ku mwisho ya hii Kitabu. Kisha Sinaksarion ya Watakatifu. Kisha Fotagogikon na sauti ya hii juma. Kisha Apostikha.*

APOSTIKHA

Sauti ya ine.

Nimevaa manguo machafu ya zambi, nimepoteza nguo yangu ya arusi na furaha ya karamu, unionyesha huruma yako kubwa, unipokee kama Mwana mpotevu, unihurumie.

Ee Mashahidi, namna gani jatutatukuza mashindano kubwa mulishindana nayo? Mwilini mwenu mulishinda adui asiye na mwili wakati mulipokiri Kristu na kushika alama ya Msalaba na adui*:* Ombeni daima kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu, wewe na taa isiyozimika, ee Bibi yetu, wewe ni Kiti cha Mfalme*:* Omba kwa ajili ya roho zetu.

MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA TATU

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo sita; Wimbo tatu ya hii inafwata na wa tatu ya Mineon.

Sauti ya kwanza. Panefimi Martires

Na msaasa wa Roho Mtakatifu tupendeni kufunga kwa roho kwenye kuregeza tamaa mbaya na kuleta nguvu ya kuzaa matendo matakatifu kwa kuinua roho yetu mbinguni na inatupa sisi maondoleo ya zambi*:* Mungu anatupatiayo kwa wema wake.

Ee Bwana, nimatumia vibaya uzima wangu wote, lakini kama Mwana mpotevu nakulalamikia*:* Ee Baba wa mbinguni, nimekosa, unihurumie na uniokoe, mbali na wewe niko maskini kwa matendo mema*:* Usinifukuze sasa.

Ingine. *Sauti ya tatu. Defte apanta ta perata.*

Kujeni tuimbe wote zaburi kwa sauti ya matoazi tukumbatineni safi kiasi; katika hii tutaweza katika roho kuangusha nyoka aliye fundi wa uovu; tunapojaa na matumaini, ee Kristu, tunakulalamikia*:* «Ee Mwokozi, utupe, bila kuhukumiwa hukumu yako, tuone Msalaba wako takatifu, na tukisujudu mbele yake, tuitukuze na furaha kwa zaburi na nyimbo zetu.

Kisha wimbo tatu ya Mineon. Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.

Prokimenon. *Sauti ya ine.* Zaburi 43.

Tumejisifu Mungu muchana kutwa.

Shairi*:* Tumesikia na masikio yetu, ee Mungu, baba zetu wametuambia.

Somo ya Mwanzo tutasoma (6, 9-22).

Hivi ni vizazi vya Noa. Noa alikuwa mutu wa haki, mukamilifu katika vizazi vyake; Noa akatembea pamoja na Mungu. Noa akazaa wana watatu, Semu, Hamu na Yafeti. Dunia ikaharibika mbele ya Mungu, dunia ikajaa na jeuri. Mungu akaona dunia, na tazama, imeharibika; kwa sababu wenye mwili wote wamejiharibia njia duniani. Mungu akamwambia Noa*:* Mwisho wa miili yote umekuja mbele yangu; kwa maana dunia inajaa na jeuri kwa sababu yao; na tazama, nitawaharibu pamoja na dunia. Ujifanyie safina ya muti goferi, utafanya vyumba ndani ya safina, na kuipakaa ndani na inje kwa lami. Utaifanya hivi*:* Urefu wa safina mikono. mia tatu, upana wake mikono makumi tano na urefu juu mikono makumi tatu. Utafanya dirisha kwa safina, na kwa mukono mumoja utai-mallza Juu; na mulango wa safina uatweka kwa mbavu yake; utaifanyia dari tatu, ya chini, na ya pili, ya tatu*:* Nami, tazama, nitaleta garika ya maji Juu ya inchi, kuharibu miili yote. wote na pumuzi ya uzima ndani yao, chini ya mbingu; kila kitu kilicho duniani kitakufa. Lakini nitasimamisha agano langu pamoja nawe; na utaingia safina, wewe na wana wako na muke wako na wake wa wana wako. Na ya kila kitu kilicho hai ya miili yote, utaleta wawili wa kila namna ndani ya safina kuwachunga hai pamoja nawe; watakuwa mume na muke. Ya ndege kwa namna yao, na ya ngombe kwa namna yao, na kila kitu kinachotambaa Juu ya inchi kwa namna yake, wawili wa kila namna watakuja kwako kuwachunga hai. Na utajitwalia chakula cho chote kinachokuliwa na kukijiokotea, na kitakuwa chakula kwako na kwao. Noa akafanya hivi; sawasawa na maneno yote Mungu aliyomwagiza, akafanya hivi.

Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 44.

Nitafanya jina lao kuwa ukumbusho katika vizazi vyote.

Shairi*:* Moyo wangu umefurika kwa neno jema.

Somo ya Mezali tutasoma (8, 1-21)

Hekima hailii, na ufahamu hautoi sauti yake? Juu ya pahali pa juu karibu na njia, kwa njia panda anasimama; kn\ando ya malango, kwa kuingia mujini, kwa kuingia milangoni, anapiga kelele*:* Ee watu, ninawaita ninyi; na sauti yangu ni kwa wana wa wtu. Ee ninyi wajinga, mufahamu akili; Na ninyi wapumbafu, muwe na moyo wa ufahamu. Sikieni, maana nitasema maneno yaliyo mazuri sana; na kufungua kwa midomo yangu kutakuwa maneno ya haki. Maana kinywa changu kitasema kweli; na uovu ni machukizo kwa midomo yangu. Maneno yote ya kinywa changu ni haki; hakuna neno lililopotoka, ao la ukaidi kati yao. Yote na wazi kwake anayefahamu, na ya haki kwao wanaopata kujua, pokea mafundisho yangu, wala si feza; na maarifa zaidi ya zahabu safi. Maana hekima ni njema kupita marijani; na vitu vyote vinavyotamaniwa haviwezi kusawanishwa naye. Mimi hekima nimefanya akili kao langu, na ninatafuta maarifa na akili njema. Kuogopa Bwana ni kuchukia uovu*:* Majivuno na kivuri, na njia mbovu, na kinywa cha ukaidi ninakichukia. Shauri ni langu, na maarifa ya kweli*:* Nina ufahamu, nina uwezo. Kwa kusaidia kwangu wafalme wanatawala, na wana wa wafalme wanahukumu haki, kwa kusaidia kwangu wana wa wafalme wanatawala, na wakubwa, waamuzi wote wa dunia. Ninawapenda wanaonipenda; nao wanaonitafuta kwa bidi watanipata. Utajiri na heshima ni pamoja nami; ndiyo, utajiri unaodumu na haki. Matunda yangu yanapita zahabu,

ndiyo, zahabu safi; na faida yangu inapita feza safi. Ninatembea katika njia ya haki, katikati ya mapito ya hukumu.

APOSTIKHA

Sauti ya mbili.

Ee Baba mwema kamili, kwa ujinga wangu nimejiondolea mema yote ulinipa; mbali yako nilikuwa mtumwa katika inchi ya ugeni na nililisha nyama wabaya bila kuweza kula ile walikula; ndiyo maana nakimbilia kwako, najua wema wako*:* Kwa rehema yako funika utupu wangu na uniokoe.*(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi *(Martirikon).*

Mashahidi Watakatifu wanatuombe, na kwa nyimbo zao wanamutukuza Kristu*:* Tangu hapo inamalizika upotevu yote na wanadamu wanaokolewa kwa imani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Toka tumbo lako la ubikira Nuru imeangaa duniani na kwa neno lako Neno. Umuombe, ee Bikira Mtakatifu kamili, aokoe roho zetu mtego wa adui.

MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA WA TATU

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya kwanza. Tu Lithu sfragisthentos.

Tujitakaseni kwa kufunga na sala na tumutumikie Mungu kwa kusaidia maskini; tulie na kuomboleza kwani tazama imekuja waakti wa kutubu kusudi tuepuke sikitiko ya milele katika zimu ya moto; Kristu atukuzwe, kwani analeta toba kwa wanadamu wote wenye kutubu katika usafi wa roho yao.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulibeba mikononi mwako Muumba aliyejifanya mtu sababu ya kutuokoa; hii mikono takatifu uyaimue sababu ya kumuomba atenge mbali yetu vishawishi na hatari; na sisi wenye kukulalamikia tunakuimbia na mapendo*:* «Utukufu kwa huyu aliyekaa tumboni mwako, utkufu kwa huyu aliyetoka kwako, utukufu kwa huyu aliyezaliwa kwako, sababu ya kutuokoa.

KATHISMA YA TATU

Sauti ya tatu. Efrenestho ta urania.

Kwa sherehe ya Kwarezima na furaha ya nyimbo zetu, kwa nguvu sala inatupatia sababu ya kushinda tamaa, tutengue werevu wa Beliali, tumufwate Kristu na kumwambia*:* Utustahilishe kuona Msalaba wako Takatifu, ee Mungu wa mapendo ukitupa sisi neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee mwenye heri Mama usiyeolewa, ponya roho yangu ya uzaifu, maana nanguka chini ya uzito wa zambi zangu na nakuita, ee Mzazi-Mungu, katika kulia kwa roho yangu. Unipokee, ee Bikira safi kamili, japo zambi nyingi ili nikijazwa na matumaini, nikulalamikia*:* Salamu, makao takaitfu ya Bwana Mungu wangu.

KANUNI YA MINEON

Elezo*: Pa fasi ya Kontakion tunasoma Martirikon (Wimbo ya mashahidi). Tafuta ku mwisho. Kisha Sinaksarion ya Watakatifu. Kisha Fotagogikon na sauti ya hii juma. Kisha Apostikha.*

APOSTIKHA

Sauti ya saba.

Nimekosa, ee Bwana, naiungama kwako, naweza kufanana na Mwana mpotevu; sisubutu kutazama mbinguni, kwani toka mbinguni nimeanguka katika hii mateso; nimekosa juu ya mbingu na juu yako, sistahili kuitwa mwana wako*:* Mimi mwenyewe nakataa hii jina, si lazima ya wenyi kushitaki ao washuhuda; upotevu inanikokotea kwa ushindi wake, nazarauliwa kwa matendo yangu mbaya; niko na haya ya utupu wangu, sisubutu kuonekana mwenyi kuvaa nguo ya vilaka; ee Baba mwema kamili, Mwana wa pekee na Roho Mtakatifu, unipokee katika toba na unihurumie. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi.

Mbele ya baraza ya hukumu ya makafiri katika uwanja mashahidi watakaitfu walilalamika na furaha*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ulizaliwa kwa Bikira kwa namna isiyoweza kufasiriwa, uliangazia wale, katika giza, walikulalamikia*:* Ee Kristu na Bwana, utukufu kwako.

MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA WA TATU

Elezo*: Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo sita; Wimbo tatu ya hii inafwata na wa tatu ya Mineon.*

Sauti ya tatu. Estisan ta triakonta.

Ee Bwana wewe ambaye Msalabani ulishinda werevu wa nyoka, okoa roho yangu yenye kupotea katika zambi; kwa hii wakati wa Kwarezima unitakase, unipe nitimize mapenzi yako kusudi nione safi, ee Rabi, mateso yako kubwa.

Upanga ya furaha imeniumiza, iliniangusha mbaya*:* Leta uzima kwa roho yangu na uniponye, ee Bwana, wewe uliyechomwa mkuki; ee Rabi na Mwokozi uliyeponyesha wale walijeruhiwa kwa mishale wa adui, unipe nisharikie Mateso yako kubwa.

Sauti ya mbili. Stavtothito ekrazon.

Ee Bwana, tunaweza kwa hii Kwarezima kupokea nuru ya roho zetu sababu ya kusyahili, bila kuhukumiwa, kuona na furaha Msalaba wako na kusujudia na mapendo*:* Imekwisha angaza mapendo yako ya kutaka ambayo kwa wema wako, ee Bwana, unatupa kuona.

Wimbo tatu ya Mineon. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya tatu. Zaburi 47.

Bwana ni mukubwa na mwenye kusifiwa sana.

Shairi*:* Katika muji wa Mungu wetu, katika mulima wake mutakatifu.

Somo ya Mwanzo tutasoma (7, 1-5).

Bwana akamwambia Noa*:* Ingia safina, wewe na nyumba yako yote; kwa sababu wewe mmekuona mwenye haki mbele yangu katika kizazi hiki. Ya nyama zote walio safi utajitwalia saba saba, mume na muke wake; na ya nyama wasio safi wawili wawili, mume na muke wake; na ndege vilevile za hewa, saba saba, mume na muke; kuchunga hai uzao juu ya uso wa inchi yote. Kwa maana bado siku saba, na nitaleta mvua juu ya dunia siku makumi ine,
muchana na usiku; na kila kitu kilicho hai nilichokifanya, nitakiharibu toka uso wa inchi. Noa akafanya sawasawa na maneno yote Bwana aliyomwagiza.

Prokimenon. Sauti ya mbili. Zaburi 48.

Kinywa changu kitasema akili.

Shairi*:* Sikieni maneno haya, ninyi mataifa yote.

Somo ya Mezali tutasoma (8, 32-9, 18)

Kwa hivi basi, wana wangu, munisikilize*:* Maana heri wale wanaoshika njia zangu. Sikieni

mafundisho, namuwe na hekima, wala musiikatae. Heri ni mutu anayenisikia, anayengalia siku zote kwa malango yangu, akingoja kwa nguzo za milango yangu. Maana yeye anayeniona mimi anaona uzima, naye atapata ukubali kwa Bwana. lakini mwenye kunikosea anaumiza nafsi yake mwenyewe*:* Wote wanaonichukia wanapenda mauti. Hekima amejenga nyumba yake, amechonga nguzo zake saba*:* Ameua nyama zake, amechanganya mvinyo yake, amestandika meza yake. Ametuma vijakazi wake, analia juu ya pahali pa juu pa muji. Mujinga ye yote ageuke na kuingia hapa*:* Naye asiye na ufahamu, anamwambia*:* Kuja ule wa mukate wangu, na kunywa wa mvinyo niliyochanganya. Ninyi wajinga, acheni ujinga, mupate kuishi; na mutembee katika njia ya ufahamu. Yeye anayekemea mwenye kuzarau anajipatia haya*:* Naye anayeonya mutu mwovu anajipatia kipaku. Usionye mwenye kuzarau, asikuchukie*:* Kemea mwenye hekima, naye atakupenda. Fundisha mwenye hekima, naye atazidi kuwa na hekima*:* Fundisha mwenye haki, naye atazidi kuwa na elimu. Woga wa Bwana ni mwanzo wa hekima*:* Na kujua Mutakatifu ni ufahamu. Maana kwa njia yangu siku zako zitazidishwa na miaka ya maisha yako itaongezwa. Kama wewe ukiwa mwenye hekima, una hekima kwa wewe mwenyewe. Na kama wewe ukizarau, utaichukua peke yako. Mwanamuke mupumbafu anapiga kelele; Yeye ni mujinga, wala hajui kitu. Naye anaketi mulangoni mwa nyumba yake, juu ya kiti pahali pa juu pa muji, ili kuita wale wanaopita, wanaipota katika njia zake, kila aliye mujinga ageuke kuingia hapa*:* Naye asiye na ufahamu, anamwambia*:* Maji ya kuiba ni matamu, na mukate unaokuliwa kwa siri unapendeza. Lakini hajui ya kuwa wafu ni pale; ya kama wageni wake ni chini katika Hedeze.

APOSTIKHA

Sauti ya mbili.

Baba, ni hivi nasubutu kukuita wewe Muumba na Bwana uliyeniumba kwa udongo kwa sura na mfano wako, hata kama nilipoteza hali yangu ya mwana kwa maisha niliishi kwa kusahau zawadi zako na kupoteza mali uliyonipa; usinifukuze nyumbani mwa Baba, wewe uliyetaka Mwana wako wa pekee auawe Msalabani kwa ajili yangu*:* Uniadibishe na unichukue pamoja nawe kwa wema wako kubwa. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi.

Kwa kundi Mashahidi watakatifu walishindana na wazulumu wakisema*:* Tunashindana kwa ajili ya Mfalme wa majeshi ya juu mbinguni; mutatuteswa kwa mapigo na moto, sisi hatutakataa uwezo wa Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.

Ee Bwana mwenye kutupatia uzima, wakati watu wasio na haki walikutundika Msalabani, Mama yako Mtakatifu kamili alisimama karibu yako akilia na kuomboleza*:* «Ee Mwanangu mpendwa, nuru ya macho yangu, namna gani unateswa kwa kusulubiwa Msalabani katikati ya waovu, wewe uliyetundika inchi juu ya maji?

MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA WA TATU.

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mukongo ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya tatu. *Tin oreotita.*

Ee Bwana, kwa mti wa Msalaba uliteketeza moto ya kutokutii, ulipoinuliwa na kuuawa kwa kutaka kwako, uliangusha adui; ndio maana nakuomba, ee Bwana*:* Regeza tamaa zote za mwili wangu, leta uzima rohoni mwangu na kwa kufunga kwenye kuharibu tamaa na haya yote ya zambi unitakase kwa wema wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Mungu wa mapendo, kwa kusulubiwa kwako uliitikia matusi ya mauti; alipoona hivi, ee Kristu Mama yako akasikitika alipojeruhiwa moyoni, akalia; kwa rehema yako na kwa maombezi yake, wewe mwenye kuondoa zambi ya dunia, umuhurumie na utuokoe.

KATHISMA YA TATU

Sauti ya mbili. Anastas ek tu mnimatos.

Tunaposhangilia hii Kwarezima ya nuru, tunakulalamikia, ee Bwana*:* Utulinde katika amani, utuokoe toka werevu wa adui, na utustahilishe, kwa wema wako, kukumbatia Msalaba wako heshimiwa katika hii unaleta duniani mapendo kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, alipoona kufa kwako Msalabani, Bikira Mama yako alilia na uchungu akasema*:* Ee Mwanangu, hii ni fumbo gani ya woga? Wewe mwenye kuwapa wote uzima wa milele, namna gani unazarauliwa na kufa Msalabani kwa kutaka kwako?

KANUNI

Ya Mineon na kisha tunatimiza na Wimbo wa tatu ya Triodi. Ni hii:

Sauti ya tatu. To stereoma.

Wimbo ya tatu.

Tuliposulubiwa na huyu aliyesulubiwa kwa ajili yetu, turegezeni viungo vyote vya mwili wetu kwa kufunga, sala na maombi.

Ee Bwana ambaye kwa lufu yako Msalabani ulinyanganya miiba ya zambi, ondoa kibanzi cha mawazo ya roho yangu.

Tunapotumia kufunga kuwa silaha ya mioyo yetu, tufukuze mashetani, tujikinge chini ya uwezo wa Msalaba.

Ee Bikira safi kamili, kwako alitoka Neno aliyejifanya mtu sababu ya kutengeneza kuanguka kwa wazazi wetu wa kwanza, kwa mapendo yake kwa ajili yetu.

IRMOS INGINE.

Sauti ya mbili. Stereoson imas.

Ee Bwana, Msalaba wako wenye kuleta uzima inaniweka alama ya wokovu; katika hii nashinda adui na naimbia uwezo wa Mungu.

Tunda la muti wa Msalaba wako kwa dunia ni uzima wa milele*:* Ee Kristu, waakti tunaionja tunaokolewa toka mauti.

Utukufu kwa Baba. . .

Natukuza watu tatu wa Mungu mumoja, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, uwezo moja wa umungu, ufalme wake tukufu.

Sasa na siku zote. . .

Kuzaa kwakop kulikuwa kwa ajabu, maana Mungu mwenyewe anajifanya mtu tumboni mwako, huyu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati bila mbegu anakuja duniani kwa nyakati za mwisho.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mungu wa mapendo, neema ya Msalaba wako imemwanga nuru yake yote duniani, inatuita kwa Mateso yako takatifu*:* «Utustahilishe tuiabudu na imani».

IRMOS*:* Ee Bwana, kwa mapendo yako sabitisha roho zetu «ambaye Msalabani uliondoa zambi, panda woga wa jina» lako mioyoni mwa wale wenye kukutukuza.

Elezo*: Pa fasi ya Kontakion tunasoma Martirikon (Wimbo ya mashahidi). Tafuta ku mwisho. Kisha Sinaksarion ya Watakatifu. Kisha Fotagogikon na sauti ya hii juma. Kisha Apostikha.*

APOSTIKHA

Sauti ya mbili.

Ee Baba Mwema kamili, kwa upumbafu nimezarau daraja yangu na nimejitenga toka utukufu wako, kwa haya nimetumia vibaya lazima ya neema yako; nilipokosa chakula nilikula kwa meza ya bwana mchafu aliyenituma katika inchi yake kupoteza roho yangu kulisha nguruwe katika uzima ya upotevu, bila kushibishwa kwa furaha nilitumikia; lakini kwa toba yangu nilimulalamikia Baba yangu mwema na mwenye huruma*:* «Nimekosa juu ya mbingu na juu yako, unihurumie.*(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Kristu, Mashahidi wengi wanakuomba*:* «Kwa wema wako kwa wanadamu, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu.

Ee Bikira Mtakatifu, wakati walimusulubisha Mwana wako tena Mungu wako Msalabani uchungu gani ulipata, ulilia, uliomboleza na kulalamika kwa uchungu*:* Ole wangu, Mwanangu mpendwa, unateswa bila haki unapotaka kuokoa uzao wa Adamu! Ndiyo maana, ee Bikira, tunakuomba na imani*:* Utupe sisi neema ya Mwana wako.

MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA WA TATU

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo kumi; Wimbo sita ya hii inafwata na wa tatu ya Mineon.

Sauti ya ine. Idiomelon.

Kwa ujinga nilitimia vibaya mali ya baba yangu, na niliteswa katika inchi ya watu wabaya, kwa mwendo yangu mbaya nimefanana na wanyama wasipo akili, nimepoteza neema yote ya Mungu, ndiyo maana kwa toba yangu narudi kwako na nakulalamikia, ee Baba mwenye huruma*:* Ee Bwana, nimekosa, pokea toba yangu, na unihurumie. *(mara mbili).*

Enyi Mashahidi Watakatifu, mikate ya uzima ya sadaka, sadaka za kiroho, sadaka zenyi kumupendeza Bwana Mungu wetu, kondoo wenyi kumujua Bwana wao Mtakatifu na yeye aanawajua ambao zizi haifunguliwe juu ya mbwa-mwitu wanyanganyi, ombeni kwa muchungaji mwema kusudi pamoja na ninyi atupeleke na sisi pia pahali pa mapumziko.

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Mianga ya siri ya Jua la kiroho, enyi Mitume muliomuona Mungu wetu, mumuombe Yeye amwangie roho zetu nuru yake, mutuokoe toka giza ya mateso, kwa sala na maombezi yenu fanyeni kusudi tuweza kuona siku ya wokovu kwa kutakasa mioyo yetu yenye kujeruhiwa na shetani, na tukiokolewa kwa imani tuwaimbie ninyi daima, ninyi ambao neno la hekima liliokoa ulimwengu.

Kama mwana mpotevu nilienda katika inchi ya uovu huko nilitumia vibaya ile mali mapendo yako ya ubaba ulinipa; naungua kwa kukosa matendo mema, tazama nguo gani uhalifu wangu imenivika; ninapoondolewa neema takatifu nakulalamikia*:* Nimekosa, lakini najua wema wako, ee Kristu, kwa rehema yako unipokee kama mumoja wa watumishi wako, kwa maombezi ya Mitume wako wapendwa.

Sauti umoja. Ek deksion tu Sotiros

Enyi Mitume wa Mwokozi, taa za dunia wenye kutupatisha sisi wokovu, na kama mbinguni munavyotangaza utukufu wa Mungu, munapojaa na maajabu na miujiza ya nuru, mutuombee daima kwa Bwana kusudi apokee maombi yetu kama manukato nzuri na atuwezesha kuona na mapendo na kukumbatia Msalaba wake wenyi kuleta uzima*:* Kwa sisi tunasujudu mbele yake, utupe, ee Bwana, rehema yako kwa mapendo yako kwa wanadamu.

Sasa tunaimba wimbo ya Mineon inne.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 51.
Ninatumainia rehema ya Mungu milele na milele.
Shairi*:* Kwa nini unajisifu kwa uovu?

Somo ya Mwanzo tutasoma. (7, 6-9).

Na Noa alikuwa na miaka mia sita wakati garika ya maji ilipokuwa juu ya inchi. Noa akaingia safina, na wana wake, na muke wake, na wake wa wana wake pamoja naye, kwa sababu ya maji ya garika. Ya nyama walio safi na ya nyama wasio safi na ya ndege na ya kila kitu kinachotambaa juu ya inchi, wakaingia safina kwa Noa wawili wawili, mume na muke, sawasawa Mungu alivyoagiza Noa.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 52.
Wakati Mungu anaporudisha wafungwa wa watu wake.
Shairi*:* Mupumbafu amesema moyoni mwake*:* Hakuna Mungu.

Somo ya Mezali tutasoma (9, 12-18).

Kama wewe ukiwa mwenye hekima, una hekima kwa wewe mwenyewe. Na kama wewe ukizarau, utaichukua peke yako. Mwanamuke mupumbafu anapiga kelele; Yeye ni mujinga, wala hajui kitu. Naye anaketi mulangoni mwa nyumba yake, juu ya kiti pahali pa juu pa muji, ili kuita wale wanaopita, wanaipota katika njia zake, kila aliye mujinga ageuke kuingia hapa*:* Naye asiye na ufahamu, anamwambia*:* Maji ya kuiba ni matamu, na mukate unaokuliwa kwa siri unapendeza. Lakini hajui ya kuwa wafu ni pale; ya kama wageni wake ni chini katika Hadeze.

MU KAZI INNE ASUBUI YA JUMA WA TATU

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya sita. Elpis tu kosmu agathi.

Enyi Wafwasi wa Mwokozi wenye kuleta nuru ya kweli duniani kote, angazeni pia roho yangu yenyi kupofuka sababu ya zambi, munifanye mimi kuwa mwana wa nuru mwenye kuchunga amri za wokovu na muniokoe toka giza za inje niwatukuze ninyi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu Mtakatifu wa Kristu Mungu wetu, uliyezaa Muumba wa ulimwengu, umuombe, pamoja na Mitume Watakatifu, Mungu wa wema kusudi tuokolewe toka mateso na tupokee maondoleo ya zambi zetu.

KATHISMA YA TATU.

Sauti ya sita. Angelike dinamis.

Enyi Mitume Watakatifu wenyi kuangaza ulimwengu, angazeni pia wale wenyi kuwatukuza ninyi kwa nyimbo zao; kwa hii Kwarezima tunawaomba ninyi neema ya kuweza kuona na macho yenye kutakaswa muti wa Msalaba wenyi kuleta uzima na kuikumbatia na midomo tukiimba*:* Ee

Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mzaz-Mungu uliye matumaini ya dunia, naomba ulinzi wako ambaye peke yako unastahili heshima, hurumia watu wenye kukimbilia kwako, umuombe Mungu atuonyeshe mapendo yake kwa kuokoa roho zetu toka azabu yote, ee Bikira Mbarikiwa katika wote.

KANUNI

Elezo*: Ya Mineon na kisha pa fasi ya Kontakion tunasoma Wimbo ya Mashahidi (martirikon), Sinaksari ya Watakatifu ya leo, na kisha Fotagogikon na Apostikha.*

APOSTIKHA

Sauti ya sita. Idiomelon.

Nimeanguka toka cheo yangu ya mwana sababu ya uzima niliishi, niliishi sawa mtumwa pamoja na nguruwe bila kuweza kushiba ile walikula, narudi kwa Baba, ee Baba Mwema kamili; safari yangu haikustahili, lakini narudi na unyenyekevu na nakulalamikia kwa moyo wa toba*:* «Baba, nimemukosea Mungu na wewe pia, unipe toba na neema ya wokovu». *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi

Mungu wetu alitenda maajabu katika Watakatifu alichagua. Shangilieni na kufurahiwa ninyi wenye kumutumikia, kwani aliwavika taji katika ufalme wa mbinguni*:* Tunawaomba ninyi musitusahau.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, uko kweli Mzabibu ulistawisha tunda la uzima; ee Bibi yetu tunakuomba; katikati ya Mitume na ya Watakatifu wote ombea roho zetu wokovu.

MU KAZI INNE MANGARIBI YA JUMA WA TATU

Kisha: «Bwana nimekuita. . . »tunaimba wimbo ya Triodi tatu na ya Mineon tatu.

Wimbo ya Triodi

Sauti ya tano. Kheris askitikon.

Ee Mwokozi, uko na upole wa kweli ambao zamani ilituliza uchungu wa maji ya Mera, ikatangulia kuonyesha muti wa Msalaba wako takatifu; waakti ulipotundikwa juu ya hii kwa kutaka kwako, ulionja uchungu wa nyongo na mukuki ikachoma ubavu wako huko ulitirikiza maji yenyi kusafisha zambi za dunia sababu ya kutengeneza upanga wa wanadamu; ndiyo maana tunatukuza uwezo wako isiyokadirika na tunakuomba, ee Bwana*:* Kwa hii wakati wa Kwarezima utupe sisi woga wa Mungu, usamehe wa makosa yetu na neema ya wokovu.

Umoja

Ee Neno uliyepanua mikono Msalabani sababu ya kukusanya wote wale walikuwa mbali na wewe, ondoa roho yangu toka tamaa zake mbaya, uipatie fazilia zote, leta woga moyoni mwangu wote wa kukuogopa wewe na rohoni mwangu ukamilifu wa mapendo yako kusudi nikiacha upendeleo wa mwili wangu, nikupendeze hii wakati kwa kufunga, sala na maombi na kwa siku nitakapoona kwa furaha Ufufuo wako takatifu nipokee neema ya wokovu

Sauti ya kwanza. Nefelin se fotos.

Ee Kristu na Neno la Mungu, tunapomaliza juma ya tatu ya Kwarezima takatifu, utupe sisi kuona muti wa Msalaba wako wenyi kuleta uzima na kusujudu mbele yake, tuimbie kama inavyostahili na kutukuza uwezo wako, kushangilia Mateso yako na kuona kwa usafi wote utukufu wako tukufu na takatifu, paska ya siri ambako Adamu anarudi katika Paradizo.

Sasa tunaimba wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya mnane. Zaburi 55.

Unirehemu, ee Mungu, kwa sababu mutu alitaka kunimeza. .
Shairi*:* Adui zangu wanataka kunimeza muchana kutwa.

Somo ya Mwanzo tutasoma (7, 11-8, 3).

Kwa mwaka wa mia sita wa maisha ya Noa, kwa mwezi wa pili, kwa siku ya kumi na saba ya mwezi, kwa siku yenyewe chemchemi zote za vilindi vikubwa zikavunjika, na madirisha ya mbingu yalifunguliwa. Mvua ilikuwa juu ya dunia siku makumi ine, muchana na usiku. Siku yenyewe Noa na Semu na Hamu na Yafeti, wana wa Noa, na muke wa Noa, na wake watatu wa wana wake pamoja naye, wakaingia safina, wao na kila nyama kwa namna yake,
na ngombe zote kwa namna yao, na kila kitu kinachotambaa juu ya inchi kwa namna yake, na kila ndege kwa namna yake, kila ndege ya kila namna. Waka-ingia safina kwa Noa, wawili wawili wa miili yote iliyokuwa na pumuzi ya uzima. Nao wakaingia mume na muke wa miili yote, sawasawa Mungu alivyo-mwagiza ; Bwana akamufunga ndani. Na garika ilikuwa siku makumi ine juu ya dunia, maji yakaongezeka, yakabeba safina, ikapandishwa juu ya inchi. Maji yakashinda, yakazidi sana juu ya inchi; safina ikaendelea juu ya uso wa maji. Maji yakashinda sana sana juu ya inchi; na milima mirefu yote iliyo chím ya mbingu nzima ilifunikwa. Maji yakashinda mikono kumi na mitano kwa urefu juu, milima ikafunikwa. Miili yote iliyotambaa juu ya inchi ikakufa, ndege, na ngombe, na nyama, na kila kitu kinachotambaa juu ya inchi, na kila mutu; wote waliokuwa na pumuzi ya roho ya uzima kwa pua yao, wa wote waliokuwa katika inchi kavu, wakakufa. Na kila kitu kilicho hai kiliharibiwa kilichokuwa juu ya uso wa inchi, mutu na ngombe na kitu cha kutambaa, na ndege za anga; wakaharibiwa toka dunia. Noa tu akabaki, nao walio pamoja naye ndani ya safina. Maji yakashinda juu ya dunia siku mia moja makumi tano. Na ilikuwa kwa mwaka wa mia sita na moja, kwa mwezi wa kwanza, kwa siku ya kwanza ya mwezi, maji yamekauka juu ya inchi ; Noa akaondosha kifuniko cha safina, akaangalia, na tazama, uso wa inchi umekauka. Kwa mwezi wa pili, kwa siku ya makumi mbili na saba ya mwezi, inchi imekuwa kavu Mungu akakumbuka Noa, na kila kitu kilicho hai, na nyama zote waliokuwa pamoja naye ndani ya safina. Mungu akapitisha upepo juu ya dunia, na maji yalipunguzwa; chemchemi vilevile za vilindi na madirisha ya mbingu yakafungwamvua toka mbingu ikazuizwa; maji yakarudirudi toka inchi; nanyuma ya siku mia moja makumi tano maji yalipunguka.

Prokimenon. Sauti ya saba. Zaburi 56.
Unirehemu, ee Mungu, unirehemu; maana nafsi yangu imekukimbia wewe.
Shairi*:* Ndiyo, nitakimbilia kivuli cha mabawa yako.

Somo ya Mezali tutasoma (10, 1-22).

Mwana mwenye hekima anafurahisha baba yake*:* Lakini mwana mupumbafu ni mugizo wa mama yake. Hazina za uovu hazifai kitu, lakini haki inaokoa na mauti. Bwana hataacha nafsi ya mwenye haki kufa kwa njaa*:* lakini anasukuma mbali tamaa ya mwovu. yeye anayetenda kwa mukono mulegevu anageuka kuwa masikini*:* Lakini mukono wake aliye na bidii unatajirisha. Mwenye kukusanya kwa wakati wa hari ni mwana mwenye hekima, lakini yeye anayelala kwa wakati wa mavuno ni mwana anayepatisha haya. Baraka ni kichwani mwake aliye haki*:* Lakini jeuri inafunika kinywa cha waovu. Ukumbusho wa wenye haki una baraka lakini jina la waovu litaoza. Wenye moyo wa hekima watapokea maagizo*:* Lakini mupumbafu mwenye maneno mengi ataanguka. Mwenye kutembea katika haki anatembea pasipo hatari*:* Lakini mwenye kupotosha njia zake atajulikana. Mwenye kukonyeza kwa jicho analeta huzuni*:* Lakini mupumbafu mwenye maneno mengi ataanguka. Kinywa cha wenye haki ni chemchemi ya uzima*:* Lakini jeuri inafunika kinywa cha waovu. Kuchukia kunaamsha magomvi*:* Lakini mapendo yanafunika makosa yote. Midomoni mwake aliye na ufahamu hekima inapatikana*:* Lakini fimbo ni kwa mugongo wake asiye na ufahamu. Wenye hekima wanaweka akiba ya maarifa*:* Lakini kinywa cha wapumbafu ni uharibifu ulio karibu. Mali ya tajiri ni muji wake wa nguvu*:* Uharibifu wa maskini ni umasikini wao. Kazi ya mwenye haki inaleta uzima; Mazidio ya waovu yanaleta zambi. Mwenye kusikia kukemea ni katika njia ya uzima*:* Lakini mwenye kuacha maonyo

anakosa. Yeye anayeficha kuchukia ni mwenye midomo ya uwongo; naye anayesingiza ni mupumbafu. Katika wingi wa maneno maovu hayakosi*:* Lakini mwenye kuzuiza midomo yake anatenda kwa hekima. Ulimi wa mwenye haki ni kama feza nzuri sana*:* Moyo wa mwovu haufai kitu. Midomo ya wenye haki inakulisha watu wengi*:* lakini wapumbafu wanakufa kwa kuwa hawana ufahamu. Baraka ya Bwana inatajirisha. Wala hachanganyi huzuni nayo.

APOSTIKHA

Sauti ya sita. Idiomelon.

Ee Kristu Mungu wetu uliye uzima wa wote, ulipotundikwa Msalabani, leta uzima rohoni mwangu yenyi kuteswa juu ya zambi, ee Mchungaji Mwema, usiache kondoo wako mwenye kupotea, kwani niliacha amri zako, kwa zambi zangu nimetumia vibaya mali ya utakaso ulinipa, nimeiharibu kwa uzima niliishi, lakini kwa wema wako wa pekee unirudishie na kufanya upya roho yangu. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi

Ee Bwana, Mashahidi wako hawakukukataa, hawakujitenga toka kanuni zako*:* Kwa maombezi yao utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Kristu wakati alikuona umesulubiwa Msalabani, huyu alikuzaa akapaza sauti na kusema*:* Mwanangu, ni muujiza gani wa ajabu ninaona machoni mwangu, namna gani unaweza kufa mwilini mwenye kutundikwa Msalabani wewe uliye Mfalme wa Uzima?

MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA WA TATU

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mukongo ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon.

Zamani tulipoonja mauti katika muti uliyokataziwa, tulipata uzima katika muti wa Msalaba; kwa uwezo wake, ee Mungu wa mapendo, utupe sisi nguvu ya kupitisha hii Kwarezima katika machozi na sikitiko sababu ya kutimiza mapenzi yako na kuona siku ya Ufufuo wako takatifu na wa nuru.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, alipokuona umetundikwa msalabani katikati ya Wanyanganyi, Mama yako, kwa moyo wenye kuvunjika, akapaza sauti*:* Ee Mwanangumpendwa, namna gani unateswa Msalabani mateso ya waovu wewe uliye bila zambi? Lakini kwa wema wako kubwa unataka kuwarudishia wanadamu uzima.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.

Ee Bwana, mwili wenyi kutakaswa kwa kiasi, roho yenyi kuangazwa kwa sala utustahilishe kuona Msalaba wako heshimiwa na takatifu, tusujudu mbele yake na kuimba*:* Utukufu kwa Msalaba wako wenye kuleta uzima, utukufu kwa Mkuki takatifu yenyi kutufungulia uzima na mapendo unapenda nayo wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Neno, kondoo jike alipoona Msalabani Mwana-kondoo wake ametundikwa katikati ya Wanyanganyi na ubavu wenye kuchomwa Mkuki, akalia na kuomboleza akisema; Ee Mwanangu, hii ni muujiza gani wa ajabu? Namna gani kaburi inaweza kumufunika Mungu wa milele? Isiyokadirika ni tendo lililotimizika! Usiniache, ee Mwanangu mpendwa.

KANUNI

Ya Mineon na kisha pa fasi ya Kontakion tunasoma Wimbo ya Mashahidi (martirikon), Sinaksari ya Watakatifu ya leo, na kisha Fotagogikon na Apostikha.

APOSTIKHA

Sauti ya sita. Idiomelon.

Nilitumia vibaya mali ya zawadi ya baba, nilichoma uzima wangu kwa furaha, nimenaswa kwa akili ya zambi kwa kutamainia uzuri wa tamaa, nimefanana na wanyama wasio na akili waakti nilivunja amri za wokovu; ee Kristu uliyetundikwa Msalabani kwa ajili yangu, usinikatalie uwana takatifu, lakini unipokee kama Mwana mupotevu na uniokoe. *(mara mbili).*

Ee Bwana, kwa kuwakumbuka Mashahidi wako ni siku Kuu ya shangwe kwa viumbe vyote*:* Dunia ya wanadamu inashangilia pamoja na Malaika mbinguni; kwa maombezi yao utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili ulipokuona umetundikwa Msalabani akalia na kulalamikia*:* Ee Mwanangu na Mungu wangu, ee Mwanadamu mpendwa, namna gani unaweza kuteswa mateso yasiyo na haki?

MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA WA TATU.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo kumi. Wimbo ifwatayo tunaiimba mara mbili.

Wimbo ya Triodio: Sauti ya saba.

Ee Bwana, nilijitenga mbali ya neema yako kama Mwana mupotevu, nilitumia vibaya mali ya wema wako, lakini narudi kwako na nakulalamikia*:* Ee Bwana, nimekosa unihurumie. *(mara mbili).*

Kisha wimbo inne ya Mashahidi ku mwisho ya hii Kitabu na inne ya Mineon.

KUINGIA.

Mwanagaza upole. . .

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 59.

Kwa sababu ya Mungu tutaenda kwa uhodari; maana ni yeye atakayekanyaga watesi wetu.

Shairi*:* Ee Mungu umetutupa, umetuangusha.

Somo ya Mwanzo tutasoma (8, 4-21).

Na mwezi wa saba, siku ya kumi na saba ya mwezi, safina ililala juu ya milima ya Ararati. Maji yakapungukapunguka hata mwezi wa kumi; kwa mwezi wa kumi, kwa siku ya kwanza ya mwezi, vichwa vya milima vilionekana. Na ilikuwa kwa mwisho wa siku makumi ine Noa akafungua dirisha la safina alilolifanya; akatoa kunguru akatoka kwenda na kurudi hata maji yalikauka juu ya inchi. Akatoa hua toka kwake kuona ya kama maji yame-punguka juu ya uso wa inchi ; 9 lakini hua hakukuta pahali pa pumziko kwa wayo wa muguu wake, akarudi kwake kwa safina, kwani maji yalikuwa juu ya uso wa dunia nzima; akanyosha mukono wake, akamutwaa, akamwmglza pamoja naye ndani ya safina. Akangoja tena siku saba nyingine; akatoa tena hua toka safina; hua akaingia kwake mangari bi; na tazama, kinywani mwake majani ya muzeituni yaliyoondoshwa; hivi Noa akajua ya kama maji yamepunguka katika inchi. Akangoja tena siku saba nyingine, akatoa hua; hakurudi kwake tena. Noa akajenga mazabahu kwa Bwana*:* akatwaa ya kila nyama aliye safi, na ya kila ndege aliyé safi, akatoa zabihu ya kuteketezwa juu ya mazabahu. Bwana akasikia harufu tamu; Bwana akasema moyoni mwake*:* Sitalaani inchi tena kwa sababu ya mutu, kwa maana mawazo ya moyo wa mutu ni mabaya tangu ujana wake; wala

sitapiga tena kila kitu kilicho hai sawasawa nilivyofanya.

Prokimenon. Sauti ya sita. Zaburi 60.

Sikia kilio changu, ee Mungu; usikilize maombi yangu.

Shairi*:* Hivi nitaimbia jina lako sifa kwa milele.

Somo ya Mezali tutasoma (10, 31-11, 1-12).

Kinywa cha wenye haki kinatoa hekima*:* Lakini ulimi wa ukaidi utakatiliwa mbali. Midomo ya wenye haki inajua yanayokubaliwa*:* Lakini kinywa cha waovu kinatoa ukaidi. Mizani ya udanganyifu ni machukizo kwa Bwana*:* Lakini vipimo vilivyo sawasawa vinamupendeza. Wakati majivuno yanapokuja, halafu haya inakuja*:* Lakini hekima ni pamoja na wanyenyekevu. Haki ya wenye haki itawaongoza*:* Lakini ukaidi wao walio wadanganyifu utawaharibu. Mali hazina faida kwa siku ya gazabu*:* Lakini haki inaokoa na mauti. Haki ya mukamilifu itaongeza njia yake*:* Lakini mwovu ataanguka kwa uovu wake mwenyewe. Haki ya wenye haki itawaokoa, Lakini wale wanaotenda kwa hila watanaswa kwa hila yao wenyewe. Wakati mwovu anapokufa, taraja yake itapotea*:* Na matumaini ya uovu yanapotea. Mwenye haki anaokolewa na taabu, Na mwovu anaingia pahali pake. Kwa kinywa chake yeye asiyeogopa Mungu anaharibu jirani yake*:* lakini wenye haki wataponyeshwa kwa hekima. Wakati wenye haki wanapositawi, muji unafurahi*:* Na wakati waovu wanapopotea, watu wanapiga kelele. Kwa baraka ya wenye haki muji unatukuzwa*:* lakini unaangamizwa kwa kinywa cha waovu. Yeye anayechukia jirani yake anakosa hekima*:* Lakini mutu wa ufahamu ananyamaza.

MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA TATU

Elezo*: Kisha Eksapsalmos tunaimba Alliluia, katika desturi na kisha Apolitikion hii:*

Sauti ya mbili.

Mitume, Manabii na mashahidi, Maaskofu Watakatifu na wenye haki wote, ninyi muliyolindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Bwana, kwa wema wako uwakumbuke, watumishi wako na wenye haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mama wa Nuru isiyokadirika, kama Malaika mbinguni tunakuimbia kwa kukutukuza.

Elezo: *Kathisma ya kitabu Paraklitiki na sauti ya hii juma.*

Kisha tunaimba Kathisma ya wafu. Ni hii:

Sauti ya tano

Ee Mungu Mwokozi, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu, pamoja na wenye haki pumzisha watumishi wako na uwaruhusu wakae katika uwanja wako, usihesabie makosa yao ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Utukufu kwa Baba. . .

Ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Kristu Mungu wetu uliyezaliwa kwa Bikira sababu ya kuangazia ulimwengu, kwa maombezi yake utufanye sisi kuwa wana wa nuru, ee Bwana, utuhurumie.

KANUNI

Elezo: *Tunaimba Kanuni ya Mineon, pa fasi ya Kontakion tunasoma wimbo ya mashahidi (Martirikon), Sinaksarion ya Watakatifu ya leo, Uliye wathamani, Fotagogikon,Masifu na Apostikha ya Paraklitiki ya hii siku.*

MU JUMA WA TATU YA KUSUJUDU MSALABA WA KRISTU

MU POSHO MANGARIBI KWA ESPERINOS KUBWA

Elezo*: Kisha Zaburi ya Proimiakos, tunaimba* «Bwana nimekuita. . . . » *na kisha tunaimba na ma shairi kumi, wimbo sita ya Ufufuo ya Kristu ku Kitabu Paraklitiki na kisha wimbo inne ya Kusujudu Musalaba wa Kristu.*

Sauti ya tano. Kheris askitikon.

Ee Msalaba wa Bwana kuleta uzima, unapoangaa na nuru ya neema yako, angaza mioyo ya wale wenyi kukutukuza na kukukumbatia na imani; katika wewe machozi ya macho yetu yamekauka katika wewe tunatoka salama katika mtego wa Hadeze, katika wewe tunasharikia furaha ya milele; onyesha nuru ya uzuri wako, leta zawadi zako na mema yako kwa waaminifu wenyi kuomba na imani ulinzi wako wa uwezo na neema ya wokovu.

Salamu, Msalaba wa Bwana wenyi kuleta uzima, paradizo ya Eklezya na muti mupya wa uzima wenyi kutupatia furaha ya utukufu wa milele; katika wewe majeshi ya mashetani yanafukuzwa, katika wewe Malaika wanafurahiwa mbinguni, kwa ajili yako makutano ya waaminifu wanashangilia, wewe uliye silaha ya ushindi, mnara isiyokamatwa, usabiti wa waongozi na nguvu ya wafalme, utupe sisi kuona tangu sasa mateso ya Kristu na Ufufuo wake takatifu.

Salamu, Musalaba wa Bwana wenyi kuleta uzima, ushindi wa imani, mulango ya Paradizo, boma la Eklezya na msaada wa waaminifu; katika wewe nguvu ya mauti imeondolewa, katika wewe laana ya kale imeondolewa, katika wewe tumeinuliwa toka dunia mpaka mbinguni; silaha ya ushindi yenyi kufukuza mashetani, bandari ya wokovu na adui wa mashetani, pambo bora la wenye haki na la watakatifu, ulete neema ya wokovu duniani.

Furahi, ee jozi la kwanza la wanadamu ambalo Adui kwa chuki aliangusha zamani toka furaha ya juu mbinguni kwa furaha ya uchungu kwa kula tunda la mauti uliyokataziwa*:* Tazama imejongea muti mupya ya uzima; kujeni mbio sababu ya kuikumbatia na furaha na ilalamikieni na hii sauti ya imani yenu*:* Musalaba heshimiwa, uko msaada wetu, tunda lako linatupatia uzima wa milele, matumaini ya paradizo na neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . . *Sauti ya tatu*

Ee Kristu Mungu wetu uliyekubali kusulubiwa msalabani sababu ya ufufuo wa wanadamu, msalabani kwa damu yako uliandika hati ya wokovu wetu; usituzarau katika hatari inatuhatarisha kujitenga mara ingine na wewe; kwa wema wako hurumia watu wako tulio katika hatari, simama na shindana na adui zetu, ee Bwana Mwenyezi.

Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION YA PARAKLITIKI**

KUINGIA
PROKIMENON
MU IBADA YA LITIA

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya tano.*

Vilivyokuona umetundikwa bila nguo msalabani wewe Muumba wa ulimwengu, viumbe vyote vikaogopa, jua halikutoa nuru yake, mawe yakapasuka, inchi ikatetemeka, na pazia ya hekalu ikapasuka vipande mbili; wafu wakafufuka kaburini mwao na majeshi ya juu mbinguni yakashangaa na kusema*:* Ni ajabu! Tazama Mwamzi anahukumiwa na kuteshwa kwa kutaka kwa

ajili ya wanadamu na ya upya wao.

APOSTIKHA

Elezo*: Apostikha tunaimba ku Kitabu ya Paraklitiki.*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Sauti ya ine.

Ee Bwana uliyemusaidia Daudi katika vita sababu ya kushinda wapagani, utusaidie na sisi kwa silaha ya Msalaba wako sababu ya kufukuza adui zetu; utuonyeshe mapendo yako kama zamani kusudi watu watambue kweli ya kama uko Mungu wetu na ya kama ushindi wetu inatoka kwako; na Mama yako Mtakatifu aombe imara ili tupewe neema ya wokovu.

Elezo*:* *Kisha Trisagion tunaimba Apolitikion ya Ufufuo na kisha hii:*

Apolitikion ya Musalaba. *Sauti ya tatu.*

Ee Bwana, okoa taifa yako na bariki urizi wako. Ukiwapa wafalme kushinda juu ya wakafiri, na kuilinda jamii yako kwa Msalaba wako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION** ya Paraklitiki na sauti ya apolitikion wa juu**.**

MU JUMA YA MSALABA KWA ASUBUI

Elezo*:* *Kisha Eksapsalmos tunaimba Bwana ndiwe. . . na Apolitikion ya Ufufuo na Musalaba na kisha. Theotokion ya Ufufuo ya Kristu, Sauti ya kwanza. Kisha padri anasema Ektenia Kidogo na waimbaji wanaimba Kathisma ya Paraklitiki. Kisha:*

KATHISMA YA MUSALABA

Sauti ya mnane. To prostakthen.

Zamani adui aliniondoa katika Paradizo; alinilisha tunda la muti akaingiza mauti; lakini duniani ikapandwa muti wa Musalaba, inawapa wanadamu nguo ya uzima na dunia yote inajaa na furaha; tunapoona Msalaba inatukuzwa, wote tumulalamikie Bwana kwa sauti moja*:* Hekalu yako imejaa na utukufu wako!

ANAVATHMI YA SAUTI YA HII JUMA
EVANGELION YA ASUBUI

Tukiona ufufuo wa Kristu, . . .

Utukufu kwa Baba. . .

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana chemchem ya uzima;. . . . . .

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya mnane.*

Uniongoze njiani ya wokovu, ee Mzazi-Mungu, ...

Sauti ya sita

Unirehemu, ee Mungu sawasawa ni wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uufute makosa yangu.

Nikikumbuka wingi wa matendo yangu mabaya, ...

KANUNI YA UFUFUO WA KRISTU
KANUNI YA SIKU KUU YA MUSALABA

Sauti ya kwanza. Anastaseos imera.

Wimbo wa kwanza

Ni siku ya shangwe mbinguni, kwani mauti imefutwa kwa ufufuo wa Kristu; uzima inaonekana mara ingine na Adamu mfufuliwa anashangilia kwa furaha. Wote tuimbie ushindi wa Bwana.

Ni siku tunasujudu mbele ya Musalaba wenye kuleta uzima*:* Kujeni wote, tuisujudie, yenyi kuangaa na nuru ya ufufuo takatifu, inajitoa machoni mwetu*:* tuikumbatie na furaha ya Roho.

Ee Musalaba kubwa wa Bwana wangu, onekana, unifunulie hali takatifu ya uzuri wako; unifanye mimi kuwa mwenyi kuabudu utukufu wako takatifu*:* Kama wewe ni muzima, nakuomba na kukuheshimu.

Duniani kama mbinguni wote kwa sauti moja waimbie Musalaba takatifu wenye kuonekana machoni mwa wote; Juu ya hii Kristu alisulubiwa mwilini kama sadaka*:* Tuikumbatie na furaha ya Roho.

Utukufu kwa Baba. . .

Umungu wenyi uso tatu, Umoja Takatifu, Baba, Mwana na Roho Mutakatifu, wenyi uwezo moja ma mapenzi moja, linda ulimwengu kwa kuipatia amani.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira usiyolewa, bila mbegu ulipata mimba ya Muumba wa ulimwengu, Kristu Mungu wetu kwa namna ya ajabu*:* Umuombe alete amani duniani.

Wimbo wa tatu. *Defte poma piomen kenon.*

Kujeni, tuimbe wote wimbo mupya sababu ya kushangilia kushindwa kwa Hadeze, kwani Kristu alipotoka kaburini aliharibu nguvu ya mauti na kuokoa ulimwengu wote.

Kujeni, wote tushote na imani apana kwa kisima huko kunatiririka uovu mingi, lakini katika Chemchem ya nuru, tukiusujudu Musalaba wa Kristu ambaye katika tunajitukuza.

Tunaposujudu sasa Musalaba ambao Musa zamani alitangulia kuonyesha katika mikono yake, tunafukuza Amaleki na tunaokolewa sisi pia.

Tunapotakasa macho yetu na midomo yetu sababu ya kuimbia furaha ya mioyo yetu, tusujudie na imani Musalaba wa Bwana, furaha yetu isikilike.

Utukufu kwa Baba. . .

Katika Uso tatu natukuza Mungu mumoja asiye na mwanzo na bila kugawanyika*:* Baba, Mwana, na Roho Mutakatifu ambao tunabatizwa kwa jina lao.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira, zamani Musa aliona kichaka cha moto bila kuteketezwa fumbo yako ilitangulia kuonekana, kwa sababu vivyo hivyo tumbo yako ilichunga, bila kuteketezwa, moto ya umungu.

KATHISMA

Sauti ya sita.

Ee Bwana, Musalaba wako imetakaswa*:* inaponyesha wale waliregea katika zambi; katika hii tunakuomba*:* Utuhurumie.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu, musujudu mbele ya kiti chake, kwani yeye ni Mutakatifu.

Ee Bwana, leo Neno la Nabii limetimizika*:* Tazama tunasujudu pahali paliwekwa miguu yako; tulipoonja muti wa wokovu, tuliokolewa toka mateso yetu na zambi kwa maombezi ya Mzazi-Mungu.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Kristu, tangu ilisimikwa muti wa Musalaba wako, uliregeza makao ya mauti; Hadeze ilijiharakisha kumeza huyu ilitapika kwa woga. Ee Mungu Mutakatifu, ulituonyesha wokovu, tunakutolea utukufu*:* Ee Mwana wa Mungu, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Ee Mzazi-Mungu na Bikira Mutukufu, umuombe Mwana wako, Kristu Mungu wetu aliyekubali kusulubiwa Msalabani na kufufuka katika wafu, sababu ya wokovu wa roho zetu.

KONTAKION

Tangu sasa upanga ya moto hailinde mulango ya Edeni, kwa sababu muti ya Musalaba inaizuia kuwaka; miiba ya mauti inaondolewa makali, Hadeze inaondolewa ushindi; ee Mungu Mwokozi, ulikuja kuwaambia wafungwa wa Hadeze*:* Ingieni mara ingine katika Paradizo.

IKOS

Pilato aliweka Misalaba tatu ku Gulgota, mbili ya Wanyanganyi na moja ya Mufalme wa uzima; ilipoona hivi, Hadeze ikawaambia Watumishi wake; ni nani aliniweka hii muti moyoni? Mukuki ya miti imenichoma na napasuka; maumivu gani inaingia tumboni m, wangu na mwilini mwangu, mateso gani inateswa roho yangu! Ninapasha kutapika Adamu na wana wake, wale nilipokea kwa muti uliyokataziwa, kwa sababu muti mupya inawaongoza waingie mara ingine katika Paradizo.

SINAKSARION

Elezo: *Tunasoma ya kwanza Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha hii ya chini.*

Leo, siku ya tatu ya kufunga, tunashangilia usujudu wa msalaba wa wamani na wenyi kuleta uzima.

Dunia yote inasujudu mbele yako, Ee Neno, pakuabudu Msalaba wako wenyi kuleta uzima. Kwa uwezo wake, ee Kristu Mungu wetu, utulinde ku hila ya Mwovu, utufanye wastahili wa kuabudu Mateso yako kimungu na Ufufuo wako wenyi kuleta uzima, kisha kumaliza muda wa siku makumi ine, na utuhurumie, katika wema wako wa pekee na mapendo yako kwa wanadamu.

KATAVASIA

Sauti ya kwanza.

Wimbo ya kwanza.

Ee Kristu Mungu wetu, zamani Musa alitangulia kuonyesha mfano wa Msalaba wako wa zamani na Takatifu wakati alipofungwa bahari Nyekundu na fimbo yake na akapitisha Waisraeli wakiimba ushindi wa Bwana.

Wimbo ya tatu.

Ee Kristu Bwana, unisabitisha pa mwamba wa imani kwa nguvu ya Msalaba wako ili roho yangu isiyumbeyumbe ku mshale wa Adui, kwani peke yako ndiwe Mtakatifu na Bwana.

Wimbo ya ine.

Ee Mungu Mwenyezi, wakati Jua lilipokuona umeteswa Msalabani, likaogopa na likazuia nuru ya miangaza yake, lakini kiumbe yote ikaimba na woga uvumilivu wako na dunia ikajaa na Sifa yako. Bwana.

Wimbo ya tano.

Tutangulie alfajiri. Bwana wa ulimwengu, tunakuimba kwani Msalaba Wako ulitupatia amani; katika hii ulifanya ubinadamu kuwa upya ambao uliyoongoza ku nuru ya milele.

Wimbo ya sita.

Yona alipopanua mikono tomboni mwa samaki akatangulia kuonyesha mfano wa Msalaba wako Takatifu, na alipotoka tumboni mwa samaki akaokoka, ee Neno, kwa uwezo wako mkuu.

Wimbo ya saba.

Huyu aliyeokoa Vijana ku tanuru ya moto alichukua mwili na alishuka duniani; alipoitika kusulibiwa Msalabani, akatupatia wokovu; ndiye Mungu wa Baba zetu, baraka na Utukufu ni Kwake peke yake.

Wimbo ya mnane.

Tunamusufu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Alipotupwa katika shimo la Simba. Nabii Danieli akapanua mikono mu alama ya msalaba na hakuwa mateka ya meno yao.

Wimbo ya tisa.

Bikira Mzazi-Mungu ambaye kweli ulizaa Kristu Mungu wetu bila mbegu, huyu aliyeinuliwa msalabani, sisi waaminifu, wote pamoja kama yeye sasa tunakutukuza.

EKSAPOSTILARION YA UFUFUO YA KRISTU
YA MUSALABA

Sauti ya pili. Tis mathites.

Leo tumeona Musalaba heshimiwa wa Kristu imewekwa*:* Tunapoisujudia, tutukuze na furaha na tumuombe Bwana aliyesulibiwapo neema ya kuweza kuona Ufufuo wake takatifu na heshimiwa.

THEOTOKION

Ee Bikira, sasa tunasujudu mbele ya Musalaba huko Mwana wako alipanua mikono yake takatifu kwa ajili ya wokovu wetu, utupe amani ili tuweze kuona Mateso takatifu yaliyotuokoa na kwa Paska ya Bwana siku ya nuru yenyi kufurahisha ulimwengu yote.

MASIFU

Sauti ya ine. Os geneon en martisin

Tusikilizishe nyimbo za shangwe na kwa mashairi yetu tutukuzeni Musalaba heshimiwa; tuilalamikieni kwa kuikumbatia*:* Ee Musalaba heshimiwa, kwa uwezo wako takasa roho zetu na miili yetu na linda kwa vidonda vya Adui waaminifu wenye kusujudu mbele yako.
(mara pili).

Shairi: Mungu ni mufalme wetu tangu zamani, anatimiza wokovu duniani.

Kujeni mushote maji isiyokauka ambayo neema ya Musalaba inachemusha. Tazama imewekwa machoni mwetu muti takatifu kamili, chemchem kunakotiririka neema iliyopewa kwa damu na maji ya Bwana wa ulimwengu aliyeinuliwa msalabani kwa kutaka kwake sababu ya kutukuza wanadamu pamoja naye.

Shairi: Tukuzeni Bwana-Mungu wetu, musujudu mbele ya kiti chake, kwani yeye ni Mutakatifu.

Tegemeo imara ya Eklezya, nguvu ya Wafalme, ulinzi na matumaini ya Watawa, ee Msalaba heshimiwa, tunasujudu leo mbele yako ambao tunaangazwa rohoni na mwilini mwetu kwa neema ya huyu alisulubiwa juu yako, akaharibu nguvu ya adui na kuondoa laana ya kale.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane*

Kwa mifano Bwana wa ulimwengu anatufundisha namna gani inafaa kujilinda na majivuno ya Wafarisayo; anatuonya juu ya majivuno na anatupa mufano akijishusha mpaka kufa, kufa msalabani. Kwa kumushukuru, tuseme pamoja na Mtoza-kodi*:* Wewe uliyeteswa kwa ajili yetu na kukaa mvumilivu kama Mungu, utuokoe kwa mateso yetu na okoa roho zetu.

Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION**

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA

Elezo*: Hile wakati waimbaji wanaimba:* «Mungu Mutakatifu. . . » *wa mwisho ya Doksologia kubwa padri anafukiza na chetezo Sahani Takatifu pa Meza Takatifu, pahali ni kati Musalaba na maua ya mbali-mbali pempeni yake. Kisha anakamata na mikono yake Sahani na maua juu yake na anatembea inje katika mulango wa kaskazini. Mutoto moja anafukiza na chetezo ku mbele. Padri anasimama katikati ya kanisa pahali ni meza. Atasimama mbele ya hii meza atasema: Hekima. Simameni. Kisha anafukiza Musalaba na anaimba:* **Ee Bwana, okoa, taifa wako. . .**
Kisha wanaimba waimbaji mara moja-moja na padri na shemasi pamoja wanaimba hii wimbo: **«Ee Bwana, tunasujudu mbele ya Musalaba wako na tunatukuza Ufufuo wako takatifu»** *na wanasujudu Musalaba. Kisha wanabusu Musalaba waaminifu wote mbili-mbili na waimbaji wanaimba hii wimbo:*

Sauti ya mbili

Ninyi waaminifu, kujeni tusujudu mbele ya Musalaba wenye kuleta uzima ambapo mfalme wa utukufu, Kristu, alipanua mikono yake kwa kutaka kwake sababu ya kutuinua mpaka kwa furaha yetu ya zamani adui alituondolea juu ya raha ya uchungu kwa kutufukuza mbali ya Mungu. Kujeni, ninyi waaminifu, tusujudu mbele ya muti yenyi kutuwezesha kuponda kichwa cha adui asiyeonekana. Kujeni, ninyi jamaa ya mataifa yote, kwa nyimbo zetu tutukuzeni Musalaba wa Bwana*:* Salamu, ee ukombozi kamili wa kosa la Adamu, salamu, ee Musalaba tukufu; tunapojaa na woga, tunakukumbatia tukitukuza Mungu wetu na kumwambia*:* Ee Bwana, wewe uliyesulubiwa Msalabani, utuhurumie kwa wema na kwa mapendo yako kwa wanadamu.

Sauti ya mnane

Leo Mufalme wa utukufu, Rabi wa ulimwengu, anasulubiwa Musalabani kwa kutaka kwake, mukuki inachoma ubavu wake; anaonja nyongo na siki, huyu ndani yake Eklezya inapata wema wake, anavikwa taji ya miiba huyu mwenyi kufunika mbingu na mawingu; anavikwa nguo ya zihaka na anapigwa makofi kwa watu huyu aliyeumba wanadamu kwa mikono yako; anapigwa fimbo mkongoni huyu mwenyi kuvika mbingu na mawingu, anapingwa makofi na wanamutemea mate, wanamutukana, anateswa hii yote sababu ya kuokoa wanadamu toka mauti, kwa sababu yeye ni Mukombozi wangu na Mungu mwenye huruma.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane*

Leo Bwana msiyekaribika amenikaribisha karibu yake, anateswa Mateso yake sababu ya kuniondolea zambi zangu; huyu mwenyi kuponyesha vipofu anatemewa mate kwa midomo ya makafiri na anapigwa fimbo sababu ya kuokoa wafungwa. Bikira, mama yake alipomuona Msalabani akamwambia akilia*:* Ole wangu, ee Mwanangu mpendwa, wewe mwenye kupita mwanadamu wote kwa wema unaoneklana bila uzuri, bila neema, bila hali nzuri na bila uzima. Ole wangu! Ee Nuru ya macho yangu, upanga inachoma moyo wangu na tumbo langu linateswa kwa kukuona hivi! Natukuza na kuimbia Mateso yako, naabudu rehema yako ya milele, ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya sita*

Leo neno la Nabii limetimizika*:* Tazama, ee Bwana, tunasujudu pahali paliwekwa miguu yako; tulipopenda muti wa wokovu tuliokolewa toka mateso yetu na toka zambi kwa maombezi ya Mzazi-Mungu.

SIKU YA YENGA MANGARIBI KWA ESPERINOS

Elezo*: Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo kumi; Wimbo sita ya hii inafwata na wa tatu ya Mineon.*

Sauti ya mnane. Kirie, i ke kritirio.

Ee Bwana uliyepanua mikono yako Msalabani kwa kutaka kwako, utupe sisi toba sababu ya kuiabudu kama inavyostahili, angazia mioyo yetu na nuru yako kwa kufunga na sala, kiasi na matendo mema, kwani wewe ni Mwema na Mpenda-wanadamu.

Ee Bwana, kwa mapendo yako kubwa zima zambi zangu nyingi, katika hii juma mupya ya Kwarezima ya nuru uipe roho yangu yenye kutakaswa kuona na kuabudu Musalaba wako Takatifu, ee Bwana Mpenda-wanadamu.

Sauti ya tatu.. Megiston thavma. Idiomelon

Hii ni ajabu kupita maajabu yote ya zamani! Tunaona muti alisulubiwa Kristu mwilini mwake; kwa nuru yake watu wanasujudu na kulalamika*:* Ee uwezo wa Musalaba! Kuonekana kwake kunafukuza mashetani, mufano yake inawaunguza kama moto. Ee Musalaba heshimiwa, nakutukuza, nakuheshimu na kwa woga nasijudu mbele yako, natukuza Mungu sababu ya uzima wa milele ananipa kwa ajili yako.

Wimbo ya Mineon tatu. Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION** ya Mineon.

KUINGIA.

Mwangaza upole. . .

Mangaribi Prokimenon*:*

Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

Shairi: 1)Toka mwisho wa dunia nitakuita.

Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

Shairi: 2)Nitakimbilia maficho ya mabawa yako.

Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

APOSTIKHA.

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Mimi ni mwenye mateso, sisubutu kuinua macho mbinguni sababu ya matendo yangu mbaya; lakini kama Mtoza-kodi nalia na kupaza sauti*:* Ee Bwana, kwa wema wako unihurumie mimi mwenye zambi na unilinde toka unafiki wa Mfarisayo *(mara mbili).*

Enyi Mashahidi wa Bwana wenyi kutakasa ulimwengu na kuponya ugonjwa wote, mutuombee sasa sababu ya kuokoa roho zetu toka mutego wa adui.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . .

Sauti ya mnane

Ee Mama usiyeolewa, mbingu zinaimbia neema yako, na tunatukuza kuzaa kwako; ee Mzazi-Mungu, ombea zetu wokovu.

MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA INE

Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya mnane. Anestis ek nekron.

Enyi waaminifu, tusujudu mbele ya Muti Takatifu kamili ambapo Muumba wa ulimwengu aliinuliwa*:* inatakasa roho na mwili kwa kuondoa wenye kuichafua zambi zote ya wale wenye kufunga na imani sababu ya kutukuza daima Kristu kama Mfazili wao peke yake.

Utukufu kwa Baba . . .*(mara ingine).*
Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**
Sauti ya mnane

Neno la Baba alishuka duniani, Malika wa nuru alimwambia Mzazi-Mungu*:* Salamu, ee Bikira Mutukufu ambaye peke yako ulipata mimba ya Mungu wa mbele ya nyakati tena Bwana wetu kusudi aokoe wanadamu toka mauti.

KATHISMA WA TATU

Sauti ya tatu. Tin oreotita

Tunapofika katika ya hii Kwarezima takatifu na kwa kuabudu Musalaba wako, tunaposujudu mbele yako, tunakulalamikia*:* Wewe ni mukubwa, ee Kristu mpenda-wanadamu, na matendo yako ni makubwa, ee Bwana, kwa sababu ulituonyesha Musalaba wako wenyi kuleta uzima; na kwa woga tunakuimbia kwa kuisujudu*:* Utukufu kwa rehema yako ya milele.

Utukufu kwa Baba...*(mara ingine).*
Sasa na siku zote...**THEOTOKION**
Sauti ya mnane

Ee Bikira, kama mzabibu isiyolimwa ulizaa zabibu ya ajabu huko kunatiririka kwa ajili yetu, divai ya wokovu yenyi kufurahisha roho zetu na miili yetu; na tunakutaja wewe mwenye heri kama Chemchem ya hii mema, tunakutolea daima hii salamu ya malaika, ee Bikira mjaliwa neema.

IRMOS: *Kisha wimbo wa tatu.Sauti ya tatu.*

Tuimbieni Bwana Mungu wetu aliyefanya maajabu zamani*:* Aliokoa wana wa Israeli toka Bahari Nyekundu, aliangamiza adui zake; kwake peke yake tumutolee nyimbo zetu, maana amevaa utukufu.

Fotagogikon tafuta ku mwisho ya hii Kitabu na sauti ya hii Juma.

APOSTIKHA

Sauti ya sita. Idiomelon

Ee Kristu ulituonyesha unyenyekevu kama njia nzuri ya kwenda mbinguni, wewe mwenyewe ulijishusha mpaka kutwaa hali ya mtumishi, haukukubali majivuno ya Mfarisayo, lakini ulipokea kusikitika kwa Mtoza kodi kama sadaka mbinguni; kama Yeye, ni mimi pia nakulalamikia*:* Unihurumie, ee Mungu wangu, unisameha, ee Mwokozi na uniokoe. *(mara mbili).*

Wimbo ya Washahidi

Ee Bwana, makumbusho ya Mashahidi wako ni siku ya shangwe kwa viumbe vyote*:* Pamoja na malaika mbinguni dunia ya watu inafurahi; kwa maombezi yao utuhurumie.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Sauti ya sita

Kwa neno ulipokea kwa malaika mkuu, ukawa kiti cha Wakheruvi na ulibeba mikononi Mwako, ee Mzazi-Mungu matumaini ya roho zetu.

MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA YA INNE

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo 3 ya hii Kitabu na 3 ya Mineon.

Sauti ya mnane. Ti imas kalesomen

Tunaposhinda sasa katikati ya Kwarezima kwa uwezo wa Musalaba tutukuzeni nguvu ya Mungu Mwokozi ile zamani ilitukuzwa duniani Msalabani na tumwambie*:* Ee Bwana, utupe sisi tuone mateso na Ufufuo wako Takatifu ukitupatia maondoleo yako na neema ya wokovu.

Turegeze tamaa za mwili kwa kufunga chakula na kutenga mbali furaha za mwili, tutukuzeni muti wa MUsalaba Takatifu; inaonekana waziwazi machoni mwetu kusudi tuisujudie na kwa neema ya Mungu itakase ulimwengu; tumulalamikie Mungu wa mapendo*:* Tunakushukuru, ee Bwana, wewe mwenye kuleta wokovu rohoni mwetu kwa Musalaba.

Sauti umoja. Ton Theotokon.

Leo tunaposujudia Musalaba, tuseme wote na Furaha*:* Salamu, ee Muti Mupya wa uzima; salamu, nguvu ya Kristu Mufalme wetu, salamu, ee utukufu wa mbinguni wa wanadamu; salamu, ee pambo la wafalme wakristu; salamu wewe uliye nguvu ya imani yetu, salamu, ewe ushindi isiyoweza kushindwa; salamu, kwani unafukuza adui; salamu, ewe nuru ya kwangaa, salamu, ewe matumaini ya Mashahidi; salamu, ewe nguvu ya wenye haki na ya Watakatifu, salamu, ewe utukufu wa Malaika, salamu, Msalaba Takatifu wa Bwana.

Kisha wimbo ya Mineon tatu. Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Prokimenon. Sauti ya mnane. Zaburi 63.

Sikia sauti yangu, ee Mungu, katika kilio changu.

Shairi*:* Chunga maisha yangu kwa woga wa adui.

Somo ya Mwanzo tutasoma (8, 21-9, 7).

Bwana akasikia harufu tamu; Bwana akasema moyoni mwake*:* Sitalaani inchi tena kwa sababu ya mutu, kwa maana mawazo ya moyo wa mutu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena kila kitu kilicho hai sawasawa nilivyofanya. Mungu akabariki Noa na wana wake, akawaambia*:* Muzidi na kuongezeka na kujaza inchi. Na woga wenu na maogopesho yenu yatakuwa juu ya kila nyama ya inchi, na juu ya kila ndege ya anga; nao wote wanaoj*:* lza inchi, na samaki zote za bahari; wametolewa kwa mukono wenu. Kila kitu kinachotam-baa kilicho hai kitakuwa chakula kwenu, sawasawa nilivyowapa ninyi mboga za majani, hivi nimewapa ninyi vitu vyote; lakini nyama na uzima wake, ndiyo damu yake, hamutakula. Na hakika nitataka damu yenu, damu ya uzima wenu kwa mukono wa kila nyama; na kwa mukono wa kila mutu, hat*:* t kwa mukono wa ndugu ya kila mutu nitataka uzima wa mutu. Yeye anayemwanga damu ya mutu, kwa mutu vilevile damu yake itamwangwa; kwa sababu alifanya mutu kwa sura ya Mungu. Nanyi muzidi na kuongezeka; muzae sana inchini na kuongezeka ndani yake.

Prokimenon. Sauti ya sita. Zaburi 64.

Ee Mungu wa wokovu wetu; wewe ni tumaini la miisho yote ya dunia.

Shairi*:* Sifa inakungojea, ee Mungu, katika Sayuni.

Somo ya Mezali tutasoma (11, 19-12, 6).

Mwenye kudumu katika haki atapata uzima*:* Lakini mwene*:* kufuata uovu anaufuata kwa

mauti yake mwenyewe. Wenye moyo wa ukaidi ni machukizo kwa Bwana*:* Lakini walio wakamilifu katika njia zao wanamupendeza. Hakika mwovu hatakosa azabu*:* lakini wazao wa wenye haki wataponyeshwa. Kama pete ya zahabu kinywani mwa nguruwe, Vivyo hivyo ni mwanamuke muzuri asiye na akili, Hamu ya mwenye haki ni nzuri tu*:* Lakini taraja ya mwovu ni gazabu. Kuna anayes;Jmbaza, na anazidi kuongezeka ; Kuna anayezuiza isiyo haki, lakini inaleta uhitaji tu. Nafsi ya mwenye ukarimu itanenepa, Naye anayenywesha; Jitanyweshwa mwenyewe. Yeye anayenyima nafaka, watu watamutukana*:* lakini baraka itakuwa kwa kichwa chake anayeiuza. Mwenyc kutafut;J mema kwa bidii, anatafuta upendeleo*:* lakini mwenye kutafuta uovu, utamupata. Mwenye kutllmainia mali zake ataanguka, lakini mwcnye haki atasitawi kama majani mabichi. Mwenye kusumbusha nyumba yake mwenyewe atariti upepo, na mupumbafu atakuwa mutumishi wa mwenye moyo wa hekima. Matunda ya mwenye haki ni muti wa uzima; Naye anayevuta roho za watu ni mwenye hekima. Tazama, mwcnye haki atalipwa duniani*:* Basi mwovu na mwenye zambi si mara nyingi zaidi? Yeye anayependa mafundisho anapenda maarifa*:* Lakini mwenye kuchukia kulaumiwa ni kama nyama Mutu muzuri atakubaliwa na Bwana; Lakini atahukumu mutu mwenye mashauri maovu. Mutu hatasimamishwa kwa njia ya uovu, Lakini shina la wenye haki halitaondolewa kamwe. Mwanamuke mwema ni taji kwa mume wake*:* Lakini mwenye kuhayarisha'ni kama kuoza mlfupanl mwake. Mafikili ya wenye haki ni haki*:* Lakini mashauri ya waovu ni udanganyifu. Maneno ya waovu ni juu ya kuvizia kwa damu*:* Lakini kinywa cha wenye haki kitawaponyesha.

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon

Mfarisayo aliyesema maneno mengi alikataliwa sababu ya majivuno yake; Mtoza kodi munyenyekevu kwa sala yake ya ndani alihakikishwa; ee roho yangu, unifundishe tafauti kati ya hawa wawili, chagua unyenyekevu, uikumbatie, kwa sababu ni kwa wanyenyekevu Kristu aliahidi kuwapa neema yake kwa mapendo yake kwa wanadamu.

Wimbo ya Mashahidi

Enyi Mashahidi wa Bwana, mbeni kwa Mungu ili kwa ajili ya roho zetu atuondolee zambi zetu kwa wema wake kubwa.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira takatifu, Mzazi-Mungu, nakimbilia kwa ulinzi wako kwa matumaini ya kupata wokovu*:* Ee Bikira safi kamili, una uwezo wa kunisaidia.

MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA INNE KWA ORTHROS

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya mnane. To asalefton stirigma.

Roho yenyi kutakaswa kwa kufunga, tusujudu mbele ya Musalaba alisulubiwa Kristu Mwokozi wetu na tuulalamikie*:* Salamu, furaha ya wenye kufunga na tegemeo yao imara, salamu wewe mwenyi kuharibu tamaa tena woga wa mashetani, salamu, muti mupya ya uzima.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu, tunakutukuza kwa nyimbo zetu wewe uliye boma imara ya imani na hazina heshimiwa ya roho zetu; salamu, kwani ulichukua tumboni mwako Chemchem ya uzima, salamu, wewe uliye matumaini ya mipaka ya dunia tena mulinzi wa wenye kuteswa, salamu, Bibi arusi usiyeolewa.

KATHISMA WA TATU

Sauti ya mnane. Os aparkhas tis fiseos.

Ee Chemchem ya uzima wa viumbe, Musalaba wako imeonyeshwa, dunia inasujudu mbele yake ikikulalamikia*:* «Kwa nguvu yake linda katika amani wale wenyi kukuimbia, ee Bwana, wale wenyi kutukuza rehema yako ya milele.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Salamu, wewe ambaye kwa sauti ya malaika ulipokea furaha ya ulimwengu, salamu, wewe uliyezaa Muumba na Bwana wako, salamu, wewe uliyestahili kuwa Mama wa Kristu Mungu wetu.

Fotagogikon tafuta ku mwisho ya hii Kitabu na sauti ya hii Juma.

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon

Ninapofikiri juu ya hukumu ya Mfarisayo mwenyi majivuno, ee roho yangu, unajua namna gani alihakikishwa Mtoza kodi ambaye unyenyekevu ilikomboa zambi; ujiharikishe kuepuka majivuno ya wa kwanza, fananisha imani ya wa pili kuwa mwangalivu na kwa utaratibu wako pokea nafasi ya juu kwa Kristu mwenye kukupa neema ya wokovu. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi.

Enyi Mashahidi, mulishindana na ushujaa, muliteswa na utukufu mateso ya makafiri na kukiri Kristu mbele ya Wafalme; kisha kuacha hii uzima, uwezo wenu inafanyika tena duniani, munaponyesha mateso na magonjwa yote. Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bikira Mzazi-Mungu, ulinzi yako kwa sisi ni dawa ya kiroho yenyi kuponyesha roho zetu toka magonjwa.

MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA YA INNE

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo 6 ya hii Kitabu.

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Duniani uliteswa Mateso na ulisulubiwa Msalabani sababu ya kuwakomboa wote na kuwapa ushindi juu ya mateso; katika ya Kwarezima leo tunaonyesha Msalaba wako na kusujudu mbele yake, tunaikumbatia na furaha; utupe sisi tuone Mateso yako na ufufuo wako wenyi kuleta uzima, kwa nuru ya fazila za mbinguni, ee Neno la Mungu ambaye peke yako mwenye huruma.

Ulikufa Msalabani kwa kutaka Kwako, ulichomwa mukuki na kunywishwa nyongo, ee Bwana mvumilivu ambaye zamani kwa mukono wa Musa aliondoa uchungu wa maji ya Mara; ndiyo maana nakuomba nikikusihi*:* Okoa moyo wangu toka uchungu wa mateso, tuliza roho yangu kwa sali ya toba na unifanye mimi kuwa mwenyi kuabudu mateso yako takatifu.

Sauti ya kwanza. O pale to Mosi.

Musalaba ambao zamani Musa alitangulia kuonyesha wakati alipanua mikono sababu ya kumushinda Amaleki leo tunaiona imewekwa mbele ya macho yetu, tuikumbatie na usafi wa midomo na mioyo yetu; Kristu alitukuzwa juu ya Musalaba kwa kushinda mauti; tunapostahiliwa neema yake, tuimbie na sauti nzuri Mwokozi wa ulimwengu na tumuombe atuonyeshe sisi wote ufufuo wake wenyi kuleta uzima.

Wimbo ingine. Sauti ya ine. Edokas simiosin.

Kujeni, tusujudu leo mbele ya muti wenyi kutupatia uzima, Musalaba wa Bwana Mungu wetu ambapo alishinda mauti na kweli kisha kuanguka kwetu alitupa sisi neema mupya ya ufufuo; ndiyo maana tumulalamikie Mkombozi*:* Wewe uliyeteswa kwa ajili yetu kw akutaka

kwako ulipotaka kuokoa ulimwengu wote, ee Bwana Mungu wetu, utukufu Kwako.

Kwa sisi wakristu tumepewa silaha ya ushindi ya Msalaba wako; ee Kristu Mwokozi unaipatia Eklezya yako amani, unaiokoa kwa jina la Musalaba wako takatifu tunatukuza leo tukikulalamikia na mapendo*:* Utupe uriti ya Watakatifu wako.

Kwa machozi yetu tunapotakasa mawazo ya mioyo yetu na kwa kufunga tunapotakasa akili yetu, kujeni tusujudu mbele ya muti wa Musalaba sababu ya kuzuia kwa kufunga, tamaa zote za mwili, na tumulalamikie Bwana aliyesulubiwa*:* Ee Mwokozi, utupe tuabudu nuru ya Ufufuo wako siku ya tatu.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . .

Sauti ya mnane

Leo Mufalme wa utukufu, Rabi wa ulimwengu anasulubiwa Msalabani kwa kutaka kwake, mukuki inachoma ubavu wake; anaonja siki na nyongo huyu ndani yake Eklezya inapata huruma, anavikwa taji ya miiba huyu mwenyi kufunika mbingu kwa mawingu; anavikwa nguo ya Zihaka na watu wanamupiga makofi huyu aliyeumba wanadamu kwa mukono wake; anapigwa fimbo mukongoni huyu mwenye kuvika mbingu kwa mawingu, wanamupiga makofi kumutemea mate, wanamutukana, anateswa hii yote sababu ya kuokoa dunia toka mauti, kwani yeye ni Mukombozi wangu na Mungu wa huruma.

Prokimenon ya magaribi. Sauti ya sita. Zaburi 67.

Imbeni kwa Mungu, imbeni sifa kwa jina lake.

Shairi*:* Fanyieni njia atakayepita kwa farasi jangwani; jina lake ni Ja.

Somo ya Mwanzo tutasoma (9, 8-17).

Mungu akamwambia Noa, na wana wake pamoja naye akisema*:* Nami, tazameni, nitasimamisha agano langu nanyi, na pamo-ja na uzao wenu nyuma yenu; na pamoja na kila kitu kilicho hai kilicho pamoja nanyi, ndege na ngombe na kila nyama ya inchi pamoja nanyi ; na wote waliotoka safina, hata kila nyama ya inchi. Na nitasimamisha agano langu pamoja nanyi; wala miili yote haitakatiwa mbali tena na maji ya garika; wala garika haitakuwa tena kuharibu dunia. Mungu akasema*:* Hii ni alama ya agano ninalofanya katikati yangu nanyi na kila kitu kilicho hai kilicho pamoja nanyi, hata vizazi vya milele*:* Ninaweka upinde wangu winguni na utakuwa alama ya agano katikati yangu na dunia. Na itakuwa wakati ninapoleta wingu . iuu ya dunia, upinde utaone-kana ndani ya wingu, na nitakumbuka agano langu, lililo katikati yangu nanyi na kila kitu kilicho hai cha miili yote; na maji hayatakuwa garika tena kuharibu miili yote. Na upinde utakuwa winguni ; na nitauangalia, nikumbuke agano la milele katikati ya Mungu na kila kitu kilicho hai cha miili yote iliyo duniani. Mungu akamwambia Noa*:* Hii ni alama ya agano nililosimamisha katikati yangu na miili yote iliyo juu ya dunia.

Prokimneon. Sauti ya sita. Zaburi 68.

Wakovu wako, ee Mungu, uninyanyue.

Shairi*:* Wapole waliona na wanafurahi.

Somo ya Mezali tutasoma (12, 8-22).

Mutu atasifiwa kwa kadiri ya hekima yake*:* Lakini mwenye moyo wa ukaidi atazarauliwa. Afazali mutu anayezarauliwa, naye ana mutumishi, Kuliko yule anayejisifu, naye anakosa chakula. Mwenye haki anafikili uzima wa nyama yake*:* Lakini huruma za waovu ni ukali. Mwenye kulima shamba Iake atakuwa na chakula tele*:* Lakini mwenye kufuata mambo bule anakosa ufahamu. Mwovu anatamani mawindo ya watu wabaya*:* Lakini shina Ia wenye haki linaleta matunda. Katika kosa Ia midomo ni mutego kwa mutu mubaya*:* Lakini mwenye haki atatoka katika taabu. Mutu atashibishwa kwa mema kwa matunda ya Kinywa chake*:* Na mutu atarudishiwa matendo ya mikono yake. Njia ya wapumbafu, ni vizuri, kwa macho, yake mwenyewe*:* Lakini mwenye heklma anasikiliza shauri. Gazabu ya mupumbafu inajulikana wazi*:* Lakini mutu mwenye akili anaficha haya. Mwenye kusema kweli anaonyesha haki. Lakini

mushuhuda wa uwongo hila. Kuna anayesema kwa haraka kama kutoboa kwa upanga*:* Lakini ulimi wa wenye hekima ni afya. Mudomo wa kweli utasimamishwa milele*:* Lakini ulimi wa uwongo ni wa dakika tu. Udanganyifu ni moyoni mwao wanaofikili uovu*:* Lakini kwa wenye mashauri ya salama kuna furaha. Hakuna matata itakayopata wenye haki*:* Lakini waovu watajazwa mabaya. Midomo ya uwongo ni chukizo kwa Bwana*:* Lakini wenye kutenda kwa haki ndio furaha yake.

APOSTIKHA.

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Kwa makosa yangu mengi nilipomupiota Mtoza Kodi sikufananishe toba yake; na bila kuwa na fazila ya Mfarisayo nafananisha majivuno yake. Lakini wewe, ee Kristu Mungu wetu ambaye kujishusha kwako imara Msalabani kulishinda shetani mwenyi majivuno, ondoa mbali yangu makosa ya wa kwanza, uniokoe toka majivuno ya wa pili, ile ilionzuri ndani ya mumoja na mwingine uisabitishe rohoni mwangu na uniokoe. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi.

Ma Nabii, Mitume wa Kristu na Mashahidi walitufundisha kuimbia Utatu wa asili moja; waliletea mataifa yenye kupotea nuru ya ubatizo*:* malaika na wanadamu wanakuwa marafiki.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . .

Sauti ya tano

Vilipokuona umetundikwa Msalabani bila nguo wewe Muumba wa ulimwengu, viumbe vyote vilishikwa kwa woga; jua likaficha nuru yake, mawe yakapasuka, inchi ikatikisika, na pazia ya Hekalu ikapasuka vipande mbili; wafu wakafufuka kaburini mwao, na Ezi za mbinguni zikashangaa na kusema*:* Ni ajabu! Tazama Mwamzi anahukumiwa na anateswa mateso ya kutaka kwake sababu ya wokovu wa dunia na matengeneo yake.

MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA YA INNE

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya sita. Elpis tu kosmu.

Inapotakasa waakti wa Kwarezima, Musalaba takatifu inaonyeshwa sababu ya kuiabudu; tujongeeni zamiri yenye kutakaswa sababu ya kushotako nuru na usafi, na kwa woga tuseme*:* Utukufu kwa rehema yako, ee Mwokozi wa wanadamu.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Aliposimama karibu ya Msalaba, mama asiyeolewa akamuambia huyu alizaa bila mbegu*:* Upanga imechoma roho yangu, nateswa kwa kukuona umesulubiwa wewe Mungu Muumba mbele yako ulimwengu inatetemeka. ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

KATHISMA WA TATU

Sauti ya kwanza. Apegnosmenin.

Tujongeeni na nuru ya fazila, na kwa kufunga tunapotakaswa tusujudu mbele ya Musalaba heshimiwa tukisema*:* takasa miili yetu na roho zetu na utustahilishe kuona pia Mateso yako takatifu, peke yako Mungu wa ulimwengu mwenyi kutupa sisi neema ya wokovu.

STAYROTHEOTOKION.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote...*Ton tafon su Sotir.*

Ee Kristu, wakati Mama yako Mutakaitfu kamili alikuona umetundikwa Msalabani, akalalamikia*:* Ee Mwana wa milele pamoja na Baba na Roho Mutakaitfu, hii ni fumbo gani ya

tendo lako la wokovu? Katika hii uliokoa kwa wema wako, ee Rabi, kazi ya mikono yako.

FOTAGOGIKON YA SAUTI YA HII JUMA

Na Eksapostilarion hii:

Sauti ya tatu. En Pnevmati to iero.

Katikati ya Kwarezima Msalaba takatifu inaalika kwa ibada wote wale wanaunganisha kama inavyostahili mateso yao kwa yale ya Kristru. Kujeni, ninyi waaminifu wote, tusujudu mbele ya fumbo ya Musalaba wenyi kuleta uzima.

STAYROTHEOTOKION. Sauti umoja.

Mama Mutakatifu kamili asiyeolewa wa Neno la Mungu akaomboleza na kulia akasema*:* Kama hii ndiyo habari ya furaha Malaika Gabrieli alinileta zamani, ujiharikishe kutimiza, ee Mwanangu, nia ya Mungu na tendo lake la wokovu.

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon

Tulipomaliza nusu ya Kwarezima njiani yenyi kwenda Msalabani, tunaweza kuona siku yako kama Abrahamu alivyojaa na furaha na kupokea Isaki muzima aliyetolewa kwa lufu; utupe na sisi pia imani yenyi kutuokoa kwa adui na ushirika kwa karamu yako ya fumbo; hapo tutakuimbia katika amani*:* Ee Bwana mwenyi kutuokoa na kutuangazia, utukufu kwako. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi

Enyi Mashahidi washindi wa Kristu muliyoshinda udanganyifu kwa uwezo wa Musalaba, mulipokea neema ya uzima wa milele; bila woga muliteswa mbele ya wazulumu, lakini sasa munashangilia na furaha, na roho zetu zinaponyeshwa kwa damu yenu*:* Ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya mnane.*

Ee Bwana, tunaposhinda nusu ya Kwarezima, tunaongojea, kama bandari ya wokovu, wakati ya Mateso yako ya kutaka; kwa rehema yako na wema wako utustahilishe kuona katika amani siku ya Ufufuo wako tukufu.

MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA YA INNE

Kisha: «Bwana nimekuita...» *tunaimba wimbo na ma shairi kumi; wa sita ya hii kitabu na wa inne ya Mineon.*

Sauti ya ine. Idiomelon.

Leo Kwarezima yenyi kuleta fazila imefika katikati yake katika furaha ya siku za mbele na mafaa ya zile zitafwata, kwani nguvu ya fazila inaongeza uwezo yao; ndiyo maana tumulalamikie na furaha Kristu muletaji wa mema yote*:* Wewe ambaye kwa ajili yetu ulifunga na kuteswa Musalabani, utustahilishe, bila kuhukumiwa, kusharikia Paska yako Takatifu kwa kuishi katika amani na kukutukuza pamoja na Baba na Roho Mutakatifu.

Wimbo ingine. Sauti ya tano.

Wale ambao kwa siri wanatimiza fazila na kupokea mema ya kiroho hawaende kujitukuza mbele ya watu, lakini wanachunga hii moyoni mwao; na huyu anaona kwa siri anatupatia tuzo yenyi kustahili. Tumalize hii Kwarezima sura safi tukiomba kwa siri rohoni mwetu na kusema daima*:* Baba yetu uliye mbinguni, usitutie katika majaribu, lakini tunakuomba, utuokoe na yule Mwovu.

Wimbo ya Mashahidi

Enyi Mashahidi watakatifu mulioteswa na namna yote ya mateso, kwa ushujaa wenu hamukumukana Kristu, lakini kwa uhodari mulishinda wazulumu na kulinda imani sababu ya

kupita toka dunia mupaka mbinguni; ndiyo maana kwa deni munayo kwa Mungu, mumuombe amani juu ya dunia na neema ya wokovu kwa ajili ya roho zetu.

Sauti ya kwanza. Panefimi Martires.

Roho yenye kutakashwa na maji ya Kwarezima, kujeni, tusujudu na imani mbele ya Musalaba Takatifu na heshimiwa wa Bwana sababu ya kupokea nuru takatifu na ya milele, amani na neema ya wokovu.

Ee Musalaba heshimwa, wewe uliye nguvu ya Mitume ambaye wanatukuza Malaika wakuu, wafalme na watawala, okoa toka uovu wote wale wenye kusujudia mbele yako, na utustahilishe tumalize hii Kwarezima kwa usafi sababu ya kuona wokovu wako na ufufuo wako tukufu.

Wimbo ingine. Sauti ya saba. Simeron grigori.

Leo tunaposujudia Musalaba wa Bwana, tuseme*:* Ee Muti ya uzima, salamu, furaha ya dunia yenyi kuondoa Hadeze na mauti, nguvu yako inafukuza mashetani; silaha ya ushindi na tegemeo la waaminifu, linda na kutakasa wale wanainama mbele yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya mnane*

Leo Bwana asiyekaribika amenifikisha kwake, anateswa mateso yake sababu ya kuniondolea mateso yangu; huyu mwenyi kuponyesha vipofu anatemewa mate ya midomo ya makafiri na anapigwa fimbo sababu ya kuokoa wafungwa. Bikira, mama yake, alipomuona Msalabani akamwambia akilia*:* Ole wangu, ee Mwanangu mupendwa, wewe uliye mzuri kupita mwanadamu wote unaonekana bila uzuri, bila hali na bila uzima. Ole wangu! Ewe Nuru ya macho yangu, upanga inachoma moyo wangu na tumbo langu linateswa kwa kukuona hivi! Natukuza na kuimbia Mateso yako, nabudu rehema yako ya milele, ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

KUINGIA.

Prokimenon ya Magaribi. Sauti ya ine. Zaburi 71.

Heri ni Bwana Mungu, Mungu wa Israeli.

Shairi*:* Umupe Mfalme hukumu zako, ee Mungu.

Somo ya mwanzo tutasoma (9, 18-10, 1).

Na wana wa Noa waliotoka safina walikuwa Semu, Hamu na Yafeti; na Hamu ni baba ya Kanana. Hawa watatu walikuwa wana wa Noa; hawa wakaenea dunia pia. Noa akaanza kuwa mulimaji, akapanda shamba la mizabibu. Akakunywa mvinyo, akalewa; akafunuliwa hemanimwake. Hamu, baba ya Kanana akaona utupu wa baba yake, akawaambia ndugu zake wawili inje. Semu na Yafetiwakatwaa vazi, wao wawili wakaliweka juu ya mabega yao,
wakakwenda na mugongo wao mbele, wakafunika utupu wa baba yao; na nyuso zao zilikuwa nyuma, wala hawakuona utupu wa baba yao. Noa akaamka toka mvinyo yake, akajua neno mudogo wa wana wake alilomufanyia. Akasema*:* Kanana alaaniwe; atakuwa mutumwa kabisa kwa ndugu zake. Akasema*:* Bwana abarikiwe, Mungu wa Semu; na Kanana awe mutumwa wake. Mungu aongeze Y afeti, akae hemani mwa Semu ; na Kanana awe mutumwa wake. Noa akaishi nyuma ya garika miaka mia tatu makumi tano. Na siku zote za Noa zilikuwa mia tisa makumi tano ; akakufa. Basi hivi ni vizazi vya wana wa Noa, Semu, Hamu na Yafeti ; wakazaliwa wana kwao nyuma ya garika.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 72.

Lakini ni vizuri kwangu kukaribia Mungu.

Shairi*:* Hakika Mungu ni mwema kwa Israeli kwao walio na moyo safi.

Somo ya Mezali tutasoma (12, 23-13, 9).

Mutu mwenye akili anaficha maarlfa*:* Lakini moyo wa wapumbafu unatangaza upumbafu. Mukono wa wenye bidii utatawala*:* Lakini muvivu atatumikishwa kodi. Uzito moyoni mwa mutu unauinamisha; Lakini neno zuri Iinaufurahisha. Mwenye haki ni kiongozi kwa jirani yake*:* lakini njia ya waovu inawakosesha. Muvivu hapiki mawindo yake*:* lakini mali za damani za watu ni kwa mwenye bidii. Katika njia ya haki ni uzima; Na katika mapito yake hakuna mauti. Mwana mwenye hekima anasikiliza maonyo ya baba yake*:* lakini mwenye zarau hasikilizi maonyo. Mutu atakula mema kwa matunda ya kinywa chake*:* lakini nafsi ya mutu mudanganyifu itakula jeuri. Mwenye kulinda kinywa chake analinda uzima wake*:* lakini yeye anayefungua midomo yake wazi atapata uharibifu. Nafsi ya muvivu inatamani pasipo kupata kitu*:* lakini nafsi ya mwenye bidii itanenepeshwa. Mwenye haki anachukia kusema uwongo*:* lakini mutu mwovu ni wa kuchukiza sana, naye anapatwa na haya. Haki inamuchunga aliye haki njiani*:* lakini uovu unaangamiza mwenye zambi. Kuna mwenye kujitajirisha, Iakini hana kitu*:* Kuna anayejifanya kuwa masikini, lakini ana mali nyingi. Ukombozi wa uzima wa mutu ni mali yake*:* Lakini masikini hasikii mahamakio. Nuru ya mwenye haki inafurahi*:* lakini taa ya mwovu itazimika.

MU KAZI INNE ASUBUI YA JUMA YA INNE

Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya kwanza. Khoros agelikos.

Enyi Mitume Watukufu wenyi kuombea roho zetu, muliposabitishwa kwa uwezo wa Musalaba, muliharibu udanganyifu wa adui; furahini leo tunapoabudu Musalaba, mukimuomba peke yake Mupenda-wanadamu kwa ajili yetu.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Maria Makao heshimwa ya Bwana, utuondoe toka zimuni huko tuliangukia utuokoe toka kutotumaini kwa ajabu, toka makosa yetu na toka sikitiko yote; wewe ni makimbilio ya wenye zambi, msaada, ulinzi na wokovu wa watumishi.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya saba. Kirie imis esmen.

Ee Bwana, tunapoona Musalaba wako imeonyeshwa leo, tunajongea na imani, tunaikumbatia na woga na furaha, kwa sauti na mashairi na ya nyimbo; kwa uwezo wa Musalaba takasa watumishi wako na leta amani duniani, ee Mungu wa mapendoi.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bwana, sisi ni watu wako, kondoo za zizi lako, rudisha kwako wana wako wenye kutawanyika, kwa uongozi wako kusanya kondoo wapotevu, hurumia kondoo zako, ee Mchungaji mwema, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, peke yako Mupenda-wanadamu na Bwana asiye na zambi.

FOTAGOGIKON YA SAUTI YA HII JUMA

APOSTIKHA

Sauti ya saba. Idiomelon

Enyi waaminifu, tufananisheni toba ya Mtoza Kodi pahali pa sisi kujitukuza kama Mfarisayo; tutoeni kulia kwa ndani ya moyo wetu kwa mfazili Mtakatifdu aliyetuamuru akisema*:* Ye yote anayejitukuza atazarauliwa, huyu anajishusha atatukuzwa! Ndiyo maana kwa sauti moja tunapaza sauti*:* Ee Bwana, utuhurumie sisi wakosefu na utuokoe. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi

Walipokuwa na ukomo moja, wazo moja, Mashahidi walifwata njia moja katika uzima yao*:* Kwa ajili ya Kristu walichagua kufa, walishindana kwa bidii sababu ya kufa; mateso iliwasaidia kuwa hazina; Ni maajabu! Wakaambiana mumoja kwa mwingine*:* kama sasa tunaepuka lufu, tunaweza kwa namna yote kulipa ushuru kwa dunia; tufanye mateso yetu kuwa heshima, kwa lufu yetu tupate uzima ya kweli! Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu leta amani katika uzima yetu wakati tunakulalamikia*:* Ee Bwana wa mapendo, utukufu kwako.

MU KAZI INE MANGARIBI YA JUMA YA INE

Elezo*: Kisha* «Bwana nimekuita*. . .* » *tunaimba wimbo tatu ya hii Kitabu na wimbo tatu ya Mineon.*

Sauti ya ine. Edokas simiosin.

Ee Bwana, tulipofaziliwa kutukuza Musalaba wako wa heri ambapo ulituokoa tunaimbia rehema yako na tunakuomba uwape watu wote furaha ya wokovu wako, kwa toba utupe sisi kuona Mateso yako takatifu na ufufuo wako tukufu.

Uliposulubiwa Musalabani, ulikua na ulishinda mauti; kwa neno lako lenyi kuleta uzima ulifufua wafu; ndiyo maana, ee Bwana, nakuomba*:* Uirudishie roho yangu neema ya wokovu ilipoteza kwa zambi, unipe sikitiko na usamehe wa makosa yangu kwa siku hizi za Kwarezima takatifu kamili.

Sauti ya inne. Ton noeron adamanta.

Ee Mungu Mwokozi, tulipofaziliwa kuona na kutukuza na furaha Musalaba wako Takatifu, tunakuomba tena tuone Mateso yako takatifu kwa nguvu ya kufunga sababu ya sisi kusujudu tukiimba mbele ya mukuki, sanda na tete ya Musalaba wako yenye kutuokoa toka mauti, inaturudisha kwa furaha ya uzima ya kwanza*:* Kwa shukrani tunakutukuza.

Wimbo ya Mineon. Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Prokimenon ya Mangaribi. Sauti ya ine. Zaburi 75.
Apeni na toeni kwa Bwana Mungu wenu.
Shairi*:* Mungu amejulikana Yuda.

Somo ya Mwanzo tutasoma. (10, 32-11, 9).

Hizi ni jamaa za wana wa Noa, kwa vizazi vyao, katika mataifa yao; na kwa hawa mataifa yamegawiwa duniani nyuma ya garika. Na dunia nzima ilikuwa na lugha moja na usemi mumoja. Na ilikuwa wakatl waliposafiri kwa mashariki, wakakuta inchi sawa katika inchi ya Sinari; wakakaa pale. Wakasemezana*:* Tufanye matofali na kuyachoma vizuri kwa moto. Wakakuwa na matofali kwa mawe, na lami kwa chokaa. Wakasema*:* Tujijengee wenyewe muji na munara, kichwa chake kifike mbinguni, na tujifanyie jina; hata tusisambazwe juu ya uso wa dunia nzima. Bwana akashuka kuona muji na munara, wana wa watu waliojenga. Bwana akasema*:* Tazama wao ni taifa moja, nao wote wana lugha moja; na maneno haya wanayaanza kuyafanya; basi sasa hakuna kitu kitakachowazuiza wanachokusudi kufanya. Tushuke tuwachanganyie usemi wao, wasisikilizane lugha. Hivi Bwana akawasambaza toka kule juu ya uso wa dunia nzima; wakaacha kujenga muji. Kwa hivi jina lake 1ilitwa Babeli kwa sababu Bwana akachanganya usemi wao dunia nzima pale; na toka pale Bwana akawasambaza juu ya uso wa dunia nzima.

Prokimenon. Sauti ya saba. Zaburi 76.
Nitapazia Mungu sauti yangu.
Shairi*:* Kwa siku ya taabu yangu, nilitafuta Bwana.

Somo ya Mezali tutasoma (13, 19-14, 6).

Kitu kilichotamaniwa kikitimizwa, ni kitamu kwa nafsi ya mulu, lakini ni machukizo kwa wapumbafu kujitenga na maoyu. Tembea pamoja na wenye hekima, nawe utakuwa mwenye hekimä*:* lakini rafìki wa wapumbafu ataumia. Ubaya unafuata wenye zambi*:* lakini mwenye haki atalipwa mema*:* Mutu mwema anaacha uriti kwa wana wa wana wake*:* Na mali ya mwenye zambi inawekwa akiba kwa mwenye haki. Chakula tele kinapatikana kwa kulima kwa masikini*:* lakini viko vinavyoharibiwa kwa sababu ya uzalimu, Yeye asiyetumia fimbo yake anachukia mwana , wake*:* lakini yeye anayemupenda anamwazibu wakatl kwa wakati. Mwenye haki anakula kwa kushibisha nafsi yake*:* lakini tumbo la mwoyu litaona njaa. Kila mwanamuke mwenye hekima anajenga nyumba yake*:* Lakini aliye mupumbafu anaibomoa na mikono yake mwenyewe. Yeye anayetembea katika haki yake anaogopa Bwana*:* lakini mwenye ukaidi katika njia zake anamuzarau. Kinywani mwa wapumbafu ni fimbo ya majivuno*:* lakini midomo ya wenye hekima inawalinda. Pasipo ngombe, zizi ni safi*:* lakini nguvu za ngombe zinaleta mazidio mengi. Mushuhuda mwaminifu hatasema uwongo*:* Lakini mushuhuda wa uwongo, pumuzi yake ni uwongo. Mwenye kuzarau anatafuta hekima naye haipati*:* lakini maarifa ni nyepesi kwake aliye na ufahamu.

APOSTIKHA

Sauti ya sita. Idiomelon

Ee roho yangu, kwa kujishusha kwa Bwana yeye mwenyewe mupaka kufa Musalabani, ulifunza kujishusha yenyi kufwata kuinuliwa na kutukuzwa unyenyekevu inaleta ujilinde basi kuharibu fazila zako; unapotazama haki ya moyo wako, usizarau jirani yako kama alivyofanya Mfarisayo mwenyi majivuno; lakini unapokumbuka zambi zako na moyo wa sikitiko na unyenyekevu umwambie Bwana kama alivyofanya Mtoza kodi*:* Unihurumie mimi mwenye zambi na uniokoe. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi

Ee Bwana, mashahidi wako hawakukukana, hawakujitenga toka mafundisho yako*:* Kwa maombezi yao utuhurumie.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Alipokuona umutundikwa Musalabani, Mutakatifu kamili akapaza sauti*:* Hii ni fumbo gani ninaona, ee Mwanangu? Namna gani unaweza kufa mwenyi kusulubiwa mwilini mwako, wewe Muletaji wa uzima?

MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA YA INE

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya ine. O Ipsothis en to stavro.

Inapotakasa muda wa Kwarezima, Musalaba takatifu inajitoa machoni mwetu; na tunaposujudu mbele yake tumulalamikie Bwana*:* Ewe Mupenda-wanadamu, kwa agano lake utupe sisi kutimiza hii Kwarezima katika toba na kuona Mateso yako ya uzima iliyotukomboa.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, huyu aliyekuzaa kwa mwisho wa nyakati alipokuona umetundikwa Musalabani wewe Neno uliyezaliwa kwa Baba wa milele akalia na kusema*:* Ole wangu, ee Mwanangu mupendwa, namna gani unasulubishwa kwa makafiri kwa kutaka kwako wewe Mungu Malaika wanaimbia mbinguni? Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

KATHISMA WA TATU.

Sauti ya ine. Takhi prokatalave

Ee Kristu katika Musalaba wako heshimiwa ni nuru ya roho zetu sasa tunaona; na tunaposujudu mbele yake, tunakupazia sauti na furaha*:* Utukufu kwako ambaye katika hii ulitukuzwa kwa kutaka kwako, utukufu kwako ambaye katika hii uliangaza viumbe vyote; katika hii tunakuimbia daima kwa kukutukuza.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Neno la Mungu, alipokuona umetukuzwa Musalabani, Mama yako Mutakaitfu akalia na kusema*:* Hii ni ajabu gani, ee Mwanangu? Wewe uliye Uzima wa ulimwengu namna gani unaweza kushuka ku mauti? Lakini kwa rehema yako unataka kuwarudishia wafu uzima.

FOTAGOGIKON YA SAUTI YA HII JUMA

APOSTIKHA

Sauti ya ine. Idiomelon.

Ee Bwana, wewe mwenyi kuonyesha waziwazi ukweli unajua siri za kila mumoja*:* Mfarisayo aliposhindwa kwa majivuno yako mwenyewe na alipojiwazia kuwa na haki kwa matendo yake ya fazila ulimuhukumu, lakini Mtoza-kodi ulimupa haki japo hukumu ya wa kwanza, kwani aliomba kwa kulia na kusikitika; ee Bwana musulubiwa, utupe sisi tufananishe toba yake na utustahilishe tupokee rehema yako. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi.

Enyi Mashahidi Watakatifu, namna gani hatutashangaa mashindano kubwa mulishindana? Mwilini mwenu mulishinda adui asiye na mwili kwa kumukiri Kristu kwa nguvu ya alama ya Musalaba; ndiyo maana mulipokea uwezo wa kufukuza mashetani na kugombanisha adui*:* Ombeni daima kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . .

Sauti ya mnane.

Leo Mufalme wa utukufu, Rabi wa ulimengu anasulubiwa Musalabani kwa kutaka kwako, mukuki inachoma ubavu wake; anaonja siki na nyongo yeye ndani yake Kanisa inapata rehema, anavikwa taji ya miiba yeye mwenye kufunika mbingu na mawingu; anavikwa nguo ya zihaka na ana pigwa makofi yeye aliyeumba watu kwa mukono wake; anapigwa fimbo fimbo mugongoni yeye mwenye kuvika mbingu na mawingu, anapigwa makofi na kutemewa mate; makofi, matusi, anateswa hii yote sababu ya kuokoa dunia toka mauti, kwani yeye ni Mkombozi na Mungu mwenye huruma.

MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA YA INE

Elezo*: Kisha* «Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo na ma shairi kumi; ya kwanza tunaimba wimbo hii.*

Sauti ya saba.

Kwa tamaa niliweka utumwani roho yangu, nimefanana na nguruwe; kwako siwezi kuinua macho, ee Mungu aliye juu, lakini kama Mtoza-kodi nainama chini udongoni, ee Kristu, nakuomba na kupaza sauti*:* Unihurumie, ee Bwana, na uniokoe.

Sasa tunaendelea twimbe wimbo wa Mashahidi. Ona ku mwisho ya hii Kitabu na sauti ya hii Juma. Kisha tunaimba wimbo ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . (*Wimbo ya wafu ku mwisho ya hii Kitabu).*

Sasa na siku zote. . . *(Theotokion ya Ufufuo na sauti ya hii Juma).*

KUINGIA

Mwangaza upole. . .

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 79.
Uturudisha tena, ee Bwana Mungu wa majeshi.
Shairi*:* Usikie, ee Muchungaji wa Israeli.

Somo ya Mwanzo tutasoma (12, 1-7).

Basi Bwana akamwambia Abramu*:* Toka wewe katika inchi yako, na katika ndugu zako, na nyumba ya baba yako hata inchi nitakayokuo-nyesha; na nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na nitakubariki, nitatukuza jina lako, nawe uwe baraka; na nitawabariki wanaokubariki; naye anayeyekulaani nitamulaani vilevile, na ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa.

Hivi Abramu akakwenda, sawasawa Bwana alivyomwambia; Loti akakwenda pamoja naye; na Abramu alikuwa na miaka makumi saba na mitano wakati alipotoka katika Harani. Abramu akatwaa Sarai muke wake, na Loti mwana wa ndugu yake, na mali zao zote walizozipata, na watu wahopata katlka Haranl; wakatoka kwenda kwa inchi ya Kanana ; wakaingia inchi ya Kanana. Abramu akapita katika inchi hata pahali Sekemu kwa mwelo wa More. Na Mukanana alikuwa inchini kwa wakati ule. Bwana akaonekana kwa Abramu akamwambia*:* Uzao wako nitawapa inchi hii; akajenga pale mazabahu kwa Bwana aliyeonekana kwake.

Prokimenon. Sauti ya mbili. Zaburi 80.
Imbieni Mungu nguvu zetu.
Shairi*:* Pazeni zaburi na pigeni matari.

Somo ya mezali tutasoma (14, 15-26)

Mujinga anaamini kila neno*:* Lakini mwenye akili anaangalia sana namna anavyokwenda. Mwenye hekima anaogopa, naye antljitenga na uovu*:* lakini mupumbafu ana jeuri na kujitumaini. Mwenye kukasirika mbio atatenda kwa ujinga*:* Na mutu mwenye kutenda uovu anachukiwa. Wajinga wanariti upumbafu*:* Lakini wenye akili wanapata taji ya maarifa. Wabaya wanainama mbele yao walio wema; Na waovu kwa malango ya wenye haki. Masikini anachukiwa hata na jirani yake mwenyewe*:* Lakini tajiri ana rafiki wengi. Mwenye kuzarau jirani yake anakosa*:* Lakini mwenye kuhurumia masikini ana herì. Hawakosi wanaowaza mabaya? Lakini rehema na kweli zitakuwa kwao wanaowaza mema. Katika kila kazi kuna faida*:* lakini maneno ya midomo yanaleta hasara tu. Taji ya wenye hekima ni mali zao*:* Lakini upumbafu wa wapumbafu ni upumbafu tu. Mushuhuda wa kweli anaponyesha nafsi za watu*:* lakini mwenye kutoa uwongo analeta udanganyifu. Kuogopa Bwana ni tumaini la nguvu*:* Na watoto wake watakuwa na pahali pa kukimbilia.

Elezo*: Sasa inaendelea Liturgia ya Vitu Vitakatifu wa Wenye Kutakaswa.*

MU POSHO ASUBUI YA JUMA YA INE

Kisha Eksapsalmos pahali pa: «Bwana ndiwe. . . » *tunaimba: Alliluia tatu mara wa ine na kisha hii wimbo:*

Sauti ya mbili.

Mitume, Manabii na mashahidi, Maaskofu Watakatifu na wenye haki wote, ninyi muliyolindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Bwana, kwa wema wako uwakumbuke, watumishi wako na wenye haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mama wa Nuru isiyokadirika, kama Malaika mbinguni tunakuimbia kwa kukutukuza.

KATHISMA YA KITABU PARAKLITIKI NA SAUTI YA HII JUMA

Kisha tunaimba Kathisma ya wafu. Ni hii:

Sauti ya tano

Ee Mungu Mwokozi, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu, pamoja na wenye haki pumzisha watumishi wako na uwaruhusu wakae katika uwanja wako, usihesabie makosa yao ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Utukufu kwa Baba. . .

Ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Kristu Mungu wetu uliyezaliwa kwa Bikira sababu ya kuangazia ulimwengu, kwa maombezi yake utufanye sisi kuwa wana wa nuru, ee Bwana, utuhurumie.

KANUNI

Tunaimba Kanuni ya Mineon, pa fasi ya Kontakion tunasoma wimbo ya Mashahidi (Martirikon), Sinaksarion ya Watakatifu ya leo, uliye wathamani, Fotagogikon na Apostikha. (Angalia ku mwisho ya hii Kitabu mu sauti ya hii Juma)

MASIFU NA APOSTIKHA YA PARAKLITIKI

Utukufu kwa Baba . . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

JUMA YA INE YA KWAREZIMA

SIKU KUU YA MTAKATIFU MUTAWA YOANO WA MUNGAZI (KLIMAKOS)

Elezo*: Kisha Zaburi ya Proimiakos na Zaburi ya* «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo sita ya Ufufuo ku Kitabu ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma na kisha wimbo ya Mt. Yoano wa Mugazi.

Sauti ya mnane. O tu paradoksu Thavmatos.

Ee Padri mutawa, Mtakatifu Yoane, uliimbia daima kwa sauti kubwa utukufu wa Mungu, ulifikiri maneno yake yenye kuongozwa kusudi yazae matunda ya hekima; na ulipokuwa mtajiri wa neema ya Juu-mbinguni, ulistahili heri ya milele. *(mara mbili).*

Kwa maji ya machozi yako, ee padri mutawa Mtakatifu Yoane, roho yako ilitakaswa, na kwa makesha yako ya usiku yote ulipokea neema kwa Mungu, ulipanda kwa mapendo yake, ee Padri mwenyi heri, kwa uzuri wake; na unafurahi katika furaha ya milele.

Ee Padri mutawa, Mtakatifu Yoane, kwa imani ulipanda kwa Mungu juu ya mabawa ya roho, uliacha machafuo wa hii dunia yenyi kutikisika; uliposhika sauti yako ulifuata Kristu, kwa utawa wako ulishinda tamaa ya mwili wako kwa nguvu yenyi kutoka kwa Roho Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya tano.*

Uliposikiliza habari njema ya Bwana, ee Padri mutawa Mtakatifu Yoane, uliacha dunia na mali yake na sifa yake ilikutolea; kisha ukawaambia watu wote*:* Mupendeni Bwana mutapata neema ya milele; kwani mapendo yake haitamainie kitu, na wakati atakapokuja katika utukufu wake mutapumuzika kati ya Watakatifu wote. Kwa maombezi yao, ee Kristu, leta neema ya wokovu rohoni mwetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION YA PARAKLITIKI**.

APOSTIKIO YA PARAKLITIKI.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita*

Tutukuzeni Mtakatifu Yoane, kwani alikuwa malaika hapa chini na mutu wa Mungu mbinguni, pambo ya dunia na hazina ya fazila, utukufu na nguvu ya watawa; alipopandwa nyumbani mwa Mungu, kama alivyo mwenyi haki, alichanuka kama muti mkubwa jangwani; alistawisha kundi la kondoo wa Kristu katika uhaki na utakatifu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ni jambo la ajabu kupita maajabu yote ya zamani*:* hakuna mutu hata mumoja amekwisha ona bikira kuzaa mutoto na kubeba mikononi mwake huyu mwenyi kukumbatia viumbe vyote; hii uzazi ni Mungu aliitaka, na kwa sababu ulimubeba mikononi mwako kama mutoto na mbele yake una matumaini ya mama, ee Bikira safi kamili, utuombee wokovu wa roho zetu.

Apolitikion ya Ufufuo na sauti ya hii Juma.

Utukufu kwa Baba. . . Apolitikion ya Mtakatifu MutawaYoane wa Mugazi. *Ni hii:*

Kwa mawimbi ya machozi yako ulistawisha jangwa kavu, kwa maombolezo yako ya ndani ulitoa ku mateso yako matunda mara mia moja na kupita, kwa miujiza yako ya ajabu umekuwa taa yenye kuangaza ulimwengu wote: Mutawa Baba yetu Yoane, umuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

Sasa na siku zote. . . Theotokion ya Ufufuo na sauti ya apolitikion ya Mt. Yoane

SIKU YA MUNGU ASUBUI YA MT. YOANE WA MUGAZI

Elezo*: Kisha Eksapsalmos, «Bwana ndiwe Mungu. . . tunaimba Apolitikia sawa jana. Kisha tunaimba kathismata ya Paraklitiki. Mahimidi ya Ufufuo. Anavathmi ya sauti ya hii Juma. Evangelion ya Asubui. Kisha:* «Tukiona ufufuo wa Kristu. . . », *Zaburi 50 (51) na wimbo haya:*

Utukufu kwa Baba. . .

Unifungulie milango ya toba, ee Bwana chemchem ya uzima;. . . . . .

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya mnane.*

Uniongoze njiani ya wokovu, ee Mzazi-Mungu, ...

Sauti ya sita

Unirehemu, ee Mungu sawasawa ni wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uufute makosa yangu.

Nikikumbuka wingi wa matendo yangu mabaya, ...

KANUNI YA UFUFUO WA KRISTU

KANUNI YA TRIODI

Wimbo wa kwanza. *Sauti ya tano. To Sotiri Theo.*

Ee Kristu, nafanana na msafiri aliyeshambuliwa na wanyanganyi, wakamupiga sana kwa sababu mimi zabihu ya zambi zangu.

Usizarau uzaifu wangu, ee Mungu Mwokozi, sikiliza kulia kwangu*:* Mali yako nimeitoa kwa wanyanganyi; ee Mungu wa mapendo, nakuomba, uniokoe.

Ulitunza roho yangu yenyi kujeruhiwa na unyanganyi wa zambi na kwa mawazo mbaya*:* Ee Kristu Mwokozi, kwa mapendo yako uniokoe.

THEOTOKION

Ee Mama wa Kristu umuombe daima huyu aliyejifanya mutu kwako bila kuacha kifua cha baba ili aokoe viumbe toka hatari yote.

KANUNI YA MUTAKATIFU MUTAWA YOANE WA MUGAZI

Wimbo wa kwanza . *Sauti ya mnane. Igran diodefsas*

Wewe uliyepanda toka mateso ya hapa chini kwenda katika nuru ya milele, ee Padri mutawa, uniangazie kwa maombezi yako kwa Bwana.

Kwa kufunga ulionja utamu wa wema na kukataa uchungu wa furaha*:* kupita sali na maji ya mukate, ee padri mutukufu, tuliza moyo wetu.

THEOTOKION

Ulizaa Hekima na Neno la Mungu kwa namna isiyokadirika*:* Ponyesha roho yangu yenyi kujeruhiwa, tuliza mateso ya moyo wangu.

Wimbo wa tatu. *Sauti ya tano.* Kanuni ya Triodi

Nilipotembea njiani mwa hii uzima, nimeumizwa kwa ubaya wa tamaa*:* Ee Kristu, nakuomba, uniamshe.

Roho yangu imeondolewa na wanyanganyi*:* Wameniacha njiani karibu kufa, nimejeruhiwa kwa mapigo ya zambi zangu; ee Bwana, sasa uniponyeshe.

Ee Kristu Mwokozi, kwa tamaa zangu nimeondolewa amri zako; furaha za dunia zimenipiga*:* unimwangie mafuta ya mapendo yako.

THEOTOKION

Ee Bikira safi kamili, umuombe daima huyu aliyeliwa tumboni mwako aokoe toka udanganyifu wale wenyi kukuimbia, ee Mtakatifu Mzazi-Mungu.

Wimbo ingine ya tatu. *Sauti ya mnane. Si i to stereoma.*

Ee Padri Mtakatifu, kwa moto ya utawa wako uliteketeza miiba ya tamaa na ulianmsha juhudi ya watawa.

Ee Padri Mtakaitfu, ulipomwanga utakatifu kwa harufu nzuri ya fazila zako, umekuwa, kwa ajili ya Kristu, manukato ya harufu nzuri.

Ulipozoea amri za utawa, kwa maji ya machozi yako ulizamisha tamaa kama yalivyoangamizwa majeshi ya Farao.

THEOTOKION

Tuliza machafiko ya mawazo yangu na ongoza, ee Mtakatifu Mzazi-Mungu, nguvu ya roho yangu kwa Mwana wako.

KATHISMA

Sauti ya tano. To ksenon tis Parthenu.

Ee Kristu Mwokozi, tunapokua na Musalaba wako kama silaha ya wokovu, katika hii tunaweza kukupazia sauti*:* Utuokoe, wewe uliyetaka kuteswa kwa ajili yetu, ee Mungu wa ulimwengu na Bwana mwenye rehema.

KATHISMA YA MT. MUTAWA YOANE

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya ine. O Ipsothis...

Ulipopandisha mbinguni nuru ya fazila zako na ulipotegemea juu ya udongo ya nguvu sana, uliinuliwa na ibada katika ukubwa wa mawazo; ulipostaki werevu wa shetani, ilikinga wanadamu toka vitendo vyake vibaya; ee Mtakatifu Yoane, Munguzi tukufu wa fazila, umuombe Bwana aokoe watumishi wake.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Bibi wetu, huyu anayekaa juu ya Kiti cha Wakheruvi na kupumuzika katika kifua cha Baba alipumuzika pia tumboni mwako kama juu ya Kiti chake cha umungu*:* Ni Mungu aliyevaa mwili wetu, huyu mwenyi kutawala mataifa yote; tunamuimbia kwa moyo wetu wote, na wewe Bikira Safi kamili, umuombe aokoe watumishi wake.

KONTAKION

Sauti ya ine. Epefanis simeron

Bwana alikuweka yulu ya cheo cha kiasi kama nyota ya ukweli ukiangaza kwa nuru yako mipaka ya ulimwengu, ee Mtakatifu Yoane padri wetu mwenyi kutuongoza kwa Mungu.

IKOS

Ee Padri Mtakatifu, unapokuwa makao ya Mungu, uliiangazia na fazila zako; kama zahabu safi kabisa, uliipamba na imani, matumaini na mapendo; ulipoonyesha mafundisho takatifu, ukawa mtawa na ukajiokoa mwilini, ukapata hekima, uhodari, usafi na unyenyekevu ambayo ulitukuzwa; ulipoangazwa daima kwa sala, ukastahili makao ya mbinguni, ewe Mtakatifu Yoane padri wetu mwenyi kutuongoza kwa Mungu.

SYNAKSARION YA SIKU YA MUNGU YA INE YA KUFUNGA

Elezo: *Tunasoma ya kwanza Sinaksari ya Watakatifu wa leo na kisha hii ya chini.*

Leo, siku ya Mungu ya ine, tunafanya makumbusho ya wapadri wetu mtukufu Mt. Yoane mwenye Mugazi (klimakos). Katika uzima wako, Mt. Yoane, ulijitesa, na hata kama umeonekana sasa bila uzima, unaishi milele.

Mungazi ambako unafasiri kupanda mbinguni unaeleza rohoni mwako kurudi kwa Mungu.

Kwa maombezi yake, ee Mungu wetu, utunurumie na utuokoe. Amin.

KATAVASIA YA MZAZI- MUNGU

EKSAPOSTILARION YA UFUFUO NA YA MUTAKATIFU YOANE

Sauti ya mbili. Ginekes akutistite

Furaha za dunia zilikuchukiza, na kwa kufunga uliteketeza mwili wako, lakini ulitayarisha nguvu ya roho yako na umepata utukufu wa milele wa mbinguni; ee Padri mtukufu Mtakaitfu Yoane, usichoke kutuombea.

THEOTOKION. *Umoja.*

Kweli tunakuyambua kuwa Mzazi-Mungu sisi wenye kuokolewa kwa ajili yako; kwani kwa namna isiyokadirika ulipata mimba ya Mungu ambaye kwa Musalaba wake alituokoa toka mauti, akivuta nyuma yake Watakatifu ambao pamoja nao tunatukuza utukufu wako, ee Bikira Mzazi-Mungu.

MASIFU YA UFUFUO WA KRISTU

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya kwanza*

Kujeni, tutumike katika mzabibu ya siri ya Bwana, katika hii tutavuna mavuno ya toba, bila sisi kuziba na chakula na kinywaji, lakini tukiendelesha fazila katika kufunga na sala; katika hii tutamupendeza Bwana na Rabi wa kazi atatulipa sisi mushahara wa feza moja sababu ya kukomboa roho zetu toka deni ya zambi kwa wema wake wa pekee.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA KUBWA

SIKU YA MUNGU WA INE KWA ESPERINOS

Elezo*: Kisha Zaburi ya Proimiakos na Zaburi ya:* Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo na ma shairi kumi; wimbo ine katika sauti ya hii Juma pa hii kitabu ku mwisho, wimbo tatu ya Triodi yafwatayo na wimbo tatu ya Mineon.*

Wimbo wa Triodi:

Sauti ya tatu. Megali tu Stavru su.

Enyi waaminifu, kwa hii waakti tujikaze ili tustahili utukufu kubwa wa mbinguni kwa rehema ya Mungu wetu mkubwa na Mwokozi mwneyi kutuokoa toka moto ya Hadeze.

Tulipopita sehemu ya kwanza ya hii Kwarezima tuonyeshe mwanzi wa toba ili ku mwisho wa uzima takatifu tupate heri ya milele.

Wimbo ingine. Sauti ya saba.

Tulipopita sehemu ya hii Kwarezima takatifu, twende na furaha mpaka mwisho yake, tupakae roho zetu mafuta takatifu juu ya mashindano kusudi tustahili kuabudu Mateso takatifu ya Kristu Mungu wetu na kuona Ufufuo wake tukufu.

Wimbo ya Mineon tatu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

KUINGIA

Mwangaza upole. . .

PROKIMENON KUBWA

Wala usifiche uso wako kwa mutumihsi wako kwa sababu mimi ni katika taabu; mbio inijibu ukaribie nafsi yangu na kuikomboa.

Shairi: Wokovu wako, ee Mungu, uninyanyue. *(mara ingine Prokimenon).*

Shairi: Wapole waliona na wanafurahi. *(mara ingine Prokimenon).*

APOSTIKHA

Sauti ya saba. Idiomelon.

Huyu aliyepanda mzabibu na kuita watumishi ni Mwokozi, tutamuona sasa hivi; Kujeni, kwa hii Kwarezima tupokee tuzo ya kazi yetu, kwa sababu Rabi analipa kwa ukarimu kadiri ya wema wake, japo tulitumika muda kidogo, tutapokea neema ya wokovu wa roho zetu.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama. . .

Sauti ya sita. Idiomelon

Alipoanguka katika ushambulio wa mawazo, Adamu alinyanganywa akili, roho ilipojaa na vidonda, alilala mtupu na kuondolewa msaada; na apana kuhani mbele ya Sheria wala Mlawi kisha Sheria walimutunza; lakini ni wewe Bwana Mungu wetu, ulikuja apana toka muji wa Samaria, lakini toka Bikira Maria; ee Mwokozi wa roho zetu, utukufu kwako.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunanyala na kuzarauliwa. . . .

Sauti ya sita. Wimbo wa Mashahidi

Ee Bwana, mashahidi wako hawakukukane, hawakujitenga ku mafundisho yako*:* Kwa maombezi yao utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Sauti ya sita

Tunapofananisha sauti ya Malaika, tuimbia na ibada ya Makao ya mbinguni, Mlango kweli wenye kufungwa*:* Salamu, katika wewe tumepewa Mwokozi wa ulimwengu, Kristu aliye Chemchem ya uzima na Mungu wetu;. Ee Bibi yetu, fukuza adui za imani yetu wenyi kutuzulumu; wajue uwezo wa mkono yako, ee Bikira Mtakatifu, wewe ni matumaini ya wakristu.

Elezo*: Ibada hii inaendelea katika desturi ya kila siku ya Mungu magaribi kwa Kwarezima.*

MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA WA TANO

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwishso ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA YA MBILI

Sauti ya tatu. Tin oreotita.

Tazama imekuja wakati ya neema na ya uzuri, kwa kufunga imeangaa siku tukufu; tujiharikishe, ee ninyi ndugu zangu, tujitakase kusudi tuonekane bila uchafu mbele ya Muumba na tusharikie kwa nuru yake isiyoweza kufananishwa, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu Mtakaitfu kamili.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Mbele ya neema isiyofafanishwa ya ubikira wako, mbele ya Nuru ya mapenzi na ya kimungu ya utakatifu wako, Gabrieli alipoogopa akalalamika, ee Mzazi-Mungu*:* Sifa gani yenye kustahili utakatifu wako minaweza kukuonyesha? Kwa Jina gani kubwa nitakuita? Sijui na ninakatazwa. Tena nikishika amri niliyopewa, nakuimba*:* Salamu, ewe Mjaliwa-neema.

KATHISMA YA TATU

Sauti ya saba.

Ee Bwana, unatupa sisi kuona hii siku sababu ya kutayarisha Juma Takatifu huko tutaona Lazare kufufuliwa katika wafu; uwape sasa watumishi wako watembee na woga mbele yako katika hii muda wa Kwarezima takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Uliye wa thamani kuwashinda Wakheruvi, ee Bikira Mtakatifu, ni wewe kweli; kwani wanaposhindwa kuvumilia nuru ya umungu, wanatimiza kazi yao kwa kujifunika macho na mabawa yao; lakini wewe mwenyewa uliweza kutazama Neno aliyejifanya mutu*:* Umuombe daima kwa ajili ya wema wetu.

Elezo*: Fotagogikon ya sauti ya hii juma.*

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Ee Bwana, mimi nafanana na msafiri aliyeshambuliwa na wanyanganyi, nilianguka mimi mwenyewe kwa zambi, kwani zimeniumiza mbaya sana; ndio maana usiniache bila kuniponyesha, wewe uliyetoka kwa Bikira Maria, apana toka Samaria*:* Ee Yesu, maana Mwokozi, unihurumie. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi

Namna gani tutawaita, enyi Mashahidi Watakatifu? Wakheruvi? Kwani ninyi ni kiti cha Kristu; Waserafi? Kwani munamutukuza daima; Malaika? Kwa sababu munakataa mwili wenu; Majeshi? Sababu ya miujiza yanatendeka*:* Muna majina mengi na zawadi nyingi sana! Ombeni ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Mbingu zanaimba huruma yako, ee Mama usiyeolewa, na sisi tunatukuza kuzaa kwako isiyokadirika; ee Mzazi-Mungu, ombea roho zetu wokovu.

MU KAZI MOJA MANGARIBI YA JUMA WA TANO

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo 3 ya hii Kitabu na 3 ya Mineon.

Sauti ya tatu. Stavrofanos Moisis.

Kwa hii Kwarezima unatupa sisi wakati wa kutubu na kuishi pahali pa sisi kufa; ee Neno la Mungu, utupe sisi tuweze kukupendeza daima na kukutumikia na nguvu ya toba kama alivyofanya zamani Mtakatifu kahaba mwenye hekima ambaye kwa manukato na machozi yake akapokea kwako maondoleo ya zambi zake.

Wimbo umoja.

Kama kipofu kwa moyo wangu wote nakulalamikia*:* Ee Mwana wa Mungu, angaza macho ya roho yangu; na kama mwanamuke Mkanana kwa imani yake*:* Ee Mungu wa mapendo, unihurumie; roho yangu yenye kulogewa kwa furaha za dunia uiondoe toka giza ya tamaa na unifanye niishi sasa katika usafi ili nitukuze wingi wa wema wako.

Sauti ya mbili. I theoklitos martis.

Kwa kufunga neema yenye kujaa na nuru ilituangazia leo kupita jua; inapomwanga nuru

yake rohoni mwetu, inafukuza zambi zetu kama mawingu; ndio maana tuendeni upesi na moyo laini tutembee na furaha katika hii kipindi takatifu, na kwa furaha tumulalamikie Bwana tukisema*:* Takasa wale wenyi kuitimiza na furaha.

Elezo*: Sasa tunaimba wimbo tatu ya Mineon.*
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 85
Unifundishe njia yako, ee Bwana, nitatembea katika kweli yako.
Shairi*:* Uiname sikio lako, ee Bwana, unijibu.
Somo ya mwanzo tunasoma (13, 12-18)

Abramu akakaa katika inchi ya Kanana, na Loti alikaa katika miji ya inchi sawa akahamisha hema yake hata Sodomo. Basi watu wa Sodomo walikuwa wabaya, na wenye zambi sana mbele ya Bwana.

Bwana akamwambia Abramu, wakati alipokwisha kutengana na Loti*:* Nyanyua, sasa macho yako, na angalia toka pahali unapokuwa, kwa kaskazini na kusini na mashariki, na manganbi; kwa sababu inchi yote unayoona, nimekupa wewe na uzao wako hata milele. Na nitafanya uzao wako kuwa kama mavumbl ya inchi; hata mutu akiweza kuhesabu mavumbi ya inchi, halafu uzao wako vilevi1e utahesabiwa. Simama, utembee inchi urefu wake na upana wake; kwa sababu nitakupa wewe. Abramu akahamisha hema yake, akakuja, akapanga kwa mielo ya Mamuri, iliyo kwa Heburoni, akajenga pale mazabahu kwa Bwana.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 86
Bwana anapenda malango ya Sayuni kuliko makao yote ya yakobo.
Shairi*:* Musingi wake ni katika milima mitakatifu.
Somo ya Mezali tunasoma (14, 27-15, 4)

Woga wa Bwana ni chemchemi ya uzima, Ili kujitenga na mitego ya mauti. Utukufu wa mufalme ni wingi wa watu wake*:* lakini uchache wa watu ni uharibifu wa mukubwa. Asiye mwepesi kwa kukasirika ana ufahamu mwingi, Lakini mwenye roho ya haraka anatukuza upumbafu. Moyo ulio muzima ni uzima wa mwili ;lakini wivu ni kuoza kwa mifupa. Mwenye kutesa masikini analaumu Muumba wake*:* Lakini mwenye kuhurumia wenye hitaji anamuheshlmu. Mwovu anasukumwa chini katika kutenda mabaya kwake*:* Lakini mwenye haki ana matumaini katika kufa kwake. Hekima ni moyoni mwake aliye na ufahamu*:* lakini yaliyo ndani ya wapumbafu yanajulikana. Haki inanyanyua taifa*:* Lakini zambi ni laumu la watu wo wote. Upendeleo wa mufalme ni kwa mutumishi anayetenda kwa hekima*:* lakini hasira yake itakuwa juu yake anayeleta haya. Lakini kinywa cha wapumbafu kinamwanga upumbafu. Macho ya Bwana ni katika kila pahali, Yakitazama wabaya na walio wema. Ulimi safi ni muti wa uzima, Lakini ukaidi ndani yake unavunja roho.

APOSTIKHA

Sauti ya saba.

Kama msafiri aliyeshambuliwa na wanyanganyi, mimi mwenyewe nimenguka kwa zambi zangu, na roho yangu imejeruliwa kama Yeye*:* Kwa nani nitakimbilia mimi maskini ila kwa Mungu mwenye huruma mwenyi kuponyesha roho zetu kama Muganga? Mwangia roho yangu neema ya wokovu.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama. . .

Sauti ya ine.

Tulipofukuzwa zamani toka furaha ya paradizo, tulishuka ku uzima wa mateso, tulipoondolewa nuru ya fazila tulishambuliwa na wanyanganyi, tumepigwa mpaka kufa kwa sababu tuliacha mafundisho yako ya wokovu; lakini tunakuomba, wewe ulionekana kwa ajili ya Maria, ee Bwana usiyeteseka uliyeteswa mateso ya lufu, tunza vidonda vyetu vya zambi

utumwangie dawa ya mapendo yako kubwa.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunanyala na kuzarauliwa. . . .

Ee Bwana mpenda-wanadamu, wewe uliyekubali uvumilivu wa Mashahidi wako Watakatifu, pokea pia heshima ya nyimbo zetu, kwa maombezi yao utupe sisi neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu na Bikira utukufu, okoa watumishi wako toka hatari yote, ili tukutukuze kama matumaini ya roho zetu.

MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA WA TANO

Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:

KATHISMA YA MBILI

Sauti ya tatu. Thias pisteos.

Kwa juhudi ya imani yetu tuchome maneno ya tamaa, tufukuze baridi ya zambi na kwa maji ya machozi tuzime moto ya milele tukipaza sauti na kusema*:* Ee Mungu wa wema, tulikosa juu yako, utusamehe na utupe neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Umekuwa makao takatifu ya Neno, ee Bikira Mama Mtakatifu kamili, wewe mwenyi kupita Malaika kwa utakatifu; mimi nimejaa na matope kuliko wote, nachafuka kwa tamaa za mwili; unitakase na maji takatifu, wewe mwenye kutupa sisi neema ya wokovu kwa maombezi yako.

KATHISMA YA TATU

Sauti ya mbili.

Neema ya Kwarezima takaitfu inajaa na utukufu, katika hii nabii Elia alipanda juu ya gari ya moto, Musa alipokea mbao ya Amri, Danieli alifanya maajabu katika zimu ya Simba, Eliseo alifufua mufu, Vijana walizima moto ya tanuru; katika hii kila mumoja amakuwa rafiki ya Mungu na kwa furaha inatupatia tunaimba*:* Umetukuzwa, ee Kristu Mungu wetu uliyetaka hivi! Utukufu Kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Wakati ninahakikishwa kwa maombezi yako ya ushindi, ee Mzazi-Mungu, ninaokolewa toka wazulumu wangu juu ya matumaini yote; kwani unasaidia waaminifu wako wenyi kukuomba na unafukuza giza ya zambi; ndio maana tunakushukuru tukipaza sauti*:* Pokea shukrani yetu ya umaskini sababu ya ulinzi yako imara.

APOSTIKHA

Sauti ya saba. Idiomelon.

Tazama vidonda vya roho yangu yenyi kuzarauliwa, ee Bwana muganga wa wagonjwa na makimbilio ya wasiyo matumaini; Uko kweli Mkombozi wa dunia anayekuja kuamsha waovu kaburini; unifufue na mimi pia kwa wema wako kubwa*. (mara mbili).*

Mbele ya baraza ya hukumu wa wakafiri katika uwanja Mashahidi Watakatifu walipaza sauti kwa furaha wakasema*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Tunakuimbia, ee Bikira Mzazi-Mungu, tunatukuza Neno ulizaa na tunakulalamikia*:* Utukufu kwako.

MU KAZI MBILI MANGARIBI YA JUMA WA TANO

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo 3 ya hii Kitabu na 3 ya Mineon.

Sauti ya mnane. Ti imas kalesomen.

Enyi waaminifu, tukamateni mapendo kuwa chakula, kwa kufunga tushinde tamaa zetu; tujikaze tuishi kama inavyomupendeza Bwana ambaye aliyeinuliwa Msalabani kwa ajili yetu na kuchomwa mkuki ubavuni kusudi sisi tupate uzima wa milele, tutukuzeni Mwokozi wa roho zetu.

Zamani tulipokufa sababu ya muti uliyokataziwa, sasa tunapata uzima kwa muti ya Msalaba; enyi waaminifu, turegeze nguvu ya tamaa zetu na tumuombe mfazili wa ulimwengu neema ya kuona ufufuo wake wa utukufu, kwa nuru ya matendo takatifu na ya fazila tukimutukuza Mwokozi wa roho zetu.

Sauti ya mbili.

Ee Bwana, tunaimba Msalaba wako wenyi kuleta uzima na Mateso yako takatifu, uliteswa kwa ajili yetu, mukuki na sadaka, zihaka, mate, mapigo na makofi, taji ya miiba na nguo ya zihaka; kwa sababu kwa kuteswa ulituokoa wote toka laana ya zamani; ndio maana tunakuomba*:* Utupe sisi tutimize wakati ya Kwarezima katika amani.

Elezo*: Sasa tunaimba wimbo tatu ya Mineon.*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya inne. Zaburi 89.

Bwana, wewe, umekuwa makao yetu, kizazi kwa kizazi.

Shairi*:* Uzuri wa bwana Mungu wetu uwe juu yetu.

Somo ya Mwanzo tutasoma (15, 1-15).

Nyuma ya maneno haya neno la Bwana lilikuwa kwa Abramu katika ndoto likisema*:* Usiogope, Abrama, mimi ni ngabo yako na zawabu yako kubwa sana. Abramu kasema*:* Ee Bwana Mungu, utanipa nini kwa kuwa mimi sina mutoto, naye atakayekuwa mwenye nyumba yangu ni Eliezeri Mudamasiki? Abrau akasema*:* Tazama, hukunipa uzao; na tazama, mumoja aliyezaliwa nyumbani mwangu ni muriti wangu. Na tazama, neno la Bwana lilikuja kwake likisema*:* Mutu huyu hatakuwa muriti wako; laikini yeye atakayetoka viunoni mwako, yeye atakuwa muriti wako. Akamutoa inje, akasema*:* Tazama sasa mbinguni, na hesabu nyota kama ukiweza kuzihesabu; akamwambia*:* Ndivyo itakavyokuwa uzao wako. Akaamini Bwana; akamuhesabia kwa haki. Akamwambia*:* Mimi Bwana niliyekuleta toka Uri wa Wakaldea, kukupa inchi hii uiriti. Akasema*:* Ee Bwana Mungu, namna gani nitajua ya kama nitairiti? Akamwambia*:* Unitwalie ndama ya miaka mitatu, na mbuzi dike ya miaka mitatu, na kondoo ndume ya miaka mitatu, na hua, na mwana-njiwa. Akajitwalia hawa wote, akawagawa katikati, akaweka kila kipande kando ya mwenzake; lakini ndege hakuwagawa. Wakati tai waliposhuka juu ya vitumba, Abramu akawafukuza. Na wakati jua lilipokuwa likishuka, usingizi muzito uliangukia Abramu; na tazama, hofu ya giza kubwa ilimwangukia. Akamwambia Abramu*:* Jua kabisa ya kwamba uzao wako utakuwa mugeni kwa inchi isiyo yake, na watawatumikia watu wale, nao watawatesa miaka mia ine. na vilevile nitahukumu taifa watakaowatumikia; na nyuma watatoka na mali nyingi. Lakini wewe utakwenda kwa baba zako kwa salama; utazikwa mwenye uzee wema.

Prokimenon. Sauti ya tano. Zaburi 90.

Yeye anayekaa kwa pahali pa maficho yake aliye juu.

Shairi*:* Nitasema juu ya Bwana, yeye ni pahali pangu pa kukimbilia na boma la nguvu langu.

Somo ya Mezali tutasoma (15, 7-19).

Midomo ya wenye hekima inasambaza maarifa*:* Lakini si moyo wa wapumbafu. Zabihu ya mwovu ni machukizo kwa Bwana*:* Lakini maombi ya mwenye haki ni furaha yake. Njia ya

mwovu ni machukizo kwa Bwana*:* Lakini anamupenda anayefuata haki. Kuna azabu kali kwake mwenye kuacha njia*:* Na mwenye kuchukia laumu atakufa. Hadeze na Abadoni ni mbele ya Bwana*:* Kuzidi sana mioyo ya wana wa watu! Mwenye kuzarau hapendi kuhamakiwa*:* Hatafika karibu na wenye haki. Moyo wa furaha unaleta uso wa furaha*:* Lakini kwa huzuni ya moyo roho inavunjika. Moyo wa mwenye ufahamu unatafuta maarifa*:* Lakini kinywa cha wapumbafu kinajikulisha upumbafu. Siku zote za mutu anayeteswa ni mbaya*:* Lakini mwenye moyo wa furaha ana karamu daima. Kuwa na mali chache pamoja na woga wa Bwana, Ni vizuri kuliko hazina kubwa pamoja na taabu. Chakula cha mboga pahali palipo mapendano Ni vizuri kupita ngombe aliyenona pamoja na kuchukia. Mutu wa hasira anaamsha ugomvi*:* Lakini asiye mwepesi kukasirika anatuliza mashindano. Njia za mutu muvivu ni kama boma la miiba*:* Lakini mapito ya wenye ha. kiyanafanywa kuwa njia kubwa.

APOSTIKHA

Sauti ya tano. Idiomelon.

Nilipojitenga toka njia sawa kwa tamaa, nimeanguka katika zimu, mimi maskini; kuhani na mlawi walipita pembeni ya njia wakizarau; lakini wewe, ee Kristu, ulinihurumia na kwa muti wa Msalaba wako ulipasua barua ya zambi zangu; ulinisabitisha kushinda tamaa, ulinisharikisha ku utukufu na Baba, ndio maana nakulalamikia*:* ee Mungu wa mapendo, Bwana, utukufu kwako.

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama. . .

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Toka Yerusalema nilishuka nikashuka nikajitenga ku amri zilizopewa kwa watu; nilienda ku Yeriko nikifananisha kwa mateso yangu wakaaji wa hii muji uliapiza zamani, ee Bwana; na kama wanyanganyi, tamaa zilinishambulia zikaumiza roho yangu kwa mapigo yao na zikanyacha karibu kufa; lakini wewe ambaye mwili ulijeruhiwa kwa mukuki na misumari sababu ya zambi za wanadamu na uliyetimiza kule Yerusalema kwa Msalaba wako wokovu wa wote, uniponyeshe, ee Bwana, na uniokoe.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunanyala na kuzarauliwa. . . .

Ee Bwana, Mashahidi wako waliposahau hii uzima na kuzarau tena mateso sababu ya uzima wa milele, walipata uriti wa mbinguni na wanafurahi pamoja na malaika*:* Kwa maombezi yao uwape watu wako neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bwana, wakati jua ilikuona, wewe uliye Jua ya haki, umetundikwa Msalabani, ikapata giza na ikaficha nuru yake, nuru ya mwezi ikawa giza, moyo wa Mama yako Mtakaitfu ikachomwa.

MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA WA TANO

Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:

KATHISMA YA MBILI

Sauti ya mnane. To prostakthen.

Adamu alipokula tunda la muti uliyokataziwa alikula matunda ya uchungu; na wewe Mungu wa mapendo ulipoinuliwa Msalabani, ukamukomboa toka laana ya uchungu; ndio maana tunakuomba, ee Bwana, utupe sisi tukatae tunda lenyi kuleta mauti na tufanye mapenzi yako sababu ya kustahili mapendo yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Bikira safi kamili, ulipoona ametundikwa Msalabani katikati ya wanyanganyi huyu aliyejifanya mutu tumboni mwako safi na kumuzaa kwa namna ya ajabu, moyo wako ikapata

uchungu na kama mama ukalia kwa kupaza sauti*:* Ole wangu, ee Mwanangu, hii ni fumbo gani isiyokadirika na ya kimungu ambayo unaokoa nayo viumbe vyako kwa kuwapa uzima! Naimbia mapendo yako na rehema yako.

KATHISMA YA TATU.

Sauti ya mbili. Tin Akhranton Ikona su.

Tunapotukuza muti takatifu kamili ya Msalaba, tunaabudu wema wako kubwa, ee Kristu Mungu wetu; Kwa hii uliharibu nguvu ya Adui, ukaifanya kuwa alama ya wale wenyi kukuamini wewe; ndio maana kwa shukrani tunakulalamikia*:* Utupe sisi tutimize wakati wa Kwarezima katika amani na katika furaha.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Kondoo mama alipokuona umetundikwa Msalabani, wewe Mchungaji mwema, akalia na kupaza sauti*:* Ee Mwanangu, watu wasio na shukrani wanakuhukumu uuawe, hawa watu uliokoa zamani kwa kuwaongoza katika wingi; amka, angaza, ee Jua, na nitatukuzwa katikati ya wana wa dunia.

APOSTIKHA

Sauti ya tatu. Idiomelon.

Ee roho yangu, ulipoacha ncha ya fazila, ulishuka ku zimu ya zambi; ulipoanguka katika mikono ya wanyanganyi, tazama umejaa na vidonda; lakini kwa kukusaidia umuite Kristu Mungu wetu aliyejeruhiwa na kusulubiwa Msalabani kwa ajili yako ukisema*:* Kuja unisaidie, ee Bwana, na uniokoe.

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Ee Bwana, nilipojeruhiwa kwa mawazo mbaya mimi maskini, nilibaki karibu kufa; Manabii wengi hawakuniangalia, wakaniona karibu kufa, sitaweza kupona kama walivyazani wanadamu; na ninapoteswa vibaya nakulalamikia kwa unyenyekevu wa moyo wangu*:* Ee Kristu Mungu wangu, umwangie kama dawa nzuri roho yangu neema ya wokovu.

Wimbo ya Mashahidi. Sauti umoja.

Ee Mashahidi washindi wa Kristu, ninyi mulioshinda udanganyifu kwa uwezo wa Msalaba, mulipokea neema ya uzima wa milele; bila woga mbele ya makamio ya wazulumu, muliteswa; sasa munafurahiwa na roho zetu zinaponyeshwa kwa damu yako*:* Ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, Mtakatifu kamili alipokuona umetundikwa msalabani kwa kutaka kwako, alipojua uwezo wako, akahuzunika na kwa uchungu wake akakulalamikia: Usimuache Mama yako, ee Mwanangu, usinyamaze kwangu, ww Mwanangu, lakini umjibu mjakazi wako, ee Neno la Mungu.

MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA WA TANO

Elezo*: Kisha Zaburi ya Proimiakos na Zaburi ya:* Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo ya Triodi na shairi hii ifwatayo:*

Shairi: Waovu waanguke katika nyavu zao wenyewe, wakati mimi ninapopona na salama*:*

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Nilipoanguka kwa uwezo wa mawazo mbaya yaliyoninyanganya roho yangu, mimi maskini, tazama najaa vidonda; roho yangu yote inajeruhiwa, nimelala bila vazi, nimeondolewa fazila njiani ya hii uzima; kuhani mumoja bila kuniponyesha alipita pembeni bila kuona uchungu wangu; mulawi mumoja alipochukizwa kwa mateso yangu, akaendelea

na safari yake; lakini wewe uliyetokea kwa Bikira Maria apana toka muji ya Samaria, kwa mapendo yako, ee Kristu, uniponyeshe ukimwangia roho yangu neema ya wokovu.

Shairi: Kwa sauti yangu ninalilia Bwana; kwa sauti yangu ninasihi Bwana. *(mara ingine).*

Shairi: Ninamwanga mashitaki yangu mbele yake; ninamwonyesha taabu yangu.

Utukufu yote na sifa yote ni ya Mashahidi*:* Walikatwa kichwa sababu yako wewe uliyeshuka kwa kuinamisha mbingu; walimwanga damu yao kwa ajili yako wewe uliyejishusha kwa kutwaa hali ya mtumwa; na walipojishusha mpaka kufa, walifwata umaskini wako*:* Ee Bwana, kwa maombezi yao na kwa rehema yako, utuhurumie.

Shairi: Wakati nilipozima roho, umejua njia yangu.

Sauti ya ine. Kirie i ke kritirio.

Ee Bwana uliyewafanya Mitume wako Watakatifu kuwa Paradizo ya roho, kwa maombezi yao uniokoe toka mateso ya hapa chini na kwa kufunga inua roho yangu ukiiondoa ku tamaa, kwa wema wako wa pekee na mapendo yako kwa wanadamu.

Shairi: Katika njia ninapokwenda wamenifichia mutego.

Wakati wa hii Kwarezima takatifu inatusaidia kupata neema ya Mungu*:* Tulieni kwa moyo wetu wote na tumulalamikie Mwokozi*:* Kwa maombezi ya Wafwasi wako, ee Bwana, okoa wale wenyi kuimnia na imani rehema yako na mapendo yako kwa wanadamu.

Shairi: Utazame kwa mukono wa kuume, uone wa maana hakuna mutu anayenijua.

Enyi Mitume wenyi kustahili sifa munaoombea dunia, munapoponyesha wagonjwa na kulinda wenye afya njema, kwa wakati wa kufunga mutulinde sisi mara mbili, mutufanye tuishi katika amani pamoja na wote, tuwe na moyo wa amani na tuopolewe toka mateso kusudi tumwimbie Kristu aliyetufufua wote kama mushindi wa mauti.

*Wimbo na Sauti ya ine*e. *Ithelon dakrisin eksalipse.*

Shairi: Makimbilio yamenipotea; hakuna mutu anayekumbuka nafsi yangu.

Nilitumia vibaya uzima yangu yote pamoja na watoza kodi na makahaba; katika uzee wangu nitaweza kutubu zambi zangu? E Muganga wa wagonjwa na Muumba wa ulimwengu, mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Nikalia kwako, ee Bwana; Ninasema*:* wewe ni kimbilio langu, sehemu yangu katika inchi yao waliohai.

Nilipovutwa kwa uzito wa zambi, nazunguka katika matope ya tamaa; nilipochomwa mikuki ya Beliali, nilichafua sura ya mfano wangu na wewe; ee Mlinganifu wa wavivu na Mwokozi wa wapotevu, mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Usikilize kilio changu; kwa maana nimeshushwa chini sana*:*

Kwa wanadamu mimi ni mnaso, kwani niliendelesha paka vitu vya hapa chini; wewe uliniumba kwa udongo usizarau kazi ya mikono yako*:* Lakini mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Sh*a*iri*:* Uniponyeshe nao wanaonifuata; kwa maana wao wana nguvu kuliko mimi.

Nilikosa kwa kutaka kwangu kuliko wote, ni kwa sababu ya hii nimehukumiwa; adui wa roho yangu ni majivuno ya mwili wangu; ee Mwongozi wa wapotevu na Nuru ya wasio na kitumaini, mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Toa nafsi yangu katika kifungo. ili nishukuru jina lako*:*

Nabii anasema*:* roho yangu itaishi na itakutukuza, ewe Bwana; mimi ni kondoo mpotevu*:* uniite nirudi katika zizi lako; unipe wakati wa mimi kutubu kusudi kwa kulia nikulalamikie*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Wenye haki watanizunguka; kwa kuwa wewe utanitendea kwa ukarimu.

Nilikosa kwa kuzarau amri zako, ee Kristu Mungu wetu; unihurumie, ee mfazili, ili macho yangu ya ndani iondoshwe giza, na kwa woga nakulalamikia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Toka vilindini nimekulilia, ee Bwana. Bwana, sikia sauti yangu.

Nyama ya pori wamenizunguka*:* Uniokoe toka kucha zao, ee Bwana, unataka wote waokoe na wajue ukweli; okoa watu wote, ee Muumba, kusudi nipate sehemu yangu pamoja na wote; mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Masikio yako yasikilize sauti ya kusihi kwangu.

Uniponyeshe, ee Mkombozi na Mfazili, Mwokozi, usikae mbale na mimi; tazama nimelela katika zambi, uniamshe, ee Mwenyezi, kusudi mimi pia niungame makosa yangu na nikulalamikie*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Kama wewe Bwana, ukihesabu maovu, ee Bwana, nani atayesimama? Lakini usameni pamoja nawe, ili uogopwe.

Nilipoficha talanta ulinipa, nikaiweka katika udongo kama mtumishi mupumbafu; nilihukumiwa kuwa wasipo mafaa na sisubutu kukuomba kitu hata moja; unihurumie kwa wema wako kusudi mimi pia niweze kukulalamikia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Ninangojea Bwana, nafsi yangu inangoja, na ninatarajia neno lake.

Kwa mwanamuke aliyetoka damu aligusa nguo yako ulikausha maji ya mateso yake; na mimi nitapokea maondoleo ya zambi zangu kwa kukujongea na imani; kama yeye, unipokee na ponyesho maumivu yangu; mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Nafsi yangu inangoja Bwana, kuliko walinzi wanaongoja asubuhi; ndiyo, walinzi wanaongoja asubuhi. Ee Israeli, utarajie Bwana.

Wewe ambaye neno liliumba inchi na mbingu, utakuja kukaa juu ya kiti cha ufalme; na sisi wote tutahukumiwa sababu ya kukuungamia zambi zetu; mbele ya hii siku ya hatari pokea toba yangu*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

S*h*airi*:* Maana pamoja na Bwana ni rehema, na pamoja naye ukooombozi mwingi. Naye atakomboa Israeli na maovu yake yote.

Unitazame kwa wema wako na unihurumie, ee Mwokozi; mwangia roho yangu maskini yenyi kuteswa maji ya maponyesho; unitakase uchafu yote ili niweze kukuimbia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Musifu Bwana, ninyi mataifa yote; mumutolee, ninyi watu wote.

Roho yangu maskini ilikatwa mbio-mbio kwa upanga Baliali alitayarisha; amenifanya kuwa mugeni ku nuru ya uso, ee Bwana; lakini kwa uwezo wa mukono yako uniokoe toka meno yake; mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Maana rehema yake kwetu ni kubwa; na kweli ya Bwana inakaa milele. *(mara ingine).*

Shairi: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama macho ya watumishi yanaangalia kwa mkono wa Bwana kama macho ya kijakazi kwa mkono wa bibi yake, hivyo macho yetu yanavyoangalia kwa Bwana Mungu wetu hata akatuhurumia.

Mimi wote nimekuwa mtumwa wa tamaa, nimeacha amri na Maandiko Takatifu; uniponyeshe mimi wote, ewe mfazili ambaye kwa mapendo yako ulijifananisha na mimi; wewe mwenye kushinda tamaa, unirudishe kwako, ee Mungu wa wema; mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa. Nafsi yetu inayala na kuzarauliwa kwa wenye kuikala na salama tena na kuzarau kwa wenye kiburi.

Mwanamuke mwenye zambi alinawisha miguu yako na machozi yake, ee Bwana; kwa kumufwata anatualika wote tupokee maondoleo ya zambi zetu; ee Mwokozi unipe na mimi imani ileile ili niweze kukulalamikia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Safisha uchafu ya roho yangu, wewe uliyetaka kujua utoto na umaskini; unimwangie maji ya mapendo yako, ee Kristu, juu ya uzaifu wangu na uregevu wangu; takasa uovu wangu, sina na nguvu, uniponyeshe; mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Sh*a*iri*:* Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Sabitisha roho yangu, ee Bwana, iwe wepesi kukutumikia; wewe ni boma langu, ulinzi wangu, msaada wao na ngao yangu; unipe, ee Neno takatifu, nguvu ya kukulalamikia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mwokozi Yesu, uwe boma letu, tegemeo yetu, wewe Mungu mwenyi kutupenda sana; kwa sababu sisi wote tulikosa katika matendo ya uwongo; ewe mwema amsha kazi ya mikono yako, kwa huruma yako utusamehe; mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mimi ni mwana mupotevu*:* Nilitumia vibaya mali yako na tazama nateswa kwa njaa; nakimbilia kwa ulinzi wako, ee Baba wa mapendo, unipokee kama Yeye unipe nishariki ku karamu yako na uniruhusu nikulalamikia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Kwa chuki Mfalme wa uovu alifukuza mutu wa kwanza mu Paradizo; Munyanganyi aliingiamo akisema Msalabani*:* Ee Bwana, unikumbuke; ninapojaa na woga na imani, nakulalamikia mimi pia*:* Unikumbuke, mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Kama kwa Petro uninyoshee mukono, uniondoe zimuni, ee Bwana, unipe neema yako na kunisamehe kwa maombezi ya Mama yako Mtakatifu kamili aliyekuzaa bila mbegu na kwa maombezi ya Watakatifu wote, mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mwana-kondoo unayeondoa zambi zangu, unipokee mimi mwenyi kukuimbia kila siku; naweka roho yangu yote na mwili wangu wote mikononi mwako; usiku kama mchana sababu ya makosa yangu nakulalamikia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Shairi: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mapendo yako ni isiyokadirika, ee Bwana wa mapendo na wa wema; peke yako usiye na zambi, usinitupe mbali ya uso wako; lakini kwa shukrani na kwa furaha niweze kukuimbia na kukulalamikia*:* Mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ni mapendo kubwa ya Bwana isiyokadirika! Ni mumoja wa kuzaa kwa ajabu! Namna gani Bikira anakubeba mikononi mwake kama mtoto wewe Muumba na Mungu wake? Ee Mfazili ulitaka kujifanya mutu ndani yake, mbele ya kupotea kwangu, ee Bwana, uniokoe.

KUINGIA.

Mwangaza upole. . .

Prokimenon. Sauti ya inne. Zaburi 93.

Ee Bwana, wewe Mungu wa kisasi.

Shairi*:* Ujinyanyue, wewe mwamuzi wa inchi.

Somo ya Mwanzo tutasoma (17, 1-9).

Wakati Abramu alipokuwa na miaka makumi tisa na tisa, Bwana, akaonekana kwa Abramu akamwambia*:* Mimi ni Mwenyezi Mungu; endelea mbele yangu na uwe mukamilifu. Na nitafanya agano langu katikati yangu nawe na nitakuzidisha sana. Abramu akaanguka kwa uso wake; Mungu akasemezana nayc akisema*:* Nami, tazama, agano langu ni pamoja nawe, na utakuwa baba ya mataifa mengi. Walajina lako halitaitwa tena Abramu, Iakini jina lako litaitwa Abrahamu ; kwa sababu nimekufanya kuwa baba ya mataifa mengi. Na nitakuzidisha sana na nitafanya mataifa nawe, na wafalme wata-toka ndani yako. Na nitasimamisha agano langu katikati yangu nawe, na uzao wako nyuma yako, kwa vizazi vyao kwa agano la milele, niwe Mungu kwako na kwa uzao wako nyuma yako. Na nitakupa wewe na uzao wako nyuma yako inchi ya kusafiri kwako, inchi yote ya Kanana, kwa uriti wa milele, nami nitakuwa Mungu wao. Mungu akamwambia Abrahamu*:* Nawe, utachunga aganolangu, wewe na uzao vako nyuma yako kwa vizazi vyao.

Prokimenon. *Sauti ya sita.* Zaburi 95.

Imbieni Bwana wimbo mupya.

Shairi*:* Imbieni Bwana, barikini jina lake.

Somo ya Mezali tutasoma (15, 20-16, 9)

Mutu mwenye hekima anafurahisha baba yake*:* Lakini mupumbafu anazarau mama yake. Upumbafu ni furaha kwake asiye na akili*:* Lakini mutu wa ufahamu ananyosha mwenendo wake. Pasipo mashauri makusudi yanazuizwa; Lakini kwa wingi wa washauri yanasimamishwa. Mutu anafurahi kwa jibu la kinywa chake*:* Na neno kwa wakati wa kufaa, ni jema sana. Kwa mwenye akili njia ya uzima inapanda juu, ili atoke katika Hadeze chini. Bwana atangoa nyumba ya mwenye kiburi*:* Lakini atasimamisha mupaka wa mujane. Mashauri mabaya ni machukizo kwa Bwana*:* lakini maneno ya kupendeza ni safi. Mwenye kutamani faida anataabisha nyumba yake mwenyewe*:* lakini mwenye kuchuka zawadi ataishi. Moyo wa mwenye haki unafikili namna utakavyojibu*:* lakini kinywa cha mwovu kinamwanga maneno mabaya Bwana ni mbali na waovu*:* lakini anasikia maombi ya mwenye haki. Nuru ya macho inafurahisha moyo*:* Nah habari njema zinanenepesha mifupa. Sikio Iinalosikiliza laumu la uzima litakaa katikati ya wenye hekima. Mwenye kukataa mafundisho anazarau nafsi yake mwenyewe*:* lakini mwenye kusikiliza kuhamakia anapata ufahamu. Woga wa Bwana ni mafundisho ya hekima, Na unyenyekevu unatangulia heshima. Mashauri ya moyo ni ya mutu*:* lakini jibu la ulimi linatoka kwa Bwana Njia. zote za mutu ni safi kwa macho yako mwenyewe*:* lakini Bwana anapima roho. Wekea Bwana kazi zako na mawazo yako ya tasimamishwa. Bwana amefanya kila kitu kwa kusudi lake*:* Ndivyo, hata waovu kwa siku ya ubaya. Kila. mutu mwenye moyo wa majivuno ni machukizo kwa Bwana*:* Hakika hatakosa azabu. Kwa rehema na kweli uovu unasafishwa*:* Na kwa woga wa Bwana watu wanajitenga na uovu. Wakati njia za mutu ziapopendeza Bwana, anamupatanlsha hata na adui zake. Afazali mali chache pamoja na haki Kuliko mapato mengi pamoja na

uzalimu. Moyo wa mtu unafikili njia yake*:* lakini Bwana anaongoza hatua zake.

MU KAZI INE ASUBUI YA JUMA WA TANO
(KANUNI KUBWA YA MT. ANDREA)

Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunasoma Zaburi 50 (51).

Sasa tunaanza kusoma ao kuimba Kanuni kubwa ya Mt. Andrea, askofu wa Kreta.

(KANUNI KUBWA YA MT. ANDREA)

WIMBO WA KWANZA.

Sauti ya sita.

IRMOS: Bwana ni msaada wangu, ulinzi wangu, ni yeye aliniokoa; ni Mungu wangu, na nataka kumutukuza, Mungu wa Baba yangu, na nitamusifu, kwa sababu amevaa utukufu.

Elezo: *Mbele ya kila wimbo tunaimba hii ombi:* Unihurumie, ee Mungu, unihurumie.

Nitanzia wapi, wakati ninapashwa kulilia matendo yote ya uzima wangu? Kwa kipindi gani yafaa kuimbia kilio changu? Lakini mu wema wako, ee Kristu, unipe maondoleo ya zambi zangu.

Twende, roho yangu, zoesha mwilo wako kwa kumutukuza Muumbaji, na tokea sasa upate haki ya kutolea kwa Mungu machozi yako ya kutubu.

Pakutembea mbali ya amri yako, nilifafanisha wazazi wetu wa kwanza, na sawa Adamu niliondolewa neema yako ya umungu na ya ufalme wasipo mwisho, sababu ya zambi yangu.

Ee, roho yangu maskini, kwa sababu gani mfano huu wa Eva wa kwanza? Mubaya ulikuwa na waangalizi wako na, udanganyifu wa uchungu, uligusa ku muti, ulionja tunda na uchungu wa zambi.

Ni uhaki, ee Mwokozi wangu, wakati Adamu sababu ya uhalifu moja alifukuzwa mu Paradizo; lakini kwa mimi, itakuwa malipizi gani, mimi niliyemkataa neno lako lenyi kuleta uzima.

Nilitembea mu nyaoyo za kaina, nilichagua kwa kuwa munaji, kwa sababu moyo wangu maskini, niuliupeleka ku lufu, pakuishi mu kimwili, katika uoyo wa matendo yangu.

Ee Yesu, kwa nini sikuweza kufwata njia ya mwenyi haki Abeli? Kwa nini sikutolea sadaka takatifu ya matendo mema, sadaka kwa Mungu, kwa usafi wa uzima wangu?

Kwa Muumbaji wa ulimwengu, sawa Kaina tulitolea matendo yetu yasipo samani, sadaka zetu mbaya, uzima wetu wasipo mafaa, na tutahukumiwa.

Ku udongo, ee Muumbaji, uliniumba na uliweka ndani yangu mwili na mifupa, na pumzi ya uzima; Bwana uliyeniumba, ee Mwamzi wangu na Mwokozi wangu, unirudishe kwako.

Naungama mbele yako, ee Mwokozi, zambi nilizotenda*:* Unaona vidonda vya roho yangu na mwili wangu, kwa sababu niliangukia mu mapigo ya Adui na mu urizi wa mawazo.

Ee Mwokozi, japo makosa yangu najuwa vema ya kama wewe ni Rafiki ya wanadamu, unapiga nani unapenda, huruma yako ni ya furaha, unaona machozi yangu, na sawa baba unakuja wepesi mbele ya mwana mpotevu.

Naongojea mbele ya mlango wako, ee Mwokozi, usinikatae, katika nzee wangu usinitume motoni, lakini mbele ya mwisho unipe, Bwana maondoleo ya zambi zangu.

Mimi ni msafiri niliyenyanganywa mawazo yangu kwa wivi; mwenyi kuponywa wote, niko paka vidonda, ee Kristu, kuja uniokoe pakuponyesha vidonda vyangu.

Kuhani mumoja ameniona, lakini anaenda njiani yake, mulawi mumoja ameona kilio changu, na amezarau utupu wangu; lakini wewe, ee Yesu, uliyekuja kwa shukrani ya maria unanisaidia.

Mwana Kondoo wa Mungu, unayeondowa zambi za dunia, punguza uzito wa mzigo wangu, uniopoe ku kifungo cha makosa yangu, unipe, mu mapendo yako, maondoleo ya zambi zangu.

Mu wakati huu wa kutubu, ee Muumbaji nakuja kwako, uniokoe ku uzito wa makosa yangu, unipe mu wema wako mkuu, maondoleo ya zambi zangu.

Japo, usinitupe mbali ya uso wako, ee Mwokozi wangu, lakini chukua mzito wa makosa yangu, mu huruma yako unipe maondoleo ya zambi zangu.

Ee Mwokozi, usamehe na uzima zambi zangu zote nilizotenda, kwa mazoezo ao kwa kutaka, mchana ao kwa siri, za kujulikana ao zasipo julikana; ee Mungu, unisamehe na uniokoe.

Tangu ujana wangu, ee Mwokozi wangu, nilizarau amri zako; niliishi bila sikitiko uzima wangu wote katika uzaifu wa tamaa; na ndiyo sababu nakulalamikia*:* Uniokoe, ee Mwokozi wangu, mbele ya mwisho wa uzima wangu.

Kwa mazimu nilitumia juu ya furaha yangu mali za roho yangu; pakukosa vyote, pakua na njaa ya fazila, nalalamika kwako, ee Baba Mwema sana*:* Unuhurumie.

Nasujudu mbele yako, ee Yesu, nilitenda zambi juu yako; unihurumie na utupe mbali yangu utumwa wa zambi zangu, na unipe mu wema wako machozi ya toba.

Mu uhaki usinistaki, ukiniita ku mapashwa, ukitezamia matendo yangu na ukiselehisha zulumu zangu, lakini, mu huruma yako, funga macho pa zambi zangu na uniokoe, Mungu Mwenyezi.

Mama Maria Mtakatifu, utuokoe.

Pakutoza ku wema wa umungu wa juu unipe neema ya nuru yako sababu ya kuanbgaza giza za tamaa zangu na sababu ya kuimba kwa furaha, ee Maria, uzima wako takatifu mu ubora wa fazila.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Kwa wewe kutii ku kanuni zake za umungu, ulimufwata Kristu, kapuwa na hekima kabisa na uwazo juu ya kishindo cha tamaa zako, na zaidi pakutumia fazila za juu kabisa.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Kwa maombezi yako, ee Mtakatifu Andrea, utulinde ku tamaa zetu; tunakuomba utustahilishe tuwe na sehemu mu ufalme wa Kristu, kisha kukuimba, tukijaa na mapendo na imani.

Utukufu kwa Baba. . .

Utatu wa mbinguni, nasujudu mbele ya ufalme wako moja; ku mabega yangu nainua mzigo

ambao utumwa wa zambi zangu unaufanya kuwa uzito juu yangu, pakunipa mu wema wako machozi ya sikitiko.

Sasa na siku zote. . .

Ee Mzazi-Mungu, matumaini na ulinzi wa hawa wanaokuimba, punguza uzito, mzigo wa zambi zangu; Bibi Mtakatifu kamili, unipokeye mwenyi kugeuzwa toba.

WIMBO YA PILI.

IRMOS: Mbingu, sikiliza sauti yangu, na nitasema juu ya kumwimba Kristu: Kisha kuchukua mwili kwa Bikira, alikuja kati ya sisi.

Mbingu, sikiliza sauti yangu, dunia, teka sikio ku makelele yangu*:* Mungu ananirudisha kwake, na nataka kumutukuza.

Bwana, Mungu wa mapendo, geuza macho yako ya huruma ku upande wangu na pokea ku midomo yangu ungamo ya zambi zangu.

Kupita mtu wowote nilitenda zambi juu yako peke, ee Bwana; lakini hurumia, Mungu Mwokozi, ku kazi ya mikono yako.

Inauguruma pempeni yangu, zaruha ya zambi, sawa kwa Petro pa mawimbi, Bwana unipe mukono.

Ee Kristu, namwanga mbele yako machozi ya Mwanamuke mwenye zambi*:* Mu mapendo yako, ee Mwokozi, unihurumie.

Furaha zinafanya giza neema ya roho yangu; na juu yao roho inarudia ku udongo.

Nilivaa shaba ya kuangara ambayo nyoka alinifunika; nilifwata shauri yake na tazama niko mwenyi haya.

Pakuona uzuri wa muti roho ilipotea, toka sasa niko mutupu na ninapata haya.

Wafitini wa uovu walichimba pa mgongo yangu, wakirefusha mpaka kwangu nfuo wa zambi yao.

Kwa kosa yangu nilipoteza uzuri wangu wa kiumbe na ukuu wa kwanza, niko mwekunda pakua mutupu.

Zambi ilinivika nguo za manyonya na ya ngozi, ilinivua vazi alinipa Mungu zamani.

Nilijifunika kwa haya sawa majani ya mtini, nikionyesha kwa hivi tamaa zinazo uwezo juu yangu.

Mchafu ni vazi lililochafua kwa haya na damu kwa wimbo wa uzima wangu uliyopotea mu furaha.

Mu matope nilikokota gwanda la mwili wangu, nikifanya, ee Mwokozi wangu, madoadoa sura yako na mfano wako.

Tamaa zilikuwa na uwezo juu yangu pamoja na uovu, na ndiyo sababu sasa Adui ananizulumu.

Ku umaskini nilipenda mali na furaha za uzima, nasasa, ee Mwokozi wangu, nainama chini ya zambi.

Nilipamba sanamu ya mwili wangu na kanzu ya rangi mbalimbali ya mawazo yangu machafu, na sasa ninahukumiwa.

Mwekevu paka ku uzuri wa inje, sikutunza ndani ya hekalu iliyofanya kwa Mungu.

Kwa mimi mwenyewe pakuficha uchafu wa tamaa zangu mu shindo ya furaha, nilififisha uzuri wa roho yangu.

Ee Mwokozi, kwa tamaa zangu, nilipoteza uzuri wa sura yako, lakini uliutafuta na uliupata sawa kichele cha zamani.

Sawa Mwanamuke mwenye zambi nakulalamikia*:* Nilitenda zambi, juu yako peke nilitenda zambi; sawa manemane ya zamani, pokea machozi yangu, Mungu Mwokozi.

Sawa Daudi nilianguka mu shimo ambamo nilitopea; lakini sawa Yeye, ee Mwokozi wangu, katika machozi unitakase.

Sawa na Mtoza ushuru, nakulalamikia*:* Unihurumie, Mwokozi, kwani hata moja wa wana wa Adamu hakutenda zambi kama mimi.

Sina na sikitiko ya zambi wala machozi ya toba; yote hii, unipeyo, ee Mwokzoi wangu na Mungu wangu.

Usinifungie mlango wako kwa wakati huu, Bwana, lakini itika kunifungulia ule wa toba.

Bwana rafiki ya wanadamu, unayetaka wokovu wa wote, unirudishe mu uzuri wako na pokea toba yangu.

Tega sikio ku vilio vyangu, ku munungunikо wa moyo wangu, pokea machozi ya macho yangu na uniokoe, ee Mungu Mwokozi.

Bikira Mzazi-Mungu, ee safi kabisa na peke yako mstahilivu wa nyimbo zetu, omba kwa imara ili tuokolewe.

IRMOS: Tazameni na oneni, ni mimi ndimi Mungu wenu, nilituma chakula zamani mu jangwa juu ya watu wangu, nilitosha maji ku jiwa kwa mkono wangu moja na ku nguvu ya mkono wangu.

Tazameni na oneni, ni mimi ndimi Mungu wenu, sikiliza Bwana, ee roho yangu, ujitenge ku upotevu wa zamani, mu woga wa Mungu wako atakaekaa juu ya kukuhukumu.

Utafananishwa na nani, roho yangu maskini? Kwa kaina, muuaji wa kwanza, ao kwa Lameki? Kwa sababu uliua kwa mawe mwili wako na uliua roho yako kwa vitendo vyako vibaya na ku ukali wako ku zambi.

Ee roho yangu, kama ulifanya sawa wale wote wa Amri ya mbele, haukufafanisha kweli wale waliobadilisha maisha, sawa na Seth, Enosi, Enoki na Nowa, apana, haukufwata uhaki wa uzima wao.

Ulifugua paka mchilizi wa hasira ya Mungu, sawa ku wakati wa garidi ulizamisha mwili wote na matendo yote ya uzima wako, na haukuingia mu safina ya wokovu.

Niliua mtu moja sababu ya kidonda kimoja, mtoto moja juu ya kidonda kimoja, ni vile alisema Lameki akilia, na wewe roho yangu haukutetemeke basi sababu ya kuchafua mwili wako

na kuchafua roho yako.

Namna gani nilitamania Lameki muuaji pakuua moyo wangu sawa mutu na roho yangu sawa mtoto? Sawa Kaina muuaji, niliua ndugu yangu mwili mu shindo la tamaa zangu.

Ee roho yangu, kwa tamaa zako uliwaza kujenga mnara na kuweka mji wa ukuta, lakini muumbaji aliharibu nia zako, aliangusha majengo yako.

Ninaumizwa, ninajeruhiwa, tazama mikuki ya Adui inatoboa roho yangu na mwili wangu, vidonda vyangu na joto ya vidonda vyangu zinaonyesha nguvu ya tamaa zangu.

Bwana wa juu ya mbinguni zamani alikunyesha garika ya moto juu ya Sodoma yenyi kuwaka na tamaa zisiyo na haki; na wewe, ee roho yangu, unachochea gehena ya moto ambamo utashuka juu ya kuungua.

Muone na musikie, ni mimi ndimi Mungu wenu, yule anayetezamia mioyo na anayeinua mawazo, anayeonyesha matendo na kuunguza zambi, na anayehukumu yatima, mzaifu na mdogo.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Pakuingia ndani ya shimo la vishawishi, ulipanua mikono, ee Maria, mpaka ku mapendo ya Mungu; na sawa kwa Petro Rafiki wa wanadamu alinyosha mkono wa msaada, kwa sababu ni maongozi yako alitafuta yulu ya yote.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Kwa pupa ya moyo wako ulimufwata Kristu, pakutoka mu njia ya zamani ya zambi sababu ya kusihi mu upekee mu jangwa, ukishika kwa moyo safi kanuni zake za umungu.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Tuone na tutazame mapendo ya Rabi Mungu juu ya wanadamu, mbele ya mwisho, tusujudu mbele yake, na mu machozi tulalamike*:* Kwa maombezi ya Mtakatifu Andrea, Bwana, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Utatu wa , milele, Umoja usiyogawanywa, pokea kitubio yangu na uniokoe, mtenda zambi, usizarau tendo la mikono yako, unilinde, uniokoe ku ndimi za moto za hukumu.

Sasa na siku zote. . .

Bibi Mtakatifu, Mzazi-Mungu, tumaini la wale wanakukimbilia, bandari linalotuokoa ku hasira ya mawimbi, umuombe Muumba wako na Mwana wako atufanyie neema kwa maombezi yako.

WIMBO WA TATU.

IRMOS*: Pa jiwe ya imara ya amri zako, ee Kristu, ulisabitisha Eklezia yako.*

Pa inchi ya Sodoma Bwana ywa juu mbinguni zamani alikunyesha garika ya moto.

Pa mlima, sawa Loti, ee roho yangu, ujiokoe, ukimbilie mpaka ku Segori.

Ee roho yangu, kimbia makaa ya moto, kimbia moto mkubwa wa Sodoma, kimbia msiba wa moto ya Mungu.

Namuungamia, ee Mwokozi wangu, bila kipimo nilitenda zambi juu yako; lakini mu wema wako zima zambi yangu.

Nilitenda zambi juu yako peke, nilikosa kupita wote, Kristu Mwokozi, unihurumie.

Uko kweli Mchungaji Mwema, kuja kunitafuta, Bwana, usizararu kondoo wako mpotevu.

Ee Yesu, uko uwema wa uzima wangu, ni wewe ulinifanya, katika wewe, Mwokozi, nitahakikishwa.

Utatu Mtakatifu, ee Mungu, utuhurumie.

Ee Utatu Mtakatifu na umoja, utuokoe ku mwendo, ku vishawishi na ku hatari yoyote.

Mtakatifu Mzazi-Mungu, utuombee.

Salamu, ee Kifua kibebaji-Mungu, salamu, ee Kiti cha Bwana; salamu, ee Mama wa uzima wetu.

IRMOS: Bwana, kaza moyo wangu pa jiwe la amri zako kusudi usipepe, kwa sbaabu uko Mtakatifu moja na Bwana moja.

Ndani yako ni chemchem ya uzima wangu, Mshindi wa lufu, na kwa moyo wote nakulalamikia mbele ya mwisho*:* Nilitenda zambi, unihurumie na uniokoe.

Wale waliyoishi wakati wa Nowa, nilitaka kuwafafanisha, nikistahili malipizi paka ile mu garika iliyowameza.

Nilitenda zambi, Bwana, juu yako, nilitenda zambi, unihurumie; kati ya wanadamu hakuna mtenda zambi niliyempita kwa zambi zangu.

Ee roho yangu, ulifafanisha watoto wa Cham wasiyo heshima, kwa sababu haukufunika haya ya jirani pa wewe kwenda bila kutafuta kuiona.

Baraka ya Sem, roho maskini, haukuitimize haukurizi shamba kubwa la Jafeti ku inchi ya maondoleo.

Pakutoka mu inchi ya Harani, roho maskini, acha inchi ya zambi wende ku inchi ambako kunatiririka hali ya milele, ile Abrahamu alipokea mu urizi.

Ee roho yangu, ulisikia*:* Abrahamu alipotoka inchi ya mababu zake, alikuwa mugeni pa dunia, fananisha mfano wake na makusudi yake.

Chini ya muti wa mambre Babu aliyewapokea Malaika kwake, japo uzee wake alipata kitu cha agano la Mungu.

Ee roho yangu, kama ulijua katika Isaka sadaka mupya, sadaka ya roho iliyotolewa kwa Bwana, ujikaze kwa kufananisha ma kusudi yake.

Ee roho yangu, uliisikia*:* Ismaeli, mtoto wa utumwa, alifukuzwa usitumikie tamaa, kusudi usiteswe na fukuzo ya namna hii.

Ulifafanisha mama yake ya Ismaeli, Agari wa Msiri ya kwanza, pa kujifanya mtumwa wa tamaa na pakujisifu kwa yote uliyofanya.

Ee roho yangu, unajua mungazi wa Yakobo toka dunia mpaka mbinguni; sababu gani haupende, wewe vilevile daraja za ibada hii?

Kuhani wa Mungu na mfalme wasipo ukoo mwenyi umbo sawa sura ya Kristu, ujikaze kwa kufananisha uvuko mu dunia hii kati ya wanadamu.

Usikue nguzo la chumvi pakugeuka juu ya kuangalia nyumba; ogopa juu yako wewe

mwenywe mfano wa Sodoma, na ujiokoe ukipanda mpaka ku Segor.

Ee roho yangu, kimbia sawa Loti mbele ya moto ya zambi, mbali ya Sodoma na Gomora kimbia moto mkubwa wa tabia zako za tamaa mbaya.

Unihurumie, Bwana, unihurumie, hii itakuwa lalamiko langu wakati utakuja kati ya Malaika zako Watakatifu kumupa kila mumoja kadiri ya matendo yake.

Ee Rabi, usitupe ombi la wale wanaokuimbia, lakini uwafanyie neema mu wema wako, ukiwapa waaminifu maondoleo ya zambi zao.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Ninashambulia kwa zaruba ya zambi zangu; ee Mama, kuja unisaidie na unipeleke mpaka ku bandari, mu njia inayonirudisha kwa Mungu.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Sala yako ya maombezi, Mama mtukudu uiongoze sasa mpaka ku mapendo ya Bikira Mtakatifu, ukinifungulia kwa hivi mlango unaopeleka mpaka kwa Mungu.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Mtakatifu Andrea, askofu wa Kreti kwa maombezi yako unipe maondoleo ya zambi zangu; kwa kitubio, lakini wewe ni mwongozi mkuu.

Utukufu kwa Baba. . .

Utatu unayostahili nyimbo zetu, Mungu moja mu watu tatu, utuokoe sisi tunaosujudu kwa uaminifu mbele ya ufalme wako.

Sasa ma siku zote. . .

Bila mbegu ulipata mimba ya Mwana wa Baba asiye wa wakati, ilimuzaa na mu wakati*:* Ni ajabu, Bikira na Mzazi-Mungu.

IRMOS: Bwana, kaza moyo wangu pa jiwe la ammri zako kusudi usipepe, kwa sababu uko Mtakatifu moja na bwana Moja.

KATHISMA.

Sauti ya mnane. To prostakthen.

Tazama nuru za Mungu, Mitume muliyemuona Mwokozi, mumwange mwangaza wenu pa giza za uzima wetu, ili tutembee kwa ustahilivu, sawa mchana, tena kimbiza tamaa za giza chini ya mwangaza wa usafi, sababu ya kuangalia mu furaha Mateso ya nuru ya kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Shirika la Mitume kumi na wawili iliyochaguliwa, onyesha maombezi yako kwa Kristu ili sisi wote tufunge vizuri, tukitimiza kanuni mu sikitiko, tuwe na furaha ya kutimiza fazila ili tustahili kwa kumuona Kristu Mungu wetu siku ya Ufufuo wake utukufu na utakatifu.

Sasa na siku zote. . .

Pamoja na Mitume, ee Mzazi-Mungu umuomba yule uliyezaa kwa namna ya ajabu, Mwana na neno la Mungu ambaye ulimwengu haiwezi kuwa naye, ili alete ku dunia amani ya kweli atupatia mbele ya mwisho maondoleo ya zambi zetu na apokee mu wema wake wa juu watumishi wako mu ufalme wa mbinguni.

WIMBO YA INE.

Sauti ya mnane.

IRMOS*: Bwana, nilisikia sauti yako na nilijazwa na woga, nilisikia tendo lako nla wokovu na ninatukuza uwezo wako, Bwana.*

Mitume Watakatifu wa Kristu, mutuombee.

Mitume Watakatifu wa bwana, muombe wote mu kundi kwa Muumbaji wa ulimwengu

ahurumie wale wanaotukuza jina lenu.

Mitume Watakatifu. . .

Mitume wa Kristu, muliyolima dunia nzima sababu ya kupandamo neno la Mungu, mumuonyeshe matunda ya kazi yenu yasipo wakati.

Mitume Watakatifu. . .

Mitume ya Bwana, mulikua juu ya Kristu mpendelevu mzabibu wenyi kuzaa vinyo ya roho inayochirizika juu ya dunia nzima.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Utatu Mtakatifu na mwenye asili moja milele, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Mungu Mwenyezi, Nuru na Uzima, linda kondoo za zizi lako.

Sauti ya sita.

IRMOS: Nabii, Bwana pakusikia kuja kwako alishangaa, kwa sababu ulipenda kuzaliwa kwa Bikira na kujionyesha kati ya watu, na alisema: Nilisikia sauti na nilijazwa na woga; utukufu ku uwezo wako, ee Bwana.

Usiache kazi ya mikono yako, usizarau chako, ee Mwamzi wa haki, hata kama peke yangu nilitenda zambi, kuliko mtu wowote, Mungu wa huruma; ni kwako sawa kwa Bwana wa ulimwengu, kwa kuondolea zambi.

Mwisho unakaribia, ee roho yangu, unakaribia na unachilia kwa wewe kujitayarisha, wakati unajiharikisha, simama, kwa sababu Mwamzi eko ku kizingiti, sawa ndoto ao ua, uzima wetu unazimia na tunajihangaisha bure.

Amuka, ee roho yangu, na waza ku vitendo vya uzima wako, pitisha machozi yako ukifikiri pa wakati wako uliyopita, ungama kwa Kristu matendo yako, mawazo yako ya siri, na utahakikishwa.

Ee Mwokozi, mu uzima huu hamuna zambi yoyote, hamuna tendo mbaya lolote sikutenda kwa maneno, kwa makusudi, ya mazungumuzo fulani mu mawazo ao mu vitendo, na ingine mu wakati wowote.

Ni kule kunatoka hukumu yangu, ni kule tena hukumu ya zamiri yangu, hakuna kilicho sawa hapa chini, wewe unayenipima na unayenijua Mkombozi, unisamehe na okoa tena mtumishi wako.

Mungazi ambao zamani Babu aliangalia, ni mpando wa utawa, ni kupanda kwa siri; ee roho yangu, kama unapenda kuvijua vyote viwili, badilisha uzima wako.

Kwa kupata bibi arusi zake wawili babu alivumilia kivugutu cha mchana, baridi ya usiku, mu kazi na mu vita, akiongeza siku pa siku, kwa uerevu, kundi lake la kondoo.

Bibi arusi wawili, itakuwa na kitendo na mawazo; Lia, ni kitendo kwa sababu eko na watoto wengi, Rakila, ni maarifa yenyi kupatikana kwa tabu, na vyote viwili ni matunda ya kazi.

Ee roho yangu, amka na shindana sawa Yakobo, kusudi ya kupata na kitendo maarifa na ndoto ya Mungu, mawazo ya furaha, ushangao huu wa bei munene.

Yakobo, pakuzaa Mababu kumi na wawili, alisimamisha kwa siri mungazi wa kupanda, pakuwa na wana wake kumi na wawili sawa daraja juu ya mumoja wa hekima sana wa mipando.

Pakufafanisha Esau mubaya, ee roho yangu, ulizisha kwa Mdanganyi uliuzisha haki ya ukubwa ya uzuri wako wa kwanza na tazama sasa hauna baraka ya baba*:* Fanya kitubio sasa.

Esau aliitwa Edomi sababu ya tamaa zake za nguvu; paluwasha na ulaji na kuchafua na furaha akaitwa Edomi, ni kusema moto mkubwa wa roho yenyi kusukuma na zambi.

Kwa Yobu ulisikia, ee roho yangu, utii ambao, pakukaa pa majivu, alitukuzwa, alkini haukufafanishe juhudi yake na usabiti wake; imara ilikukosa.

Ye ule mutupu pa samadi, yeye ambaye zamani alikaa pa kiti cha Ufalme; baba mtukufu wa zamani hana na makao wala watoto, majivu inakawa nyumba, na vidonda vinapata fasi ya johasi ya samani kwake.

Tamani tena alivaa alama ya ufalme, akivaa nguo nyekundu na taji, Mwenyi haki alikuwa na mali nyingi na kundi nyingi za kondoo, lakini Ye ule anaondolewa mara moja sifa yote.

Wakati mwenyi haki mumoja sawa Yovu, mutu safi kuwapita wote hakuweza kujitayarisha ku mateso ya Muovu, roho maskini ya zambi, utafanya namuna gani wakati bahati mbaya itakuangukia?

Mwili wangu na roho yangu zinachafua na zinaoza, Mganga wa roho, ee Kristu, ponyesha vidonda vyangu, kwa kitubio unisafisha, unitakase na unipe weupe wa zeluji.

Pa msalaba, juu ya wokovu wa wote, ee Neno, ulitoa mwili wako na damu yako; mwili wako sababu ya kuumba mara ingine wangu, damu yako sababu ya mimi kunawa; kwa Baba yako ulipatia, ee Kristu, rogho yako juu ya kunifikisha mpaka kwake.

Bwana, ulifanya wokovu katikati ya dunia, sababu ya kutuokoa; na ulipanda pa msalaba juu ya kutufungulia paradizo, kiumba chote nzima na mataifa yaliyokombolewa zinasujudu mbele yako.

Damu na maji yanayochirizika ku ubavu wako ziwe kwangu ubatizo na kinywaji ya ukombozi, ili, nikitakaswa mara mbili, nishote ku kikombe na ku mpako neno lako lenyi uzima.

Ninafukuzwa ku nyumba ya arusi, mbali ya arusi ya Mwana Kondoo; taa yangu haina mafuta na milnago yakufunga, karamu inamalizika na ninatupwa inje, miguu na makonde yakufunga.

Mwokozi, kanisa ilirizi ku ubavu wako wenyi kuleta uzima sawa ku kikombe mu mchilizi moja wingi mbili wa maarifa na wa rehema kwa sura ya yule anayeunganisha Maangano, ya Kale na mupya.

Uzima wangu ni wa muda mufupi, wenyikujaa na maovu na mateso, pokea kutubu kwangu, uniite mu nuru yako sababu ya kuepuka kuwa mateka ya Adui; Bwana, unihurumie.

Nuilijifanya sananu yangu mwenyewe, nilichafua roho yangu kwa tamaa lakini pokea kutubu kwangu, uniite mu nuru yako sababu ya kuepuka kuwa mateka ya Adui, Bwana, unihurumie.

Pahali pakufwata sauti yako nilivunja amri ya Sheria yako, pokea kutubu kwangu, uniite mu nuru yako sababu ya kuepuka kuwa mateka ya Adui; Bwana, unihurumie.

Mama Maria Mtakatifu, uniombee.

Ulipoangukia chini ya shimo ya zambi, haukubakiamo mateka, lakini ulipopata mwanzo

wako mzuri, kwa matendo yako ulijipandisha mpaka yulu ya fazila.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Utukufu wa Baba zetu, ee Mtakatifu Andrea, ku Kreti mapambo, usikose, kuusihi Utatu Mtakatifu kwa ajili yetu kusudi ya kuokoa hii malipizi ya milele wale wanaomba msaada wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Nakuungamia sawa Mungu, Utatu moja, pa kiti cha Ufalme kinachogawanywa kwa watu tatu, wasiyogawanywa kwa hali, wasiyofujo lakini, na wimbo tatu wa malaika unatumwa kwa sauti yangu.

Sasa na siku zote. . .

Ee Bikira, ulizaa na ulikaa Bikira, kwa sababu uzuzi wako wa ubikira ulizaa yule anayebadirisha amri*:* Mungu mwenyewe anapenda hivi.

WIMBO YA TANO.

IRMOS: Usiku ninakesha mbele yako, Bwana rafiki wa wanadamu, nakuomba, uniangaze, uniongoze mu njia ya amri zako, na unifundishe, Mungu Mwokozi, kwa kufanya mapenzi yako.

Uzima wangu ulipita usiku, ilikuwa giza, fujo ya ndani sana, usiku wa zambi; Mwokozi uniangaze ili niwe mtoto wa nuru.

Kwa yote nafanana na Rubeni, mimi mwenyi mateso, nilitenda zambi bila heshima kwa Mungu wa Juu, pakutukana mapendo yake ya ubaba.

Namuungamia mbele yako, Kristu, ee Mfalme wangu, nilitenda zambi nilitenda zambi sawa ndugu za Yosefu ambao zamani waliuzisha tunda la hekima na usafi.

Kwa ndugu zake uzima wa mwenyi haki Yosefu uliuzishwa, na kijana mwanaume mpendelevu akawa mtumwa, kwa sura ya Bwana; na wewe, roho yangu, ulijiuzisha ku zambi.

Fwata alama ya Yosefu, roho maskini ya kukataliwa, fafanisha uhaki na usafi wa moyo wake, pahali pa kujitia ku mshituko wa tamaa zinazokuweka mbali na Mungu.

Kama zamani Yosefu alishuka mu shimo, ee Rabi mfalme, ilikuwa ni alama ya kuwekwa kwako kaburini na ya Ufufuo wako Takatifu.

Ee roho yangu, unajua habari ya Musa aliyeelea mu mlezi yake pa maji ya mtoni sawa mu safina ya wokovu, alipokimbia uzulumu wa mchungu wa nia ya Farao.

Kwa hekima, wazalisha walipashwa kuuwa tunda lolote la kiuma; ee roho yangu, unajua vizuri, na sawa Musa zamani alinyonya maziwa ya hekima.

Ee roho yangu, haukupiga Mumsiri rohoni*:* Sawa Musa alipokwisha kukomea, utaweza kukaa, kwa kutubu kwako, mu jangwa ya tamaa?

Musa alikaa mu jangwa*:* Ee roho yangu, fwata alama ya uzima wake sababu ya kutazama vilevile mu kijiti kuonekana kwa umungu.

Ee roho yangu, kwa mufano wa bakora ya Musa iliyopiga bahari na kugandisha shimo la mawimbi mu alama ya Msalaba Takatifu ambapo wewe vilevile, utafanya ajabu.

Aruni alitolea kwa Mungu moto safi na wasipo mchunganyiko, wakati Ofni na Fineo walimutolea sawa wewe, ee roho yangu, uchafu wa uzima wao.

Moyo wangu unakuwa gumu sawa ule wa Farao; Ninafanana sasa na Jannesi na Jamhesi kwa roho na kwa mwili, na uzito wa akili yangu; Bwana, kuja unisaidie.

Helas! Tazama mu matopa*:* ee Rabi wangu, unioshe mu bikira ya machozi yangu, na angazisha vazi la mwili wangu sawa zeluji.

Kwa kidogo niangalie, Bwana, aina ya matendo yangu, kwa zaidi sawa wengine najiona najipakiza na maovu, kwa sababu nilitenda zambi kwa kujua haika kwasipo kujua.

Bwana, epusha kazi ya mikono yakop, nilitenda zambi, unihurumie, kwa sababu juu yako peke ulimwengu utakuwa utakatifu, ni wewe peke wasipo zambi.

Sababu ya kuniokoa ulifungua umungu wako na nguo ya ubinadamu wangu, na ulifanya maajabu pakuponyesha wenye ukoma, pakusimamisha wenye kupooza na kukausha wingi wa damu kwa tamvua ya nguo yako.

Fwata mfano wa mwenye kutoka damu, ee roho yangu, jongea sababu ya kugusa nguo ya Kristu atakayekuokoa na utamusikia akisema*:* Kama! Imani yako inakuokoa.

Ukifafanisha mwanamuke wakukujama, ee roho yangu, jongea na usujudu ku miguu ya Yesu ili akusimamisha ku maji ya uzima wako.

Machozi yangu, Bwana Mungu, iwe kwangu chemchem ya Siloe ili niweze kunawishamo macho ya moyo wangu sababu ya kuangalia mwangaza wako wa milele.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Wakati uliyosumwa kwa mapendo yasipo sawa, ulitamani kusujudu mbele ya Muti wa uzima, naziri yako ilikibaliwa; unifanye mstahiulivu wa utukufu wa juu.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Ulipovuka mawimbi ya Yordani, ulipata mapumziko pakutikisa kifungo cha furaha za mwili; utuokoe vilevile, ee Maria, kwa maombezi yako Matakatifu.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Mtakatifu Andrea, mchungaji wa hekima, Mteule wa Mungu, nakuomba kwa moyo wote na katika woga nakuomba ya kunikamatia kwa maombezi yako wokovu nzima wa milele.

Utukufu kwa Baba. . .

Tunakutukuza sawa Mungu Moja, mara tatu Utatu Mtakatifu; Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, umungu mwenye asili moja, tena na tena tunakuabudu.

Sasa na siku zote. . .

Kwako, ee Bikira Mtakatifu, Mtakatifu Mzazi-Mungu, Mungu Muumba wa milele, aliyepata mwili sababu ya kujiunga ku hali ya mauti.

WIMBO YA SITA.

IRMOS: Nililalamika kwa moyo wote mpaka kwa Mungu wa mapendo, anasikiliza mwito wangu tangu chini sana ya gehena na ku shimo anakuomba uzima wangu.

Nakutolea mu usafi wote, ee Mungu Mwokozi, machozi ya macho yangu, vilio vyangu vya ndani na lalamiko la moyo wangu*:* Nilitenda zambi, unihurumie.

Ulijitenga mbali na Bwana wako, ee roho yangu, saswa Dathani na Abironi, lakini umulalamikia kwa moyo wako wote*:* Bwana unisamehe na dunia isifunguke juu ya kunimeza.

Unafanana na Efraimu, ngombe kijana mwenyi kusukumwa; sawa kasha inje vifungo vyake, ee roho yangu, uniokoe pa mabawa ya matendo mema na ya mawazo.

Mkono wa Musa, ee roho yangu, ukuhakukushe namna gani Mungu anaweza kusafisha na kutakasa ukomo wa uzima wetu.

Sawa mawimbi ya bahari mwekunda, bahari kuu ya zambi zangu ilinifunika kwa mara moja sawa wamsiri zamani.

Sawa Israeli ya zamani, ee roho yangu, ulifanya uchaguzi wasiyo na akili*:* Pahali pa chakula cha mbinguni ulipenda zaidi chakula cha tamaa.

Ee roho yangu, ulitamania visima vya Kanana ku chemchem ya Jiwe ambako kunachirizika hekima na maarifa ya Mungu kwa ajili yako.

Wakati Musa, mtumishi wako, kwa bakora yake alipiga jiwe, alitangulia kuonyesha ubavu wako wenyi kuleta uzima ambako sisi wote tunashota uzima na wokovu.

Vumbua, ee roho yangu, inchi iliohaidia, angalia urizi wako sawa Yoswa, na ikaa ndani yake, ukifwata Amri.

Simama sababu ya shinda tamaa za mwili, sawa zamani Yoswa aligombana juu ya Amaleki tena usidanganywe kwa mawazo sawa ilikuwa kwa watu wa Gabaoni.

Vuka mtoni wa uzima sawa Safina ya maangano zamani, ee roho yangu, tena shika ahadi ya Mungu.

Sawa uliokoa zamani Petro pa maji, Mwokozi ujiharikishe kwa kuniokoa; nyolosha kwangu mukono wako sababu ya kuniokoa ku shimo la zambi.

Kwako ninaona bandari ya wokovu, ee Rabi na Bwana yesu, uniokoe ku shimo la chini la sikitiko na la zambi.

Niko drakhme yenyi sura ya Mfalme, ambayo ulipoteza zamani, Bwana*:* Wakisha taa kwa kunitafutia mwanga wako wa kwanza tena pata mara ingine sura yako.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Kwa kuzimisha moto ya tamaa zangu, ee Maria, ulimwanga machozi yako mingi, unipe nisharikia vilevile ku neema hii.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Kwa uzima wako mkuu wa hapa chini, ee Maria, ulipata mapumziko ya mbinguni; kwa wale wanaoimba sifa yako pokea kwa Bwana waokolewa ku tamaa zao.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Ku Kreti ulikuwa Mwongozi na Mchungaji, na mu ulimwengu uko muombezi*:* Tena nakuja kwako, Baba Mtakatifu, uniokoe ku shimo ya zambi.

Utukufu kwa Baba. . .

Ndimi Utatu usiyogawanywa na kwa hali na Umoja, ndivyo anasema baba pamoja na mwana na Roho ya Mungu.

Sasa na siku zote. . .

Uzazi wako ulizaa kwa ajili yetu Mungu moja anayejifatanisha na ubinadamu wetu, ee Mzazi-Mungu, umusihi muumba wa ulimwengu ili kwa maombi yako tutukuzwe.

IRMOS: Nililalamika kwa moyo wangu wote mpaka kwa Mungu wa rehema, anasikiliza

mwito wangu tangu chini sana ya Gehena, na ku shimo anakomboa uzima wangu.

KONTAKION.

Sauti ya sita.

Ee roho yangu, roho yangu, amka, sababu gani kulala, gani kulala hivi? Kwani tazama, mwisho umekaribia, na utasamba ku hukumu. Tubu, basi, ee roho yangu, ili Kristu Mungu akusemehe, yeye aliye popote mu ulimwengu wote anayejaza kuwako kwake.

IKOS.

Pakuona maponyesho yaliyofanyiwa kwa Kristu, na wokovu uliyochirizika pa Adamu, Shetani alipata uchungu, na akalalamika mbele ya hatari, akawaambia rafiki zake*:* Nitafanya nini kwa Mwana wa Maria? Kwa sababu ataniua, yule aliyezal;iwa ku Betlehemu yeye aliye popote, mu ulimwengu wote anayejaza kwako kwake.

SINAKSARION.

Kwa siku hii ya leo, kazi Ine ya Juma ya tano ya Kufunga, kufwata desturi ya zamani, tunaimba kanuni Mkubwa ya Kutubu.

Kwa wale ambao sasa wanaimba Kanuni Mkubwa, uwape, ee Bwana, machozi ya sikitiko.

Kwa maombezi ya Mtakatifu Andrea, utuhurumie, ee Mungu, na utuokoe.

HERI.

Sauti ya sita.

Utukumbuke mu ufalme wako, ee Bwana, wakati utaingia mu Ufalme wako.

Mwivi Mwema alikulalamikia pa Msalaba*:* Unikumbuke, Bwana, ulitangulia kumufwanya mwana inchi wa paradizo; vilevile kwa mimi mtumishi wako msiyestahili, unipe nifafanishe kutubu kwake.

Heri walio maskini wa roho, maana Ufalme wa mbinguni ni wao.

Unajua, ee roho yangu, habari ya Manoe aliyemupokea Mungu na tasa la ahadi, fafanisha mapendo yake kwa Bwana.

Heri wenye huzuni, maana wao watafarijiwa.

Ulipofafanisha ukosefu wa Samsoni, ulijipunguza ku matendo yako matukufu, ee roho yangu, pakutoa kwa Adui kwa mapendo ya furaha heri ya uzima takatifu.

Heri wenye upole, maana wao watariti inchi.

Yule ambaye zamani na mataya ya punda alipiga ma adui, anakua sasa mchezo wa tamaa za mwili*:* ee roho yangu, kimbia mfano wa ukosefu wa namna hii.

Heri wenye njaa na kihu kwa haki, maana wao watashibisha.

Barak na Yefte walichanguliwa kwa kuhukumu Israeli na kuongoza jeshi lake, na pamoja nao mshujaa Debora*:* Fafanisha, ee roho yangu, fazila zao za dume.

Heri wenye rehema, maana wao watapata rehema.

Unajua, ee roho yangu, ushujaa wa Jaheli aliyesabitisha wokovu wa Israeli pakutoboa kichwa cha Sisara; Alina Adui na muti unaokukumbusha ule wa msalaba.

Heri wenye moyo safi, maana wao wataona Mungu.

Tolea, ee roho yangu, sadaka ya sifa ukitumia usafi wa uzima wako sawa binti wa Yefte, onyesha mu sadaka kwa Bwana sadaka ya tamaa zako za mwili.

Heri wenye kufanya salama, maana wataitwa wana wa Mungu.

Unajua, ee roho yangu, nywele ya Gideoni*:* Pokea majira ku mbinguni; ujishushe sababu ya kuangaza ku wimbi la Sheria ile inayotoka ku kanuni za Bwana.

Heri walioteswa kwa sababu ya haki, maana ufalme wa mbinguni ni wao.

Ee roho yangu, ulijivutia hukumu ya kuhani Heli, pakuleta njia kwa tamaa zako, pakukosa usabiti, sawa kuhani wa Silo alipofunga macho pa ukafiri wa wana wake.

Heri ninyi, wakati wanapowatukana ninyi na kuwatesa ninyi na kuwasemea ninyi kila neno baya kwa uwongo, kwa sababu yangu.

Chini ya Wamzi Mulawi mumoja, mu alama ya kilio, kati ya makabila kumi na mbili ya israeli akagawanya mwili wa muke wake sababu ya kuletesha uadua na uzulumu wa Benjamino.

Furahini, Shangilieni, kwa sababu zawabu yenu ni kubwa mbinguni.

Anna, mama wa Samueli, alipotikisa midomo yake sababu ya sala bila kusikia sauti yake, na japo utasa wake, akazaa mtoto aliyeomba kwa Bwana.

Utukumbuke, Bwana, wakati utaingia mu ufalme wako.

Samueli Mkubwa akahesabiwa kati ya Waamzi, muzaliwa wa Arimathea, aliyetukuzwa mu nyumba ya bwana; ee roho yangu, kamata mfano pa yeye na hukumu mbele vitendo vyako kisha vya wengine.

Utukumbuke, Bwana, wakati utaingia mu ufalme wako.

Daudi alipochaguliwa sawa mufalme akapokea kwa ufalme mpako wa mafuta matakatifu; na wewe, roho yangu kama unataka ufalme wa mbinguni, ujimwangie mpako wa machozi yako.

Utukumbuke, Bwana, wakati utaingia mu ufalme wako.

Samehe kiumbe cha mikono yako, Mungu wa wema epusha wale waliotenda zambi, na kuliko wote, mutumishi wako aliyezarau amri zako.

Utukufu kwa Baba. . .

Naabudu Baba aliyezaa kwa namna ya milele, matukuza Mwana aliyezaliwa na naimba Roho Mtakatifu anayeangaa na mwangaza sawa Baba na Mwana.

Sasa na siku zote. . .

Tunaabudu Tunda la ajabu la Mzazi wako, bila kubagua utukufu wa Mwana wako, kwa sababu tunaungama ku nafsi yake umoja na ku hali zake uwili.

WIMBO YA SABA.

IRMOS: Tulitenda zambi, uovu, uzulumu mbele yako, hatukuchunga wala kutimiza Amri zako: Usitutupe mpaka ku mwisho, Bwana, Mungu wa Baba zetu.

Nilitenda zambi, nilivunja, nilizarau amri zako, kwa sababu nilizaliwa katika zambi tena nilizidisha vidonda vyangu, lakini unifanyie neema mu wema wako, Bwana Mungu wa Baba zetu.

Niliungama mbele yako, ee Muamzi wangu, siri za moyo wangu; tazama azabu yangu na haya yangu, uwe muekevu kwa kunihukumu, na unifanyie neema mu wema wako, Bwana, Mungu wa Baba zetu.

Saulo alipokwenda kwa kutafuta punda jike za baba yake, alipata kwa ziada mwito wake wa ufalme; na wewe, ee roho yangu, ujilinde kwa kutamania kundi la tamaa zako ku ufalme wa Kristu.

Kama Daudi alitenda zambi mara mbili, yeye, babu wa Bwana pakujachilia kutoboliwa na mukuki wa tamaa na kisha pakutumia upanga mkali wa uuaji, wewe, ee roho yangu unateswa tena zaidi na uzito wa tamaa zako.

Zamani Daudi aliongeza hatari ya zambi yake, pakuunganisha uuaji ku uzima, lakini alifanya kwa mara moja kitubio mara mbili; na wewe, ee roho yangu, mwendo wako ni mbaya zaidi vilevile pasipo kutubu mbele ya Mungu.

Zamani Daudi aliweka mu mwimbo sura ya kutubu kwake, akastaki matendo yake mbele ya watu wote na akasema*:* Mungu wa ulimwengu unihurumie, nilitenda zambi juu yako peke, unitakase mu wema wako, unihurumie, nilitenda zambi juu yako peke, unitakase mu wema wako.

Wakati Sanduku la Maagano ilibebewa pa gari, Oza, alipoona ngombe wakitelemuka, akaweka mukono pa Sanduku Takatifu na paka kwa hii akapatikana na hasira ya Mungu; usifafanishe ujasiri wake, lakini tendea na heshima, ee roho yangu, vitu vitakatifu.

Unajua habari ya Absaloni na wasi wake juu ya ulimwengu, hausahau machukizo yake ilifika kwa kuchafua kitanda cha baba yake, kwa lakini unafafanisha, ee roho yangu, tamaa zake na vishindo vyake mpaka ku furaha.

Ukubwa wako, uhuru wako, uliufanya kuwa mutumwa wa mwili wako; ulipopata katika Adui Akitofeli mwingine, ulifwata shauri zake, lakini Kristu alizivunja sababu ya kukuokoa.

Alipojazwa na neema na maarifa, mwenyi ajabu Solomoni alijitenga na Mungu, pakufanya ubaya ku macho yake*:* Na wewe mwenyewe roho yangu, kwa uzima wako uliyolaaniwa, ulikamata mfano peke yeye.

Alipokokotwa kwa furaha, kuchukizwa kwa tamaa; mchumba wa hekima alibembeleza washarati, akajitenga na Mungu, na ulifwata njia yake, mu haya ya tamaa.

Mshindani wa Roboani akazarau Shauri la baba yake, ulifwata vilevile ukafiri wa zamani wa Yeroboami, mtumishi huyu mubaya; usifafanishe, lakini lalamika kwa Bwana*:* Unihurumie, mimi mtenda zambi.

Kwa uchafu wako ulifwata njia ya Achabi, akawa makutanio ya machukizo ya mwili tena chombo yasipo heshima cha tamaa za haya lakini lilia chini ya moyo ukiungama kosa lako kwa Bwana.

Elia walimushinda mara mbili, watu makumi tano wa Okozias, kisha kuharibu manabii wa Yezabeli sababu ya kunyamazisha Achabi, usiwafafanishe, lakini lalamika kwa Bwana*:* Unihurumie, mimi mtenda zambi.

Mbingu zinafungana juu yako na njaa iliyotumwa na Mungu inakukamata, sawa Achabi, asiyeongeza imani ku mashauri ya Elia wa Tisbe. Tafazali kufafanisha mujane wa Sarepta pakupokelea wajumbe wa Mungu.

Kwa mapenzi yako ulizidisha, ee roho yangu, mihalifu ya Manasse; pakuweka pa altare machukizo ya tamaa zako, pakuongeza matendo yaliyo muchukiza Bwana; fafanisha basi kugeuka kwake ukipata sikitiko.

Nasujudu mbele yako tena nakuletea ungamo langu sawa machozi*:* Nilikosa kupita kahaba, nilitenda zambi kupita mtu wowote pa dunia; lakini kwa kiumbe chako, Bwana, unirehemu, unirudishe ku zizi lako.

Nilififisha nuru ya sura yako, nilivunja Amri yako, uzuri wangu ulififia ku pmuzi ya tamaa, taa langu haliungue, lakini unipe, Mwokozi, pamoja na neema yako, furaha sawa anavyoimba Daudi.

Fanya kitubio, rudia kwa mpaka kwa bwana, umujulishe mawazo yako ya siri, umwambie Mungu anayesoma ndani ya mioyo*:* Wewe peke Bwana, unajua siri zangu, lakini sawa anavyoimba Daudi, unihurumie Bwana, mu wema wako.

Siku zangu zinazimia sawa pakuamuka pa ndoto; tena ninalia, kama alivyofanya Azekias, ili miaka ya maisha yangu yaongezeke; lakini Isaya mwengine nani, ee roho yangu, atakusaidia, ijapokuwa Mungu wa Juu Mbinguni?

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Ulipoomba msaada wa Mtakatifu Mzazi-Mungu, ulipoteza nguvu ya tamaa tena ulijiweka mu boma juu ya hila ya Adui. Kwa mimi niliye mutumishi wako, unisaidie mu mateso.

Mama Maria Mtakatifu, unisaidie.

Yule Ulitamania sana, ambaye ulifwata hatua, alikuongoza na alikulinda mu njia ya kutubu na ni Mungu wa huruma tena umuombe ili atuokoe ku tamaa na atuokoe ku hatari yoyote.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Kaza moyo wangu pa jiwe la imabni, ee Baba Mtakatifu; unizungushe ne woga wa Mungu, ee Mtakatifu Andrea, nakuomba unipe neema ya kitubio na uniokoe kwa Adui anayependa kunikamata ku wavu wake.

Utukufu kwa Baba. . .

Utatu Moja na usiyogawanywa, Umoja mwenye asili moja, Nuru ya miangaza tatu, chemchem ya uzima tena Mungu wa wote.

Sasa na siku zote. . .

Tunakuimba, tunakushukuru, tunasujudu mbele yako, ee Mzazi-Mungu, kwa sababu ulizaa Mumoja wa Utatu Mtakatifu, Mwana wako na Mungu wako, ukitufungulia sisi mbingu pa dunia.

WIMBO YA MNANE.

Sauti ya mnane.

IRMOS: Mfalme wa utukufu wa milele ambaye mbele yake ezi za mbinguni zimetetemeka na malaika wa Mungu wametetemeka, makuhani, mumutukuze, taifa nzima, umusifu milele na milele.

Mitume Watakatifu wa Kristu, mutuombee.

Mitume Watakatifu wa Kristu, ni mu maarifa ya Roho ambamo mulijenga Kanisa mu jumla yake*:* katika yeye mumushukuru Kristu milele na milele.

Walipopasha kwa furaha mafundisho yao, Mitume walibomoa ibada ya sanamu, wakifukuza kosa kwa mlio wa sauti yao sababu ya kutukuza Kristu milele na milele.

Mitume Watakatifu wa Bwana, walinzi wa dunia tena wanainchi wa mbinguni, muokoe hii hatari yoyote wale wanaoimba sifa bila mwisho.

Utukufu kwa Baba. . .

Bwana Mungu unayeangaa sawa jua tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, unayejinganyia

utukufu wa kiti moja cha ufalme, nakuimba milele na milele.

Sasa na siku zote. . .

Sawa kiti cha ufalme cha juu, mataifa, tumwimbe bila mwisho Mzazi-Mungu ambaye yeye peke kisha kuzaa anaweza kuitwa kwa mara moja Bikira na Mzazi.

Sauti ya sita.

IRMOS: Yeye ambaye Malaika wote wanatukuza, mbele yake Wakeruvu na Waserafi wametetemeka, na ile iliohai na pumuzi, na kiumbe chote kimwimbe, kimushukuru na kumutukuze milele na milele.

Nilitenda zambi, Mwokozi unihurumie, kakamisha roho yangu kwa kuongoka tena unifanyie neema wakati ninapolalamika*:* Nilitenda zambi juu yako peke, unihurumie.

Elie alipopanda gari la moto akachukuliwa pa mabawa ha fazila tangu dunia mpaka mbinguni*:* Fafanisha, ee roho yangu, kupnda kwake.

Zamani alipopokea nguo ya Elia, alipata neema mbili kwa Bwana; lakini wewe, roho maskini, uko mbali na neema hii.

Zamani mto wa Yordani ulikaushwa kwa Elisee aliyeupasua ngambo na ngambo, pakuupiga na nguo ya Elia; lakini wewe, roho maskini, uko mbali na neema hii.

Mwanamuke Musunamite mu wema wake alimutolea Mwenye Haki mapokeleo, lakini wewe, ee roho yangu, haukumpokea mugeni, msafiri, tena utalia mbnali ya nyumba ya Bwana Arusi.

Roho maskini, ulifananisha ukosefu wa Ghiezi, ku mwisho wa siku zako kataa tamaa yako sababu ya kuepuka Gehena ambayo inastahili maovu yako.

Alipolalamika mu matope. Yeremia zamani akalialia, akatoa machozi pa muji wa Sayuni; fananisha machozi yake na utaokolewa.

Alipotambua kugeuka kwa Waniniwa, Yona zamani akakimbilia ku Tarsis, kwani alitangulia kujua huruma ya Mungu wake, siku zote tayari kwa kurudia pa amri zake.

Ndani ya shimo nabii Danieli alifunga kinywa cha Simba, na vijana wanaume tatu walizima kwa imani yao tanuru kubwa ya moto ya wakaldea

Ee roho yangu, nilikuonyesha mifano yote ya SAgano la kale*:* Fananisha vitendo vya wenye haki rafiki za Mungu, tena epuka mufano wa waovu.

Sawa Mwivi mwema, nakulalamikia, Bwana*:* Unikumbuke. Sawa Petro nalia kwa unchungu; sawa Mtoza ushuru, nalalamika*:* Unihurumie; sawa Mwanamuke wa zambi nyingi na wa kanana*:* Bwama, pokea machozi yangu.

Mwokozi, ponyesha roho yangu yenyi kuumizwa, wewe peke mganga, unibandikie kitambaa, na mafuta na vinyo, matunda ya kutubu na machozi ya sikitiko.

Sawa mwanamuke wa Kanana, nakulalamikia*:* Mwana wa Daudi, unihurumie; sawa mwanamuke wa kotoa damu, nagusu ku nguo yako, tena nalia sawa Martha na Maria peko Lazaro.

Ee Mwokozi wangu, namimia pa kichwa chako chombo cha jiwe kilicho na manemane ya machozi yangu, sawa Mwanamuke wa zambi nyingi zamani, naomba huruma yako; sikiliza ombi langu na unipe rehema yako.

Kama hata mumoja hayatukana wema wako sawa mimi, ee Mwokozi wangu, lakini pokea kutubu kwangu mlio wangu wa mapendo na wa heshima*:* Unihurumie, mimi mwenye zambi.

Mwokozi, samehe kazi ya mikono yako, Mchungaji mwema, tafuta kondoo wako aliyepotea; unilinde kwa mbwa-mwito munyanganyi na unifanye mwana kondoo wa zizi lako.

Ee Kristu, wakati utakapokaa kwa kuhukumu, wakati utukufu wako utangaa, Oh! woga gani ku wakati huu, wakati itawaka tanuru ya moto na kila mutu atatetemeka mbele ya Korti yako ya kuogopesha.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Ulipoangazwa kwa mama wa Nuru ya milele, ulikimbia ku giza za tamaa; walipopokea kwa ajili yako neema ya Roho, angaza, ee Maria, waaminifu wanaokuimba.

Mama Maria Mtakatifu, utuombee.

Mtakatifu Zosima ulishangaa pakuona muujiza huu mupya, kwani ulikuwa, ee Maria, malaika ya mwili, na aliposyaajabu, akatukuza Kristu milele.

Mtakatifu Andrea wa Kreti, utuombee.

Wewe unayeweza kusema kwa Bwana, ee Mtakatifu Andrea, nakusihi*:* Kwa maombezi yako matakatifu uniokoe ku zambi ili niimbe utukufu wako kati ya Watakatifu.

Tumushukuru Bwana, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Baba wa neno Mungu, Mwana wa milele tena Neno la Baba wasipo wakati, Roho Mfariji na muumba wa uzima, Utatu Mtakatifu, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Emmanueli alivaa damu yako, ni kwa ukweli, ee Bikira Mtaktifu tunaheshimu uzazi wako.

Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Yeye ambaye Malaika wote wanatukuza, mbele yake Wakeruvu na Waserafi wametetemeka, na ile iliohai na pumuzi, na kiumbe chote kimwimbe, kimushukuru na kumutukuze milele na milele.

WIMBO YA TISA.

Sauti ya mnane.

IRMOS: Mpatanishi kati ya dunia na mbingu, tunakusifu kizazi na kizazi, ee Bikira, umungu wote ulikaa kwa mwili ndani yako.

Mitume Watakatifu, wote mu kundi, kwa nyimbo zetu tunamitukuza, kwa sbaabu mu dunia ninyi ni taa za mwangaza tena mulifukuza giza za udanganyifu.

Mu wavu wenu wa habari njema mulikamata samaki za siri, tena na tena, Mitume wenye heri, munawapeleka ku Meza ya Bwana.

Miutume Watakatifu, mutukumbuke mu ombi lenu mbele ya Bwana tena muopoe ku kishawishi chochote wale wanaomiimba kwa moyo wote.

Utukufu kwa Baba. . .

Naimba umungu wa asili umoja, katika watu tatu umoja wa Baba, wa mwana na wa Roho Mtakatifu, na uwezo wa usawa wa Utatu wa milele.

Sasa na siku zote. . .

Bikira na Mzazi, tunakusifu kizazi na kizazi kwa sababu ulituokoa ku apizo pakumuzaa

Bwana, Furaha yetu.

Sauti ya sita.

IRMOS: Ulipata mimba pasipo mbegu, uzazi wako ni usiyokadirika, ee mama msiyeolewa: kwa ubikira Mungu alijifanya mtu na anabadilisha sheria za dunia; tena kufwata imani ya kweli, ee Bikira Mzazi-Mungu, tunakusifu kizazi na kizazi.

Moyo wangu ni wenyi kuumizwa, mwili wangu unaregea, akili yangu inapunguka, wazo langu halina nguvu, mwisho umekaribia, uzima wangu umezimia*:* Roho maskini, utafanya nini wakati Mwamzi atakuja kufumbua matendo yake ya siri?

Ee roho yangu, niliweka mbele yako maandiko ya Musa yanayoelekea mwanzo wa dunia na mashauri yake yote, habari ya wenyi haki na makafiri; ulifananisha hawa wa mwisho na haiko wale wa kwanza, kwa sababu utenda zambi, ee roho yangu, juu ya Mungu.

Amri inabaki bila utimizo, Evangelio bila matunda, hauna na sikitiko ya Andiko lote, Manabii hawana na uwezo, vilevile na maandiko ya wateule, vidonda vyako, ee roho yangu, vinaongezeka, kwani hauna mganga ataweza kukuponyesha.

Ku Agano jipya mifano ya kukualika, ee roho yangu, ku sikitiko*:* Tumainia watu wenye haki, epuka wenye zambi, tolea neema ya Kristu kwa kufunga na sala na usafi wa uzima wako.

Kristu alijifanya mtoto kidogo, alijiunga ku mwili wangu; sababu ya kutimiza kwa mapendo yake hali yote ya ubinadamu ila zambi; anakuonyesha, ee roho yangu, mfano na sura ya ukubali wake haujaonekana.

Kristu alijifanya mtu, akaita makahaba na wanyanganyi ku toba, fanya kitubio, ee roho yangu, kwa sababu mlango wa Ufalme ulisha kufunguka na tunatanguliwa kwa wafarisayo, watoza ushuru na wanawake wenye zambi waliotubu.

Kristu aliokoa Majusi na alikusanya Wachungaji wa kondoo, anattosha ku kifo watoto wasiyo zambi, mu hekalu anatukuza Mzee na Mujane ku mwisho wa siku zake; ee roho yangu, haukufananishe matendo ya uzima wao, tena mateso kwako wewe utakayepita ku hukumu.

Alipofunga siku makumi ine mu jangwa, Bwana akaonyesha ubinadamu wake pakusikia njaa; vilevile, roho yangu, usiregee ku mashambulio ya Adui*:* Utamukanyanga na miguu pa kufunga na ku sala.

Kristu alijiribiwa, Shetani alimujaribu; akamuonyesha mawe sababu ya kuifanya mkate; akamupeleka pa mlima sababu ya kumuonyesha ufalme wote wa dunia; ongopa sana, ee roho yangu, mambi hii*:* Uwe macho na umuombe Bwana mu kila wakati.

Njiwa anayezoea pahali pasipo watu, sauti inayovuma mu jangwa*:* Ni taa linalitangulia Kristu, anahuburu kutubu, Herodi na Herodiada wanatenda zambi juu ya Mungu; na wewe, ee roho yangu, kesha usiangukie mu wavu wa wachafu, lakini rudia mpaka kwa Bwana.

Alikaa mu jangwa, Mtangulizi wa Mungu; Yudea na samaria walikuja wapesi ku sauti yake; wakiungama zambi zao, walipokea ubatizo mu furaha; wewe peke, ee roho yangu haukufananisha kuongopa kwao.

Ndoa inastahili heshima, kitanda na arusi haistahili magombezi, kwa sababu Kristu alizibariki ku amri ya Kanana wakati alivaa mwili wetu, akageuza maji kuwa vinyo, ni muujiza

wa kwanza aliyefanya kati ya miujiza zake sababu ya kukugeuza.

Kristu alisimamisha Mwenye kupooza, alimubebesha kitanda chake, alifufua toka wafu mtoto wa mujane wa ku Naini na mtumishi wa Akida; kisha akajionyesha kwa mwanamuke wa Samaria, katika yeye, alikufundisha, ee roho yangu, Ibada ya roho.

Kwa tamvua ya nguo yake Kristu aliponyesha mwanamuke mwenye kutoa damu; alitakasa wenye ukoma, akaleta nuru na nguvu kwa vipofu na vilema, na kwa neno lake alitunza viziwi na viwete na mwanamuke mwenye kukujama; kwa wewe, roho yangu, analeta tena wokovu.

Wagonjwa wanaponyeshwa, habari njmea inatangaziwa kwa wamasikini kwa kristu na neno la Mungu anayeponyesha kilema chochote; anakula ku meza ya wafarisayo na anatembelea wenyezambi; na pakukamata binti wa Yairo ku mukono anarudisha mu mwili wake pumuzi ya uzima.

Mtoza ushuru alifanya wokovu wake, kahaba alipata usafi wa roho, lakini Mufarisayo mwenye majivuno alihukumiwa, kwa sababu mumoja alisema*:* Unirehemu; wa pili*:* Unihurumie; lakini wa tatu alijisifu*:* nakupigia aksanti, ee Mungu wangu, akijitukuza bila haki.

Zakayo alikuwa mtoza ushuru, lakini alipokea wokovu, na Simoni Mfarisayo akanungunikia udanganyifu wake wakati kahaba alipokea uokozi na rehema ya yule anaye uwezo wa kuondolea zambi; ee roho yangu, ujiharikishe kwa kupokea vilevile maondoleo yake.

Ee roho yangu, haukufananishe mfano wa kutubu wa Mwanamuke mwenye zambi*:* alipokamata chombo cha manukato na kuongezako machozi yake, akaimwangia ku miguu ya Bwana, na nywele yake akazima hati ya zambi zake.

Ee roho yangu, ulijua mkoshi gani ilipata muji mule Kristu alileta habari ya wokovu; usifwate mufano wao, kwa kuepuka bahati yao mbaya*:* Pakuwafananisha na Sodoma rabi akawahukumu wastahili wa Gehena.

Ee roho yangu, usikose tumaini, Mwanamuke wa Kanana asikutangulie, kwa sababu unajua imani yake kubwa na namuna ambayo Bwana kwa neno lake la uwezo aliponyesha mwana wake, na lalamika chini ya moyo wake sawa alivyofanya mbele ya Kristu*:* Uniokoe, ee Mwana wa Daudi.

Mu huruma yako uniokoe, unihurumie, Mwana wa daudi, wewe unayeokoa kwa neno lako wenye kuwa na Shetani, tuma juu yangu, sawa zamani kwa Mwivi mwema mapendo ya sauti yako*:* Kweli, ninakwambia leo utakuwa pamoja nami katika Paradizo.

Mwivi moja alikutykana pa msalaba, mwengini akaungama umungu wako; lakini wote wawili walikuwa na mateso ya namuna moja. ee Bwana wa wema wote, sawa kwa Mwivi wakop mwaminifu aliyekujua sawa Mungu, unifungulie mlango wa Ufalme wako utukufu.

Kiumbe kilipata woga, Bwana, pakukuona ma Msalabna, milima na mawe zilipasuka kwa hofu, udongo ulitikisika na gehena ikapoteza mateka yake; nuru ikageuka giza katika mchana, ee Yesu pakukuona umesulubiwa.

Usilazimihe kwangu matunda ya heshima ya kutubu, kwa sababu nguvu yangu inaisha, lakini unipe siku zote sikitiko ya moyo na roho ya umaskini ili niweze, ee Mwokozi wangu, kukutoleazo mu sadaka.

Elezo*: Sasa ku mwisho tunaimba mara ingine Irmos wa Tisa:*

Ulipata mimba pasipo mbegu, uzazi wako ni usiyokadirika, ee mama msiyeolewa*:* kwa ubikira Mungu alijifanya mtu na anabadilisha sheria za dunia; tena kufwata imani ya kweli, ee Bikira Mzazi-Mungu, tunakusifu kizazi na kizazi.

FOTAGOGIKON.
DOKSOLOGIA KIDOGO

APOSTIKHA

Sauti ya mnane

Ee roho yangu, ulipoanguka katika mikono ya wanyanganyi, tazama umejeruhiwa vibaya, unatolewa kwa hasira ya adui kwa zambi zako mwenyewe; lakini kwa hii wakati yenyi kufaziliwa umulalamikie Bwana katika sikitiko*:* Wewe mwenyi kuleta nguvu ku roho yasipo matumaini, ee Mwokozi, uniamshe na uniokoe.

Shairi: Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia . . .

Tunaimba mara ingine hii wimbo ya yulu.

Shairi: Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya. . .

Kwa uhodari mulivaa kanzu ya chuma ya imani, mulishika alama ya Msalaba kama silaha, mulionekana kuwa waaskari washujaa, mulishindana vema na wazulumu, muliondoa uwongo ya Shetani, mulistahili taji ya washindi*:* Ombeni Kristu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Pokea mwito ya watumishi wako, ee Bikira Mtakatifu Mzazi-Mungu, na omba kusudi tupate amani na maondoleo ya zambi zetu.

MU KAZI INE MANGARIBI YA JUMA WA TANO

Elezo*:* Kisha*:* «*Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo na ma shairi kumi; wimbo sita ya Triodi ile inafwata na wa inne ya Mineon.*

Sauti ya mnane. Idiomelon

Kwa kutaka kwangu, kwa kutokutii kwangu kwa kwanza niliondolewa nuru ya fazila*:* Kwa mapendo yako, ee Neno wa Mungu, naivaa mara ingine; kwa sababu hauzarau roho yangu yenyi kuchafuliwa kwa tamaa na kujeruhiwa vibaya na wanyanganyi, lakini kwa uwezo wako wote ulikuja kuniokoa, ukanistahilisha msaada wako, ee Bwana mwenye rehema. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi.

Enyi Mashahidi wa Bwana, ninyi wenyi kutakasa ulimwengu na kuponyesha ugonjwa wote, mutuombee sasa sababu ya kuokoa roho zetu toka mutego wa adui.

Sauti ya kwanza. Panefimi Martires

Ee Bwana, uliposulubiwa Msalabani, kwa mkuki takatifu ulipasua deni ya Adamu; Vunja pia minyororo yangu, ee Neno wa Mungu, ili nikutolee sadaka ya sifa kwa furaha na imani, na kwa hii Kwarezima nipate wakati wa fazila unatupa sisi kwa ajili ya wokovu wetu.

Alipoangazwa sura kwa kufunga, Musa aliona utukufu wa Mungu; ee roho maskini, ujikaze kumufananisha, na kwa sababu Mwokozi alipanua mikono Msalabani, nyanyua mikono yako sababu ya kumuomba, kumutumikia katika kufunga na matendo mema sababu ya kupata kitulizo cha Mungu.

Wimbo ingine. *Sauti ya sita. Arkangelikos...*

Ee Kristu, tunaposujudia Msalaba wako wenyi kuleta uzima ambao katika hii ulituonyesha wema wako isiyokadirika na roho yenyi kuangazwa kwa nuru yake, tunakuimbia daima, tunakuomba kwa moyo wote tutimize kipindi cha Kwarezima katika furaha na tutukuze, ee Bwana, Mateso yako ulituokoa nasi.

Wimbo ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa a siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya saba. Zaburi 98.

Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa mulima wake mutakatifu; maana Bwana Mungu wetu ni Mutakatifu.

Shairi*:* Bwana anatawala, mataifa watetemeke.

Somo ya Mwanzo tutasoma (18, 20-33)

Bwwana akasema: Kwa sababu kilio cha Sodomo na Gomora ni kikubwa, na kwa sababu zambi zao ni nzito sana; nitashuka sasa nione kama walivyofanya kwa kipimo cha kilio chake kilichofika kwangu; na kama sivyo, nitajua. Watu wakageuka toka pale, wakakwenda Sodomo; lakini Abrahamu alikuwa angali akisimama mbele ya Bwana Abrahamu akakaribia, akasema*:* Utahanbu wenye haki pamoja na waovu? Labda wenye haki makumi tano ni mujini; utaharibu wala hutaacha pahali pale kwa ajili ya wenye haki makumi tano walio ndani yake? Haiwezekani kwako kufanya namna hii, kuharibu wenye haki pamoja na waovu, wenye haki wawe kama waovu; sivyo, haiwezekani kwako; mwamuzi wa dunia nzima hatatenda kwa haki? Bwana akasema*:* Kama nikikuta ndani ya Sodomo wenye haki makumi tano mujini, nitaacha pahali pale pote kwa ajili yao. Abrahamu akajibu, akasema*:* Tazama, sasa nimeshika kusema na Bwana, mimi niliye mavumbi na majivu tu; Labda wenye haki makumi tano watakosa watano; utaharibu muji wote kwa sababu ya kukosa watano? Akasema*:* Sitauharibu kama nikikuta makumi ine na watano. Akasema naye tena, akisema*:* Labda makumi ine wataonekana. Akasema*:* Sitafanya kwa ajili ya makumi ine. Akasema*:* Bwana asikasirike, na nitasema*:* Labda makumi tatu wataonekana pale. Akasema*:* Sitafanya nikikuta makumi tatu pale*:* Akasema*:* Tazama sasa, nimeshika kusema na Bwana*:* Hakose makumi mbili wataonekana pale. Akasema*:* Sitauharibu kwa ajili ya makumi mbili. Akasema*:* Bwana asikasirike, na nitasema mara moja tu*:* Labda kumi wataonekana pale. Akasema*:* Sitauharibu kwa ajili ya kumi. Bwana akakwenda zake alipokwisha kuse-mezana na Abrahamu. Abrahamu akarudi kwa pahali pake.

Prolimenon. Sauti ya sita. Zaburi 99.

Mufanyie Bwana shangwe, ninyi inchi zote.

Shairi*:* Tumikieni Bwana kwa furaha.

Somo ya Mezali tutasoma (16, 17-17, 17).

Njia kubwa ya mwenye haki ni kujitenga na uovu*:* Mwenye kushika njia yake analinda nafsi yake, Majivuno yanatangulia uharibifu, Na roho ya kiburi inatangulia kuanguka. Afazali kuwa na roho ya unyenyekevu pamoja na masikini, Kuliko kugawa nyara pamoja na wenye majivuno. Mwenye kuangalia neno atapata mema*:* Na mwenye kutumainia Bwana ana heri. Mwenye moyo wa hekima ataitwa mwenye akili*:* Na utamu wa midomo unaongeza elimu. Ufahamu ni chemchemi ya uzima kwake aliye nao*:* Lakini kufundishwa kwa wapumbafu ni upumbafu wao. Moyo wa mwenye hekima unafundisha kinywa chake, na unaongeza elimu ya midomo yake. Maneno ya kupendeza ni kama sega la asali, Matamu kwa nafsi, na afya kwa mifupa. Kuna njia inayoonekana kuwa sawa kwa macho ya mutu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti. Njaa ya mutu wa kazi inamufanyia kazi;Maana kinywa chake kinamutia bidii. Mutu asiye na faida anachimba shimo la matata*:* Na ndani ya midomo yake ni kama moto unaoteketeza. Mutu wa ukaidi anasambaza ugomvi*:* Na muchongezi anagawa rafiki. Mutu wa jeuri anashawishi jirani yake, na kumwongoza katika njia isiyo njema. Mwenye kufunga macho yake, kusudi lake ni kuwaza maneno ya kuasi*:* Mwenye kukaza midomo yake anatokeza mabaya.

Kichwa cha imvi ni taji ya utukufu. Kitapatikana katika njia ya haki. Yeye asiye mwepesi kukasirika ni mwema kuliko wenye uwezo; Naye anayetawala roho yake ni mwema kuliko yeye anayekamata muji. Kura inatupwa katika mikunjo ya nguo; Lakini hukumu zake zote zinatoka kwa Bwana. Mutenda mabaya anasikiliza midomo miovu, na muwongo anasikiliza ulimi wa matata. Mwenye kuzihaki masikini analaumu Mwumba wake*:* Naye anayefurahia hasara hatakosa azabu. Wana wa wana ni taji ya wazee; Na utukufu wa watoto ni baba zao. Maneno mazuri hayapendezi kinywani mwa mupumbafu*:* Wala midomo ya uwongo kinywani mwa mukubwa. Zawadi ni kama kito cha neema kwa macho yake aliye nacho*:* Pahali po pote kinapogeuka kinasitawi. Mwenye kufunika kosa anatafuta mapendo*:* Lakini mwenye kurudi tena na tena juu ya neno moja anatenga rafiki. Laumu Iinaingia moyoni mwa mwenye ufahamuKuliko mapigo mia moja moyoni mwa mupumbafu, Mutu mwovu anatafuta kuasi tu; Kwa hivi mujumbe mukali atatumwa juu yake. Afazali dubu aliyenyanganywa watoto wake akutane na mutuKuliko mupumbafu katika upumbafu wake. Mwenye kurudisha mabaya kwa mema, Mabaya hayataondoka nyumbani mwake. Mwanzo wa ugomvi ni kama kuacha maji kutoka*:* Kwa hivi acheni mabishano mbele ya kugeuka kuwa magomvi. Mwenye kuhesabia mwovu haki naye anayehukumu mwenye haki, Wao wawili ni machukizo kwa Bwana. Kwa nini kuna feza mukononi mwa mupumbafu ili anunue hekima, Naye hana ufahamu? Rafiki anapenda siku zote, na kuna ndugu aliyezaliwa kwa siku ya taabu.

MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA WA TANO

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.

Ee Kristu ulipopanua mikono Msalabani, kwa vidonda vyako uliponyesha kidonda cha Adamu; ndio maana nakuomba uponyeshe vidonda Muovu aliumiza roho yangu na unistahilishe, ee Mwokozi, nikutumikie katika sala na maombi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, wakati Mama yako Mtakatifu kamili alikuona umetundikwa Msalabani, akalalamika*:* Ee Mwanangu wa milele pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, hii ni fumbo gani ya tendo lako la wokovu? Katika yeye uliokoa, kwa wema wako ee Rabi, kazi ya mikono yako.

KATHISMA YA TATU

Sauti ya sita. Elpis tu kosmu.

Ee Msalaba takatifu, mlinzi wa dunia, wewe mwenyi kufukuza mashetani, uwape wale ambao wewe ni ulinzi wa ushindi watimize hii sehemu ya Kwarezima inabaki katika usafi na ongoza roho zetu kwa Kristu ambaye sura iliangaa juu yetu sisi juu ya Msalaba.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakaitfu, wewe uliye utukufu ya Malaika mbinguni, wakati ulisimama chini ya Msalaba ukiona Mwana na Mungu wako akitukanwa na wakafiri, kama mama kwa kulia kwako ulipaza sauti na kusema*:* Namna gani unateswa kwa hii maneno ya mateso? Ee mpenda-wanadamu na Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

FOTAGOGIKON.

APOSTIKHA.

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Ee Kristu Mungu wetu, uliposulubiwa Msalabani pamoja na wanyanganyi, uliponyesha kidonda cha wanadamu; usizarau roho yangu yenyi kuangukia mikononi mwa wevi na wanyanganyi wasioonekana walinyanganya fazila zake na kuiumiza vikali; hakuna hata mumoja wa Wataaktifu wako hakuweza kuniponyesha kwani mimi ni karibu kufa, bahati yangu moja ya kuishi ni kukutumainia wewe, kwa sababu unafufua wafu, unatunza vidonda vyangu kwa kuipakaa dawa ya huruma yako kwa mapendo unatupenda nayo, ee Bwana. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi

Namna gani tutawaita, enyi Mashahidi Watakatifu? Wakheruvi? Kwani ninyi ni kiti cha Kristu; Waserafi? Kwani munamutukuza daima; Malaika? Kwa sababu munakataa mwili wenu; Majeshi? Sababu ya miujiza yanatendeka*:* Muna majina mengi na zawadi nyingi sana! Ombeni ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ni ajabu wa kweli! Ni fumbo ya ajabu na mupya, ndivyo alivyosema Bikira alipoona Msalabani ametundikwa katikati ya wanyanganyi huyu alizaa bila uchungu, kwa kuomboleza, akalia akisema*:* Ole wangu! Ee Mwanangu, namna gani hawa watu waovu kwa kukosa kwao imani wanakusulubisha Msalabani?

MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA WA TANO

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo 3 ya hii Kitabu na 3 ya Mzazi-Mungu.

Sauti ya sita. Idiomelon.

Nilipoacha Yerusalema, maana mafundisho yako takatifu, kwenda yeriko, maana tamaa, nikashuka nikishulikia hii uzima katika njia ya haya, nikanguka katika udanganyifu wa mawazo na kwa hii nikaondolewa njuo wangu nzuri ulinipa kwa neema ya upokeleo; tazama mimi ni karibu kufa na mwili wangu wote unajua vidonda; kuhani mumoja alipita na aliona mateso yangu, akajiendea; mulawi mumoja alichukizwa, hakuniangalia; lakini wewe, Bwana, uliyejifanya mutu kwa Bikira, ulimimia kama mafuta na mvinyo damu na maji ilitoka katika ubavu wako wenyi kuleta uzima, sababu ya kutunza na kufunga na vitambaa vidonda vyangu*:* Ee Kristu Mungu wetu, kwa mapendo yako ya huruma, unipe fasi mbinguni. *(mara mbili).*

Wimbo ya Mashahidi.

Ee Bwana, Mashahidi wako hawakukukana, hawakujitenga ku mafundisho yako*:* Kwa maombezi yao utuhurumie.

Wimbo ya Mzazi-Mungu. Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Ee Bikira, alipotambua nia yako ya milele, Gabrieli alisimama mbele yako na akakuamkia akisema*:* Udongo isiyo na mapendo, salamu wewe kichaka chenyi kuwaka bila kuungua, zimu refu kwa kuitazama; salamu, wewe kilalo yenyi kupeleka toka dunia mpaka mbinguni, mungazi ambao Yakobo aliona, chombo takatifu cha maana ya mbinguni; salamu Wewe mwenyi kutuokoa ku laana, salamu, wewe matumaini ya Adamu na kuinuka kwake*:* Bwana ni pamoja nawe.

Bikira safi kamili alimwambia Malaika wa Mungu*:* Umeonekana kwangu kama mwanadamu na maneno yako yanapita mawazo ya watu! Unasoma ya kwamba Bwana ni pamoja nami na ya kama atakaa tumboni mwangu, namna gani nitakua uniambie, ni makao ya wa milele,

ni hekalu takatifu ya Bwana anayeketi katika kiti cha Wakheruvi? Hii itakua namna gani? Kwa sababu sijui mume namna gani basi nitazaa mtoto?

Malaika akamujibu*:* Wakati Mungu anataka hivi, sheria za watu zinavunjwa, anatenda miujiza isiyo ya watu; unisadiki, nakuambia ukweli, ee Bikira Mtakatifu kamili. Hapo, Bikira akapaza sauti na kusema*:* Ifanyike kwangu kama unavyosema, nitazaa Mungu mkubwa, peke yake Mwenyezi atajifanya mutu mwilini mwangu sababu ya kurudisha wanadamu ku hali yao ya zamani kwa mchanganyo wa umungu wake na ubinadamu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Sauti ya mbili

Leo imefunuliwa fumbo ya milele, Mwana wa Mungu anakua Mwana wa mutu kusudi aondoemo ile iliyo mbaya na anipe ile iliyo nzuri zaidi; zamani Adamu alidanganyika*:* Alipotaka kufanana na Mungu, hakuweza; lakini sasa Mungu yeye mwenyewe anajifanya mutu ili Adamu awe Mungu. Viumbe vishangilie, dunia ifurahiwe kwa sababu Malaika, mwenyi kujaa na heshima, anakuja kumwambia Bikira*:* Salamu! Anageuza kilio cha wazazi wetu wa kwanza kuwa furaha. Wewe ambaye kwa mapendo ulijifanya mutu, ee Bwana Mungu wetu, utukufu kwako.

KUINGIA.

Mwangaza upole.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 102.

Bwana anajaa huruma, ni mwenye neema.

Shairi*:* Bariki, Bwana, ee nafsi yangu.

Somo ya mwanzo tutasoma (22, 1-18).

Na ilikuwa nyuma ya maneno haya Mungu akajaribu Abrahamu, akamwambia*:* Abrahamu; naye alisema*:* Mimi ni hapa. Akasema*:* Twaa sasa mwana wako, mwana wako wa pekee unayemupenda, hata Isaka, uende zako hata inchi ya Moria; umutoe pale kwa sadaka ya kuteketezwa juu ya mumoja wa milima nitakaokuambia. Abrahamu akaondoka asubui mapema, akatandika punda yake, akatwaa wawili wa vijana wake pamoja naye na Isaka mwana wake ; akapasua kuni kwa sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akakwenda kwa pahali Mungu alipomwambia. Siku ya tatu Abrahamu akanyanyua macho yake, akaona pahali penyewe mbali. Abrahamu akawaambia vijana wake*:* Mukae hapa pamoja na punda, nami na kijana tutakwenda kule ; na tutaabudu na kurudi tena kwenu. Abrahamu akatwaa kuni kwa sadaka ya kuteketezwa, akabebesha Isaka mwana wake ; akashika moto na kisu mukononi mwake; wakakwenda pamoja wao wawili. Jsaka akamwambia Abrahamu baba yake, akasema*:* Baba yangu; akasema*:* Mimi ni hapa, mwana wangu. Akasema*:* Tazama moto na kuni; lakini wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa? Abrahamu akasema*:* Mungu atajipatia mwenyewe mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa; basi wakakwenda pamoja, wao wawili. Wakafika kwa pahali Mungu alipo-mwambia. Abrahamu akajenga mazabahu pale, akatengeneza kuni, akafunga Isaka, mwana wake, akamuweka juu ya mazabahu, juu ya kuni. Abrahamu akanyosha mukono wake, akatwaa kisu achinje mwana wake. Na malaika ya Bwana alimwita toka mbingu, akasema*:* Abrahamu, Abrahamu; naye alisema Mimi ni hapa. Akasema*:* Usitie mukonojuu ya kijana, wala usimufanyie kitu, kwa sababu sasa ninajua ya kama unaogopa Mungu, kwa sababu hukukataa kunipa mwana wako, mwana wako aliye wa pekee. Abrahamu akanyanyua macho yake, akaangalia na tazama, nyuma yake kondoo ndume amefungwa na pembe zake katika kichaka. Abrahamu akakwenda, akatwaa kondoo ndume, akamutoa kwa sadaka ya kuteketezwa kwa pahali pa mwana wake. Abrahamu akaita jina la pahali pale Yehova Yire, kama inavyosemwa hata leo*:*

Katika mulima wa Bwana itapatikana. Malaika ya Bwana akaita Abrahamu mara ya pili toka mbingu, akasema*:* Nimeapa kwa mimi mwenyewe, Bwana anasema, kwa sababu wewe ulifanya kitu hiki, wala hukukataa kunipa mwana wako, mwana wako atiye pekee ; basi katika kubariki

nitakubariki, na katika kuongeza nitaongeza uzao wako kama nyota za mbingu ; kama muchangaulio juu ya pwani ya bahari; na uzao wako watariti lango la adui zake; na kwa uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa; kwa sababu umetii sauti yangu.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 103.
Ee Bwana, kazi zako ni ninyi sana! Kwa akili ulijifanya yote
Shairi*:* Bariki Bwana, ee nafsi yangu.

Somo ya Mezali tutasoma ((17, 17-18, 5)

Rafiki anapenda siku zote, Na kuna ndugu aliyezaliwa kwa siku ya taabu. Mutu asiye na ufahamu anapiga mikono, na kuwa zamana mbele ya jirani yake. Mwenye kupenda magomvi anapenda makosa*:* Naye anayenyanyua lango lake juu anatafuta uharibifu.

Mwenye moyo wa ukaidi hatapata mema*:* Naye aliye na ulimi wa ukaidi anaanguka katika matata. Mwenye kuzaa mupumbafu, ni kwa huzuni yake mwenyewe*:* Na baba ya mupumbafu hana furaha. Moyo wa furaha ni dawa nzuri*:* Lakini roho inayovunjika inakausha mifupa, Mutu mwovu anatoa zawadi kifuani, Ili kupotosha njia za hukumu. Hekima ni mbele ya uso wake aliye na ufahamu*:* Lakini macho ya mupumbafu ni katika miisho ya dunia. Mwana mupumbafu ni huzuni kwa baba yake, na uchungu kwake aliyemuzaa. Tena kuazibu mwenye haki si vizuri, Wala kupiga wakubwa kwa haki yao. Mwenye kuzuiza maneno yake ana maarifa*:* Na mwenye roho ya baridi ni mutu wa ufahamu. Hata mupumbafu, wakati anaponyamaza, anahesabiwa kuwa mwenye hekima*:* Wakati anapofunga midomo yake anahesabiwa kuwa na akili. Mwenye kujitenga na wenzake anatafuta kutaka kwake mwenyewe, Na anashindana na kila shauri jema. Mupumbafu hapendezwi na ufahamu, lakini moyo wake tu ujifunue. Wakati mwovu anapokuja, kuzarau kunakuja vilevile, na pamoja na haya laumu. . . . . Maneno ya kinywa cha mutu ni kama maji ya vilindi;Chemchemi ya hekima ni kama kijito kinachotembea. Kukubali uso wake aliye mwovu si vizuri, Wala kupotosha mwenye haki hukumuni.

MU POSHO YA JUMA WA TANO YA KWAREZIMA

SIKU KUU YA WIMBO AKATHISTE YA MZAZI-MUNGU.

Elezo*: Mu Posho asubui, kisha somo ya eksapsalmos tunaimba:* «Bwana ndiwe Mungu. . . . » *na kisha Wimbo hii:*

To prostakthen Sauti ya mnane

Nyimbo zetu za ushindi zisikilika kwa ajili yako, Malkia mshindi, wewe mwenyi kutuokoa ku hatari ya vita, ee Mzazi-Mungu, Bikira Malika! Sifa na nyimbo zetu za shukrani zinapanda kwako. Mkono wako wa uwezo inasimika pembeni yetu boma ya nguvu sana, utuokoe ku hatari yote, saidia kwa haraka waaminifu wenyi kukuimbia*:* Salamu, ee Bibi usiyeolewa.

KATHISMA. *Sauti ya mnane.*

Kwako jemadari kunilinda nina deni kukushukuru kwa wokovu na kushinda wangu mimi mji wako, ee Mzazi-Mungu. Tena kwa mamlaka yakosi kushindwa, na hatari kila namna niepuwe kukuimba, kwa kelele kuu*:* Salamu, Bibi Arusi, usiolewa. *(mara mbili)*

Kisha padri anasoma kipande moja ya Wimbo Akathiste, katikati ya Kanisa.

FUNGU WA KWANZA

I K O S 1

Alitumwa toka mbinguni Malaika Mkuu kumwambia Mzazi-Mungu*:* Salamu. Yeye alipokuona wewe, ee Bwana, ukipata mwili mara ileile kwa sauti yake ya bila-mwili, alistaajabu, akasimama na akasema na sauti kubwa.

Salamu, kwa kuwa unaangaza wokovu wetu.
Salamu, kwa kuwa katika wewe uovu uliondolewa.
Salamu, uliyemusimamisha tena Adamu aliyeanguka.
Salamu, uliyemwoka Eva halii tena.
Salamu, ndiwe mlima kutofikika kwa mawazo ya wanadamu;
Salamu, ndiwe bahari isiyoweza kufumbuliwa hata kwa macho ya Malaika.
Salamu, kwa kuwa wewe ni kiti cha ezi na makao ya Mfalme.
Salamu, kwa kuwa unamubeba Muumba wako.
Salamu, ndiwe nyota iliyoonyesha Jua, Salamu, ndiwe tumbo Mungu alimojifanya mtu.
Salamu, kwani katika wewe kiumbe kinapata upya;
Salamu, kwani kwako Muumba anakuwa mtoto.
Salamu, Bibi-Arusi usiyeolewa.

I K O S 2

Bikira Mtakatifu alipojua hali ya ubikira wake akamujibu Malaika Gabrieli na uhodari*:* Neno lako ni la ajabu rohoni mwangu, namna gani unasema nitachukua mimba, maana sijui mume?

Alliluia.

I K O S 3

Kwa kufahamu fumbo isiyo julikana. Bikira akamuelekea Mtumishi na akauliza namna gani anaweza kuzaliwa Mwana tumboni mwake. Malaika mwenye kujaa na heshima akamuambia na furaha*:* Salamu, maana umefumbuliwa shauri iliyo siri. Salamu, mlinzi wa fumbo yenye kufichwa. Salamu, ewe utangulizi takatifu wa miujiza ya Kristu. Salamu, ewe jumla ya Kanuni zake kimungu.

Salamu, ewe mungazi ya mbinguni huko Mungu alishuka;
Salamu, ewe kilalo chenye kutuongoza toka dunia mpaka mbinguni.
Salamu, ewe mastaajabu ya Malaika Watakatifu yasiyokwisha.
Salamu, kisa ya maombolezo ya Hadeze na ya mashetani.
Salamu, ewe uliyezaa nuru kwa njia isiyoelezwa;
Salamu, ewe usiyemufumbulia namna gani mtu hata mmoja;
Salamu, ewe unayepita maarifa ya wenye hekima;
Salamu, unayeiangazia akili ya waaminifu
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 4

Uwezo wa aliye-Juu ukamufunika na kivuli chake Bikira msiyeolewa kwa kupata mimba, na tumbo lake likawa Shamba tamu kwa wote watakao kuvuna wokovu kwa kuimba*:*

Alliluia.

I K O S 5

Alipochukua Bwana Mungu tumboni mwake. Bikira akaenda kuonana na Elisabeti*:* Mwana wake akatambua wokovu wa ajabu na akaruka tumboni mwa Mama yake akaimba kwa ajili ya Mzazi-Mungu*:* Salamu chipukizi la ua la milele;

Salamu, shamba la tunda tamu kabisa, bustani ya Bwana rafiki yetu.
Salamu, shamba munamoota uzima wetu.
Salamu, udongo wa kutoa wingi wa ukombozi.
Salamu, meza Takatifu na musamaha wa zambi;
Salamu, kwani unaotesha kwa ajili yetu shamba nzuri;
Salamu, kwani unatengenezea roho zetu bandari ya amani*:*
Salamu, uvumba wa harufu nzuri;
Salamu, ufidio wa ulimwengu wote;
Salamu, urazi wa Mungu kwa ajili ya wenye kufa;
Salamu, mwombezi wa wanadamu kwa Mungu.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 6

Roho ilipopata mashaka. Yosefu mtu wa haki akasikitika, kwani alijua ubikira wako, akizani wewe umejua mume kwa siri, ewe Mama usiye na doa, lakini mara alipata habari ya kuwa umepata mimba kwa tendo la Roho Mtakatifu akasema*:*
Alliluia

Elezo*: Kisha Waimbaji wanaimba Kontakion ya Mzazi-Mungu (mara mbili). Ni hii:*

Kwako jemadari kunilinda nina deni kukushukuru kwa wokovu na kushinda wangu mimi mji wako, ee Mzazi-Mungu. Tena kwa mamlaka yakosi kushindwa, na hatari kila namna niepuwe kukuimba, kwa kelele kuu*:* Salamu, Bibi Arusi, usiolewa.
Kisha, kama ni padri mwingine, ataendelesha kusoma Fungu wa mbili.

FUNGU 2

I K O S 7

Wachungaji waliposikia Malaika wakiimba umwilisho wa Kristu, wakamwendea Mchungaji wao ili wamutazame Mwana-Kondoo, mzaliwa mpya aliyelishwa tumboni mwa Maria, wakaimba wakasema*:*
Salamu, Mama wa Mwana-Kondoo na Mchungaji Mwema;
Salamu, zizi la Kondoo kwa akili;
Salamu, ulinzi juu ya maadui wasiyoonekana;
Salamu, funguo ya milango ya Paradizo.
Salamu, kwani mbingu inafurahi pamoja na dunia;
Salamu, maana wanadamu wanashangilia pamoja na Malaika;
Salamu, kinywa cha Mitume kisichonyamaza;
Salamu, uhodari wa Mashahidi washindaji usioshindwa.
Salamu, tegemeo sabiti ya imani.
Salamu, alama ya neema ya Mungu;
Salamu, kwani kwa ajili yako Gehena imenyanganywa mateka yake;
Salamu, kwa ajili yako tumevaa utukufu.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 8

Majusi walipoiona ile nyota ya njia-Kimungu, wakafuata mwangaza wake, wakaikamata kama taa kwa kumutafuta nayo mfalme Mwenyezi. Walipomufikia Msiyekaribika wakafurahi na wakasema*:*
Alliluia.

I K O S 9

Majusi wa Kaldea walipomuona Muumba wao mikononi mwa Bikira, wakamwabudu Bwana wao mu hali yake ya utumwa na wakamtolea zawadi zao, wakamsema na furaha mbarikiwa kamili*:*

Salamu, Mama wa Nuru ya milele.
Salamu, pambazuko ya siku iliyo Siri;
Salamu, uliyezimisha moto ya Gehena;
Salamu, taa yenye kutuonyesha Utatu.
Salamu, kwani ulimufuka mzalimu ku utawala wake;
Salamu, uliyemuonyesha Kristu Bwana mpenda-wanadamu;
Salamu, kwani ulituopoa ku ibada za upagani;
Salamu, kwani ulituondoa ku matendo yetu mabaya.
Salamu, uliyeizuia ibada ya moto;
Salamu, kwani ulizima moto ya tamaa;
Salamu, kwani unatuongoza ku hekima ya Mungu;
Salamu, ewe Shangilio ya vizazi vyote.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 10

Walipokuwa wanadi wabebaji-Mungu. Majusi wakarudi ku Babyloni wakitimiza unabii wako na kukuhubiri mbele ya wote kama Kristu, wakamwacha Herodi sawasawa mpumbafu asiyejua kuimba*:*

Alliluia.

I K O S 11

Ku Misri, ee Bwana, alipoangazwa na ukweli wako, ukafukuza giza ya uongo; maana sanamu zao zilishindwa na nuru yako, tena watu waliookolewa wakamwimbia Bikira*:*

Salamu, ewe matumaini ya wanadamu na ukombozi wao;
Salamu, ewe mregeo na anguko la mashetani;
Salamu, ewe uliyekanyanga hila ya nyoka.
Salamu, ewe uliyeangusha uongo ya sanamu.
Salamu, ewe bahari uliyemzamisha Farao;
Salamu, Mwamba unayowapa kinywaji wale wenye kiu ya uzima;
Salamu, Mwongozi na nguzo ya moto yenye kuwaongoza walio gizani;
Salamu, ewe boma la ulimwengu, pana zaidi kuliko mbingu.
Salamu, kikombe munamolindwa manna mkate wa mbinguni;
Salamu, mtumishi unayetayarisha furaha takatifu;
Salamu, Paradizo ya siri ya inchi ya ahadi;
Salamu, inchi yenye kubarikiwa vinayotaa asili na maziwa.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 12

Simeoni alipokuwa karibu kuondoka katika dunia hii ya udanganyifu, ukapewa kwake kama kitoto; Lakini akatambua katika wewe kuwa Mungu kamili, na alipostaajabia hekima yako, akapaza sauti na kusema*:*

Alliluia.

Elezo*: Kisha Waimbaji wanaimba Kontakion ya Mzazi-Mungu (mara mbili). Ni hii:*

Kwako jemadari kunilinda nina deni kukushukuru kwa wokovu na kushinda wangu mimi mji wako, ee Mzazi-Mungu. Tena kwa mamlaka yakosi kushindwa, na hatari kila namna niepuwe kukuimba, kwa kelele kuu*:* Salamu, Bibi Arusi, usiolewa.

Elezo*: Kisha Padri Mkubwa ao Msomaji moja watasoma Zaburi 50 (51) na Waimbaji wataimba Kanuni ya Mzazi-Mungu.*

KANUNI YA MZAZI-MUNGU

WIMBO 1. *Sauti ya ine.*

Kinywa changu kitafunguka, na kitajaa na Roho Mtakatifu*:* Natolea Shairi yangu kwa Mama wa Mfalme; na wataniona, katika hii siku kuu kubwa, nikiimba na furaha maajabu yake yote.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi Mungu, utuokoe.

Malaika mkuu Gabrieli akakutambua kama Kitabu cha hai cha Kristu chenye kutiliwa muhuri ya Roho Mtakatifu, na akakulalamikia, ee Bikira Safi*:* Salamu, chombo cha furaha humo munapotea laana ya Mama ya wenye hai.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi Mungu, utuokoe.

Salamu. Bibi Bikira wa Mungu, matumaini ya Adamu na ya ukombozi wake, woga wa Hadeze uliyoua, makao takatifu ya Mfalme wetu, Salamu, kiti cha moto cha Bwana Mwenyezi.

Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Salamu peke yako ulitoa ua halitafifia kamwe; Salamu, wewe uliyezaa tunda nzuri na manukato ya Mfalome wetu, Salamu, Bibi-Arusi usiolewa mwenye kuleta wokovu duniani.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Salamu, hazina ya usafi yenye kutuamusha humo tuliangukia; Salamu, ua mweupe ya ufalme ambayo manukato yanapakwa waaminifu, ubani wa harufi nzuri na manukato ya Samani kamili.

Elezo*: Waimbaji mbele ya kila wimbo wataendelesha kusema sawa vile walisema pa Ode wa kwanza. Ni kusema: Mtakatifu kamili. . . . Utukufu. . . . Sasa na siku zote. . . .*

WIMBO 3

Chunga kwa ulinzi wako, ee Mzazi-Mungu na Chemchem isiyokauka, waimbaji wote wenye kukutukuza kwa nyimbo zao, na katika utukufu wako kimungu uwape taji la washindaji.

Ulioteshe ngano ya mbinguni mu udongo wasipo kulima; Salamu, meza ya fumbo iliyochukua mkate wa uzima, Salamu, Bikira Malkia, Chemchem isiyokauka ya wimbi lenye kuleta uzima.

Salamu, maana ulizaa kwa ajili ya waaminifu sadaka yasipo kilema; Salamu, Mama wa Mwana kondoo anayeondoa zambi ya dunia yote; Salamu, majaliwa ya heri.

Salamu, alfajiri ya kwangaa ambaye peke yako ulichukua Kristu Jua letu. Salamu, hema ya Nuru iliyofukuza giza za mauti na kuondoa giza ya Hadeze.

Salamu, Mlango wa peke ambamo mulipita Neno peke yake. Bikira uliyevunja katika uzazi wako milango na makomeo ya Hadeze; Salamu, mlango kimungu wa taifa lililokombolewa. Bikira mstahili kamili wa nyimbo zetu.

Shemasi*:* Tena na tena kwa amani tumwaombe Bwana.

Waimbaji*:* Bwana hurumia.

Shemasi*:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

Waimbaji*:* Bwana hurumia.

Shemasi*:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa,...

Waimbaji*:* Kwako, ee Bwana.

Padri*:* Kwa kuwa wewe ni Mungu wetu, na kwako tunakutolea utukufu kwa baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Waimbaji*:* Amina.

Elezo*: Kisha Waimbaji wanaimba Kontakion ya Mzazi-Mungu (mara mbili). Ni hii:*

Kwako jemadari kunilinda nina deni kukushukuru kwa wokovu na kushinda wangu mimi mji wako, ee Mzazi-Mungu. Tena kwa mamlaka yakosi kushindwa, na hatari kila namna niepuwe kukuimba, kwa kelele kuu*:* Salamu, Bibi Arusi, usiolewa.

Elezo*: Kisha Padri ataimba Funfu wa tatu:*

FUNGU 3

I K O S 13

Mungu alifanya mpya kazi yake wakati alizaliwa mbele ya sisi viumbe vyake, akajifuma*:* Bila mbegu akachipuka tumboni takatifu, akailinda bila kuiharibu, ili sisi tukiona mwujiza huo, tuisifu tukisema kwa sauti kuu*:*

Salamu, ua lisiloharibika milele;
Salamu, taji ya utakatifu;
Salamu, nuru ya mfano wa ufufuo;
Salamu, peke yako mshindani wa Malaika na wa hali yao.
Salamu, mumea wa matunda bora, wenye kulisha waaminifu;
Salamu, mti wa kivuli na wa ubaridi, wa majani ya ulinzi;
Salamu, kwani ulizaa Mwongozi wa wenye kupotea;
Salamu, kwani kwa wafungwa unawapa Mwokozi.
Salamu, ewe Mwombezi wetu kwa Mwamzi wa haki na mwema;
Salamu, ewe mupatanishi wa wakosefu wengi;
Salamu, mavazi ya Wauchi;
Salamu, ewe moyo wa kushinda kila tamaa.
Salamu, Bibi-Arusi usiyeolewa.

I K O S 14

Tukiona kuzaliwa kwa namna kigeni, tujifanye wageni katika dunia hii, na kuweka mioyo yetu na akili zetu mbinguni, Ni kwa ajili yetu Mungu aliye-Juu akajionyesha duniani kama mtu munyenyekevu kamili, kwani alitaka kuvuta juu wale wote wanaomwimbia*:*

Alliluia.

I K O S 15

Aliyeko mbinguni, bila mageuzo ya fasi, wote hapa chini. Neno msiyeteseka, kwa sababu ya upendeleo wa Mungu, anakua Mwana wa Bikira tunayeshangilia hivi*:*

Salamu, ewe kiti cha Mungu kisichoweza kukaliwa;
Salamu, ewe mlango wa siri;
Salamu, ewe habari isiyosikika kwa waaminifu;
Salamu, tukufu bila shaka wa waaminifu.
Salamu, gari ya huyu anayekaa juu ya Wakheruvi.
Salamu, makao ya Mungu anayeketi juu ya Waserafi;
Salamu, kwani unavifanya vitu vyote kuwa vya mafaa;
Salamu maana katika wewe bikira amezaa.
Salamu, ewe mwenye kutuopoa ku mauti na kaburini;

Salamu, katika wewe Paradizo imefunguliwa tena;
Salamu, ewe funguo ya ufalme wa Kristu na ya mlango wa mbinguni;
Salamu, rala ya matumaini ya mema ya milele.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 16

Rabi. Malaika wote mbinguni walistaajabu kwa umwilisho wako, maana walimwona Mungu msiyekaribika karibu ya wanadamu, akizungumuza na watu na kupokea shangwe yao*:*
Alliluia.

I K O S 17

Wasemaji wa maneno mengi wamenyamaza bila sauti kama samaki sababu yako, ewe Mzazi-Mungu, hawajui kueleza namna ulipata mimba katika ubikira, lakini tunastaajabu fumbo yako na tunapaza sauti*:*
Salamu, ewe chombo cha hekima ya ajabu ya Mungu;
Salamu, ewe sanduku ya maongozi ya mbinguni;
Salamu, mbele yako wenye akili hawana maarifa hata moja;
Salamu, kwani wenye hekima hawana uwezo.
Salamu, kwani wanenaji wakubwa wamekuwa wapumbafu;
Salamu, kwani watungaji wa hadizi wanayumbayumba.
Salamu, kwani ulifumua matanzi ya Waathina;
Salamu, uliyejaza wavu wa Wavuvi wa watu.
Salamu, unayetukokota inje ya zimu ya ujinga.
Salamu, unayetupatia nuru ya hekima ya kweli;
Salamu, mashua yenye kutuokoa baharini kali;
Salamu, bandari ya amani ya wasafiri baharini wa hii uzima.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 18

Alipotaka kuokoa dunia Muumba wa ulimwengu alikuja kwa kutaka kwake; Mchungaji wetu alijifanya mtu kati yetu na kwa ajili ya wokovu wetu akaonekana kwetu kama Mwana-Kondoo wa Mungu; anaita kiumbe chake ku mfano wake na anatusikiliza tunajibu ku mwito wake*:*
Alliluia.
Elezo*: Kisha Waimbaji wanaimba Kontakion ya Mzazi-Mungu (mara mbili). Ni hii:*
Kwako jemadari kunilinda nina deni kukushukuru kwa wokovu....

Shemasi*:* Tena na tena kwa amani tumwaombe Bwana.
Waimbaji*:* Bwana hurumia.
Shemasi*:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.
Waimbaji*:* Bwana hurumia.
Shemasi*:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa,...
Waimbaji*:* Kwako, ee Bwana.
Padri*:* Kwa kuwa wewe ni Mungu wetu, na kwako tunakutolea utukufu, kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
Waimbaji*:* Amina.

KATHISMA *Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Ee Bikira Mtakatifu kamili, alipokuja katika muji wa Nazareti, mkubwa wa majeshi ya Malaika akakupasha habari ya Mfalme wa milele, ndiye Bwana, akakuambia*:* Salamu,

mbarikiwa, ee Maria, bahari isiyoweza kufumbuliwa huko msiyekaribika anakuja kufufua wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote *(mara ingine).*

Elezo*: Kisha tunaendela kuimba ma Ode nyingine ya Kanuni.*

WIMBO 4

Huyu mwenye kukaa na utukufu pa kiti cha umungu alikuja pa wimgu nyepesi*:* Ni Yesu. Mwokozi wetu kimungu; na kwa mkono wake safi Kamili aliokoa wale wenye kumwimbia*:* Ee Kristu Mungu wetu, utukufu ku uwezo wako,

Kwa myimbo zetu na kwa masauti yetu tunakupazia sauti na ibada. Bikira mstahili wa nuimbo zetu*:* Salamu, mlima wa ustawi wenye kunyanyuliwa na Roho Mtakatifu. Salamu, kinara cha zahabu na chombo ambamo maua inalindwa, uzuri wa waaminifu.

Mjaliwa ya ulimwengu, Salamu, Malkia usiye na doa, Salamu, mungazi wenye kutuongoza toka dunia mpaka ku wokovu. Salamu, Kilalo chenye kufufua waaminifu wote wenye kukutukuza na nyimbo zao.

Nguzo refu zaidi kuliko mbingu, Salamu, ee Bikira Safi, uliyechukua bila uchungu msingi wa ulimwengu tumboni mwako; Salamu, Shinikizo uliyetosha kwa damu yako nyekundu kimungu ya Mfalme Mwenyezi.

Ulizaa Mpana-Sheria wetu, Salamu, Malkia kweli, kwani anazima bure uhalifu wetu, Salamu, bahari isiyoweza kupimwa, ncha isiyokadirika. Bibi-Arusi usiyeolewa ambaye katika wewe tunakuwa miungu.

Kwa ajili ya ulimwengu ulisuka taji isiyofanyika na mkono wa mwanadamu; tunakuimbia na tunakulalamikia*:* Bikira Mtakatifu. Salamu, mlinzi wa ulimwengu, boma imara, ngome na kimbilio takatifu.

WIMBO 5

Ulimwengu umechukuliwa kwa utukufu wako kimungu, ee Bikira usiyeolewa, kwani ulichukua Mungu Mkuu tumboni mwako na ulizaa Mwana asiye wa wakati mwenye kuleta wokovu kwa wale wenye kuimba sifa yako.

Wewe uliyezaa njia ya uzima; Salamu, usiye na doa, kwani uliokoa ulimwengu ku garika na ku zambi, Salamu, mchumba takatifu uliyepokea Neno ya Mungu na woga, Salamu, makao ya Muumba na ya Bwana.

Salamu, siye na doa, ngome na boma la wanadamu, makao ya utukufu na woga wa Hadeze, nuru ya mabikira, furaha ya Malaika mbinguni, mlinzi wa waaminifu wenye kukuomba.

Gari la moto la neno Mtakatifu, Salamu, Malkia, Paradizo ya fumbo ambamo katikati Bwana anakuwa mti mpya wa uzima ambao utamu unakaa pahali pa uchungu wa mauti kwa ajili ya waaminifu wenye kuonja tunda lake lenye kuleta uzima.

Tunaposabitishwa kwa uwezo wako, tunakupazia Sauti na ibada*:* Salamu, mji wa Mfalme Mkuu; mwenye kusema juu yako anakutukuza na ustahilivu, Salamu, zimu isiyoweza kupimwa na mlima haramu.

Hema kubwa ya Neno la Mungu, Salamu, usiye na doa, kwani uliumba johari kimungu, Salamu, ajabu isiyosawanishwa; pamoja na Mungu unapatanisha wale wenye kukutangaza mwenye heri, ee Mzazi-Mungu.

WIMBO 6

Tunapotukuza hii siku Kuu kimungu na takatifu ya Mzazi-Mungu, njooni, enye waaminifu, tupigeni mikono, tukimutukuza Mungu aliyezaa.

Chumba cha arusi takatifu kamili cha Neno la Mungu, kisa ya umungu wetu, Salamu, ee Bikira Safi, utukufu wa Manabii waliokutukuza, pampo la Mitume, Salamu.

Ulikomesha umande uliyozimisha moto ya miungu ya uongo; tena tunakupazia sauti*:* Salamu, manyonya ya fumbo yenye kufunikwa na umanda ambayo Gideoni alitangulia kufikiri.

Kwa sisi wenye kukuimbia*:* Salamu, uwe bandari ya amani katikati ya mawimbi, kimbilio katika bahari ya mateso, makimbilio juu ya werevu wa Adui.

Kisa ya furaha yote, utupe hekima ya kukuimbia*:* Salamu, kichaka cha moto bila kuteketezwa, Salamu, wingi la nuru lenye kufuwanika waaminifu na kivuli chake cha milele.

Shemasi*:* Tena na tena kwa amani tumwaombe Bwana.
Waimbaji*:* Bwana hurumia.
Shemasi*:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.
Waimbaji*:* Bwana hurumia.
Shemasi*:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa,...
Waimbaji*:* Kwako, ee Bwana.
Padri*:* Kwa kuwa wewe ni Mfalme wa amani tena Mwokozi wa roho zetu na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
Waimbaji*:* Amina.

Elezo*: Kisha Waimbaji wanaimba Kontakion ya Mzazi-Mungu (mara mbili). Ni hii:*
Kwako jemadari kunilinda nina deni kukushukuru kwa wokovu...
Elezo*: Sasa Padri anasoma Fungu wa inne.*

FUNGU 4

I K O S 19

Bikira Mzazi-Mungu, boma ya mabikira, ulinzi wa wote wenye kukimbilia Kwako Mungu Muumba amekutengeneza sababu ya kukaa tumboni Mwako, na tunaimba kwa ajili yako*:*
Salamu, nguzo ya moyo safi na ya ubikira;
Salamu, mlango ya wokovu na ya ukombozi.
Salamu, mwanzo ya uumba wetu upya;
Salamu, mtume wa wema kimungu.
Salamu, unayewapa wenye zambi kuzaliwa kupya;
Salamu, mletaji nuru ku akili zetu;
Salamu, ewe uliyekanyanga nyoka muharibifu;
Salamu, ewe uliyezaa Mwana-Kondoo mpandaji wa usafi.
Salamu, Chumba-arusi bila mwungano;
Salamu, unayewaunganisha waaminifu na Mwana;

Salamu, mtunzaji mwema wa mabikira na wa vijana;
Salamu, mpambaji wa mioyo ku arusi ya Mwana-Kondoo.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 20

Bwana, wimbo wote ni zaifu wakati inajikaza kujisawanisha na wingi wa rehema zako; tutaweza kukuletea nyimbo nyingi kama mchanga wa bahari bila kuufikia ukamilisho wenye kustahili zawadi uliotufanyia pakuturuhusu kukuimbia*:*
Alliluia

I K O S 21

Kama taa yenye kwangaa katika giza. Bikira Mtakatifu anawakisha nuru ya kiroho sababu ya kutuongoza wote ku maarifa ya mbinguni; tutukuze mwangaza wake wenye kustahili zaidi nyimbo zetu*:*
Salamu, mwangaza wa Jua la wakristu;
Salamu, mwana wa Nuru ya milele;
Salamu, umeme wenye kuangaza mioyo yetu;
Salamu, mungurumo wenye kumuogopesha Adui.
Salamu, Mtume-mbebaji taa takatifu;
Salamu, pwani kunakoingia mto wa maji mengi;
Salamu, mfano takatifu na wa hai wa kisima cha maji ya ubatizo;
Salamu, kwani unaondoa alama ya zambi mioyoni mwetu.
Salamu, Bikira munamosafishwa zamiri yenyewe;
Salamu, kikombe chenye kutapanya furaha na uzima; ;
Salamu, manukato ya harufu nzuri ya kiroho; ;
Salamu, nuru ya hai ya Karamu ya mbinguni.
Salamu. Bibi-Arusi Usiyeolewa.

I K O S 22

Alipotaka kuwasamehe wenye deni wake wa zamani, huyu mwenye kuhurumia deni za wanadamu alikuja kwa kutaka kwake kuwaletea neema wale waliojitenga mbali; alipopasua hati ya deni zetu, akasikia watu wote wakimuimbia*:*
Alliluia.

I K O S 23

Tunaposifu uzazi wako, tunakutukuza ewe Mtakatifu Mzazi-Mungu, hekalu la hai alimokaa Bwana wa milele, na alipokutakasa na kukutukuza, akatufundisha wote tuimbe*:*
Salamu, hema takatifu ya Mungu-Neno;
Salamu, pahali takatifu kuu zaidi kuliko Patakatifu;
Salamu, sanduku iliopambwa kwa zahabu na Roho Mtakatifu;
Salamu, hazina ya uzima isiyomalizika.
Salamu, ewe taji heshimiwa ya Wafalme Wakristu;
Salamu, sifa ya kiroho ya Mapadri Watakatifu;
Salamu, ewe njia pana ya Eklezia isiyotikisika;
Salamu, ewe boma la Wakristu lisiloweza kuharibika.
Salamu, utukufu wa ushindi wetu;
Salamu, kwani katika wewe adui ameshindwa;
Salamu, ewe maponyesho ya mwili wangu;
Salamu, ewe wokovu wa roho yangu.
Salamu. Bibi-Arusi usiyeolewa.

I K O S 24

Ee Mama mstahili kamili wa nyimbo zetu, uliyezaa Neno Takatifu kuwapita watakatifu wote, pokea sasa heshima tunayokutolea, utuopoe ku mateso yo yote na linda ku azabu ijayo hawa wanaokuimbia na moyo mmoja*:*

Alliluia.

Elezo*: Kama ni Shemasi mu Kanisa yeye atasoma hii Ikos wa kwanza. Kama hakuna ataisoma padri.*

I K O S 1

Alitumwa toka mbinguni Malaika Mkuu kumwambia Mzazi-Mungu*:* Salamu. Yeye alipokuona wewe, ee Bwana, ukipata mwili mara ileile kwa sauti yake ya bila-mwili, alistaajabu, akasimama na akasema na sauti kubwa.

Salamu, kwa kuwa unaangaza wokovu wetu.

Salamu, kwa kuwa katika wewe uovu uliondolewa.

Salamu, uliyemusimamisha tena Adamu aliyeanguka.

Salamu, uliyemwoka Eva halii tena.

Salamu, ndiwe mlima kutofikika kwa mawazo ya wanadamu;

Salamu, ndiwe bahari isiyoweza kufumbuliwa hata kwa macho ya Malaika.

Salamu, kwa kuwa wewe ni kiti cha ezi na makao ya Mfalme.

Salamu, kwa kuwa unamubeba Muumba wako.

Salamu, ndiwe nyota iliyoonyesha Jua, Salamu, ndiwe tumbo Mungu alimojifanya mtu.

Salamu, kwani katika wewe kiumbe kinapata upya;

Salamu, kwani kwako Muumba anakuwa mtoto.

Salamu, Bibi-Arusi usiyeolewa.

Elezo*: Kisha Waimbaji wanaimba Kontakion ya Mzazi-Mungu (mara mbili). Ni hii:*

KONTAKION

Kwako jemadari kunilinda nina deni kukushukuru kwa wokovu...

SINAKSARI

Msomaji sasa atasoma Sinaksari ya Watakatifu ya hii siku ya leo na kisha atasoma hii:

Hii siku ya leo Posho asubui ya Juma wa tano ya Kwarezima tunashangilia Wimbo Akathiste ya Mzazi-Mungu Malkia wetu na Bikira daima Maria.

Kwa maombezi ya Mzazi Wako, ee Kristu Mungu wetu utuchunge ku kila mateso na sikitiko kama mmoja mupenda wanadamu.

Elezo*: Kisha Waimbaji wataimba Ode wa saba.*

WIMBO 7

Hawakuabudu kiumbe pahali pa Muumba, waaminifu wa Mungu Aliye-Juu, lakini wakapambana kwa furaha na moto uliyowatisha; na wakaimba katika tanuru ya moto*:* Utukuzwe, ee Bwana mwenye kustahili Sifa. Mungu wa Baba zetu.

Tunakuimbia na tunakupazia sauti*:* Salamu, gari la Jua la roho, ndiwe, kweli mzabibu uliyotoa zabibu tamu ambayo divai inafurahisha waaminifu wenye kukutukuza.

Ulizaa huyu mwenye kuponyesha kidonda yote. Salamu, mchumba wa Mungu, tawi la fumbo uliyechanukisha umilele; Salamu, ee Malkia mwenye kutujaza na furaha na mwenye kutufanya wariti wa uzima.

Ulimi wa wasemaji unahangaishwa kwa kukutukuza, ewe Mzazi-Mungu; uliinuka juu zaidi kuwapita waserafi ulipomza Kristu Mfalme wetu; umuombe ili awaokoe ku hatari yote waaminifu wenye kusujadu mbele yako.

Mipaka ya dunia inakutangaza mwenye heri na inaimba na mapendo*:* Salamu, Kitabu takatifu humo kidole cha Baba iliandika Neno ambaye tunakuomba umusihi ili awaandike watumishi wako ku kitabu cha uzima.

Sisi watumishi wako tunakusihi na tunainamisha mioyo yetu mbeele yako*:* Inamisha sikio lako kwa sisi na utuokoe ku zimu ya vishawishi; kinga taifa lako ku mishale ya Adui, ewe Mtakatifu Mzazi-Mungu.

WIMBO 8

Vijana walikombolewa ku tanuru ya moto na huyu aliyezaliwa kwa Mzazi-Mungu; hii zamani ilikuwa ni mfano sasa inakuwa kweli, kwani anakusanya ulimwengu wote wenye kwendelea kuimba*:* Enye wote, viumbe vya Bwana, tukuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa mbele.

Ulimupokea Neno tumboni mwako, ulichukua huyu anayachukua dunia mkononi mwake, ulilisha na maziwa Yako huyu mwenye kulisha na alama moja ulimwengu wote; tena tutaimba kwa ajili yake*:* Enyi wote, viumbe vya Bwana, tukuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Musa alitambua katika kichaka cha moto fumbo kubwa ya uzazi wako; Vijana walitangulia kuuona wazi kabisa wakati waliposimama katikati ya moto bila kuteketezwa; Bikira Mtakatifu na usiye na do, tunaimba sifa yako ya milele.

Zamani tulipotwaliwa kwa werevu wa nyoka, tulipata vazi la umilele katika uzazi wako, sisi ambao zamani tulikaa katika giza ya zambi tuliona Nuru ikikaa tumbon*i* mwako; ee Bikira, hema ya nuru, tutaimba sifa yako milele.

Kwa ajili ya ulimwengu ulizaa Mwokozi mwenye kutuchukua toka dunia mpaka mbinguni; Salamu, ewe Mbarikiwa kamili, nguvu na ulinzi, ngome na boma ya wale wenye kuimba pamoja nawe*:* Enyi wote, viumbe vya Bwana, tukuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

KATAVASIA*:*

Wimbo ya kwanza.

Nitafungua kinywa changu, na kitajazwa Roho, nikatoa maneno kwa Malkia Mama, nikaonyesha, kushangilia na furaha, nikayaimbia miujiza yake na furaha.

Wimbo ya tatu.

Ee Mzazi-Mungu, uliye chemchem ya uhai na kujaa tele, usifu wao waliochanganya kwa mchango wa Roho, uwape mkazo; tena kuwastahilisha kuona taji tukufu kwa utukufu wako wa kimungu.

Wimbo ya ine.

Mapenzi yako ya kimungu, yalio si kuchungwa, ili kupata mwili na Bikira, ewe uliye juu pia, akimwangazia yule nabii Abakuki, alipaza sauti na kusema*:* utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya tano.

Ulimwengu ulistaajabu na utukufu wako wa kimungu; kwa kuwa wewe, ee Bikira usiyolewa, ulimshika mimba yeye, aliye Mungu wa wote, tena ulimzaa aliye Mwana bila mwanzo, ili kuwapa wasifu wako wote, kipaji cha wokovu.

Wimbo ya sita.

Sisi tunaofikiri kimungu, ikiwa tunaazimisha siku Kuu hii ya Mama-Mungu, iliyo kimungu na ya samani kamili, njoni tuyapigie mikono tukimtukuza Mungu aliyezaliwa naye.

Wimbo ya saba.

Waliofikiri kimungu hawakuabudu umbo, ila Muumba, bali waliukanyanga, hodari ogofyo ya moto, wakishangilia waliimba*:* Ewe Mungu na Bwana wa mababu zetu, uliye msifiwa bila kiasi, uhimidiwe U.

Wimbo ya mnane.

Tunamsifu, tunamuhimidi, tunamusujudu Bwana.

Vijana wa tabia njema tanuruni, mzao wa Mzazi-Mungu aliwaokoa, mfananishwapo, tena sasa mtimilizwapo, anakusanya ulimwengu wote ukiimba*:* Enyi viumbe msifuni Bwana, na kumtukuza milele na milele.

Elezo*: Hatuimbe:* «Uliye watamani. . . » *lakini tunaimba Ode wa tisa.*

Mbele ya kila wimbo tunasema: Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

WIMBO 9

Kila mwana wa dunia afurahiwe rohoni, achukuwe taa yake yenye kuwaka, Malaika mbinguni washangilie na furaha Siku kuu Takatifu ya Mzazi-Mungu na wamuimbie*:* Salamu, ee mwenye heri na Bikira daima. Mtakatifu Mzazi-Mungu.

Ili tukuimbie*:* Salamu, sisi waaminifu tunaokuwa washariki wa furaha yako, utuokoe ku majaribu yasipo mwisho, ku minyororo ya Adui na ku mateso mengine yote yenyi kututisha sababu ya wingi wa zambi zetu.

Ndiwe matumaini yetu na nuru yetu, tena tunakulalamikia*:* Salamu, nyota yasipo mwisho uliyeingiza Jua letu ulimwenguni; Salamu, Bikira usiye na doa, kwani umetufungulia Edeni iliyofungwa mpaka ku inchi yao ya mbinguni.

Tusimame na woga katika nyumba ya Mungu na tuseme*:* Salamu, Malkia wa ndunia, salamu, Maria, Mama wa sisi wote, Salamu, ewe mzuri kamili na usiye doa kamili hombo cha manemane uliyepokea mpako usiyokwisha uliyomwangwa pa wewe.

Njiwa Bikira daima. Salamu, uliyezaa Mungu wa wema. Salamu, utukufu wa Wakakatifu wote na taji ya Mashahidi, pambo la wenye haki na wokovu wa roho zetu sisi wote.

Bwana, samehe uriti wako, ukifunga macho pa zambi zetu zote, pokea vema ombi la huyu aliyekuchukua duniani, ee Kristu, wakati katika mapendo yako kubwa ulikubali kuvaa hali ya wanadamu.

Wimbo ya tisa.

Mwana wowote wa dunia furahi rohoni, akishikataa yake, yenyi kuwaka Malaika mbinguni. Watukuze wa furahi siku Kuu Takatifu ya Mzazi-Mungu na wamuimbie salamu, ee mwenye heri na Bikira daima Mtakatifu Mzazi-Mungu.

EKSAPOSTILARION

Sauti ya mbili. Ginekes akutistite

Leo fumbo ya milele imefunuliwa: Kwa mapendo yake kwa ajili yetu Mwana na Neno la Mungu amekuwa wa Bikira Maria, Malaika Gabrieli anatangaza habari njema ya furaha; na sisi wote tuseme pamoja naye: Salamu, Mama Mtakatifu wa Bwana.

MASIFU

Sauti ya ine. Os geneon en martisin.

Fumbo ya siri kabisa hata Malaika wenye hawakujua inapewa kwa Malaika Gabrieli; sasa anajongea kwako, wewe njiwa safi kamili na wa uzuri wote wenyi kuwafanya wapya wanadamu, na anakupazia sauti, ewe Mtakatifu kamili*:* Salamu, ujitayarishe kupokea tumboni mwako kwa neno langu Neno wa Mungu*. (mara ingine).*

Nyumba ya nuru imetayarishwa juu yako, ee Bwana*:* Ni tumbo la Bikira Safi kamili; unashuka juu ya kukaa humo kwa mapendo yako kwa ajili yetu sababu ya kutuondoa ku utumwa wa mauti na kutengeneza uzuri yetu ya zamani, kwa kuja kwako unatuletea wokovu na amani.

Malaika Gabrieli anashuka kwako waziwazi na anakuambia, ee Bikira Safi kamili*:* Salamu, kwani unakomboa laana ya zamani, salamu, wewe kuinuka kwa watu wenyi kuanguka, salamu, wewe kondoo mchanguliwa, peke yako mwenyi kumupendeza Mungu, salamu, wewe kiti cha siri cha Jua, pokea wa milele mwenyi kutaka kukaa tumboni mwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya ine. Idiomelon.*

Mzazi-Mungu alisikia luga ya kigeni waakti Malaika alisema maneno ya habari njema*:* ndio maana nii kwa imani alipokea salamu na kupata mimba ya Mungu wa mbele ya nyakati; na sisi pia tunakulalamikia kwa furaha*:* Ee Mungu uliyejifanya mutu bila kugeuka, leta amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Elezo*: Ndani ya Ibada ya Liturgia takatifu tunasoma APOSTOLOS na EVANGELION ya Mzazi-Mungu.*

JUMA YA TANO YA KWAREZIMA
MAKUMBUSHO YA MTAKATIFU MUTAWA MWANAMUKE MARIA WA MISRI

MUPOSHO MANGARIBI

Elezo*: Kisha Zaburi ya Proimiakos tunaimba: «Bwana nimekuita. . . ». Kisha tunaimba wimbo kumi: Sita kwa Ufufuo wa Kristu na wimbo inne ya Mtakatifu Maria wa Misri.*

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Kwa mawazo ya umungu ulijitenga na uzito wa tamaa, kisha uligeuza mawazo na matendo yako ku mema kubwa; unapotazama sura ya Bikira Mtakatifu kamili na sasa unapoacha zambi yote; uliabudu na matumaini Musalaba heshimiwa. *(mara ingine).*

Kwa furaha ulienda kuangalia Mahali patakatifu, ulikusanya fazila katika njia ya wokovu; mbiombio ulitenda katika njia ya utakatifu; ulivuka mtoni wa Yordani na ulikaa katika jangwa ya Mbatizaji; ulishinda mwili, ulifukuza hali mbaya ya tamaa, ee Mama mtukufu, kwa uzima yako takatifu.

Ulipokaa jangwani ulitenga mbali rohoni mwako tamaa sababu ya kuwekamo sura ya Mungu kwa nuru ya fazila; uliangaa na nuru hata ukatembea polepole juu ya maji, kwa sala yako uliondolewa duniani mpaka kwa Mungu; ee Maria mwenyi heri, sasa umuombe Kristu kwa deni uliyo naye kwake, kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mbili.*

Uwezo wa Msalaba wako ilifanya maajabu, ee Bwana, hata kahaba wa zamani akaingia katika mashindano ya uzima ya utawa; japo uzaifu wake alishindana na shetani kwa ushujaa, na kwa ushindi wake alipopokea mshaha, anaombea roho zetu kwako.

Sasa na siku zote. . . *(Wimbo ya Mzazi-Mungu kwa Ufufuo wa Kristu na sauti ya hii Juma).*

APOSTIKHA YA UFUFUO

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mbili. Idiomelon.*

Tamaa za roho na za mwili ulizikata na upanga wa kiasi; mawazo mbaya uliyasonga kwa ukimya ya uzima wa utawa, kwa machozi yako ulimwangia jangwa maji na ulipata matunda ya toba; ee Mama mtukufu, tunashangilia makumbusho yako ya usafi.

Sasa na siku zote. . . *Sauti umoja*

Muujiza mupya kupita miujiza yote ya zamani! Kwani ni nani alijuwa mama kuzaa, pasipo bwana, na kuchukuwa mikononi mwake, Yule anayekumbatia kiumbe chote? Uzazi huu ni mapenzi ya Mungu; kwa sababu ulimuchukua mu mikono yako, sawa mtoto, ewe Bikira msiyedoa, na ya kama mbele yake uko na hakika ya mama-mzazi; usihii bila kuacha, kwa ajili ya wale wanaokuheshimu, ahurumie na aokoe roho zetu.

Elezo*: Kisha Trisayo tunaimba Apolitikion ya Ufufuo wa Kristu. Kisha:*

Tropari ya Mtakatifu Mama Maria. *Sauti ya mnane.*

Katika wewe Mama, sura ya umungu ilionekana kabisa, kwa kufanana nayo ulichukua msalaba wako na ulimufwata Kristu; na kwa uzima wako ulifundisha kuzarau mwili, kwa sababu ni ya kupotea, kwa kushurulika na roho isiyokufa hata milele; ni hivi roho yako inafurahiwa, ewe Mutawa Maria, pamoja na Malaika.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION YA UFUFUO**

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

SIKU YA MUNGU YA JUMA YA TANO

Tunafata desturi ya hii siku ya Mungu. Kisha tunaimba wimbo ya Kanuni ya Triodi na ya Mtakatifu Maria wa Misri.

KANUNI YA TRIODI

Sauti ya mnane. Igran diodefsas

Wimbo wa kwanza

Nilipofanana na mtajiri ambaye kila siku alifurahi kwa furaha nyingi, nakuomba, ee Mwokozi, uniokoe kama Lazaro ku moto ya milele.

Ee Mwokozi, japo furaha nilivaa kama mtajiri mwenyi kujipamba na nguo nyekundu, na nguo za hariri, na nguo za zahabu, usinitupe katika moto kama yeye.

Katika hii dunia yenyi kupita na kutoweka mtajiri aliishi na uzima nzuri na ya furaha; ndio maana alihukumiwa kuteswa, lakini maskini Lazaro alitulizwa kwa umande.

THEOTOKION

Malaika na wanadamu wanakuimbia daima, ee Mama usiyeolewa*:* Kwani ulibeba mikononi mwako kama mtoto huyu aliye Muumba wa ulimwengu.

KANUNI YA MT. MARIA.

Sauti ya sita. Kimati Thalasis.

Natukuza na mapendo makumbusho yako takatifu na ya nuru*:* Tuma nuru rohoni mwangu, ewe Mtukufu mwenyi kusimama karibu ya Kristu Nuru yetu ya milele, na uniokoe ku vishawishi vya hii uzima.

Huyu alikaa katika Misri wakati alikua mtoto mchanga, huyu dunia haiwezi kuzungusha, ni yeye Bwana mwenyi kujua yote kama nyota ilivyokufunulia tangu Misri ya nuru.

Ulipokosa kujua mafundisho takatifu, ulichafua sura ya Mungu; lakini, uliporudi wepesi, uliitakasa mbio kwa matendo yako takatifu, ee Mama mtukufu mwenyi kustahili nyimbo zetu.

THEOTOKION

Mapendo yako ni kubwa kwa ajili yetu, mapendo yako ni isiyokadirika, ee Mungu wangu! Kwa kahaba wa zamani ulimupa afanane na Malaika kwa usafi kwa ajili ya maombezi ya Mama yako Mtakatifu kamili.

Wimbo ya tatu.

Sauti ya mnane. Si i to stereoma.

Kwa Lazaro ulimuondoa mu moto*:* ee Kristu, uniondoe mu Gehena mimi pia mtumishi wako nisiyestahili.

Mimi ni mtajiri wa tamaa na wa furaha za dunia, lakini maskini kwa kukosa fazila*:* Kama Lazaro, ee Bwana, uniokoe.

Nguo nyekundu na hariri mtajiri alivaa ni mfano wa furaha na zambi*:* Ni kwa sababu ya hii anaungua katika moto.

THEOTOKION

Bikira Mtakatifu kamili, kwa maombezi yako kuja utusaidie kwa kutuondolea hatari zenyi kutuzunguka.

Sauti ya sita. Se ton epi idaton.

Kwa zambi ulifika karibu ya milango ya upotevu, lakini huyu ambayo kwa nguvu ya umungu wake amekwisha kuvunja milango ya Hadeze alikufungulia ya toba, yeye aliye Mlango ya Uzima.

Ee Bwana mvumilivu, zamani huyu alikuwa chombo cha uovu, kwa kuabudu Msalaba wako takatifu, ulimuondoa ku matendo ya uwongo ya shetani.

Huyu alimwanga damu yake zamani kwa maondoleo ya zambi yote na mwenyi kuwapa wanadamu uzima kwa machozi yako mengi alikutakasa wewe wote ku ukoma mbaya wa zambi zako.

THEOTOKION

Ee Bikira Neno hata moja hailiwezi kusema fumbo yako ya umungu; kwani Neno wa Baba alikaa tumboni mwako, kwa neno lake anawapa waovu maondoleo ya zambi.

KATHISMA

Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.

Kwa utawa ulizuia vishindo vyote vya mwili na ulionyesha roho yako nguvu na imara; ulitamainia kuona Msalaba wa Bwana, kwa dunia yenyi kusulubiwa wewe ni mwenyi heri milele, ulifananisha uzima wako na ule wa Malaika. Kwa hivi tunatukuza, ewe Maria, makubusho wako katika imani kwa kuomba maondoleo ya zambi zetu na maombi nyingi wako.

Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. **THEOTOKION**. *Umoja.*

Nimezama katika matope ya zambi, nguvu imenikosa; makosa yangu mengi yamenizamisha, lakini wewe uliyezaa Neno, peke yako rafiki yetu, nakuomba, tazama mtumishi wako; uniokoe ku zambi, ku mateso ya lufu na ku hasara yote ya adui yangu ili nikuimbie na furaha, ee Bibi yetu*:* Umuombe Kristu Mungu wetu aniondolee zambi zangu, kwani mimi ni mtumishi wako na wewe ni matumaini yangu.

KONTAKION

Sauti ya tatu. I Parthenos simeron.

Huyu ambaye ya kwanza alijitoa ku uovu na ku tamaa, kwa toba amekua leo bibi arusi wa Kristu, mshindani wa malaika kwa uzima yake, muharibifu wa mashetani kwa silaha za Msalaba; na ndio maana, ee Maria, ulionekana kuwa bibi-arusi mtukufu katika ufalme wa mbinguni.

IKOS

Kwa nyimbo zetu tunakutukuza sasa, ee Mwana-Kondoo jike na binti wa Kristu, ee Maria mtukufu, wewe ambaye ya kwanza ulionekana kama chipukizi la Wamisri, umekuwa na heshimiwa la Eklezya, unazoea katika kiasi na sala yulu ya kipimo cha wanadamu; ndio maana ulitukuzwa katika Kristu kwa haki za uzima yako na matendo yako na ulionekana, ee Maria, kuwa bibi-arusi mtukufu katika ufalme wa mbinguni.

SYNAKSARION

Leo, siku ya Mungu ya tano ya kufunga, tunafanya makumbusho ya mama wetu mtukufu Maria mu Misri.

Ilipojitenga na roho yake, mwili ulikufa; udongo, funika sasa mwili wa Maria.

Kwa maombi yake, ee Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

EKSAPOSTILARION

Sauti ya tatu. Ton Uranon tis astris.

Katika wewe tuna mfano wa toba*:* Ee Maria Mtakatifu, umuombe Kristu ili kwa hii waakti ya Kwarezima tupewe kukuimbia na mapendo na imani.

THEOTOKION. *Umoja.*

E furaha ya Malaika, mfariji wa wenyi kuteswa, mlinzi wa wakristu, Bikira Mzazi-Mungu, uniopoe toka mateso ya milele na uniokoe.

MASIFU

Elezo*: Tunaimba wimbo ya Ufufuo ya Kristu ku Kitabu ya Paraklitiki.*

Utukufu kwa Baba*. . . Sauti ya kwanza. Idiomelon.*

Ufalme wa Mungu hauko katika kunywa na kula, lakini ni haki na utakaitfu; ndio maana watajiri hawataingiamo, ila wawape maskini mali zao; kwani nabii Daudi anaifundisha akisema*:* «Mwneyi haki ana huruma kila siku na anawema furaha yako katika amri ya Bwana, anatembea katika nuru, hatua zake hazisite». Yote hii imeandikwa juu ya kutufundisha kusudi tuunganisha matendo ku Kwarezima; na Bwana kwa mema ya dunia atatupa mali ya mbinguni.

Sasa na siku zote*. . .*

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA MKUBWA

SIKU YA MUNGU WA TANO KWA MANGARIBI

Elezo*: Kisha Zaburi 103 (104) nikusema Proimiakos, tunaimba: «Bwana nimekuita. . » na wimbo kumi, nikusema: Wimbo wa inne na sauti ya hii Juma ku mwisho ya hii Kitabu, wimbo tatu ya Triodio na wa tatu ya Mineon.*

Wimbo ya Triodi

Sauti ya kwanza. Panefimi Martires.

Ee Kristu, wewe ulikuwa mtajiri umekuwa maskini sababu ya kutajirisha wanadamu na mali ya nuru yako ya milele; mimi niliyejifanya maskini sababu ya furaha ya hii uzima unipe fazila nyingi, uniweke pamoja na maskini Lazaro, uniondoe ku azabu ya mtajiri na ku gehena inastahili mateso yangu.

Nilikusanya mali katika mapambo na uovu; nilifurahi na furaha za hii uzima, nitateswa na moto ya gehena; roho yangu inajua umaskini ya Lazaro, nimeachwa mbele ya mlango ya matendo mema*:* Ee Bwana, unisamehe mimi mwenyi mateso.

Enyi waaminifu, tunapoanza na moja Juma ya Sita ya Kwarezima takatifu, tumuimbie Bwana wimbo wa sifa kwa ajili ya Siku kuu yenyi kutangulia Matawi, kwani anakuja katika utukufu na uwezo wa umungu wake, anaenda Yerusalema sababu ya kuharibu mauti, tutayarisheni basi alama za ushindi, matawi ya fazila zetu sababu ya kulalamika Hosanna kwa Muumba wa ulimwengu.

Wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba*. . .* Sasa na siku zote*. . .* **THEOTOKION**

KUINGIA.

Mwanagaza upole (ilaron). . .

PROKIMENON KUBWA

Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

Shairi: 1)Toka mwisho wa dunia nitakuita.
Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

*Shairi:*2) Umenipa uriti wao wanaoogopa jina lako, ee Bwana.

APOSTIKHA.

Sauti ya kwanza. Idiomelon.

Ya ajabu ni matengeneo ya wema wa Mwakozi kwa ajili yetu; anajua mambo itakayokuja ao ya sasa, anatuonyesha uzima ya Lazare na ya Mtajiri, tukiona mwisho ya kila mumoja tutaepuka upendeleo na ugumu wa huyu, wa mwisho tutafananisha nguvu na uvumilivu ya wa kwanza sababu ya kuweza kulalamika pamoja naye katika kifua cha Abrahamu*:* Ee Bwana na Mwamzi wa haki, utukufu kwako.

Kituo: Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama macho ya watumishi yanaangalia kwa mkono wa Bwana kama macho ya kijakazi kwa mkono wa bibi yake, hivyo macho yetu yanavyoangalia kwa Bwana Mungu wetu hata akatuhurumia.
(Mara ingine wimbo wa juu)

Kituo: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa. Nafsi yetu inayala na kuzarauliwa kwa wenye kuikala na salama tena na kuzarau kwa wenye kiburi.

Ee Mungu wa mapendo, kwa maombezi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, utupe amani na utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote.

Furaha ya Msalaba mbinguni, mulinzi wa wanadamu duniani, ee Bikira Safi kamili, utuokoe sisi wenyi kukukimbilia wewe, kwani kisha Mungu matumaini yetu ni kwako, ee Mzazi-Mungu.

Padri*:* Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.
Msomaji*:* Trisayo. *Na tunaendelea desturi katika hii wakati ya Kwarezima.*

MU KAZI MOJA ASUBUI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.

Ee Bwana, sukuma mbali yangu jiwe la moyo wangu mgumu, kwa wema wako amsha roho yangu yenyi kuuawa kwa tamaa na uistahilishe kukuletea kwa toba, kama Mshindi wa Hadeze, matawi ya fazila ili ni uzima wa milele na niimbie uwezo wako na mapendo yako, peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. Umoja.

Muujiza wa ajabu, ee Mjaliwa neema, kiumbe kilishangilia na furaha pakukuona, bila mbegu ukupata mimba na ukamzaa namna isiyokadirika huyu ambaye Malaika mwenyewe hawawezi kutazama, ee Bikira Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

KATHISMA YA TATU.

Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.

Tunapoingia katika Juma ya sita ya Kwarezima Takatifu, tumuimbie Kristu anayekuja kwa ajili yetu mwenyi kukaa juu ya punda jike wimbo wa Siku Kuu mbele ya Matawi; kwa sababu anajongea kama Mfalme sababu ya kutiisha mataifa kwa Baba yake; tumutayarishieni matawi ya fazila zetu kusudi tuone pia na furaha Ufufuo wake tukufu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Umoja.*

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulibeba mikononi mwako Muumba aliyejifanya mtu sababu ya kutuokoa; hii mikono takatifu uinue sababu ya kuomba atuondolee vishawishi na hatari; na sisi wenyi kukushangilia wewe tunakuimbia na mapendo*:* Utukufu kwa huyu alikaa ndani yako, utukufu kwa huyu alitoka kwako, utukufu kwa huyu alizaliwa kwako sababu ya kutuokoa.

KANUNI

Kanuni ya Tiodi

Wimbo wa kwanza. *Sauti ya kwanza.* Odin epinikion.

Kwa kufunga turegeze mateso yetu kwa matendo yetu takatifu tulete uzima ku roho yetu ili kwa moyo wenyi kutakaswa tuweze kuona maateso ya kristu.

Nilifananisha tabia mtajiri asiye na huruma; ee Bwana mwenye huruma, nakuomba lakini uniweke pamoja na maskini Lazaro kusudi niepuke moto ya milele.

Nilikataa tendo lolote nzuri, nilifurahia makosa yangu mpaka kushinda; sasa, ee Bwana, niko na njaa ya wokovu wake, unizibishe na chakula chako takatifu.

THEOTOKION.

Mimi nimehukumiwa, uniokoe ku matendo yangu ya uovu; wewe ulizaa Mungu mwenyi huruma, ee Bibi yetu, unihurumie.

Kanuni ingine ya Triodi. *Sauti ya kwanza.* To voithisanti Theo.

Enyi waaminifu, kwa furaha tangu leo tutangulieni Siku Kuu ya Matawi kusudi tupewe kuona Mateso ya Bwana yenyi kuleta uzima.

Kristu anaenda ku Yerusalema kama Mfalme, anapanda juu ya punda jike, kwani anataka kutiisha mataifa kwa Mungu na chini ya hekima yake.

Utukufu kwa Baba. . .

Umoja wa watu katika umungu moja, Mungu na Baba asiyezaliwa, Mwana wa pekee na Roho Mtakaitfu, ufalme wa asili moja, utuokoe.

Sasa na siku zote. . .**THEOTOKION**

Fasi yote wanasema juu ya utukufu wako, maana ulizaa mwilini Muumba wa ulimwengu, ee Mzazi-Mungu na Bikira maria, wewe mwenyi kustahili nyimbo zetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Tazama Kristu katika muji wa Bethfaje; salamu, Bethani, inchi ya Lazaro, kwani atakuonyesha muujiza wa ajabu kwa kufufua Lazaro katika wafu.

IRMOS*:* Tumuimbie Mungu wetu wimbo wa ushindi yeye aliye kumusaidia Musa juu ya Wamisri; katika Yeye majeshi ya Farao yaliangamizwa, kwani amevaa utukufu.

Fotagogikon na sauti ya hii Juma na kisha tunaimba Apostikha

APOSTIKHA

Sauti ya tano. Idiomelon

Ee Kristu, usinihukumu ku gehena ya moto kama yule mtajiri hakuhumia Lazaro; lakini ukisikiliza ombi ninalokutolea kwa machozi, kwa mapendo yako unipe tone la maji, ee Mungu wa mapendo na Bwana mwenyi huruma. *(mara mbili).*

Yatukuzwe majeshi ya Mfalme wa mbinguni kwa sababu walipozaliwa duniani Mashahidi washindi hawakutamainia cheo cha malaika*:* Walipozarau mwili na kuteswa, walistahili utukufu wa Malaika; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Umoja.*

Ee Mjaliwa neema, utuombee, ombea roho zetu rehema nyingi ya Mungu na maomdoleo ya zambi zetu nyingi.

MU KAZI MOJA MAGARIBI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Kisha «*Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo tatu ya hii Kitabu na wimbo tatu ya Mineon.*

Sauti ya sita. Olin apothemeni.

Mimi ni maskini! Roho yangu inaregea sababu ya zambi nyingi, kwa furaha ya hii uzima; nalala katika uzaifu yangu na nakulalamikia, ee Bwana mwenye huruma*:* Kuja, unitazame, kwa mapendo yako unipe nguvu, usiniache, kusudi nisianguke katika usingizi wa mauti na Adui asifurahiwe kupotea kwangu, ee Bwana, yeye mwenyi kutafuta kunikokota katika zimu ya Hadeze.

Kwa upumbafu wangu nilifananisha mtajiri asiye na huruma, nilipata furaha na nilizama katika tamaa; nilipoona roho yangu kama Lazaro mwenyi kulala mbele ya milango ya toba, nilipita pembeni bila huruma wakatipo ilikuwa na ugonjwa, ilikuwa na njaa, yenyi kujeruhiwa kwa tamaa; ndio maana ninateswa katika gehena ya moto, lakini uniokoe, peke yako Bwana mwenye huruma.

Sauti ya tano. Kirie epi Moiseos.

Ee Bwana, unapotembea ngambo ya Yordani, unaeleza ya kwamba magonjwa ya Lazaro haiongoze ku mauti, lakini itasaidia ku utukufu wako, ee Mungu wetu; Utukufu kwa uwezo wako wa milele, maana unaharibu mauti kwa wema wako kubwa, ee Mpenda-wanadamu.

Wimbo ya Mineon tatu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 106.

Mushukuru Bwana; kwa kuwa yeye ni mwema*:* Kwa maana rehema yake ni ya milele.

Shairi*:* Wakombolewa wa Bwana wasaeme hivi.

Somo ya Mwanzo tutasoma (27, 1-41)

Na ilikuwa wakati Isaka alipokuwa muzee, na macho yake yamepo-fuka, akaita mwana wake muzaliwa wa kwanza, akamwambia*:* Mwana wangu; naye alimwambia*:* Mimi ni hapa. Akasema*:* Tazama sasa, mimi ni muzee, sijui siku ya kufa kwangu. Basi sasa twaa, ninakuomba,

silaha zako, podo yako na upinde wako, na toka kwenda polini, uniwindie mawindo;
unifanyie muchuzi namna ninayopenda, na kuuleta kwangu nipate kula; nafsi yangu ikubariki mbele ya kufa kwangu. Rebeka akasikia wakåti Isaka alipo-kuwa akisema na Esau, mwana wake. Esau akakwenda polini kuwinda ma-windo na kuyaleta. Rebeka akamwambia Yakobo, mwana wake akisema*:* Tazama, nimesikia baba yako akisema na Esau, ndugu yako akisema*:* Uniletee mawindo uni-fanyie muchuzi nipate kula, na kukubariki mbele ya Bwana mbele ya kufa
kwangu. Basi sasa, mwana wangu, tii sauti yangu kwa yale ninayokuamuru. Kwenda sasa kwa kundi uniIetee wana-mbuzi wawili walio wema; na nita-fanyia baba yako muchuzi nao, namna anayopenda; nawe utauleta kwa baba yako apate kula na kukubariki mbele ya kufa kwake, Yakobo akamwambia Rebeka, mama yake*:* Tazama, Esau ndugu yangu ni mwenye nyole nyingi, na mimi ni mutu laini, Labda baba yangu atanigusa, na nitaonekana kwake kama mudanganyi ; na nitaleta laana juu yangu wala si baraka. Mama yake akamwambia*:* Laana yako iwe juu yangu, mwana wangu, tii tu sauti yangu na kwenda kuwatwaa. Akakwenda, akatwaa, akawaleta kwa mama yake ; mama yake akafanya nao muchuzi namna baba yake aliyoupen. da. Rebeka akatwaa mavazi mazuri ya Esau, mwana wake mukubwa, yaliyokuwa pamoja naye nyumbani, akavalisha Yakobo mwana wake mudogo nayo. Akafunika mikono yake na ulaini wa shingo yake kwa ngozi za wana-mbuzi; akaleta muchuzi na mukate aliyotayarisha mukononi mwa mwana wake Yakobo. Naye alikuja kwa baba yake, akasema*:* Baba yangu; naye allsema*:* Mimi ni hapa; wewe ni nani, mwana wangu? Yakobo akamwambia. baba yake*:* Mimi ni Esau muzaliwa wako wa kwanza; nimefanya sawasawa ulivyoniomba; simama ninakuomba, keti na kula mawindo yangu, nafsi yako inibariki. Isaka akamwambia mwana wake*:* Namna gani umeyapata upesi hivi, mwana wangu? Naye alisema*:* Kwani Bwana Mungu wako amenisaidia. Isaka aka-mwambia Yakobo*:* Kuja karibu, ninakuomba, nikuguse, mwana wangu, kama wewe ni mwana wangu Esau kweli kweli ao hapana. Yakobo akakaribia Isaka baba yake; akamugusa, akasema*:* Sauti ni sauti ya Yakobo, lakini mikono ni mikono ya Esau. Wala hakumutambua kwa sababu mikono yake ulikuwa na nyole nyingi, kama mikono ya ndugu yake Esau ; hivi akamubariki. Akasema*:* Hakika wewe ni mwana wangu Esau? Naye alisema*:* Ndimi. Akasema*:* Uulete karibu nami na nitakula ya mawindo ya mwana wangu, nafsi yangu ikubariki. Akauleta karibu naye akakula akamuletea mvinyo akakunywa. Baba yake Isaka akamwambia*:* Kuja karibu sasa unibusu, mwana wangu. Akakaribia, akamubusu; naye alisikia manuko ya mavazi yake, akamubariki akasema*:* Tazama, manuko ya mwana wangu ni kama manuko ya po1i Bwana aliyobariki, na Mungu akupe wa umande wa mbingu, na ya manono ya inchi, na wingi wa nafaka na mvinyo; Mataifa wakutumikie, na makabila wainame mbele yako;uwe mukubwa juu ya ndugu zako na wana wa mama yako wainame mbele yako. Alaaniwe kila mutu anayekulaani, na abarikiwe kila mutu anayekubariki. Na ilikuwa wakati Isaka alipokwisha kubariki Yakobo, na Y akobo a1ikuwa ametoka sasa tu mbele ya uso wa Isaka baba yake, Esau ndugu yake akakuja toka kuwinda kwake. Naye vilevile alifanya muchuzi, akauleta kwa baba yake; akamwambia baba yake*:* Baba yangu asimame, apate kula ya mawindo ya mwana wake, nafsi yako inibariki. Isaka baba yake akamwambla*:* Wewe ni nani? Akasema*:* Mimi rn mwana wako, muza1iwa wa kwanza wako, Esau Isaka akatetemeka sana sana, akasema*:* Basi ni nani aliyetwaa ma-windo na kuyaleta kwangu na nimekula yote mbele ya kuja kwako, na kumu-bariki? Ndiyo, naye atabarikiwa. Wakati Esau a1iposikia maneno ya baba yake, akalia kilio kikubwa na kichungu sana, akamwambla baba yake*:* Unibariki hata mimi vilevile. Ee baba yangu. Akasema*:* Ndugu yako amekuja kwa hila amekutwalia baraka yako. Akasema*:* Jina lake haliitwi Yakobo kwa kusudi? Kwa sababu amenidanganya mara hizi mbili; akanitwalia haki yangu ya kuzaliwa kwanza, na tazama, sasa amenitwalia baraka yangu. Akasema*:* Hukuniweka mimi baraka? Isaka akajibu, akamwambia Esau*:* Tazama nimemuweka mukubwa wako, nimemupa ndugu zake zote wawe watumishi wake; na nimemutegemeza na nafaka na mvinyo; nawe, nitakufanyia nini sasa, mwana wangu? Esau akamwambia baba yake*:* Una baraka moja tu, baba akalia. Isaka baba yake akajibu, akamwambia*:* Tazama, ya manono ya inchi yatakuwa makao yako na ya umande wa mbingu toka juu; na utaishi kwa upanga wako, na utatumikia ndugu yako; na itakuwa wakati

utakapojifungua utavunja kongwa yake toka shingo yako.

Prokimenon. Sauti ya saba. Zaburi 107.

Utukuzwe, ee Mungu, juu ya mbingu.

Shairi*:* Moyo wangu umefanywa imara, ee Mungu.

Somo ya Mezali tutasoma (19, 16-25)

Mwenye kushika amri analinda nafsi yake*:* lakini yeye asiyeangalia njia zake atakufa. Yeye anayehurumia masikini anakopa kwa Bwana, naye atamulipa kwa tendo lake zuri. Azibu mwana wako kwa maana tumaini liko;Wala usiweke moyo wako juu ya uharibifu wake. Mutu wa gazabu kubwa atachukua azabu*:* Maana ukimuponyesha ni sharti kwako kufanya tena. Sikia shauri na pokea mafundisho, ili upate kuwa mwenye hekima kwa siku zako za mwisho. Kuna hila nyingi moyoni mwa mutu;lakini shauri la Bwana, ndilo litakalosimama. Mahitaji ya mutu ni wema wake*:* Na masikini ni mwema kuliko muwongo. Woga wa Bwana unaelekea uzima ;Naye aliye nao atakaa ameshiba ;Ubaya hautafika karibu naye. Mutu muvivu anatia mukono wake ndani ya sahani, Na hataki hata kuupeleka kwa kinywa chake tena. Piga mwenye kuzihaki, na wajinga watafundishiwa akili*:* Na umuhamakie yeye aliye na ufahamu, naye atafahamu maarifa.

APOSTIKHA

Sauti ya ine. Idiomelon.

Ee Mwokozi, utuokoe ku choyo mbaya, pamoja na maskini Lazaro utuhesabie kati ya wale watapumzika katika kifua cha Abrahamu; wewe mwenyewe ulikuwa mtajiri kwa kutaka kwako ulijifanya kuwa maskini kwa ajili yetu sababu ya kutufufua kaburini mpaka uzima wa milele kwa wema wako wa umungu na kwa mapendo yako kwa wanadamu. *(Mara mbili).*

Ee Bwana mpenda-wanadamu wewe uliitikia uvumilivu wa Mashahidi wako Watakatifu, pokea pia heshima ya nyimbo zetu, kwa maombezi yao utupe neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mama wa Kristu Mungu wetu uliyezaa Muumba wa ulimwengu, utuokoe ku hatari yote ili tukuimbie daima*:* Salamu, Mlinzi wa roho zetu.

MU KAZI MBILI ASUBUI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya sita. Agelike dinamis.

Ninapoteketezwa kwa ugonjwa wa zambi na kulala katika kitanda cha kutotumaini, nakuomba, ewe Mganga wa wagonjwa, unisikilize, usiruhusu nilale katika mauti ili niweze kukulalamikia*:* Ee Chemchem ya huruma, Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Umoja.*

Mwanzo wa wokovu wetu ilikuwa ni habari njema ya Malaika Gabrieli kwa Maria; wakati Malaika alionekana kwake, hakukatae salamu; hakusita kama alivyofanya Sara katika hema, lakini alisema*:* «Mimi ni mtumishi wa Bwana, ifanyike kwangu kama ulivyosema».

KATHISMA YA TATU.

Sauti ya tano. Lambi simeron.

Jana na leo Lazaro anateswa na magonjwa*:* Dada zake walimuambia Kristu; Bethania,

ujitayarishe kwa furaha upokee Rabi na Mfalme wako na imba pamoja nasi*:* Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**. *Umoja.*

Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu, mlinzi wa wakristu, okoa watu wako wenyi kukuita na matumaini na moyo*:* Fukuza haya ya mawazo yetu ya upotevu kusudi tukulalamikie*:* Salamu, Mama Bikira daima.

APOSTIKHA

Sauti ya tano. Idiomelon.

Ee roho yangu, ulipofungwa kwa minyororo ya zambi, ulitelemuka katika uzaifu na kutofanya kazi; acha Sodoma na Gomora kama Loti sababu ya kuepuka moto ya muovu; usirudi nyuma, utakuwa nguzo ya chumvi; kimbilia ku mlima ya fazila; kimbia moto anaungua mtajiri asiye na huruma, wende ku kifua cha Abrahamu kama Lazaro na kwa unyenyekevu wa moyo wako lalamika*:* matumaini yangu na kimbilio langu, ee Bwana, utukufu kwako. *(mara mbili).*

Ee Bwana, Mashahidi wako Washindani wa Malaika Wabila mwili waliposhinda katika mashindano yao walivumilia mateso; kwa tumaini moja walipata mema iliyoahidiwa; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira mtukufu, tunakuomba kama Mzazi-Mungu*:* Ombea roho zetu wokovu.

MU KAZI MBILI MAGARIBI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Kisha* «Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo tatu ya hii Kitabu na wimbo tatu ya Mineon.*

Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu se nekron.

Mishale yote ya adui imechoma moyo wangu wenyi kuelemezwa*:* tangu sasa inakaa ku kaburi ya uzaifu, yenyi ngumu kama jiwe la kaburi; lakini wewe Mwokozi ambaye kwa muti ya Msalaba wako uliwapa wafungwa wa Hadeze uzima, uniamshe sababu ya kunifufua ili kwa woga nitukuze umungu wako.

Na msaada wa shetani nilipendelea mali ya furaha mbaya na nilipata majivuno bila kujua; kama Lazaro mwingine nilizarau roho yangu yenyi kulala, yenyi njaa ya chakula cha juu-mbinguni, ee Neno la Mungu, uniokoe ku moto yenyi kunishambulia ili nitukuze rehema yako na mapendo yako kwa wanadamu.

Wimbo ingine. *Sauti ya tatu. Estisan ta triakonta argiria.*

Leo Lazaro anakufa, Bethania inaomboleza na kulia huyu wewe Mwokozi ulifufua toka wafu sababu ya kusabitisha ndani ya rafiki yako imani katika Ufufuo wako takatifu wenyi kuua mauti na kutupa sisi uzima, ndio maana tunakutukuza na kukuimbia.

Wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 110.

Woga wa Bwana ni mwanzo wa akili.

Shairi*:* Musifu Bwana. Nitashukuru Bwana kwa moyo wangu wote.

Somo ya Mwanzo tutasoma (31, 3-16).

Bwana akamwambia Yakobo*:* Rudi kwa inchi ya baba zako na kwa jamaa zako; na nitakuwa pamoja nawe. Yakobo akatuma akaita Rakeli na Lea shambani kwa kundi lake, akawaambia*:* Ninaona uso wa baba yenu nya kama si kwangu tena kama mbele; lakini Mungu wa baba yangu amekuwa pamoja nami. Na munajua ya kama kwa uwezo wnagu wote nilitumikia baba yenu. Na baba yenu alinidanganya na kugeuza mishahara yangu mara kumi; lakini Mungu

hakumwacha kuniumiza. Na alisema*:* Madoadoa watakuwa mushahara wako; halafu kundi lote wakazaa madoadoa; naye akisema*:* Wenye mistari watakuwa mushahara wako; halafu kundi lote wakazaa wenye mistari. Hivi Mungu ameondosha ngombe za baba yenu na kunipa mimi. Na ilikuwa kwa wakati kundi walipochukua mimba, nikanya-nyua macho yangu, nikaona katika ndoto, na tazama, mbuzi ndume waliopandia kundi walikuwa wenye mistari, madoadoa na mabatobato. Na malaika ya Mungu aliniambia katlka ndoto*:* Yakobo; nami nilisema*:* Mimi ni hapa. Akasema*:* . Nyanyua sasa macho yako na ona, mbuzi ndume wote wanao-pandia kundi ni wenye mistari madoadoa na mabatobato*:* Kwani nimeona yote Labani a1iyokufanyia. Mimi ni Mungu wa Beteli pahali u1ipomwangia nguzo mafuta, paha1i u1iponiapia kiapo; simama sasa, ondoka toka inchi hii na rudi kwa lnchi ya kuza1iwa kwako. Rakeli na Lea wakajibu, wakamwambia*:* Sehemu ni tena kwetu ao uriti nyumbani mwa baba yetu? Hatuhesabiwi naye kama wageni? Kwa sababu a1ituuza naye amekula feza yetu kabisa. Kwa sababu ma1i zote Mungu a1izoondosha kwa baba yetu ni yetu na ya watoto wetu ; basi sasa, kitu gani Mungu alichokuambia, fanya.

Prokimenon. Sauti ya inne. Zaburi 111

Ana neema na anajaa rehema, ni mwenye haki.

Shairi*:* Heri mutu, anayeogopa Bwana.

Somo ya Mezali tutasoma (21, 3-21).

Kutenda haki na hukumu Kunapendeza Bwana kuliko sadaka, Macho yenye kiburi, na moyo wa majivuno, Hata taa ya waovu ni zambi. Mafikili ya wenye bidii yanaelekea utajiri tu*:* Lakini kila mutu anayetenda kwa haraka anaelekea uhitaji. Kupata hazina kwa njia ya ulimi wa uwongo. Ni moshi unaopeperushwa huku na huku ; wao wanaozitafuta wanatafuta mauti. Jeuri ya waovu itawaondoa mbali; Kwa sababu wanakataa kufanya hukumu. Njia yake anayelemewa na zambi inakunjama sana*:* lakini mwenye safi, kazi yake ni ya haki. Ni afazali kukaa katika pembe darini mwa nyumba, kuliko katika nyumba moja pamoja na mwanamuke mugomvi. Nafsi ya mwovu inatafuta ubaya*:* Jirani yake hakubaliwi kwa macho yake. Wakati mwenye kuzihaki anapoazibiwa, mujinga anapata hekima*:* Na wakati mwenye hekima anapofundishwa, anapata maarifa. Mwenye haki anafikili nyumba ya mwovu;

Ya kuwa waovu wanaangamizwa na kuharibiwa. Mwenye kufunga masikio yake kwa kilio cha masikini, atalia vilevile, Iakini hatasikiwa. Zawadi ya siri inatuliza hasira, na zawadi kifuani gazabu kali. Ni furaha kwa wenye haki kutenda hukumu; Lakini ni uharibifu kwa watenda uovu. Mutu anayehangaika na kuacha njia ya ufahamu Atapumzika katika makutano ya wafu. Yeye anayependa anasa atakuwa masikini*:* Yeye anayependa mvìnyo na mafuta hatakuwa tajiri. Mwovu ni ukombozi wa wenye haki ; Naye anayefanya hila ni pahali pa wenye haki. Ni afazali kukaa katika inchi ya ukiwa, kuliko kukaa pamoja na mwanamuke mugomvi na muchokozi. Kuna hazina ya damani na mafuta katika kao Ia mwenye hekima; lakini mupumbafu anaimeza. Yeye anayefuata haki na rehema anapata uzima, haki na heshima.

APOSTIKHA

Sauti ya kwanza. Idiomelon.

Ee roho yangu, wewe ulivaa nguo nzuri ya ufalme Mungu alifuma na hariri ya milele ulikosa juu ya heshima yako mwenyewe, mbali ya Mungu ulitafuta utajiri na furaha, ulijipandisha yulu ya jirani zako kwa majivuno kama mtajiri alivyozarau Lazaro na umaskini wake; lakini bila kuazibiwa kama yeye, uwe maskini katika roho na umulalamikie Bwana aliyejifanya maskini kwa ajili yako*:* Ee Mwokozi uliyevaa nguo nyekundu ya zihaka mbele ya kusulubiwa Msalabani na kutwaliwa nguo juu yangu wakati ulipanda Msalabani, unipe nguo ya Ufalme wa mbinguni na uniokoe milele ku haya *(mara mbili).*

Enyi Mashahidi Watakatifu, neema gani kwa ushijaa yenu! Mulitoa damu yenu na munapokea uriti wa mbinguni; kwa jaribu ya wakati kidogo furaha yenu inadumu milele; hii

kweli ni badilisha ya ajabu*:* maana muliacha uharibifu sababu ya kupokea mema ya milele; sasa munafurahi pamoja na malaika na munaimbia daima Utatu wa sili moja.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Alipoona Kristu ametundikwa Msalabani, Bikira akasema*:* Upanga imechoma moyo wangu kama alivyoagua mzee Simeoni; lakini fufuka, ee Bwana wa milele, nakuomba atukuzwe pamoja nawe Mama yako na mtumishi wako.

MU KAZI TATU ASUBUI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya mbili. Ton lithon tu mnimatos.

Nilipovutwa kwa uzito wa zambi zangu, tazama sasa nimelala katika kaburi ya uzaifu*:* Uniokoe, ee Bwana, kwa wema wako kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Tunapolindwa kwa Msalaba heshimiwa wa Mwana wako, ee Malkia Mzazi-Mungu, tunaweza wapesi kuacha akili yote ya adui, ndio maana tunakutaja mwenye heri, Mama wa Nuru na peke yake matumaini ya roho zetu.

KATHISMA YA TATU.

Sauti ya tatu. Tin oreotita.

Leo Lazaro alikufa amezikwa na ndugu zake wanalia juu yake, kama Mungu, kwa kujua kwako yatakayokuja nyuma uliwaambia Wafuasi magonjwa ukasema*:* Lazaro amelala, lakini sasa nitamufufua huyu niliumba. Ndio maana wote tunaimba*:* Utukufu kwa uwezo wako kubwa, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee kristu, Mama yako Mtakatifu asiyeolewa alipoona mwili wako imetundikwa Msalabani akalia machozi kama mama, akapaza sauti na kusema*:* Tazama tuzo la watu wasiyo na shukrani wao walipata mema mengi! Ee Mwanangu, naimbia na kutukuza mapendo yako kubwa.

Ode ya tatu. *Sauti ya mbili. Stirothenta.*

Inaposabitishwa kwa uwezo wa Msalaba wako, roho yangu yenyi kuvunjika kwa mishale ya shetani uiongoze kwa amri zako, ee Bwana.

Ninaposinzia katika uzaifu kitandani mwa furaha, uniamshe, ee Kristu toka usingizi wangu na unipe nitukuze Mateso yako.

Tunapotakaswa kwa kufunga na roho yenyi kuangaziwa tuendeni kukutana na kristu anaenda ku Yerusalema.

THEOTOKION.

Ee Bikira safi kamili ambaye moto ya Umungu haikuunguza choma mwilini mwangu nguvu ya tamaa zangu ili nikutukuze milele.

Irmos ingine. Sauti ya tatu. Stira psikhi.

Leo Lazaro anakufa lakini lufu yake haifichame machoni mwa Yesu; ndio maana aliwaambia Wafuasi wake akisema*:* Lazaro rafiki yangu amelala, lakini nitamufufua.

Ee Bwana, uliposema juu ya kurudi katika Yudea, uliogopesha Mitume wake; lakini Tomasi mwenyi kujaa moyo akapaza sauti na kusema*:* Tuendeni, kwa sababu yeye ni Uzima wetu; kama tutakufa atatufufua.

Utukufu kwa Baba. . .

Utatu wa asili moja wa Baba mwenyezi, wa Mwana wa milele na wa roho Mtakaitfu, Umungu mkono hata mumoja haikuumba, wenyi kutawala na kutukuzwa pamoja, tunakuimbia kwa sauti moja.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Mama Bikira Mtakatifu kamili, shina la Yesse kulitoka Yesu kama Jua lenyi kuleta uzima kwa wanadamu sababu ya kutuokoa ku mauti na kaburini, tunakuimbia kwa sauti moja.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Salamu, Sayuni, kwani tazama anakuja Mfalme wako mwenyi kujaa na huruma kama alivyogua Nabii, mwana-punda anachukua mwili wa huyu mwenyi kushika ulimwengu wote mkononi mwake; tuimbieni nguvu ya Bwana Mungu wetu.

IRMOS: Ee roho tasa isiyo na watoto, uzae tunda la utukufu na kwa furaha utaimba*:* Nguvu yangu inatoka kwako, ee Mungu wangu, hakuna hata mumoja aliye mtakaitfu, hakuna hata mumoja aliye mwenye jaki ila Bwana peke yake.

APOSTIKHA

Sauti ya kwanza. Idiomelon.

Wafarisayo walipoona manguo nyekundu na ya hariri waliangaa kwa mavazi yao ya kuhani na ya Wafalme; Sheria na Manabii walikua hazina yao walifurahi kwa ibada yao; wewe, Maskini, walikusulubisha inje ya milango ya muji na walikukataa japo Ufufuo wako, wewe uliye milele katika kifua cha Baba; neema itakuwa kwako kama tone ya maji kama alivyoitamani mtajiri asiye na huruma ambaye pahali pa nguo nyekundu na ya hariri alifunikwa katika moto ya milele; wataona watu wa mataifa ambao zamani waliwaombaomba makombo ya ukweli, wenyi kufarijiwa kwa imani katika kifua cha Abrahamu, wenyi kuvaa kanzu nyeupe ya ubatizo na nguo nyekundu ya Damu yako, wenyti kufurahi na neema yako na wakisema*:* Ee kristu Mungu wetu, utkufu kwako. *(mara mbili).*

Enyi Mashahidi Watakatifu wenyi kustahili sifa yote, haiko ao majaribu, ao sikitiko, ao njaa, ao uzulumu, ao hatari, ao ukali wa nyama ya pori, ao upanga, ao moto ambayo kwa makamio yao yaliweza kuwatenga ninyi na Mungu; lakini ni kwa map[endo kwa ajili yake mulisahau dunia mukawa wageni juu ya mwili wenu na mulishindana kwa kuzarau mauti; ndio maana mulipokea tuzo la kazi yenu mukawa wariti wa ufalme wa mbingu*:* Ombeni roho zetu wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, Mama yako Mtakaitfu alipokuona umetundikwa Msalabani, wewe mwenye kutundika inchi juu ya maji, akakulalamikia*:* Ole wangu! Hii ni ombi ya ajabu! Wapi uzuri wako wa mapendo, ee Mwanangu wa milele? Naimbia rehema yenyi kukuteswesha kwa ajili ya wanadamu.

MU KAZI TATU MANGARIBI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Kisha* «Bwana nimekuita. . . » *tunaimba wimbo sita ya hii Kitabu na wimbo inne ya Mineon.*

Sauti ya tano. Idiomelon.

Mimi niliye mtajiri wa namna ya tamaa navaa kanzu ya uongo ya unafiki, nafurahi katika ulevi wa zambi; nakosa huruma, nazarau roho yangu yenyi kulala mbele ya milango ya toba,

inatamani mema na inateswa na magonjwa; lakini wewe, ee Bwana, unifanye mimi maskini Lazaro kwa zambi kusudi nisiombeombe tone ya maji juu ya ulimi wangu wenyi kuteswa na kiu katika moto ya milele; ee mpenda-wanadamu, uniweke katika kifua cha Baba Abrahamu. *(mara mbili).*

Kwa nguvu yenu imara hamukukataa Kristu, enyi Mashahidi Watakatifu mulioteswa mateso ya kila namna, lakini mulishinda ujasiri wa wazulumu na mulilinda bila kosa imani sababu ya kupita toka dunia kwenda mbinguni; ndio maana kwa deni munayo kwa Mungu, mumuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Katika nguvu yenu imara hamukumukana Kristu, ee Mashahidi Watakatifu muliyoteswa mateso ya namna yote, lakini mulishinda nguvu ya wazulumu na mukalinda bila kosa imani sababu ya kupita duniani kwenda mbinguni; umuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Wimbo ingine. Kheris askitikon. Sauti ya tano

Ee Bwana, ulipotembea ngambo ya Yordani, uliwaambia Wafuasi wako*:* Lazaro rafiki yetu amekwisha kufa, wamemuzika; ndio maana nafurahi juu yenu nini rafiki zangu kusudi mujue ya kama najua yote kwa sababu japo mwili wangu wenyi kuonekana mimi ni Mungu aliye pahali pote; tuendeni basi tukamufufue kusudi mauti ijue ya kama imeshindwa na ya kama Mimi kweli ni Mkombozi wenyi kuyleta neema ya wokovu duniani

Ninyi waaminifu, tufuate mfano wa martha na wa Maria, tumutumie Bwana matendo yetu matakatifu ili akuje na afufue roho yetu yenyi kulala bila uzima kaburini, isiyoogopa Mungu na haina na nguvu ya kuishi; tumulalamikie*:* Ee Bwana, tazama, kama zamani ulivyomufufua rafiki yako Lazaro wewe mwenyewe, ee Mungu wa wema, vivyo leta uzima duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Wimbo ingine. Sauti ya sita. Epi ton tafon Kirie.

Lazaro eko ndani ya kaburi tangu siku ya mbili, anaona wale walikufa tangu m, ilele, anaona jambo la ajabu, watu wengi sana wamefungwa minyororo ya Hadeze; dada zake wanalia machozi ya uchungu mbele ya kaburi yake; Kristu anakuja kumufufua rafiki yake sababu ya kuamusha furaha ileile katika roho zote; Umetukuzwa, ee Mwokozi, utuhurumie.

Wimbo inne ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 114.

Aligeuza mwamba kuwa ziwa la maji.

Shairi*:* Ninap[enda Bwana kwa sababu amesikia sauti yangu na kusihi kwangu.

Somo ya Mwanzo tutasoma ((43, 25-30 na 45, 1-16).

Wakaweka zawadi tayari kwa Yosefu aliyekuja saa sita, kwa sababu wamesikia ya kama watakula pale. Na wakati Yosefu alipokuja kwake, wakamuletea zawadi iliyokuwa mukononi mwao nyumbani, wakajiinama mbele yake hata udongo. Akawauliza hali, akasema*:* Baba yenu muzee muliyesema juu yake ni muzuri? Anaishi hata leo? Wakasema*:* Mutumishi wako baba yetu ni muzuri; anaishi hata leo. Wakainama vichwa, wakajiinama. Akanyanyua macho yake akaona Benyamina ndugu yake, mwana wa mama yake akasema. Huyu ni ndugu yenu mudogo muliyeniambia juu yake? Akasema*:* Mungu akurehemie, mwana wangu. Yosefu akafanya mbio; kwa sababu moyo wake ulikuwa na hamu sana kwa ndugu yake; akatafuta pahali kwa kulia, akaingia chumbani mwake, akalia pale. Halafu Yozefu hakuweza kujizuiza tena mbele yao wote waliosimama karibu naye; akalia*:* Toeni kila mutu mbele yangu. Wala hakusimama mutu pamoja naye wakati Yosefu alipojitambulisha kwa ndugu wakasikia. Yosefu akawaambia ndugu zake*:* Mimi ni Yosefu; baba yangu anaishi haya lao? Wala ndugu zake hawakuweza kumujibu, kwa sababu wakaogopa mbele yake. Yosefu akawaambia ndugu zake*:* Karibieni kwangu, ninawaomba ninyi. Wakakaribia. Akasema*:* Mimi ni Yosefu ndugu

yenu, uliyemwuza kwenda kwa Msiri. Basi sasa musihuzunishwe, wala isiwe hasira kwa macho yenu ya kwamba muliniuza hapa; kwa sababu Mungu alinituma mbele yenu kwa kuponyesha maisha za watu. Kwa sababu miaka hii miwili njaa imekuwa inchini; na miaka mitano mingine itakuwa isiyo na kulima wala kuvuma. Mungu amenituma mbele yenu kuponyesha baki duniani, na kuwaponyesha ninyi kwa wokovu mukubwa. Basi sasa hakuna ninyi mulionituma hapa, lakini Mungu; naye amenifanya kuwa baba kwa Farao, na bwana ya nyumba yake yote, na mutawala juu ya inchi nzima ya Msiri. Fanyeni mbio, pandeni kwa baba yangu mumwambie*:* Mwana wako Yosefu anasema hivi*:* Mungu ameniweka bwana juu ya Msiri yote; shuka kwangu, usikawie; nawe utakaa katika inchi ya Goseni, na utakuwa karibu nami, wewe na wana wako; na wana wa wana wako, na kondoo zako na ngombe zako na yote uliyo nayo; na nitakukulisha pale; kwa sababu miaka mitano mingine ya njaa itakuwa; usiwe masikini, wewe na nyumba yako, na yote uliyo nayo. Na tazama, macho yenu yanaona, na macho ya ndugu yangu Benyamia ya kama ni kinywa changu kinachosema nanyi. Na mutamwambia baba yangu juu ya utukufu wangu wote katika Msiri na juu ya vyote mulivyoviona; na mutafanya mbio na kushusha baba yangu hapa. Akaangukia Benyamina kwa shingo yake, akalia, Benyamina akalia juu ya shingo yake. Akabusu ndugu zake zote, akalia juu yao; nyuma ya yale ndugu zake wakasemezana naye. Habari zake zikasikiwa nyumbani mwa Farao kusema*:* Ndugu za Yosefu wamekuja; ikakuwa njema kwa macho ya Farao na watumihsi wake.

Prokimenon. Sauti ya ine. Zaburi 115.
Nitatembea mbele ya Bwana, katika inchi ya wahai.
Shairi*:* Bwana ni mwenye neema na haki.
Somo ya Mezali tutasoma (21, 23-22, 4).

Yeye anayezuiza kinywa chake na ulimi wake analinda nafsi yake na taabu. Mutu mwenye majivuno na kiburi, jina lake ni muzihaki, anatumika katika majivuno ya kiburi. Kutaka kwa muvivu kunamwua; Maana mikono yake inakataa kutumika. Kuna anayetamani muchana kutwa*:* lakini mwenye haki anatoa wala hanyimi. Zabihu ya waovu ni machukizo*:* Kuzidi gani wakati anapoitoa kwa nia mbaya ! Mushuhuda wa uwongo atapotea ; Lakini mutu anayesikia atasema maneno yanayodumu. Mwovu anafanya uso wake kuwa mugumu*:* Lakini mwenye haki anatengeneza njia zake. Hakuna hekima wala ufahamu wala shauri juu ya Bwana. Farasi anawekwa tayari kwa siku ya vita*:* Lakini Bwana analeta kushinda. Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi, na ukubali kuliko feza na zahabu. Tajiri na masikini wanakutana*:* Bwana ndiye aliyewaumba wawili. Mutu mwenye akili anaona uovu na kujificha*:* Lakini wajinga wanaendelea mbelc na wanaumia. Zawabu ya unyenyekevu na woga wa Bwana. Ni mali na heshima na uzima.

MU KAZI INNE ASUBUI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon.

Tuunganishe kuona na tendo sababu ya kuituma kwa Kristu kusudi kwa kuja kwake alete uzima rohoni mwetu isiyo na uzima kama Lazaro kaburini; tumutolee matawi yetu ya haki tukisema*:* Atukuzwe huyu anayekuja kwa jina la Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Uhiharikishe kuponyesha magonjwa ya mwili wangu na tamaa mbaya za roho yangu, linganyisha nafsi za roho yangu, unistahilishe, ee Mzazi-Mungu na Bikira Mtakatifu kamili,

nitolee kwa utulivu wa mawazo yangu ibada safi kwa Mfalme wa ulimwengu na nimuombe maondoleo ya zambi zangu.

KATHISMA YA TATU

Sauti ya sita. Agelike dinamis.

Lazaro eko ndani ya kaburi tangu siku mbili, dada zake wawili, Martha na Maria wanafanya kilio kubwa juu yake, wakitazama kwa huzuni jiwe la kaburi; Muumba anajongea pamoja na Wafuasi wake sababu ya kuondoa mauti na kutupa sisi uzima; ndio maana tunamulalamikia*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mama Mtakatifu wa Kristu Mungu wetu, ulizaa Muumba wa ulimwengu, pamoja na Mitume Watakatifu umuombe Mungu wa wema ili tuokolewe toka tamaa zetu na tupokee maondoleo ya zambi zetu.

APOSTIKHA

Sauti ya tano. Idiomelon.

Kujemi, ninyi ndugu wote, mbele ya mwisho kwa moyo mumoja tumjongee Bwana wa huruma, tuache shuruli zote za hii uzima, tushurulikie paka roho yetu tukatae kwa kadiri chakula cha furaha, tutolee sadaka ya mali zetu; kama inavyoandikwa, katika hii wengine, bila kujua, walipokea Malaika nyumbani mwao; katika maskini tulishe huyu alitulisha mwili wake; tuvae huyu mwenyi kuvaa nuru kama nguo kusudi kwa maombezi ya Mtakatifu Mzazi-Mungu tupate maondoleo ya zambi zetu na kwa machozi tumulalamikie Bwana; Utuokoe ku laana yenyi kuongozwa, utustahilishe tusimame kuume kwako mbinguni, maana wewe ni mwema na mpenda-wanadamu. *(mara mbili).*

Katika mateso Mashahidi wakalalamika kwa furaha*:* Hii ndio njia ya sisi kupatana na Mungu; kwa malipo ya vidonda vyenyi kujaa katika miili yetu, tutapokea mavazi meupe ya ufufuo; pahali pa matusi tutapokea utukufu wa mbinguni; pahali pa gereza tutapata Paradizo; pahali pa kuhukumiwa kama waovu tutakuwa pamoja na malaika mbinguni. Ee Bwana, kwa maombezi, okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira mwenyi kuchaguliwa katika majamaa yote ya wanadamu, sikilia mwito wetu, leta rohoni mwetu ile inataka, kwa maombezi ya Mitume Watakatifu, ewe Bikira Mama mwenyezi kwa Mungu, utuokoe ku tamaa na mateso yetu.

MU KAZI INNE MANGARIBI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Kisha «*Bwana nimekuita*. . . » tunaimba wimbo tatu ya hii Kitabu na wimbo tatu ya Mineon.*

Sauti ya ine. O ek ipsistu klithis.

Ee Krist, wawili kati ya Mitume Watakatifu walipokutambua kuwa mumoja wa Utatu Mtakatifu leo unawatuma kutimiza Maandiko kwa kutafuta mwana-punda mtoto wa yule mwenyi kuchukua nira; utakaa na unyenyekevu juu yake, ee Mungu wa mapendo, kwani unataka kuwatayarishia wale wenyi kukupenda kiti juu mbinguni na kuwapa wasiyo na akili wenyi kuelemezwa kwa nira ya tamaa, hekima ya kukulalamikia*:* Hosanna.

Ee Sayuni, pokea Mfalme wako; tazama Yeye anajongea mwenyi kujaliwa na wema kusudi amufufue Lazare na kuharibu ufalme wa mauti, na ninyi Watawa Watakatifu wengi Mungu alikusanya, kujeni kukutana na Kristu mukishika matawi na kuimba*:* Abarikiwe huyu anayekuja kuokoa wanadamu kwa Mateso yake Msalabani sababu ya kuleta uzima wa milele rohoni mwetu.

Wimbo ingine. Sauti ya mnane. O en Edem paradisos.

Ee Kristu, wewe unayeketi juu ya Waserafi wa mbinguni katika ufalme takatifu wa Muumba wa ulimwengu, wewe mwenyewe duniani unajiharikisha kukaa juu ya mwana-punda; Bethania inafurahi kukupokea kama Mwokozi; Yerusalema inashangilia kwa kupokea Masiya; Mauti inateswa kwa kuona Lazaro inamukimbia; sisi pamoja na matawi tunaenda kukutana na Wewe katika furaha, tunatukuza uwezo wa wema wako, ee Bwana.

Wimbo tatu ya Mineon.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Prokimenon. Sauti ya sita. Zaburi 119.

Katika taabu yangu nililia kwa Bwana.

Shairi*:* Uponyeshe nafsi yangu, ee Bwana, na midomo ya uwongo, na ulimi wa hila.

Somo ya Mwanzo tutasoma (46, 1-7)

Israeli akasafiri pamoja na yote*:* aliyokuwa nayo, akafika kwa Beri-Seba, akatoa zabihu kwa Mungu wa baba yake Isaka. Mungu akamwambia Israeli kwa maono yausiku akiesema*:* Yakobo, Yakobo. Akasema*:* Mimi ni hapa. Akasema*:* Mimi ni Mungu, Mungu wa baba yako; usiogope kushuka kwa Msiri; maana nitakufanya taifa kubwa pale; nitashuka pamoja nawe kwa Msiri, na hakika nitakupandisha tena;a Yosefu ataweka mukono wake juu ya macho yako. Yakobo akaondoka kwa Beri-Seba; wana wa Israeli wakabeba Yakobo baba yao, na watoto wao, na wake wao ndani ya magari Farao aliyotuma kumubeba. Wakatwaa nyama zao na mali zao walizopata katika inchi ya Kanama, wakakuja kwa Misri; Yakobo na uzao wake wote pamoja naye wana wake na wana wa wana wake pamoja naye, binti zake na binti za wana wake, uzao wake wote akaleta pamoja naye kwa Misri.

Prokimenon. Sauti ya mnane. Zaburi 120.

Bwana atakuchunga katika mabaya yote; atachunga nafsi yako.

Shairi*:* Nitanyanyua macho yangu kwa milima.

Somo ya Mezali tutasoma (23, 15-24, 5)

Mwana wangu, kama moyo wako ukiwa na hekima, moyo wangu utafurahi, ndiyo, wangu*:* Ndiyo, viuno vyangu vitafurahi, wakati midomo yako inaposema maneno yaliyo haki. Moyo wako usione wivu kwa wenye zambi*:* Lakini wewe uogope Bwana muchana kutwa. Maana hakika kuna zawabu; wala taraja yako haitakatiliwa mbali. Sikia, mwana wangu, na uwe na hekima, na ongoza moyo wako njiani. Usiwe katikati ya walevi; Katikati yao wanaokula nyama kama walafi*:* Maana mulevi na mulafiwataingia umasikini*:* Na utepetevu utavalisha mutu na nguo za kupasuka. Sikiliza baba yako aliyekuzaa, wala usizarau mama yako kwa wakati wa uzee wake.

Nunua kweli, wala usiiuze; ndiyo, hekima na mafundisho, na ufahamu. Baba ya mwenye haki atashangilia*:* Naye anayezaa mutoto mwenye hekima atafurahishwa naye. Baba yako na mama yako wafurahi, na yeye aliyekuzaa ashangilie, Mwana wangu, unipe moyo wako, na macho yako yapendezwe na njia zangu. Kwa maana kahaba ni shimo refu;na mwanamuke mugeni ni shimo nyembamba. Ndiyo, anavizia kama mwizi, na anacngeza wenye hila katikati ya watu. Nani ana taabu? Nani ana huzuni? Nani ana mabishano? Nani ana manunguniko? Nani ana vidonda visivyo na sababu? Nani ana macho mekundu?Wale wanaokawa saa ndefu kwa mvinyo;Wao wanaotatuta mvinyo iliyochanganyika. Wewe usiangalie mvinyo wakati ilipo nyekundu, wakati inapotoa rangi yake ndani ya kikombe, wakati inaposhuka pasipo matata. Kwa mwisho inauma kama nyoka, na kuchoma kama fira; macho yako yatatazama mambo mageni, moyo wako utatoa maneno yasiyofaa. Ndiyo utakuwa kama yeye anayelala katikati ya bahari, Ao kama yeye anayelala juu ya mulingoti. Wamenipiga, utasema, nami sikuumizwa; Wamenipiga, nami sikuisikia*:* Nitaamka wakati gani? Nitazidi kuitafuta tena. Usione wivu kwa watu wabaya, wala usitamani kuwa pamoja nao*:* Maana moyo wao unafikili mateso, na midomo yao inasema mabaya. Nyumba inajengwa kwa hekima; na inasimamishwa kwa ufahamu*:* Na nyumba

vinajazwa kwa maarifa, na mali zote za damani na za kupendeza. Mutu mwenye hekima ni mwenye nguvu*:* Ndiyo, mutu wa maarifa anaongeza uwezo.

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Ee Kristu Mungu wetu, uniokoe ku choyo ya mtajiri asiye na huruma, wewe ulizima zambi zetu kwa Msalaba wako; unipe nifanane na uzima wa maskini Lazaro yenyi kujaa na uvumilivu na wema, kwa wema wako kubwa usinitenge mbali ya kifua cha Abrahamu. *(mara mbili).*

Enyi Mashahidi wa Bwana wenyi kutakasa ulimwengu na kuponyesha magonjwa yote, ombeni sasa kwa ajili yetu sababu ya kuokoa roho zetu ku mtego wa adui.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ni ajabu kweli! Ni fumbo ya ajabu na mupya, ndivyo alivyosema Bikira wakati alipoona Msalabani ametundikwa katikati ya wanyanganyi huyu alizaa bila uchingu, alipoomboleza akalia akisema*:* Ole wangu! Ee Mwanangu mpendwa, namna gani hawa watu wabaya kwa kukosa kwao shukrani wanakusulubisha Msalabani?

MU KAZI TANO ASUBUI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Tunasoma Eksapsalmos, na tunaimba Alliluia, Wimbo ya Utatu Mtakatifu na kisha Kathisma wa kwanza ya Paraklitiki na sauti ya hii Juma (tafuta ku mwisho ya hii Kitabu). Na kisha tunaimba Kathisma ya hii Kitabu:*

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya ine. Takhi prokataleve.

Kama ilivyoandikwa, Mitume wawili walitumwa kutafuta mwana-punda Kristu atapanda sababu ya kupokea sifa takatifu ya watoto wadogo; tuendeni kukutana naye na furaha sababu ya kumutolea matawi ya fazila zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Bikira Mtakatifu kamili na mama wa kristu Mungu wetu, upanga ilichoma roho wakati uliona Mwana na Mungu wako Msalabani*:* Umuombe daima kwa ajili ya maondoleo ya zambi.

KATHISMA YA TATU.

Sauti ya mnane. Anestis ek nekron.

Wafuasi wawili wanatumwa leo kutafuta mwana-punda juu ya Rabi wa ulimwengu mwenye kuketi juu ya Waserafi wengi; mauti yenyi kuharibu wanadamu inaanza kutetemeka, kwani Kristu anainyanganya mateka yake ya kwanza na Lazaro atainyanganya wanadamu wote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Bikira Safi alipoona mateso ya Mwana wake, kwa kulia na kuomboleza akasema katika sikitiko ya moyo wake*:* Ole wangu! Ee Mwanangu, namna gani watoto wa Waebrania walikutoa kwa Pilato sababu ya kusulubiwa wewe ambaye Malaika wanatukuza daima? Ee Neno, naimbia rehema yako ya milele.

APOSTIKHA

Sauti ya ine. Idiomelon

Ee roho yangu, ulipozarau mafundisho takatifu ulianguka katika mitego ya adui, kwa kosa lako ulitolewa ku mauti, na kwa usingizi wa zambi ulichafua nguo yako, kiumbe cha Mungu ukaichafua ku arusi ya Mfalme; na kama hautake kufukuzwa sababu ya zambi yako ao kukaa ku

karamu na nguo ya tamaa zako sababu ya wewe kuingia na kufukuzwa katika nyumba ya karamu, umulalamikie Mwokozi*:* Ee Mwamzi wa haki, uliyejifananisha na mimi bila kupoteza vile ulikuwa, mbele ya kusulubiwa Msalabani ulivaa kwa ajili yangu nguo ya zihaka*:* Pasua basi nguo ninavaa, univike kanzu ya furaha, uniokoe ku giza za inje na msago wa meno, na unihurumie. *(mara mbili).*

Kujeni, enyi mataifa yote, tuimbe nyimbo na shairi za kiroho sababu ya kutukuza Mashahidi washindi wa kristu, wahubiri wa imani na taa ya ulimwengu, chemchem isiyokauka huko kunatiririka maponyesho; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani yako duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane. Idiomelon*

Tunapofika ku mwisho wa siku makumi ine, ee Bwana mpenda-wanadamu, tunakuomba tuone pia Juma Takatifu ya Mateso yako sababu ya kutukuza mema yako ya juu na tendo lisilokadirika la wokovu wako tukiimba kwa sauti moja*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . *(Mara ingine hii).*

MU KAZI TANO MANGARIBI YA JUMA YA SITA

Elezo*: Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo kumi. Hivi:*

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Tunapofika ku mwisho wa siku makumi ine, ee Bwana mpenda-wanadamu, tunakuomba tuone pia Juma Takatifu ya Mateso yako sababu ya kutukuza mema yako ya juu na tendo lisilokadirika la wokovu wako tukiimba kwa sauti moja*:* Ee Bwana, utukufu kwako. *(mara mbili).*

Enyi mashahidi wa Bwana, muombeni Mungu kwa ajili ya roho zetu na kwa wema wake atuondolee zambi zetu nyingi mno.

Wimbo ya Lazaro. Sauti ya sita. Idiomelon.

Ee Bwana, ulipotaka kuona kaburi ya Lazaro, wewe ulikaa kaburini kwa kutaka kwako uliuliza*:* Wapi mulimuweka? Wakati ulisikia hii haukujua, ulimuita huyu ulipenda*:* Lazaro, toka Kaburini! Mufu alimutii Huyu mwneyi kuleta uzima, Mwokozi wa roho zetu. *(mara mbili).*

Ee Bwana, ulikua siku ya ine ku kaburi ya Lazaro na ukalia machozi juu ya rafiki yako, kwa mufu wa siku ine ulimufufua, mauti ilifungwa kwa msalaba wako, ulifungua sanda kwa mikono yako; halafu Mitume walijazwa na furaha, na roho zote ziliimba kwa sauti moja*:* Umetukuzwa, ee Mwokozi, utuhurumie. *(mara mbili).*

Ee Bwana, kwa sauti yako ufalme wa Hadeze iliharibiwa, neno lako la uwezo liliamusha kaburini mufu mumoja wa siku ine, Lazaro akawa mwanzo wa wokovu wa upya wetu; hakuna kitu kisichowezekana kwa Mfalme wa ulimwengu*:* Ee Bwana uwape watumishi wako maondoleo na neema ya wokovu.

Ee Bwana, ulipotaka kusabitisha imani ya Wafuasi wako kwa ufufuo wako katika wafu, ulikuja ku kaburi ya Lazaro na ulimuita, Hadeze iliondolewa, ukaokoa mufu wa siku ine aliyelalamikia*:* Umetukuzwa, ee Bwana, utukufu kwako.

Ee Bwana, ulipochukua Wafuasi wako pamoja nawe, ulikuja ku Bethania sababu ya kuamuasha Lazaro katika wafu, na ulipolia machozi juu yake sababu ya kutii ku ubinadamu, kama Mungu ulifufua huyu mufu wa siku ine aliyekulalamikia, ee Mwokozi*:* Umetukuzwa, ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mnane. Idiomelon.*

Bwana, ulikuja ku kaburi ya Lazaro, ulimuita mufu kama juu ya kumuamusha mu usingizi yake*:* Alikunguta vumbi ya kaburi kwa pumuzi yako ya milele na kwa mwito wa sauti yako alitoka mwenyi kufungwa sanda; maana una uwezo na utawala juu ya vitu vyote, ee mpenda-wanadamu, wewe ni Rabi wa ulimwengu wote*:* Ee Mwokozi, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . Sauti umoja. *Idiomelon.*

Tunapofika ku mwisho wa siku makumi ine, tunapaza sauti na kusema*:* Salamu, ewe muji wa Bethania, inchi ya Lazaro; Sakamu, Martha na Maria; Kesho Kristu atakuja, kwa neno lake atafufua marehemu ndugu yenu. Hadeze mbaya na isiyowezakushiba ikisikia sauti yake, itatetemeka kwa woga na italia, itarudisha Lazaro kisha siku ine; kisha kushangaa Waebrania na mingazi na matawi mikononi watamutangulia mbele; na tutaona watoto wakimutukuza huyu baba zao waliochukia*:* Abarikiwe yeye anayekuja kwa jina la Bwana, Mfalme wa Israeli.

KUINGIA.

Mwangaza upole.

Prokimenon. Sauti ya sita. Zaburi 123.

Kusaidia kwetu ni kwa jina la Bwana.

Shairi*:* Kama si Bwana aliyekuwa upande wetu, Israeli asema sasa.

Somo ya Mwanzo tutasoma (49, 33-50, 26)

Na wakati Yakobo alipomaliza kuamuru wana wake, akakunja miguu yake kitandani, akatoa roho, akakusaywa kwa watu wake. Yosefu akaangukia baba yake usoni, akamubusu. Uosefu akaagiza watumishi wake waganga kupakaa maiti ya baba yake kwa dawa isioze; waganga wakapakaa maiti ya Israeli isioze. Siku zake makumi ine zikatimizwa, kwa maana hivi zilitimizwa siku za kupakalia; Wamisri wakamulilia siku makumi ine. Na wakati siku za kumulilia zilipopita, Yosefu akawaambia nyumba ya Farao akisema*:* Kama sasa nilipata neema kwa macho yenu, musema, ninawaomba ninyi, masikioni mwa Farao kusema*:* Baba yangu aliniapiza akisema*:* Tazama, ninakufa; kaburi langu nililojichimbia katika inchi ya Kanana, pale utanizika. Basi muniruhusu nipande sasa, ninakuomba, nizike baba yangu nami nitarudi tane. Farao akasema*:* Panda na zika baba yako, sawa sawa alivyokuapiza. Yosefu akapanda kuzika baba yake; watumishi wote wa farao wakapanda pamoja naye, wazee wa nyumba yake, na wazee wote wa inchi ya Msiri, na nyumba nzima ya Yosefu, na ndugu zake, na nyumba ya baba yake; watoto wao tu, na kondoo zao na ngombe zao wakaacha katika inchi ya Goseni. Wakapanda pamoja naye magari na wapandaji farasi vilevile; na walikuwa jeshi kubwa sana. Wakafika kwa chumba cha kupeperusha cha Atadi, iliyo ngambo ya Yorodani, wakaomboleza pale maombolezo makubwa mazito sana; akaomboleza baba yake siku saba. Na wakati wenyeji wa inchi, Wakanana, walipoona maombolezo kwa sakafu ya Atadi, wakasema*:* Haya-Misuraimu, palipo ngambo ya Yorodani. Wana wake wakamufanyia sawasawa alivyowaagiza; kwa sababu wana wake wakamubeba hata inchi ya Kanana, wanamuzika kwa pango la shamba la Makipela, Abrahamu alilonunua pamoja na shamba kuwa uriti wa maziko, kwa Efuroni Muhiti mbele ya Mamure. Yosefu akarudi kwa Misri, yeye na ndugu zake, na wote waliopanda pamoja naye kuzika baba yake, nyuma ya kuzika baba yake.

Na wakati ndugu za Yosefu walipoona ya kama baba yao amekufa, wakasema*:* Labda Yosefu atatuchukia naye atatulipa mabaya yote tuliyomutendea. Wakatuma kwa Yosefu wakisema*:* Baba yako aliagiza mbele ya kufa kwake akisema*:* Hivi*:* Samehe, ninakuomba sasa, kosa la ndugu zako na zambi yao, wakiwa mutamwambia Yosefu wamekutendea vibaya. Na sasa tunakuomba, samehe kosa la watumishi wa Mungu wa baba yako. Yosefu akalia wakati waliposema naye. Ndugu zake, wakakwenda vilevile, wakaanguka mbele ya uso wake; wakasema*:* Tazama, sisi ni watumishi wako. Yosefu akawaambia*:* Musiogope; mimi ni pahali pa Mungu? Nanyi, mulikusudu mabaya juu yanga, lakini Mungu alikusudu mema yafanywe, kama ni leo, kuponyesha uzima wa watu wengi. Kwa hivi sasa musiogope, nitawakulisha ninyi, na

watoto wenu. Akawafariji, akasema vema nao. Na yosefu alikaa kwa Misri, yeye na nyumba ya baba yake; Yosefu akaishi miaka mia moja na kumi. Yosefu akaona wana wa Efuraimu, hata uzazi wa tatu; wana wa Makiri vilevile mwana wa Manase wakazaliwa juu ya magoti ya Yosefu. Yosefu akawaambia ndugu zake*:* Ninakufa, lakini hakika Mungu atawaangalia ninyi, na kuwapandisha ninyi toka inchi hii hata inchi aliyoapia Abrahamu, Asaka na Yakobo. Yosefu akaapiza wana wa israeli, akisema*:* Hakika Mungu atawaangalia ninyi, na mutabeba mifupa yangu toka hapa. Hivi Yosefu akakufa, mwenye miaka mia moja na kumi, wakapakaa maiti yake isioze, akatiwa ndani ya sanduku katika Misri.

Prokimenon. Sauti ya inne. Zaburi 124.

Wenye kutumainia Bwana, ni kama mulima Sayuni.

Shairi*:* Usiweza kutikisika, lakini unakaa milele. Kama milima inavyozunguka Yerusalema.

Somo ya Mezali tutasoma (31, 8-31).

Fungua kinywa chako kwa ajili yake aliye bubu, kwa maneno ya wote walioachwa peke yao. Fungua kinywa chako, hukumu kwa haki, na pata masikini ni wenye hitaji haki yao. Mwanamuke mwema, nani nayeweza kumwona? Mana bei yake inapita mbali bei ya marijani. Moyo wa mume wake unamwamini, naye hatakosa kupata faida. Anamutenda mema wala si mabaya siku zote za maisha yake. Anatafuta sufa na kitani, na kufanya kazi yake ya mikono kwa moyo tayari. Yeye ni kama merikebu za biashara; analeta chakula chake toka mbali. Anaamka unganli usiku na kuwapa watu wa nyumba yake chakula, na vijakazi wake sehemu zao. Anaangalia shamba na kulinunua*:* Kwa mapato ya mikono yake anapanda shamba la mizabibu. Anajifungia nguvu viunoni kwa uwezo, na kutia mikono yake nguvu. Anaona kama biashara yake ina faida*:* Taa yake haizimiki usiku. Anatia mikono yake juu ya kusokota, na mikono yake inashika pia. Ananyosha mikono yake kwa masikini*:* Ndiyo, ananyosha mikono yake kwa wenye hitaji, Haogopi theluji kwa watu wa nyumba yake; Maana wote wa nyumba yake wanavikwa nguo nyekundu. Anajifanyia mazulia ya urembo; Mavazi yake ni kitani safi na urujuani. Mume wake anajulikana malangoni, wakati anapoketi katikati ya wazee wa inchi. Anafanya mavazi ya kitani na kuyauza; na kuwapa wafanya biashara mishipi. Nguvu na adabu ni mavazi yake, anacheka wakati unaokuja. Anafungua kinywa chake kwa hekima; na sheria ya wema ni katika ulimi wake. Anaangalia sana njia za watu wa nyumba yake, wala hakuli chakula cha uvivu. Watoto wake wanaondoka na kumwita heri*:* Mume wake vilevile, na kumusifu akisema*:* Binti za watu wengi wamefanya mema, lakkini wewe umewapita wote. Upendeleo unadanganya, na uzuri ni ubatli*:* Lakini mwanamuke anayeogopa Bwana ndiye atakayesifiwa. Umupe ya mapato ya mikono yake; na kazi zake zimusifu malangoni.

SIKU YA POSHO YA JUMA YA SITA
SIKU KUU YA UFUFUO YA LAZARO

Elezo*: Kisha Eksapsalmos tunaimba: Bwana ndiwe Mungu. . . » na wimbo ya Ufufuo ya Lazaro:*

Apoolitikion*. Sauti ya kwanza*

Ewe Kristu Mungu, mbele ya mateso yako ulimufufua Lazaro katika wafu na unatuonyesha ufufuo wa watu wote. Alafu na sisi kama watoto tunakamata alama ya ushindi na tunapaza sauti kwako Mshahidi wa lufu*:* Hosana juu mbinguni. Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana*. (mara tatu).*

KATHISMA YA KWANZA

Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.

Ee Kristu wetu, uliposikia huruma juu ya kulia kwa Martha na Maria, uliamuru lisukumwe jiwe la kaburi, kwa mwito wako ulifufua mufu na kuvunja milango ya Hadeze sababu ya kuweka imani yetu katika ufufuo wa watu wote. Utukufu kwa uwezo wako, ee Mwokozi,

utukufu kwa mamlaka wako kubwa, utukufu kwako ambaye kwa neno lako unasabitisha dunia yote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(mara ingine).*

Elezo*: Sasa tunaimba:* **MAHIMIDI YA UFUFUO YA KRISTU (EVLOGITARIA)**

KATHISMA WA MBILI

Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon.

Ewe Chemchem ya hekima na maarifa ya milele, ulipofika kule Bethania, uliwauliza wale walikuwa karibu ya Martha*:* Wapi mulimuweka Lazaro rafiki yangu? Ukalia juu yake machozi ya huruma, huyu mufu wa siku ine, na ukamufufua kwa sauti yako ewe Chemchem ya uzima na Bwana wa huruma.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(mara ingine).*

Elezo*: Hatusome Evangelion ya asubui, lakini tunasoma:*

MSOMAJI*:* Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye peke yake bila zambi. Tunausujudu msalaba wako, ee Kristu, tena tunausifu na kuutukuza ufufuo wako takatifu. Kwa kuwa wewe Mungu wetu, la wewe peke yako hatumjui mwengine, jina lako tunaliita. Njoni enyi waaminifu wote, tuusujudu ufufuo takatifu wa Kristu. Kwa kuwa. je! Kwa ajili ya msalaba umefika furaha katika dunia mzima. Tukimhimidi Bwana daima, tunasifu ufufuo wako; kwa sababu akiuvumilia masalaba kwa ajili yetu, aliangamiza kifo kwa kifo chake.

ZABURI 50 (51)

KANUNI YA LAZARO

Wimbo wa kwanza.

Sauti ya mnane.

IRMOS: Tumuimbie Bwana wimbo wa ushindi yeye aliyevukisha zamani watu wake Bahari Nyekundu, maana amevaa utukufu.

Elezo*: Mbele ya kila wimbo tunaimba:* Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Lazaro alifufuliwa toka wafu kwa alama yako, ewe Chemchem ya uzima, mpenda-wanadamu.

Kwa neno lako siku ya ine ulimufufua Lazaro, ewe Mungu wa milele, kwa uwezo wako uliharibu ufalme wa Hadeze.

Ee Bwana, kwa kuwaonyesha watu wote umungu wako kubwa, ulifufua katika wafu Lazaro aliyelala tangu siku ine.

Leo Bethania inatangulia kutukuza Ufufuo wa kristu Chemchem ya uzima; inashangilia Lazaro mfufuliwa.

Wimbo ingine. *Sauti ya mnane. Igran diodefsas.*

Ee Kristu ulijepata mwili kwa Bikira, kama mutu ulitaka kujua fasi gani alipumzika Lazaro, lakini kama ulijua wapi alikuwa.

Ee Neno, kwa kuweka imani yetu katika Ufufuo wako, ulifufua rafiki yako kaburini yeye alikufa tangu siku ine kama katika usingizi.

THEOTOKION

Makundi ya Malaika na ya wanadamu wanakuimbia daima, ee Mama usiyeolewa, kwani mikononi mwako ulibeba Muumba wa ulimwengu kama mtoto.

IRMOS: Walipovuka bahari pakavu na kukimbia utumwa wa Wamisri, Waisraeli walipata sauti na kusema*:* Tumuimbie Mungu wetu alitukomboa.

Wimbo ya tatu. *Sauti ya mnane. Si i to stereoma.*

IRMOS: Wewe ni boma la wale wenyi kukukimbilia wewe, wenyi kukaa katika giza wanapata kwako nuru yao na roho yangu inakuimbia, ee Bwana.

Mwokozi, ulionekanisha hali zako mbili na nguvu zako mbili kwa umungu wako na kwa ubinadamu wako.

Zimu ya maarifa na Chemchem ya uzima, unauliza wapi eko huyu utafufua katika wafu.

Wewe ni Bwana, unabadilisha wakati iliwekwa kwa mipaka ya wanadamu, wewe uliye Mungu wa milele mwenyi kujaza ulimwengu.

Ee Kristu, kwa neno lako takatifu ulifufua Lazaro, na mimi makosa mengi yaliua nakuomba unifufue.

Wimbo ingine. Uranias apsidos. *Sauti ya mnane.*

Bwana ku Bethania ulikuja ku kaburi ya Lazaro na ulilia kama ilivyo kanuni ya wanadamu, ee Mungu Mwokozi, sababu ya kuweka imani yetu katika ukweli wa umwilisho wako.

Mwokozi, kwa kuonyesha uwezo wako, uliisha kilio cha Martha na Maria, kwani, kama ulivyosema, wewe kweli ni ufufuo, Uzima na bwana wa ulimwengu.

Ee Bwana, ulimuondoa Lazaro rafiki yako katika nafasi ya giza ya Hadeze na kwa neno lako lenyi uwezo kamili ulivunja makomeo na kuharibu ufalme wa mauti.

THEOTOKION

Bwana, ulipokaa tumboni mwa Mikira, ulionekana kwa wanadamu kama ilivyofaa wewe kuonekana; ee mpenda-wandamu, ulimutaja kama Mzazi-Mungu na msaada wa waaminifu.

IRMOS: Ee Bwana uliyefunika paa ya mbinguni na kujenga Eklezya katika siku tatu, unisabitishe kwa mapendo yako, peke yako mpenda-wanadamu, nafasi ya juu ya matumaini yetu na ngome ya waaminifu.

KATHISMA

Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.

Dada za Lazaro walisimama karibu ya Kristu wakilia na uchungu wakisema*:* Bwana, Lazaro amekufa, lakini Yeye mwenyewe Mungu bila kusahau kaburi yake akauliza*:* Mulimuzika wapi? Alipojongea kaburini akaita Lazaro aliyelala tangu siku ine; palepale mufu akafufuka na akasujudu mbele ya Mkombozi wako.

KATHISMA INGINE.

Sauti ya mnane. Tin sofian ke Logon.

Ewe Muumba mwenyi kutangulia kujua yote, uliwaambia Wafuasi wako*:* rafiki yetu Lazaro analala leo ku Bethania; japo iliijua, uliuza*:* Muliweka wapi? Ulimuomba Baba yako na kama mutu ulilia, kisha ulimwita ku Hadeze huyu ulipenda, ee Bwana, na ulimufufua Lazaro siku ya ine. Ndio maana tunakuambia, ee Kristu Mungu wetu*:* Pokea sifa ya wale wenyi kusubutru kukuomba na utustahiulishe utukufu wako, ee Bwana.

KONTAKION

Kristu aliye furaha ya watu wote, Ukweli, Nuru, Uzima na Ufufuo wa wandamu alionekana duniani mwetu kwa wema wake, akawa alama ya ufufuo sababu ya kuleta neema ya wokovu duniani.

IKOS

Muumba wa ulimwengu alipozungumuza na Wafuasi wake aliwaambia*:* Ndugu na wasiri, rafiki yetu Lazaro amelala; usingizi tuendeni tukaone kaburi ya Lazaro na kilio ya maria, kwa sababu nitafanya maajabu pa hii fasi, nitatimiza mwanzo wa Msalaba wangu sababu ya kuleta neema ya wokovu duniani.

SINAKSARION

Hii siku ya leo, mu Posho mbele ya Siku Kuu ya Matawi, tunashangilia Ufufuo ya Mtakatifu na mwenye haki, rafiki ya Kristu, Lazaro aliyekuwa siku ine mu kaburi yake.

KATAVASIES YA SIKU KUU YA LAZARO

Wimbo wa kwanza.

Israeli akipita Baharini, kama inchi kavu, na akikimbia ubaya wa wamisri, aliita*:* tuimbie. Mukombozi na Mungu wetu.

Wimbo wa tatu.

Ee Bwana Mjengaji, wa anga ya mbinguni, na Mujengazi wa Kanisa, unisimamishe, mapendoni mwako, utimilifu wa tamaa, msaada wa waaminifu, peke yako Mupenda-wanadamu.

Wimbo wa ine.

Nikasikia, ee Bwana, siri ya ikonomia yako, nilifahamu kazi zako, na nilitukuza umungu wako.

Wimbo wa tano.

Utuangaze, kwa amri yako ee Bwana, na kwa mukono yako munyanguliwa, utupe amani yako, ee Mupenda-wanadamu.

Wimbo wa sita.

Ninamwanga, mashitaki yangu mbele ya Bwana, ninamwonyesha taabu yangu, maana nafsi yangu ilijazwa na ubaya, na uzima wangu unakaribia Hadeze, na ninakusihi kama Yuna*:* Mungu wangu, unitoshe toka uharibifu.

Wimbo wa saba.

Watoto toka Yudea, waliofika Babyloni zamani, kwa imani ya Utatu, walishinda moto ya tanuru wakiimba*:* Mungu wa Mababu wetu, uko Mubarikiwa.

Wimbo wa mnane.

Tunamusufu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Mumwimbie, mufalme wa mbinguni, aliyeimbiwa na Majeshi ya Malaika, na mumutukuze, katika milele yote.

Wimbo wa tisa.

Sisi tunakushukuru, Muzazi-Mungu kweli, tuliookolewa kwa njia yako, tukikutukuza pamoja na Malaika.

EKSAPOSTILARION

Bwana Mungu wetu ndiye Mtakatifu. *(mara tatu).*

Ee Neno la Mungu, kwa neno lako, leo Lazaro anafurahi, anafufuka, na anaishi tena duniani; watu wanakutukuza na mingazi na matawi, kwa maana kwa lufu yako uliharibu milele ufalme wa Hadeze, ewe Mwenyezi.

Ingine, Umoja.

Ee mauti katika Lazaro Kristu anakuharibu, wapi ushindi wako? Wapi uchungu wako? Kilio ya Bethania ni wewe unailia sasa! Tunaposhika matawi yetu mikononi tuimbia wote ushindi wa Kristu.

MASIFU

Sauti ya kwanza . Idiomela.

Ee Kristu uliye uzima wetu na Ufufuo wetu, ulikua ku kaburi ya Lazaro sababu ya kusabitisha imani yetu kwa hali yako mbili, ewe Bwana mvumilivu uliyezaliwa kwa Bikira Mtakatifu kamili; kwa ubinadamu wako unauliza*:* Mulimuzika wapi? Kwa umungu wako kwa alama yenyi kuleta uzima, unafufua mufu wa siku ine.

Ee kristu, Lazaro alipokufa tangu siku ine, ulimufufua toka Hadeze*:* Mbele ya lufu yako wewe mwenyewe unaharibu nguvu ya mauti, unakomboa kaburini mumoja wa marafiki zako sababu ya kutangaza ufufuo wa wote; ndio maana tunasujudu mbele ya uwezo wako kubwa, tunapaza sauti*:* Umetukuzwa, ee Mwokozi, utuhurumie.

Martha na Maria walimuambia Mwokozi*:* Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yetu asingalikufa! Na Kristu aliye ufufuo wa wafu, akamufufua huyu mufu wa siku ine. Kujeni, waaminifu wote, tujujudu mbele yake huyu anayekuja katika utukufu kwa ajili ya wokovu wetu.

Ee kristu, uliwaonyesha Wafuasi wako alama za umungu wako, lakini watu hawakuijua kwa sababu unyenyekevu wako haukutaka kuifunua hata mara moja; kwa Mitume ulitangulia kuwaambia kama Mungu ya kwamba Lazaro amekufa; na mbele ya watu kule Bethania, kama mwanadamu ulitaka kujua wapi amelala rafiki yako; lakini huyu ulifufua siku ya ine alionyesha umungu wa uwezo wako*:* Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Sauti ya ine.

Ee Kristu, ulifufua rafiki yako siku ya ine, ukanyamazisha kulia kwa Martha na Maria, na ukawafunuliwa watu ya kama wewe kweli ni huyu ambaye kwa ushirika wako wa kimungu unajaza ulimwengu na mapenzi yako, huyu ambaye Wakheruvi wanaimbia daima*:* Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Mungu mkubwa, utukufu kwako.

Martha alimwambia Maria*:* Mwalimu amekuja na anakuita wende ukutane naye! Akaenda wepesi mahali alipokuwa Bwana na alipomuona akapaza sauti akainama, akamusujudu mbele yake, akabusu miguu yake takatifu na akamuambia*:* Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yetu asingalikufa.

Sauti ya mnane.

Kule Bethania uliamusha Lazaro toka usingizi wa siku ine*:* Tangu ulifika kaburini mufu alifufuka kwa mwito wa sauti yako; Hadeze ikatetemeka na woga na ikamuacha. Ni ajabu kweli! Ee Bwana wa mapendo, utukufu kwako.

Bwana, wakati ulimwambia Martha*:* «Mimi ni Ufufuo», ulihakikisha kwa tendo lako neno lako la ukweli wakati ulimwita Lazaro toka Hadeze. Na mimi tamaa zilinigeuza kuwa mauti nakuomba, unifufue, ewe mpenda-wanadamu na Bwana mwenye huruma.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya mbili*

Leo fumbo kubwa imetimizika! Mufu mumoja wa siku ine amefufuliwa kaburini kwa sauti ya kristu aliita rafiki yako. Tumutolee utukufu kubwa yenyi kumustahili kusudi mwenyi haki Lazaro kwa maombezi yake atupokelee sisi wokovu wa roho zetu.

Sasa na siku zote. . .

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

DOKSOLOGIA MKUBWA

SIKU YA MUNGU YA MATAWI

SIKU YA POSHO KWA MANGARIBI (ESPERINOS)

Elezo*: Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo tano, lakini tunaimba kila kimoja mara mbili, nikusema tunaanza na ma shahiri kumi.*

Sauti ya sita. Idiomelon.

Leo neema ya Roho Mtakatifu inatuanganisha na tunaposhukua Msalaba wako, sisi wote tunasema*:* «Abarikiwe Yeye anayekuja kwa jina la Bwana! Hosanna juu mbinguni». *(mara mbili).*

Huyu mwenye kutawala mbingu na inchi, Mwana na Neno la Baba anayetawala naye milele, anapanda mwana-punda anapotoka kule Bethania; wana wa Israeli wanaposhika matawi mikononi wanamushangilia wakisema*:* Hosanna juu mbinguni, abarikiwe yeye anayekuja kwa Mfalme wa Israeli. *(mara mbili).*

Leo amekuja Israeli yote mpya, sisi wote, Eklezya ya mataifa, tupaze sauti pamoja na Nabii Zakaria*:* Salamu, binti wa Sayuni, binti wa Yerusalema, umutukuze; tazama*:* Mfalme wako anajongea kwako, ni Mwokozi munyenyekevu na mwema, anapanda juu ya mwana-punda, ya huyu mwenyi muchukua nira; mtukuzeni kama watoto; munapochukua matawi mikononi, mshangilieni mukisema*:* Hosanna juu mbinguni, abarikiwe yeye anayekuja kama Mfalme wa Israeli. *(mara mbili).*

Kwa kutangulia kutuonyesha sisi Ufufuo wako takatifu, kwa amri yako, Bwana, ulifufua Lazaro rafiki yako kaburini siku ya ine kisha kufa; na ulipanda juu ya mwana-punda sababu ya kuonyesha mbele ya mataifa ushindi wa Mwokozi; ndio maana Israeli mpenda wako anakutolea sifa yake, ee Kristu, kwa kinywa oha watoto wachanga washuhuda wa kuingia kwako katika Muji takatifu siku sita mbele ya Pasha. *(mara mbili).*

Siku sita mbele ya paska yesu alikuja kule Bethania, Wafuasi wake wakamuuliza*:* Bwana, unataka tutayarishie Paska sababu ya kuikula pamoja na Wewe? Akawatuma akasema*:* «Kuendeni katika muji na mutakutana na mwanamume anayebeba mutungi wa maji. Mumufuate, na pahali atakapoingia, mumuambie mwenye nyumba*:* «Mwalimu anakwambia*:* Ni kwakonitakula Paska na Wafuasi wangu».

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya sita.*

Leo neema ya Roho Mtakatifu inatuanganisha na tunaposhukua Msalaba wako, sisi wote tunasema*:* «Abarikiwe Yeye anayekuja kwa jina la Bwana! Hosanna juu mbinguni».

Sasa na siku zote. . . *(mara ingine).*

KUINGIA

Mwangaza upole

PROKIMENON

Bwana anatawala, amevikwa utukufu *(mara tatu).*

Somo ya Mwanzo tutasoma (49, 1 na 8-12)

Yakobo akaita wana wake, akasema*:* Mujikusanye nipate kuwaambia ninyi yatakayowapata ninyi siku za mwisho*:* Mujikusanye, musikie, ninyi wana wa Yakobo; na musikilize Israeli baba yenu. Yuda, ndugu zako watakusifu ; Mukono wako utakuwa shingoni mwa adui zako ;Wapa wa baba yako watainama mbele yako. Yuda ni mwana-simba. Toka mawindo, mwana wangu,

umepanda; Akainama, akajificha kama simba, na kama simba muke ; nani atakayemushutusha? Fimbo haitaondoka katika Yuda, wala gongo la mutawala kati ya miguu yake Hata Shilo anakuja. Na kwake kutii kwa watu kutakuwa. Akifungia muzabibu kipunda chake, na muzabibu muzuri sana mwana-punda wake; Amevua mavazi **y**ak**e k**wa mvinyo, na nguo zake kwa damu ya zabibu. Macho yake yatakuwa mekundu kwa mvinyo; na meno yake meupe kwa maziwa.

Somo ya Unabii Zefania tutasoma. (3, 14-19).

Imba ee Binti ya Sayuni; paza sauti, ee Israeli, furahi na kushangilia kwa moyo wote, ee Binti ya Yerusalema. Bwana ameondosha hukumu zako, ametupa inje adui yako; mufalme wa Israeli, hata Bwana, ni katikati yako; hutaogopa ubaya tena. katika siku ile itaambiwa kwa Yerusalema*:* Usiogope, ee Sayuni, mikono yako isilegee. Bwana, Mungu wako ni katikati yako mwenye uwezo kuokoa; atafurahi juu yako kwa furaha, atapumzika katika mapendo yake, atafurahi juu yako na kuimba. Nitawaokota wanaohuzinishwa kwa kusanyiko la dini, walio wa kwako; muzigo juu yake ulikuwa laumu kwao. Tazama, kwa wakati ule nitapatiliza wote waliokutesa; na nitaokoa mwenye kuchechemea, na kuokota mwenye kufukuzwa, na nitawafanyia kuwa sifa na jina, wale waliokuwa na haya katika ulimwengu wote.

Somo ya Unabii ya Nabii Zekaria tutasoma (9, 9-15)

Furahi sana , ee Binti ya Sayuni; piga kelele, ee Binti ya Yerusalema, tazama Mfalme wako anakuja kwako; mwenye haki, na akiwa na wokovu, mwenye unyenyekevu na anapanda kipunda, hata mwana wa punda. Na nitakatilia mbali gari toka Efuraimu, na farasi toka Yerusalema, na upinde wa vita utakatika; naye atawaambia mataifa salama, na mamlaka yake itakuwa toka bahari hata bahari, na toka Muto hata miisho ya dunia. Hata kwa wewe vilevile, kwa sababu ya damu ya agano lako nimetoa wafungwa wako toka shimo linalokosa maji. Geukeni kwa boma la nguvu, ninyi wafungwa wa tumaini; hata leo, ninashuhudu ya kama nitakurudishia mara mbili. Kwa maana nimejikunjia Yuda, nimejaza upinde wa Efuraimu, nami nitaamsha wana wako, ee Sayuni, juu ya wana wako. Ee Yunani, na nitakufanya kama upanga wa mutu wa uwezo. Na Bwana ataonekana juu yao, na mushale wake utatoka kama umeme; na Bwana Mungu atapiga baragumu, naye atakwenda kwa pepo za kuzunguka za kusini. Na Bwana wa majeshi atawalinda; nao watamezameza, kukanyaga mawe ya kombeo; nao watakunywa na kufanya kelele kama kwa mvinyo; na watajaa kama mabakuli, kama pembe za mazabahu. Na Bwana Mungu wao atawaokoa kwa siku ile kama kundi la watu wake; kwa maana watakuwa kama mawe ya taji, yamenyanyuliwa juu ya inchi yake. Kwa maana wema wake ni mukubwa sana, na uzuri wake ni mukubwa sana! Nafaka itafanyiza vijana kusitawi, na mvinyo mpya wasichana.

L I T I A

Sauti ya kwanza. Idiomelon.

Kama Roho Mtakatifu alivyowafundisha Mitume kusema luga za kigeni, kwa watoto waliwaongoza kuimba*:* «Hosanna juu mbinguni, abarikiwe Yeye anayekuja kama Mfalme wa Israeli.

Mwana na Neno la Mungu mwenyi kutawala milele pamoja na Baba anakuja leo mwenyi kukaa juu ya mwana-punda katika muji wa Yerusalema; yeye ambaye hata Wakheruvi hawasubutu kutazama watoto wanamutukuza na mingazi na matawi, wakiimba sifa yake kwa siri*:* Hosanna juu mbinguni, abarikiwe Yeye anayekuja kuokoa wanadamu.

Bwana, siku sita mbele ya Paska sauti yako ilisikilika mpaka chini ya Hadeze kule ulifufua Lazaro siku ya ine; Wana wa Waebrania walikulalamikia*:* Hosanna, Mungu wetu, utukufu kwako.

Sauti ya mbili.

Bwana, wakati uliingia katika Muji takatifu, ukijiharakisha kwenda ku Mateso yako sababu ya kutimiza Sheria na manabii, Wana wa Waebrania walitangulia kuonyesha Ufufuo wako wa ushindi, wakakutangulia mbele na matawi na mingazi wakisema*:* «Umetukuzwa, ee Mwokozi! Utuhurumie.

Utukufu kwako, ee Kristu, wewe mwenye kukaa juu mbinguni, na sasa umeongojewa na Msalaba wako heshimiwa; binti wa Sayuni anafurahi, watu wa dunia wanashangilia na furaha, watoto wanatikisa matawi, Wafuasi wanatandika nguo zao, ulimwengu wote inafunza kukuimbia*:* Umetukuzwa, ee Mwokozi! Utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya tatu.*

Siku Sita mbele ya Paska Yesu alikuja ku Bethania kumufufua Lazaro siku ya ine kisha kufa kwake na kutangaza Ufufuo; dada za Lazaro, Martha na maria, wakuenda kukutana naye na wakamwambia*:* «Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yetu asingalikufa». Lakini Bwana akawajibu*:* «Yeye anayeniamini mimi, ijapokuwa anakufa, ataishi! Sikuwaambia ninyi hivi? Munionyesha wapi mulimuweka! Na Muumba wa ulimwengu kwa sauti kubwa akaita*:* «Lazaro, toka inje na kuja hapa».

APOSTIKHA

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Salamu, ewe Muji wa Sayuni, cheza kwa furaha, ewe Eklezya ya Mungu, kwani tazama Mfalme wako anakuja kwako katika upole na unyenyekevu, Watoto wanamutukuza wakiimba*:* «Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Bwana wa map[endo, utuhurumie.

Shairi: Kinywa cha watoto, watoto wadogo, kinafunguka sababu ya kutukuza ufalme wako kubwa.

Mwokozi alikuja katika muji wa Yerusalema sababu ya kutimiza Maandiko leo, watu walitandika nguo zao njiani na walishika mingazi na matawi, walitambua ya kama ni Mungu wetu, kwa sababu Wakheruvi wanaimba daima mbele yake*:* «Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Bwana wa mapendo, utuhurumie».

Shairi: Bwana Mungu wetu, jina lako ni kubwa duniani kote.

Wewe mwenyi kukaa juu ya kiti cha ufalme cha Wakheruvi na wanaimbia Waserafi, ulipanda juu ya punda kama Daudi. Watoto wanakuimbia kama Mungu, Wafarisayo wanakufuru bila haki, na kupanda kwako juu ya nyama na mfano wa kuamini kwa wapagani. utukufu kwako, ee Kristu, peke yako mpenda-wanadamu na Bwana mwenye rehema.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya sita.*

Leo neema ya Roho Mtakatifu inatuanganisha na tunaposhukua Msalaba wako, sisi wote tunasema*:* «Abarikiwe Yeye anayekuja kwa jina la Bwana! Hosanna juu mbinguni».

Padri: Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

Msomaji: Amina. Mungu Mtakatifu. Mweza Mtakatifu. Msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie, *(mara tatu).* . . Baba yetu. . .

Apolitikion. *Sauti ya kwanza*

Ewe Kristu Mungu, mbele ya mateso yako ulimufufua Lazaro katika wafu na unatuonyesha ufufuo wa watu wote. Alafu na sisi kama watoto tunakamata alama ya ushindi na

tunapaza sauti kwako Mshahidi wa lufu*:* Hosana juu mbinguni. Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana*. (mara mbili).*

Apolitikion ingine. *Sauti ya ine.*

Ewe Kristu Mungu wetu, tulipozikwa pamoja nawe katika ubatizo, tulistahili uzima wa milele katika Ufufuo wako, na tunapaza sauti katika wimbo*:* Hosana juu mbinguni, Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana*. (mara moja).*

SIKU YA MUNGU ASUBUI. SIKU KUU YA MATAWI

Elezo*: Kisha Eksapsalmos, tunaimba Apolitikia ya jana Mangaribi.*

KATHISMA YA KWANZA

Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.

Tunapochukua matawi rohoni na roho yenye kutakaswa, kama watoto zamani tumushangilie Kristu na imani. Tumwambie kwa Sauti kubwa*:* Umetukuzwa wewe Mwokozi unayekuja katika hii dunia kuokoa Adamu toka laana ya zamani na ulitaka kuwa Adamu mupya rohoni; ewe Neno uliyefanya yote juu ya kutuokoa, mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

KATHISMA INGINE.

Sauti ya ine. Epefanis simeron.

Bwana, ulipofufua Lazaro kaburini tangu siku ine, unatufundisha kukulalamikia na mingazi na matawi*:* Abarikiwe Yeye anayekuja!

KATHISMA WA MBILI.

Sauti ya ine. Kateplagi Iosif.

Ee Kristu, unalia machozi juu ya rafiki yako, unafufua Lazaro kaburini toka wafu, unaonyesha huruma yako, ee Mwokozi, na watoto wengi waliposikia kuja kwako, wanakuja leo na matawi mikononi kukulalamikia*:* Hosanna! Abarikiwe yeye anayekuja kuokoa wanadamu.

KATHISMA INGINE

Sauti ya kwanza. Tu lithu sfragisthentos.

Ninyi mataifa na watu, imbani kwa sauti moja*:* «Mfalme wa Malaika anakuja, mwenyi kupanda juu ya mwana-punda sababu ya kushinda adui kwa uwezo wa Msalaba, na watoto wanapochukua matawi wanamulalamikia*:* «Utukufu, ushindi na shangilia! Utukufu kwako, ee Kristu Mwokozi, utukufu na sifa kwa Mungu wetu peke yake.

Elezo*: Kisha Polieleo tunaimba Kathisma hii:*

KATHISMA

Sauti ya mnane. To prostakthen.

Yeye mwenyi kukaa juu ya kiti cha Wakheruvi na kwa ajili yetu anapanda leo juu ya mwana-punda anasikia Watoto wakimulalamikia*:* Hosanna! Na watu wakipaza sauti*:* Umetukuzwa, Mwana wa Daudi! Okoa wepesi wale mikono yako iliumba, kwani ul;ikuja kufunua utukufu wako kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(mara ingine)*

KONDAKION. *Sauti ya sita.*

Ewe Kristu Mungu wetu, unashuka toka kiti cha mbinguni na unatembea katika inchi juu ya punda, unapokea wimbo wa Malaika na wale watoto wa wayuda, wote wanakupazia sauti*:* Ndiwe Mbarikiwa anayekuja kumurudisha Adamu.

IKOS

Ee Bwana msiyekufa uliyeshinda Hadeze uliyeshinda mauti na kufufua dunia yote, ee Kristu, watoto wanapochukua matawi wanatukuza ushindi wako na wanakulalamikia leo*:* Hosanna Mwana wa Daudi! Hata mara moja watoto hawatauawa juu ya mwana wa Maria; lakini kwa ajili ya wokovu wa wote, wakubwa na watoto, wewe peke kwa kutaka kwako utasulubiwa; hata mara moja upanga haitatukata, kwa sababu mkuki itachoma ubavu wako; ndio maana kwa furaha tunasema*:* Abarikiwe yeye anayekuja kuondoa Adamu kaburini.

SINAKSARION

Hii siku ya leo, Siku ya Mungu wa Matawi, tunashangilia Siku Kuu kitukufu ya kuingia Bwana wetu Yesu Kristu mu muji Yerusalema.

Katika wema wako kubwa, ee Kristu Mungu wetu, utusaidie tushindi zambi zetu yasiyoakili na utustahili tuone ufufuo wako wa furaha na ubebaji-uzima na utuhurumie.

KATAVASIA SIKU YA MUNGU YA WATAWI.

Wimbo ya kwanza. *Sauti ya ine.*

Chemchem za kuzimuni zilizuia wimbi lao, pofu ya bahari haifiiiche misingi yake; kwa alama moja ulirudisha nyuma sababu ya kuokoa taifa lako teule lenyi kukuimbia, ee Bwana, wimbo wa ushindi.

Wimbo ya tatu.

Waisraeli walikunywa maji ku mwamba gumu kabisa ambao kwa amri yako ukageuka kuwa chemchem; na Wewe mwenyewe, ee Kristu, ndiwe mwamba wa uzima wetu; na juu ya mwamba huo palijengwa Eklezia yenye kukulamikia*:* Hosana, Bwana unayekuja, umetukuzwa.

Wimbo ya ine.

Kristu anayekuja na mwenye kufunuliwa kama Mungu wetu atafika bila kukawia*:* alipozaliwa kwa Bikira asiyeolewa ametokaa ku mlima wa kivuli kama alivyosema Nabii zamani, na tunaunganisha masauti yetu sababu ya kuimba*:* Utukufu ku uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya tano.

Kuja utangaze mlimani wa Sayuni habari njema ya Yerusalema, paza sauti kwa kutangaza utukufu unaokuja ku mji wa Mungu*:* Amani kwa Israeli na wokovu ku mataifa.

Wimbo ya sita.

Moya wa wenye haki unafurahiwa*:* Kwa ulimwengu inanza angano Jupya*:* Agano inabadirika kwa damu ya Mungu.

Wimbo ya saba.

Ku tanuru ya moto ukawaokoa waana wa Abrahamu, ukama wakaldea kwa moto waliyotayarisha wenyewe. Bwana mstahili kamili wa nyimbo zetu, Mungu wa Baba zetu, umetukuzwa.

Wimbo ya mnane.

Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

FurahiwaYerusalema, shangilieni, ninyi munaopenda Sayuni*:* Huyu anayetawala milele Bwana wa majeshi, amekuja, ulimwengu uiname mbele yake, dunia iimbe mbele yake*:* Viumbe vyote vya Bwana, tukuzeni Bwana.

Wimbo ya tisa.

Bwana ni Mungu, ameonekana kwetu, shangilieni hii Siku Kuu, na katika furaha nujeni, tutukuzeni Kristu na mitende na matawi*:* tumulalamikie na furaha*:* Mbarikiwa anayekuja kwa Jina la Bwana Mwokozi wetu.

EKSAPOSTILARION

Bwana Mungu wetu ndiye Mtakatifu. *(mara tatu).*

MASIFU

Sauti ya ine. Idiomelon.

Bwana, watu wengi walitandika nguo zao njani ulimopita; wengine walikata matawi sababu ya kuiweka njiani; makundi ya watu waliyokutangulia na wale waliyokufuata walikusindikiza wakiimba*:* Hosanna Mwana wa Daudi, abarikiwe yeye anayekuja na atakayekuja kwa jina la Bwana. *(mara mbili)*

Bwana, kwa kuingia kwako katika muji takatifu, watu wengi waliyochukua matawi, walipokuimbia kama Rabi wa ulimwengu na walipokuona umeketi juu ya mwana-punda kama juu ya kiti cha Wakheruvi, wakakuimbia wakisema*:* «Hosanna juu mbinguni, Abarikiwe yeye anayekuja na atakayekuja kwa jina la Bwana. *(mara mbili).*

Kujeni, watu na mataifa, tazameni leo Mfalme wa mbinguni*:* kwa unyenyekevu amekaa juu ya mwanza-punda, anaenda kule Yerusalema kama juu ya kiti cha ufalme cha juu kabisa; enyi mataifa, tazameni Bwana anayejifanya mutu sababu ya kutuokoa kama ilivyo aguzi ya nabii Isaya. Tazama Bwana-arusi wa Sayuni mupya, na kwa ajili ya hii ndoa sadi na takatifu kundi la watoto wengi safi wanakimbia mbio wakiimba; na sisi pia kama malaika, tutaimba*:* Hosanna juu mbinguni, abarikiwe yeye anayetuletea wokovu.

Ee kristu Mungu wetu, mbele ya Mateso yako kwa kusabitisha imani ya ufufuo wa wote, kwa uwezo wako ulifufua Lazaro siku ya ina kule Bethania na iliponyesha vipofu, ee Mwokozi Chemchchem ya nuru. Kisha uliingia pamoja na Wafuasi wako katika Muji takatifu, ee Bwana, mwenyi kukaa juu ya mwana-punda kama juu ya kiti cha ufalme cha Wakheruvi sababu ya kutimiza manabii, watoto wa Waebrania wenyi kuchukua matawi walikusindikiza na sisi pia tunapochukua matawi, kwa shukrani tunakuimbia*:* Hosanna juu mbinguni, abarikiwe yeye anayekuja kwa jina la Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *Sauti ya sita.*

Siku sita mbele ya paska yesu alikuja kule Bethania, Wafuasi wake wakamuuliza*:* Bwana, unataka tutayarishie Paska sababu ya kuikula pamoja na Wewe? Akawatuma akasema*:* «Kuendeni katika muji na mutakutana na mwanamume anayebeba mutungi wa maji. Mumufuate, na pahali atakapoingia, mumuambie mwenye nyumba*:* «Mwalimu anakwambia*:* Ni kwakonitakula Paska na Wafuasi wangu».

SIKU YA MUNGU YA MATAWI MANGARIBI

Elezo*: Kisha» «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo sita, kila kimoja mara mbili:*

Sauti ya mnane. Idiomelon.

Salamu, ewe Muji wa Sayuni, cheza kwa furaha, ewe Eklezya ya Mungu, kwani tazama Mfalme wako anakuja kwako katika upole na unyenyekevu, Watoto wanamutukuza wakiimba*:* «Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Bwana wa mapendo, utuhurumie.

Mwokozi alikuja katika muji wa Yerusalema sababu ya kutimiza Maandiko leo; Watu walitandika nguo zao njiani na walishika mingazi na matawi, walitambua ya kama ni Mungu wetu, kwa sababu Wakheruvi wanaimba daima mbele yake*:* «Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Bwana wa mapendo, utuhurumie.

Salamu, ewe Muji wa Sayuni, cheza kwa furaha, ewe Eklezya ya Mungu, kwani tazama Mfalme wako anakuja kwako katika upole na unyenyekevu, Watoto wanamutukuza wakiimba*:* «Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Bwana wa mapendo, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Salamu, ewe Muji wa Sayuni, cheza kwa furaha, ewe Eklezya ya Mungu, kwani tazama Mfalme wako anakuja kwako katika upole na unyenyekevu, Watoto wanamutukuza wakiimba*:* «Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Bwana wa mapendo, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Salamu, ewe Muji wa Sayuni, cheza kwa furaha, ewe Eklezya ya Mungu, kwani tazama Mfalme wako anakuja kwako katika upole na unyenyekevu, Watoto wanamutukuza wakiimba*:* «Hosanna juu mbinguni, umetukuzwa, ee Bwana wa mapendo, utuhurumie.

KUINGIA

Mwangaza upole

PROKIMENON YA SIKU.

APOSTIKHA

Sauti ya mbili. Idiomelon.

Enyi waaminifu, tunapotoka katika shangilio ya Matawi na kuingia katika Shangilio tukufu na ya wokovu ya Mateso ya Kristu, tumuone akijitoa kwa ajili yetu kwa Mateso yake ya kutaka na kwa shukrani tumuimbie*:* ee Chemchem ya mapendo na bandari ya wokovu, Bwana, utukufu kwako.

Shairi: Muimbieni Bwana wimbo mupya, kwa maana ametenda maajabu.

Sauti ya tatu

Ni ajabu kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai! Kwa maana anatuambua mawazo yetu na siri za roho zetu. Mutu hata mumoja asijaribu usabiti yake safi! Lakini kwa woga na unyenyekevu tumuendee krtistu sababu ya kupata kwake msaada na neema ya wokovu.

Shairi: Mipaka yote ya dunia yaliona wokovu wa Mungu wetu.

Sauti ya saba.

Yerusalema, washa taa yako sababu ya kupokea Bwana atakuja katikati ya usiku kama Bwana-Arusi, fanya agano mupya pamoja naye, ee Sayuni mupya, kwa ahadi utakayoriti. Apana inje ya kuta zako, ee Yerusalema, atateswa na kufa huyu Baba alituma, huyu Manabii walitangaza kama Mwana wake na anayekuja kutimiza manabii, huyu watoto walitukuza wakisema*:* Hosanna Mwana wa Daudi, abarikiwe Yeye anayekuja kwa jina la Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . .

Enyi waaminifu, tunapotoka katika shangilio ya Matawi na kuingia katika Shangilio tukufu na ya wokovu ya Mateso ya Kristu, tumuone akijitoa kwa ajili yetu kwa Mateso yake ya kutaka na kwa shukrani tumuimbie*:* ee Chemchem ya mapendo na bandari ya wokovu, Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . *Sauti ya tatu.*

Ni ajabu kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai! Kwa maana anatuambua mawazo yetu na siri za roho zetu. Mutu hata mumoja asijaribu usabiti yake safi! Lakini kwa woga na unyenyekevu tumuendee krtistu sababu ya kupata kwake msaada na neema ya wokovu.

NYIMBO ZA UTATU MTAKATIFU NA FOTAGOGIKA

WAKATI YA TRIODE MBELE YA PASKA.

Kila mwaka Kanisa yetu Orthodokse iko na wakati ya Kwarezima mkubwa mbele ya siku Kuu ya Paska. Ile wakati ya ma siku makumi ine, kila siku ya kila Juma, bila siku ya Posho na siku ya Bwana, tunaimba, kisha Eksapsalmos, wimbo ingine. Nikusema pa ile fasi tunaimba: «Bwana ndiwe. . . » hii wakati ya Kwarezima tunaimba Alliluia, Alliluia, Alliluia, mara ine. Kisha tunaimba Apolitikia ya Watakatifu, lakini zile nyimbo za Utatu Mutakatifu katika sauti ya ile Juma.

Ya kuimba wakati ya kwarezima mkubwa ya sauti ya wakati kwa mwimbo ya kwanza (ya Utatu) ku mwisho yake na ku mwisho ya mwangaza (Fotagogikon) tunaimba hivi:

Kila mu kazi moya: kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Mukazi mbili: Kwa maombi ya Mtakatifu Mubatizaji Yoane, utuhurumie.

Mukazi Tatu: Kwa nguvu ya Musalaba wako na utuokoe.

Mukazi Ine: Kwa maombi ya Wamitume wako, utuhurumie.

Mukazi Tano*:* Kwa nguvu ya Musalaba wako na utuokoe.

Mu Posho: Hatuimbe Nyimbo ya Utatu Mtakatifu na Fotagogikon. Tunaimba kisha Eksapsalmos: «Bwana ndiwe Mungu. . . » *pamoja na Shairi ya Ine ya Zaburi na kisha wimbo ya Wafu. Iko ndani ya hii kitabu Triodi.*

SAUTI YA KWANZA

Ya Utatu

Kwa umbo ya Majeshi ya Wabila-mwili tumefika ku hali isiyo mwili na ya kiroho, na kwa wimbo wa Trisayion tulipokea nuru ya umungu katika watu tatu; tuimbe pamoja na Wakeruvi kwa ajili ya Bwana wetu peke Yake*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu Wetu, kwa ulinzi wa Malaika utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Pamoja na Majeshi ya mbinguni, kama Wakeruvi tumuimbie Aliye-Juu, tukiimba sifa ya Trisayion*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu Wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Tukiamka usingizini, tunasujudu mbele Yako na pamoja na Malaika tunasema tena wimbo*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

FOTAGOGIKON.

Ee Kristu unayeonekanisha nuru, takasa roho yangu ku zambi yo yote kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

SAUTI YA PILI

Ya Utatu

Sisi duniani tunayofananishwa Majesi ya Juu mbinguni, tunakotolea wimbo wa ushindi tukiimba*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Hali isiyoumbwa Fundi wa ulimwengu, mungua midomo yetu na kinywa chetu kitatangaza sifa yako pakuimba*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Bwana uliyeniamusha usingizini mwangu, angaza moyo wangu na roho yangu, fungua midomo yangu ili ni kuimbie, ee Utatu Mtakatifu*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wangu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

FOTAGOGIKON

Tuma nuru yako ya milele, ee Kristu Mungu wetu, angaza macho yangu na moyo wangu kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

SAUTI YA TATU

Ya Utatu

Utatu wa asili moja na usiyogawanyika, Umoja katika watu tatu wa milele, pamoja na Malaika tunakuimba, ee Bwana*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Baba wa milele, Bwana wa milele pia, Roho Mtakatifu anayegawanya umilele wa Mungu mmoja, pamoja na Wakeruvi tunasubutu kukutukuza tukisema*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Mwamzi atakuja kama umeme kufumia matendo ya kila mmoja; na woga tunakuimbia katikati ya usiku*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu utuhurumie.

FOTAGOGIKON

Tuma nuru yako, ee Kristu MUngu wetu, angaza moyo wangu kwa maombi ya Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

SAUTI YA INE

Ya Utatu

Pamoja na watumishi wako wa mbinguni, sisi wenye mauti tunasubutu kukuimbia*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi ya Malaika utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Kama jeshi la Malaika mbinguni, na woga duniani tunakutolea wimbo huu wa ushindi, ee Bwana*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Pamoja na Baba yako wa milele na Roho Mtakatifu Kamili, ee Kristu Mungu, tunasubutu kukutukuza kama Wakeruvi tukisema*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

FOTAGOGIKON

Wewe unayeleta nuru duniani, angaza roho yangu ukiitakasa ku zambi yo yote kwa ulinzi ya Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

SAUTI YA TANO

Ya Utatu

Ni Malaika wa kuimba na kuomba, bila kwacha tumulalamikie Bwana*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi ya Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Tunaposubutu kuwafananisha Majeshi ya mbinguni japo masauti yetu yasiostahili tunakuimbia, ee Utatu wa milele*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Ee Kristu uliyekaa tumboni mwa Bikira bila kutengana na kifua cha Baba, pokea sauti yetu pamoja na ile ya Malaika*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

FOTAGOGIKON

Bwana, Chemchem ya nuru, tuma mwangaza wako, angaza moyo wangu kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

SAUTI YA SITA

Ya Utatu

Wakeruvi na woga, Waserafi na kutetemeka, wanaimba bila kwacha wimbo mara tatu*:* Mtakatifu; na sisi wenye zambi tunapaza sauti pamoja nao*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Wakeruvi na vinywa vyao vya mwili, Waserafi na doksologia yasipo kwacha, wanakuimbia wimbo mara tatu Mtakatifu, ee Mungu wetu, na sisi duniani namidomo yetu isiyostahili kuimba tunakutolea sifa yetu tukisema*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Tutukuzeni watu tatu wa umungu moja, wenyi kuungana bila fujo, na tunaimbatenawimbo wa Malaika tukisema*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

FOTAGOGIKON

Bwana, tuma rohoni mwangu nuru yako ya milele kwa ulinzi ya Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

SAUTI YA SABA

Ya Utatu

Bwana, Wakeruvi wanaimba juu ya utukufu wako wa juu na Malaika wanaabuduukuu wako kimungu, pokea ku midomo yetu ya zambi wimbo wetu*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Tutolee sifa tatu za Waserafi ku Umungu usiyokaribika, ku Utatu moja na tuimbe na woga na mtetemeko*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

FOTAGOGIKON

Bwana, angaza moyo wangu ili ukuimbe, unifundishe kufanya mapenzi yako kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

SAUTI YA MNANE

Ya Utatu

Tunapoinua mioyo yetu mbinguni, tufananishe Majeshi ya mbingu, tusujududu na woga mbele ya Bwana, tukimwimbia wimbo wa ushinda tukisema*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Wakeruvi bila kusubutu kunyanyua macho yao Kwako wanaimba na furaha maneno kimungu ya Trisayon; na sisi wenye zambi pia, tunapaza sauti pamoja nao*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Tunapoelemewa na uzito wa zambi zetu na tunaposubutu kuinua macho ku mbingu yako roho na mwili zenye kuinamishwa, tunaimba pamoja na Malaika*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

FOTAGOGIKON

Ee Kristu, nuru ya milele, uniangaze mimi wote kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

STIKHIRA NA KATHISMATA YA PARAKLITIKI
(TUNAIMBA KILA SIKU WAKATI YA KWAREZIMA)

SAUTI YA KWANZA

SIKU YA MUNGU MANGARIBI KU ESPERINOS

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba hii wimbo ya kutubu, kisha wimbo ya Triodio na Mineon.

Bahari ya makosa yangu ni kubwa, ee Mungu Mwokozi; nazama katika shimo la zambi*:* Kama kwa Petro mkono; uniokoe, ee Mungu wangu, na unihurumie.

Ee Mwokozi, tazama nahukumiwa kwa mawazo yangu na matendo yangu ya ukafiri; unipe nia za toba ili nikuombe, ee Mungu wangu*:* Uniokoe katika wema wake na unihurumie.

Ulimwengu ingine umekuongojea, ee roho yangu na Mwamuzi atatangaza siri zako na zambi zako; usidumu katika uovu, lakini ujiharikishe kupaza sauti*:* Ewe Mwamuzi wangu na Mungu wangu, unisamehe na uniokoe.

Ewe Mwokozi, usimzarau mtumishi wako mfungwa wa uzaifu na zambi, lakini amsha moyo wangu ku toba, unifanye kuwa mtumishi wa shamba lako la ms\zabibu, ee Bwana, ukinipa mshahara wa saa ya kumi na moja na neema ya wokovu.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA KUTUBU

Mama yangu alinichukua mimba katika zambi, na kama mpotevu sisubutu kutazama juu mbinguni, lakini mapendo yako inaniotumainia, na napaza sauti kwako*:* Ewe Mungu, unisamehe na uniokoe.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Kama mwenye haki anaokoa, wapi nitajionyesha mimi mwenye zambi? Sikuchukua wala uzito wala joto ya mchana, lakini unihesabie pamoja na wale wa saa ya kumi na moja, ee Mungu wangu, na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Muujiza wa ajabu, ee Mjaliwa neema, kiumbe kilishangilia na furaha pakukuona, bila mbegu ukapata mimba na ukamzaa namna isiyokadirika huyu ambaye Malaika mwenyewe hawawezi kutazama, ee Bikira Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Bwana, utukufu wa mashindano na taji la Washindaji, ndiwe uzuri wa Mashahidi Watukufu*:* Kwa imara yao katika majaribu wakawakimbiza makafiri na wakapokea ushindi mbinguni kwa uwezo wa Mungu; ee Bwana, kwa maombezi yao uniokoe kwa Adui msiyeonekana na uniokoe.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA KUTUBU

Sauti ya kwanza.

Ewe Bwana, ujiharikishe kunifungulia mikono yako ya ubaba, kwani nilitumia vibaya uzima wangu; tazama hazina ya huruma yako isiyokuisha, ee Mwokozi, usizarau umaskini wa moyo wangu; kwako, ee Bwana, napaza sauti nikijaa na sikitiko*:* Ee Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Korti ni ya hatari, hukumu yako ni ya haki, na matendo yangu ni mbaya; lakini wewe, Mungu wa mapendo, kuja uniokoe na kuniokoe ku azabu; ee Rabi, unilinde ku hali ya wenyi kulaaniwa, na unistahilishe nisimame kuume kwako, ewe Mwamuzi wa haki.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ulipopata mimba bila kuteketezwa na moto kimungu, na bila mbegu ulipochirikizisha Bwana Chemchem ya uzima, ee Bikira mjaliwa neema na Mzaz-Mungu, utuokoe sisi tunaotukuza.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Sauti ya kwanza. Tu Lithu sfragisthentos

Kama maaskari wema, na shauri moja katika imani, bila woga na bila lauma mbele ya vitisho vya wazuluma, Wahodari, mulienda mbele ya Kristu, mkichukua msalaba wake wa samani. Ku mwisho wa Safari na wa mashindano mukapokea ushindi wa Juu-mbinguni. Utukufu kwa huyu ambaye nguvu yake ikawa tegemeo yenu, utukufu kwa huyu aliyemivika taji, utukufu kwa huyu anayetenda ndani yenu kwa kutuponyesha.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA KUSULUBIWA

Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.

Ulipanua mikono yako Msalabani, ewe Mungu wa mapendo sababu ya kuleta watu waliyojitenga kwako kwa kutukuza wema wako mkuu; tazama urisi wako, ee Bwana, na angusha adui kwa Msalaba wako wa Samani.

Shairi*:* Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Sauti ya kwanza. Tu Lithu sfragisthentos

Ewe Mpenda-wanadamu, tunasujudu mbele ya muti ya Msalaba wako; ulisulubiwa pa hii, wewe Uzima wa ulimwengu; kwa Mnyanganyi aliyekuamini, ewe Mwokozi, ukamfungulia Paradizo; na akapata heri ya milele alipokulalamikia*:* Bwana, unikumbuke mimi; kama yeye, utupokee sisi tunaokulalamikia*:* sisi wote tumetenda zambi, usituzarau katika wema wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAYROTHEOTOKION.**

Ee Bikira, tumesabitishwa na ulinzi wako na kwa maombezi yako tumeopolewa ku hatari yote; tunapolindwa wakati wote kwa Msalaba wa Mwana wako, sisi waaminifu wako, tunakutukuza.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Kwa mateso waliyoteswa Watakatifu kwa ajili yako, tunakuomba ukubali, ewe Mungu wetu, kuponya mateso yetu yote, ee Bwana Mpenda-wanadamu.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS

KATHISMA WA MITUME.

Sauti ya kwanza. Tu Lithu sfragisthentos

Waliposhinda na tete la Msalaba na wavu wa Neno werevu wa Wasemaji, wavuvi wa watu wakaangaza mataifa ili wakutukuze kama Mungu kweli; ee Bwana, chemchem ya nguvu yao, tunakuimbia wimbo wetu wa sifa ya milele*:* Utukufu kwa Baba na kwa Mwana, utukufu kwa Roho wa asili moja, utukufu kwa huyu ambaye Mitume walileta nuru duniani.

Shairi*:* Sauti yao imeenea duniani mwote na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Wenyi Mitume wenyi hekima muliyovua ulimwengu wote na kupokea kwa Mungu mapendo yake mtuombee sisi tunaoimba sasa*:* Ee Bwana, kwa maombezi ya Mitume wako, okoa watu wako wa Kristu ukilinda roho zetu ku hatari yote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Kwa namna isiyokadirika ukamzaa bila Baba hapa chini huyu asiye na mama mbinguni; karibu yake, ee Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili wa wokovu wa roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ton tafon su Sotir.

Wote tuwaombe Mashahidi wa Kristu wenye kutupmbea wokovu wetu na wa wote, tuendeni tukutane nao katika imani kwa kupata neema na maponyesho kwa walinzi hawa wa imani wenye kukimbiza mashetani mbali.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS .

KATHISMA WA USULUBIO

Ewe Kristu, ulipopanda msalabani, uliharibu uzulumu na nguvu ya adui; apana ao Malaika ao mwanadamu aliyetuokoa, lakini ni Mungu yeye mwenyewe*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Shairi*:* Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Zamani, Silaha ya Msalaba ikafunuliwa kwa mfalme Konstantino katika vita sababu ya kuwa ukumbusho wa ushindi wa imani isiyoweza kushindwa; katika hii Mtakatifu Paulo anajitukuza, inatetemesha nguvu za Hadeze na imekuwa wokovu wa waKristu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira, tunasabitishwa na ulinzi wako, na kwa maombi yako tunaokolewa ku hatari yote na kulindwa kila wakati na Msalaba wa Mwana wako, sisi waaminifu, tunakutukuza.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Bwana, utukufu wa mashindano na taji la Washindaji, ndiwe uzuri wa Mashahidi Watukufu*:* Kwa imara yao katika majaribu wakawakimbiza makafiri na wakapokea ushindi mbinguni kwa uwezo wa Mungu; ee Bwana, kwa maombezi yao uniokoe kwa Adui msiyeonekana na uniokoe.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo ya Triodion na kisha hii wimbo ya mashahiodi:

Sauti ya kwanza.

Ewe Mungu wa mapendo, kwa maombi ya watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu utupe amani na utuhurumie.

Enyi Mashahidi kustahili sifa yote, apana dunia iliyowaficha, ni mbingu iliyowapokea; milango ya Paradizo imefunguliwa kwa ajili yenu, na huko munakuwa na mti wa uzima; muombeni Kristu alete amani na neema ya wokovu ku roho zetu.

Hakuna mtu hata mmoja hana zambi ile wewe, peke yako Msiyekufa; tena, ewe Mungu wa wema, weka watumishi wako katika nuru ya milele ili waimbe pamoja na Malaika mbinguni, na kwa rehema yako usiangalie zambi zao, lakini uwahurumie.

Utukufu kwa Baba. . . *Sauti ya kwanza.*

Wimbo ya wafu.

Furaha gani ya uzima huu inakaa bila huzuni? Utukufu gani duniani haujui mateso? Yote inafika kama kivuli na kama ndoto ya uwongo; kwa rafla, mauti inaondoa yote, lakini kwa nuru ya uso wako, ee Bwana, na kwa mapenzi ya uzuri wako, ee Kristu Mpenda-wanadamu, uwape wateule wako mapumziko.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Utukufu wa ulimwengu, uliyopandwa kwa watu, na ulizaa Bwana, mlango wa mbinguni, tumusifu Bikira Maria, wimbo wa wasiyo mwili, na pambo ya waaminifu; kwa sababu yeye alikuwa mbingu, na Hekalu la umungu; yeye alipomoa ukuta ya adui, alibadilisha kwa amani, na alifungua ufalme. Basi pakuwa na hii, nanga ya imani, tuiko na mlinzi, Bwana hivi aliyezaliwa Kwake. Kwa hivi kuwa na moyo, kuwa na moyo taifa la Mungu; kwa sababu yeye anagombanisha adui sawa mwenyezi.

SIKU YA SITA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MASHAHIDI.

Sauti ya kwanza. Tu Lithu sfragisthentos

Kama ma askari wema, wenyi shauri moja katika imani, bila woga na bila laumu mbele ya makanio ya wazulumu, wahodari, mumenjongea Kristu mkishika Msalaba wake boga. Ku mwisho wa safari na wa mashindano mukapata ushindi wa Juu-mbinguni.

Shairi*:* Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Kwa mateso waliyoteswa Watakatifu kwa ajili yako, tunakuomba ukubali, ewe Mungu wetu, kuponya mateso yetu yote, ee Bwana Mpenda-wanadamu.

Shairi*:* Watakatifu walio duniani, wao ni wale wazuri sana ninaopendezwa nao.

Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.

Wote, tuwasihi Mashahidi wa Kristu wenye kutuombea wokovu wetu, na wote tuendeni kukutana nao katika imani kwa kusamehewa na kuponyeshwa kwa walinzi hawa wa imani wenye kuwafukuza mashetani.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*
Ton tafon su Sotir.

Ee Mwokozi, pumzisha marehemu katika kundi la wenye haki, pahali pa nuru; walikutumainia wewe, ee mpenda-wanadamu; pokea ombi la kila mmoja kwa ajili ya wazazi wake na watoto wake, na kwa wema wako mkuu hakikisha wale tunakumbuka leo.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION.**

Wakati Gabrieli alisema kwako Bikira, salamu, kwa sauti; Rabi wa wote alichukua mwili, ndani yako safina takatifu, sawa mwenye haki Daudi alivyosema. Ulionekana kuwa munene sana kuliko mbingu, kwa sababu ulichukuwa Muumbaji wako. Utukufu kwa yule alikaa ndani yako; utukufu kwa yule alitoka kwako; utukufu kwa yule alitupatia uhuru, juu ya uzazi wako.

MASIFU.

Tunaimba wimbo wa ine, hii:

Njooni, enyi mataifa yote, tuimbe mashairi na nyimbo za kiroho kwa kuwatukuza Mashahidi watukufu wa kristu, Watangazaji wa imani tena taa za ulimwengu, Chemchem isiyokauka ambako kunatiririka maponyesho; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani ku dunia na neema ya wokovu ku roho zetu.

Tazama ma askari wa mfalme mkuu*:* Walishindana na amri za wazulumu wa walizarau mateso, kwa usharifu, wakakanyanga na kuvunja kosa lote; walipopokea taji walilostahili wanatupokelea amani kwa Mwokozi na neema ya wokovu kwa ajili ya roho zetu.

Mashahidi watakatifu wenye kustahili sifa yote, apana wala jaribu, wala huzuni, wala njaa, wala uzulumu, wala hatari, wala hasira ya wanyama kali, wala upanga, wala moto ambazo kwa vitisho vyao viliweza kuwatenga mbali na Mungu; lakini ni kwa mapendo kwa ajili yake mulisahau ulimwengu mukiwa wageni ku mwili wenu na mukishindana kwa kuzarau mauti; na tena mukapokea tuzo la kweli la kazi yenu, mukawa warisi wa ufalme wa mbingu*:* Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Enyi Mashahidi Watakatifu, furahini katika Bwana, kwani mumeshindana Wazulumu; wala upanga, wala vema sana; mumeshindana na wafalme na mumewashinda wazulumu; wala upanga, wala moto haukuwaogopesha ninyi, wala wanyama kali waliyorarua mwili wenu, lakini pamoja na Malaika mukamwimbia Kristu na mukapokea taji la mbinguni*:* Ombeni ili tupewe neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. *Wimbo ya wafu.*

Katika tendo lako, ee Mwokozi wangu, umeonyesha ya kama ndiwe ufufuo wa wote, Neno ambaye kwa neno lako ukamfufua Lazaro katika wafu; hapo makomeo ya kapasuka na milango ya Hadeze yakapepea, kwa watu mauti yakaonekana kama usingizi, ee Bwana uliyekuja kuokoa ulimwengu na apana kuhukumu, ee Mpenda-wanadamu, uwape wateule wako mapumziko.

Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ajabu wa maajabu, ee Mjaliwa neema, kiumbe kinafurahiwa pakuukuona; ulipata mimba bila mbegu na ulinzi huyu Malika wenyewe hawaweze kumtazama; ee Bikira Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

APOSTIKHA

Tunaimba hii wimbo ya wafu.
Sauti ya kwanza. Panefimi Martires.

Tunakuomba, ee Mungu Mwokozi*:* Kwa huruma yako uwape marehemu mapumziko na uwaweke katika hema za wenyi haki pamoja na Watakatifu wako katika uwanja wa mbinguni, na kwa huruma yako usiangalie zambi zao, lakini uwape mapumziko.

Shairi: Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

hakuna mutu hata mmoja asiye na zambi ila Wewe, peke yako Msiyekufa; tena, Mungu wa wema, weka watumishi wako katika nuru ya milele ili waimbe pamoja na Malaika mbinguni, na kwa huruma yako usiangalie zambi zao, lakini uwape maondoleo.

Shairi: Makumbusho yao ni ya milele.

Ee Mwokozi, ahadi zako ni isiyokadirika, ni vitu jicho haikuona, sikio halikusikia, na moyo wa mwanadamu haukuzania*:* Kwa huruma yako uwafundisheyo marehemu, ukiwapa uzima wa milele.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Bwana, marehemu wako ambao Msalaba wako ulikuwa nguvu na furaha yao wapate katika hii kama msaada ya zambi zao, na kwa damu heshimiwa uliyomwanga kwa ajili ya uzima wetu uwape, katika wema wako, utukufu wako na nuru yako ya milele.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Mama Bikira, umuombe Kristu Mwana wako awaondolee Watumishi wake zambi ambao ibada inakutangaza kama Mzazi-Mungu kadiri ya mafundisho na ya neno la ukweli, na uwafanye wastahili utukufu wa Watakatifu katika nuru ya ufalme wa mbingu.

SAUTI YA MBILI.

SIKU YA MUNGU MANGARIBI

Mimi mwana mupotevu, nimekosa mbele yako, ee Mwokozi*:* Ee Baba pokea toba yangu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Ee Kristu Mwokozi wangu, nafananisha sauti ya mtoza-kodi*:* Unirehemu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Ninapoona matendo yangu ya mazimu, nakimbilia ku rehema yako kwa mfano wa Mtoza-kodi, kama mwana mpotevu na kahaba, na nasujudu mbele yako*:* Mbele ya kunihukumu, ee Mungu wangu, unisamehe na unihurumie kwa wema wako.

Ee Bwana, usitazame zambi zangu, wewe uliyezaliwa kwa Bikira, lakini takasa moyo wangu uifanye kuwa hekalu la Roho Mtakatifu; usinitupe mbali ya uso wako, wewe mwenye wokovu mingi.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA KUTUBU.

Zambi zangu zimetokea nyingi juu yangu kama mawimbi ya bahari na kama mashua baharini na kubwa na mawimbi ya uovu; ee Bwana, uniongoze ku bandari ya amani na uniokoe ukinirudisha tena kwako.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Mimi ni muti kavu, ee Bwana, sitoe tunda la toba, naogopa shoka na moto usiyozimika; ndiyo maana nakuomba, mbele ya mwisho, uniokoe, ee Bwana, ukinirudisha tena kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Chemchem ya rehema, ewe Mzazi-Mungu, utustahilishe na huruma yako; tazama watu wenye zambi, onyesha uwezo wako wa siku zote; tunakutumainia wewe na tunakulalamikia*:* Salamu! Kama alivyofanya zamani Malaika mkuu Gabrieli.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ewe Bwana mwenye kuvika mbingu na mawingu, umekuwa duniani humo vazi la Mashahidi*:* Walivumilia mateso ya makafiri na wakaharibu uwongo wa miungu ya uwongo; kwa maombezi yao, utuopoe kwa adui msiyeonekana na utuokoe, ee Mungu Mwokozi.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA KUTUBU.

Sauti ya mbili

Kama Daudi mimi pia nakulalamikia*:* Unihurumie, nimetenda zambi; katika machozi ya toba, ee Bwana, safisha zambi zangu na unihurumie.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Unihurumie, ee Mungu, unihurumie, ndivyo alivyolia Daudi juu ya zambi yake, nami nahesabia makosa yangu kuwa mengi sana, lakini sina hata moja ya machozi aliyotoa*:* Unihurumie, ee Mungu, katika wema wako kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ewe Mzazi-Mungu, usimzarau mtumishi wako mwenye kuhitaji msaada wako, kwani roho yangu inakutumainia wewe*:* Unihurumie.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Uliwaangaza Mashahidi wako kupita zahabu, na ukawatukuza Watakatifu wako katika wema wako; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu. Mpenda-wanadamu, leta amani ku uzima wetu, pokea ombi letu kama ubani, wewe mwenye kupumzika kati ya Watakatifu.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS

KATHISMA YA USULUBIO

Sauti ya mbili.

Tunakutolea, ee Bwana, talasimu ya Msalaba wenye kuleta uzima uliyotupatia kwa wema wako japo uovu wetu; kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, linda inchi yetu na wa Kristu wote, ewe pepe yako Mpenda-wanadamu.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Ewe Msalaba wako uliangaza ulimwengu, uliwaalika waovu ku toba, ewe Muchungaji mwema, usinitenge ku zizi lako, lakini kuja unitafute, ee Rabi, mimi kondoo wako mpotevu; unihesabie katika kundi la wateule wako kwa mapendo yako kwa wanadamu na kwa wema wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Alipotazama, ee Kristu, lufu yako Msalabani, Bikira Mama yako akalia na uchungu akasema*:* Ee Mwanadamu, ni fumbo gani hii ya kuogopesha? Wewe mwenye kuleta uzima wa milele kwa wote, namna gani unaweza kuteswa na haya kwa kutaka kwako msalabani na lufu?

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Kwa Musalaba wako uliangaza ulimwengu, uliwaalika waovu ku toba, ewe Mchungaji mwema, usinitenge ku zizi lako, lakini kuja unitafute, ee Rabi, mimi Kondoo wako mpotevu. ; unihesabie katika kundi la wateule wako kwa mapendo yako kwa wanadamu kwa wema wako.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA MITUME.

Sauti ya mbili.

Uliwapa Wavuvi hekima mingi kuliko Wasemaji na ukawatuma duniani kote kama Watangazaji; kwa sababu ya mapendo yako isiyokadirika, ee Kristu Mungu wetu, kwa tegemeo lao uipatie Eklezya yako nguvu, tuma baraka yako kwa waamini wako, ewe peke yako Mpenda-wanadamu na Bwana mwenyi hurumu.

Sh*a*iri*:* Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Walipovua mataifa katika nyavu zao, Wavuvi wakafundisha ku mipaka ya ulimwengu kusujudu mbele yako, ee Kristu Mungu wetu, kama mbele ya Baba na ya Roho Mtakatifu*:* Kwa maombezi yao sabitisha Imani yetu, uwatumie watu rehema yako, wewe peke mwenye kupumzika kati ya Watakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba*:* Salamu, Wingu la Nuru yasipo mwisho, Bwana wa utukufu uliyechukua tumboni mwako.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Enyi Mitume, Manabii na Mashahidi, Watakatifu wakuu na Wenyi haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kukesha kwa kulinda imani, kwa waminifu wenu kwa Mwokozi mtupokelee sisi kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya mbili

Tunasujudu mbele ya Ikona yako Takatifu, ewe Mungu wa wema, tukiomba maondoleo ya makosa yetu, ee Kristu Mungu wetu, kwani ulipenda kuteswa ulipopanda Msalabani kwa kuokoa kiumbe chako ku utumwa wa adui; na kwa shukrani tunakulalamikia*:* Umejaza ulimwengu na furaha, ewe Mwokozi wetu, ulipokuja kuleta wokovu duniani.

Shairi*:* Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Umetimiza wokovu duniani, ee Kristu Mungu wetu; uliponua mikono yako takatifu msalabani kwa kuwakusanya mataifa yote yenye kukuimbia*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Umetukuzwa kuwapita wote, tunakuimbia, ee Mzazi-Mungu; mauti imeuawa, na Hadeze imevunjwa kwa Msalaba wa Mwana wako; ametufufua ku lufu, ametupatia uzima wa milele; paradizo imepewa mara iongine kwa sisi sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena kwa shukrani tunatukuza mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ewe Bwana mwenye kuvika mbingu na mawingu, umekuwa duniani humo vazi la Mashahidi*:* Walivumilia mateso ya makafiri na wakaharibu uwongo wa miungu ya uwongo; kwa maombezi yao, utuopoe kwa adui msiyeonekana na utuokoe, ee Mungu Mwokozi.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS

Sauti ya mbili.

Walipokataa furaha za hapa chini, Mashahidi. Watakatifu wakapokea hazina za mbinguni, wakawa Wenzao wa malaika*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie na utuokoe.

Mashahidi Watakatifu wanatuombea na kwa nyimbo zao wanamutukuza Kristu*:* Tangu hapo upotevu wote umemalizika, na ubinadamu umeokolewa kwa imani.

Washahidi Watakatifu waliposhika Msalaba wa Kristu kama ushindi, wakavunja nguvu ya shetani, na walipotukuzwa mbinguni, wakawa walinzi wetu wenye kutuombea daima.

Kwa imani mulipata utukufu kubwa*:* Apana paka mulishinda adui mulipoteswa, lakini tena mulifukuza mashateni, na munaponyesha magonjwa yote, enyi waganga wa roho na wa miili; enyi Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa Mungu ili ahurumie roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya Wafu.*

Ole, sikitiko gani inapata roho yenyi kuzimia wakati inatengana na mwili wake! Ole, machozi gani, hakuna mtu wa kuhurumia! Ikitazama ku upande wa malaika, inaomba bure, ikigeuka ku upande wa wanadamu, haipate msalaba. Na tena, ee Ndugu zangu wapenzi, tukiangalia ufupi wa uzima, tumuombe Kristu mapumziko ya Wafu na neema ya wokovu wa roho zetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Kivuli cha Sheria kinafifia, kwani ilikuja neema; sawa kichaka kiliwaka moto bila kuteketezwa, hivyo ulizaa Bikira, na ulibaki Bikira; pahali pa nguzo ya moto, Jua la uhaki lilipanda pa fasi ya Musa, Kristu, wokovu wa mioyo zetu.

SIKU YA SITA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MASHAHIDI.

Sauti ya mbili.

Uliangaza Mashahidi kupita zahabu, na Watakatifu wako uliwatukuza katika wema wako; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, mpenda-wanadamu, leta amani ku uzima yetu, pokea ombi letu kama ubani, wewe mwenye kupumzika kati, ya Watakatifu.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Heri ni udongo wenye kunyunyiziwa na damu yenu, enyi Washindani wa Bwana, na takatifu ni makao yenye kufunika miili yenu, kwani katika uwanja mulimushinda adui wakati mulimutangaza Kristu na uhodari*:* Kwa maombezi yenu mutupokelee ku wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Shairi: Watakatifu walio duniani, wao ni wale wazuri sana ninaopendezwa nao.

Mitume, Manabii na Mashahidi, Watakatifu wakuu na wenyi haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee ku wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Chemchem ya uzima uliye na uwezo pa wote, wazima na wafu, kama Mungu, sikiliza ombi la watumishi wako na utuonyeshe huruma yako, leta maondoleo ya zambi ku roho zenye kukutumainia wewe, ee Mungu wa huruma na wema kubwa.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Mama wa Nuru isiyokadirika, tunakuimbia kwa kukutukuza kama Malaika mbinguni.

MASIFU.

Sauti ya mbili.

Mulipoteswa kwa ajili ya Kristu mpaka kufa, enyi Washuhuda Washindaji wa Bwana, mukatoa mbinguni roho yenu mikononi mwa MUngu, na masalio yenu yanapelekwa duniani kote; makohani na Wafalme wanasujudu mbele hii, na mataifa yote yanapaza sauti kwa furaha*:* Ni ya samani ku macho ya Bwana; lufu ya marafiki zake.

Mashahidi Watakatifu walipochukua Msalaba wa Kristu kama ukumbusho wa ushindi, waliharibu nguvu ya Shetani, na walipotukuzwa mbinguni, wakawa walinzi wetu wenye kutuombea daima.

Ee Kristu, Mashahidi wengi wanakuomba*:* Kwa wema wako kwa ajili ya wanadamu, utuhurumie.

Enyi Mashahidi Washindaji masalio yenu yanaheshimiwa katika mji wote, mu inchi yote, kwani mulishindana na ukarimu na mulipokea taji mbinguni, ninyi ni utukufu wa makohani na wa Wafalme tena mapambo ya ma Eklezya takatifu ya Mungu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Bwana, uwakumbuke watumishi wako kwa wema, uwasamehe zambi zote walizotenda mu hii uzima*:* hakuna hata mmoja asiye na zambi ila wewe peke mwenye kuweza kuwapa wafu mapumziko.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Salamu, Bikira Mzazi-Mungu, Hekalu la Mwokozi lisiloweza kuharibiwa, patakatifu ambao Nabii alisema*:* Takatifu ni Hekalu lako, la ajabu kwa wenyi haki.

APOSTIKHA

Sauti ya mbili. Ote ek tu ksilu

Ee Bwana, katika lufu yako yenyi kuleta uzima, uliharibu nguvu ya mauti na ya kuzimuni; uliwatirikizia wote uzima wa milele, uliwafufua wafu*:* ndio maana tunakuomba*:* Leta mapumziko kwa marehemu waaminifu, ee Bwana mpenda-wanadamu, na uwastahilishe ku utukufu wako wa milele.

Shairi: Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Kwa kuwawezesha wanadamu kuingia katika Ufalme wako takatifu, ukakubali kufa msalabani; tena tunakuomba, kwa rehema yako, gawanya Ufalme wako na wale waliyokukuta kwa imani, na uwastahilishe ku heri na ku utukufu wa milele.

Shairi: Makumbusho yao ni ya milele.

Tangu milele wafu wanaongojea na woga hukumu yako ya haki mbele ya korti yako ya ajabu*:* leo, ee Bwana na Mwokozi, uwasamehe watumishi wako waliyokukuta kwa imani na uwape heri ya milele.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Che, chem ya uzima uliye na uwezo pa wote, wazima na wafu, kama Mungu, sikiliza ombi la watumishi wako na utuonyesssshe huruma yako; leta maondoleo ya zambi ku roho zenye kukutumainia wewe, ee Mungu wa huruma na wema kubwa.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Njooni wote tuimbe daima kwa nyimbo zetu tukimtukuza Mama wa Nuru*:* Ni yeye aliyezaa wokovu wetu, tumwambie basi*:* Salamu, kwani peke yako ulipata mimba ya Mungu wa mbele ya nyakati; salamu wewe uliyezaa Muumba aliyetengeneza sura ta Eva msalabani; salamu, Mama Mtakatifu kamili na Bikira Msiyeolewa.

SAUTI YA TATU

SIKU YA MUNGU MANGARIBI KU ESPERINOS.

Tunakutolea shairi yetu ya mangaribi na ubani na nyimbo za kiroho*:* Ee Kristu Mwokozi, hurumia roho zetu.

Uniokoe, ee Bwana Mungu wangu*:* Ndiwe wokovu wa Wanadamu; mawimbi ya mateso yananitikisa na nazama kwa uzito wa zambi zangu; unisaidie na mkono wako na uniongoze ku nuru ya toba, ewe Bwana mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

Ee Bwana, kusanya akili yangu yenye kutawanyika, takasa miiba ya moyo wangu, kama kwa Petro unipe toba, na kama kwa mtoza-kodi unipe pumuzi, kama kahaba unipe machozi ili nikupazie sauti*:* Uniokoe, ee Mungu wangu, mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

Mara nyingi, wakati niliimba kwa ajili yako, nilipatikana mu hali ya zambi, na wakati kinywa yangu ilikutukuza, roho yangu ilijivuna; kwa ttoba uniadibishe mimi wote, ee Kristu Mungu wetu, unihurumie na uniokoe.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA TOBA.

Sauti ya tatu.

Mbele ya haki ya korti yako ya ajabu hakuna lazima ya wenyi kushitaki wala ya washuhuda*:* Vitabu vitafunguliwa na siri zitaonekana; lakini mbele ya wewe kutafuta matendo ya uzima wangu duniani, ee Mungu, unihurumie na uniokoe, ee Bwana.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ee roho yangu, mpaka wakati gani utakaa katika zambi? Mpaka wakati gani utazarau toba? Ona hali ya hukumu na lalamikia Bwana*:* Nimekosa, lakini uniokoe, ee Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Kila mwanadamu anakimbilia kule anakopata wokovu*:* Katika wewe peke tunapata kimbilio, ee Mzazi-Mungu, mlinzi wa roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Uniokoe, ee Bwana Mungu wangu*:* Ndiwe wokovu wa wanadamu; mawimbi ya mateso yananitikisa na nazama kwa uzito wa zambi zangu; unisaidie na mkono wako na uniongoze ku nuru ya toba , ewe Bwana mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA TOBA

Sauti ya tatu

Ee roho yangu, wewe ni mgeni duniani, tubu, kwani uvumbi hauimbake kaburini, na juu ya zambi hakuna ukombozi; tangu sasa lalamikia Kristu Mungu wetu*:* Nimekosa, ee Bwana mwenyi kuvumba yengi kuwa moyoni, usinihukumu, lakini unihurumie.

Shairi: Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Tunakutolea shairi yetu ya mangaribi na ubani na nyimbo za kiroho*:* Ee Kristu Mwokozi, hurumia roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, nguvu yetu na boma yetu, mpatanishi wa nguvu wa ulimwengu, ewe Bikira mbarikiwa katika wote, kwa maombezi yako okoa watumishi wako ku hatari yote.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ushujaa wenu na imara yenu zilishinda uerevu wa adui; ee Mashahidi Washindaji, wenyi kustahili heshima yote, mumestahili heri ya milele; ninyi washuhuda wa Mungu kweli; ombeni kwa Bwana ili aokoe kondoo zake wenyi kumpenda Kristu.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO

Sauti ya tatu. Tin oreotita.

Ee Bwana, kwa amri yako, wakati tutakapoitwa mbele ya korti yako ya ajabu, usiwahukumu wale waliyokusadiki*:* Ssisi wote tumetenda zambi, lakini bila kukurudiria wewe Mungu Mwokozi; na wale uliyochukua pamoja nawe, tunakuomba uwaweke, ee Kristu, kwa wema wako, katika hema ya wenyi haki na ya Watakatifu.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Msalaba ulisimikwa duniani, ukainuka mpaka mbinguni, apana kwa urefu wa muti wake, lakini kwa sababu katika hii ulitimiza vitu vyote. Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Tuna Msalaba wa Mwana wako kama fimbo ya nguvu, ee Mzazi-Mungu; katika hii tunashusha majivuno ya adui, sisi wenye kukutukuza daima na moyo wote.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Bwana mwenyezi, uliangaza makumbusho ya Mashahidi wako, uliwapa nguvu ya kufafanisha mateso yako; walishinda bora nguvu ya shetani na wakapokea kipaji cha kuponyesha magonjwa*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana mpenda-wanadamu, utupe amani na neema ya wokovu wa roho zetu.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA MITUME

Sauti ya tatu. *Thias pisteos.*

Mitume walinyunyizia dunia yote na mawimbi ya neno-Mungu, walistawisha suke la imani yetu na dunia ikajaa mpaka mwisho wa mipaka yake, kwani ndago imetangua;

waliangaza wanadamu wote kwa kuwatolea kwa Kristu Mungu wetu, wakiwabatiza kwa jina la Utatu usiyogawanywa.

Shairi: Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Njooni wote tuwaimbie Mitume Watakatifu kama waongozi wetu katika imani*:* Wakipofukuza uwongo wa miungu ya uwongo, wakatuongoza ku nuru na ku uzima, na wakatufundisha kutukuza Utatu Mtakatifu; tunapoheshimu makumbusho yao takatifu, tunamtukuza na ibada Mwokozi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Nilipofikiri juu ya hazina ya milele ya huruma yako na juu ya nguvu isiyoweza kushindwa ya uwezo wako, nikakimbilia ku ulinzi wako, na katika sikitiko yenyi kunisonga, katika mashaka ya mawazo yangu ya sikitiko, nakulalamikia toka chini ya moyo wangu*:* Kuja unisaidie, ee Bikira Mzazi-Mungu, na okoa mtumishi wako msiyestahili.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Mulipovikwa silaha za Kristu, mulipovaa silaha za imani, mukapambana na majeshi ya adui na mukawaangusha sabiti; mulisaidiwa na matumaini ya uzima, mukapambana na mateso na makamio ya wazulumu na mukapokea taji, enyi Washuhuda wahodari wa Kristu Mungu wetu.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO

Sauti ya tatu. Tin oreotita.

Ulipochagua kufa msalabani, ukaupanda moyoni mwa viumbe; kwa kutuokoa ukakubali mwili wako upigiliwe msalabani, alafau jua likaficha miangaza yake; ni hii aliyoona Munyanganyi akakutambua kama Mungu na kwa imani yake akaingia Paradizoni wakati alipokulalamikia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Umetukuzwa pa msonobari, pa mti wa kasuku wa Libano, ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, sababu ya kuokoa wale wenyi kuabudu na imani kusulubiwa kwako kwa kutaka*:* Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**

Tin oreotita.

Kiumbe chote kimefurahiwa pa kukuona, ewe Bwana mvumilivu na furaha ya wote, umepandishwa Msalabani, ndivyo alivyosema Bikira Safi na Mtakatifu kamili, kwani alipata ukombozi kwa ajili yako, ee Mwana mpenzi; kwa muti uliponyessha mwanadamu aliyehukumiwa sababu ya muti; kwa mimi, nina moyo wa sikitiko, siwezi kuteswa pa kukuona umeingia katika mauti.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Kwa imani munaangaa kama nyota za mwanga, enyi Mashahidi Watakatifu ambao tunatukuza mashindano; bila woga mbele ya uzulumu wa wazulumu, mukamaliza kufuru ya miungu ya uwongo paka na silala ya ukweli na ushindi wa Msalaba usiyoweza kushindwa.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba hii wimbo ya Mashahidi.

Ee Bwana, mashahidi wako walipotegemezwa kwa imani na kusabitishwa kwa matumaini, walipoungana katika roho na mapendo ya Msalaba, wakavunja uzulumu wa adui; walipopokea taji la milele, wanaomba pamoja na malaika wabila-mwili kwa ajili ya roho zetu.

Manabii, Mitume wa Kristu na Mashahidi walitufundisha kuimbia Utatu wa asili moja; wakaleta nuru ku mataifa yenye kupotea*:* Malaika na wanadamu wamekuwa marafiki.

Ee Bwana, uwezo wa msalaba wako ni kubwa sana*:* Uliposimikwa kule kalvario, unatawala dunia yote; uligeuza wavuvi kuwa Mitume, na wapagani kuwa kundi la Washuhuda wenyi kuombea roho zetu wokovu.

Nguvu ya mashahidi ni kubwa sana*:* Wanapolala kaburini, wanafukuza pepo za uovu; walishinda nguvu ya adui waliposhindania imani katika Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. *Wimbo ya wafu.*

Tendo lote la ubinadamu ni bure kama haliendelee kisha kufa; hakuna kitu inabakia pa mali, utukufu hautufwate kule juu mbinguni; kwani lufu inapokuja, inapoteza hii yote. Tena, tumuombe Kristu msiyekufa awape marehemu mapumziko katika makao ya furaha ya milele.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Namna gani hatutashangaa, Muheshimiwa kamili, uzao wa Mungu na mtu? Kwa sababu bila kujua mwanaume, ee Bikira usiye na doa, ulizaa Mwana kwa namuna ya mwili pasipo baba, bila kupokea geuzo, ao mchanganyo, ao mgawanyo, lakini mwenye kushika tabia zake nzima za kila moja asili ya yote mbili. Kwa hii, Mama Bikira bibi malkia, umusihi kwa sababu ya wokovu, wa roho ya wale wanakusadiki kwa namuna ya kiorthodoksi, ya kama uko Mzazi-Mungu.

SIKU YA SITA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MASHAHIDI

Sauti ya tatu. Tin oreotita.

Ee Bwana Mwenyezi, uliangaza makumbusho ya Mashahidi wako, uliwapa nguvu kufuasa mateso yako; walishinda vema zaidi nguvu ya shetani na wakapokea kipaji cha kuponyesha; kwa maombezi yao, ee Bwana mpenda-wanadamu, utupe amani na neema ya wokovu wa roho zetu.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Ushujaa wenu na imara yenu zilishinda uerevu wa adui; ee Mashahidi Washindaji, wenyi kustahili heshima yote, mumestahili heri ya milele; ninyi washuhuda wa Mungu kweli; ombeni kwa Bwana ili aokoe kondoo zake wenyi kumpenda Kristu.

Shairi: Watakatifu walio duniani, wao ni wale wazuri sana ninaopendezwa nao.

Kwa imani munaangaa kama nyota za mwanga, enyi Mashahidi Watakatifu ambao tunatukuza mashindano; bila woga mbele ya uzulumu wa wazulumu, mukamaliza kufuru ya miungu ya uwongo paka na silala ya ukweli na ushindi wa Msalaba usiyoweza kushindwa.

Utukufu kwa Baba. . .
Wimbo ya wafu. Tin oreotita

Ee Bwana, kwa amri yako, wakati tutakapoitwa mbele ya korti yako ya ajabu, usiwahukumu wale waliyokusadiki*:* Sisi wote tumetenda zambi, lakini bila kukurudiria wewe MUngu

Mwokozi; na wale uliyochukua pamoja nawe, tunakuomba uwaweke, ee Kristu, kwa wema wako, katika hema ya wenyi Haki na ya Watakatifu.

Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimba, wewe mupatanishi ya wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa Msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa mpenda-wanadamu.

MASIFU

Wimbo ya Mashahidi.

Njooni mataifa yote, tutukuze makumbusho ya Mashahidi wa Bwana, kwani walipokea kwa Kristu mbele ya Malaika na ya Wanadamu taji la washindi na wanamuomba kwa ajili ya roho zetu.

Maaskari wa Kristu walivunja woga wote mbele ya wafalme na wazulumu na uhodari kubwa walimuungama Bwana wa ulimwengu, Mungu na Mfalme wetu, na sasa wanaombea roho zetu.

Majeshi ya mbinguni ya malaika Watakatifu walishangaa ushujaa wa Mashahidi*:* Katika sura mwili wao walizarau lakini mateso sababu ya kuwa Wafuasi wa mateso ya Kristu Mwokozi, na wanaombea sasa roho zetu.

Kama nyota, munaangaza ulimwengu hata kufa kwenu, ee mashahidi Watakatifu; muliposhindana vema zaidi, muna uwezo wa kumuomba Kristu ili alete neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Sababu gani kuhangaika bure? Safari tunayotembea ni mfupi! Uzima wetu unafifia kama moshi, unasaidia kwa muda kidogo kama majivu na uvumbi na unapotea mbio-mbio. Na tena, tunakuomba mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ewe Mzazi-Mungu, mlinzi wa wote wale wenyi kukuomba, unatupatia nguvu na uhodari, tunakutumainia wewe*:* Umuombe, Mwana wako kwa ajili ya Watumishi wako wasiyo na mafaa.

APOSTIKHA YA WAFU

Natukuza Msalaba wako mweshimiwa ambao unaleta heri na uzima kwa waaminifu wenye kukuimbia na mapendo, ee peke yako Bwana mwenyi huruma. Tena tunakuomba, ee Kristu Mungu wetu*:* Uwape marehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

Shairi*:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe.

Peke yako Bwana wa mapendo na wa huruma, bahari wa wema isiyoweza kufumbuliwa, unajaa mwanadamu, ulimuumba; tunakuomba, ee Kristu Mungu wetu, uwape marehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

Na makumbusho yao ni ya milele.

Kaburini mwili ulilala usingizi, lakini kwa uwezo wako usiyoweza kushindwa ukafufuka kama Mungu; wale waliyojuwa kaburini wakakutukuza wakikuimbia daima nyimbo zao milele. Na tena tunakuomba, ee Kristu Mungu wetu*:* Uwape merehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, tunatambua katika wewe taa kiroho iliyoleta nuru ya umungu sababu ya kumukutanisha na hali ya mwanadamu. Umuombw Mwana wako na Mungu wetu ili awape marehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

SAUTI YA INE

SIKU YA MUNGU MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba hii wimbo ya kutubu.

Ee Bwana, nilitaka kuzima katika vidonda vyangu daftari ya zambi zangu ili kuamini kuangu kukupendeze katika muda wa maisha yangu, lakini kwa hila yake adui akasirika juu ya roho yangu*:* Ee Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Mwenyi kuzama gani akifika ku bandari yako hataokolewa? Mgonjwa gani hatapata maponyesho kwako? Ee Muumba wa wote na mganga wa wagonjwa, Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Ee Mwokozi, unisafishe na machozi yangu, mimi mwenyi kuchafuka na zambi nyingi; tena nasujudu mbele yako*:* Nimekosa, ee Mungu; unihurumie.

Mimi ni mpotevu kati ya kondoo zako wa siri na nakimbilia kwako, ewe Mchungaji mwema*:* Ee Mungu, unihurumie.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU

Sauti ya ine.

Ee Bwana, rudisha kwako roho yangu maskini, kwani nimetumia vibaya maisha yangu yote katika zambi, unipokee kama mwanamuke mwenye zambi na uniokoe.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ninapovuka bahari ya hii uzima, natazama shimo ya zambi zangu, na nisipojuwa wapi nitaenda, nakulalamikia kama Petro*:* Uniokoe; ee Kristu Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Kwa huyu aliyelishwa hekaluni, katika Patakatifu ya watakatifu, mwenye kupambwa na hekima, na imani, na ubikira Safi, Malaika mkuu Gabrieli akamuletea habari ya mbinguni*:* Salamu, Bikira mbarikiwa na mjaliwa na utukufu, Bwana ni pamoja nawe.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Leo Majeshi ya mbinguni wanapoikumbuka Mashahidi washindaji, wanakuja kuangaza moyo wa waaminifu na wanaangazisha neema ulimwenguni; kwa maombezi yao, ee Mungu Mwenyezi, utupe neema ya wokovu.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU

Sauti ya ine. Takhi prokatalave.

Sisi wote pamoja tukimbilieni mbio ku chumba cha Bwana Arusi sababu ya kusikiliza sauti nzuri ya Kristu Mungu wetu*:* Njooni, enyi marafiki wa utukufu wa mbinguni; na kama zamani mabinti wenye akili, tuangaze taa yetu katika imani.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Kateplagi Iosif.

Tazama, ee roho yangu, namna gani tutahuzuria ku hukumu*:* Kwa hii wakati wa woga viti vitasimikwa; hapo Mwamzi wa haki atahukumu matendo ya kila mmoja; tazama, moto wa hatari umetayarishwa sababu ya kufunika vitu vyote kama bahari kali. Ee roho yangu, tubu mbele ya mwisho.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION**

Ni wewe kweli Mzazi-Mungu na kama mama unauwezo wa kumuomba Mwana wako na Mungu wetu alinda waaminifu wenye kukukimbilia; katika wewe kuna nguvu yetu na makimbilio yetu, ndiwe boma letu, bandari yetu ya wokovu na peke yako mlinzi wa wanadamu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Mashahidi wako walipamba Eklezya kwa damu yao ulimwenguni kote*:* Inapovaa sufi na kitani, kwa kinywa yao, inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu*:* Onyesha huruma yako kwa hawe watu walio wako, leta amani kwa watawala wetu wote na neema ya wokovu ku roho zetu.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya ine.

Umetukomboa ku laana ya Sheria kwa Damu yako heshimiwa; ulipigiliwa Msalabani na kuchomwa Mkuki, ukawa kwa wanadamu Chemchem ya umilele; ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Shairi*:* Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Ujiharikishe kutangulia, ee Kristu Mungu wetu, mbele ya sisi kuwa watumwa wa maadui wenyi kukufuru na kutuegemeza; wale wenyi kutugombanisha ywapunguze kwa Msalaba wako, wajuwe nguvu ya imani ya kweli, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION**.

Bikira safi na mama ya Kristu Mungu wetu, upanga ulichoma moyo wako wakati uliona Mwana wako na Mungu wako Msalabani*:* Umuombe bila kuacha kwa ajili ya maondoleo ya zambi zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Mashahidi wako, ee Bwana, kwa ajili ya mashindano walioshindana walipokea kwako, Mungu wetu, taji ya milele, waliposukumwa na nguvu yako waliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MITUME.

Sauti ya ine. Takhi prokatalave.

Ee Kristu, Mitume wako waliangaa kama mwana ulimwenguni, wanaangaza roho zetu na nuru ya mafundisho yako takatifu; katika wao uliondoa uwongo wa miungu ya uwongo, wanaangaza dunia na mafundisho ya imani. Kwa maombezi yao okoa roho zetu.

Ee Mwokozi, uliwachagua Wafuasi wako duniani kama Watangazaji wa imani, wakiwapeleka wanadamu ku maarifa ya Mungu; wanaangaza ulimwengu na miangaza ya neno lako, wakipanda kweli mbegu ya ibada*:* Kwa maombezi yao okoa roho zetu.

Shairi: Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

O ipsothis en to Stavro.

Ee Kristu. Mitume wako waliangaa kama mwanga ulimweguni, wanaangaza roho zetu na nuru ya mafundisho yako takatifu; katika wao uliondoa uwongo wa miungu uwongo, wanaangaza dunia na mafundisho ya imani. Kwa maombezi yao okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Neno la Baba, Kristu Mungu wetu, tunajuwa ya kama alitwaa mwili tumboni mwako, ee Mzazi-Mungu na Bikira safi, mbarikiwa katika wote, na bila kuacha tunakuimba kwa kukutukuza.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Takhi prokataleve.

Walipovaa silaha ya Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu, Mashahidi wako wakashinda uerevu wa adui; wakaangaa kama nyota, wakaongoza wanadamu; kwa wale wenyi kuwaomba na imani wanawaponyessha kwa maombezi yao, okoa roho zetu.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya ine Takhi prokatalave.

Ulipigiliwa Msalabani sababu ya kutuita kati ya wapagani, ee Mpenda-wanadamu, ulipanua mikono kwa kutaka kwako na ukaitika ili ubavu wako uchomwe mkuki. Ee Mungu wa mapendo, utukufu kwako.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Wewe uliyeteswa kwa kutaka kwako sababu ya kutukuzwa Msalabani, leta wema wako kwa watu wapya wenye kuitwa kwa jina lako, ee Kristu Mungu wetu, leta nguvu kwa watumishi wako waaminifu, ukiwalinda ku mateso*:* Agano lako liwe kwao silaha ya amani, ushindi usiyoweza kushindwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umetukuzwa Msalabani, Mama yako Mtakatifu, ee Neno la Mungu, akalia kwa umama na akasema*:* Hii ni mambo gani ya ajabu, ee Mwanangu? Wewe uliye uzima wa ulimwengu namna gani unaweza kushuka ku mauti? Lakini kwa huruma yako unapenda kuwafufua wafu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Leo Majeshi ya mbinguni wanapokumbuka Mashahidi washindaji, wanakuja kuangaza moyo wa waaminifu na wanaangazisha neema ulimwenguni; kwa maombezi yao, ee Mungu mwenyezi, utupe neema ya wokovu.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha: «Bwana nimekuita. . . » tunaimba hii wimbo ya Mashahidi:

Ee Kristu Mungu wetu, unapotukuzwa katika makumbusho ya Watakatifu wako, kwa maombezi yao ututumie neema ya wokovu.

Ee Bwana Mpenda-wanadamu uliyepokea uvumilivu wa Mashahidi wako Watakatifu, pokea pia heshima ya nyimbo zetu, ukitupatia kwa maombezi yao neema ya wokovu.

Kwa deni munayo kwa Mwokozi, ee Mashahidi watakatifu, mutuombee daima sisi wakosefu, mukiomba maondoleo ya zambi zetu na neema ya wokovu ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Wapi tamaa za dunia? Wapi wadanganyo yenyi kupita? Wapi zahabu na feza na makelele ya Watumishi? Hii wote ni uvumbi na bure; njioni tumuimbie Mfalme msiyekufa*:* Bwana, leta mema yako ya milele na uwape marehemu wetu mapumziko katika heri ya milele.

Zabihu mzima, sadaka za kiroho, ee Mashahidi Watakatifu, zabihu zenyi kumpendeza Bwana Mungu wetu, Kondoo wenyi kumjua Bwana wao Mtakatifu na mwenyi kuwajua ambao zizi halifunguliwa kwa mbwa-mwitu, ombeni kwa Mchungaji Mwema ili pamoja nanyi atupeleke pia ku fasi ya mapmziko.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Nabii Daudi aliyekuwa Babu-Mungu kwa ajili yako, alikutabiri katika zaburi kwa yule aliyekufanya maajabu*:* Malkia anasimama ku mukono wako wa kuume. Kwa sababu Mungu alikuonyesha wewe mama muletaji-uzima, yeye aliyetwaa mwili toka wewe kwa mapenzi yake bila baba, kusudi aumbe mara ingine mufano yake, iliyoharibika kwa tamaa, na kupata kondoo alliyepotea mulimani, kumubeba ku mabega yake, na kumutoa kwa Baba, kwa kuiunganisha pamoja na Ezi za mbinguni kwa kutaka kwake, na kuokoa dunia, ee Mzazi-Mungu; yeye ni Kristu, mwenye kuwa na rehema kubwa zaidi.

SIKU YA SITA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MASHAHIDI.

Sauti ya ine. Takhi prokatalave.

Mashahidi wako, ee Bwana, kwa ajili ya mashindano walioshindana walipokea kwako, Mungu wetu, taji ya milele, waliposukumwa na nguvu yako waliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Mashahidi wako walipamba Eklezya kwa damu yao ulimwenguni kote*:* Inapovaa sufi na kitani, kwa kinywa yao, inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu*:* Onyesha huruma yako kwa hawe watu walio wako, leta amani kwa watawala wetu wote na neema ya wokovu ku roho zetu.

Shairi: Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Takhi prokataleve.

Walipovaa silaha ya Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu, Mashahidi wako wakashinda uerevu wa adui; wakaangaa kama nyota, wakaongoza wanadamu; kwa wale wenyi kuwaomba na imani wanawaponyessha kwa maombezi yao, okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Kristu Mungu wetu, kwa uwezo na wema wako leta mapumziko ku roho za waaminifu waliyokuja kwako toka ku vitu visivyodumu, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, samehe makosa yao ya zamani, hurumia kazi ya mikono yako, ee peke yako mpenda-wanadamu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, kwa ajili yako, fumbo ya ficho na ambayo hata malaika hawakujua ilifunuliwa kwa sisi duniani*:* Mungu amejifanya mutu bila kuchanganya hali zake mbili katika hii muungano, na kwa kutaka kwake aliteswa Msalabani kwa ajili yetu sababu ya kumfufua Adamu na kuokoa roho zetu ku mauti.

MASIFU YA MUPOSHO ASUBUI.

Sauti ya ine Wimbo ya Mashahidi.

Ee Mashahidi Watakatifu, mumukuwa marafiki ya malaika mulipomtangaza Kristu uwanjani, mulizarau furaha za hii dunia, mukishika kweli nanga ya imani, ninyi ni Chemchem ya kuponyesha ya Wazaifu*:* Ombeni daima kwa ajili ya roho zetu.

Ee Mashahidi Watakatifu, tunashangaa mashindano yenu, kwani, mulipovaa mwili usiyokufa, mulifukuza adui msiyeonekana; mumeteswa mateso kali zaidi bila woga mbele ya wazulumu; sasa mumepata kwa Kristu utukufu wenyi kustahili, yeye mwenyi kuleta neema ya wokovu ku roho zetu.

Ee Bwana, lufu marafiki zako ni heshimiwa*:* Kwa upanga, kwa moto ao kwa baridi, walitoa uzima wao katika matumaini ya kupata tunzo ya matendo yao, na uvumilivu wao uliwafaidia kwako, ee Mwokozi, neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

EeBwana, kwa wema wako pumzisha watumishi wako katika uwanja wako humo wanapumzika watakatifu wote.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, matumaini na ulinzi wetu, hatuogope fitina za adui, kwani unalinda roho zetu.

APOSTIKHA YA MUPOSHO ASUBUI.

Sauti ya ine.

Fumbo ya woga ni ile ya lufu! Namna gani roho yetu inaondolewa mwilini mwake; inatengana na umoja wenyi kulingana? Namna gani mapatano ya kweli inavunjwa kwa mapenzi kimungu? Tena tunakuomba leta mapumziko kwa marehemu waaminifu katika hema ya watakatifu wako, ee mpenda-wanadamu na Chemchem ya uzima.

Shairi: Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe.

Kwa waaminifu lufu ni usingizi tangu ulipumzika kaburini, wewe Rabi wa ulimwengu wote, na kuharibu ufalme wa mauti; tena tunakusihi*:* Leta mapumziko kwa marehemu waaminifu katika hema ya Watakatifu, ee Mpenda-wanadamu na chemchem ya uzima.

Shairi: Na makumbusho yao ni ya milele.

Katika wewe tumepata haki na utakatifu, na ukombozi wa roho zetu; unatuongoza kwa baba wenyi kusubutishwa na kukombolewa kwani ulichukua malipizi ya zambi zetu; na sasa tunakuomba*:* Leta mapumziko kwa marehemu waaminifu katika nuru na furaha, ee Bwana; mfazili na Mwokozi wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Mufuatana na unabii, ee Bikira, tunakutukuza kama Mzazi-Mungu*:* Ni Mungu ulizaa kwa namna ya ajabu; amejifanya mutu tumboni mwako sababu ya kutukomboa ku zambi iliyotufunga; umuombe tena sasa aangaze marehemu Watumishi wako kwa nuru yake.

SAUTI YA TANO.

SIKU YA MUNGU MANGARIBI

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba Wimbo ya kutubu, hii:

Ee Bwana, siache kutenda zambi, nasahau mapendo uliyonizungusha*:* ponyesha ugumu wa moyo wangu; peke yako Mungu wa wema, unihurumie.

Ee Bwana, sina hata woga juu yako lakini natenda maovu; mtu gani haogopi mwamzi ku korti? Mgonjwa gani akitamani kupona, anasirikisha mganga wake kama mimi? Ee Bwana mvumilivu na mwenyi kujaa mapendo, tazama uzaifu wangu na unihurumie.

Ole, wangu! Tazama nafanana na mtini usiyozaa matunda! Naogopa laana na shoka, lakini wewe mtunza-bustani wa mbinguni, ee Kristu Mungu wetu, stawisha roho yangu yenyi kukauka, unipokee kama mwana mpotevu na unihurumie.

Ee Bwana, usitazame wingi wa zambi zangu, wewe Bikira alizaa; zima makosa yangu yote, na unipe mawazo ya kuongoka; peke yako mpenda-wanadamu, unihurumie.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU.

Sauti ya tano.

Ee roho yangu, wakati atakapokaa mwamzi na malaika watakapokuwa huko, kwa sauti ya baragumu na mbele ya tanuru ya moto utafanya nini wakati utakapopelekwa ku hukumu? Hapo matendo yako ya giza yataonekana, hapo mawazo yako ya siri yatastakiwa; mbele ya mwisho umwambie Kristu Mungu wetu*:* Wewe mwenye kusoma mioyo unihurumie mimi muovu.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ee roho yangu, vitu vya hapa chini vinadumu muda mfupi tu, vila vya Juu-mbinguni vinakaa milele, naona korti, mwamzi amekaa juu kiti chake naogopa kuhukumiwa; ee roho yangu, tubu mbele ya mwisho. Hukumu hai takuwa na huruma.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Pamoja na Malaika mbinguni, pamoja na wanadamu duniani, tunakuimba katika shangwe, ee Mzazi-Mungu*:* Salamu, mlango pana kuliko mbingu, salamu, msaada wa pokee wa wenye mauti, salamu, Mjaliwa neema ambaye katika mwili ukamzaa Mungu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Mashahidi wako, ee Bwana, kisha wewe walikunywa kikombe cha mateso yako, walikataa furaha za hii uzima; wakawa wenzao wa malaika. Kwa maombezi yao, ee Bwana, samehe roho zetu na leta neema ya wokovu ku roho zetu.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU.

Sauti ya tano.

Ee roho yangu, vitu vya napa chini vinadamu muda mfupi tu, vile vya juu-mbinguni vinakaa milele; naona korti, mwamzi amekaa juu ya kiti chake, naogopa kuhukumiwa; ee roho yangu, tubu mbele ya mwisho*:* Hukumu haitakuwa na huruma.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Sisi wote wakosefu rusikilize sauti ya bwana na muchungaji mkuu*:* Alionekana mwilini duniani kwa ajili yetu, akawaita wakosefu kama mimi kwa kutubu; muwe na moyo, msiogope*:* Mateso ni zaifu mshahara ni bora.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Toka kwa Bikira Fumbo ya ajabu ilifunuliwa mbebaji wa wokovu duniani; bila mbegu furaha ya wote ikazaliwa kwake na inaonekana takatifu katika mwili. Bwana, utukufu kwako.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Umetupatia miujiza ya mashahidi wako Watakatifu kama boma isiyoweza kushindwa*:* Kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu haribu fitina ya wapagani, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu sabalisha utawala wa imani.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon.

Enyi Waaminifu, tumuimbie na kumtukuza Bwana mfufuliwa, huyu aliyetaka kutukomboa, kwani yenye mwenyewe alipigilia Msalabani zambi za wenyi kufa, akiopoa wanadamu ku udanganyifu sababu ya kutuingiza katika ufalme wa mbinguni.

Shairi*:* Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Ee Mwokozi, muti wa Msalaba wako umeleta wokovu duniani, uliitika kupigiliwapo sababu ya kuondoa laana ya wenyi kufa*:* Ee Mwokozi, furaha yetu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Aliposimama karibu ya Msalaba wa Bwana, Mzazi-Mungu akalalamika akilia*:* Ole wangu, ee Mwanangu mpendwa, ole wangu, ee Nuru ya macho yangu, namna gani umepanuliwa msalabani wewe uliyetandaza mbingu kama nguo na uliyetokeza kuzimuni chemchem ya maji kwa mapenzi yako?

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Majeshi ya mbinguni walishangaa ushujaa wa Mashahidi Watakatifu kwani na mwili wa mauti walishinda bora adui msiyeonekana kwa uwezo wa Msalaba na wanamuomba Bwana kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA MITUME.

Sauti ya tano. Ton Sinanarkhon Logon.

Tuwaimbie kwa mashairi na nyimbo za kiroho Mitume watakatifu waliyomuona Neno na kumtumikia Kristu, kwani, wanamuomba Kristu kwa ajili yetu sisi tunaikutukuza makumbusho yao takatifu.

Shairi*:* Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Tuwaimbie Mitume waliyohubiri kwa mwaminifu wowote kadiri ya imani ya kweli mafundisho ya kweli ya Bwana, wakakataa giza za fitina, wakaeneza nuru ya kiroho duniani, na neema ya mafundisho kimungu, nawanaomba kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira msiyeolewa, bibi bikira daima, tunakuimbia pamoja na washuhuda wa Mungu, kwani katika wewe Mwenyezi alifanya maajabu; huyu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati alitwaa mfano wetu, akakaa rumboni mwako na ikamupendeza kuzaliwa na mwili wetu sababu ya ukombozi na wokovu wa wanadamu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Majeshi ya mbinguni walishangaa ushujaa wa mashahidi watakatifu, kwani na mwili wa mauti walishinda vema adui msiyeonekana kwa uwezo wa Msalaba na wanamuomba Bwana wokovu wa roho zetu.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya tano

Pahali pa mfupa ya kichwa pamekuwa Paradizo*:* Kwa muda kidogo kisha kusimika mti wa Msalaba, palepale ikastawisha mzabibu wa uzima*:* Ee Bwana furaha yetu, utukufu kwako.

Shairi*:* Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Ee Mwokozi, mti wa Msalaba wako umeleta wokovu duniani; uliitika kupigiliwapo sababu ya kuondoa laana ya wenyi kufa*:* Ee Mwokozi furaha yetu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, alipokuona umesulubiwa Msalabani kwa kutaka kwako kama mwana-kondoo asiye na kosa, Mama yako akalia na akalalamika kwa huzuni*:* Ole wangu, alivyolalamika, namna gani imezimika nuru ya macho yangu? Namna gani unakula kama muovu katikati ya wanyanganyi, ee Mwanangu, wewe Mfalme wa ulimwengu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Leo imeangaa makumbusho ya mashahidi na mbingu ikaongezaka mwangaza wake*:* Malaika wanashangilia pamoja nasi kama wanadamu duniani; Mashahidi wanamuomba Mungu ili ahurumie roho zetu.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba hii wimbo ya kutubu.

Sauti ya tano.

Ee Mashahidi wakuu muliyozarau mema ya hii uzima sababu ya kupambana vema na mateso, hamukuzeka katika matumaini yenu ya heri, lakini kwa uriti mukapokea ufalme wa mbinguni; na kwa sababu muna uwezo wa kumdai Mungu mwema, mumuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Ee Bwana walipolindwa na nguo ya imani, waliposabitisha na alama ha Msalaba, Mashahidi wako Watakatifu walivumilia mateso; walishinda vema uwongo na nguvu ya shetani; kwa maombezi yao, ee Mungu Mwenyezi, tuma amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Ee Mashahidi watakatifu, mutuombee ili tusafishwe zambi zetu*:* Mulipokea neema ya kutuombea.

Katika nguvu yenu imara hamukumukana Kristu, ee Mashahidi Watakatifu muliyoteswa mateso ya namna yote, lakini mulishinda nguvu ya wazulumu na mukalinda bila kosa imani sababu ya kupita duniani kwenda mbinguni; umuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Nikikumbuka Nabii aliyesema*:* Mimi ni uvumbi na matope, mimi pia nilitazama kaburini, niliona mifupa yenye kukauka na nikasema*:* Huyu ndiye mfalme, mtajiri, askari, maskini mwenyi haki muovu? Ee Bwana, kwa mapendo yako kwa wanadamu, pumzisha watumishi wako pamoja na wenyi haki.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Katika Bahari Nyekundu, wakati moja mufano wa Bibi-Arusi musiyeolewa ulijionyesha. Kule Musa alikuwa mugawanyi wa maji, hapa Gabrieli alikuwa mutumishi wa ajabu. Wakati ule Israeli alipita vilindini bila kulowanishwa, sasa Bikira alizaa Kristu bila mbegu; Bahari kisha kupita kwa Israeli ilibaki isiyowezekana kupita; Musiyeolewa kisha kuchukua Emmanueli, alibaki bila kuharibiwa. Mungu ndiwe uliye na uliyekuwako, na uliyefunuliwa sawasawa na mutu, utuhurumie.

SIKU YA SITA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MASHAHIDI.

Sauti ya tano.

Ee Bwana, kisha wewe mashahidi wako walikunywa kikombe cha mateso yako, walikataa furaha ya hii uzima; wakawa marafiki za malaika. Kwa maombezi yao, ee Bwana, leta maondoleo na neema ya wokovu ku roho zetu.

Shairi: Mungi ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Umetupatia miujiza ya mashahidi wako Watakatifu kama boma isiyoweza kushindwa*:* Kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu haribu fitina ya wapagani, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu sabalisha utawala wa imani.

Shairi: Watakatifu walio duniani, wao ni wale wazuri sana ninaopendezwa nao.

Katika nguvu yenu imara hamukumukana Kristu, ee Mashahidi watakatifu muliyoteswa mateso ya namna yote, lakini mulishinda nguvu ya wazulumu na mukalinda bila kosa imani sababu ya kupita duniani kwenda mbinguni; umuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Mungu Mwokozi, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu, pamoja na wenye haki pumzisha watumishi wako na uwaruhusu wakae katika uwanja wako, usihesabie makosa yao ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Kristu Mungu wetu uliyezaliwa kwa Bikira sababu ya kuangazia ulimwengu, kwa maombezi yake utufanye sisi kuwa wana wa nuru, ee Bwana, utuhurumie.

MASIFU.

Sauti ya tano.

Litukuzwe jeshi la mfalme wa mbinguni! Kwani walipozaliwa duniani mashahidi washindaji hawakutumainia cheo cha Malaika*:* Walipozarau mwili na kuteswa mateso yao, wakastahili utukufu wa malaika; kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie neema ya wokovu.

Ee Bwana, waliposhinda katika mashindano yao, Washindani wa malaika Wabila-mwili, Mashahidi wako walivumilia mateso; kwa matumaini moja walifurahia mema iliyoahidiwa; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani duniani na neema ya wokovu ku roho zetu.

Mashahidi Watakatifu walishindana duniani, walipotolewa motoni na kuangamizwa majini, sasa wanaweza kuimba*:* Tumepita katika moto na katika maji na umetupatia mapumziko. Ee Bwana, kwa maombezi yao, utuhurumie.

Katika mateso Mashahidi wakalalamika kwa furaha*:* Hii ndio njia ya sisi kupatana na Mungu; kwa malipo ya vidonda vyenyi kujaa katika miili yetu, tutapokea mavazi meupe ya ufufuo; pahali pa matusi tutapokea utukufu wa mbinguni; pahali pa gereza tutapata Paradizo; pahali pa kuhukumiwa kama waovu tutakuwa pamoja na malaika mbinguni. Ee Bwana, kwa maombezi, okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Bwana, uliniumba, ukaniwekea mkono, ukaniinua na ukaniambia*:* Utarudi udongo. Uniongoze katika njia yenyi kwenda kwako, unisamehe makosa yangu, na kwa mapendo yako kwa wanadamu, uniokoe.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Sisi waaminifu tunakutaja mwenyi heri, ee Bikira Mzazi-Mungu, na tunakutukuza kama inavyofaa, muji imara, boma isiyoweza kuharibika, mlinzi mhodari na makimbilio ya roho zetu.

APOSTIKHA YA MUPOSHO ASUBUI
(WIMBO YA WAFU).

Sauti ya tano. Kheris askitikon.

Kwa nuru ya uso wako, ee Kristu, kwa mema wako, pumzisha marehemu katika mahali pa baridi, karibu ya maji ya mapumziko, katika kifua cha Abrahamu; kule kuangaa nuru yako safi na kunatiririka chemchem ya heri, kule makundi ya watakatifu wanafurahiwa na wanatukuza wema wako kimungu, pumzisha pia watumishi wako ukiwapa neema ya wokovu.

Shairi: Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Ee mpenda-wanadamu na Bwana wa ulimwengu, wale wenyi kutoka ku vitu visipodumu na wanakuja kwako uwape waimbie na kutukuza uwezo wako; uwafanye wangae na uzuri wako, wapate mapendezi yako na huruma yako na waonje furaha safi zaidi, kule makundi ya Malaika na watakatifu wengi wanafurahiwa pumzisha pia watumishi wako ukiwapa neema ya wokovu.

Shairi: Na makumbusho yao ni ya milele.

Kule wanaimba makundi ya ma Nabii, ya Mitume na ya Mashahidi na wale wote waliyohakikishwa tangu milele kwa Mateso yako ya wokovu na kwa bei ya damu uliyokomboa nayo mwanadamu mfungwa wa zambi, mahali hapo pumzishapo marehemu waaminifu na kwa mapendo yako kwa ajili yao uwape maondolea ya zambi zao; kwani duniani ulikuwa peke yako asiye na zambi, peke yako Mtakatifu na peke yako mwenyi uhuru kati ya wafu; pumzisha pia watumishi wako ukiwapa neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulituopoa, sisi tuliyotumikia chini ya sheria ya zambi, wakati ulipata tumboni mwako mimba ya Muumba wa sharia, Mfalme na Mungu wetu ambaye ndani yake tunahakikishwa kwa zawadi ya ukarimu; umuombe sasa andike katika Kitabu cha uzima roho za wale wenyi kukuimbia, ee Mzazi-Mungu, ili wakiokolewa kwa usimamizi wako, tupate kwa Mwana wako ukombozi tunaposujudu mbele ya huyu mwenyi kuleta duniani neema ya wokovu.

SAUTI YA SITA

SIKU YA MUNGU MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha «Bwna nimekuita. . . » tunaimba hii wimbo ya kutubu.

Sauti ya sita.

Sina na machozi ya toba, nakuomba tena, ee Mungu Mwokozi*:* Mbele ya mwisho uniongoze na unipe toba ili niepuke ku azabu.

Ku siku ya ajabu ya majilio yako hatutaweza kusikia, ee Kristu*:* Siwajui ninyi! Kwani matumaini yetu ni kwako hata kama sisi ni wazaifu na hatushike amri zako; ee Mwokozi, tunakuomba, samehe roho zetu.

Ee Mwokozi, ponyesha vidonda vya moyo wangu wenyi kujeruhiwa na zambi nyingi, kwani ndiwe mganga wa roho na wa miili; kwa wale wenyi kukuomba unawasamehe zambi, unipe machozi ya toba na maondoleo ya makosa yangu*:* Ee Bwana mwenyezi, unihurumie.

Nilipotwaliwa nguvu, adui akanipiga mshale wa zambi, lakini wewe, ee Mganga wa roho na wa miili, ponyesha vidonda vya roho yangu; ee Mungu wa mapendo, unihurumie.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU.

Sauti ya sita

Nawaza siku ya ajabu ya hukumu na nalilia matendo yangu mabaya; nitasema nini kwa Mfalme msiyekufa? Nitasubutu nemna gani kumtazama Mwamuzi wangu mimi maskini? Ee Baba Mwema kamili, Mwana wa pekee na Roho Mtakatifu, unihurumie, ee Bwana.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ee Mungu wa mapendo, kwa machozi yangu mengi; mahali hapa ulipochagua kwa kuketi na kutoa hukumu ya haki usifumbuo siri za moyo wangu ili nisipate haya mbele ya malaika wako, lakini, ee Mungu wangu, unihurumie, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION.**

Mzazi-Mungu mtukufu, aliye mtakatifu kuwapita malaika watakatifu, tunamuimbia daima kwa kinywa na kwa roho na tunamtambua kama Mzazi-Mungu, kwani alizaa kweli Bwana aliyejifanya mtu na anaombea imara roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Kwa Wenyi hali ni nuru ya milele*:* Walipoangazwa na nuru yako, Watakatifu wanangaa daima kama nyota kuangaa, wakififisha taa ya makafiri; kwa maombezi yao, ee Bwana na Mwokozi, angaza roho yangu na uniokoe.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU.

Sauti ya sita.

Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, urazi wote umetukosa; kama maskini waovu tunakutolea hii ombi*:* Utuhurumie, ee Bwana.

Ee Bwana, utuhurumie sisi wenyi kukutumainia wewe; usitusirikie, usikumbuke maovu yetu, lakini kwa wema wako ututazame sasa na utuopoe kwa maadui zetu; kwani ndiwe Mungu wetu, na sisi ni watu wako; sisi wote ni kazi ya mikono yako, ni jina lako tunaita daima.

Shairi*:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ee Bwana, utuhurumie sisi wenyi kukutumainia wewe; usitusirikie, usikumbuke maovu yetu, lakini kwa wema wako ututazame sasa na utuopoe kwa maadui zetu; kwani ndiwe Mungu wetu, na sisi ni watu wako; sisi wote ni kazi ya mikono yako, ni jina lako tunaita daima.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Utufungulie mulango wa huruma, ewe Mzazi-Mungu mubarikiwa. Tukikutumaini wewe, tutakuwa bila kuanguka. Kwako tutaziepuka taabu; kwa kuwa wewe wokovu wa muzao wa wakristu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Watakatifu walishindana mashindano bora, wakapokea kwako tunzo ya Washindaji; na walipozarau hukumu ya makafiri, wakapata utukufu wa milele; kwa maombezi yao, ee Mungu wetu, utupe sisi neema ya wokovu.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya sita.

Leo limetimia neno la Nabii*:* Tazama tunasujudu mahali palipokanyanga miguu yako, ee Bwana, tulipoonja muti wa wokovu, tumefunguliwa ku mateso yetu na ku zambi kwa maombezi ya Mzazi-Mungu.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Ee Bwana, Msalaba wako, imetakaswa*:* Inawaponyesha wale waliyeregea katika zambi; katika hii tunakuomba*:* Utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Kristu, mama Bikira daima aliyekuzaa alipokuona umeteswa kwa ajili yetu Msalabani, moyo wake ukachomwa kwa huzuni na akalia. Kwa maombezi yake, utuhurumie.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Kama washindani katika uwanja, ndivyo walivyopigana wazulumu juu ya mashahidi; makundi ya malaika waliwatayarishia taji la Washindaji; hekima yao iliwasangaza wazulumu na wafalme; walimushinda shetani walipomuungama Kristu. Wewe uliyewapa nguvu, ee Bwana, utukufu kwako.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA MITUME.

Sauti ya sita.

Kama ulivyoonekana katikati ya Wafuasi wako ukiwapa amani, kuja pia kati yetu, ee Mungu Mwokozi na uniokoe.

Shairi*:* Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Ee Kristu zamani Wafuasi wako walipotikiswa katika chombo, wakalalamika*:* Ee Rabi, utuokoe, tunakufa! Sasa sisi wenyewe tunalalamika*:* Ee Mwokozi mpenda-wanadamu, tunakuomba, utuokoe ku hatari yoyote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bibi Mtakatifu tena Mzazi-Mungu uliyezaa duniani Muumba wa ulimwengu, pamoja na Mitume watakatifu umuombe kila siku kwa wema wake atuokoe ku mateso na atuondolee zambi zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Bwana, makumbusho ya Mitume wako inakumbusha Mateso na Adeni; katika hii viumbe vyote vinafurahiwa, na kwa maombezi yao utupe, ee Bwana, amani na neema ya wokovu.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya sita.

Ee Kristu, tangu ilisimikwa muti wa msalaba wako, ukaregeza nguvu za mauti; Hadeze ikajiharikisha kumeza huyu atakayerudisha na woga. Ee Mungu Mtakatifu, ulituonyesha wokovu na tunakutolea utukufu*:* Ee Mwana wa Mungu, utuhurumie.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Ee Bwana, wana wa Israeli walikuhukumu ukufe, wewe uzima wa ulimwengu wote; wao waliyovuka Bahari Nyekundu kwa sababu ya bakora ya Musa, wakakupigilia misumari Msalabani; wao waliyofunza sali ya mwamba, wakakupa nyongo kuwa chakula; lakini uliteswa kwa kutaka kwako ili tukombolewe ku utumwa wa adui. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Mzazi-Mungu na Bikira mbarikiwa, umuombe Mwana wako, Kristu Mungu wetu, aliyejiachilia kupigiliwa Msalabani sababu ya kuokoa ulimwengu ku udanganyifu, ahurumie roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Watakatifu walishindana mashindano bora, wakapokea kwako tunzo ya Washindaji; na walipozarau hukumu ya makafiri, wakapata utukufu wa milele; kwa maombezi yao, ee Mungu wetu, utupe sisi neema ya wokovu.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo hii ya mashahidi:

Ee Kristu, Mashahidi wako waliteswa mateso mengi, mwisho wakapokea utukufu mbinguni ili waombee roho zetu.

Ee Kristu, natumainia Msalaba wako, ninapotukuzwa katika hii nalalamika*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, shusha majivuno ya wale wasiyotambua ya kwamba ndiwe kweli Mungu na mutu.

Mashahidi watukufu wakaaji wa inchi ya mbinguni, walipoanindana duniani wakateswa mateso mengi; kwa maombezi yao na kwa maombi yao, ee Bwana, utulinde.

Ee Bwana, Msalaba wako umekuwa kwa Mashahidi utukufu usiyeweza kushindwa; walipoona lufu iliyowapeleleza na walipotangulia kuona uzima gani unawaongojea, wakapata nguvu kwa matumaini waliyokutumainia wewe; kwa maombezi yao, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Kwa neno lako la uumbaji uliniruhusu nizaliwa na niishi, kwa kunifanya mtu mzima uliunganisha ndani yangu yenyi kuonekana na isiyoonekana, kwa udongo ukaumba mwili wangu, ukanipa vilevile roho kwa pumuzi yako kimungu na yenyi kuleta uzima; ndie maana, ee Mungu Mwokozi, uwapumzishe watumishi wako katika hema za wenyi haki pa inchi ya wazima.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Nani hatakuita wewe mwenye heri, Bikira Mtakatifu kamili? Nani ataimba kuzaliwa kwa Mwana wako bila mume? Kwani Mwana wa pekee aliyeangaa mbele ya wakati kwa Baba, yeye vilevile alitokea kwa wewe uliyesafi, akitwa mwili usiyosemwa; yeye ni Mungu sawasawa na hali yake, na akajifanya mutu kwa kadiri ya hali ya watu kwa ajili yetu; yeye hagawanyike kwa uso mbili, lakini anajulikana kwetu katika hali mbili bila muchanganyo. Umusihi, ee Bikira mutaratibu na heri daima, kwa kurehemu nafsi yetu.

SIKU YA SITA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MASHAHIDI.

Sauti ya sita.

Watakatifu walishindana mashindano bora, wakapokea kwako tunzo ya Washindaji; na walipozarau hukumu ya makafiri, wakapata utukufu wa milele; kwa maombezi yao, ee Mungu wetu, utupe sisi neema ya wokovu.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika watakatifu wake.

Kama washindani katika uwanja, ndivyo walivyopigana wazulumu juu ya mashahidi; makundi ya malaika waliwatayarishia taji la Washindaji; hekima yao iliwasangaza wazulumu na wafalme; walimushinda shetani walipomuungama Kristu. Wewe uliyewapa nguvu, ee Bwana, utukufu kwako.

Shairi: Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Ee Bwana, makumbusho ya mashahidi wako inatukumbusha Paradizo na shamba ;a Edeni; katika hii viumbe vyote vinafurahiwam na kwa maombezi yao, ee Bwana, utupe amani na neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Kweli, yote ni ya bure! Uzima unapita kama ndoto, kama kivuli, wafu wanaogopa bure, kama yanavyosema Maandiko; wakati tutapoondoka ulimwenguni, tutakaa lakini kaburini, maskini kama watajiri. na tena, ee Kristu Mungu wetu, kwa mapendo yako kwa wanadamu, uwape marehemu watumishi wako mapumziko.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Matumaini ya ulimwengu, bikira Mzazi-Mungu, naomba ulinzi wako wa pekee wenye kuongoza heshima; hurumia taifa lenye kusongana ku upande wako, umusihi Mungu ili atuonyeshe mapendo yake akiokoa roho zetu ku azabu zote, ee Bikira mbarikiwa katika wote.

MASIFU MU POSHO.

Sauti ya sita. Wimbo ya mashahidi.

Ee Bwana, kukumbuka mashahidi wako ni siku Kuu kubwa kwa viumbe vyote; dunia ya wanadamu inafurahi pamoja na malaika mbinguni; kwa maombezi yao, utuhurumie.

Ee Bwana, kama hatunolikuwa na usimamizi wa watakatifu wako na matumaini ya wema wako wa huruma, namna gani tutasubutu kukuimbia, ewe Mwokozi mwenye kutukuzwa milele na malaika? Wewe mwenyi kuvumbua yenyi kuwa moyoni mwa wanadamu, utuhurumie.

Makumbusho ya mashahidi inawafurahisha wale wenye kumuogopa Bwana*:* Waliposhindana juu ya Kristu, wakapata utukufu mbinguni, na sasa wana uwezo wa kuomboa roho zetu wokovu.

Mungu wetu alifanya maajabu katika watakatifu aliyochagua. Furahini na shangilieni ninyi wote wenyi kumutumikia, kwani aliwatukuza ninyi katika ufalme wa mbingu*:* Tunawaomba ninyi msitusahau.

Utukufu kwa Baba. . *Wimbo ya wafu.*

Adamu akapata uchungu wakati alipoonja tunda iliyokataziwa zamani katika shamba la Edeni, kwani nyoka akamwingiza sumu yake, na katika huyu mauti yenyi kuwaangamiza wanadamu ikaingia duniani; lakini Bwana alikuja, akamuua yule nyoka na akamupatia mapumziko; tumulalamikie*:* Ee Bwana Mwokozi samehe wale uliyochukuwa pamoja nawe, na uwapumzishe kati ya wateule wako.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Kristu, kwa maombezi ya huyu aliyekuzaa, ya Manabii, ya Mitume, ya Mashahidi, ya Wakubwa wa dini, ya wenyi haki, ya wenyi heri na kwa maombezi ya Watakatifu wote, uwape marehemu watumishi wako mapumziko ya milele.

APOSTIKHA YA MUPOSHO

Sauti ya sita. Wimbo ya wafu. Olin apothemeni.

Ee Bwana, kwa mapendo isiyokadirika unaye kwa ajili yetu na kwa chemchem isiyokwisha ya wema wako, pokea wafu katika inchi ya wazima, uwaweke katika hema ya milele, ukiwawekea furaha ya mema waliyotamainia, kwani ulimwanga damu yako, ee Kristu, kwa kuikomboa dunia na bei ya uzima wake.

Shairi: Heri uliyochagua, wale uliyochukua pamoja ee Bwana.

Kwa sisi kuishi uliitikia kufa, ulitirikisha chemchem ya uzima, kwa waaminifu unawapa heri ya milele*:* Uipane pia kwa wale waliyolala katika matumaini ya ufufuo, kwa wema wako

zima zambi zao zote, kwani peke yako usiye na zambi; utuonyeshe mapendo yako ili litukuzwa jina lako, na tukiokolewa nawe, ee Kristu, tukutukuze milele.

Shairi: Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Kristu, tunajuwa ubwana wako kimungu juu ya wazima na wafu; uwape watumishi waaminifu wako waliyomupata mfazili wao pekee yako makao ya watule wako, mahali pa baridi, katika utukufu wa Watakatifu wako, kwani ndiwe Mungu uliye na huruma na mwenyi kuokoa kwa wema wako wale uliyeumba kwa mfano wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ni wewe makao ya Mungu, ulimulinda tumboni mwako na bila ndoa ulizaa mtu mmoja mwenyi hali mbili; umuombe Mwana wa pekee na mzaliwa wa kwanza aliyeacha salama ubikira wako hata kisha kuzaa awape waaminifu waliyolala na ibada mapumziko katika heri na nuru ya milele.

SAUTI YA SABA

SIKU YA MUNGU MANGARIBI KU ESPERINOS.

Elezo*: Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba hii wimbo ya kutubu.*

Sauti ya saba.

Nakuja kwako kama mwana mpotevu, ee Mungu wa wema, nasujudu mbele yako, unipokee kama mmoja wa watumishi wako*:* Ee Bwana, unihurumie.

Kama msafiri aliyeanguka katika mikono ya wanyanganyi, mimi mwenyewe nilianguka katika zangu, roho yangu imejerihiwa kama yeye*:* Kwa nani nitakimbilia mimi maskini ila kwa Mungu wa huruma mwenyi kuponyesha roho zetu kama mganga wa hekima? Vimwangie roho yangu neema ya wokovu.

Ee Mwokozi, usinikate na shoka kama mtini usiyozaa matunda, ongojea miaka mingi, unisamehe zambi zangu, nyunyizia roho yangu machozi ya toba na nitakutolea matunda yenyi kustahili.

Kama Jua la haki, angaza mioyo ya wale wenyi kukuimbia*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU.

Sauti ya saba.

Ee roho yangu, tubu, jongea ukilia na kulalamika, umuambie mganga wa roho na wa miili*:* Ee mpenda-wanadamu, uniopoe ku zambi zangu; unitendee kama kahaba, munyanganyi na Mtoza-kodi, ukisisamehe makosa yangu, ee Bwana, uniokoe.

Sikufananisha toba ya Mtoza-kodi, sikulia kama kahaba; moyo wangu mgumu hauniruhusu salehisho ya hii namna*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, katika wema wako uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Uliye kweli mtukufu kuwashinda wakeruvi, ee Bikira Mtakatifu, kwani wasipoweza kuvumilia nuru ya umungu, wanatimiza kazi yao wakijifunika macho na mabaya yao, lakini

wewe mwenyewe uliweza kumtazama Neno aliyejifanya mutu umuombe daima kwa ajili ya roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Bwana, Mashahidi wako waliposhindana duniani wakamshinda adui tena wakaharibu uwongo wa miungu ya uwango; na tnea wakapokea ku mkono wako taji ya washindaji, ee Bwana na Mungu wa wema mwenyi kutupatia neema ya wokovu.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU.

Sauti ya saba.

Ninapongamia katika bahari ya hii uzima, nazama katika mawimbi ya zambi zangu, lakini wewe, ee Bwana, nyosha mkono uniokoe kama Petro, ee Mpenda-wanadamu.

Shairi: Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ulizima na kusamehe kukana kwa Petro na makosa ya Mtoza-kodi wakati ulipoona kulia na malalamiko*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Uliye mtukufu kuliko Majehsi ya mbinguni, umekuwa hekalu kimungu, ee Mzazi-Mungu na Bikira mbarikiwa, kwani ulizaa Kristu, Mwokozi wa roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Wenyi haki wafurahiwe, mbingu zishangilie, kwani mashahidi duniani wameshinda udanganyifu; Eklezya icheze na furaha ikitukuza ushujaa wa washindaji na imwimbie Bwana wa mashindano, Kristu Mungu wetu mwenyi kuleta neema ya wokovu duniani.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya saba.

Eklezya yako inaposujudu mbele yako, inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu*:* Leta ushindi kwa wakristu na katika Mzazi-Mungu utuhurumie.

Shairi*:* Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Wewe uliyeteswa kwa ajili yangu uliposulubiwa Msalabani, unipe sifa ya milele, ee mpenda-wanadamu tena Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, umusihi Kristu Mungu wetu aliyesulubiwa kwa ajili yetu na aliyevunja nguvu ya mauti, aokoe roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Mashahidi Watakatifu, mulipozarau vitu vyote vya hapa chini, mukamtabgaza na usabiti Kristu katika uwwanja; mukapokea kwake tuzo la mateso yenu, na kwa sasa maana munauwezo, muombeni Mungu mwenyezi aokoe roho zetu.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA MITUME.

Sauti ya saba.

Ee Neno, uliwafanya Mitume wako kuwa watumihsi wa mavuno yako; waliondosha miungu ya uwongo walitangaza ubwana wako; wakakutukuza na mapendo mbele ya mataifa.

Shairi*:* Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Enyi Mitume Watakatifu wa Bwana, munapokuwa miangaza mikubwa ya hii dunia, munangaza waaminifu na neno lenu, mukifukuza mbali giza za upotevu; kwa Ubatizo munangaza mataifa, ee watangazaji watukufu wa Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Muchumba kimungu, tunda la tumbo lako ameonekana kuwa chemchem ya wokovu*:* Na tena, ee Mzazi-Mungu, tunapokutukuza kwa kinywa na kwa moyo, sisi waaminifu tunakusifu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Bwana, walipolindwa kwa uwezo wa Msalaba, mashahidi wako wakakimbiza adui, wakatangaza uwongo wa miungu ya uwongo; sasa wanaimba pamoja na malaika mbinguni wimbo wwa ushindi kwa kukutukuza, ee Kristu; kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya saba.

Uliangazisha muti wa Msalaba wako kushinda moto*:* Inanguza zambi za wagonjwa na inangaza mioyo ya wale wenyi kuimbia kusulubiwa kwako*:* Ee Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Ee Bwana wa majeshi ya mbinguni, wewe unajua uzaifu wa moyo wangu, uniokoe, ee Kristu Mungu wetu, kwa Msalaba wako na wema wako wa pekee.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, umuombe daima Kristu Mungu wetu aliyesulubiwa kwa ajili yetu na aliyeharibu nguvu ya mauti aokoe roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Ee Bwana, walipolindwa kwa uwezo wa Msalaba, mashahidi wako wakakimbiza adui, wakatangaza uwongo wa miungu ya uwongo; sasa wanaimba pamoja na malaika mbinguni wimbo wwa ushindi kwa kukutukuza, ee Kristu; kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo ya mashahidi.

Sauti ya saba.

Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu, matumaini ya Mitume tena furaha ya Mashahidi waliyotangaza Utatu wa asili moja usiyotengana.

Enyi Mashahidi Watakatifu mulioshindana bora na kutukuzwa mbinguni muombeni Bwana aokoe roho zetu.

Ee Mashahidi Watakatifu, mulipozarau vitu vyote vya hapa chini, mukamtangaza na usabiti Kristu katika uwanja; mukapokea kwake tuzo la mateso yenu, na kwa sasa maana munauwezo, muombeni Mungu mwenyezi aokoe roho zetu.

Ee Mashahidi wenyi kustahili sifa yote, sadaka zenyi uzima, zabihu za kiroho, sadaka zenyi kumpendeza Kristu Mungu wetu, dunia haikuwaficha ninyi, ni mbingu iliwapokea ninyi, mukawa wenzao wa malaika; pamoja nao muombeni amani ya dunia na wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Mungu Mwokozi, pumzisha marehemu ndugu zetu wenyi kukulalamikia*:* Ee Chemchem ta uzima, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ulijulishwa kama mama kuliko asili, ee Mzazi-Mungu; ulibaki Bikira usiyosikilikwa kwa neno na mawazo; na ajabu ya uzazi toka kwako, usiyoweza kufasiriwa katika lugha; kwani uchukuo wa mimba yako, ewe uliye safi, ni wa ajabu, na namna ya mimba ni isiyosikilikwa*:* Kwani popote Mungu anataka, usawa wa hali unashindwa; kwa hii sisi wote tukikujuwa sawa mama wa Mungu, tunakusihi bila kuchoka*:* Umupatanishe kwa wokovu wa nafsi yetu.

SIKU YA SITA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA MASHAHIDI.

Sauti ya saba.

Wenyi haki wafurahiwe, mbingu zishangilie, kwani Mashahidi duniani wameshinda udanganyifu; Eklezya icheze na furaha ikitukuza ushujaa wa washindaji na imwimbie Bwana wa mashindano, Kristu Mungu wetu mwenyi kuleta neema ya wokovu duniani.

Shairi: Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Ee Mashahidi Watakatifu, mulipozarau vitu vyote vya hapa chini, mukamtabgaza na usabiti Kristu katika uwwanja; mukapokea kwake tuzo la mateso yenu, na kwa sasa maana munauwezo, muombeni Mungu mwenyezi aokoe roho zetu.

Shairi: Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Ee Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa ajili ya maondoleo ya zambi zetu ili tuokolewe ku uchungu wa mauti na ku hatari yoyote.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Bwana, zamani ulipamuumba mtu wa kwanza kwa sura na mfano wako, ukamuweka katika Paradizo, ili awe mfalme wa viumbe vyote; lakini shetani kwa wivu wake alipomudanganya, akavunja kanuni zako wakati alipoonja tunda lililokataziwa; na tena, ee Bwana, ukamurudisha ku udongo kwenye ulimutosha zamani, katika matumaini ya kama utamupa mapumziko.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Wewe uliyechunga hazina ya ufufuo wetu, ee Mtukufu kamili, okoa kuzimuni ya zambi wale ambao wenyi kukutumainia wewe*:* Ulipazaa wokovu wetu, ukatuokoa ku nguvu ya zambi, wewe ambaye ulipokuwa bikira mbele ya kuzaa, umekaa bikira katika kuzaa kwako, na hata tena bikira kisha kuzaa.

MASIFU MUPOSHO ASUBUI.

Sauti ya saba.

Ee Kristu, tunaposhangilia makumbusho ya Mashahidi wako Watakatifu tunakuimbia tukisema*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Katika uwanja mbele ya baraza ya hukumu ya makafiri, Mashahidi Watakatifu wakalalamika kwa furaha*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Mashahidi Watakatifu waliyojitukuza kwa ushindi wao katika mashindano wakawa taa kwangaza ulimwengu wote; wanamwaambia Kristu*:* Ee Bwana utukufu kwako.

Walipokuwa na ukomo moja, na moyo mmoja, mashahidi wakafuata njia moja ya uzima wao*:* Kwa ajili ya kristu wakachagua kufa, wakashindana kwa bidii sababu ya kufa; mateso ikawasaidia kuwa hazina; ni vizuri sana! Wakaambiana mmoja kwa mwingine*:* Kama sasa tunakimbia kufa, tunapashwa kwa namna yote kulipa haki ku dunia, tufanye mateso yetu kuwa utukufu, kwa lufu yetu tupate uzima wa kweli! Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Mungu Mwokozi ya dunia, pumzisha marehemu nfugu zetu wenyi kukulalamikia*:* Ee Chemchem ya uzima, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION**.

Salamu wewe uliyekuwa fasi ya huyu hata mbingu haikuweza kuchunga; salamu, chombo cha mafundisho ya manabii, ee Bikira uliyezaa Emmanueli, Mama wa Kristu Mungu wetu.

APOSTIKHA YA MUPOSHO ASUBUI.

Sauti ya saba. Wimbo ya wafu.

Ulikufa Msalabani, ee Bwana msiyekufa, ukawekwa kaburini kama mufu, ukakomboa kuzimuni na ku mauti wanadamu wenyi kuharibika na zambi; Ee bahari ya wema usiyoweza kuisha, chemchem ya huruma ya milele, uwape marehemu wetu mapumziko.

Shairi: Heri wale waliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Kwa mapendezi ya milele ya uzuri wako na miangaza ya nuru yako kimungu, angaza marehemu watumishi wako katika nuru ya kiroho yenyi kutokea kwako ili pamoja na Malaika watukuze ubwana wa ufalme wako.

Shairi: Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Hazina ya wema isiyokwisha yenyi kugawanya zawadi zako nyingi, uwape marehemu watumishi wako fasi ya mapumziko na makao ya wateule wako, nyumba ya utukufu wako na nyumba ya mabikira, na kwa wema wako uwape furaha za Paradizo.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Mama, unazaa ukamilifu wa Sheria, Mkombozi aliyejifanya mtu kwa ajili yetu; hakuwa wa kweli kwa wale waliyoishi zamani chini ya Sheria, lakini Kristu alitimiza haki yote wakati alisulubiwa Msalabani kwa kutaka kwake kwa ajili yetu. Umuombe Bwana wako wa huruma apumzishe roho za marehemu waliyokufa na ibada, ee Bikira mwenyi kustahili nyimbo zetu.

SAUTI YA MNANE.

SIKU YA MUNGU MANGARIBI.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo hii:

Malaika wanakuimba daima kama Rabi na Mfalme wao, na mimi nasujudu mbele yako kama Mtoza-kodi na nakulalamika*:* Unihurumie, ee Bwana na uniokoe.

Ee roho yangu, wewe ni mwenyi kufa, usijiachilie kuangamizwa na mawimbi ya hii uzima, amka na umulalamikie Mungu mfazili wako*:* Unihurumie, ee Bwana, na uniokoe.

Unipe machozi, ee Bwana, kama zamani kwa Mwanamuke mwenyi zambi tena unihurusu niyamwangia pa miguu yako, kwani yameniondoa ku njia ya uovu; kama manukato ya harufu nzuri nitakutolea toba ya moyo wangu na usafi wa maisha yangu sababu ya kusikia tena sauti yako pole*:* Wende na amani, imani yako imekuokoa.

Wakati ninapotazama wingi wa matendo yangu mbaya, wakati ninapowaza hukumu ya ajabu, ninapoogopa, nakimbilia kwako*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, usinizarau, peke yako ndiwe usiye na zambi; mbele ya mwisho unipe toba tena uniokoe.

SIKU YA KWANZA ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA KUTUBU.

Sauti ya mnane.

Ee Bwana, tazama mateso yangu na unihurumie, kwani uzima wangu ni karibu kuungua, sina na mateso yenyi kuniongoza ku wokovu*:* Ndio maana nakuomba, ee Bwana, kwa mapendo yako ona mateso yangu na uniokoe.

Shairi: Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ee roho, tazama hali ya hukumu, ujitayarishe ku majilio ya hii siku ya woga*:* Kwa mioyo mbaya hana huruma; na tena lalamika mbele ya mwisho*:* Unisamehe, ee Mwokozi mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Mulango wa siri wa uzima wetu, Mzazi-Mungu na Bikira safi, okoa ku hatari yote waaminifu wenye kukukimbilia, ili tutukuze uzazi wako takatifu kamili kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Enyi mashahidi Watakatifu, mumeonekana kama taa za siri, kwa imani yenu muliondoa giza za uovu, muliangaza taa ya mioyo yetu katika utukufu wa mbinguni mulifikilia chumba cha Bwana Arusi*:* Muombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

SIKU YA MBILI ASUBUI KU ORTHROS.

WIMBO YA KUTUBU.

Sauti ya mnane.

Nasujudu kwako kama kahaba, sababu ya kupata maondoleo ya zambi zangu, pahali pa manemane nakutolea machozi ya moyo wangu; ee Kristu Mungu wetyu, unizungushe na rehema ileile tena unisamehe makosa yangu; kama yeye basi nakulalamikia, ee Mungu Mwokozi*:* Uniokoe ku matope ya zambi zangu.

Shairi: Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ee roho yangu, uwe macho ukiwaza hii siku ya ajabu, tayarisha mafuta yako tena shika taa yako yenyi kuwaka, kwa sababu haujui wakati gani itafika sauti itakayokuambia*:* Tazama Bwana Arusi wako! Kesho basi, ee roho yangu, usilale, ili mulango usifungwe kwako kama zamani kwa mabikira wapumbafu, lakini uwe imara na mwenyi kuangalia kusudi upatane katika nuru yote na Kristu Mungu wetu, ili akuingize katika chumba cha arusi cha utukufu wake kimungu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee boma imara la imani tnea hazina bora ya roho zetu, tunakutukuza kwa nyimbo zetu, ee Mzazi-Mungu; salamu kwani ulichukua tumboni mwako Chemchem ya uzima, salamu, matumaini ya mipaka ya ulimwengu tena mlinzi wa wenyi kuhuzunika, salamu, ewe Bibi usiyeolewa.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Leo hema ya mbinguni imeangaziwa katika hii majeshi ya mbinguni pamoja na makundi ya watakatifu wanafurahiwa kwa makumbusho ya Mashahidi watukufu; kwa maombezi yao, ee Kristu, tuma amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

SIKU YA TATU ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya mnane.

Alipomuona Mfalme wa Uzima ametundikwa Msalabani, Munyanganyi akalalamika na imani*:* Kama huyu anayesulubiwa pamoja nasi hakuna Mungu aliyejifanya mtu, jua halikupashwa kuficha miangaza yake wala dunia haikupashwa kutetemeka na woga; na wewe mwenyi kuvumilia hii yote, unikumbuke mimi, ee Bwana, katika ufalme wako.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Msalaba wako ilisimikwa kule Kalvario, mizazi ya haki kati ya Wanyanganyi wawili ambao mmoja akakokotwa kwa uzito wa kufuru yake mpaka mu Gehena, na mwingine aliposamehewa makosa yake, akapanda ku maarifa ya Mungu. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona wewe Mwana kondoo Msalabani, Mchungaji tena Mwokozi wa dunia, huyu aliyekuzaa akalia machozi na akasema*:* Dunia inafurahi kwa kupokea ukombozi na tumbo langu linaungua kwa kuona kusulubiwa uliyosulubiwa kwa ajili yetu kwa mapendo ya moyo wako, ee

Wema kubwa tena Bwana, utuhurumie na uwaondolee zambi zao waaminifu wenyi kusujudu mbele ya mateso ya Mwana wako.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Enyi Mashahidi wa Kristu wasiyoweza kushindwa muliyoshinda upotevu kwa uwezo wa Msalaba, mulipokea neema ya uzima wa milele; bila woga muliteswa ku makamio ya wazulumu, sasa munafurahiwa tena roho zetu zinaponyeshwa kwa damu yenu; ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

SIKU YA INE ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA WA MITUME.

Sauti ya mnane.

Uhimidiwe, ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyewashushia Mitume wako Roho Mtakatifu, ukiwageuza kwa hekima yako wavuvi kuwa wavuvi wa watu ambao nyavu yatavua dunia yote. Bwana Mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Shairi: Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Tunawatukuza Mitume Watakatifu wa Mungu wetu kama waongozi, taa za ulimwengu na malimbuko ya wokovu wetu, kwani walishushe nuru juu ya giza zetu tena walituonyesha Jua la Haki; walifukuza uwongo wa miungu ya uwongo, wakitangaza Utatu Mtakatifu mu umungu moja; Ndio maana tunawaomba, enyi Mitume Watakatifu wa Kristu Mungu wetu, muwasamehe zambi zao wale wenyi kutukuza na mapendo makumbusho yenu takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Salamu, wewe uliyepokea furaha ya ulimwengu kwa sauti ya malaika, salamu; wewe uliyezaa Muumbana Bwana wako; salamu, wewe uliyestahili kuwa Mama wa kristu Mungu wetu.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Mulipovaa silaha ya imani, muliposhika alama ya Msalaba kama silaha mumeonekana kuwa maaskari washujaa; mukashindana vema na wazulumu, mukaondoa uongo wa shetani, mukastahili taji la Washindaji*:* Ombeni kwa Kristu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

SIKU YA TANO ASUBUI KU ORTHROS.

KATHISMA YA USULUBIO.

Sauti ya mnane.

Katikati ya shamba la Edeni muti ilizaa mauti, katikati ya dunia muti ikachanua uzima; tulipoonja ya kwanza tukufe, ku wa pili tukapata furaha ya milele, kwa sababu Msalabani, ee Mungu, uliokoa wanadamu.

Shairi: Tukuzeni Bwana Mungu wetu na kuabudu kwa kiti cha miguu yake.

Zamani adui aliniondoa ku Paradizo, akanipa kuonja tunda la muti akaingiza mauti; lakini muti wa Msalaba ukasimikwa duniani, ikamuvika mtu vazi la uzima tena dunia yote inajaa na

furaha*:* Tunapoona Msalaba umetukuzwa, sisi wote tumulalamikie Bwana kwa sauti moja*:* Hekalu yako imejaa na utukufu wako!

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulipomuona huyu aliyejifanya mtu tumboni mwako kwa namna ya ajabu ametundikwa Msalabani katikati ya Wanyanganyi, moyo wako ukahuzunika na kama mama ukalia ukilalamika*:* Ole wangu, ee Mwanangu, hii ni fumbo gani isiyokadirika na takatifu ambayo unaokoa nayo viumbe vyako ukiwapatia uzima? Naimba mapendo yako na rehema yako.

Kisha Ode ya sita tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon).

Walipoteshwa kwa kukataa ukali na woga na mateso yao, Mashahidi wa kristu wakapokea uwezo wa kufukuza uzaifu wote na ugonjwa wote na wa kufanya miujiza ya uzima hata kisha kufa kwao. Ni ajabu ya kushangaa! MIfupa ya bure imekuwa chemchem ya kuponyesha. Tutukuzeni hekima ya pekee ya Mungu Muumba.

SIKU YA TANO MANGARIBI KU ESPERINOS.

Kisha «Bwana nimekuita. . . » tunaimba wimbo ya mashahidi.

Enyi Mashahidi wa bwana, ombeni kwa Mungu ili kwa wema wake atusamehe zambi zetu nyingi.

Enyi mashahidi wa Bwana, muombeni Mungu kwa ajili ya roho zetu na kwa wema wake atuondolee zambi zetu nyingi mno.

Ee Bwana, mashahidi wako waliposahau hii uzima tena walipozarau pia mateso sababu ya uzima wa milele, wakariti mbingu na wanafurahiwa pamoja na Malaika*:* Kwa maombezi yao uwape watu wako neema ya wokovu.

Utukufu wote na sifa yote ni kwa Mashahidi walikufa ku upanga kwa ajili yako wewe uliyeshuka ukiinamisha mbingu; walimwanga damu yao kwa ajili yako wewe uliyejishusha wakati ulitwaa hali ya mtumwa; na walipojinyenyekeza mpaka kufa, wakafwa umaskini wako*:* Ee Bwana, kwa maombezi yao na kwa rehema yako, utuhurumie.

Utukufu kwa baba. . . *Wimbo ya wafu.*

nalia tena naomboleza nikiwaza lufu, wakati ninapoona imelala kaburini bila hali, bila utukufu na bila mapendo, neema tuliyopewa kwa mfano wa Mungu*:* Ni fumbo ya ajabu! Namna gani tutaweza kushuka kaburini? namna gani tutaunganishwa ku mauti? Kama ilivyo Maandiko Takatifu ni kwa amri ya Mungu mwenyi kuwapa marehemu mapumziko.

Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION**

Mfalme wa mbinguni, kwa kupenda-wanadamu, alionekana juu ya inchi akazoea kati ya watu; kwani alipotwaa mwili kwa Bikira safi, na alipotokea kwa huyu, pamoja na hali ya umutu, huyu ni Mwana moja, kwa hali mbili, lakini hana uso mbili; kwa hii tukihubiri ya kama huyu kweli ni Mungu Mukamilifu na Mutu mukamilifu, tunaungama Kristu Mungu wetu; umusihi ewe Mama usiyeolewa, kwa huruma wa nafsi yetu.

SIKU YA MUPOSHO ASUBUI KU ORTHROS

KATHISMA YA WAFU.

Sauti ya mnane.

Enyi mashahidi Watakatifu, mumeonekana kama taa za siri, kwa imani yenu muliondoa giza za uovu, muliangaza taa ya mioyo yetu katika utukufu wa mbinguni mulifikilia chumba cha Bwana Arusi*:* Muombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Shairi*:* Mungu ni wa ajabu katika watakatifu wake.

Kwa imani ya ushuhuda mumefunuliwa kama taa za ulimwengu, wenyi kuangaa daima; mulipomtumainia Kristu, mukawakisha taa ya mioyo yenu na mafuta ya fumbo ya Roho Mtakatifu; na kama vikombe vya kiroho munamwanga maponyesho mengi kwa ajili ya Kristu. Ee Mashahidi Takatifu wenyi kustahili sifa yote, ombeni kwa Kristu Mungu wetu awaondolee zambi zao wale wenyi kutukuza na mapendo makumbusho yenu takatifu.

Shairi: Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

Walipoteshwa kwa kukataa ukali na woga na mateso yao, Mashahidi wa kristu wakapokea uwezo wa kufukuza uzaifu wote na ugonjwa wote na wa kufanya miujiza ya uzima hata kisha kufa kwao. Ni ajabu ya kushangaa! MIfupa ya bure imekuwa chemchem ya kuponyesha. Tutukuzeni hekima ya pekee ya Mungu Muumba.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Kisima cha hekima mwenyi kuwapenda wanadamu tnea mwenyi kuongoza vitu vyote ku wokovu, peke yako Muumba ambaye kila mmoja anapokea ile yenyi kumfaa, ee Bwana, pumzisha roho za watumishi wako, kwani wamekutumainia wewe asili yetu, Muumba wetu na Mungu wetu.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, wewe ni boma letu na bandari yetu ya wokovu, msimamizi wa kweli kwa Mungu uliyezaa, ee Bikira Mzazi-Mungu, ndiwe wokovu wa wakristu.

MASIFU MUPOSHO ASUBUI

Sauti ya mnane.

Namna gani tutawaita ninyi, ee Mashahidi Watakatifu? Wakheruvi? Maana ninyi ni kiti cha ezi cha Kristu; Waserafi? Maana munamutukuza daima; Malaika? Kwani mumekataa mwili wenu; Majeshi? Kwa ajili ya miujiza ombeni kwa ajili ya roho zetu.

Ee Mashahidi, mulishindana kwa ushujaa, mukateswa vema na mateso ya makafiri tena mukamuungama Kristu kwa wafalme; kisha kuacha hii uzima, uwezo wenu unatendeka duniani, munaponyesha mateso yote na ugonjwa wote. Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Enyi Mashahidi wa Kristu wasiyoweza kushindwa muliyoshinda upotevu kwa uwezo wa Msalaba, mulipokea neema ya uzima wa milele; bila woga muliteswa ku makamio ya wazulumu, sasa munafurahiwa tena roho zetu zinaponyeshwa kwa damu yenu; ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

Mulipovaa silaha ya imani, muliposhika alama ya Msalaba kama silaha mumeonekana kuwa maaskari washujaa; mukashindana vema na wazulumu, mukaondoa uongo wa shetani, mukastahili taji la Washindaji*:* Ombeni kwa Kristu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . *Wimbo ya wafu.*

Ee Bwana, lufu yako inatupatia uzima wa milele na kwa kushuka Kwako kaburini unatufungulia Paradizo*:* Uwape marehemu mapumziko na amani.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mzazi-Mungu, ulinzi wako ni dawa ya kiroho kwa sisi yenyi kuokoa roho zetu ku magonjwa.

APOSTIKHA YA MUPOSHO ASUBUI

Sauti ya mnane. O tu paradoksu thavmatos.

Ee Bwana, kama Mfalme ulisahihisa uhuru wangu kwa damu yako, sasa nakuomba kwa wema wako, andika marehemu waaminifu ku kitabu cha wazaliwa wa kwanza; ukiwapa furaha ya wateule wako.

Shairi: Heri wale waliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Ulipoteswa kama kohani na kutolewa sadaka kama Mwana-kondoo, ulitolea kwa baba yako wanadamu waliyokombolewa ku mauti; ee Mpenda-wanadamu, weka marehemu waaminifu katika inchi ya wenyi hai, huko kunamwangika heri nyingi na chemchem ya uzima wa milele.

Shairi: Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Kisima cha hekima ya milele, iliweka mpaka wa uzima, na uliweka tayari ukomo wetu utakaokuja*:* Unawaita watumishi wako ku uzima ingine, ee Bwana uwapeleke ku maji ya mapumziko, katika nuru ya watakatifu, kule kunasikilika sifa na furaha.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Neno la Mungu msiyeonekana, wa hali moja na Baba na mwenyi utukufu uleule na Roho Mtakatifu, ulijifanya mtu kwa ajili ya sisi wanadamu; kwa rehema na mapendo yako, uwape waaminifu waliyoondoka hii uzima wangae na nuru yako, na ukuu wako tena na uzuri wako.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mama uliyezaa Neno la Mungu, kwa deni unayo kwake umuombe aweke watumishi wake katika makao ya furaha ya milele pamoja na wale wenyi kutukuza jina lako, kule kunangaa nuru ya milele na kunasikilika sauti ya furaha, ee Mzazi-Mungu.

MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIO
KILIMA TAKATIFU
HELLAS-GREKIA
2001